

Kamati ya Kisayansi ya Kimataifa ya UNESCO kwa ajili ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika

HISTORIA KUU YA AFRIKA •

Juzuu
Lililofupishwa

II Staarabu za Kale za Afrika

MHARIRI G. MOKHTAR



TUKI • CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM • UNESCO

Kamati ya Kisayansi ya Kimataifa ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika (UNESCO)

Historia Kuu ya Afrika · II

Staarabu za Kale za Afrika

MHARIRI G. MOKHTAR

TUKI . CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM . UNESCO

Jina la Asili: GENERAL HISTORY OF AFRICA, VOL II

© UNESCO 1999

ISBN 9976 911 35 1

Maelezo yaliyotolewa na uwasilishaji wa matini zote kwenye chapisho hili haumaanishi maoni yoyote yale kwa upande wa UNESCO kuhusu sheria ya nchi yoyote ile, mji au eneo au mamlaka yake, au kuwekea mipaka eneo lolote lile.

Waandishi wanahusika na uteuzi na uwasilishaji wa taarifa za kweli zilizopo kwenye kitabu hiki na kwa maoni yaliyoelezewa ndani, ambayo si lazima yawe yale ya UNESCO na hayalifanyi Shirika liwajibike.

Toleo la Tafsihi ya Kiswahili limechapishwa kwa msaada wa kifedha wa UNESCO.

Staarabu za Kale za Afrika

Toleo Lililofupishwa

UNESCO Historia Kuu ya Afrika

- Juzuu I** *Mbinu na Historia ya Awali ya Afrika*
Mhariri J. Ki-Zerbo
- Juzuu II** *Staarabu za Kale za Afrika*
Mhariri G. Mokhtar
- Juzuu III** *Afrika kuanzia Karne ya Saba hadi ya Kumi na Moja*
Mhariri Msaidizi I. Hrbek
- Juzuu IV** *Afrika kuanzia Karne ya Kumi na Mbili hadi ya Kumi na Sita*
Mhariri D.T. Niane
- Juzuu V** *Afrika kuanzia Karne ya Kumi na Sita hadi ya Kumi na Nane*
Mhariri B.A. Ogot
- Juzuu VI** *Afrika kuanzia Karne ya Kumi na Tisa hadi Miaka ya 1880*
Mhariri J.F. A. Ajayi
- Juzuu VII** *Afrika Chini ya Utawala wa Kigeni 1880 - 1935*
Mhariri A. Adu Boahen

Toleo Lisilofupishwa la Jalada Jepesi

- Juzuu VIII** *Afrika Kuanzia 1935*
Mhariri A.A. Mazrui
Mhariri Msaidizi C. Wondji

**Toleo lililofupishwa la
HISTORIA KUU YA AFRIKA YA UNESCO**

Limechapishwa na:

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI)
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
S.L.P. 35110,
Dar es Salaam, Tanzania


Pamoja na:
UNESCO publishing
7 Place de Fontenoy, 75700, Paris

**Kimepangwa na kuchapwa na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha
Dar es Salaam, S.L.P. 35110, Dar es Salaam, Tanzania.**

Yaliyomo

Dibaji na Amadou -Mahtar M'Bow aliyekuwa Mkurugenzi wa UNESCO (1974-87)	vii
Wasifu wa Mradi na B.A. Ogot, aliyekuwa Mwenyekiti, Kamati ya Kisayansi ya Kimataifa ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika	xii
Maelezo ya Wendo	xv
Wanakamati wa Kamati ya Kisayansi ya Kimataifa ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika	xvi
Wasifu wa Waandishi	xviii
<i>Utangulizi</i>	<i>1</i>
<i>1 Asili ya Wamisri wa Zamani</i>	<i>16</i>
<i>Nyongeza ya Sura ya Kwanza: Taarifa ya Kongamano</i>	
<i>2 Misri ya Farao</i>	
<i>3 Misri ya Farao: jamii, uchumi na utamaduni</i>	<i>70</i>
<i>4 Uhusiano wa Misri na sehemu zingine za Afrika</i>	<i>89</i>
<i>5 Matokeo ya utawala wa Mafarao Misri</i>	<i>102</i>
<i>6 Misri katika enzi ya Uyunani</i>	<i>116</i>
<i>7 Misri chini ya utawala wa Kirumi</i>	<i>134</i>
<i>8 Umuhimu wa Unubi: uhusiano baina ya Afrika ya Kati na Mediterani</i>	<i>148</i>
<i>9 Unubi kabla ya Napata (-3100 hadi -750)</i>	<i>160</i>
<i>10 Himaya ya Kushi: Napata na Meroe</i>	<i>168</i>
<i>11 Ustaarabu wa Napata na Meroe</i>	<i>183</i>
<i>12 Usambaaji wa Ukristo huko Nubia</i>	<i>196</i>
<i>13 Utamaduni wa kabla ya Waaxumi</i>	<i>210</i>
<i>14 Ustarabu wa Axum kuanzia karne ya kwanza hadi ya saba</i>	<i>218</i>
	<i>231</i>

15	<i>Axum: mfumo wa siasa, uchumi na utamaduni karne ya kwanza hadi ya nne</i>	244
16	<i>Axum ya Ukristo</i>	257
17	<i>Waberiberi wa Awali</i>	272
18	<i>Kipindi cha Ukatheji</i>	283
19	<i>Kipindi cha Warumi na baada ya Warumi huko Afrika Magharibi</i>	300
20	<i>Sahara kwenye ukale wake</i>	327
21	<i>Madokezo ya mwanzo ya historia ya awali ya baadaye ya Kusini mwa Sahara</i>	337
22	<i>Pwani ya Afrika Mashariki na dhima yake katika biashara ya majini</i>	349
23	<i>Afrika Mashariki kabla ya karne ya Saba</i>	357
24	<i>Afrika Magharibi kabla ya karne ya Saba</i>	367
25	<i>Afrika ya Kati</i>	384
26	<i>Kusini mwa Afrika: wawindaji na wakusanyaji chakula</i>	398
27	<i>Mianza ya Enzi ya Mawe kusini mwa Afrika</i>	411
28	<i>Madagaska</i>	423
29	<i>Jamii za Afrika kusini mwa Sahara kwenye enzi ya mawe ya Mapema</i>	434
	<i>Hitimisho</i>	442
	<i>Bibliografia</i>	447
	<i>Faharasa</i>	462
	<i>Sherehe</i>	485



Dibaji

AMADOU - MAHTAR M'BOW

Mkurugenzi Mkuu wa Zamani wa UNESCO (1974-1987)

Kwa muda mrefu, aina zote za uzushi na kashfa zilificha historia halisi ya Afrika kwa dunia nzima. Jamii za Kiafrika zilionekana kama jamii zisizoweza kuwa na historia. Licha ya kazi muhimu zilizofanywa na waasisi kama Leo Frobenius, Maurice Delafosse na Arturo Labriola tangu miongo ya mwanzoni mwa karne hii, wataalamu wengi wasio Waafrika hawakuweza kuondoa fikra fulani za awali walizozishikilia na wakadai kwamba kukosekana kwa kumbukumbu za maandishi kulifanya isiwezekane kufanya utafiti wowote wa kisayansi wa jamii kama hizo.

Ingawa tenzi za *Iliad* na *Odysey* kwa usahihi zilichukuliwa kama kumbukumbu muhimu za historia ya Ugiriki ya kale, mapokeo simulizi ya Kiafrika, ambayo ndiyo kumbukumbu za pamoja za watu yanayounganisha matukio mengi yenye kuonyesha maisha yao, yanakataliwa kuwa hayana thamani. Kwa kuandika historia ya sehemu kubwa ya Afrika, kumbukumbu tu zilizotumika ni zile za kutoka nje ya bara. Matokco yake ni kuwa kale walichoandika kilitoa sura ambayo sio ya njia halisi walizopita Waafrika, bali zile ambazo maandishi walifikiria kuwa pengine ndimo walimopita. Kwa kuwa Enzi za Kati za Ulaya mara nyingi ndizo zilizotumika kama kijiuno, njia za uzalishaji, mahusiano ya kijamii na asasi za kisiasa zilitazamwa tu kwa kurejelea zama za Ulaya.

Kwa hakika, maandishi hao walikataa kuwachukulia Waafrika kama waumbaji wa tamaduni za asili ambazo zilichanua na kuduini kwa karne nyingi katika ruwaza walizozibuni na ambazo wanahistoria hawawezi kuzibaini isipokuwa pale tu watakapokubali kuachana na mawazo yao ya kashfa.

Zaidi ya hayo, bara la Afrika halikutazamwa hata kidogo kama eneo moja kihistoria. Kinyume chake, nikazo uliwekwa kwenye kila kitu kilichoclekea kuhalalisha wazo kwamba mgawanyiko ulikuwepo toka zama za kale, kati ya 'Afrika ya weupe' na 'Afrika ya Weusi', kila upande ukiwa haujui kuwa kuna watu wa upande mwingine. Mara nyingi Sahara ilielezwa kama eneo lisilopitika na hivyo kuzuia kuchanganyikana kwa makundi ya kimbari na watu au mabadilishano ya

bidhaa, imani, desturi na mawazo baina ya jamii zilizozidi kukua katika kila upande wa jangwa. Mipaka iliyofungwa kabisa iliwekwa baina ya staarabu za Misri ya Kale na Unubi na ile ya watu wa kusini mwa Sahara.

Ni kweli kwamba historia ya Afrika kaskazini mwa Sahara imchusishwa kwa karibu mno na ile ya nchi za bonde la Bahari ya Mediterani kuliko ilivyokuwa kwa historia ya Afrika Kusini mwa Sahara, lakini hivi sasa inafahamika zaidi kwamba staarabu mbalimbali za bara la Afrika, pamoja na tofauti zao za lugha na tamaduni, zinawakilisha, kwa kiasi kikubwa au kidogo, michepuo ya kihistoria ya makundi ya watu na jamii yanayounganishwa na mahusiano ya karibu yenye umri wa kame nyingi.

Jambo jingine ambalo halikutendea haki utafiti wa uhakika wa Afrika ya Kale ilikuwa ni tokcazaji wa ubaguzi wa rangi, ikiwa ni pamoja na biashara ya utumwa na ukoloni, ambao ulizaa dharau na kutokuelewana na hata kupata mashiko kiasi kwamba hisia hizo kuvuruga hata dhana za msingi za uandikaji historia. Tokca wakati dhana za "mweupe" na "mweusi" zilipoanza kutumika kama vitambulisho vya jumla na wakoloni, ambao walichukuliwa kuwa watu wa daraja la juu, ilibidi Waafrika waliotawaliwa wapambane dhidi ya utumwa wa kiuchumi na wa kisaikolojia. Waafrika walitambuliwa kwa rangi ya ngozi zao, walifanywa kama bidhaa, walitayarishwa ili kufanya kazi ngumu na hatimaye, katika fikra za waliowatawala, waliishia kuashiria mbari ya *kinegro* ambayo ilibuni wa na kudaiwa kuwa mbari duni. Ruwaza hii ya utambulisho wa uwongo ilidhalilisha historia ya watu wa Afrika katika fikra za watu kufikia kiwango cha historia ya kimbari, ambamo ufahamu wa ukweli wa kihistoria na kitamaduni ulikuwa lazima upotoshwe.

Hali imebadilika vya kutosha tangu mwishoni mwa Vita Vikuu vya Pili vya Dunia na hasa toka nchi za Kiafrika zipate uhuru na kuanza kushiriki kikamilifu katika maisha ya jumuiya ya kinataifa na katika mabadilishano ambayo ndiyo sababu ya kuwepo kwake. Idadi kubwa ya wanahistoria wamejitahidi kukabili utafiti wa Afrika kwa mtazamo thabiti, usiopendelea na wa wazi kwa kutumia - pamoja na tahadhari zote - kumbukumbu halisi ya Kiafrika. Kwa kutumia haki yao ya kuchukua jitihada za kihistoria, Waafrika wenyewe wamechisi haja kubwa ya kuanzisha upya ukweli wa kihistoria wa jamii zao kwenye misingi thabiti.

Katika muktadha huu, umuhimu wa majuzuu haya nane ya *Historia Kuu ya Afrika*, ambayo UNESCO inachapisha unajieleza wenyewe.

Wataalamu kutoka kwenye nchi nyingi ambao wanashughulikia mradi huu walianza kwa kuweka misingi ya kinadharia na ya kimbinu kwa ajili ya *Historia* hii. Wamekuwa katika hali ngumu ya kuutilia shaka urahisishaji mno wa historia ya

Afrika unaotokana na dhana ya wazo la upande mmoja na finyu kuhusu historia ya dunia na kuanzisha upya taarifa za kweli kila ilipolazimu na ilipowezezana. Wamejitahidi kuonyesha bayana data za kihistoria zinazotoa picha ya wazi kuhusu mabadiliko ya watu tofauti wa Afrika katika mandhari yao maalum ya kijamii na kitamaduni.

Ili kuikabili kazi hii kubwa, ambayo ilifanywa kuwa yenye utata na ngumu zaidi na wingi wa kumbukumbu za aina nyingi na ukweli kwamba nyaraka zilikuwa zimesambaa sana, imebidi UNESCO icnde hatua kwa hatua. Hatua ya kwanza, kuanzia 1963 hadi 1969, ilikuwa ni ya kukusanya nyaraka na kutayarisha mpango wa kazi. Migawanyo ya kazi ilifanyika uwandani na ilijumuisha kampeni za kukusanya mapokeo simulizi, uundaji wa vituo vya nyaraka vya kikanda kwa ajili ya mapokeo simulizi, ukusanyaji wa miswada isiyochapishwa ya Kiarabu na Kiajemi (lugha za Kiafrika zilizoandikwa kwa hati za Kiarabu), utengenezaji wa orodha ya kumbukumbu za kale na utayarishaji wa Kiongozi cha Kumbukumbu za Historia ya Afrika (*A guide to the sources of the History of Africa*) kutokana na hifadhi za nyaraka na maktaba ya nchi za Ulaya na baadaye kuchapishwa katika majuzuu kuni na moja. Zaidi ya hayo, nukutano iliandaliwa kuwawchezsha wataalamu kutoka Afrika na mabara mengine kujadili masuala ya mbinu, na kuweka misingi wazi ya utekelezaji wa mradi huu baada ya uchunguzi makini wa kumbukumbu zilizokuwepo.

Hatua ya pili, ambayo ilianza 1969 hadi 1971, ilihusika na uwekaji sawa wa *Historia* na kuunganisha schemu zake tofauti. Madhumuni ya mikutano ya kimataifa ya wataalamu iliyofanyika huko Paris mwaka 1969 na Addis Abbaba mwaka 1970, yalikuwa ni kuchunguza na kufafanua matatizo yaliyopo kwenye kusawidi na kuchapisha *Historia*; kuitoa historia hiyo katika majuzuu manane, kuwa na chapa kuu katika Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu, kuitafsiri katika lugha za Kiafrika kama vile Kiswahili, Kihausa, Kifulfulde, Kiyoruba au Kilingala, matarajio ya chapa za baadaye kwa Kijerumani, Kirusi, Kireno, Kihispania na Kichina na vilevile chapa zilizofupishwa kwa ajili ya umma mpana wa Kiafrika na Kimataifa.

Hatua ya tatu imchusu usawidi wenyewe na uchapishaji. Hatua hii ilianza kwa kutculiwa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi yenye wajumbe 39, theluthi mbili miongoni mwao wakiwa Waafrika na theluthi moja wasio Waafrika, ambayo ndiyo Kamati inayochukua jukumu la kitaaluma kwa *Historia* hii.

Mbinu iliyotumika ni ya taaluma fungamano na imekitwa kwenye mkabala wenywe jiha za namna tofauti na kumbukumbu za aina nyingi. Ya kwanza miongoni mwa hizi ni akiolojia, ambayo ndiyo taaluma yenye ufumbuzi kwa mambo mengi ya historia ya tamaduni na staarabu za Afrika. Kutokana na akiolojia, inakubalika sasa

kuwa Afrika hucnda ndio ilikuwa chanzo cha wanadamu na cneo - katika kipindi cha Neolithi — la moja ya mapinduzi ya kiteknolojia ya kwanza katika historia. Akiolojia pia imconygesha kwamba Misri ilikuwa mahali ambapo kulikuwa na mojawapo ya tamaduni za kale maarufu mno duniani. Lakini kumbukumbu nyingine muhimu sana ni mapokeo simulizi ambayo baada ya kudharauliwa kwa muda mrefu, sasa yamecibuka kama chombo muhimu cha kuvumbulia historia ya Afrika, kwa kufanya iwecekane kufuatilia mijongeo ya watu wake mbalimbali katika kitambo cha nafasi na wakati, kuelewa maono ya Kiafrika kuhusu dunia kutokca ndani mwake na kuzingatia sifa za asili za amali ambamo ndimo zilipokitwa tamaduni na asasi za bara lili.

Tunaishukuru Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi inayosimamia *Historia Kuu ya Afrika*, na kwa Waandishi, Wahariri na Watunzi wa majuzuu mbalimbali na sura zake, kwa kuipatia mwanga mpya ukale wa Afrika katika uasilia na muundo wake mzima na kwa kupukana na inadi katika utafiti wa masuala muhimu. Miongoni mwa masuala haya tunaweza kutaja: biashara ya watumwa, "jeraha lisilopona", ambayo ilisababisha mojawapo ya uhamishaji wa kikatili wa watu wengi katika historia ya mwanadamu, ambao ulifyonza uhai wa bara la Afrika na papo hapo kuchangia sana katika upanuzi wa uchumi na biashara huko Ulaya. Masuala mengine ni ukoloni na athari zake zote kwa idadi ya watu, uchumi, saikolojia na utamaduni, mahusiano kati ya Afrika kusini mwa Sahara na ulimwengu wa Kiarabu; na mwisho, harakati za kutokomeza ukoloni na za ujenzi wa taifa ambazo ziliamsha akili na hisia za watu ambao baadhi yao wangali hai na pengine wangali wakicendesha harakati. Masuala haya yote yametajwa kwa kuzingatia ukweli na umakini aambazo ni sifa kubwa za *Historia* hii. Kwa kuchunguza ujuzi wetu wote wa Afrika, kutoa mawazo ya namna mbalimbali juu ya tamaduni za Afrika na kwa kutoa mtazamo mpya wa historia, *Historia* hii ina faida ya pkecc ya kubainisha mwanga na kivuli na ya kudhihirisha wazi tofauti za inaoni ambazo yaweckana zikawepo kati ya wataalamu.

Kwa kuonyesha kasoro katika mikabala ya kimbinu iliyotumika kwa muda mrefu katika kufanya utafiti kuhusu Afrika, *Historia* hii inadaai kufanyike utafiti mpya na wenyec uangalifu kwa macneo ya matatizo ya namna mbili ya uandikaji wa historia na mahusiano yaliyopo kati yake, namna ambazo zinaunganishwa na uhusiano wa kutegemeana. Kama vile ilivyo kazi yoyote ya kihistoria yenyc thamani, *Historia* hii inaandaa njia kwa ajili ya utafiti mwingi zaidi kuhusu mada za aina mbalimbali.

Ni kwa sababu hiyo kwamba Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi, ikishirikiana kwa karibu na UNESCO, iliamua kuanzisha tafiti za ziada katika kujaribu kuyaingia kwa kina masuala kadhaa yatakayoweckesha kueleweka kwa vipengele

fulani vya kale ya Afrika. Matokeo ya tafiti hizo yanayochapishwa katika mfululizo wa *Mitaala na Nyaraka za UNESCO- Historia Kuu ya Afrika*¹ yatakuwa kijalizo muhimu kwa *Historia* hii kama zitakavyokuwa pia kazi zilizopangwa kufanyika juu ya vipengele vya historia ya taifa au ya majimbo ya Afrika.

Historia Kuu inatoa mwanga kuhusu umoja wa kihistoria wa Afrika na pia mahusiano ya bara hili na mabara mengine, hasa Amerika na Caribbean. Kwa muda mrefu mambo ya kibunifu ya vizazi vya Waafrika katika Amerika yalilundikwa pamoja na baadhi ya wanahistoria kama mkusanyo wa mambo mchanganyiko wa *Uafrika*. Kwa hakika huu si mtazamo wa wandishi wa *Historia* hii ambamo upinzani wa watumwa waliosafirishwa kwenda Amerika, kushiriki mfululizo na kwa wingi kwa vizazi vya Waafrika katika mapambano kwa ajili ya uhuru wa mwanzo wa Amerika na katika harakati za ukombozi wa kitaifa, yanatazamwa vizuri kama yalivyokuwa: utetezi wa dhati wa kujitambua, uliosaidia kuunda dhana ya kilimwengu ya jamii ya watu. Ingawa jambo hili linaweza likatofautiana katika sehemu mbalimbali ni dhahiri sasa kuwa namina za kuhisi, kufikiri, kuota ndoto na kutenda katika mataifa fulani ya magharibi zimeathiriwa na urithi wa Kiafrika. Urithi wa kitamaduni wa Kiafrika unaonekana kila mahali kutoka kusini mwa Marekani hadi kaskazini mwa Brazil, katika Caribbean na kwenye pwani ya Bahari ya Pacific. Katika sehemu fulani urithi huo ni msingi wa ubainisho wa kitamaduni wa baadhi ya vipengele muhimu kabisa ya watu.

Historia hii pia huonyesha dhahiri mahusiano ya Afrika na kusini mwa bara la Asia kupitia Bahari ya Hindi na michango ya Kiafrika katika staarabu nyinginezo kutokana na mabadilishano baina yake na maceo hayo.

Nina hakika kuwa juhudi za watu wa Afrika za kutwaa kwa nguvu au kuimarisha uhuru wao, za kupata maendeleo yao na kutetea maumbile yao ya kitamaduni lazima zitokane na utambuzi wa kihistoria uliohuishwa, wenyewe kushabikiwa na wa kuzingatiwa na kila kizazi.

Kwa kuangalia historia ya maisha yangu, uzoefu nilioupata kama mwalimu na kama mwenyekiti, toka siku za awali za uhuru, wa tume za mwanzo zilizoundwa kurekebisha mitaala ya historia na jiografia katika baadhi ya nchi za Afrika

¹ Majuzuu kumi na mbili yafuatayo yamekwishachapishwa katika mfululizo huu:

Kikaliwa kwa Misri ya Kale na yfasiri wa hati za Kimeroi; Biashara ya Utumwa Afrika tangu karne ya kumi na tano hadi karne ya kumi na tisa; Mahusiano ya kihistoria kuvuka Bahari ya Hindi. Uandikaji wa historia wa Kusini mwa Afrika; Kuondoka kutoka ukoloni Afrika Kusini mwa Afrika na Penbe ya Afrika; Majina ya mbari na ya sura ya nchi ya Afrika; Mahusiano ya kihistoria kijamii na kitamaduni baina ya Waafrika wengi na Waarabu tangu 1935 hadi leo; Mbinu za historia ya sasa ya Afrika; Afrika na vita vya Pili vya Dunia; Uelimishaji na uandikaji historia Afrika Kale ya Libya; Dhima ya Vyama vya Wanafunzi wa Kiafrika kwenye mabadiliko ya kisiasa na kijamii ya Afrika kuanzia 1900 hadi 1975.

Magharibi na Kati, ulinifundisha jinsi ilivyokuwa muhimu kwa climu ya vijana na kwa taarifa kwa watu wote kwa jumla, kuwa na vitabu vilivyochapishwa na wataalamu wenyec ujuzi wa ndani kuhusu matatizo na matumaini ya Afrika na wenyec uwezo wa kuyaelewa mambo yote ya bara zima.

Kutokana na sababu zote hizi, shabaha ya UNESCO itakuwa ni kuhakikisha kwamba hii *Historia Kuu ya Afrika* inasambazwa katika lugha nyingi na kutumiwa kama msingi wa kuandaaa vitabu vya watoto, vitabu vya kiada na vipindi vya radio na televisheni. Hivyo vijana wakiwa watoto wa shule au wanafunzi, na watu wazima katika Afrika na pengicpo, wataweza kupata picha kamili ya kale ya bara la Afrika na vipengele vinavyoclezea picha hiyo na vilevile kuolewa vizuri urithi wake wa kitamaduni na mchango wake katika maendeleo ya jamii ya watu. Kwa hivyo, *Historia* hii itaweza kuchangia katika ushirikiano bora wa kimataifa na mshikamano imara miongoni mwa watu katika matumaini yao ya kupata haki, maendeleo na amani. Hii, walau, ndio tumaini langu kubwa.

Kinachobakia ni kwa mimi kutoa shukrani zangu za dhati kwa wajumbe wa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi, mwandishi, wahariri wa majuzuu inbalimbali, waandishi na wale wote walioshiriki katika kazi hii kubwa. Kazi waliyokamilisha na mchango waliutoa unadhahirisha jinsi watu wenyec usuli tofauti lakini wenyec moyo mmoja wa ridhaa na hamasa wa kuhudumia ukweli wa kilimwengu wanavyoweza, ndani ya kiunzi cha kimataifa kilichotolewa na UNESCO, kufanikisha mradi wenyec unuhumu mkubwa kisayansi na kitamaduni. Natoa shukrani pia kwa mashirika na serikali ambazo ukarimu wake umeiwezesha UNESCO kuchapisha *Historia* hii katika lugha tofauti na hivyo kuhakikisha kwamba itapata uzito inaostahiki duniani kote, na kwa jinsi hiyo kuhudumia jumuiya nzima ya kimataifa.

Shukrani za kupatiwa picha

- Allen na Thompson, *Narrative of an Expedition*, London, 1848, 27.4*
- Al-Refei, Abdel-Rahman., *Açr Mohammad 'Ali*, Dar al-Nahdal al-Micriyyah, Kairo, 1930, 13.3 (Tol. 4) 1982, Dar el-Maaref, Kairo, © Judge Helmy Shahin, 13.4
- Archives du Ministère des Affaires étrangères, Paris, kwa ruksa ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje ya Ufaransa, p. 4.1
- Arhin, K., kwa ruksa ya Asantehene wa Ghana, 25.2
- © *Arts of Asia*, Hong Kong, Machi-Aprili 1978, uk. 89, 28.1
- Barbour, N., *Morocco*, Thames na Hudson, 1965, Paris, 19.3
- Basel Mission Archives, 25.9
- Bennet, N.R na Brooks G. E. (wah.) *New England Merchants in Africa: A history through documents, 1802-1865*, Boston University Press, Boston, 1965, © Peabody Museum of Salem, picha na Mark Sexton, 9.3
- Bennet, N. R., *Miranbo of Tanzania*, Oxford University Press, New York, 1971, © Junba la Makumbusho ya Taifa, Dar es Salaam, 10.4
- Binger, L., *Du Niger au Golf de Guinée*, Hachette, Paris, 1892, 24.2*, kwa ruksa ya Bodleian Library (shubaka na.: 710.11.s.8/1), Juz. I, uk. 19, 25.5*, 25.6**, Juz. II, 25.7*
- Bowdich, T. E. *A Mission From Cape Coast Castle to Ashantee*, John Murray, London, 1819, 25.3*
- Burton, R., *The Lake Region of Central Africa*, Longman, Green Longman na Roberts, London, 1860, Juz. II, ak. 80 and 278, © Royal Geographical Society, London, 10.2, 10.3
- Burton, R., *First Footsteps in East Africa*, Routledge na Kegan Paul Ltd, London, 1894, picha zilitolewa tena na Sasor Publisher, London, 15.4
- Cameron, V.L., *Across Africa*, Daldy, Isbister na Co, London, 1877, Juz. I, uk. 352, 12.2* *Church Missionary Gleaner*, 1855, 26.3*
- Collection Bibliothèque Générale et Archives, Rabat 18.3
- de Chassiron, Ch., *Aperçu pittoresque de la Régence de Tunis*, Imprimerie de Bénard, Paris, 1849, 17.4**
- Denham, Clapperton and Oudney, *Narrative of Travels and Discoveries in Northern and Central Africa*, London, 1826, 22.3*

- Deschamps, H. *Histoire de Madagascar*, Berger-Levrault, Paris, 1960, 16.4** (haki zote zimehifadhiwa)
- Ellis, W., *Three Visits of Madagascar*, J. Murray, London, 1858, picha ya mbele ya jalada, kwa ruksa ya Maktaba ya Uingereza, 16.6, 16.7
- Evans Pritchard, E., *The Sanusiya of Cyrenaica*, Oxford University Press, Oxford, 1949, © Oxford University Press, 17.5*
- Fagg, W. B. na Pemberton, III, J. (mh. Holcombe, Bryce), *Yoruba Sculpture of West Africa*, New York, 1962, © National Museum, Lagos, 26.1
- French National Museums, 17.3
- Frey, Colonel, *Côte Occidentale d'Afrique*, Flammarion, Paris, 1890, 20.1*
- Gamitto, A. C. P. (taf. I. Cunnison), *King Kazembe*, Atica, Lisbon, 1960, © Atica, Lisbon, 12.6*
- Holt, P.M. na Daly, M., *History of the Sudan*, Weidenfeld na Nicolson, London, 1979, kwa ruksa ya The National Trust, Kingston Lacy, Bankes Mss, 14.2, kwa ruksa ya George Weidefeld na Nicolson Ltd, London, 14.3, © BBC Hulton Picture Library, 14.5
- Ikime, O., *Merchant Prince of the Niger Delta: the rise and fall of Nana Olomu, Last Governor of the Benin River*, Heinemann, London, 1968, 27.2
- Institut fondamental d'Afrique Noire (I.F.A.N.), Dakar, 23.2
- Johnston, H.H., *British Central Africa*, Greenwood Press, London, 1897, 3.1*
- Johnston, H.H., *British Central Africa*, Methuen and Co., London, 1897, nk.421, 8.2*
- Julien, Ch. A., *Histoire de l'Algérie contemporaine: conquete et colonisation*, Presses Universitaires de France, Paris, 1964, 17.1**, 17.2**, 19.2**
- Laroui, A., *Origines sociales et culturelles du nationalisme marocain*, Maspéro, Paris, 1977, 18.4
- Lefebvre, T., *Voyage en Abyssinie (1845-54)*, Paris, picha zimetolewa na Sasor Publisher, 15.2, 15.3
- Ling Roth, H., *Great Benin, Its Custom, Art and Horrors*, Kings na Sons, Halifax, 1903 (nakala halisi kutoka kwa Globus, 1897. Juz. I, uk. xxii), 26.4, 26.5*
- Mage, E., *Voyage dans le Soudan occidental*, Hachette, Paris, 1868, © Hachette, Paris, 23.5, 23.6
- Magyar, L. *Reisen in Sud Afrika in den Jahren 1849 bis 1857*, Pest na Leipzig, 1859, 12.7*, 12.8
- M'Bokolo, E., *Noirs et Blancs en Afrique équatoriale*, Editions de l'Ecole des Hautes Etudes en sciences sociales, Paris, 1981 (picha zilitolewa kutoka du Belley, Griffon, 'le Gabon', *Le Tour du Monde*, 1865), 27.5, 27.6
- Miers, S., *Britain and the Ending of the Slave trade*, Longman, London, 1975, © The Illustrated London News Picture Library, 4.2
- Museum of the Institute of Ethiopian Studies, Addis Ababa, 15.7
- Museum of Toulouse, © Jean Dieuzaide, Toulouse, 18.1
- Museum of Versailles, photothèque, Groupe Press de la Cité, Paris, 19.1
- Mutibwa, Ph., *The Malagasy and the Europeans*, Longman, London, 1974, Direction e la Presse et de la Publication, Ministère de l'Information, Madagascar, 16.2, 16.3

- Nachtigal, G. (taf. na mh. Fisher, A. G. B. and H.J.), *Sahara and Sudan*, Hust, London, 1974, © Hust, London, Juz. II, 1980, 22.2*, 22.4*
- National Army Museum, London, 7.2
- Nigerian Information Service Centre, Ubalozzi wa Nigeria, Paris, 27.3
- Omer-Cooper, J., *The Zulu Aftermath*, Longman, London, 1966 (nakala halisi kutoka Gardiner, A. F., *Narrative of a Journey to the Zoolu country*, London, 1836), © Slide Centre Ltd, 1.1 (nakala halisi kutoka Livingstone, D. and C., *Narrative of an Expedition to the Zambezi*, John Murray Publishers, London, 1865), 8.3*
- Photothèque, Musée de l'Homme, Paris, © 26.6
- Pogge, P., *Im Reiche des Muata Jamvo*, Berlin 1880, 12.11*
- Porter, A. T., *Creoledom*, Oxford University Press, Oxford, 1963, kwa ruksa ya Foreign and Commonwealth Office Library, 3.3.
- Raison-Jourde, F., *Les Souverains de Madagascar*, Karthala, Paris, 1983, Fonds Grandidier du Musée des Collections scientifiques. Tsimbazaza, Antananarivo, 16.5
- Rassan, H., *Narrative of a British Mission to Theodore, King of Abyssinia*, Murray, London, 1869, picha zilitolewa na Sasor Publisher, London, 15.5, 15.6
- Roger Viollet, H., © Harlingue-Viollet, Paris, 28.3
- Rohlf, G., *Meine Mission nach Abessinien*, Leipzig, 1882, picha zilitolewa na Sasor Publisher, London, 15.8
- Saunders, C., *Black Leaders in African history*, Heinemann, London, 1978 (nakala halisi kutoka kwa John Aitken Chalmers, *Tiyo Soga, A Page of South African Mission Work (Vol. 1) 1877*), 3.2
- Schweinfurth, G., *The Heart of Africa*, Sampson, Low, Marston, Low na Searle, London, 1873, Juz. I, Frontispiece, 12.5*, 14.4
- Snouk Hurgronje, C., *Mekka in the latter part of the nineteenth century: daily life, customs and learning: the Muslims of the East-Indian Archipelago*, E.J. Brill, Leiden, 1870, © E. J. Brill, 28.2*
- Stanley, H.M., *Through the Dark Continent*, Sampson, Low, Marston, Low na Searle, London, 1878, Juz. I, uk. 89, 11.2*, 11.3*, uk. 474, 11.4*, uk. 322, 11.5*
- Sullivan, G. L., *Dhow chasing in Zanzibar Waters*, Frank Cass Publishers, London, 1873, © Frank Cass Publishers, 4.1*
- © The Tate Gallery, London, 13.2
- Vansina, J., *Art history in Africa*, Longman, London, 1984, © Staatl. Museum für Völkerkunde, Munich, 6.1, © Photo Institut des Musées Nationaux du Zaïre (IMNZ), no. 73.381.1.1, 73.381.2, 70.8.2 (kushoto kwenda kulia), 12.3, © The Walters Art Gallery, Baltimore, 12.9, © Museum für Völkerkunde, Berlin, 12.10, © Werner Forman Archive, London, 20.2, © Frobenius Institut, 25.4
- * kwa ruksa ya Syndics of Cambridge University Library
- ** kwa ruksa ya Bibliothèque Nationale, Paris.
- Tunasikitika kuwa hatukuweza kupata hati miliki ya wenye pleti 27.5, 27.6 na tutafuralu kupata taarifa zozote zitakazotuwzesha kupata hati miliki hizo.



Wasifu wa Mradi

B.A. OGOT¹

*Rais wa Zamani, Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi
kwa ajili ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika (1978-1983)*

Mkutano Mkuu wa UNESCO katika Kikao chake cha 16 ulimwagiza Mkurugenzi Mkuu kushughulikia usawidi wa *Historia Kuu ya Afrika*. Kazi hii kubwa ya kutekeleza mradi ilikabidhiwa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi ambayo ilianzishwa na Bodi ya Utendaji mnamo 1970. Kamati hii kwa mujibu wa Sheria iliyopitishwa na Bodi ya Utendaji ya UNESCO mnamo mwaka 1971, ina wajumbe thelathini na tisa (theluthi mbili miongoni mwao wakiwa Waafrika na theluthi moja ni watu wengine wasio Waafrika) wanaoshiriki kwa nafasi zao binafsi na kutuliwa na Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO kwa kipindi ambacho Kamati itadumu.

Kazi ya kwanza ya Kamati ilikuwa ni kufafanua sifa kuu za kazi hii. Hizi zilifafanuliwa katika kikao cha kwanza cha Kamati kama ifuatavyo:

- (a) Ingawa lengo lake ni kiwango cha juu kabisa cha kisayansi, Historia hii hainuii kuwa timilifu na ni kazi ya usawidi inayoepukana na inadi. Katika hali zake nyingi, historia hii ni taniko juu ya matatizo yanayoonyesha hali ya sasa ya maarifa na mikondo makuu ya utafiti, na haisiti kuonyesha hitilafu za mtazamo pale ambapo zipo. Kwa namna hii inaweka msingi kwa kazi za siku zijazo.
- (b) Katika kazi hii Afrika inatazamwa katika ujumla wake. Nia ni kuonyesha mahusiano ya kihistoria kati ya sehemu zote za bara ambazo mara nyingi hutengwa katika kazi ambazo zimchapishwa hadi sasa. Mahusiano ya kihistoria ya Afrika na mabara mengine yanashughulikiwa ipasavyo kwa kuchangauuliwa kuzingatia mabadilishano baina yake na athari kutoka pande

¹ Wakati wa Mikutano Mkuu wa Sita wa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi kwa ajili ya Kusawidi Historia Kuu ya Afrika (uliofanyika Brazaville Agosti 1983), uchunguzi wa wajumbe wanya ulifanyika na nafasi ya Profesa Ogot ilichukuliwa na Profesa Albert Adu Boahen.

zote na kudhihirisha, katika mwanga halisi, mchango wa Afrika kwa historia ya mwanadamu.

- (c) Kwa mahususi, *Historia Kuu ya Afrika* ni historia ya mawazo na staarabu, jamii na asasi. Imetegemezwa kwenye vyanzo vingi vya aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na mapokeo simulizi na namna za sanaa.
- (d) Kimsingi, *Historia* inatazaniwa kutokea ndani. Ingawa ni kazi ya kitaalamu, pia kwa kadri kubwa, inaakisi kwa uaminifu jinsi waandishi wa Kiafrika wanavyotazama ustaarabu wao wenyewe. Pamoja na kuandaliwa kwa mtazamo wa kimataifa, na ikichota maarifa yote ya kisayansi yaliyopo wakati huu, yapaswa pia iwe kipengele muhimu kabisa katika utambuzi wa urithi wa Kiafrika na yapaswa kudhihirisha vipengele vinavojenga umoja barani. Juhudi hii ya kutazama mambo kutokea ndani ni sifa mpya ya mradi huu na pamoja na thamani yake ya kisayansi, inapaswa kuipatia mradi umuhimu wa kujadifiwa vipana. Kwa kuonyesha sura halisi ya Afrika, *Historia* inaweza, katika enzi iliyozama kwenye mapambano ya kiuchumi na kiufundi, kutoa dhana mahususi ya amali za mwanadamu.

Kamati imeamua kuwasilisha kazi ya miaka milioni tatu ya historia ya Afrika katika majuzuu manane, kila moja likiwa na karibu kurasa mia nane za matini na mifano, picha, ramani na michoro.

Mhariri Mkuu akisaidiwa, pale inapolazimu, na wahariri wasaidizi wawili, ana jukumu la kuandaa kila juzuu. Wahariri wanachaguliwa na Kamati ama kutokana na wajumbe wake au kutoka nje kwa wingi wa theluthi mbili. Hawa wana jukumu la kuandaa majuzuu kulingana na maamuzi na mipango iliyokubaliwa na Kamati. Kuhusu mambo ya kisayansi wanaiwajibikia Kamati, au kati ya mikutano miwili ya Kamati watawajibikia Idara kuhusiana na maudhui ya majuzuu, miswada ya mwisho ya matini, mifano na kwa jumla, vipengele vya kisayansi na kiufundi vya *Historia*. Idara mwishowe huthibitisha muswada wa mwisho. Inapoonwa kwamba muswada uko tayari kuchapishwa inaukabidhi kwa Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO. Hivyo, katika kipindi kati ya Vikao Viwilj, Kamati au Idara huendelea kusimamia mradi.

Kila juzuu lina kama sura thelathini. Kila sura ni kazi ya mwandishi mkuu, akisaidiwa, inapolazimu, na mshiriki mmoja au wawili. Waandishi wanachaguliwa na Kamati kutokana na sifa na uzoefu wa kitaaluma. Waandishi wa Kiafrika hupewa upendeleo alimradi wawe na sifa zinazohitajika. Juhudi maalumu pia hufanywa kuhakikisha kwamba kila inapowezekana kanda zote za bara na vile-vile kanda nyingine zenye historia au utamaduni unaohusiana na Afrika zinapata uwakilishi sawa miongoni mwa waandishi.

Pale mhariri wa juzuu anapothibitisha matini za sura, zinapelekwa kwa wajumbe wote wa Kamati kwa uhakiki. Zaidi ya hayo, matini ya mhariri wa juzuu inawasilishwa kwa uchunguzi, kwa Kamati ya Wasomaji, iliyoundwa ndani ya Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi kulingana na uwezo wa wajumbe wake katika uwanja wa kitaaluma. Kamati ya Wasomaji inachanganua sura kimaudhui na kimuundo. Kisha Idara hutoa uthibitisho wa mwisho kwa miswada.


Utaratibu kama huu unaonckana mrefu na mgumu, unaonckana kuwa wa lazima kwani unatoa uthibitisho bora kabisa wa uhakika wa kisayansi wa *Historia Kuu ya Afrika*. Kwa hakika, kumewahi kuwepo matukio ambapo Idara imeikataa miswada au kusisitiza ifanyiwe marekebisho makubwa au hata mwandishi mwingine kuombwa asawidi sura. Hutokca pia wataalamu wenyec ujuzi wa kipindi fulani cha historia au wa swali fulani mahsus kuombwa ushauri ili kukamilisha juzuu fulani.

Kazi hii itachapishwa kwa mara ya kwanza katika matolco ya jalada gumu kwa lugha za Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu na baadaye katika matolco ya jalada laini kwa lugha hizo. Matolco yaliyofupishwa kwa lugha za Kiingereza na Kifaransa ndiyo yatatafsiriwa kwa lugha za Kiafrika. Kamati imechagua lugha za Kiswahili na Kihausa kama lugha za kwanza za Kiafrika za kufanyia tafsiri za kazi hii.

Aidha, kila juhudi itafanywa kuhakikisha *Historia Kuu ya Afrika* inachapishwa katika lugha nyingine kubwa kimataifa kama vile Kichina, Kireno, Kirusi, Kijerumani, Kiitaliano, Kihispania, Kijapani, n.k.

Hivyo, ni dhahiri kwamba hii ni kazi nzito inayotoa changamoto kubwa kwa wanahistoria wa Kiafrika na kwa wasomi kwa jumla, na vilevile kwa UNESCO ambayo kazi hii inafanywa chini yake. Hii ni kwa kuwa ni jukumu kubwa mno kuandika historia ya bara la Afrika ya miaka milioni tatu iliyopita kwa kutumia kanuni makini kabisa za kitaaluma na kulazimika kuwahusisha wataalamu kutoka nchi, tamaduni, itikadi na mahusiano ya kihistoria tofauti. Mradi huu unabeba peo kubwa za mambo ya bara, ya kimataifa na ya taaluma mbalimbali.

Kwa kuhitimisha, ningependa kusisitiza umuhimu wa kazi hii kwa Afrika na dunia. Katika kipindi ambamo watu wa bara la Afrika wanajitahidi kuunda umoja na ushirikiano mkubwa ili kutoa mweloleo kwa mwenendo wa maisha yao, uclewa muafaka wa kale ya Afrika na utambuzi wa uhusiano midngoni mwa Waafrika na baina ya Afrika na mabara mengine, usingekuwa tu mchango mkubwa kwa maclewano miongoni mwa watu duniani bali pia chanzo cha maarifa ya urithi wa kitamaduni ambacho ni cha wataalamu wote.



Maelezo kuhusu Wendo


Imckubaliwa kufuata utaratibu ufuatao wa kuandika tarehe. Ama kuhusu kipindi kabla ya historia, tarehe zinaweza kuandikwa kwa njia mbili.

Njia ya kwanza ni kwa kurejca enzi ya sasa yaani tarehe KS (Kabla ya Sasa), mwaka unaorejewa ukiwa ni + 1950; tarehe zote zinakuwa hasi kuhusiana na + 1950.

Njia nyingine ni kwa kurejca mwanzo wa enzi ya Ukristo. Kuhusiana na enzi hii, tarehe huwakilishwa kwa kutumia alama + au - kabla ya tarehe. Zinaporejewa kame, vifungu KK na WK nafasi yake huhukuliwa na 'kabla ya enzi ya Ukristo' na '-a enzi ya Ukristo'.

Baadhi ya mifano ni kama hii lfuatayo:

- (i) $230 \text{ KS} = - 350$
- (ii) $2900 \text{ KK} = - 2900$
 $1800 \text{ WK} = + 1800$
- (iii) $\text{Kame ya tano KK} = \text{Kame ya tano kabla ya enzi ya Ukristo}$
 $\text{Kame ya tatu WK} = \text{Kame ya tatu ya enzi ya Ukristo.}$



*Wanakamati wa Kamati ya
Kimataifa ya Kisayansi ya
Kusawidi Historia Kuu ya Afrika*

Tarehe zilizotajwa chini zinaonyesha tarehe za kuwa wajumbe

Profesa J.F.A. Ajayi
(Nigeria), 1971
Mhariri Juzuu VI

Profesa F.A. Albuquerque Mourao
(Brazil), tangu 1975

Profesa A. Adu Boahen
(Ghana), tangu 1971
Mhariri Juzuu VII

Hayati H.E. Boubou Hama
(Niger), 1971- 8 (alijiuzulu 1978);
alifariki 1982

Dkt. (Bibi) Mutumba M. Bull
(Zambia), tangu 1971

Profesa P. Chanaiwa
(Zimbabwe) tangu 1975

Profesa P.D. Curtin
(Marekani), tangu 1975

Profesa J. Devisse
(Ufaransa), tangu 1971

Profesa M. Difuila
(Angola) kuanzia 1978

Hayati Profesa Cheikh Anta Diop
(Senegal), 1971- 86; alifariki 1986

Profesa H. Djait
(Tunisia), tangu 1975

Profesa J.D. Fage
(Uingereza), 1971 - 81 (alijiuzulu)

H.E.M. El Fasi
(Moroko), tangu 1971
Mhariri Juzuu III

Hayati Profesa J.L. Franco
(Cuba), tangu 1971; alifariki 1989

Hayati Bw. M.H.I. Galaal
(Somalia), 1971 - 81;
alifariki 1981

Profesa Dkt. V.L. Grottanelli
(Italia), tangu 1971

Profesa E. Haberland
(Ujerumani Magharibi),
tangu 1971

Dakta Aklilu Habte
(Ethiopia), tangu 1971

H.E.A. Hampaté Bâ
(Mali), 1971 - 8;
alijiuzulu

Dkt. I.S. El-Hareir
(Libya), tanqu 1978

Dkt. I. Hrbek
(Chekoslovakia), tangu 1971
Mhariri Msaidizi
Juzuu III

Dkt. (Bibi) A. Jones
(Liberia); tangu 1971

Hayati Abbe Alexis Kagame
(Rwanda), 1971 - 81; alifariki 1981

Profesa I.N. Kimambo
(Tanzania), tangu 1971

Profesa J. Ki-Zerbo
(Burkina Faso), tangu 1971
Mhariri Juzuu I

Bw. D. Laya
(Niger), tangu 1979

Dkt. A. Letnev
(Urusi), tangu 1971

Dkt. G. Mokhtar
(Misri), tangu 1971
Mhariri Juzuu II

Profesa P. Mutibwa
(Uganda), tangu 1975

Profesa D.T. Niane
(Senegal), tangu 1971
Mhariri Juzuu IV

Profesa L.D. Ngcongco
(Botswana), tangu 1971

Profesa T. Obenga
(Jamhuri ya Watu wa Kongo),
tangu 1975

Profesa B.A. Ogot
(Kenya), tangu 1971
Mhariri Juzuu V

Profesa C. Kavoajanahary
(Madagaska), tangu 1971

Hayati Profesa W. Rodney
(Guyana), 1979 - 80; alifariki 1980

Hayati Profesa M. Shibeika
(Sudan), 1971 - 80; alifariki 1980

Profesa Y.A. Talib
(Singapore), tangu 1975

Hayati Profesa A. Teixeira da Mota
(Ureno), 1978 - 82; alifariki 1982

Mgr T. Tshibangu
(Zaire), tangu 1971

Profesa J. Vansina
(Ubelgiji), tangu 1971

Hayati Mheshimiwa Dkt. E. Williams
(Trinidad na Tobago), 1976-8;
alijiuzulu 1978; alifariki 1980

Profesa A.A. Mazrui
(Kenya)
Mhariri Juzuu VIII,
Siyo mwanakamati

Profesa C. Wondji
(Ivory Coast)
Mhariri Msaidizi wa Juzuu VIII
Siyo mwanakamati


Ukatibu wa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi
A. Gatera Mkurugenzi
Kitengo cha Taaaluma za Utamaduni na
Sera
1, rue Miollis, 75015 Paris

Wasifu wa waandishi waliochangia kwenye toleo kuu

*Toleo lililofupishwalilitayarishwa kutokana na matini za toleo kuu
lililoandikwa na waandishi wafuatao:*

- UTANGULIZI G. Mokhtar (Misri); mtaalamu wa akiolojia; mwandishi wa machapisho mengi kuhusu historia ya kale ya Misri; alikuwa Mkurugenzi wa Huduma za Mambo ya Kale.
- SURA 1 Cheikh Anta Diop (Senegal); mtaalamu wa sayansi za jamii; mwandishi wa kazi nyingi na makala kuhusu Afrika na asili ya binadamu; Mkurugenzi wa Maabara ya Radio-kaboni, Chuo kikuu cha Dakar.
- SURA 2 A. Abu Bakr (Misri); mtaalamu wa historia ya kale ya Misri na Unubi; mwandishi wa machapisho mengi kuhusu Misri ya Kale; Profesa kwenye Chuo Kikuu cha Kairo; amefariki.
- SURA 3 J Yoyotte (Ufaransa); mtaalamu wa Taaluma za Misri, mwandishi wa machapisho mengi kuhusu taaluma za Misri, Mkurugenzi wa Taaluma kwenye taasisi ya *Ecole Pratique des Hautes Etudes*.
- SURA 4 A.H. Zayed (Misri); mtaalamu wa Taaluma za Misri na historia ya kale; mwandishi wa kazi nyingi na makala kuhusu Misri ya Kale; Profesa wa Historia ya Kale.
- SURA 5 R. El Nadoury (Misri); mtaalamu wa historia ya kale; mwandishi wa kazi nyingi na makala kuhusu historia ya Maghrib na Misri; Profesa wa Historia ya Kale na Makamu wa Mwenyekiti, Kitivo cha Sanaa, Chuo Kikuu cha Alexandria.
- SURA 6 H. Riad (Misri) mtaalamu wa historia na akiolojia; mwandishi wa kazi nyingi kuhusu vipindi vya Farao na Graeco-roman; Msimamizi Mkuu wa Jumba la Makumbusho la Kairo.
- SURA 7 S Donadoni (Italia); mtaalamu wa historia ya Misri ya Kale; mwandishi wa kazi nyingi kuhusu historia ya utamaduni; Profesa kwenye Chuo Kikuu cha Rome.
- SURA 8 S. Adam (Misri) mtaalamu wa historia na akiolojia ya Misri; mwandishi wa machapisho mengi kuhusu Misri ya Kale; Mkurugenzi wa Kituo cha kutunzia Nyaraka na Taaluma za Sanaa na Ustaarabu wa Misri ya Kale.
- SURA 9 N.M. Sherif (Sudani); mtaalamu wa akiolojia; mwandishi wa kazi nyingi kuhusu akiolojia ya Sudani. Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa ya Khartoum.
- SURA 10 J. Leclant (Ufaransa); mtaalamu wa taaluma za Misri; mwandishi wa kazi nyingi na makala kuhusu Misri ya Kale; Profesa huko Sorbonne; Mjumbe wa *Academic des Inscriptions et Belles Lettres*.
- SURA 11 A.A. Hakem (Sudan); Mtaalamu wa historia ya Kale; mwandishi wa kazi nyingi kuhusu Sudan ya Kale; Mkuu wa Idara ya Historia, Chuo Kikuu cha Khartoum.
- SURA 12 K. Michalowski (Poland); Mtaalamu wa akiolojia ya Mediterani; mwandishi wa machapisho mengi kuhusu sanaa za Misri ya Kale; Naibu Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa, Warsaw.
- SURA 13 H. de Contenson (Ufaransa) mtaalamu wa historia ya Afrika; mwandishi wa kazi zihusuzo akiolojia ya Ethiopia na Unubi ya Kikristo; alijishughulisha na utafiti kwenye Kituo cha Taifa cha Utafiti wa Kisayansi (CNRS).
- SURA 14 A. Anfray (Ufaransa); mtaalamu wa akiolojia; mwandishi wa makala kadhaa kuhusu utafiti wa kiakiolojia huko Ethiopia; Mkuu wa Msafara wa Kiakiolojia na Wafaransa huko Ethiopia.

- SURA 15 Y.M. Kobishanov (Urusi); mwanahistoria ; mwandishi wa makala nyingi kuhusu anthropolojia ya Afrika; mjumbe wa Akademia ya Sayansi ya Urusi.
- SURA 16 Tekle Isadik Mekouria (Ethiopia); mwanahistoria; mwandishi; mtaalamu wa historia ya Siasa, Uchumi na Jamii ya Ethiopia kuanzia asili yake hadi karne ya ishirini; amestaaafu.
- SURA 17 J. Desanges (Ufaransa); mtaalamu wa historia ya Afrika ya Kale; mwandishi wa kazi nyingi na makala kuhusu Afrika ya Kale; mhadhiri Chuo Kikuu cha Nantes.
- SURA 18 B.H. Warmington (Uingereza); mtaalamu wa historia ya Roma ya Kale; mwandishi wa kazi nyingi kuhusu Afrika ya Kaskazini; mhadhiri wa Historia ya Kale.
- SURA 19 A. Mahjoubi (Tunisia); mtaalamu wa Historia ya Kale ya Afrika ya Kaskazini; mwandishi wa kazi nyingi na makala kuhusu akiolojia ya Tunisia; Profesa Msaidizi kwenye Chuo Kikuu cha Tunis
P. Salama (Algeria); mwanaakiolojia; mtaalamu wa historia ya asasi za Kale za Maghrib; Profesa kwenye Chuo Kikuu cha Algiers.
- SURA 20 P. Salama
- SURA 21 M. Posnansky (Uingereza); mwanahistoria na mwanaakiolojia; mwandishi wa kazi nyingi muhimu kuhusu historia ya kiakiolojia ya Afrika Mashariki.
- SURA 22 A.M.H. Sheriff (Tanzania); mtaalamu wa historia ya biashara ya utumwa Afrika Mashariki mhadhiri Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
- SURA 23 J.E.G. Futton (Uingereza); mtaalamu wa historia ya awali, mwandishi wa kazi nyingi na makala kuhusu historia ya Afrika; alikuwa Mwenyekiti kwenye Idara ya Akiolojia, Chuo Kikuu cha Oxford.
- SURA 24 B. Wai-Andah (Nigeria); mtaalamu wa akiolojia; mwandishi wa kazi nyingi kuhusu akiolojia ya Afrika ya Kati; mhadhiri Chuo Kikuu cha Ibadan.
- SURA 25 F. Van Noten (Ubelgiji); mtaalamu wa historia ya awali na akiolojia; mwandishi wa kazi nyingi na mchapisho kuhusu historia ya awali ya Afrika ya Kati; msimamizi wa Nyumba ya Makumbusho ya Kifalme Kuhusu Historia ya Awali na Akiolojia.
- SURA 26 J.E. Parkington (Uingereza); mwanaakiolojia; mwandishi wa kazi za historia ya awali ya Kusini mwa Afrika; Profesa wa Akiolojia.
- SURA 27 D.W. Philipson (Uingereza); mwanaakiolojia; mwandishi wa kazi za akiolojia ya Afrika Mashariki na Kusini.
- SURA 28 P. Verin (Ufaransa); mtaalamu wa historia na akiolojia; mwandishi wa machapisho mengi kuhusu Madagaska na kuhusu Madagaska ya Hindi; anashughulikia utafiti kuhusu Madagaska.
- SURA 29 M. Posnansky
- HITIMISHO G. Mokhtar.



Utangulizi

Juzuu hili la *Historia Kuu ya Afrika* linazungumzia kipindi kirefu cha historia ya bara la Afrika kinachozungumzwa tangu mwisho wa enzi ya Neolithiki (enzi ya mawe), yaani tangu elfia ya nane kabla ya wakati wetu hadi karne ya saba ya wakati wetu.

Kipindi hicho ambacho ni cha takriban miaka elfu tisa ya historia ya Afrika, kimegawanywa katika kanda kuu nne za kijiojografia:

- (1) bonde la Mto Nili, Misri na Unubi (Sura 1 hadi 12)
- (2) nyanda za juu za Uhabeshi (Sura 13 hadi 16)
- (3) sehemu ile ya Afrika ambayo baadaye ilijulikana kama “Maghareb” na bara yake ya Sahara (Sura 17 hadi 20)
- (4) sehemu ya Afrika iliyobaki pamoja na visiwa vya Kiafrika katika Bahari Kuu ya Hindi (Sura 21 hadi 29).

Mgawanyo huu umetokana zaidi na tabia ya kutenga kimkoa utafiti katika historia ya Afrika. Pengine kinantiki juzuu hili lingefaa lipangwe kufuatana na mgawanyo mikuu ya kiekolojia ya bara la Afrika ambamo hali ya maisha ya watu waishimo ni ya aina moja bila ya kuathirika na vikwazo vya kimaumbile.

Mgawanyo huu wa kiekolojia, hata lau kama ungekuwa wa kuridhisha zaidi kuliko ule uliofanywa katika juzuu hili, usingewezekana kwa sababu nyaraka kuukuu za Afrika, ambazo ni ripoti za uchimbaji au za matini na usawiri, kwa baadhi ya mikoa hukusanywa, huainishwa na kuchapishwa kwa mpangilio usiofuata misingi maalumu na ambao hauhusiani na hali ya sasa ya Afrika. Hata hivyo, huwa ni vigumu sana kuisaili mipangilio ya namna hii.

Juzuu hili la *Historia Kuu ya Afrika*, halina budi kutegemea tathmini zisizokamilika na za muda kuliko juzuu lililolitangulia. Hii ni kwa sababu kipindi kinachozungumziwa ni kinyenyezi, kutokana na uhaba wa vyanzo vya habari kwa jumla na hususan vyanzo vya habari vyenye tarehe thabiti — isipokuwa kwa baadhi ya maeneo kama vile Bonde la Mto Nili na “Maghareb” ambayo kwa bahati habari zake zinapatikana. Kwa sehemu kubwa ya bara hili vyanzo thabiti vya mambo mengi kwa kipindi tunachozungumzia ni nadra sana kupatikana.

Jambo jingine pia linalohitaji kusisitizwa ni kwamba vyanzo vya habari vya kiakolojia vilivyopo na ambavyo vyaweza kutumiwa na wanahistoria havitoshi

kabisa. Utafiti wa kiakiolojia haukuenea sawa barani Afrika kwa jumla. Utafiti wa aina hii umefanywa vizuri zaidi sehemu za mwambao, sehemu za bara kwa upande wa kaskazini, na fauka ya yote, katika Bonde la Mto Nili kutoka bahari ya Mediterania hadi Maporomoko ya Pili.

Uhaba huu wa habari za kiakiolojia hauwezi kujalizwa kwa ripoti za wasafiri wa kigeni, watu waliopo walioishi wakati wa matukio au mambo ambayo yanahusu juzuu hili. Vipingamizi vya kijiografia na hasa ukubwa wa bara hili, viliwakatisha tamaa wageni kuingia ndani zaidi katika bara. Itafahamika kuwa kwa kadri ya ujuzi tulionao sasa, Afrika ndilo bara pekee ambapo safari kwenye mwambao wake zimetoa taarifa muhimu za historia.

Ingawa mambo ni hivyo, tathmini zisizokamilika za historia ya Afrika tangu -8000 hadi + 700 si za kudhaniwa; zimetokana na maelezo ambayo yapo lakini ambayo kwa hakika ni nadra na yasiyotosheleza. Kazi ya waandishi wa historia hii imekuwa ya kukusanya, kupima na kutathmini vyanzo hivyo kwa uangalifu sana. Wakiwa ni wataalamu wanaohusika na mikoa ambayo historia yake inatafutwa, wataalamu hao wametoa ufafanuzi unaoridhisha kulingana na data walizo nazo. Tathmini zao hizo ambazo zitahitaji kuchambuliwa tena wakati vyanzo vingine vya habari vitakapopatikana, twafikiria zitawatia moyo na kutoa miongozo ya utafiti kwa wanahistoria wa siku za mbele.

Tathmini ya wingi wa watu katika Afrika wakati wa kipindi kati ya - 8000 na -5000, ni muhimu sana kwani ndicho kipindi cha kuzaliwa kwa tamaduni ambazo baadaye zilitofautiana. Aidha hali ya idadi ya watu kwa wakati huo ingeweza kuathiri chanzo na maendeleo ya sanaa ya uandishi: idadi kubwa au idadi ndogo ya watu huweza kushawishi au kuondoa haja ya kuendeleza sanaa ya uandishi. Utamaduni wa Misri ya Kale, kinyume na sehemu nyingine za Afrika ya wakati huo, pengine ulitokana na msongamano mkubwa wa watu kwenye kingo za Mto wa Nili, kati ya Maporomoko ya Kwanza na sehemu ya kusini ya Delta. Hali hii polepole ililazimisha matumizi ya inaandishi, katika kuratibu mfumo wa umwagiliaji ambao ulikuwa wa muhimu kwa maisha ya watu. Kusini mwa Maporomoko ya Aswani, kinyume na hali kaskazini, matumizi ya maandishi hayakuhitajika kwa sababu sehemu hii ilikaliwa na vikundi vidogo vidogo vya watu ambavyo havikutegemeana. Hivyo ni jambo la kusikitisha kuwa suala la msongamano wa watu kwa kipindi hicho halijaweza kuchunguzwa na kuthibitishwa kisayansi.

Suala la mwisho lahusu ekolojia, ambayo ilibadilika kwa kiasi kikubwa kadri wakati ulivyopita na pia ilikuwa na nafasi muhimu. Mazingira ya wakati wa kipindi kati ya - 7000 na - 2400, kipindi cha miaka 4600, ambacho ni zaidi ya nusu ya kipindi kiziina kinachozingatiwa katika juzuu hili, yalikuwa tofauti kabisa na yale yaliyokuwepo baada ya nusu ya pili ya elfia ya tatu. Mazingira hayo ya baadaye, ambayo yaelekea yalifanana sana na mazingira ya sasa, yaliukilia sana sulubu za jamii za watu zilizoishi humo. Maisha ya kijumuiya hayawi, wala hayawezi kuwa sawa katika kanda kubwa za jangwa za kitropiki, za kusini na kaskazini, na yale katika

kanda za misitu mikubwa ya Ikweta; au maisha ya mtambao wa milima kuwa sawa na yale katika mabonde ya mito mikubwa; au yale ya makokoni kufanana na yale ya maziwa makubwa. Athari za kanda kuu hizi za kiekolojia ni ya muhimu sana katika kukua kwa njia ambazo zilirahisisha safari kutoka eneo moja hadi jingine, kwa mfano, kutoka Maghrib au milima ya Ethiopia au Bonde la Nili kuelekea sehemu za kati za Mito Kongo, Niger na Senegal, au pia, kutoka pwani ya Atlantiki kuelekea Bahari ya Shamu na Bahari ya Hindi. Lakini njia hizi bado hazijachunguzwa sawasawa. Inafikiriwa tu kuwa njia hizo zilikuwapo bila uthibitisho wowote wa hakika. Uchunguzi wa hatua kwa hatua wa kiakiolojia juu ya njia kuu hizi utatufundisha mambo mengi kuhusu historia ya Afrika. Mafanikio ya utafiti wa kiakiolojia kuhusu njia hizi ndiyo yatakayotuwezesha kuelewa hali ya uhamaji ilivyokuwa kati ya - 8000 na - 2500 ambacho ni kipindi kilichotangulia mabadiliko makubwa ya hali ya hewa yaliyoambatana na mtwanyiko wa vikundi mbalimbali vya watu barani Afrika.

Kama itakavyoonekana, sura za juzuu la pili la *Historia Kuu ya Afrika* zinaonyesha zaidi mahali pa kuanzia utafiti katika siku za mbele kuliko kurudia hakika zilizokwishathibitishwa. Kwa bahati mbaya, hakika kama hizi hupatikana kwa nadra sana isipokuwa zile zinazohusu baadhi ya sehemu fulani ndogo tu barani Afrika.

Misri: hali ya kijiografia

Kwa sehemu kubwa Bonde la Mto Nili lipo mkabala na Bahari ya Shamu na Bahari ya Hindi. Inawezekana kulifikia bonde hili kutoka miambao ya bahari hizi mbili kwa kupitia kwenye mabonde yaliyosulubiana na mwelekeo wake. Kati ya latitudo ya nane na Bahari ya Mediterania bonde hili linapanuliwa sana kwa upande wa Magharibi na mabonde mengine yanayoanzia huko Chad, Tibesti na Enedi. Mwisho, delta iliyo pana, Oasisi za Libya na shingo ya nchi ya Suez vyote kwa pamoja vimefanya mwingio wa Mto Nili kwenye Bahari ya Mediterania kuwa wa upana mkubwa. Hivyo kuwa wazi kwa bonde hili la Nili kutokea pande zote kumefanya sehemu hii iwe yenye mahusiano ya fadhila, siyo tu kati ya mikoa ya Afrika iliyopakana nayo bali hata na sehemu za Arabuni na nchi zilizo kandokando ya Bahari ya Hindi na Mediterania.

Hata hivyo, umuhimu wa nafasi hii ya kijiografia ulibadilika kufuatana na wakati. Katika Afrika, mwisho wa enzi ya Neolithiki uliambatana na kipindi cha mvua kubwa kilichodumu hadi - 2300 kikiwa kimekumba kizio cha kaskazini. Katika kipindi hicho ambacho kilienea tangu elfia ya saba hadi ya tatu ya kabla ya enzi yetu, mikoa ya mashariki na magharibi ya Mto Nili ilikuwa na hali za hewa muafaka kwa makazi ya wanadamu. Kwa hivyo, mawasiliano na mahusiano kati ya mashariki na magharibi ya bara hili yalikuwa muhimu kama yale yaliyokwishaanzishwa kati ya sehemu ya kaskazini na ile ya kusini.

Kinyume chake, baada ya - 2400, kukauka kwa sehemu ile ya Afrika iliyoko kati

ya latitudo kumi na tatu na kumi na tano kaskazini kulifanya bonde la Nili kuwa njia kuu ya mawasiliano kati ya mwambao wa bara ya Mediterania na sehemu ambayo sasa inajulikana kama Afrika kusini mwa Sahara. Ni kupitia njia hii ya bonde la Nili ndipo malighafi, vitu vilivyoundwa, na bila shaka inawazo, yalipita toka kaskazini hadi kusini na vivyo hivyo kinyume chake.

Ni dhahiri kuwa kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa, katika kipindi kati ya - 7000 na - 2400, nafasi ya kijiografia ya sehemu ya kati ya Bonde la Mto Nili, ilivyokuwa pia huko Misri, hayakuwa na umuhimu au athari, sawa na jinsi hali ilivyotokea kuwa katika miaka ya baadaye. Katika miaka hiyo, makundi ya watu na tamaduni zao yaliweza kweenda na kurudi pasi vikwazo katika kizio cha kaskazini baina ya inashariki na magharibi na baina ya kusini na kaskazini. Hiki kilikuwa kipindi cha kuundwa na kutengana kwa tamaduni za Afrika.


Lakini tangu - 2400 hadi karne ya saba ya enzi yetu, bonde la Nili likawa njia yenye kupendelewa zaidi kati ya kaskazini na kusini mwa bara hili. Na kupitia njia ya bonde hilo ndipo inabadilishau ya aina mbalimbali yalifanyika kati ya Afrika ya watu weusi na bonde la Mediterania.

Vyanzo vya historia ya bonde la Nili siku za kale

Kumbukumbu tulizonazo ni za aina ya akiolojia na maandishi ya kale. Ni hivi karibuni tu ndipo jitihada ya kukusanywa inabaki ya akiolojia katika eneo hili zilipofanywa kwa ustadi. Lakini vyanzo vya kimaandishi ni vya zamani sana.

Miaka mingi hata kabla ya Jean - Francois Champollion (+1790 hadi + 1932) hajatoa tafsiri ya hati ya Kimisri. Maajabu ya Misri yalikuwa yamekwisha waua watu wengi moyo wa udadisi. Mapeina tangu karne ya sita kabla ya enzi zetu Wagriki walikuwa wamekwisha ashiria tofauti kati ya desturi na imani zao na zile za bonde la Nili. Mmoja kati ya hao waliofanya jitihada kubwa ni Herodotus. Wafalme wa Kitolemi pia waliandikisha historia ya Misri ya Mafarao katika karne ya tatu kabla ya enzi yetu ili wawaelewe vizuri raia wao wapya. Manetho, ambaye alikuwa Misri, alikabidhiwa kazi ya kuandika historia hii kuu ya Misri. Alipata nafasi ya kupitia nyaraka kuukuu za kale. Kama kazi yake ingebakia hadi leo ingesaidia kuondoa mashaka katika historia ya kale ya Misri. Kwa bahati mbaya kazi hii ilitoweka wakati Maktaba ya Alexandria ilipotekezwa. Hata hivyo vidondo vilivyohifadhiwa katika majuzuu mbalimbali vikiwa vimekusanywa kwa madhuni ya kuelezea mkabala fulani, bado vinatoa kionzi madhubuti cha historia ya Misri. Kwa hakika, Falme thelathini na moja za Kimanethonia hadi leo zimekuwa ni msingi madhubuti wa mtiririko wa kitarehe wa historia ya Misri.

Amri ya Mfalme Justinian I ya kuzifunga hekalu za mwisho za Misri katika karne ya sita ya enzi zetu, ilisababisha watu waache kutumia namna mbalimbali za maandishi ya Kifarao. Lugha yao ya maongezi tu ndiyo iliendelea kuwepo katika kikoptiki. Vyanzo vya kimaandishi navyo viliacha kutumiwa muda ulivyopita. Ni



Jiwe la Palermo (A.H. Gardiner, Misri ya Mafarao, OUP, 1961)



Mafunjo ya Turin (A.H. Gardiner, Oxford 1954)

mnamo mwaka +1822, *Jiwe la Palermo* (A.H. Gardiner, *Misri ya Mfarao*, OUP, 1961). *Mafunjo ya Turin* (A.H. Gardiner, *Oxford*, 1954) maandishi hayo yalipofumbuliwa na Jean -Francois Champollion ndipo kwa inara nyingine tena takaweza kusoma nyaraka za kale zilizoandikwa na Wamisri wenyewe.

Nyaraka hizo za historia ya Misri zinahitaji kutumiwa kwa uangalifu maana ni za aina maalum. Aghalabu nyaraka hizo ziliandikwa kwa madhumuni maalum: kueleza mafanikio ya Farao fulani au kuhakikisha kuwa Farao huyo anaabudiwa maisha milele. Katika aina hizi mbili za nyaraka kuna matini ndefu na taswira za kihistoria ambazo zimepamba baadhi ya sehemu za hekalu za Misri. Vilevile humo mna orodha ya watukufu wa kale kama zile zilizonakishiwa katika hekalu za Karnak wakati wa ufalme wa kumi na nane na katika Ab-ydos wakati wa ufalme wa kumi na tisa.

Katika kutengeneza orodha za kifalme waandishi walitumia hati zilizoandikwa na mapadri au watumishi wa wafalme. Hivyo ingemaanisha kwamba kungekuwepo nyaraka rasmi zilizotunzwa vizuri. Kwa bahati mbaya, nyaraka mbili tu ndizo zimewahi kupatikana, nazo pia hazikukamilika. Nyaraka hizo ni:

Jiwe la Palermo (linaitwa hivyo kwa sababu sehemu kubwa ya waraka huo umehifadhiwa katika makumbusho ya mji huo wa Sisili) ni bamba la mwamba asili ulionakishiwa pande zote mbili, ambalo limetuhifadhi majina ya Mafarao waliotawala Misri tangu mwanzoni hadi ufalme wa tano, kwenye - 2450. Kuanzia ufalme wa tatu, *Jiwe la Palermo* limeorodhesha majina ya wafalme kwa utaratibu wa utawala wao pamoja na matokeo muhimu ya mwaka hadi mwaka katika kila enzi.

Mafunjo ya Turin yaliohifadhiwa katika makumbusho ya mji wa Turin nchini Italia ni muhimu kama jiwe la Palermo, ingawa mafunjo hayo yameorodhesha tu majina ya watawala, pamoja na itifaki zao na idadi ya miaka, miezi na siku walizotawala kwa utaratibu wa kikronolojia. Mafunjo haya yanatoa orodha kamili ya Mafarao wote tangu miaka ya awali hadi kwenye mwaka - 1200.

Kronolojia ya Misri

Jiwe la Palermo, Mafunjo ya Turin na orodha za wafalme kwenye makumbusho mengineyo ni ya muhimu sana kwa historia ya Misri kwa vile Wamisri hawakutumia enzi za mfululizo au za mzunguko kama mifumo tunayotumia sisi kama vile, kabla au baada ya Kristo, miaka ya Hijra au ya Olympiki. Mahesabu yao yalikitwa kwenye nafsi ya Farao mwenyewe na kila tarehe ilitajwa kwa jina la mfalme aliyetawala wakati waraka fulani ulipoandikwa. Desturi hii inaeleza umuhimu wa kuanzisha utaratibu wa kronolojia na kujua majina ya Mafarao wote waliotawala na muda wa utawala wa kila mmoja wao. Katika kuandaa kronolojia kama hii mgogoro luzuka kuhusu utaratibu wa kurithiana nadaraka ya kifalme katika vipindi fulani, hasa pale Mafunjo ya Turin na Jiwe la Palermo yasipoonyesha chochote. Taarifa kamili juu ya

urefu wa vipindi walimotawala baadhi ya wafalme nayo pia haijulikani. Tunachoweza kuwa na hakika nacho lau kwa uchache ni tarehe ya awali ya Farao fulani, lakini yawezekana utawala wake ulidumu muda mrefu hata baada ya kujengwa kwa mnara wa makumbusho yake unaoonyesha tarehe ile tuijuayo.

Hata pamoja na mapengo hayo, tarehe zote zilizotajwa katika kumbakumbu hizo tulizonazo zikijumlishwa hufikia zaidi ya miaka 4000. Huo ni utaratibu mrefu wa kronolojia uliokubaliwa na wataalamu wa awali wa Mambo ya Misri hadi mwaka +1900. Lakini iling'amuliwa baadaye kwamba kipindi cha muda mrefu kama huo kisingewezekana, kwani utafiti zaidi ulidhihirisha, kwanza, kuwa katika vipindi fulani Mafarao kadha walitawala kwa wakati mmoja na kwamba kulikuwepo falme sambamba, na pili, kuwa wakati mwingine Farao fulani alimshirikisha mwanee mmojawapo kama mtawala mshiriki. Kwa kuwa kila mmoja wa wafalme hao aliandika tarehe kwenye makumbusho yake kufuatana na enzi yake mwenyewe, kulikuwa na kurudiarudia. Kwa kujumlisha tawala za falme sambamba na zile za watawala washiriki, pamoja na vipindi vya utawala wa wafalme rasmi, hapakuwa na budi ila kufikia jumla iliyoonyesha kipindi cha muda mrefu mno.

Pengine isingewezekana kutatua tatizo hili kama hali mojawapo maalumu ya kalenda ya kale ya Mafarao haikutoa kiunzi cha kronolojia chenye uhakika. Hali hii ilihusisha kalenda hiyo na utaratibu wa kudumu wa kinajimu ambao jedwali zao ziliweza kuthibitishwa kwa urahisi. Hapa tunazungumzia kutokea kwa nyota ya Sothis ijulikanayo leo hii kwa jina Sirius. Kutokea kwa nyota hii huandamana kwenye latitudo ya Heliopolis - Mephis. Tukio hili limejulikana kama "kutokea kwa Sothis Kiheliaki" na lilichunguzwa na kurekodiwa zama za kale na Wamisri. Taarifa juu ya tukio hili ndizo zimetupatia tarehe za "Sothis" na ndio msingi wa utaratibu wa kronolojia ya Misri leo hii.

Tangu mwanzo, Wamisri, kama watu wengi wa zamani, inaelekea walitumia kalenda ya mwezi, hasa katika kupanga tarehe za maadhimisho ya kidini. Lakini pamoja na kalenda hiyo ya kinajimu walitumia pia kalenda nyingine, kalenda ya asilia iliyoogemea marudio ya kipindi hadi kipindi ya tukio ambalo lilikuwa muhimu kwa maisha yao, yaani mafuriko ya mto wa Nili.

Katika kalenda hiyo msimu wa kwanza wa mwaka ulioitwa "Akhet" katika Kimisri, ulianza kwa mafuriko. Kwa muda wa miezi minne hivi makonde yalikuwa yamejaa maji. Msimu uliofuata maji yalianza kunyauka kidogokidogo na hivyo ardhi ikawa tayari kwa kupanda mbegu. Msimu huu ulijulikana kama Peret yenye maana "kutokeza nje." Katika msimu wa tatu na wa mwisho, Wamisri walivuna na halafu kuweka ghalani mavuno yao. Huu ulikuwa msimu wa "Shemou."

Kwa sababu zao zozote zile ziwazo, Wamisri, kwa kuhusisha mwanzo wa mafuriko, na hivyo siku ya kwanza ya mwaka mpya, na shani hii ya kinajimu, wametupatia njia ya kupanga vigezo maalumu vya kuelewa historia yao ndefu.

Kwenye latitudo ya Memphis mwanzo wa mafuriko ulikuwa katikati ya mwezi wa Julai. Kuzingatia jambo hilo kwa miaka michache kulitoshleza kuwaonyesha

Wamisri kuwa mafuriko hayo yalikuwa yanatokea kwa wastani kila baada ya siku 365. Kwa hiyo, waligawa mwaka wao wa misimu mitatu ya kimatendo, katika miezi kumi na miwili yenye siku thelathini kila moja. Kila msimu ulichukua muda wa miezi minne. Kwa kuongeza siku 5 zaidi waandishi walipata mwaka wa siku 365 ambao ulikuwa ndio mzuri zaidi kuliko miaka yote iliyokuwa ikitunika zamani. Hata hivyo, ingawa utaratibu wa kuugawa mwaka namna hiyo ulikuwa mzuri sana, lakini haukuwa kamili. Kwa hakika, dunia haitimizi mzunguko wake wa jua katika siku 365, bali katika siku 365¼. Kila baada ya miaka minne, mwaka rasmi wa Misri uliselelea kwa siku moja nyuma ya mwaka wa kinajimu, na ni baada ya miaka 1460 - kipindi kijulikanacho kama kipindi cha Sothis - ndipo matukio natatu, kucha kwa jua, kutokeza kwa nyota Sothis na mwanzo wa mafuriko, yalipotokea pamoja katika siku ya kwanza ya mwaka rasmi.

Hii tofauti iliyoonyeshwa kati ya namna mbiliza kuhesabu mwaka inekuwa na matokeo muhimu: inewasaidia wanajimu wa sasa kugundua ni lini Wamisri walianza kutumia kalenda yao, tarehe ambayoni lazima ilingane na mwanzo wa kipindi cha Kisothi.

Kwa kuchanganya tarehe hizi za kinajimu na tarehe linganifu zilizotokana na nyaraka tulizonazo - Mafunjo ya Turin na Jiwe la Palerino, na makumbusho ya tarehe ya enzi mbalimbali - tumeweza kufikia msingi wa utaratibu wa kronolojia ambao ni wenye uhakika kuliko yote katika Masharki ya Kale. Utaratibu huo wa kronolojia unaonyesha, mwanzo wa historia ya Misri kuwa ni mwaka wa - 3000.

Ushindi wa Alexander wa Makedonia katika mwaka - 332 unaashiria mwisho wa historia ya Misri ya Mafarao na mwanzo wa kipindi cha Waheleni (angalia Sura ya 6).

Mazingira ya Waniloti

Pengine yafaa hapa kudondoa sentensi moja iliyoandikwa na Herodotus (11,35) inwishoni mwa maelezo yake ya Misri: "siyo tu hali ya hewa ya Kimisri kuwa mahususi kwa nchi hiyo, na into Nili kuwa na tabia tofauti na mito mingine kwingincko, lakini Wamisri wenyewe pia katika mwenendo wa desturi zao yaelekea wamegeuza desturi za kawaida za wanaadamu." Hapana shaka kuwa alipokuwa anaandika sentensi hiyo Herodotus alikuwa anafikiria nchi zile tu zilizopakana na Mediterania. Hata hivyo, ni hakika kuwa kati ya nchi zote za Afrika, Misri ni nchi moja pekee yenye mazingira maalum. Hali hii inasababishwa na kuwepo kwa mto Nili. Bila ya into huo, Misri isingeweza kuwepo. Tamko hilo limerudiwa mara kwa mara tangu siku za Herodotus: na ni ukweli wa kimsingi.

Kuanzia mwisho wa enzi ya Neolithiki, kwenye miaka - 3300 hadi - 2400, nchi za Afrika ya Kaskazini Magharibi, ikiwemo Sahara ndani yake zilinufaika kutokana na hali ya hewa ambayo haikuwa kame sana. Wakati huo Misri haikutegemea mto wa Nili peke yake kwa maisha yake. Mapululu bado yalienea mashariki na magharibi ya bonde, yakajenga mazingira mwafaka kwa wanyama pori na kuleta mshawasha wa

ufugaji wa wanyama. Kilimo wakati ule kilikuwa ni sehemu mojawapo tu ya maisha ya kila siku. Ufugaji wanyama - hata uwindaji — vilikuwa na nafasi muhimu. Kila baada ya miaka miwili utajiri huo ulihesabiwa. Mandhari yaliyopamba makaburi ya ufalme wa zamani tangu mwishoni mwa ufalme wa nne hadi ufalme wa sita (- 2500 hadi - 2200) yanadhihirisha kuwa ufugaji wa wanyama ulikuwa na nafasi muhimu katika maisha ya Misri wakati ule.

Hivyo, inawezekana juhudi zao za kudhibiti mto — ambayo ni mafanikio ya kimsingi ya ustaarabu wa Kimisri,— zilifanywa si kwa madhuniuni ya kutumia vizuri mafuriko kwa ajili ya kilimo, bali hasa zaidi kuzuia madhara ya mafuriko. Pengine inasahaulika kuwa mafuriko ya Nili hayaleti nafuu peke yake: yanaweza pia kuleta madhara na bila shaka watu walioishi mabondeni walijifunza kujijengea miambaduki na mabwawa kuinga vijiji vyao na kuchimba mifereji kukausha makonde yao. Hivyo, polepole wakapata uzoefu ambao ulikuwa muhimu kwao wakati hali ya hewa ya Afrika kati ya latitudo kumi na tatu na kumi na tano kaskazini ilipoanza kukauka taratibu na kubadilisha kuwa jangwa halisi maeneo nchini Misri na Nubia yaliyo karibu na Bonde la Nili. Baada ya hapo maisha yote katika bonde yalitawaliwa na mafuriko ya mto.

Kwa kutumia mbinu za kujengea miambaduki na uchimbaji wa mifereji walizozidhibiti vema kutokana na uzoefu wa muda mrefu, karne na karne, Wamisri kidogo kidogo waliendeleza mfumo wa umwagiliaji maji mashamba yao. Kwa njia hii walijihakikishia uwezo wa kuishi katika mazingira ambayo yaliendelea kuwa ya kijangwa.

Halitakuwa jambo la kupiga chuku iwapo tutasema kuwa mfumo huu wa namna ya pekee wa umwagiliaji ni msingi hasa wa maendeleo ya ustaarabu wa Kimisri. Mfumo huo unaeleza jinsi maarifa ya binadamu yanavyoweza kushinda matatizo makubwa na kufanikiwa katika kubadilisha ekolojia asili ya bonde.

Kwa kujitanidi awezavyo kubadilisha hali za kiasili zinazomkabili, binadamu ndiye hasa amekuwa kiini katika kuleta na kupanua ustaarabu kwenye Bonde la Nili. Misri si zawadi tu ya Mto Nili, bali juu ya yote, ni matokeo ya juhudi za mwanadamu.

Makazi katika Bonde la Nili

Mapema tangu Enzi za Paleolithi wanadamu waliishi mabondeni au jirani jirani na mabonde, hususan kwenye matungazi yanayozunguka bonde. Mfuatano wa vipindi vya umajimaji na ukame wakati wa enzi za Paleolithi na Neolithi (angalia juzuu I) ulibadilisha msongamano wa watu, kutegemeana na hali hizo mbili. Lakini ukweli unabakia palepale kuwa tangu zama za kale binadamu (homosapiens) amekuwa akiishi Misri.

Binadamu huyo alikuwa wa asili gani? Matatizo machache ya kiantropolojia yanuezusha mijadala mikali kuhusu suala hilo. Lakini, suala lenyewe si jipya. Mnamo mwaka +1874 kulizuka mabishano juu ya suala la “weupe” au “weusi”. Hata baada ya karne moja kwenye kongamano lililofadhiliwa na UNESCO ilitibitika kuwa mijadala

huo haukumalizika wala hautamalizika upesi. Hivi karibuni mwana-anthrolojia mmoja amesaili uwezekano wa kupata njia madhubuti ya kutambua asili ya mtu kwa kuchunguza tu mifupa yake - walau kuhusu mabaki ya kale ya wanaadamu, kama vile yale ya tangu enzi ya Paleolithiki. Vigezo vya zamani ambavyo vimekuwa vikitumiwa na wanaanthropolojia wa miili - faharisi ya uso, urefu wa viungo n.k. - siku hizi havikubaliwi na kila mtu. Zaidi ya hapo kuna wasiwasi mkubwa kama wakazi walioanzisha ustaarabu katika Bonde la Mto Nili kweli walikuwa watu wa kabila moja. Utafiti wa kihistoria juu ya watu wa kale wa bonde la Mto Nili haujaweza kuthibitishia juu ya suala hilo.

Binadamu hakuingia kwa mara inoja katika bonde lililokuwa tupu au lililokuwa likikaliwa na wanyama pori tu. Mwanadamu alianza kujijengea makazi taratibu katika muda wa miaka maelfu, kadri msongamano wa vikundi vya watu au mabadiliko katika hali ya hewa yalivyomlazimisha kutafuta maliasili zaidi au usalama mkubwa. Kutokana na nafasi yake kwenye pembe ya kaskazimi mashariki ya bara la Afrika, ilikuwa hapana budi ila Bonde la Nili kwa jumla, na hususan Misri, kuwa kituo cha mwisho kwa misafara ya watu waliotoka sehemu mbalimbali za Afrika, Mashariki ya Kati, na hata kutoka Ulaya. Kwa hiyo, haistaajabishi kuwa wanaanthropolojia waliamini kuwa kutokana na mifupa michache waliyoipata ya Wanailotiki wakongwe wangeweza kugundua watu wawakilishi wa makabila ya Wakromagnoidi, Waarmenoidi, Wanegro na Walukodami, ingawaje istilahi hizi inabidi zitumiwe kwa hadhari. Kama kulikuwepo kabila la Kimisri - na jambo hilo ni la wasiwasi - basi hilo kabila lilikuwa la mchanganyiko lenye maumbile yaliyobadilika kulingana na wakati na mahali.

Lakini hakika moja inabaki pale pale, kwamba nchini Misri kama ilivyokuwa huko Unubi, kuliishi watu wenye umbo fulani ambao kwa kweli haistahili kuwaita kabila maalumu, kwani sura zao zilitofautiana kulingana na sehemu walikotoka nchini humo. Watu wa kusini walikuwa weusi zaidi kuliko watu wa kaskazini, na kwa jumla watu wote wa sehemu hizi ni weusi zaidi walivyo wale waishio katika bonde la Mediterania, ikiwemo Afrika Kaskazini. Nywele zao ni nyeusi na za msongo na uso ukiwa wa mvingo zaidi usio na nywele na ambao katika sura za watu wa Ufalme Kongwe hupamba kwa sharubu. Watu hawa ambao kwa kawaida ni wembamba ndio aina ya watu ambao sura zao tumeziona katika picha, nakshi na sanamu za Mafarao.

Hii inaonyesha kuwa katika bonde la Nili unazungumzia aina ya watu, si kabila. Watu hawa walipata maumbile yao maalum kutokana na hali ya mazingira na maisha katika bonde hilo pamoja na athari za mchanganyiko wa watu mbalimbali. Upo uwezekano mkubwa kwamba rangi ya Kiafrika - nyeusi au maji ya kunde - ilijitokeza sana katika maumbile ya Mmisri wa kale, lakini si rahisi kutumia ujuzi tulio nao leo hii kuthibitisha jambo hili kwa hakika.

Mwandiko na Mazingira

Iwapo tutaangalia matumizi ya mlumo wa inaneno-picha yaliyowakilisha vitu

ambavyo kwa muda mrefu vilikuwa havitumiki tutaona kuwa Misri ilikuwa nchi ya kwanza ya Kiafrika iliyotumia maandishi. Yumkini maandishi hayo yalivumbuliwa katika kipindi cha Amratia, ambacho pia kinajulikana kama Nagada I (angalia juzuu la 1) yaani, takriban -4000 iwapo tutafuata tarehe zilizobainika kutokana na ugunduzi wa Kabomi 14, mwanzoni mwa kipindi cha historia. Ndiyo maana twaweza kusema kuwa mfumo huu wa maandishi ni mojawapo kati ya aina za kale za mifumo ya maandishi inayojulikana. Maandishi haya yaliendelezwa kwa haraka kwani inaelekea yalikuwa yameshashika mizizi kwenye ubao wa Narner, ambao ni ukumbusho wa kwanza wa historia ya Misri ambayo inawezekana kuwa ni ya takriban - 3000. Fauka ya hayo, wanyama na mimea inayoonekana katika picha hizi ni ya Kiafrika.

Uandishi wa Misri kimsingi ni picha, kama aina nyingi nyingine za miandiko ya kale ilivyo. Lakini, wakati huko China na Mesopotamia, kwa mfano, inaandishi-picha ya asili yaligeuka haraka kuwa na umbo la dhahania, Misri ilishikilia mfumo wake hadi mwisho.

Lakini mfumo huu ulikuwa na dosari kadha. Ulilazimika kutumia idadi kubwa ya picha, zaidi ya 400, ambazo zilimbabaiisha msomaji jinsi ya kuzisoma. Vilevile, haikuwezekana kutambua mara ikiwa picha fulani ilitumika kuwakilisha neno lililoonyesha kitu kilichokusudiwa, au ikiwa ilitumika kama alama ya ki-fonetiki. Wamisri wa kale pia walivumbua vijalizo vya kifonetiki. Wamisri wa kale pia walivumbua vijalizo vya kifonetiki. Vijalizo hivyo vilikuwa ni alama 24 za maneno ambazo kila moja iliwakilishwa na konsonanti moja. Polepole wataalamu wa maandishi walianza kuvitumia vijalizo hivyo kuonyesha matamshi ya alama za maandishi yao.

Ni dhahiri kuwa vijalizo hivyo kwa hakika ni kama herufi zetu na kuwa maandishi-picha ni chimbuko la uvumbuzi wa alfabeti, kwa sababu picha hizo huonyesha konsonanti za lugha ya Kimisri na kwa sababu Kimisri kama Kiarabu na Kiibrania hakiandiki vokali. Hivyo, hapakuwa na neno katika lugha ya Kimisri ambalo lisingeweza kuandikwa kwa picha. Hata hivyo, Wamisri badala ya kutumia alama rahisi kama za kifabeti peke yake, pamoja na alama zilizotumika kifonetiki na vijalizo vyake vya kifonetiki, waliingiza alama mpya za kipicha. Alama hizi zililwekwa inwishoni mwa maneno. Hizo zilisaidia kuyaainisha mara moja maneno yale katika kategoria fulani. Kwa mfano vitenzi vilivyoonyesha kitendo cha kimwili, kama vile "kupiga," "kuua," vilifuatwa na alama za mkono wa mwanadamu ulioshika silaha.

Jainbo moja lililosababisha uvumbuzi na ukuzaji wa maneno-picha katika Bonde la Mto Nili bila shaka linatokana na haja ya wakazi wake kushirikiana pamoja katika kupambana na maafa yaliyokuwa yanawatisha niara kwa mara, miongoni mwao ikiwemo mafuriko ya mto Nili.

Umoja wa kisiasa wa Misri ulioletwa na Menes kwenye mwaka - 300 uliimarisha zaidi maendeleo ya utawala na, kwa hivyo, ya maandishi. Vilevile, kutokana na hali geugeu ya mafuriko, mojawapo ya wajukumu ya serikali kuu ilikuwa kuhifadhi kiasi

kikubwa ilivyowezezana cha chakula nyakati za neema, ili kujikinga na upungufu ambao ungeweza kutokea ghafla. Kwa hiyo, viongozi, yaani Mafarao, walipaswa kujua barabara nini kilikuwepo nchini ili wakati wa shida kuweza ama - kugawa kwa resheni au kugawa mali iliyopo kwa mikoa iliyoathirika sana na njaa. Huo ulikuwa ndio msingi wa utaratibu wa kiuchumi wa Misri na, kwa hakika, ndio ulikuwa uhai wa nchi hiyo. Taratibu hizi zilihitiwa mfumo thabiti wa uhasibu wa viingiavyo na vitokavyo kwa upande wa bidhaa na watu. Hii inaeleza nafasi muhimu ya maandishi katika ustaarabu wa Misri ya kale.

Tofauti kati ya Misri na Bonde la Nili la Unubi inatuelewesha vizuri zaidi dhima ya maaudishi na sababu za kuwepo kwake katika chanzo na maendeleo ya ustaarabu wa Misri. Kutokana na mahusiano ya kudumu yaliyokuwepo kati yake na Misri, Nubia lazima ilikuwa na fununu kuhusu matumizi ya maandishi. Hata hivyo watu wa Nubia hawakutaka kuyatumia maandishi hayo. Sababu ya hali hii inaelekea imo katika tofauti kwenye namna ya kuishi. Kwa upande mmoja kuna msongamano mkubwa wa watu ambao kutegemea kwao umwagiliaji na udhibiti wa mto kama tegemeo la pekee la maisha yao kumewafanya washikamane katika jamii ya kitabaka ambamo kila mmoja ana nafasi maalumu katika maendeleo ya nchi.

Kwa upande wa pili, katika Unubi kuna msongamano wa watu ambao wakati wa pambazuko la historia walimiliki utamaduni wa kuonekana ambao ulilingana na, au pengine kuzidi, ule wa Misri ya Juu. Lakini watu hao waligawanyika katika vikundi vidogovidogo vilivyotawanyika. Vikundi hivi vilikuwa vya watu walio huria zaidi na ambao ni wahamaji kwani ufugaji wa wanyama uliwhitaji kuhama mara kwa mara na pia ufugaji ulikuwa na nafasi muhimu walau kama ile ya kilimo katika uchumi. Kilimo hicho kilikuwa katika eneo dogo mno katika bonde lililo finyu kuliko la Misri. Wanubi hawakuhisi haja ya kuwa na maandishi. Daima walikuwa wakitumia masimulizi ya mdomo. Maandishi yalitumika kwa nadra na, inavyoelekea, kwa ajili ya shughuli za kidini tu au wakati walipotawaliwa na utawala wa kifalme (angalia Sura 10 na 11 chini).

Misri ya Kiafrika - chombo cha kukingia athari

Kwenye mwaka -3700 kunaonekana dalili za mwungano wa utamaduni wa kuonekana katika vituo viwili vya ustaarabu katika Bonde la Mto Nili. Pengine kwa usahihi zaidi kituo cha kusini wakati kikiendelea kuwa na sifa zake maalumu, kilingiza sehemu ya utamaduni wa kitovu cha kaskazini. Kuingia huko kusini kwa utamaduni wa kaskazini aghalabu huhusishwa, na uvumbuzi wa maandishi na pia kujitokeza huko Misri kwa wavamizi ambao walikuwa wameendelea zaidi kuliko wenyeji wazawa.

Ama kuhusu maandishi, tumeshaona hapo awali kuwa asili yake ni Kinailotiki hasa, hivyo uasili wake wa Kiafrika siyo tu kuwa unajitokeza bali pia unaakisi ukweli. Hata hivyo, uasili na ukale wa ustaarabu wa Misri usifiche uhakika kuwa Misri ilikuwa chombo cha kukingia athari mbalimbali. Kadhalika, nafasi yake ya kijiografia pia iliivutia Misri ileleke upande huo.

Hali yake ya hewa yenye unyevunyevu tangu mwisho mwa enzi ya Neolitikani katika muda wote wa kabla ya ufalme, ambamo ustaarabu wa Misri uliimarika, vilifanya jangwa la Uarabuni kati ya Bahari ya Shamu na bonde la Nili liweze kupenyeka. Bila shaka ni kupitia njia hiyo ndipo athari za Mesopotamia, ambazo huenda umuhimu wake umekuzwa mno, ziliingia Misri. Pia inaelekea kuwa ijapokuwa uchunguzi wa kutosheleza umekosekana, kulikuwepo uhusiano wa kiasi fulani kati ya watu wa jangwa la Libya na wale wa bonde la Nili.

Inaelekea kuwa kaskazini, mahusiano tangu zama za awali, kupitia shingo la Suez kati ya Misri na bonde la Siria na Palestina, hayakuwa ya karibu kama yalivyokuwa baada ya kuanzishwa kwa Ufalme Kongwe. Hata hivyo, huko pia, alama za kale za mahusiano na Palestina zinaonekana, na hekaya ya Osiris huenda ilitokana na mahusiano kati ya kituo cha ustaarabu cha Delta na mwambao wa misitu wa Lebanon - kwa hiyo ni mahusiano ambayo yameanza zama za kale kabisa.

Kwa kutupia jicho tu inaelekea kuwa mahusiano kati ya kaskazini na kusini yalikuwa ya dhahiri, lakini umuhimu wake ni vigumu kuathmini. Tangu karne ya nne kabla ya enzi zetu watu wa kusini mwa maporomoko ya kwanza walikuwa na mahusiano ya karibu na sehemu za kusini niwa Nili. Katika enzi za kabla na mwanzo wa ufalme mabadilishano kati ya vikundi vya ufanyanji na utengenezaji wa udongo wa enameli, matumizi ya ufuaji chuma wa aina moja, matumizi ya silaha aina moja, imani ya aina moja katika maisha ya baada ya kufa, na mila za mazishi. Wakati wa mawasiliano hayo Wamisri lazima walikuwa na mahusiano ya moja kwa moja au ya kupitia kwa wajumbe, na watu wa sehemu za mbali zaidi za Afrika kama inavyoweza kufasirika kutokana na idadi ya mapambo ya pembe za ndovu na mpingo ambavyo vimekusanywa kutoka makaburi ya kale sana ya Misri. Hata kama tutachukulia kuwa mstari wa mpaka wa ekolojia wa mpingo ulikuwa mbali zaidi kaskazini kuliko siku hizi, Misri bado ilikuwa mbali sana kutoka Nubia ya Chini na hiyo imetupa ushahidi madhubuti kuhusu mawasiliano kati ya Afrika kusini mwa Sahara na Misri. Mbali na pembe za ndovu na mpingo, udi — ambao ulionekana mapema — na marumaru nyeusi ambavyo vyote viwili ni vigeni kwa bonde la Nili, huenda viliagizwa na Wamisri. Kwa njia ya biashara hiyo, ufundi na mawazo yangepita kwa urahisi kutoka sehemu moja kwenda ya pili kwa sababu, kama tulivyokwishaona, Wamisri walikuwa na asili ya kutosha ya Kiafrika.


Hivyo, popote pale tutakapoangalia, magharibi au mashariki, kaskazini au kusini, tutaona kuwa Misri ilipata athari za nje. Hata hivyo, athari hzo hazikuathiri uasili wa ustaarabu ambao ulijengeka polepole kwenye kingo za mto Nili, kabla ustaarabu huo wenyewe haujaathiri sehemu zilizopakana nayo. Ili kupata fununu kuhusu kiasi cha athari za nje mwanzoni mwa ustaarabu katika Bonde la Mto Nili, kunahitajika ujuzi mkubwa wa kiakolojia wa nchi nzima katika zama za kale.

Kunahitajika ujuzi mkubwa ili iwezekane kufanya ulinganisho wa kufaa wa vitu vya kiakolojia vilivyokusanywa Misri na vitu vilivyotoka kwenye tamaduni za jirani. Ulinganisho huo una dhamira ya kudhihirisha uingizaji au uigaji wa vitu hivyo,

ambao kwao ni ushahidi wa pekee unaoonekana wa mawasiliano makubwa.

Lakini, ingawa akiolojia ya elfia ya nne kabla ya enzi zetu inajulikana vya kutosha, katika sehemu zote mbili, yaani Misri ya Juu na katika Unubi ya Chini (kati ya Maporomoko ya Kwanza na ya Pili), hali hii haipo katika sehemu nyinginezo za mto Nili. Kwa mahususi, hatujui habari za Delta kuhusu vipindi vya kabla na vya mwanzo wa Ufalme, isipokuwa katika sehemu chache athari zilizotokeza bara la Asia katika nyakati hizo, kupitia shingo la Suez au mwanibao wa Mediterania, bado yangali yanahitaji kuthibitishwa kwa utafiti.

Hali kadhalika, matatizo hayo pia yanatukabili katika Bonde la Nili ya juu, kati ya Maporomoko ya Pili na ya Sita. Kutokuwa na maelezo kuhusu akiolojia ya awali kabisa ya sehemu kubwa kunasikitisha zaidi, kwa sababu ndipo hapo ambapo mawasiliano na biashara kati ya bandari ya Misri kwenye bonde la Nili na Afrika kusini mwa Sahara zilifanyika.



Asili ya Wamisiri wa Zamani

Inawezekana kuuliza vipya kabisa swali kuhusu historia ya Misri kukaliwa na watu na hata jinsi dunia nzima ilivyokaliwa na watu. Inawezekana hivi kwa sababu matokeo ya kazi ya Profesa Leakey yamesababisha kukubaliwa na watu wengi sana kwa wazo la msingi kwamba, asili ya binadamu katika kuzaliwa ni moja na pia kwamba asili hiyo ni Afrika. Zaidi ya miaka 150,000 iliyopita viumbe waliokuwa sawa kabisa na binadamu wa siku hizi kimaumbile walikuwa wakiishi katika sehemu za maziwa makubwa mto Nili unakoanzia; hawakuishi mahali pengine popote. Dhana hii ina maana kwamba kama walivyokuwa wakifikiri wazee wa zamani, asili ya binadamu wote ni sehemu za chini chini za Milima ya Mwezi. Kutokana na jambo hili mambo mawili mengine niuhimu sana yanafuata:

- (a) Watu wa kwanza kabisa walikuwa na asili moja na walikuwa weusi. Sheria ya Gloger inayoweza kutumika pia wanapohusika binadamu, nayo inasema kwamba wanyama wenye damu ya moto wanaokaa katika hali ya hewa ya joto na yenye majimaji hutoa weusi wa nywele au mwili (eumelanin). Kwa hiyo, kama asili ya binadamu ilikuwa sehemu za tropiki usawa wa latitudo za maziwa makubwa, ilibidi awe na rangi kahawia toka mwanzo kabisa na ilikua ni kutokana na mabadiliko ya polepole tu katika sehemu zenye aina nyingine ya hali ya hewa kwamba kundi la uanzilishi liligawanyika katika makundi tofauti ya rangi;
- (b) Palikuwa na njia mbili tu walizoweza kutumia watu hawa wa mwanzo kwenda kuishi katika Kontinenti nyingine, hususan jangwa la Sahara na bonde la Mto Nili. Hapa tutajadili eneo la njia hii ya pili.

Kuanzia enzi za inwishi za enzi ya Paleolithiki hadi enzi za wafalme, sehemu yote ya bonde la mto Nili likaliwa pole pole na watu hawa weusi.

Ushahidi wa Anthropolojia maumbo kuhusu rangi ya Wamisri wa zamani

Inawezekana kufikiwa kwamba, kwa kutumia ushahidi wa maungo ya binadamu,

ugunduzi wa wanaanthropolojia ungeondoa mashaka yote kwa kuonyesha ushahidi wa kuaminika na uliodhahiri kabisa. Lakini hivyo siyo mambo yalivyo; kutumiwa kwa vigezo visivyokuwa na kanuni maalum pamoja na kufuata kabisa uwezekano wa kuwa na hitinuisho linalokubalika bila maelezo ya nyoungeza, kumeleta ubishi mwingi, wa kisayansi usiokuwa wa lazima.

Hata hivyo, ingawa matokeo ya utafiti huu wa kianthropolojia hauufikii ukweli kamili, wanaanthropolojia hukubaliana kwa pamoja kwamba palikuwa na watu weusi tangu enzi za zamani sana hata kabla ya enzi za wafalme. Hatuwezi kuyaorodhesha yote yaliyoandikwa kama ushuhuda wa ukweli huu kwani hayo yanaweza kupatikana katika sura ya kumi ya kitabu cha Dkt. Emile Massoulard kiitwacho *Historie et protohistoire d'Egypte* (Taaasisi ya Anthropolojia, Paris 1949). Ila itabidi kukariri mambo fulani maalum tu.

Bi Fawcett ni mmoja wa wanataaluma wanaoamini kwamba mafuvu yaliyokusanywa Negada ni mengi ya kutosha na hufanana kiasi kwamba yanatosheleza kutumiwa kuthibitisha kuwapo hapo kale kwa kabila la Negada. Amedai kuwa aina hii ya watu inafanana sana na watu weusi katika urefu wa kichwa, urefu wa masikio, urefu na upana wa uso, urefu wa pua, na faharisi ya kisogo na uso. Watu hawa imedaiwa kuwa hufanana na watu wa Kijerumani katika upanda wa pua, urefu wa jicho, urefu wa kaakaa, na faharisi ya pua. Kwa hiyo, wakazi wa Negada kabla ya enzi za kifalme wanaonekana kuwa walifanana sana na watu weusi katika baadhi ya maumbo yao na watu weupe katika maumbo mengine.

Hoja hizi ambazo huacha mwanya wa kuchagua kati ya kingo mbili zinazowakilishwa na watu weusi na Wajerumani inatoa kielelezo cha mnyumbuko wa vigezo vilivyotumiwa.

Falkenburger naye katika kitabu chake cha hivi karibuni anatoa maelezo juu ya mafuvu ya wanaume 1,787 walioishi kati ya miaka kabla ya enzi za ufalme na enzi zetu. Mafuvu hayo aliyagawa katika mafungu manne. Kutengwa kwa mafuvu ya kipindi kabla ya ufalme kulingana na makundi haya manne kunatoa matokeo yafuatayo kwa kipindi chote hicho. Watu weusi 36%, watu wa Mediterani 33%, watu wa Kromagnoidi 11% na watu ambao hawawezi kuingizwa katika fungu lolote kati ya haya lakini wanakaribia watu wa Kikro-Magnoidi au watu weusi 20%.

Jambo muhimu katika mahitimisho haya ni kwamba ingawa kuna tofauti ya mawazo, kiasi wanachofanana kinahakikisha kwamba msingi wa watu wa Kimisri katika miaka kabla ya ufalme ulikuwa wa watu weusi. Mahitimisho haya hayalingani kabisa na nadharia zisemazo kwamba mbegu ya watu weusi ilijipenyeza katika Misri baadaye. Ushahidi unaonyesha kwamba aina ya watu waliokuwa weusi ndiyo iliyokuwa kubwa zaidi ya nyingine zote tangu mwanzo. Elliot - Smith naye amewaorodhesha watu hawa walioishi kabla ya Wamisri kama tawi la watu awaitao wa rangi ya kahawia, jina ambalo ni sawa na lile la Sergei aliyewaita: "Watu wa Mediterani au Waafrika-Wazungu." Neno "kahawia" katika matunizi haya linaeleza rangi ya ngozi na limetumiwa badala ya watu weusi. Kwa hiyo ni wazi kwamba jumuiya yote ya watu wa Misri ilikuwa ya watu weusi waliowazuia watu weupe wa

kinomani wasijipenyeze nchimi mwao miaka michache kabla ya enzi za ufalme.

Kwenye uchunguzi wa Petrie kuhusu mbari ya Wamisri tunaelezewa kuhusu uwezekano wa uainishaji kwa wingi ambao hauwezi kumshangaza msomaji.

Petria ameonyesha katika utafiti wake kwamba mbali ya watu wa aina ya *steatopigia*, kulikuwa na aina nyingine sita tofauti: aina ya watu wenye pua kama tai waliofika kama wavamizi kutoka labda kandokando ya Bahari ya Sham; watu wenye pua yenye ingongo mwembamba kutoka katika jangwa la Uarabuni, watu wenye pua iliyojipinda mbele kidogo kutoka Misri ya Kati; watu wenye kidevu kilichochoongoka kutoka sehemu ya Misri ya chini (kusini) watu wenye pua nyembamba kutoka sehemu za Misri ya juu (kaskazini). Kwa kufuata sura hizo zilizoonyeshwa twapata makabila ya aina saba yaliyoishi nchini Misri katika vipindi tunavyovichunguza.

Njia hii ya kuainisha watu iliyotumika hapo juu inatoa wazo jinsi vigezo vya kuainisha watu wa Misri vilivyokuwa havina kanuni thabiti. Hata hivyo, ni wazi kwamba anthropolojia haijafaulu hata kidogo kuhakikisha kwamba kulikuwa na taifa la watu weupe Misri na inaelekea kwamba ushahidi uliopo waelekea kuonyesha kinyume cha fikra hizi.

Katika vitabu vilivyotolewa siku za karibuni jambo hili limefifishwa kabisa: mahali pengi sana hudaiwa tu kwamba Wamisri walikua weupe na msomaji asiye mtaalam na ambaye huamini bila kudadisi lubaki na wazo kwamba madai yoyote ya namna hii lazima yawe na kiini chao katika utafiti timamu. Lakini sura hii imeonyesha kuwa hakuna kiini cha namna hiyo. Hivyo vizazi vyote vilivyotangulia vilidanganywa kuhusu swala hili.

Sura za watu katika siku za mwanzo wa historia: thamani yao katika anthropolojia

Uchunguzi wa sura za watu uliofanywa na Flinders Petrie katika nyanja nyingine huonyesha kwamba kabila la watu wa Misri lilikuwa la watu weusi: kufuatana na Petria watu hawa walikuwa ni Wa-Anu ambao jina lao linetafutwa na kugunduliwa katika siku za awali za historia kabla maandishi hayajagunduliwa.

Inasemekana kuwa mtu aliyeabudiwa na WaAnu alijulikana kama "mtu mkuu mweusi."

Baada ya kuangalia aina mbalimbali za watu wa kigeni waliogonbania bonde la Mto Nili na watu wa awali, ambalo ni Wa-Anu waliokuwa wakiishi katika sehemu za Misri ya Kusini na Unubi, Petria anawaainisha kwa kulingana na sanamu moja ya Tera Neter kuwa walikuwa weusi.

Amélineua anaorodhesha kijiografia miji iliyozungushiwa maboma ambayo ilijengwa na Wa-Amvi weusi penbeni mwa Bonde la mto Nili; Esneh, 'On ya kusini' au Hermonthis, Denderah, mji ulioitwa On upande wa Tinis, na 'On ya kusini' au Heliopolis.

Vile vile kuna picha katika kaburi moja inayowaonyesha watu weusi wakipigana na kuwashinda wavamizi wekundu. Kaburi-hilo liko Hierakonpolis. Kaburi SD 63 (lenye tarehe ya 63). Kama tukikubaliana na maelezo ya Petrie: chini kuna meli

nyeusi Hierakonpolis inayomilikiwa na watu weusi wanaoonyeshwa kama wamewashinda watu wekundu.

Tunachoweza kusema kwa mujibu wa maelezo hayo hapo juu ni kwamba sura za watu wa siku za awali ya historia kabla ya kugunduliwa kwa maandishi na za wale wa enzi za ufalme hazilingani hata kidogo na maoni yanayopendelewa na wana-anthroplojia wa nchi za Ulaya Magharibi kuhusu watu wa Misri. Popote ambapo aina ya watu wa asili walipochorwa wazi wazi, huonyeshwa kama watu weusi. Hakuna mahali popote ambapo aina ya watu ambao ni wa asili ya Ulaya na Asia au wa asili ya Kisemitiki wanapoonyeshwa hata kama raia huru wa kawaida wakimtumikia mtawala wa ngazi ya chini kabisa. Watu wa makundi hayo siku zote huonyeshwa kama wageni waliotekwa katika vita. Picha chache zinazoonyeshwa huwa na alama za wazi za watu waliotekwa wakiwa na mikono iliyofungwa nyuma au iliyokazwa mabegani. Sanamu moja ndogo ya enzi kabla ya ufalme wa Misri imemwonyesha mtu wa asili ya Asia-Ulaya mwenye nywele ndefu zilizosukwa akiwa amepiga magoti na mikono yake imefungwa mwilini kwake. Sanamu yenyewe inaonekana kama ilikuwa mguu wa samani fulani na imewakilisha watu walioshindwa.

Sifa halisi za kinegro za Mafarao (Narmer, wa utawala wa kwanza na mwanzilishi hasa wa familia ya Mafarao; Zoser, wa utawala wa tatu; Cheops, aliyejenga Piramidi la Ajabu; aliyekuwa na sura ya Kikameruni; Mentuhotep, mwanzilishi wa utawala wa kumi na moja aliyekuwa mweusi sana; Sesostris I, Malkia Ahmosis Nefertari; na Amenhophis I) zinaonyesha kuwa tabaka zote za jamii za kimisri zinatokana na asili hiyo hiyo ya watu weusi.

Kuna aina mbili tofauti za watu weusi:

- (a) wenye nywele zilizonyooka, ambao huko Asia wanawakilishwa na Wadravidi na Afrika na Wanubi na Watubu au Wateda, wote wakiwa na ngozi nyeusi sana,
- (b) wenye nywele za kipilipili kutoka kwenye eneo la Ikweta.

Aina zote hizi zilichanganyika na kuunda idadi ya watu wa Misri.

Upimaji wa kiasi cha Melanini

Inawezekana kabisa kuhakikisha aina ya rangi ya ngozi na hatimaye kujua asili ya Kikabila ya watu wa Misri wa zamani kwa kutegemea upimaji na uchunguzi unaotumia darubini katika maabara. Sidhani kwamba busara ya wachunguzi walioshughulikia swali hili imepuuza uwezekano huu.

Melanini, kemikali ambayo hujenga rangi ya ngozi, kwa kawaida haiyeyuki na huhifadhika kwa mamilioni ya miaka katika ngozi za wanyama wenye mifupa. Kwa hiyo inawezekana kabisa kupata kwa urahisi kutoka katika ngozi za maiti za kimisri zilizohifadhiwa zisioze, ziiwazo mumiani, au maiti kongwe. Ingawa melanini hupatikana hasa katika tabaka ya juu ya ngozi, chembechembe zake zinazojipenyeza katika tabaka kuu ya ngozi, kupitia kwenye mpaka kati yake na sehemu ya juu huwa




1.1 Picha ya Tera-Neter wa mame-historia, mnero wa heshima wa mbari ya Anous ambayo ilikuwa ndiyo ya wakazi wa mwanzo wa Misri (C.A. Diop, 1967)

1.2 Farao wa Nasaba ya Kwanza ya Kimisri, inasemekana ni Narmer (C.A Diop, 1967 p.



1.3 Djeser – Mnegro halisi, farao wa Nasaba ya Tatu (C.A. Diop, 1967)



na kiasi cha melanini ambayo haipo kwa watu wenye ngozi nyeupe. Kiasi hiki huonekana hata tabaka fulani zinapokuwa zimeharibiwa. Sampuli ambazo mimi mwenyewe nimezichunguza zilipatikana kutoka kwenye maiti za Wamisri wa zamani zilizohifadhiwa na kuchimbuliwa kutoka katika machimbo ya Mariette huko Misri na kuhifadhiwa katika maabara ya anthropolojia ya viumbe katika Jumba la Makumbusho la Paris liitwalo *Musee de L'Homme*. Njia hiyo hiyo inaweza kabisa kutunika kuchunguza maiti zilizohifadhiwa za wafalme Thutmoses III, Seti I na Ramses II zilizo katika Jumla la Makumbusho la Kairo na zilizohifadhiwa katika hali nzuri sana. Makumbusho la Kairo na zilizohifadhiwa katika hali nzuri sana. Ni kiasi kidogo tu kwa vipimo vya mraba vya milimita chache kinachohitajiwa kama sampuli, nene kidogo na iliyolainisha na dawa itwayo ethili benzoati. Vipande hivi vya ngozi vinaweza kuchunguzwa katika mwanga wa kawaida au kwa kutumia mionzi ya urujuani kali ambayo hufanya vijipunje vya melanini ving'ae sana.

Kwa vyovyote vile, tuseme tu kwamba tathmini ya kiasi cha melanini kwa kutumia darubini ni njia moja ya kimaabara ambayo hutawezesha kuainisha Wamisri wa zamani kama sehemu ya kundi la watu weusi bila wasiwasi wowote.

Vipimo vya osteolojia

Kati ya vigezo vinavyokubalika katika anthropolojia ya viumbe vipimo vya osteolojia ndivyo ambavyo vinaweza kupotosha kwa kima kidogo sana kulinganisha na vipimo vya nafuvu katika kumtofautisha mtu mweusi na mtu mweupe kwa kutumia kigezo hiki. Pia imethibitika kwamba Wamisri ni watu walio katika kundi la watu weusi. Uchunguzi huu ulifaywa na Lepsins mwishoni mwa karne ya kumi na tisa na mahitimisho yake bado yana uzito mkubwa mpaka leo. Maendeleo yaliyofuata katika njia za uchunguzi za anthropolojia ya maungo hayapingi hata kidogo kile kiitwacho "sheria ya Lepsin" ambayo hutoa vipimo mbalimbali vya mwili wa mtu asiyehitilafiana na wa Misri, ambaye ana mikono mifupi na maungo ya Kinegro.

Makundi ya damu

Ni jambo linalojulikana sana kwamba hata leo Wamisri, hasa wale wa sehemu ya Misri ya Juu, wana damu ya aina ya kundi B kama watu wa Afrika ya Maghribi wanaoishi pwani ya Bahari ya Atlantiki. Hawamo katika kundi la damu A2 ambalo ndimo walimo watu weupe wengi kabla hawajaoana na watu wa mataifa mengine. Lingekuwa jambo la kisisimua kuchunguza ni kwa kiasi gani damu ya Kundi A2 imo katika maiti za kale zilizohifadhiwa Misri, jambo ambalo utaalumu wa kisasa unaweza kulifanya.

Asili ya Wamisri kufuatana na Waandishi wa Zamani wa Mambo ya Kale

Maumbo ya Wamisri wa zamani hayakuwatatanisha waandishi wa Kiyunani na

Kirumi walioishi wakati mmoja nao. Kwao ilikuwa wazi kwamba Wamisri walikuwa weusi, wenye midomo minene, nywele za kipilipili na miguu myembamba. Baadhi ya ushahidi ufuatao unaeleza jambo hilo vizuri sana.

(a) Herodotus 'baba wa historia' aliyeishi kati ya - 480 (?) na -425.

Aliandika kama ifuatavyo kuhusu Wakolchi waliokuwa wakiishi pwani ya Bahari Nyeusi:

Ni wazi sana kwamba Wakolchi ni Wamisri kufuatana na makundi ya binadamu..... Wamisri kadhaa waliniambia kuwa walifikiri Wakolchi walitokana na maaskari wa Sesostris. Mimi mwenyewe nilikuwa nimefikiri hivyo kutokana na mambo mawili. Kwanza kwa kuwa wana ugozi nyeusi na nywele za kipilipili na pili kwa sababu ambayo ni ya kuaminika zaidi kwamba katika binadamu ni Wamisri na Wahabeshi tu ambao walikuwa na tabia ya kutahiri na kutahiriwa tangu enzi za wahenga na wahenguzi. Wafenisi na Wasiriya wa Palestina hukiri wenyewe kwamba waliiga desturi hii kwa Wamisri. Wasiriya waishio katika bonde la mto Thermodon na Wamakroni husema kwanba walijifunza mila hii kutoka kwa Wakolchi. Haya ndiyo makabila pekee yanayotahiri na njia wanayofuata ni ile ya Wamisri.

Herodotus amerudia mara nyingi kusema kwamba Wamisri wana maumbo ya watu weusi na kila mara hutumia jambo hili kama hoja ya kutetea dhiana ambazo zina utata zaidi.

(b) Aristotle: aliyeishi toka - 389 mpaka - 332 alikuwa mwana sayansi, mwanafalsafa na mkufunzi wa Mfalme Alexandra Mkuu.

Katika kitabu chake kimoja kidogo Aristotle alijaribu kuonyesha uhusiano kati ya maumbo ya watu na tabia zao na ametuachia ushahidi kuhusu watu wa Misri na Uhabeshi ambao unalingana na yale aliyosema Herodotus.

(c) Lusiano; mwandishi wa Kiyunani, aliishi toka +125 (?) mpaka + 190.

Ushahidi wa Lusiano uko wazi kabisa kama ule wa waandishi wawili waliotajwa hapo juu. Anatomia Wayunani wawili, Lisino na Timelao wakiongea kama kielelezo.

Lisino (akielezea maumbo ya Mmisri kijana): Mvulana luyu si mweusi tu bali ana midomo niinene na miguu yake ni myembamba mno. Nywele zake zilizosukwa na kufungwa pamoja kisogoni zinaonyesha kwamba si mtu huru."

Timolao: Lakini Lisino hiyo ni alama ya mtu aliyezaliwa katika familia mashuhuri sana huko Misri. Watoto wote waliozaliwa huru husuka nywele zao mpaka wafikie utu uzima. Ni mila tofauti kabisa na ile ya wazee wetu walioona kwamba wazee



1.4 ▲ *Mateka wa Kihindi-Kizungu (C.A. Diop, 1967)*



1.5 ◀ *Mateka wa Kisemitiki wakati wa Mafarao; Mwamba wa Sinai (C.A. Diop, 1967)*

1.6 ▼ *Mfungwa wa Kilbya (C.A. Diop, 1967)*





1.7 Cheops, Farao wa Nasaba ya Nne ya Kimisri, mjenzi wa
Piramidi Kuu (C.A. Diop, 1967)




1.8 *Mentuhotep I (C.A. Diop, 1967)*



1.9 Ramses II na Mbatutsi wa kisava (C.A. Diop, 1967)



1.10 Sfinkisi kama ilivyokutwa na kundi la kwanza la wanasayansi wa Kifaransa karne ya kumi na tisa. Sura halisi ya Mnegro inadhaniwa kuwa ile ya Farao Khafre au Khefren (-2600. Nasaba ya IV, mjenzi wa piramidi ya pili ya Giza (C.A. Diop, 1967)



walipendeza sana walipobana nywele zao na kipini cha dhahabu ili zisichezecheze.

(d) Apollodorus: aliishi karne ya kwanza ya enzi ya Kikristo, alikuwa mwanafalsafa Myunani. Yeye aliandika ifuatavyo:

'Aegiptos aliiteka nchi ya watu wenye miguu myeusi na akaiita Misri kulingana na jina lake.'

(e) Aeschylus: aliishi toka - 525 (?) mpaka - 456; alikuwa mshairi aliyetunga mashairi ya kuomboleza na alikuwa mtu aliyebuni michezo ya kusikitisha ya Kiyunani, aliandika ifuatavyo:

Katika kitabu kiitwacho *Waombaji* (The Suppliants) Danaos akikimbia na wanawe wa kike, Wadanao, na akikimbizwa na ndugu yake wa kiume, na watoto wake Aegiptos ambao walitaka kuwaoa binadamu zao kwa nguvu, alipanda mwinuko mdogo akiangalia baharini na kutoa habari kuhusu Wanamisri wanaopiga kasia kwa mbali kama ifuatavyo: "Ninaweza kuwaona mabaharia wenye mikono myeusi na kanzu nyeupe".

Maelezo ya aina hii hii kuhusu watu wa aina ya kimisri kunaonekana tena mistari michache baadaye katika ubeti 745.

(f) Achilles Taitus wa Alexandria.

Aliwalinganisha wachungaji wa delta ya mto Nili na Wahabeshi na kueleza kwamba wao ni weusi kidogo kama machotara.

(g) Strabo: aliishi toka - 58 mpaka + 25.

Yeye anakubaliana na wazo kwamba Wamisri na Wakolchi ni watu wa asili moja. Lakini anatoa hoja kwamba uhamiaji kwenda Uhabeshi na Ukolchi ulikuwa na kiini chake Misri tu. Wamisri walikaa Uhabeshi na Ukolchi.

(h) Diodorus wa Sisilia aliyeishi kutoka - 63 mpaka +14; alikuwa mwana historia wa Kiyunani na mtu aliyeishi wakati wa Kaisari Augusto.

Kulingana na maoni ya Diodorus haiyumkini Uhabeshi ndiyo iliyoteka na kumiliki Misri na wahabeshi waliongozwa kwenda Misri na Osiris.

Ammiano Marcellino aliyeishi toka mwaka +330 mpaka +400; alikuwa mwanahistoria wa Kirumi na anaandika ifuatavyo: "Watu wengi sana wa Misri wana rangi kahawia au nyeusi na wanaonekana wainekonda sana; ngozi zao ni kavu."

Maelezo haya juu ya ushahidi wa waandishi wa zamani wa Kiyunani na Kirumi kuhusu watu wa Misri yanaonyesha kwamba wanakubaliana katika maoni yao kwa kiwango kikubwa sana. Kukubaliana huku ni jambo ambalo haliwezi kupuuzwa kwa urahisi au kufichwa.

Tunaongeza hapa ushahidi wa Volney ambaye alisafiri nchini Misri kati ya miaka +1783 na +1785, yaani wakati utumwa wa watu weusi ulipokuwa umekomaa. Alitoa

maoni yafuatayo kuhusu asili ya Wamisri halisi, yaani watu walio asili ya Mafarao - Wakopti:

Wote wana sura zilizovimbavimba, wana macho makubwa na midomo minene, kwa kifupi wana sura za kichotara kabisa. Nilifikiria mwanzo kuwa hii ilisababishwa na hali ya hewa. Nilipotembelea sanamu kuhwa ya Sfinki, sura yake ilinipa wazo kuhusu jambo hili la kushangaza. Nikiangalia kichwa hicho ambacho kina sura ya Kinegro katika maumbile yake yote nilikumbuka dondoo moja la Herodotus linalojulikana sana lilemalo: "kwa upande wangu nafikiri Wakolchi ni wakoloni wa Misri kwa sababu wao pia wana ngozi nyeusi na nywele za kipilipili." Kwa maneno mengine Wamisri wa zamani walikuwa Wanegro halisi wenye asili moja kama watu wote wenyeji wa Afrika. Kutokana na asili hii mtu anaweza kuona kuwa *taifa* lao lililazimika kupoteza weusi wao kamili wa awali lakini likabakiza maumbo yake ya mwanzo baada ya karne nyingi za kuchanganya damu na Wayunani na Warumi.

Champollion - Figeac, kaka wa Champollion Mdogo, aliyakataa mawazo haya ya Volney katakata akisema kwamba alama mbili za maumbo, ngozi nyeusi na nywele za kipilipili hazitoshi kusema kwamba aina fulani ya watu ni ya Kinegro. Kwa hiyo hitimisho la Volney kwamba Wamisri Wakale wana asili ya watu weusi halikubaliki.

Jinsi Wamisri walivyojiona wenyewe

Halipaswi kuonekana kama wazo la kupoteza muda kupata maoni ya wahusika wenyewe. Je, Wamisri wa zamani wenyewe walijionaje? Walijiweka katika kundi gani? Walijiitaje? Lugha na maandishi tuliyoachiwa na Wamisri wa enzi za Mafarao hutoa majibu kamili kabisa kuhusu maswali haya, majibu ambayo wataalamu wa aina mbalimbali huona lazima wayapuuze, wayapotoshe au "wayatafsiri" waonavyo wenyewe.

Wamisri walitumia neno moja tu kujitita = *kmt* (kwa maana sisi) = wanegro. Hili ni neno la wazi kabisa lipatikanalo katika lugha ya Kifarao kuonyesha weusi. Neno hili ndilo kiini cha shina *kamit* ambalo limeenea katika vitabu vya kisasa vya anthropolojia. Shina la kibiblia "*kam*" limetokana na neno hilo na kwa hiyo imekuwa lazima kupotosha mambo kuliwezesha shina hili kuwa na maana ya "eupe" katika utaalamu wa Misri ya kale ambapo katika lugha asilia ya Kifarao, ambayo ndiyo chanzo chake, lilikuwa na maana ya "eusi."

Ni jambo linalopaswa kusisitizwa kwamba Wamisri wa zamani eti hawakupata kamwe wazo la kutumia visifa hivi kwa Wanubi na watu wengine wa Afrika ili kujitofantisha nao. Wamisri walitumia neno = *nahas* kuwaita Wanubi. *Nahas* ni jina la watu katika Kimisri ambalo halileti wazo la rangi. Kwa hiyo ni tafsiri mbaya ya makusudi kabisa kulipa neno hilo inaana ya "eusi" kama ifanyikavyo katika karibu vitabu vyote vya siku hizi.

Visifa vya kimungu

Mwisho kabisa 'mweusi' au 'mnegro' ni neno linalotumiwa kila mara

linapoambatanishwa na miungu wapaji wa Misri ambapo mashetani wote hupewa kisifa cha desret = ekundu. Tunajua pia kwamba kwa Waafrika neno hili lilitumiwa kuhusu watu wa mataifa meupe; kuna uwezekano mkubwa sana kwamba lilitumika likiwa na maana hiyo hiyo na Wamisri pia, lakini ningependa katika sura hii kugusia mambo ambayo hayazushi ubishi mwingi sana.

Majina ya ukoo ya miungu ni haya:

- = *Kmwr* = “Mnegro Mkuu” yaani Osiris.
- = *Km* = mweusi + jina la mungu wa kiume
- = *Kmt* = mweusi + jina la mungu wa kike

Kisifa *Km* (eusi) hutumika kuhusiana na Hathor, Apis, Min, Thoth, n.k. Alama set *Kmt* = mwanamke mweusi = *Isis*. Upande mwingine ‘seth,’ yaani jangwa tasa, hupewa kisifa *desret* = ekundu. Wanyama pori aliopigana nao Horus ili kulea ustaarabu huambatanishwa na kisifa dešê = ekundu, hasa kiboko.

Ushahidi wa biblia

Biblia hutuambia: ‘...Watoto wa Ham walikuwa Kush na Mizraim (yaani Misri), na Phut, na Canaan. Na watoto wa Kushi, Seba, na Havilath na Sabtah, na Raamah, na Sabtechah.’

Kwa jumla watu wote wenye asili ya Kisemitiki (Wayahudi na Waarabu) huiweka Misri katika fungu la nchi za watu weusi.

Umuhimu wa ushahidi huu hauwezi kupuuzwa kwa sababu watu hawa (Wayahudi) walioishi pamoja nao hawakuwa na sababu yoyote ya kuwapamba na kabila la uongo. Haikubaliki pia kusema kwamba mambo hayakutafsiriwa vilivyo.

Ushahidi wa mambo ya kitamaduni

Tunataka kuongelea kuhusu kutahiri na sanamu zilizotumika katika tambiko tu kati ya mila nyingi sana za kitamaduni zilizohifadhiwa Misri na katika Afrika na ambazo zinafanana kabisa.

Kufuatana na dondoo kutoka kwenye maandishi ya Herodotus aliyenukuliwa hapo awali, desturi ya kutahiri ina asili ya Kiafrika. Utaalamu wa akiolojia umethibitisha wazo la Herodotus na Elliot - Smith ametuthibitishia kwamba kutahiri kulikuwa jambo la kawaida kati ya Wamisri wa zamani hata katika enzi za historia ya awali yaani kabla ya mwaka - 4000. Alifikia hitimisho hili baada ya kuchunguza maiti za zainani za Kimisri zilizohifadhiwa vizuri sana.

Kutambika katika koo mbalimbali kwa kutunia sanamu ya aina moja kuliendelea mpaka siku za Warumi; Plutarch pia anagusia jambo hili. Utafiti wa Amelineau, Loret, Moret na Adolf Reinach umeonyesha wazi kuwepo kwa mila hii katika Misri.

Kufanana kwa lugha

Kiwolof, ambayo ni lugha ya Senegal isemwayo inagharibi kabisa mwa Afrika, pwani ya Bahari ya Atlantiki, imekaribiana sana na Kimisri cha zamani kama kikoptiki kilivyo. Uchunguzi mkubwa sana na wa undani kabisa kuhusu jambo hili umefanyika hivi karibuni. Katika sura hii mifano ya kutosha itatolewa kuonyeshwa kwamba uhusiano kati ya Kimisri cha zamani na lugha za Kiafrika si wa kuzua tu bali unaweza kuonyeshwa wazi wazi, na wataalamu wa sasa hawawezi kuupuuza.

Kama tutakavyoona kufanana kwa maneno hayo kuna asili ya kinasaba.

KIMISRI	→	KIKOPTIKI	KIWOLOF
= <i>Kef</i> =	kushika, kuchukua kipande (cha kitu)	(Lugha ndogo ya Saidiki)	<i>Kef</i> = kukamata mawindo
		<i>Keh</i> = kufuga	

KIMISRI	KIWOLOF
= <i>feh</i> = kuondoka	<i>feh</i> = kuondoka kwa kasi

Tuna uwiano ufuatao kati ya maunbo ya vitenzi na usawa au kufanana kwa maana: vitenzi vyote vya Kimisri vimo pia katika lugha ya Kiwolof isipokuwa vitenzi viwili.

KIMISRI	KIWOLOF
feh - ef	feh - ef
feh - es	feh - es
feh - n - ef	feh - on - ef
feh - n - es	feh - on - es
feh - w	feh - w
feh - wef	feh - w - ef
feh - w - es	feh - w - es
feh - w - n - ef	feh - w - on - es
feh - w - n - es	feh - w - on - es
feh - in - ef	feh - il - ef
feh - in - es	feh - il - es
feh - t - ef	feh - t - ef
feh - t - es	feh - t - es
feh-tyfy	feh-ati-fy
feh-tysy	feh-at-ef
feh-tw-ef	mar-tw-ef
feh-tw-es	mar-tw-es
feh-kw(i)	fahi-kw

feh-n-tw-ef
 feh-n-tw-es
 feh-y-ef
 feh-y-es

feh-an-tw-ef
 feh-an-tw-es
 eh-y-ef
 feh-y-es

KIMISRI

KIWOLOF

mer = mapenzi

mar = lamba

Vionyeshi Vya Kiwolof na Kimisri

Kuna uwiano wa kifonetiki ufuatao kati ya vionyeshi vya Kimisri na vile vya Kiwolof.

KIMISRI

KIWOLOF

= pw
 (ipw) → bw

ep → w
 p → b
 w → w

= pwy
 (ipw) → bwy

p → b
 w → w
 y → y

= pn {bane
 ipn → { bale →

p → b.
 n → n
 p → b

n → I

= pf bafe
 (ipf) →

p → b
 f → f

= pf3 → bafa

p → b
 f → f
 3 → a

= pfy
 ipfy → bafy

p → b
 f → f
 y → y

= p3 → ba

p → b

= iptw → batw	3 → â p → b t → t w → w
= iptn → batné Batalé	p → b t → t n → n n → l
= iptf batafé	p → b
= iptf	t → t f → t

Ulinganifu wa namna hii ungeweza kuendelezwa kuonyesha kwamba fonimu nyingi zaidi hazibadiliki kati ya lugha hizo mbili. Mabadiliko machache ambayo yanapaswa kuangaliwa kwa makini ni haya yafuatayo:

(a) Uwiano n (M) → l (W)

KIMISRI

n
= nad = omba; uliza
= nah = linda
= ben ben = ibuka (maji)
= teni = zeeka
= tefnwt = mungu wa kike
aliyezaliwa na kwa mate ya Ra

= nebt = suka

KIWOLOF

l
lad = omba; uliza
lah = linda
bel, bel - ibuka (maji)
tale = muhimu
tefnit = "tema" mtu

reflit → = mate

tefli → = mtemaji

let = suka

nab = suka nywele kwa muda

(b) Uwiano h (Kimisri) → g (Kiwolof)

KIMISRI

h
= hen = sanamu ya mboo
inayotambikiwa
= hwn = kijana aliyebalehe
= hor = Horus
= hor gwn = kijana Horus

KIWOLOF

g
gen = sanamu ya mboo
inayotambikiwa
gwne) =
gone) = kijana aliyebalehe
gor = vir (niwanaume?)
gor gwné = kijana wa kiume
(m.ä.m)

Ni mapema mno kuongea kwa uhakika kuhusu sauti zinazoambatana na fonimu za Kimisri. Lakini njia ni wazi kugundua tena sauti za Kimisri cha kale kwa kukilinganisha na lugha nyingine za Afrika katika uchunguzi.

Hitimisho

Muundo wa jamii za kifalme za Kiafrika, hadi kifo cha Mfalme, ikiwa kifo halisi au cha kiishara, baada ya enzi ambayo ilitofautiana lakini iliyokuwepo kwa miaka minane, una kumbusha maadhiinisho ya ufufuo wa Farao katika sherehe ya Sedi. Pia kumbukumbu za Misri ni pamoja na taratibu za kutahiri zilizotajwa hapo awali na utambikaji, nadharia kuhusu chanzo cha ulimwengu, usanii majengo, ala za muziki, n.k. za Afrika ya giza. Manibo ya kale ya Kimisri ni kwa utamaduni wa Kiafrika ambapo mambo ya zamani ya Kigiriki (Graeco) - Kiroma ni kwa utamaduni wa magharibi. Kuongezeka kwa mkusanyiko wa mambo ya kiutu kunapaswa kugemezwa katika hoja hizi.

Itaeleweka jinsi ilivyo vigumu kuandika sura hii katika kazi ya aina hii, ambapo tasifida na maafikiano ni sheria. Katika kujaribu kuepuka kafara ya ukweli wa kisayansi, tulijenga hoja ya kushauri mambo matatu ya awali katika maandalizi ya juzuu hili; yote yaliyokubaliwa katika kikao chenye uwezo kilichofanyika 1971. Mbili za mwanzo zilipelekea kufanyika kwa kongamano huko Misri kuanzia Januari 28 hadi Februari 3 inwaka 1974. Kutokana na hili ningependa kurejelea katika kurasa kadhaa katika taarifa kuhusu kongamano hilo. Profesa Vercoutter, ambaye alitumwa na Unesco kuandika utangulizi wa taarifa iliyofikiwa baada ya mjadala wa kina, kuwa wazo lililoafikiwa kuwa watu wa Misri walikuwa wamegawanyika katika idadi sawa kati ya weusi, waupe na machotora, haliwezi kuungwa mkono. Kwa upande wa utamaduni wa Wamisri usio huru. Profesa Vercoutter alibainisha kuwa, katika mtizamo wake, namna ya uandishi wake Misri ilikuwa Afrika, kiutamaduni na namna ya kufikiri (kifikra).

Profesa Leclant kwa upande wake 'alitambua tabia ile ile ya Kiafrika katika silika na fikra za Wamisri'.

Kulingana na isimu inaelezwa katika ripoti kuwa kipengee hiki, kikitofautishwa na vile vilivyoadiliwa awali, kinahakiki kiwango kikubwa cha makubaliano miongoni mwa washiriki. Muhtasari wa taarifa ya Profesa Diop na ripoti ya Profesa Obenga ilichukuliwa kama yenye maoni kuntu.

Vilevile kongamano lilikataa wazo kuwa Kifarao cha Misri ilikuwa lugha ya mamlaka. Kugeukia katika suala pana Profesa Sauneron alitaka umakini mvuto wa njia iliyoshauriwa na Profesa Obenga kumsuatia ile ya Profesa Diop. Kimisri kilibaki lugha thabiti kwa kipindi kisichopungua miaka 4500. Misri ilikuwapo katika mahala pa makutano ya athari za nje na inategemewa kuwa ukopwaji ulifanywa kutoka lugha za kigeni, lakini lugha ya mamlaka ilikuwa na idadi ndogo ya maneno ikilinganishwa na jumla ya maelfu mengi ya maneno. Lugha ya Kimisri haiwezi ikatengwa katika

muktadha wake wa Kiafrika na uasili wake usingeweza kuelezwa kwa undani kutokana na lugha ya mamlaka; kwahiyo ilikuwa kawaida kutegemea kukuta lugha zinazofanana katika Afrika.


Kinasaba, ndio kusema uhusiano wa kibahati kati ya lugha ya Kiinisri na lugha ya Kiafrika ulitambuliwa; Profesa Sauneron alibainisha kuwa njia iliyotumika ilikuwa ya kuaminika na kuvutia. Tena hangeweza kubahatisha kabisa kuwa kulikuwa na mfanano kati ya kiambishi tamati cha nafsi ya tatu, umoja katika Kimisri cha kale na Kiwolof; alitumaini kuwa jaribio litafanywa kufufua lugha ya Kiafrika ya Paleo kwa kutumia lugha za sasa kama sehemu ya kuanzia. Sura mpya ya maelezo ya historia ya Kiafrika iliandikwa vilivyo huko Kairo. Kongamamo lilishauri kuwa utafiti zaidi ufanyike katika dhana ya mbari. Tafiti kama hizo zimekuwa zikifanyika, lakini hazijachangia kitu chochote kipya katika njadala wa kihistoria.

Kugunduliwa tena kwa ukweli wa zamani wa watu wa Afrika kusichukuliwe kuwa kigezo cha mgawanyo, lakini inapaswa kuchangia kuwaunganisha. Kila mmoja na wote, kuwaweka pamoja kutoka kaskazini hadi kusini mwa bara ili kuwawezesha kueleza kwa pamoja ujumbe wa historia mpya kulusu mambo mazuri ya wanadamu; na hii inalingana na mawazo sahihi Unesco .

KIDOKEZO CHA MHARIRI WA JUZUU

Maoni yaliyotolewa na Profesa Cheikh Anta Diop katika sura hii ni yale ambayo aliyawasilisha na kuyaendeleza katika kongamano la Unesco kulusu 'Wakazi wa Misri ya zamani' lililofanyika Kairo mwaka 1974. Hoja zilizowekwa mbele katika sura hii bado hazijakubaliwa na wataalamu wote waliovutiwa na suala hili. (taz. utangulizi, juu).

Gamal MOKHTAR



*Nyongeza ya sura ya kwanza:
Taarifa ya kongamano kuhusu
'kukaliwa kwa misri ya zamani na
ufumbuzi wa maandishi ya
Kimeroe'¹*

Kairo, 28 Januari – 3 Februari 1974

Muhtasari wa taarifa zilizojadiliwa²

Kongamano lilifanyika kwa awamu mbili: la kwanza lilifanyika kutoka tarehe 28 mpaka 31 Januari 1974; ilihusu 'Makazi ya Misri ya Kale.' Awamu ya pili ilihusu "Ufumbuzi wa Maandishi ya Kimeroe" na ilifanyika kutoka tarehe 1 mpaka 3 Februari 1974.

Waliohudhuria walikuwa wafuatao:

- Profesa Abdelgadir M. Abdalla (Sudan)
- Profesa Abu Bakr (Jamhuri ya Kiarabu ya Misri)
- Bibi N. Blanc (Ufaransa)
- Profesa F. Debono (Malta)
- Profesa J. Devisse (Ufaransa)
- Profesa Cheikh Anta Diop (Senegal)
- Profesa Ghallab (Jamhuri ya Kiarabu ya Misri)
- Bibi J. Gordon B. Jaquet (U.S.A.)
- Profesa L. Habanchi (Jamhuri ya Kiarabu ya Misri)
- Profesa R. Holthoer (Finland)
- Profesa S. Husein (Jamhuri ya Kiarabu ya Misri)
- Profesa Kaiser (Jamhuri ya Ujerumani)
- Profesa J. Leclant (Ufaransa)

¹ Kiambatisho kilipaswa kuingizwa kama Kiambatisho cha juzuu zima na kuwekwa mwisho baada ya Hitimisho.

² Taarifa hii ni kifupisho cha taarifa kamili ya kongamano. Ilitayarishwa na Waandishi wa Kongamano wa Kamati ya Kimataifa ya Kisayansi kwa kuombwa na Kamati, ili kuingizwa kwenye juzuu hili. Makala za kongamano zimechapishwa kwenye mfululizo wa The General History of Africa - Studies and Documents No. 1, Unesco, Paris, 1978.

Profesa G. Mokhtar (Jamhuri ya Kiarabu ya Misri)
 Profesa R. El Nadury (Jamhuri ya Kiarabu ya Misri)
 Profesa Th. Obenga (Jamhuri ya Watu wa Kongo)
 Profesa S. Sauneron (Ufaransa)
 Profesa T. Save-Soderbergh (Sweden)
 Profesa P.L. Shinnie (Canada)
 Profesa J. Vercoutter (Ufaransa)

Profesa Hintze (Jamhuri ya Kidemokrasi ya (Burkina Faso) (Ujeruman), Profesa Knorossov, Profesa Piotrovsk (USSR) na Profesa Ki-Zerbo (Upper Volta) walialikwa kwenye kongamano lakini hawakuweza kuhudhuria na waliomba radhi.

Kulingana na uamuzi wa Kamati ya Kisayansi ya Kimataifa, Profesa J. Devisse, Katibu wa Kamati alikuwapo na aliandika ripoti ya mwisho ya kongamano.

UNESCO iliwakilishwa na Bw. Maurice Glélé, mtaalamu wa mipango katika Idara ya Uchunguzi wa Utamaduni; alikuja kumwakilisha Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO. Pia kutoka UNESCO alikuja Bibi Monique Melcer wa Idara ya Uchunguzi wa Utamaduni.

1 Kongamano kuhusu Makazi ya Misri ya Zamani

Makala mbili ambazo UNESCO iliwaomba Profesa J. Vercoutter na Bibi N. Blanc³ kuandaa ndizo zilituniwa kama msingi wa majadiliano.

Hatua tatu muhimu zinaweza kuonekana katika majadiliano.

- A. Muhtasari wa Makala za Utangulizi
- B. Hoja za awali zilizotolewa na idadi kubwa ya wale walioshiriki
- C. Majadiliano kwa jumla.

A. Muhtasari wa makala za utangulizi

(1) Profesa Vercoutter alitilia mkazo mawazo kadhaa aliyokuwa ameyazungumzia kwa kirefu na kwa undani zaidi katika ripoti aliyoiandika. Alitoa pia maoni kadhaa kama ifuatavyo:

- (a) Ingawa kumekuwa na maendeleo siku za karibuni, anthropolojia ya viumbe ilikuwa mpaka sasa imetoa ushahidi kidogo sana wa kuaminika isipokuwa kuhusu Urubi. Habari zilizokuwapo hazikutosha kuwezesha kufanya mahitimu ya awali kuhusu makazi ya watu wa Misri ya Kale na hatua mbalimbali zilizopitiwa katika shughuli hiyo. Zaidi ya hayo, habari hizi hazikuwa zinakubaliana kabisa kuhusu wakati na mahali matukio mbalimbali yalikotokea na wanahistoria hawakukubaliana mara nyingi jinsi ya kuzitafsiri. Hata njia za

³

Nyaraka hizi zimeambatanishwa kwenye Taarifa Kamili, 1974

utafiti na uchambuzi zenyewe zilianza kushambuliwa. Ilikuwa imekubalika na wataalamu wengi kwamba uchunguzi unaotumia njia ya kupima mafuvu haukuridhisha yale yote yaliyokuwa yanatakikana katika uchunguzi wa namna hii.

Sehemu nyingi zilikuwa bado hazijachunguzwa kwa undami. Hii ilikuwa kweli kuhusu sehemu yote ya delta ya mto Nili kabla ya enzi za ufalme, na Misri ya juu kabla ya enzi za Neolithiki. Habari kidogo tu zilijulikana juu ya sehemu kati ya

Maporomoko ya pili na Maporomoko ya Sita katika enzi za Neolithiki na katika kipindi cha Ufalme wa awali. Uhusiano uliokuwapo siku za zamani kati ya jangwa la Sahara, Darfur, na mto Nili ulikuwa umechunguzwa kidogo sana mpaka hapo.

Mambo yote haya yakiangaliwa kwa pamoja, kazi iliyokuwa imefanywa ilikuwa nyuma sana ya ile iliyokuwa imekamiliwa Afrika ya Kaskazini na katika Ukanda wa Siria na Palestina.

Ushahidi uliopo sasa haukufanya iwezekane kusema kwamba watu wa Misri ya Kaskazini walikuwa tofauti na wale wa Misri ya Kusini. Vivyo hivyo yawezekana pengo kati ya enzi za Paleolithiki na zile za Neolithiki lilitokana na sababu kwamba hata utafiti kidogo ulikuwa haujaanyika uwandani kuhusu vipindi hivyo.

- (b) Usawiri ulikuwa haujatumiwa vya kutosha na kwa namna ya kuridhisha katika utafiti; uchunguzi uliokwisha fanywa ulitegemea mno vigezo vya kitamaduni. Lakini Sanamu za usawiri zilizopo zilipata tu maumbile muhimu sana kuanzia ufalme wa kuni na nane na kuendelea.
- (c) Madondoo ya nadharia mbili zinazopigana mno:

- (i) Watu walioishi Misri ya kale, hata wakati kabla ya enzi za ufalme walikuwa "Aweupe" ingawa rangi ya ngozi zao ilikuwa ya kahawia au hata nyeusi.

Wanegro walianza kuonekana kuanzia ufalme wa kuni na nane na kuendelea.

Baadhi ya wataalamu waliamini kwamba kuanzia siku za mwanzo za enzi za ufalme watu walibaki vilevile; lakini wengine waliamini kwamba kuingiliwa kwa Afrika na wageni kulibadilisha kabisa hali ya maisha ya kitamaduni.

- (ii) Misri ya kale ilikaliwa na Waafrika weusi "tangu mwanzo kabisa wa siku za Neolithiki mpaka mwisho wa enzi za falme za vizalia."

- (2) Bibi Blanc alitoa inaelezo kuhusu matokeo ya utafiti wake.

- (a) Alitilia maanani wazo kwamba kwa ajili yasababu ambazo nazo ni za kilistoria, maandishi juu ya historia ya mabonde ya mto Nili yalikuwa yametegemea dhana isemayo kwamba palikuwa na bonde la Kimisri lililokuwa limestaarabika na lililokuwa na ushahidi mwingi wa kihistoria, na bonde jingine kusini zaidi ambalo lilikaliwa na watu weusi waliokuwa bado hawajastaarabika. Utafiti juu ya sehemu hii ya kusini iliwavutia tu wanaanthropolojia. Bibi Blanc alitumaini kwamba katika siku za usoni utafiti

wa kihistoria wa bonde lote ungepewa uzito sawa. Jambo hili lingemaanisha kuachwa kwa njia za kale za utafiti wa kihistoria na kupanuliwa kwa uchunguzi wa kutumia njia mpya. Bibi Blanc alifikiri kwamba kazi ambayo ilikuwa inafanyika huko Nubia kwa miaka kama ishirini ilikuwa ni hatua ya mwanzo katika kuchunguza upya swali lililokuwa limewasilishwa katika kongamano.

- (b) Bibi Blanc aliwaomba wahudhuriaji waangalie kwa uangalifu zaidi sehemu ya bonde la mto Nili kati ya latitudo ya ishirini na tatu Kaskazini mwa Ikweta na mwanzo wa mto huko Uganda ili kuepukana na mtazamo wa zamani kuhusu bonde la mto Nili. Katika mtazamo huu wa zamani maendeleo ya kihistoria yalianza kaskazini na kuelekea kusini kutoka kwa watu “waliostaarabika zaidi” kwenda kwa wale “waliostaarabika kidogo tu.” Uchambuzi wake ulitilia maanani mstari wa mgawanyo ambao ni latitudo kumi kaskazini mwa Ikweta mahali ambapo kujiingiza kwa Uislamu kuelekea Kusini kulikonca. Mstari huu ulikuwa muhimu sana kimazingira.

Kwa kuwa into Nili ulikuwa unapitika kati ya latitudo ishirini na tatu na latitudo kumi, ungeweza kuleta maendeleo kama yale yaliyotokea kaskazini zaidi huko Misri. Haya hayakutokea na bila shaka hali ya mazingira katika sehemu hizi za mto ndiyo sababu kubwa.

Bibi Blanc aliendelea kufanya uchambuzi wa jumla akitumia maelezo haya kuhusu mchango wa watu waliokaa mahali pamoja na wale wanaohamama katika kulcta maendeleo.

Lakini, kisha kuangalia historia ya mabadiliko ya watu tangu kufika kwa Waislamu wa Kiarabu, alitilia mkazo kuangalia upya dhana mbalimbali kuhusu kukaliwa kwa sehemu hii kabla ya kufika kwa Waarabu. Alisisitiza kwamba bonde la into Nili lilifanikisha mawasiliano baina ya Afrika ya Magharibi na Afrika Kusini mwa jangwa la Sahara. Lilikuwa pia wazo zuri kufikiri kwamba ustaarabu uliobuka huko kimsingi ulikuwa wa Kiafrika na sio wa mchanganyiko kati ya ule wa sehemu ya Bahari ya Kati na Afrika ya watu weusi.

Upande wa magharibi kuna Darfur, nchi ambayo ilikuwa kiini na kituo cha maendeleo ingawa watu wanafahamu mambo machache sana kuhusu muundo wake wa jamii na siasa kabla ya karne ya kumi na saba.

Sehemu kati ya Mto Nili na Bahari Nyekundu ikaliwayo na Wabeja ilikaliwa na wakazi kwa shida tu sababu ya hali yake ngumu ya mazingira.

Upande wa mashariki, eneo la Sennar, lililokaliwa na Wafundj, ilikuwa ni kituo cha ‘usultani mweusi’ ambao asili yake haikiwa Kiarabu au Kiislamu.

Ukanda baina ya Nili na Bahari ya Shamu uliokaliwa na Wabedja ulikuwa hauwezi kuhimili watu wenye makazi ya kudunuu, kutokana na mazingira mabaya.

Kusini mwa latitudo ya kumi hali ya mazingira ilikuwa tofauti kabisa. Katika sehemu hii kulikuwa na makundi ya watu waliotawanyika hapa na pale ambayo utafiti

wa kiakiolojia na mapokeo simulizi umetoa habari chache tu juu yake. Nadharia tete kuhusu kukaliwa kwa sehemu hii na historia yake leo hii zina ushahidi mdogo sana wa kuaminika. Ni katika mikoa ya kusini zaidi kwenye ukanda wa maziwa makubwa Afrika Mashariki ndiko uchunguzi wa kihistoria ulipokwishafanyika kwa makini zaidi.

B. Hoja za awali zilizotolewa na washiriki

(1) Profesa Save-Soderbergh alitoa taarifa kuhusu machimbo ya Waskandinavia nchini Sudan yaliyofanywa kati ya miaka 1960 na 1964. Machimbo haya yalithibitisha kwamba palikuwa na uhusiano kati ya bonde la mto Nili na Afrika ya Kaskazini na Sahara. Mambo yaliyogusiwa baadaye katika maandishi yalihusu picha 7000 zilizochorwa kwenye miamba na uchambuzi wa mabaki ya watu 1546. Van Nielson alikuwa ameeleza uhusiano uliopo kati ya Kundi A, Kundi C, Kundi la Ufalme Mpya na kadhalika. Ulinganishi wa kazi inbalimbali za utafiti zilikuwa na matokeo tofauti kutegemea hasa mbinu za uchunguzi zilizotumiwa, kama ni uchunguzi wa mafuvu tu au wa mambo ya kiantropolojia na teknolojia kwa jumla. Matokeo ya uchunguzi wa usawiri na antropolojia yaliunga mkono wazo la uhamaji wa watu wa Sahara na wa makundi kutoka kusini na kwamba hawa wote walikuwa na uhusiano mkubwa sana na Wamisri wa kale. Kuhusu kipindi cha kati cha Mesolithiki, ulinganishi ulifanywa kutokana na mifupa isiyozidi 100. Mahitimisho ya kuaminika hayakuweza kufikiwa kuhusu Unubi ingawa habari za kuaminika zaidi zilipatikana kuhusu kipindi cha Neolithiki.

Jambo muhimu la kakumbuka ni kwamba Profesa Save-Soderbergh alifikiri kwamba ilikuwa haiwezekani kabisa kufanya tofauti za kitaifa kuwa msingi wa uchunguzi unaohusu kukaliwa kwa Misri siku za zamani au uchunguzi mwingine wowote wa namna hii. Katika siku za usoni njia nyingine za uchunguzi zinapaswa kufuatwa. Aina tofauti za utamaduni zilizokuwepo wakati mmoja hali zikiwa zimetengana, zingeweza kabisa kuwa sehemu ya mfumo mmoja wa teknolojia. Njia hii mpya ilithibitisha kwamba Misri ilikuwa sehemu ya Afrika. Lakini mtu alipoangalia mbele zaidi ya ufumbuzi huu, ilikuwa wazi kwamba kulikuwa na matatizo mengine mengi zaidi. Nagada I na II hazikuwa sehemu ya mfumo mmoja wa teknolojia na Nubia au Sudan ya wakati ule. Nchimi Sudan sehemu kutoka Kasaala mpaka Chad na kutoka Wadi Halfa mpaka Khartoum ilikuwa sehemu moja kubwa iliyokuwa na mfumo mmoja wa teknolojia. Kundi A lilikuwa mfumo inwingine wa teknolojia ya karibuni kati ya Maporomoko ya Kwanza na ya Tatu.

(2) Profesa Cheikh Anta Diop alitoa maelezo marefu ya mawazo yake. Alifupisha mada yake kwa kudondoa maoni muhimu kama ifuatavyo:

(a) Kulingana na mtazamo wa kiantropolojia, utafiti uliofanywa tangu uvumbuzi wa Profesa Leakey umewezesha kufikiwa kwa hitimisho kwamba binadamu walianza kuishi Afrika katika sehemu za mwanzo wa mto Nili. Sheria ya Gloger

ambayo ingeweza kutumiwa kwa binadamu kama inavyotumiwa kwa viumbe wengine inasema kwamba viumbe wenye damu yenye joto waliokulia na kubadilikabadilika katika hali ya hewa ya joto na yenye unyevunyevu walikuwa na rangi ya ngozi nyeusi (melanini). Kwa hiyo binadamu wa kwanza kabisa duniani walikuwa wa namna moja tu kikabila na walikuwa weusi. Watu hawa walitawanyika duniani kutoka sehemu hii ya mwanzo na kufikia sehemu nyingine za dunia kwa kupitia njia mbili tu: bonde la mto Nili na jangwa la Sahara.

Katika bonde la mto Nili mtawanyiko huu ulianza kusini kwenda kaskazini. Watu walitawanyika polepole kati ya mwanzo wa enzi za Paleolithiki na wakati wa historia ya awali.

Hata Profesa Massoulard amefikia hitimisho kwamba watu wa Misri ya kale waligawanyika labda katika makundi matatu ya kitaifa: watu weusi waliokuwa zaidi ya theluthi moja ya watu wote, watu wa aina ya Mediterania na watu wa aina ya Kromagnoni. Profesa Diop alielekea kusema kwamba kutokana na mgawanyiko huo, watu wa Misri walikuwa hasa weusi kabla ya enzi za ufalme. Hitimisho hili linapinga wazo lisemalo kwamba watu weusi waliingia Misri baadaye zaidi.

Mifupa ya watu waliokufa zamani sana kabla desturi ya kuhifadhi maiti haijaanza iligunduliwa na Elliot Smith ikiwa na vipande vya ngozi. Profesa Diop alisena kwamba vipande hivi vya ngozi vilikuwa na kiasi kikubwa cha melanini kilichoviwezesha kutambulikana kama ngozi za watu weusi.

Katika harakati za kutafuta ushahidi kamili, Profesa Diop alikuwa ameangalia vielelezo vichache vilivyochunguzwa katika maabara mjini Dakar. Vielelezo hivi vilikuwa vipande vyangozi vilivyotolewa kwenye mumiani zilizogunduliwa katika machimbo ya Mariette. Vyote vilionyesha kuwepo kwa melanini nyingi sana kati ya ngozi ya juu kabisa na ngozi nene ya chini. Profesa Diop aliwaomba wataalamu waliokuwapo kuchunguza vielelezo hivi. Melanini ambayo haipatikani katika ngozi za watu weupe ilibaki kwa mamilioni ya miaka (kinyume na uthibitisho wa mara kwa mara uliofanywa awali) kama vilivyoonekana baada ya kuchunguza ngozi za wanyama wenye niufupa. Profesa Diop alitumaini kwamba angepewa fursa ya kufanya uchunguzi wa aina hiyohiyo akitumia ngozi kwenye mumiani za Mafarao zilizokuwa zimehifadhiwa katika Jumba la Makumbusho la Kairo.

Aliendelea kusema kwamba uchunguzi kamili wa kiantropolojia ungeangalia pia vipimo vya mifupa na aina ya damu. Kwa mfano, mi jambo linalohitaji kuangaliwa kwa makini kwamba Wamisri wa siku hizi na hasa wale wa Misri ya juu wana kundi la damu B sawa na watu wa Afrika ya Magharibi na siyo kundi A2 ambayo huwa ndiyo wanayo watu weupe.

- (b) *Usawiri:* Profesa Diop, akitumia mchoro mmoja muhimu wa usawiri na maelezo yaliyotolewa juu yake, alidadi kwamba haikuwa laziuna kushikilia

mambo madogo madogo ambayo kwa mfano yaliwatofautisha katika misingi ya kitabaka, watu weusi na watu wengine ambao walikuwa wa familia za kifalme waliopatikana katika kaburi moja. Michoro hii iliwapambanua watu wa kawaida na wale wa jamii iliyokuwa ikitawala.

- (c) Profesa Diop aliendelea kueleza juu ya ushahidi kutoka kwenye maandishi ya kale. Alionyesha kwamba maandishi wa Kiyunani na Kirumi waliwaeleza Wamisri kama watu weusi. Alirejea maandishi ya Herodotus, Aristotle, Lusiano, Apollodorus, Chylus, Achilles, Titius, Strabo, Diodorus, Siculus, Diogenes Laertius, na Ammianus Marsellinus. Aliendelea kusema kwamba wasomi wa siku hizi walikataa kuangalia maandishi hayo, ingawa mwandishi mmoja wa karne ya kumi na nane, Volney, alisema kwamba Wamisri wa Kale walikuwa weusi. Zaidi ya hayo, mapokeo ya kibiblia nayo yameonyesha nchi ya Misri kama nchi ya watoto wa Ham. Profesa Diop alisema kwamba Sayansi ya Elimu juu ya Misri ya zamani ambayo hasa ni zao la ubeberu inahusika sana katika kuyakana yale yote aliyoyadondoa.
- (c) Profesa Diop aliendelea kueleza jinsi Wamisri wenyewe walivyojiona. Walitumia neno moja tu kujieleza: KMT⁵ “neno lenye uzito kuliko yote katika lugha ya Mafarao kueleza weusi,” Profesa Diop alilitafsiri neno hili kama “Negro” au watu weusi. Matokeo yake maandiko B picha yaliyowakilisha neno hili hayakuandikwa kwa magamba ya namba bali kwa kipande cha mkaa.

(3) Profesa Debono alitoa maoni marefu kuhusu habari zilizoimo katika Juzuu la Kwanza.

(4) Profesa Leclant alianza kwa kutilia mkazo maumbile ya Kiafrika katika ustaarabu wa Kimisri. Lakini ilikuwa lazima kupambanua bayana kati ya “taifa” na utamaduni, alivyokuwa amekwishafanya Profesa vercouter.

Anthropolojia maumbo ya Misri ilikuwa ingali changa. Hata hivyo, hapakuwa na sababu yoyote ya kuendelea kutegemea uchunguzi uliokwishachujaka wa akina Chantre, Elliot Smith, Sergi, au Dr. Derry. Zaidi ya hayo mambo yanayojulikana sasa yalikuwa yanekwishaelezwa vipya kabisa na watu kama Wierczinski⁶. Makundi ya wataalam waliokuwa wakifanya uchunguzi huko Unubi yalikuwa yameonyesha pia kupendelea anthropolojia maumbo. Mapendeleo yao haya yalifanya Unubi ambao haukuwa na mabaki mengi ya kiakiolojia ujulikane kuliko hata Misri⁷ kwenye masuala hayo. Misafara ya kiakiolojia ilianza kuupa uzito zaidi uchunguzi wa osteolojia, somo ambalo kuibuka kwake kumepokelewa vizuri sana⁸.

⁵ Neno hili lilizaa neno ‘Hamite’ ambalo limekuwa, ikitunika zaidi. Pia linapatikana kwenye Biblia kama ‘Ham’.

⁶ *Jarida la chama cha Jiografia cha Misri*, 31, 1958, uk. 73-83.

⁷ Profesa Leclant aliirejelea kazi ya Nielsen, Strouhal, Armelagos, Rogalsky, Prominska, Chemla na Billy

⁸ Angalia makala muhimu ya hivi karibuni, D.P. Van Gerven, D.S. Carlson na G.J. Armelagos, kwenye JAH, Juz. XIV na 4, 1973

Katika uchunguzi wa mambo ya kitamaduni, michoro kwenye miamba ambayo ilikuwa ikifanana sana kutoka Bahari ya Sham hadi Bahari ya Atlantiki ilistahili kuchunguzwa kwa makini sana. Alama hizi zilikuwa zimeachwa na inakundi yaliyofuatana ya kitamaduni, wawindaji, wachungaji, au wengineo.

Suala la kukaliwa kwa Misri ya Kale lilikuwa ni tatizo kubwa sana na itakuwa mapema mno kujaribu, katika hatua hii kulitatua kwa mkato. Tatizo hili linapaswa kukabiliwa kwa kufanya uchunguzi tofautitofauti ulio kamili. Ili kufanikisha kazi hii, ushirikiano wa wataalam katika taaluma ambazo hazikuwakilishwa kwenye kongamano ulikuwa wa lazima sana. Washiriki wote walikuwa “wanahistoria wa jumla” wenye uwezo wa kusanisi data zilizotolewa na wataalamu; mpaka sasa data kama hizo hazitoshelezi kabisa.

Kwa hali yoyote ile itakuwa ni hatua ya kurudi nyuma iwapo tutazidi kukimbilia kazi zilikwishapitwa na wakati kama zile za akina Lepsius au Petric. Ingefaa tu kutambua kazi hizi kama kazi zenye umuhimu kihistoria, lakini Elimu juu ya Misri ni dhahiri imekwishapiga hatua kubwa sana tokea kazi hizo zitokee.

Kuhusu ushahidi uliotokana na usawiri, tatizo tu lililokuwepo ni kujua jinsi Wamisri wenyewe walivyojiona kwa kujilinganisha na watu wengine. Walijiita RMT, (Rame) yaani “watu” hali wakiwaclukulia watu wengine kama umma usio na umbo maalumu uliozagaa katika pande zote za dira. Kwa mfano, sanamu za wafungwa huko Sakkara (Ufalme wa sita uliotawala miaka 2300 kabla ya enzi zetu) zinaonyesha baadhi yao walikuwa watu wa kaskazini (Waasia, Walibia) na baadhi nyingine watu wa kusini (Wanubi na Wanegro). Picha nyingine nyingi za watu wa kaskazini (weupe) na wa kusini (weusi) wakiwa chini ya viatu vya Farao ziuathibitisha jinsi Wamisri waliyowaclukulia watu wengine wote.

(5) Profesa Ghallab alizungumzia inambo fulani yaliyofuatana ambayo yangepambanuliwa kuhusiana na kukaliwa kwa Afrika na watu kati ya enzi za Paleolithiki na elfia ya tatu kabla ya enzi zetu.

Katika Afrika ya kaskazini mashariki vifaa vingi sana vya mawe vya kipindi cha pili cha mvua viligunduliwa katika bonde la mto Nili na katika maosisi. Profesa Ghallab alipambanua makabila kama sita hivi yaliyoishi Misri katika kipindi cha Mesolithiki wakiwa na utamaduni unaofanana. Alifikiri kwamba katika kipindi cha Paleolithiki binadamu walikuwa wakifanana kwa kila hali na wa jamii ya watu wa “Ulaya-Asia”. Watu wa kwanza weusi barani Afrika walikuwa Asselar na Omdurman. Katika miaka ya mwisho ya enzi za Paleolithiki jamii ya watu weusi walionekana toka Bahari ya Atlantiki mpaka Bahari ya Sham. Lakini zimeonekana dalili zinazoonyesha kwamba “Makoiki” ambao maumbile yao yalikuwa yamebadilishwa kidogo na hali ya mazingira ya Mediterania walikuwa kati ya Wamisri wa kale. Hata leo kuna mabaki ya aina hii ya watu kati ya Wamisri. Utamaduni wa watu weusi haukujitokeza kabla ya kipindi cha Neolithiki.

(6) Profesa Abdelgadir M. Abdalla hakuona unuhimu wa kujaribu kuthibitisha kama Wamisri wa kale walikuwa weusi au wanegro. Kilichohitaji kutazamwa ni

kipimo cha utamaduni waliokwisha kuujenga.

Ushahidi kutokana na usawiri ulionyeshwa wazi kabisa kwamba waanzilishi wa utamaduni wa Napata hawakufanana hata kidogo na Wamisri: maumbo ya miili yao yalikuwa tofauti kabisa. Kama Wamisri walikuwa weusi je watu wa Napata walikuwa na rangi gani?

Agigusia suala la isimu, Profesa Abdalla alisema kwamba neno KM (Kem) halikuwa na maana ya “eusi” na maneno yaliyotokana nalo hayakuhusiana hasa na rangi ya watu. Alitoa mfano wa isimu kuelezea nadharia yake ambayo ilikuwa tofauti na ile ya Profesa Diop. Alilitimisha kwamba lugha ya Kimisri haikuwa lugha ya Kiafrika pekee; ilikuwa katika kundi la lugha za proto-semitiki kama ilivyoweza kuonekana katika mifano mingi. Profesa Abdalla alisema kwamba mifano ya kiisimu iliyotolewa na Profesa Diop haikuwa ya kuaminika wala kamili na ilikuwa hatari kung’ang’amiza, bila kuweka hadhari snala la kuwepo kwa uhusiano kati ya lugha na muundo wa kabila au na mtu binafsi. Kufananisha lugha iliyokwisha kufa na lugha hai hakuwezi kudhihirisha mambo yote kikamilifu. Kufanana kulikoonyeshwa kati ya lugha hizi kulitokea kwa bahati tu na hadi leo hii hapajawa na taarifa kamili kuhusu jinsi lugha za kale za Kiafrika zilivyozuka. Ushahidi uliotolewa kueleza dhana ya uhusiano wa lugha unatetea zaidi nadharia ya kuenea kwa Kimisri cha kale katika Afrika kuliko nadharia ya uhusiano kati yake na lugha za Kiafrika zilizopo leo hii. Kuna misingi gani kwa mfano, ya kufanya ifikiriwe kwaniba Kimisri cha kale na Kiwolof vilikuwa na uhusiano, lakini kwamba uhusiano wa namna hiyo liaukuwapo kati ya Kimisri cha kale na Kimeroe. Lugha ya Napata na Kimeroe zilikuwa hazifanani kabisa.

Profesa Abdalla alitumaini kwamba uchunguzi ungeendelezwa kwa uangalifu nikubwa.

- (a) Alifikiri kwamba haiwezekani kuonyesha uwiano wa moja kwa moja kati ya kabila, mfumo wa uchumi na jamii na lugha.
- (b) Ilikuwa haiwezekani kufikia mahitimisho yenye msingi kisayansi kwa kujumlisha mambo mengi. Hakuna mifano ya historia ya uhamiaji wenye kuandamana na mabadiliko makubwa ya kitamaduni, isiyo na utata.
- (c) Hadileo hii wanaanthropolojia maumbo hawajafafanua sawasawa dhana “Unegro”. Mabaki ya mifupa hayawezi kutuniwa kutoa ushahidi juu ya rangi ya ngozi. Uthibitisho wa rangi yangozi unaweza kutokana tu na nyama na ngozi yenyewe.
- (d) Ilikuwa lazima kufanya uchunguzi wa ujuzi wa matibabu ya kale na mila za mazislii sasa hivi bila kuchelewa.

(7) Profesa Sauneron aliingilia kati wakati majadiliano ya kuisimua juu ya masuala ya Kiisimu kati ya Maprofesa Abdalla na Diop. Profesa Sauneron alisema kuwa katika Misri neno KM (la kike KMT) lilikuwa na maana ya “-eusi”; neno KMU

(kernou) lilikuwa wingi kiume na KMNT wingi kike. Muundo KMTYW ulikuwa na maana mbili tu: “Wale wa Kmt”, “wakazi wa Kmt” (“nchi nyeusi”). Neno hilo lilikuwa kivumishi kilichotokana na istilahi ya kijiografia ambayoilikuwa imekwishakuwa jina la pekee. Maana yake ya asili ilikuwa “haihisiki” katika umbo lake hili jipya. Ili kutoa maana ya “watu weusi” Wamisri wangalisema *Kmt* au *Kmu* na siyo *Kmtyw*. Hata hivyo, hawakutumia kivumishi hiki kuonyesha watu weusi wa barani Afrika waliokuwa wakiwafahamu tangu wakati wa Ufalme Mpya na kuendelea. Kwa jumla hawakutumia majina ya rangi kuwatofautisha watu mbalimbali.

(8) Profesa Obenga kwa upande wake alirudia maelezo yakiisimu aliyokuwa meyaanza Profesa Diop.

(a) Baada ya kuhakiki mbinu alizotumia Profesa Greelerg kulingana na maoni katika kazi mpya ya Profesa Istran Fodor⁹ na baada ya kutaja kwamba ushahidi wa Kiisimu ndio umekwishakubalika tokea enzi za Ferdinand de Saussure kama njia ya kuthibitisha kuwapo kwa uhusiano wa kitamaduni kati ya jamii, Profesa Obenga alijaribu yeye mwenyewe kuthibitisha kuwepo kwa uhusiano wa kijenetiki kati ya Kimisri (Kimisri cha kale na Kikoiti) na lugha za sasa za Kiafrika.

Kabla ya kulinganisha vitu, ni lazima kuwa macho kutochanganya uhusiano wa lugha kwa kufanana tu kwa baadhi ya vitu kusikodokeza hali katika lahaja za awali na uhusiano wa kijenetiki (yaani uhusiano kutokana na vitukuwa na asili moja). Ukilinganisha Kiingereza na Kichina kwa mfano, wakuta kwamba zinahusiana kutokana na kufanana kwa baadhi ya vitu, lakini hazina uhusiano wa kijenetiki kwani ni vizalia vya jamii tofauti kabisa za lugha. Profesa Obenga pia katika misingi hiyohiyo alikataa kabisa hoja ya kuwapo lugha iliyochanganyika.

Uhusiano wa Kijenetiki hutegemea uthibitisho wa kanuni za kifonetiki zinazopatikana kwa kulinganisha mofimu na fonimu za lugha zinazofanana. Kwa kuchunguza uwiano uliopo wa kimofolojia, kimsamiati na kifonetiki baina ya lugha moja na nyingine inawezekana kugundua inaumbo ya awali ya lugha hizo. Hizi ndivyo lugha yakinadharia ya “Indo-European” ilivyoundwa kidhahania na baadaye kutumiwa kama kifani cha rejea. Lugha kama hii ilikuwa kama kionyeshi cha muundo mpana wa utamaduni wa aina moja ambao maumbile yake yalirithiwa na lugha ambazo baadaye zilikuwa katika mikondo tofauti.

(b) Profesa Obenga alionyesha baadhi ya mifano ya kufanana kwa baadhi ya vitu katika sarufi: maneno ya jinsi yaliundwa kwa kutumia kiambishi B t, na wingi wa majina kwa kutumia kiambishitamati -w (*ou, u*). Halafu alichanganua maumbo ya

9 Makala kamili, kama ilivyotafsiriwa kwa Waandishi na Profesa Obenga, yameambatanishwa kama kiambatisho kwenye Ripoti Kamili ya kongamano.

10 I. Fodor, *The Problems in the Classification of the African* (Kituo cha Utafiti wa Afrika na Asia cha Akademia ya Sayansi ya Hungary Budapest, 1966) uk, 158

maneno yaliyo kamili na kuonyesha jinsi yale ya Kimisri cha kale yalivyofanana na yale katika baadhi kubwa ya lugha za Kiafrika. Maumbo ya maneno kama haya katika Kimisri yalifanana kabisa na yale ya Kiwolof. Vielelezo hivi vilimfanya Profesa Obenga afikie hitinuisho kwamba kufanana kwa maumbo, msamiati na Sarufi miundokti ya lugha hizi kulikuwa ushahidi wa kutosha wa uhusiano wa karibu sana kati ya Kimisri cha kale na lugha za leo za Waafrika weusi. Haiwezekani kupata uwiano kama huu kati ya lugha za Semitiki, Kiberiberi na Kimisri.

Baada ya hayo aliendelea kulinganisha namna ya kueleza “kuwa” katika miunganiko ya vitenzi na majina. Umbo la kale linalotokea sana katika lugha za Kibantu lilikuwa sawa na umbo la kale kabisa katika Kimisri cha kale. Uchambuzi wa mofimu za kanusho, msisitizo wa wakati ujao na viungishi, ulileta matokeo kama hayo aliyoyapata katika mifano iliyotangulia. Haya yote yalimfanya Profesa Obenga afikirie kwamba upo uwezekano wa kugundua muundo wa Kijenetiki wa namna moja kwa lugha hizi.

- (c) Mwisho Profesa Obenga alizunguiza kitu alichokifikiria kuwa ndicho kilikuwa cha kuvutia mno katika ulinganisho alioufanya. Alijaribu kuonyesha uwiano kati ya maumbo ya maneno yanayotokoa katika lugha mbalimbali na pia kati ya fonimu fulani ndogondogo. Mifano ya maumbo ya maneno ni kama kiganja cha mkono, mzimu, mti, mahali; na ile ya fonimu kama vile, KM (Kem) B “eusi” katika Kimisri cha kale. Neno hili huwa *kame*, *kemi*, *kem* katika Kikopti; ikama katika Kibantu (neni lenye inaana ya kugeuzwa mkaa na joto kubwa sana), *Kame* katika Kiazari (mkaa). Neno *Rome*, “inwanaume” katika Kimisri cha kale huwa *lomi* katika Kibantu. Katika mifano hii Fonimu zilezile hufanyakazi ileile katika lugha mbalimbali zinazolinganishwa.

Profesa Obenga alifikiri kwamba kwa sababu hizi ingeweze kana hapo baadaye kupambana lugha ya “Kinegro B Kimisri” inayofanana na lugha ya kinadharia ya “Indo-European” iliyotajwa juu. Katika muktadha huu, na kwa kuzingatia ukweli kwamba lugha zote hizi zina utamaduni wa asili moja, yawezekana kusema kwamba kuna msingi madhubuti wa kuendeleza uchunguzi kwa siku zijazo.

- (9) Profesa Gordon-Jaouet alitoa maoni kwamba uchunguzi toponimia ya Kimisri labda pia ungeweza kutumiwa kuunga mkono hoja kwamba hapakuwa na uhamiaji mkubwa nchini Misri au uvamizi wake na wageni walau tangu enzi za Neolithi. Ni jambo linalojulikana sana kwamba majina ya milima na mabonde hubaki kwa muda mrefu sana na kwamba kila kundi lifuatalo la watuma lugha liishilo katika sehemu hiyo huacha alama yake katika eneo hilo kwa njia ya majina wanayoita sehemu mbalimbali. Majina hayo huweza kuwa mengi au inachache kutegemea idadi ya watu hao na urefu wa muda wa kukaa kwao katika sehemu hiyo. Kama kundi lolote kubwa lingehamia kabisa nchini Misri lazima lingeacha majina yake ya sehemu humo nchini. Lakini mambo hayakuwa hivyo. Majina ya sehemu za nchi ya Misri yalibaki

bila mabadiliko kwa muda mretu sana. Majina karibu yote yaliyotumika yaliweza kuelezwa kwa kutafuta asili zao katika lugha ya Kimisri yenyewe. Majina ya Kiyunani na baadaye yale ya Kiarabu yaliyoanza tu kutumiwa kuita baadhi ya sehemu za Misri mnamo enzi za Ptolemi na baada ya uvamizi wa Waarabu. Majina ambayo asili zao zilikuwa katika lugha za kigeni yalipatikana katika mikoa ya pembeni tu kama vile Unubi, Maoasisi ya Magharibi na Delta ya Mashariki, mikoa ambayo ilipakana na majirani waliokuwa wakiongea lugha nyingine.

(10) Profesa Devisse alitacha kazi yake kama Mwandishi kwa nuuda kuljeleza kongamano kuhusu ¹²matokeo ambayo hayakutarajiwa ya uchunguzi wa Usawiri ¹¹

Miswada mitatu ¹² ilikuwa na maelezo ya Wamisri weusi ambazo zilistalili kuchunguzwa. Baada ya kuondoa picha ambazo ni dhahiri zilitokana na maelezo ya Biblia (kama vile masimulizi juu ya watoto wa Ham), na zile zilizokuwa za mafumbo yamakusudi kabisa katika msemu (kama vile Jehenam, Usiku), palibakia picha nyingi zilizoonyesha Wamisri wenye maumbile ya watu weusi. Ni kweli wengine kati yao walikuwa watumishi lakini kuhusiana na suala hili ziko baadhi ya picha zilizoonyesha matukio mazuri sana -, wengine walikuwa Wamisri huru. Baadhi yao — kama theluthi moja ya waliokuwa wakishiriki — waliituzuka meza ya Yusufu alipowaandalia nduguzake Waisraeli karamu. Hawa walikuwa wameketi kwenye meza nyingine. Wengine walishiriki wakati Yusufu alipokuwa alikiuzwa kwa Potifari ambaye alichorwa kama mtu meupe. Jambo linalovutia sana katika picha hizi ambazo zilirudia ukweli ulerule, lilikuwa ni mavazi mahsusii yaliyovaliwa na Wamisri weusi (hasa katika picha za karne ya kumi na moja ya vitabu vinane vya mwanzo vya Biblia). Watu weusi hawa waliotofautishwa waziwazi na Wamisri waliokuwa na ndevuna kuvaa vilemba, walitokea kila inara wakiwa wamebeba niukuki na wakiwa wamevaa “ngozi ya chui” iliyoiliacha bega la upande wa kulia wazi. Profesa Devisse alifikiri kwamba mambo yote haya yalikuwa ya maana sana kwa sababu palikuwa na uhusiano mkubwa sana kati ya Uturuki na Misri katika enzi na Wafatinidi na pia kwa kuwa picha za wakati huu na baadaye zilikuwa za kweli zaidi kuliko katika miswada ya zamani mno.

Ilikuwa vigunuu sana kutafsiri miswada hii kwa kuwa ilionyesha ntamaduni wa Kituruki na masimulizi ya kibiblia. Hata hivyo, miswada hii ilionyesha jinsi “mtu wa Kaskazini” alivyowaona Wamisri; mtazamo ambao unatofautiana na ule uliozingatiwa kwa kawaida na “watu weupe”.

¹¹ Utafiti mpana ya kimataifa utakuwa ndio mada ya chapisho la majuzuu matatu, ambayo mawili yari yamechapishwa. Utafiti huu umefanywa na Menil Foundation (Houston, Marekani), kituo ambacho huko Paris kimeratibu mkusanyo wa data nyingi.

¹² Paris, bibliotheque Nationale, New Acquisitions:

C. Majadiliano ya jumla

Majadiliano ya jumla yalidhihirisha kwamba baadhi ya washiriki walifikiri ni muhimu kufanya uchambuzi mpana ambao ungeihusisha historia ya Misri ya kale yote au hata bara lote la Afrika. Baadhi nyingine ya washiriki walifikiri kwamba lingalikuwa jambo la busara zaidi kuendeleza uchambuzi mdogomdogo kijiografia kwa nisingi ya taaluma moja au nyingi kwa pamoja.

(I) Uchambuzi wa matokeo ya uchunguzi kwa kufuata miaka

Profesa Cheikh Anta Diop alianzisha majadiliano kuhusu swala hili. Alisema kwamba kuanzia mwanzo wa kipindi cha Paleolithiki ule mfanano waliokuwa nao binadamu hapo awali ulianza kutoweka polepole. Wamisri kama watu wengine kote duniani nao walikumbwa na mabadiliko haya. Inaaminika leo hii kwamba binadamu wa kwanza alianza kuonekana barani Afrika mnamo miaka 5,300,000 kabla ya enzi zetu. Asili yake ilikuwa mumo humo barani.

Binadamu (=homo sapiens) walionekana kama miaka - 150,000 na kusambaa polepole katika sehemu nyingine za bonde la mto Nili zilizoweza kakalika. Watu waliokuwa wakiishi Misri enzi hizo walikuwa weusi.

Hali akikataa nadharia inayopingana na yake iliyorejewa na Profesa Vercoutter katika taarifa kuhusu kukaliwa kwa Misri na watu miaka kabla ya enzi za ufalme, Profesa Diop alisema kwamba ile asilimia 33 ya Wamisri "weupe" waliokuwa na rangi ya kahawia au hata nyeusi walikuwa kwa hakika weusi kaina walivyokuwa asilimia 33 ya machotara. Baada ya kujumlisha asilimia 33 ya mwisho iliyotajwa na Dakta Massoulard na ambao pia walikuwa watu weusi, Profesa Diop alitoa rai kwamba watu wa Misri kwa ujumla walikuwa weusi tokea kipindi cha mwanzo wa ufalme.

Aliendelea kusesitiza tena nadharia ya jumla aliyokuwa ameitoa hapo awali kuhusu watu weusi wa Misri ambao walibadilika kuwa mchanganyiko.

Baadaye tena katika majadiliano, Profesa Diop alisema waziwazi kwamba watu weusi wa Misri ya Juu walianza kurudi nyuma wakati nchi ilipovamiwa na kukaliwa na Wapersia.

Alimaliza kwa kutoa maomni mawili ya jumla; Oni la kwanza lilihusu matumizi ya neno "-a kinegro", ambalo alifikiri halikuwa la lazima na lilikuwa la dharau; onila pili lilihusu sababu zilizokuwa zikitumiwa kupinga mawazo yake na ambazo alisema zilikuwa za kupinga tu bila insingi na hazikuwa na udadisi wa kimsingi ulioimarishwa na ushahidi mzuri.

Mmoja wa washiriki aliikataa katakata nadharia ya Profesa Diop.

Hakuna mshiriki yeyote aliyeunga mkono waziwazi nadharia ya awali kuhusu watu "weupe" waliokuwa na rangi nyeusi kidogo au hata nyeusi sana. Palikuwa na kukubaliana kwa kimyakimya kulitupilia mbali wazo lili la zamani.

Mawazo mengi kati ya yale yaliyotolewa Profesa Diop yalipingwa. Upinzani huu ulionyesha hali ya kutokubaliana kimsingi kati ya washiriki, ingawa haikudhihirishwa waziwazi. Kuhusu maelezo fulani, upinzani ulitokea juu ya mambo ambayo hayakuhusiana na maelezo yaliyokuwa yanewasilishwa. Kuhusu enzi za kale kabisa yaani enzi kabla ya zile ambazo Wafaransa huendelea kuziita enzi za Neolithiki washiriki walikubaliana kwamba ilikuwa vigumu sana kupata majawabu yanayoridhisha.

Profesa Dedono alionyesha jinsi utamaduni wa kutumia mawe yasiyochongwa kama vifaa ulivyofanana sana pale pote ulipokuwa umegunduliwa (Kenya, Ethiopia, Uganda, Misri). Hali kama hii ilikuwa kweli pia kuhusiana na wakati wa Akeuli ambapo vifaa vyenye bapa pande zote mbili vilikuwa vinafanana sana katika sehemu mbalimbali za Afrika.

Kwa upande mwingine, umoja wa shughuli za viwanda za Sango zilizopatikana Afrika ya Mashariki ulipungua kadri mtu alivyoelekea kaskazimi zaidi. Huko Khor Abu Anga (Kisiwa cha Saihuko Sudan) kulikuwa na baadhi kubwa ya vyombo mbalimbali vilivyotokana na viwanda hivi. Kuanzia Wadi Halfa na kuendelea baadhi ya vyombo hivi vilianza kupotea. Huko Misri ni sehemu moja tu ya inaumbile ya viwanda hivi vya Sango ilibakia kati ya Thebes and Dahshur karibu na Kairo.

Katika kipindi cha kati cha enzi za Paleolithiki kupatikana kwa vyombo vidogovidogo vya mawe vijulikanavyo sana kwa jina la Levalleis pamoja na vile vya Musteri kulitofautiana sana kati ya Misri na sehemu zilizokuwa kusini zaidi au magharibi.

Katika enzi za Paleolithiki Misri ilitengwa na sehemuningine za afrika kuhusiana shughuli za utengenezaji wa vifaa vya mawe. Mambo yaliyosababisha hali hii hayajulikani sawasawa lakini yawezekana hali hii ililetwa na mabadiliko ya hali ya hewa na mazingira. Katika kipindi hiki cha kutengwa Misri ilijianzishia viwanda vyake yenyewe.

Zaidi ya hayo, wakati huohuo wageni waitwao Waateri walijaribu kujiingiza nchini kutoka kaskazini mashariki ya Afrika. Alama zao ziliweza kuonekana hata kusini mwa jangwa la Sahara. Baada ya kuifikia oasisi ya Siwan na pia, oasisi ya Kharg, kwa wingi sana, walisambaa katika bonde la mto Nili na alama zao zimeonekana Thebes. Ushahidi mwingine wa kipindi hichohicho ulipatikana Wadi Hamamat (Jangwa la Mashariki), Esna (ukichanganyika na mabaki ya Kharg), Dara, Jebel karibu na Kairo, na hata Wadi Tumilat katika sehemu ya Mashariki ya Delta yamto Nili (hapa umechanganyika na mabaki ya Epi-Levalle). Yawezekana wakati huohuo palitokea mchanganyiko kidogo wa watu wa mataifa uengine ambao walimezwa haraka haraka na wenyeji wakazi.

Uvamizi mwingine wa wageni katika Misri unaofaa kuangaliwa ulikuwa wa Wanatufi kutoka Palestina ambao, ilijulikana tangu zamani sana kwamba waliwahi kukaa Halwan karibu na Kairo. Machimbo ya hivi karibuni yameonyesha kwamba watu hawa walikaa katika sehemu kubwa zaidi. Vifaa vya mawe vinavyofikiriwa

kuwa vilikuwa vya hawa Wanatufi, viligunduliwa Fayum na katika Jangwa la Mashariki kwenye ukanda wa kutoka mashariki kwenda magharibi unaokatisha bonde la Mto Nili katika sehemu hii.

Profesa Sauneron alifikiri kwamba inawezekana kwa vifaa vya mawe vilivyochongwa katika tabaka ya Pleistosini kongwe kwenyemachimbo ya vilima vya Thebes.

Profesa Ghallab alisema kwamba wakazi wa Misri katika enzi za Paleolithiki walikuwa weupe (caucasoidj). Aliendelea kueleza kwamba machimbo ya hivi karibuni yalitoa ushahidi wa kuwepo kwa watu wa aina ya "San" kati ya watu walioishi Misri enzi za kabla ya mwanzo wa ufalme.

Profesa Shinnie alikubaliana na yale yaliyokuwa yanieseniwa kuhusu makazi ya homo sapiens (binadamu), lakini hakusema walikuwa na rangi gani ya ngozi. Alifikiri kwamba waliingia katika bonde la mto Nili kama miaka 20,000 iliyopita. Baada yahapo vikundi mbalimbali vya watu vilifika kutoka sehemu mbalimbali vikaongeza hesabu ya watu hawa na kubadilisha hali ya jamii zilizoishi humo.

Majadiliano yalizidi kupamba moto kuhusiana na enzi za Neolithiki na enzi kabla ya mwanzo wa ufalme. Profesa Abu Bakr alisisitiza kwamba Wamisri kamwe hawakupata kutengwa na watu wengine. Walikuwa hawajaunda kabila safi la Kiniisri na ilikuwa haiwezekani kulikubali wazo kwamba katika enzi hizi watu wote wa Misri walikuwa weusi. Watu wa Misri katika enzi hizi za Neolithiki walikuwa ni mchanganyiko wa watu kutoka magharibi na mashariki ambao walikuwa wameitwa Wahamitiki kwa miakosa.

Hii ilikuwa pia ndiyo nadharia ya Profesa El Nadury. Katika enzi za Neolithiki wahamiaji kutoka sehemu zote za Sahara walikuwa wamewaingilia watu waliokuwa wakirishi sehemu za Kaskazini magharibi ya Delta. Matokeo yake yalikuwa ni mchanganyiko wa makabila mengi. Kutoka wakati kuhusu makazi ya watu nipaka enzi za ufalme. Sehemu ya uchunguzi ya Merimde ambayo ina vitu vingi sana vya kiakiolojia vilivyopangika kwa matabaka ilionyesha kwamba watu walifika na kukaa katika sehemu hizo polepole sana.

Profesa Vercoutter alitoa maoni yake kwa dhati kuhusu kukaliwa kwa Misri katika siku za kale. Alisema kwamba watu wa bonde la mto Nili walikuwa wamechanganyika siku zote. Wageni kutoka magharibi na mashariki walikuwa wengi sana hasa kabla ya enzi za ufalme.

Katika miaka kabla ya enzi za ufalme na wakati wa enzi za ufalme watu zaidi kutoka kaskazini mashariki waliosemekana kuwa Wasemitiki waliongezeka na kuwa sehemu ya watu wa Misri. Profesa El Nadury kama Profesa Abu Bakr alifikiri ni ukweli unaovutia kwamba katika ufalme wa kwanza ngone zilijengwa Abidos ambazo huenda zilikuwa kwa ajili yakuzuia uhamiaji kutoka kusini kuelekea kaskazini.

Profesa Abu Bakr alidokezea tena swala la mke wa Cheops aliyekuwa na nywele za njano na macho ya buluu kama mfano wa kuwepo Misri kwa watu ambao

“hawakuwa weusi.” Profesa Diop alifikiri kwamba mfano huu wa pekee ulikuwa tofauti na hautoshelezi kutangua ukweli wenyewe.

Katika majadiliano Profesa Obenga aliongezea mambo muhimu kadhaa na kusesitiza suala la maslahi ya vyanzo vya maandishi ya kale kuhusu watu wa Misri. Katika maelezo kuhusu Wakolchoi ambalo halijapingwa na utaalamu wa siku hizi wala kuonyesha kwamba haufai kwa uchambuzi linganishi wa maandishi uliofanywa na uliokuwa makimi, Herodotus alijitahidi kuonyesha kwamba Wakolchoi walifanana na Wamisri. Ilikufanya hivi alitumia hoja nyingi zilizokuwa zimetilia maanani mambo mengi. Aliandika: “Wanaongea kama Wamisri wanavyoongea; wao na Wamisri ndio watu pekee wanaotahiri; wanafuma nguo za kitani kama Wamisri.” Kufanana huku kulikuwa ni ziada ya mambo mengine mawili ambayo walikuwa nayo wote, yaani rangi yao nyeusi na nywele zao za kipilipili.

Profesa Leclant aliendelea kushikilia kwamba waandishi wa kale walitumia msemu “nyuso zilizoungua” (Waethiopia) kuwaita Wanubi na watu weusi na siyo Wamisri. Profesa Obenga alijibu akisema kwamba Wayunani walitumia neno “Eusi” (melas) walipokuwa na maana ya Wamisri. Profesa Vercoutter aliuliza ni katika hali gani hasa ambapo Herodotus alisema Wamisri weusi. Profesa Diop akijibu alisema kwamba Herodotus aliwaita weusi mara tatu: alipokuwa akiongelea juu ya asili ya Wakolchoi, alipokuwa akiongea juu yakiini cha mafuriko ya mto Nili, na alipokuwa akieleza mambo kuhusu ubashiri wa Zeus-Amon.

Rai ya Profesa Leclant ilikuwa kwamba umoja wa watu wa Misri haukuwa katika rangi ya ngozi na maumbo yao, bali katika utamaduni wao. Ustaarabu wa Kimisri ulidumu bila kuyumba kwa miaka elfu tatu. Wamisri walijiita REMET (*Rome* katika Kikopti) na kutokana na ushahidi wa usawiri walionyesha tofauti kati yao na watu wa kaskazini na kusini ambao walikuwa hawafanani nao. Profesa Obenga alilipinga wazo lililosema kwamba Wamisri walipotumia neno REMET walitaka kuonyesha tofauti kati yao na jirani zao. Alifikiri kwamba tofauti ilikuwa sawa na ile iliyowafanya Wayunani wajitofautishe na watu wengine ambao waliwaita washenzi.

Profesa Leclant alisema kwamba ilifaa kuchunguza sehemu muhimu za sura za kale sana za Kiafrika katika maisha ya kiutamaduni ya Wamisri. Alitoa mfano wa nyani aliyetuniwa kuwakilisha mungu Thoth na ngozi ya “chui” ambayo kutokea kwake mara nyingi sana katika usawiri ulionyesha ni vazi la ibada lililotumiwa na Harus wakati wa kumwabudu Osiris. Lakini alifikiri kwamba Wamisri ambao utamaduni wao ulidumu imara kwa miaka elfu tatu hawakuwa weupe wala weusi.

Profesa Sauneron alianza kusaili hilo wazo lenyewe la kuwapo kwa watu wa aina moja hasa kutokana na dai kwamba watu wa namna hii waliishi Misri tokea binadamu alipoanza kuonekana humo hadi katika kipindi mpaka sikukabla ya enzi kabla ya ufalme. Alifikiri kwamba kati ya sababu zote zilizotolewa hapana hata moja iliyoweza kuitilia shaka hoja kwamba watu wa Misri walikuwa watu mchanganyiko.

Mawazo ya mwisho ya wataalamu ambao hawakukubaliana na nadharia hii iliyotolewa na Maprofesa Cheikh Anta Diop na Obenga kwamba bonde la mto Nili

lilikuwa na watu wa aina moja tangu zamani sana mpaka wakati wa asili ya Wamisri walihamia huko katika nyakati za Neolithiki na kwamba wengi wao walitokea Sahara na kwamba kati yao wengine walitoka kaskazini na wengine kusini mwa Sahara wakiwa wanatofautiana katika rangi. Wakipinga nadharia hii Maprofesa Diop na Obenga walipendekeza wazo lao kwamba bonde lilikaliwa na watu weusi tu na kwamba walijiingiza bondeni toka kusini kuelekea kaskazini.

(2) *Kuwepo aukutokuwepo kwa uhamaji mkubwa kuelekea bonde la Mto Nili*

Kuhusu kichwa cha habari hapo juu, majadiliano katika kongamano yalibakia kuwa yenye mikanganyiko mingi. Mengi kati ya maoni yaliyotolewa hayakutoa mahitimisho ya kuridhisha.

Kwa jumla washiriki walifikiri kwamba nadharia ya “uhuanaji wa watu wengi sana pamoja” haikufaa tena kutumiwa kama maelezo ya kukaliwa kwa bonde la mto Nili angalau mpaka kipindi cha Hiksos, wakati inabadilishano ya kiisimu (lugha) kati yasehemu hii na nchi za Mashariki ya karibu yalipoanza (Holthoer). Kwa upande mwingine, wataalamu kadhaa walifikiri kwamba uhamaji wa watu kuelekea pande zote ulifanyika tu kati ya sehemuhii na sehemu zilizopakana nayo. Lakini mawazo yaliyotofautiana kabisa yalitolewa kuhusu dhima ya maumbile ya kijiografia na sababu za kiekolojia kama vikwazo vyaasili au vya makusudi katika kuzuia uhamaji wa namna hii wa watu.

Baada ya kuangalia nambo yote kwa makini ilikubaliwa kwa jumla kwamba Misri ilikuwa imepokea wahamiaji hawa kutoka makabila mbalimbali. Kwa hiyo washiriki wa kongamano kwa kiasi fulani walikubali kwamba msingi wa watu wa bonde la mto Nili ulibaki iwara na uliathiriwa kidogo tu na uhamaji kwa miaka elfu tatu.

Lakini vipindi vya baadaye vilipochunguzwa ilidhiliirika kwamba hapakuwa na uwzekano wa kufikia makubaliano mapana ya kinadharia.

Kuhusu enzi za Paleolithiki, Profesa Cheikh Anta Diop alipendekeza dhana isemayo kwamba binadamu walilikalia bonde la mto Nili polepole mpaka usawa wa latitudo ipitayo Memphis. Profesa Abu Bakr alisema kwamba kulikuwa na habari kidogo mno kuhusu kipindi hiki na kwamba huenda sehemu ya kaskazini ya bonde la mto Nili haikukaliwa kabisa. Profesa Obenga kwa upande wake alifikiri kwamba kati ya enzi za Paleolithiki na zile za Neolithiki watu wa aina moja walikuwa wakiikalia nchi hii. Wamisri wenyewe walikuwa wametilia mkazo jambo hilikatika hadithi zao na katika fasihi simulizi zao. Waliseua kwamba maziwa makubwa yalikuwa ndiyo nchi yao ya asili na Nubia ilikuwa nchi iliyofanana na nchi yao ya asili.

Inawezekana kwamba makundi makubwa ya watu yaliingia bonde la mto Nili kutoka Sahara kipindi cha Melithiki kilipoingiliana na kile cha Neolithiki (Profesa Vercoutter) au katika kipindi cha Neolithi (Maprofesa Habachi na Ghallab). Profesa Vercoutter alieleza matumaini yake kwamba kuhama huku kwa watu, ambako ni mambo machache tu yanajulikana juu yake mpaka sasa, kungeweza kupata tarehe kamili na kwamba mabaki ya kale yanayohitajika yangekusanywa na kuchunguzwa.

Profesa Cheikh Anta Diop alitoa maelezo zaidi kujibu mawazo hayo hapo juu: Utambuaji wa tarehe kwamba kutumia ufundi wa radio-kaboni ulionyesha kwamba katika sehemu yamagharibi ya Sahara hali ya hewa ya unyevunyevu ilidumu kati ya 30,000 na 8,000 kabla ya enzi zetu. Hali hii iliingiliwa na vipindi vya mara kwa mara vya ukame. Tarehe za vipindi vya ukame vilivyotokea navyo vimeanza kufahamika viizuri zaidi kwa kutumia njia hiyohiyo. Tarehe kama hizo ziuapaswa kupatikana pia kuhusu Sahara ya Mashariki. Mambo aliyotaka kupata Profesa Vercoutter yangalipatikana kwa kuweka pamoja matokeo ya utafiti wa hali ya hewa ya enzi za kale sana na uchunguzi wa makaburi na michoro.

Profesa Habachi aliunga mkono bila kusita hata kidogo wazo kwamba uhamiaji ulitoka sehemu za Sahara kutokana na misingi ya uchunguzi unaojulikana. Profesa Save-Soderbergh alifikiri kwamba mengi kati ya tamaduni za enzi za Neolithiki katika bonde la mto Nili zilikuwa sehemuchangamano ya kiufundi ya tamaduni za Sahara na Sudani. Hata hivyo misafara ya uhamaji huenda ilikuwa mingi hasa kabla ya na mwishoni mwa kipindi cha mvua kidogo cha enzi za neolithi.

Kama kibadala cha nadharia-tete juu ya uhamiaji kutoka Sahara siku za neolithiki. Profesa Diop alitoa nadharia-tete kwamba watu walisambaa kutoka kusini kuelekea kaskazini. Alizungumzia tena wazo lililokuwa limerejelewa mara nyingi wakati wa majadiliano kwamba katika kipindi cha Kaspiani utamaduni huu ulikuwa umeenea vipana mno kntokea Kenya hadi Palestina.

Kuhusu vipindi vya mwanzo wa enzi za ufalme na vile kabla ya ufalme, Maprofesa Diop na Vercoutter walikubaliana kwamba watu wa eneo la Misri katika bonde la mto Nili walikuwa wa aina moja mpaka kufikia sehemu ya kusini kabisa ya Delta. Wataalamu hawa wawili walikubaliana kidogo tu kuhusu nadharia-tete kwamba watu walihama kutoka kaskazini kuelekea kusini. Profesa Vercoutter aliona ugumu kukubali nadharia-tete hii hali Profesa Diop aliukataa kabisa. Wataalamu hawa pia hawakukubaliana juu ya jinsi ya kufafanua maumbile ya hawa watu kikamilifu. Profesa Diop alisema kwamba walikuwa Wa-Anu na aliwapambanua katika picha katika Hekalu la Abidos aliyोजना Petrie.

Wakati wa enzi za ufalme, uimara wa watu wa eneo la Misri la bonde la mto Nili ulijidhihirisha katika uimara wa utamaduni wao. Profesa Diop alionyesha kwamba kalenda ya Kimisri ilikuwa imeanza kutumika mapema sana mnamo mwaka - 4236 na tangu mwanzo ilikuwa na mwenendo wa kurudiarudia wa miaka - 1461. Alisema kwamba hadi wakati wa uvamizi wa Waajemi uimara huu ulipata kuathiriwa tu na mtetemeko mkubwa wa ardhi uliotokea mwaka -1450. Tukio hili lilisababisha uhanaji wa makundi mengi ya watu ulioathiri hali ya utulivu ya nchi zote zilizokuwa kandokando ya Bahari ya Mediterania kwa upande wa mashariki. Makundi ya mabaharia yaliishambulia Delta ya Misri wakati Wahittiti walipokuwa wakipotea na walipoanza kuonekana huko Afrika ya Kaskazini Waberiberi wa mwanzo. Mbali na msukosuko huu mkubwa, tukio jingine muhimu katika maisha ya Wamisri hata kama halikuhusika na uhamaji wa aina yoyote ilikuwa ni kutekwa kwa Misri kutoka kusini

kuelekea kaskazini kulikofanywa na Farao Narmer aliyeiunganisha Misri mnamo mwaka -3300.

Hapakuwa na majadiliano kuhusu uchanganuzi huu lakini changanuzi za aina nyingine zilitolewa: Profesa Save-Soderbergh akitumia ushahidi wa machimbo ya Unubi alijaribu kuthibitisha vipindi na hali ambapo Misri ya Mafarao ilitengwa na sehemu za kusini. Huko Unubi, utamaduni wa kale kabisa ulikwisha polepole mwishoni mwala ufalme wa kwanza au labda niwanzoni mwa ufalme wa pili. Kundi C lililoufuatia halikujitokeza kabla ya ufalme wa sita. Hii ina maana kwanba palikuwa na “pengo katika mfululizo wa wakati” la miaka kama 500 hivi kati ya miaka -2800 na -2300. Hakuna habari zozote siku hizi kuhusu kipindi hiki. Ilikuwa wazi kwamba kwa sababu ya hali hii uhusiano mzuri kati ya Misri ya Mafarao na maeneo ya Kusini uliharibika au ulikoma. Kulikuwa na hali nyingine ya namna hii: hakuna mabaki yoyote ya kiakiolojia ambayo ni ya kipindi kati ya mwaka -1000 na mwanzo wa enzi za Ukristo yanayopatikana Unubi ya Chini. Mabaki ya Kimeroe yaliyogunduliwa na ya karne ya kwanza ya enzi zetu. Hii yaonyesha mabadilishano kati ya Misri na Kusini mwake yalitofautiana sana kati ya mwaka -2800 na kipindi cha Kimeroe.

Maprofesa Vercoutter na Laclant walionyesha kutokea kwa aina za picha za watu weusi ambazo zilikuwa tofauti kabisa na zile zilizokuwepo hapo awali kuanza ufalme wa kumi na nane na kuendelea. Mifano ya hizi picha ni zile zionekano katika kaburi la Houy au kaburi la Rekhmire. Je watu hawa wavya walianzaje kutokea katika usawiri wa Misri? Je yalikuwa matokeo ya uhusiano kati ya Misri na maeneo ya kusini au yalitokea kwa sababu ya uhamiaji wa watu wa zaidi kuelekea kaskazini kuingia Unubi? Profesa Shinnie alisema kwamba taarifa hizi hazikuwa sababu za kutosha kusema kwamba palikuwa na uhamiaji kutoka kusini uliowaathiri watu wa Misri.

Profesa Leclant alifikiri kwamba ukiachwa kando mfano wa ufalme wa kumi na nane uliokwishatajwa hapo juu hakuna mabadiliko muhimu yaliyotokea kabla ya ufalme wa ishirini na tano wakati watu wa Kush kutoka Dongola walipoanza kuonekana Misri. Alielekea kufikiri kwamba kuonekana huku kwa watu wa Kush Misri kulitokana na kuongezeka kwa athari ya maisha ya Wamisri na si Okutokana na sababu za uhamiaji wa watu. Mambo mawili yalijitokeza wazi sana wakati wa majadiliano nayo hayakuzua mabishano makali:

- (a) Kulikuwa na matatizo mawili yaliyokuwa hayajatatuliwa kuhusu Delta ya Nili¹³ katika enzi kabla ya historia.

Kwanza sehemu hii inajulikana kidogo sana ikilinganishwa na Misri ya juu

13

Profesa Holthoer drew alielezea kazi ifuatayo: D.G. Réder, 'The economic development of Lower Egypt (Delta) during the archaic period (V-IV Centuries) before our era' mkusanyiko wa makala yaliyotolewa kwenye *Journal of Ancient Egypt*, 1960 (tafsiri ya jina la mada lililoandikwa Kirusi).

kama alivyosema Profesa Debono. Sababu yake ni kwamba uchunguzi unaoendelea kwa kuchimba sehemu za Merinde, El Omari na Meadi-Heliopolis haujakamilika. Mabaki ya binadamu yaliyogunduliwa mpaka sasa ambayo ni ya enzi kabla ya historia na pia ya kipindi cha kale zaidi na tofauti na yale yaliyopatikana Misri ya Juu.

Pili, ni dhahiri kwamba matendo ya binadamu yaliyoathiri maisaha katika sehemu za Misri ya chini au katika Delta, ikiwa yanaweza kuonekana ya kipindi kabla ya enzi za ufalme, ni tofauti na yale yaliyohusika kwenye bonde kusini mwa eneo hili.

- (b) Uchunguzi wa watu wa kale katika sehemu ya kaskazini ya Unubi umewezekana kutokana na utafiti thabiti wa kiakiolojia uliodhaminiwa na UNESCO kwa sababu nyingi zinazotafautiana uchunguzi wa namna hii haujawezekana katika sehemu zilizobaki za bonde la mto Nili lililopo nchini Misri ambako matokeo ya uchunguzi kuhusu nyakati kabla ya enzi za ufalme na utamaduni wa kuonekana wa kale yalikuwa machache sana kulinganisha na Unubi ya Kaskazini. Yawezekana ukweli huundio umefanya baadhi ya wataalamu wasite au kukataa kufikia mahitimisho kamili.

Hapana shaka kwamba kuna jambo jingine lilizidisha utatanishi katika majadiliano ambayo yalijitokeza kama hotuba zilizofuatana na zenye mambo yaliyopingana. Jambo hili lilijitokeza waziwazi, kutokana na tamshi la Profesa Obenga ingawa halikujadiliwa. Profesa Obenga anafikiri watu wenye utamaduni mmoja ni lazima wawe wa kabila moja. Hata kama mawazo haya mawili yanaweza kutazamwa pamoja au la, ni dhahiri kwamba hayakutengwa kiasi cha kutosha wakati wa majadiliano na matokeo yake, mahitimisho yaliyotokana nayo hayakuweza kuwa dhahiri zaidi kama yaliyopaswa kuwa. Uwezekano wa kutafuta misingi ya makubaliano juu ya masuala haya uliathiriwa na kutofanywa kwa mambo hayo.

Yawezekana watu wa bonde la mto Nili lililoko nchini Misri waliathiriwa sana na uhamiaji mkubwa wakati wa Neolithiki. Ziko nadharia mbili siku hizi huhusiana na suala hili: ya kwanza inasema kwamba wahamiaji walikuja kutoka kaskazini kuelekea kusini wakitoka sehemu yote ya Sahara ya Mashariki.

Nadharia ya pili inasema kwamba watu hawa walihama kutoka kusini kufuata bonde la mto Nili. Na kuanzia nyakati za mwanzo wa ufalme na kuendelea wakazi wa Misri walibakia imara sana.

Hali ya wakazi haikubadilishwa sana na kuhamahama kwa watu mbalimbali kulikoathiri hali ya Misri kisiyasa na kijeshi, wala matokeo ya uhusiano wa kibiasara wa Misri, au na jitihada za Wamisri kupanua sehemu ya ardhi waliyokuwa wakilima pia na kuingiliwa na watu kutoka maeneo waliyopakana nayo. Hali hii ya kutokuwa na msukosuko wa makabila iliambatana na utamaduni uliokuwa imara kabisa.

Lakini wakati wa majadiliano kuhusu wazo lililopendelewa na Profesa Diop kwamba watu wa Misri walikuwa wa aina moja na lile lililoungwa mkono na

wataalamu wengine wachache kwamba wakazi walikuwa na asili mbalimbali, ilikuwa wazi kwamba hapakuwa na hata chembe ya makubaliano.

(3) Matokeo ya Uchunguzi wa Anthropolojia Maumbo

Ilikuwa wazi hapa na pale katika majadiliano kwamba istilahi zilizokuwa zimetunika mpaka sasa kueleza tofauti ya rangi na ukabila wa watu zilihitiwa kufafanuliwa vizuri zaidi.

Bw. Glélé, aliyekuwa mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO aliingilia kati kuwahakikishia wataalamu waliotaka maneno "negro", "-eusi" au "-a aina ya Kinegro" yafutwe kwa sababu maneno hayo sasa yakuwa ya zamani mno na yenye kuambatana na dharau na hivyo kucheza ubaguzi baina ya wakazi mbalimbali wa bara hili.

Glélé aliwakumbusha washiriki katika majadala kwamba shirika la UNESCO lilikuwa limejizatiti kuleta uelewano baina ya mataifa na ushirikiano katika uwanja wa utamaduni. Aliendelea kusema kwamba haikuwa nia ya UNESCO, ilipoamua kugharimia kongamano hili, kuleta kutoelewana kati ya watu au mataifa, bali kwa kadri hali ya maumbo ilivyo sasa, nia ilikuwa kueleza na kutoa mwanga zaidi kuhusu suala moja kati ya mengi ambayo bado yalikuwa hayajatatuliwa; yaani la kukaliwa kwa Misri ya kale. Madhumuni ya kongamano hilo yalikuwa kutoa fursa ya kulinganisha nadharia mbalimbali, kupima uzito wa hoja za kisayansi zinazotolewa kuzieleza nadharia hizo na kupima hali ilivyo ili kuziba mapengo pale panapotakikana. Alisisitiza kwamba maneno negro, -a kinegro, -cusi, yalikuwa yakitumika mpaka sasa na kwamba yaliweza kuonekana katika vitabu vyote vya kisayansi yalivyo maneno kama Hamitiki au Chamitiki ingawa nayo matumizi yake yalikuwa yametiliwa mashaka katika majadala kwenye kongamano. Aliendelea kusema pia kuwa waandishi wa *Historia ya Afrika* wangetumia maneno ambayo wasomaji walikuwa wamekwishakuyazoea. Kwa vyovyote vile ilibakia kweli; kwamba maneno haya kama yalivyotumika katika vitabu vya kitaalamu au vya kawaida yalikuwa na maana fulani na hayangeweza kutengwa na mitazamo ya namna fulani ya thamani zake yaliyo dhahiri au vinginevyo. Alitoa maelezo zaidi kuhusu usemi wa mtaalamu mmoja kuhusu vitabu vya UNESCO juu ya matatizo ya tofauti ya rangi na ukabila tofauti ya rangi. Shirika hili lilikuwa limeandaa mpango maalumu wa kuchunguza uhusiano kati ya mataifa tofauti na lilikuwa limeongeza harakati za kupambana na matatizo ya ubaguzi wa rangi na wa kikabila. Vitabu kadhaa vilikuwa vimekishachapishwa juu ya suala hili muhimu. Kwa hiyo haiwezekani kwa kongamano hili katika kuchunguza jinsi Misri ilivyokaliwa na watu kukataa moja kwa moja na bila kupendekeza njia nyingine, mtaratibu unaokubalika unaotumiwa kuwaainisha watu katika makundi ya weupe, wa kimanjano na weusi; na ambao ulitumiwa pia na wataalamu wa Elimu ya Misri ya kale huwaainisha watu wa nchi hiyo. Zaidi ya hayo ikiwa kuna haja ya kubadilisha msamiati unaotumiwa sasa hivi na wanahistoria basi mabadiliko hayo yalikuwa historia ya dunia nzima na si ile ya Afrika

tu. Ikiwa itafikiriwa katika kongamano kuwa suala hili ni muhimu basi ingefaa lipelekwe kwenye kikao cha chama wanahistoria ili kijadiliwe katika kiwango cha kimataifa. Wakati tukizingojea hizo istilahi mpya maneno kama - eusi, negro, - kinegro, na Hamitiki yanayotumika siku hizi ingefaa yafafanuliwe kwa wazi zaidi.

Majadiliano kulusu jambo hili yalifunguliwa na Profesa Vercouter. Alikunibusha kwamba suala hili lilianza kuzungumzwa katika kitabu cha Junker alipotumia neno "Negro" kueleza picha zilizochorwa katika ufalme wa na nane. Baada ya hapo Wamisri walizichora picha hizo kama vichekesho. Junker alilitumia neno "negro" kuhusiana na watu wa Afrika magharibi akiwa anatilia maanani hasa hali ya rangi yao ya ngozi na maumbile fulani ya nyuzo zao.

Profesa Vercouter alielekea kufikiri kwamba badala ya maoni haya ya zamani kulikuwa na hapa ya kupata vigezo maalumu vya kutumiwa kuwaeleza watu weusi kisayansi. Alitaja hasa damu kutumwa kama kigezo suala la umuhimu maalumu wa kiwango cha rangi ya niwili, na kuuliza ikiwa, kwa mfano Wanubi nao wangeweza kuitwa watu weusi?

Fikra mbalimbali zilizuka kulusiana na maswali haya. Washiriki kadhaa walitoa matumaini yao kwamba neno "taifa" lilitambuliwa kama safi na uchunguzi wa Kisayansi na kwamba uchunguzi wa watu na rangi mbalimbali haukuwa na maana ya ubaguzi wa rangi.

Majadiliano yalionyesha matatizo ya kuyapa maneno yaliyokuwa yakijadiliwa maana za kisayansi. Ilionekana pia kwauba baadhi ya Wataalamu walikuwa hawapendi kuyatumia maneno hayo kwa sababu zilizokuwa nzuri kabisa kwa kuwa yalionekana kuwa na fasiri zenye hatari au inatusi. Aidha baadhi ya wataalam walionyesha kwaamba majibu ya msingi ya maswali haya hayawezi kutegemewa kutoka kwa wanahistoria na wataalamu wa akiolojia bali kutoka kwa wataalamu wa anthropolojia maumbo tu.

Profesa Save-Soderbergh aliungwa mkono na washiriki wengi ambao walitoa matumaini yao kwamba istilahi zinazohusu inasuala ya taifa zingechunguzwa na wataalamu wa sasa wa anthropolojia maumbo. Maana dhahiri za kisayansi zingefaa si kwa Afrika tu bali pia kuhusu Asia. Vivyo hivyo iikuwa muhimu kutoa fafanuzi za wazi zaidi kuhusu inawazo juu ya watu waliochanganyika, watu walioungana, na vikundi mbalimbali vya watu. UNESCO tayari ilikuwa imekwishawasilishiwa ombi la namia hii kuhusiana na uchunguzi unaofanyika huko Unubi.

Bw. Glélé' alisema kwamba ikiwa vigezo vilivyokuwa vikitumiwa kuwaainisha watu kwa rangi zao vilikuwa haviridhishi na ikiwa dhau zilizokuwa zimejadiliwa zilikuwa zimeclezwa ovyoovyo bila kuzingatia kweli maalum au bila kulingana na fikra za kawaida, hii ingefaa ilezwe hivyo na marekebisha yaanze kufanywa kwa istilahi zote za historia duniani kulingana na vigezo vipya vya kusayansi. Hii ingeweza kufanya msamiati kuwa wa namna moja na maneno kueleweka kwa maana moja ili kuepnkua na upotovu wa fikra na kuleta uelewano na makubaliano.

Lakini Maprofesa Diop na Obenga yaonekana wakishauriwa vibaya waliporejelea

vigezo kadhaa vilivyokuwa vikitumiwa na wanaanthropolojia kuwapambanua watu weusi. Vigezo hivi vilikuwa ni ngozi nyeusi, uso wenye taya zilizotokeza mbele, nywele za kusokotana, pua pana na muundo wa mifupa wa kinegro. Kulingana na maoni ya Montel watu weusi walikuwa na uso mpana "uliosimama wima." Profesa Abu Bakr alisema kwamba ikiwa watu weusi walikuwa na maumbile kama haya basi Wamisri wasingefikiriwa kuwa watu weusi. Profesa Diop alieleza kwamba vipimo vya mafuvu vilikuwa havijatumika hata siku moja kama msingi wa kitakwimu wa kupambanua ukubwa wa aina fulani wa ubongo kuwa wa watu wa taifa fulani.

Alifikiri kwamba kulikuwa watu weusi wa aina mbili. Aina ya kwanza ilikuwa ya wale wenye nywele laini na ya pili wenye nywele zilizosokotana. Na kama rangi ya ngozi ilikuwa nyeusi basi alama nyingine muhimu ambazo alikuwa ameziorodhesha hapo awali zisingekosekana. Mwisho alisema kwamba wakati aina ya danu A2 ilipatikana zaidi kwa atu weupe, watu weusi walielekea kuwa na damu ya aina B au wachache zaidi walikuwa na Aina C.

Profesa Shinnie alijibu akisema kwamba wataalamu wa Kimarekani aliokuwa amewaomba ushauri wakati akijiandaa kwa ajili ya kongamano walisema kwamba uchunguzi wa mafuvu ulikuwa na uuhimu lakini mafuvu yenyewe yasingetumwa kama msingi wa kuukilia taifa. Aliongeza kusema kwamba vigezo ambavyo Profesa Diop alifikiri vinatosheleza, vilikuwa havifikiriwi hivyo na wataalamu wa Kimarekani.

Profesa Obenga naye alifikiri kuwa kulikuwa na makundi mawili katika taifa moja la watu weusi: wenye nywele laini na waliona nywele zilizosokotana. Profesa Obenga aligeukia swali la jumla lililokuwa likiikabili kongamano. Nalo lilikuwa kwamba ikiwa wazo la taifa linakubalika kuwa la msingi ikiwa wazo la taifa la watu weusi nalo halikukataliwa basi ni maoni gani yatolewe juu ya uhusiano kati ya watu hawa na Wamisri wa kale?

Profesa Diop alifikiri kwamba matokeo ya uchunguzi wa kiantropolojia tayari yalikuwa yamektoa msingi madhubuti unaoweza kutumiwa kufikia mahitimisho. Yajulikana kwa mfano kwamba watu weusi wa Kigrimaldi walitokea mnamo mwaka -32,000, watu wa Kro-Magnoni ambao ndio mababu wa watu weupe walitokea mnamo mwaka -20,000, na watu wa Chankelada ambao ni mababu wa watu wa kimanjano walitokea katika kipindi cha Magdalena mwaka -15,000. Watu wa aina ya Kisemitiki walikuwa wa aina ya jamii ya watu walioishi katika mazingira ya mjini na walikuwa ni matokeo ya kuona baina ya watu weusi na watu weupe.

Kwa hiyo Profesa Diop hakuwa na shaka lolote aliposema kwamba wakazi wa kwanza wa bonde la mto Nili walikuwa weusi kama alivyofanuliwa katika matokeo ya uchunguzi uliofanywa na wataalamu wa anthropolojia na wa kipindi kabla ya historia. Profesa Diop aliamini kwamba mambo yaliyofanya ukweli huu usikubaliwe yalikuwa ni hisi za ndani za watu binafsi na jinsi walivyoeelimishwa.

Kwa kuwa fikra inayoongoza katika utafiti unaofanyika huko Unubi inapendelea komi kwamba sehemu hizi zilikalikiwa na watu kutoka sehemu mbalimbali, matokeo ya

utafiti hayakuwa ya manufaa katika majadiliano yaliyokuwa yakifanyika. Profesa Diop hakupendelea kuundwa kwa tume ya kuthibitisha mambo yaliyokuwa wazi kabisa, mambo ambayo kwa sasa yalihatiji tu kukubaliwa rasmi. alifikiri kwamba mambo yote yanayojulikana kwa wakati huu hata yale ambayo ni matokeo ya uchunguzi wa juujuu uliofanywa katika karne ya kumi na tisa yaliunga mkono nadharia kwamba katika siku za kale sana Wamisri walikuwa na ngozi nyeusi na walibakia hivyo mpaka Misri ilipopoteza uhuru wake.

Akijibu maswali mbalimbali aliyoulizwa Profesa Diop alisema kwamba sampuli zilizokwishapatikana kutokana na machimbo ya akiolojia zilikuwa zinatoshwa kuunga mkono hoja yake. Hakuwa tayari kukubali rai ya Profesa Vercoutter kwamba maandishi ya anthropolojia ya kabla ya mwaka 1939 yasiaminike kwa urahisi kwa sababu hayakuwa na usanifu wa kisayansi.

Washiriki wengi walipinga mbinu aliyoitumia Profesa Diop ya kulazimisha fikra zake. Profesa Sauneron aliuokosoa msimamo huo kwa kusema kwamba jumla ya watu waliokuwa wameishi katika bonde la mto Nili tangu historia ilipoanza kuandikwa mpaka leo iliweza kubuniwa kuwa kama milioni mia kadhaa. Uchunguzi kwa kuchimba ulikuwa umefanywa katika sehemu mia kadhaa na miili 2,000 ilikuwa imechunguzwa. Kwa kuwa matokeo ya uchunguzi yalikuwa kidogo sana halikuwa jambo la busara kuyatumia kama msingi wa nahitumisho mukubwa hivyo. Kwa sababu sampuli zilizopo hazikutoa sura kamili, lilikuwa jambo zuri kungoja mpaka uchunguzi kamambe utakapokuwa umetoa ushahidi unaokubalika.

(3) Ukweli wa Uchunguzi wa Usawiri

Katika uwanja huu kulikuwa pia na mawazo mawili yaliyopingana. Profesa Diop alifikiri kwamba kwa kuwa Wamisri walikuwa weusi usawiri uliokuwa wa rangi ambao hakuweza kuonyesha kuthibitishia maoni yake, lazima uliwakilisha watu weusi tu. Profesa Vercoutter aliyeyungwa mkono na Maprofesa Ghallab na Laclant alisema kwamba usawiri wa Kimisri wa tangu ufalme wa kumi na nane na kuendelea ulionyesha maumbile ya watu weusi ambao walikuwa hawajachorwa kabla ya hapo. Hii ingeweza kufasiriwa kwamba tokea ufalme huo na kuendelea Wamisri walikuwa na uhusiano na watu waliofikiriwa kuwa tofauti nao kikabila.

Profesa Diop alisema kwamba katika utangulizi wake alitoa pia picha nyingi zilizochorwa kutokana na sanamu tu. Alifikiri kwamba zote hizi ziliwakilisha watu weusi au kwamba zilionyesha maumbile maalumu ya jamii za watu weusi. Aliomba ufanywe uhakiki thabiti wa nyaraka hizi na kuwataka washiriki katika kongamano kuleta picha kama hizo za watu weupe waliokuwa na nafasi za heshima au za mamlaka kuanzia enzi za mwanzo za Mafarao. Washiriki mbalimbali walijibu kwamba palikuwa hapajazuka swali la kugunduliwa nchim Misri kwa sanamu zenye hadhi sawa na zile za Uyunani, kwa mfano. Profesa Vercoutter alisema kwamba inawezekana kutoa sahamu nyingi zinazowaonyesha watu waliochorwa kwa rangi

nyekundu na si nyeusi, lakini Profesa Diop angekataa kuzitambua kama sanamu za watu wasio weusi. Profesa El Nadury hakukana kwamba palikuwa watu weusi kati ya Wamisri katika enzi za Ufalme Mkongwe lakini aliseina ilikuwa hailekei kwamba watu wote wa nchi hiyo walikuwa weusi.

Profesa Vercontter aliseina kwamba picha ya Farao Narmer ilikuwa imekuzwa mno na yawezekana maumbile yake fulani yalipotoshwa. Alisema pia kwamba kuamua kuwa mtu aliyechorwa ni mwesu hakutegemea misingi yoyote maalum. Profesa Save-Soderbergh alifikiri vivyo hivyo akiongeza kwamba picha hiyo ingaliweza pia kuonwa kama ya mtu wa Lapland.

Profesa Vercontter hakupinga oni kwamba labda kulikuwa watu weusi wachache katika historia yote ya Misri. Yeye mwenyewe alitoa mfano zaidi ya watu hao walivyokuwa waniechorwa. Lakini alipinga jinsi kweli fulani zilivyowasilishwa kutokana na mainbo mawili: kwanza picha zilikuwa zimechorwa kiholelaholela katika kipindi chote walipotawala marejeo dhahiri, na pili kuchaguliwa kwa baadhi ya picha kama hizi kutumwa kuunga mkono dhana. Profesa Diop akijibu hoja hizo alisema kuwa alianua kutumia vitu vilivyochongwa tu na madhari ili kuepuka uwezekano wa kujadili umuhimu wa rangi. Lakini ilibidi atumie vifaa vile tu vilivyopatikana Dakar. Orodha ilikuwa ndefu sana na ilihusu vifaa vya toka enzi za Ufalme Mkongwe mpaka mwisho wa enzi za Mafarao. Ushahidi uliunga mkono nadharia; na nadharia yoyote kinyume chake ilibidi ipate ushahidi wa usawiri ulioonyesha Wamisri ambao hawakuwa weusi.

Wakati wa majadiliano marefu sana kuhusu rangi, Maprofesa Vercontter, Sauneron, na Save-Soderbergh, kwa upande mmoja, na Profesa Diop kwa upande mwingine hawakukubaliana tena. Janibo lililokubalika tu ni kwamba somo hili lilihitaji uchunguzi zaidi likisaidiwa na maabara maalumu.

Profesa Vercontter akikubali kwamba palikuwa na uwakilishi wa watu weusi katika sanamu za Wamisri wa Ufalme Mkongwe na akatoa mfano. Lakini hakufikiri kwamba sanamu hizi ziliwakilisha Wamisri wote, kwani hawa pia waliwakilishwa pia sanamu nyingine za wakati huo zinazoonyesha mauumbile tofauti kabisa.

Profesa Vercontter alishangaa ni kwa nini, kama kweli walikuwa weusi watumie rangi nyeusi mara chache sana walipojichora wenyewe na badala yake kutumia rangi nyekundu. Profesa Diop alisema rangi nyekundu hii iliawakilisha taifa la watu weusi wa Misri na kwamba rangi ya njano iliyotumiwa kuchora picha za wanawake iliwiana na dokezo walilolitoa Wanaanthropolojia wa Kimarekani kwamba, katika mataifa mengi wanawake kwa kawaida walikuwa na rangi hafifu zaidi kuliko wanaume.

(5) Uchanganuzi wa Kiisimu

Kichwa hiki cha habari kilileta maelewano makubwa zaidi kati ya washiriki kuliko vile vilivyojadiliwa hapo awali. Vidokezo vya ripoti ya Profesa Diop na ripoti ya Profesa Obenga vilifikiriwa kuwa vya insingi. Majadiliano yalifanyika katika viwango

viwili. Akijibu hoja ya Profesa Diop kwamba Kimisri hakikuwa lugha ya Kisemitiki, Profesa Abdalla alisema kwamba oni hili lilikuwa kinuume cha oni lililoelezwa mara nyingi kwamba lugha hii ilikuwa ya Kisemitiki.

Mjadala kuhusu sarufi na maana ya maneno ulizuka kati ya Profesa Diop na Profesa Abdelgadir M. Abdalla juu ya neno KMT. Profesa Diop alisema kwamba neno analolifasiri KMT lilitokana na KM, - "eusi." Kwa maoni yake hili lilikuwa neno la jumla lenye maana ya "watu weusi" yaani "Wanegro." Profesa Abdelgadir M. Abdallah alichukua fasiri inayokubalika KMTYW lenye maana "Wamisri" iliyo wingi wa KMTY "Mimisri" na umbo la *nisha* KMT yenye maana "nchi nyeusi, yaani Misri". Profesa Sauneron, alikubaliana na jinsi Profesa Abdallah alivyofasiri na kutafsiri maandislii hayo.

Profesa Sauneron akigcukia inasuala mapana zaidi aliwaelekeza watu kwenye mbinu iliyopendekezwa na Profesa Obenga akimfuata Profesa Diop. Alisema Kimisri kilibakia lugha imara kwa kipindi cha miaka 4500. Misri ilikuwa mahali ambapo athari zote za nje zilikutana na katika hali hii ilikuwa lazima kwa lugha kutohoa inaneno kutoka lugha za kigeni. Lakini mizizi ya Kisemitiki ilikuwa mia chache tu kati ya jumla ya maelfu mengi ya maneno. Kimisri kisingeweza kutolewa katika muktadha wake wa Kiafrika na asili yake isingeweza kuelezwa kikamilifu kutokana na msingi ya Kisemitiki. Kwa hiyo lilikuwa jambo la kawaida kutegemea kupata lugha zinazofanana nacho barani Afrika.

Lakini matumizi ya mbinu thabiti yalilitajika kukabili tatizo gunu la pengo la miaka 5000. Huu ndio muda unaotenga Kimisri cha kale na lugha za Kiafrika za siku hizi.

Profesa Obenga alieleza ukweli kuwa lugha ambayo ilikua kikawaida tu ingeliweza kubakiza miundo fulani ya kale. Alikuwa ametoa mifano ya jambo hili katika mada yake ya siku ya kwanza ya kongamano.

Profesa Sauneron alisema kuwa mbinu iliyokuwa imetumika ilikuwa ya kuvutia sana kwani isingewezekana kwa kiwakilishi cha nafsi ya tatu umoja katika Kimisri cha kale kufanana kwa bahati tu na kile cha kiwolof. Vyote hutokea kama viambishi tamati. Alikuwa na matumaini kwamba jaribio liugfanywa la kuunda lugha ya Kiafrika ya awali kwa kuanza na lugha za Kiafrika zilizopo wakati huu. Hatua kama hii ingewezesha kufanyika ulinganifu kati ya lugha za Kiafrika na Kimisri cha kale. Profesa Obenga aliona kwamba njia hiyo ilikuwa inakubalika. Profesa Diop alifikiri ilikuwa muhimu kupata mbinu ya utafiti kutokana na ulinganishi wa maumbile ya kiisimu na alitoa mfano mmoja kueleza alikuwa na maana gani. Alifikiri kwamba Wadiuka, Wanuer, na Washilluk pamoja na lugha zao kwa upande mmoja, na Wawolof kwa upande mwingine, walikuwa na uhusiano kikabila na pia, kwa kiasi kidogo, kusinu. Majina ya pekee ya Kisenegali hutumiwa pia na koo kwenye makabila haya. Profesa Diop hasa aliamini kwamba lugha ya Wakaw-Kaw waishio katika milima ya Unubi ni kiungo dhahiri kati ya Kimisri cha Kale na Kiwolof. Kama nyongeza tu Profesa Vercoutter alieleza kwamba katika kaburi la Sebek-Hotep

kulikuwa na picha za Waniloti watatu ambao bila shaka yoyote walikuwa mababu wa Wadinka na Wanuer.

(6.) *Uendelezaji wa mbinu za Taaluma fungamano na Taaluma mbalimbali*

Palikuwa na makubaliano kamili kuhusu jambo hilo juu ya ulazima wa kufanya uchunguzi kamambe wa maeneo yanayopakana na bonde la mto Nili ambayo yangeweza kutoa habari mpya kuhusu maswali yaliyoletwa kwenye kongamano.

Profesa Vercoutter aliona kwamba ilikuwa lazima kuipa uzito unaostahili ekolojia ya kale ya Delta na pia eneo kubwa sana ambalo Profesa Balout aliliita eneo lenye rutuba la umbo la mbalamwezi.

Profesa Cheikh Anta Diop alipendekeza kwamba uchunguzi ufanywe kuhusu njia walizofuata watu waliohama kutoka Darfur kuelekea magharibi hadi wakafika pwani ya Atlantiki kwa kutumia njia mbalimbali; wale walioelekea kusini wakifuata bonde la mto Kongo na Kaskazini kuelekea senegal. Alionyesha pia jinsi ambavyo ingalikuwa vizuri kuchunguza kwa undani zaidi uhusiano wa Misri na sehemu zilizobaki za Afrika. Mathalani kuna sanamu ndogo ya Osiris ya karne ya saba kabla ya enzi zetu ambayo imegunduliwa katika mkoa wa Shaba, nchini Zaire.

Ingekuwa vizuri vilevile kuchunguza dhana isemayo kwamba matukio makubwa yaliyoliathiri bonde la mto Nili kama kuchomwa moto na kuteketewa kwa Thebes na Wasiria au uvamizi wa Wapersia mnamo mwaka - 525 yalileta matokeo makubwa sana katika bara zima la Afrika.

D. Mahitimisho ya Jumla

Inategemewa kwamba matokeo ya mijadala katika kongomano hili yatathminiwa na washiriki kwa namna mbalimbali.

Ingawa mada za awali zilizotumwa na UNESCO zilieleza ni mambo gani yalikuwa yanahitajika washiriki wengi hawakutayarisha mada zilizokuwa zimefuatia utafiti mkubwa kama ule uliofanywa na Maprofesa Cheikh Anta Diop na Obenga. Matokeo yake ni kuwa majadiliano hayakuwa na ulingano wowote.

Hata hivyo majadiliano yalikuwa ya manufaa makubwa kwa sababu zifuatazo.

1. Yalionyesha wazi mara nyingi umuhimu wa kubadilishiana habari za kisayansi.
2. Yaliwaonyesha washiriki, dhahiri kabisa kasoro za mbinu ambazo mpaka wakati huu zilikuwa zikitumika katika utafiti.
3. Yaliwafanya walioshiriki waone mifano mipya ya mbinu za uchunguzi ambazo zingeweza kutumiwa kulichunguza kisayansi zaidi swali lililolikabili.
4. Mkutano huu wa kwanza ulipaswa kwa vyovyote kuangaliwa kama msingi wa majadiliano ya baadaye ya kimataifa na ya taaluma fungamano. Unapaswa pia kama mwanzo wa utafiti zaidi ambao kama ilivyoonekana ulikuwa unahitajika. Mapendekezo mengi yaliyotolewa yanaonyesha hamu ya washiriki kwenye kongamano ya kutaka kupendekeza mpango wa utafiti kwa wakati ujao.
5. Mwisho, kongamano lililawezesha wataalamu ambao mpaka sasa walikuwa

hawajapata fursa ya kulinganisha na kutofautisha mawazo yao kugundua njia nyingine za kukabili matatizo, na za kupata vyanzo vya taarifa na mbinu nyingine za utafiti tofauti na zile ambazo walikuwa wamezizoea. Kongamano lilikuwa la manufaa makubwa sana katika nyanja hizi pia.

E. Mapendekezo

Kongamano linapendekeza UNESCO na mashirika mengine yanayohusika yaangalie mambo yafuatayo:

(1) Anthoropojia Maumbo

Ingefaa:

- (i) Uchunguzi wa kimataifa utayarishwe ua UNESCO. UNESCO ama ishauriane na vyo vikiu katika nchi nyingi za kutosha au na wataalamu binafsi wanaotambulika kimataifa, au vinginevyo kuitisha kongamano ambalo litaweka viwango kamili vinafuata misingi ya kisayansi ya kufafanua mataifa na kupambanua mataifa ya wenye mifupa inayofukuliwa;
- (ii) Kushirikisha vituo vya huduma za afya katika nchi wanachama wa UNESCO kwa madhumuni ya kupata takwimu kamili za matokeo ya uchunguzi wa mabaki ya mifupa ya maiti;
- (iii) Mabaki yote ya imili ya watu ambayo yako katika majumba ya kuhifadhi mambo ya kale kote duniani yachunguzwe tena na pia uchunguzi wa mabaki yaliyogunduliwa hivi karibuni huko Misri yachunguzwe haraka iwezekanavyo, hasa yale yaliyopatikana katika Delta. Nia ya uchunguzi huu ni kuongeza habari muhimu kuhusu mabaki haya;
- (iv) Wakuu wa nchi huko Misri wajaribu kadri iwezekanavyo kuruhusu uchunguzi wa mabaki ya ngozi ufanywe na wakubali kuunda idara itakayoshughulikia anthropolojia maumbo.

(2) Uchunguzi wa Uhamiaji

Ingefaa uchunguzi ufuatao ufanyike:

- (i) Uchunguzi makini wa akiolojia wa vipindi vya kale wakati ambapo Delta ilikuwa ikikaliwa na watu. Uchunguzi huu ungeweza kutanguliwa na uchanganuzi wa sampuli za udongo kutoka Delta. Uchunguzi na utoaji wa tarehe za sampuli hizi muhimu za udongo unaweza kufanyika wakati mmoja huko Kairo na Dakar;
- (ii) Utafiti wa namna hiyohiyo ufauywe katika maeneo ya Sahara yaliyo karibu na Misri na katika Maoasisi. Utafiti huu utathmimi michoro iliyochongwa kwenye majabali au ile iliyotumia rangi na mabaki mengine yote yaliyochimbuliwa na yanayoweza kupatikana. Sampuli hizi za machimbo zinaweza kuangaliwa kwa makini na kupewa tarehe wakati uleule;

- (iii) Utafiti katika bonde lenyewe unaolingana na ule uliokwishafanyika Unubi utakaohusu makaburi ya watu weugine ainbao hawakuwa Mafarao pamoja na baki ya utamaduni wa kale na kwa jumla bonde katika kipindi chote kabla ya historia.
- (iv) Utafiti kuhusu alama za Waafrika wa kale katika Usawiri wa Kimisri na umuhimu wake kihistoria. Mifano ya nyani na igozi ya chui ("duma") imekwishatajwa katika kongamano. Bila shaka itawezekana kugundua mifano mingine.

(3) Isimu

Kongamano liuapendekeza kwamba uchunguzi wa isimu ufanywe bila kuchelewa kuhusu lugha za Kiafrika ambazo zimo katika hatari ya kutoweka. Ilifikiriwa kwamba Ki-Kaw-Kaw ni lugha ambayo ni mfano mzuri sana wa lugha kama hizo.

Wakati huo inapendekezwa wataalamu wa Isimu-Linganishi washirikiane kimataifa ili waweze kuchunguza uhusiano wowote uliopo baina ya lugha za Kiafrika na Kimisri cha Kale.

(4) Mbinu za Taaluma Fungamano na Taaluma Mbalimbali

Kongamano linatumaini kwa dhati kwamba:

- (i) Uchunguzi wa kimkoa wa taaluma fungamano waweza kufanyika katika maeneo mengi kwa kuanza na sehemu zifuatazo:

Dārḥur

Eneo lililo kati ya mto Nili na Bahari ya Sham mipaka ya Mashariki ya Sahara,

Eneo la Mto Nili lililo kusini mwa latitudo kumi,

Bonde la Mto Nili kati ya Maporomoko ya Pili na ya Sita.

- (ii) Uchunguzi wa taaluma fungamano ufanywe haraka kuhusu Wa-Kaw-Kaw ambao wamo katika hatari kubwa ya kutoweka.

II. Ufumbuzi wa Maandishi ya Kimeroe

(1) Taarifa ya awali ilikwishatayarishwa na Profesa Leclant baada ya kuombwa na UNESCO¹⁴. Maoni yake ni kama ifuatavyo:

(a) Lugha ya Kimeroe ambayo ilituniwa na watu wa Napata na Meroe ilikuwa bado haeleweki ingawa maandishi yake yalikuwa yamekwishafumbuliwa.

Taarifa za kihistoria za uchunguzi uliofanywa wa mambo ya Meroe zimeonyesha jinsi utafiti uliofanywa kwa inakini juu ya maandishi yaliyokusanywa polepole bila utaratibu maalumu ulivyoanza kufanywa hivi karibuni. Utafiti wa kiakiolojia ungefanikisha ugunduzi wa maandishi mengine hapo baadaye. Hadi sasa hakuna

14

Angalia taarifa hii ya awali kwenye kiambatisho IV cha taarifa ya mwisho ya kongamano (1974)

maandishi yaliyokwishagunduliwa katika eneo lililo kati ya Maporomoko ya Pili na ya Nne. Hakuna kilichokwishagunduliwa pia katika Bahari ya Sham, mabonde yaliyoko upande wa Magharibi, Kardofan na Darfur.

Ilikuwa muhimu sana kuendelea na uchimbaji bila kukata tamaa kwani inawezekana kabisa siku moja maandishi katika lugha mbili yakagunduliwa.

(b) Matokeo ya utafiti wa awali yamechapishwa kwa kirefu katika *Meroitic Newsletter*. Jarida hili lilifanya iwezekane kuchapisha matokeo ya utafiti hata uchunguzi ulipokuwa bado haujakamilika kabisa. Mikutano mingi ya wataalamu ilikuwa imefanyika - Khartoum inwezi Desemba 1970, Berlin ya Mashariki Septemba 1971, na Paris Juni 1972 na tena Julai 1973. Matokeo ya mkutano wa pili wa Paris yalichapishwa katika jarida litwalo *Information Note No. 34* iliyotolewa na Kamati ya Kisayansi ya Kimataifa ya Kusawidi Historia ya Afrika, UNESCO.

Mashine za kompyuta nazo pia zimetumiwa kila inapobidi kuchambua lugha ya Kimeroe kwa muda wa miaka kadhaa. Matokeo yake ni kwamba maendeleo makubwa na ya haraka yalikuwa yameonekana katika shughuli hii.

(b) Mpaka sasa imewezekana kuanza kuchambua muundo wa lugha kwa kuorodhesha *stichs*. Orodha ya maneno yalinyonukuliwa imefikia 13,405; na imekwishapatikana njia ya kuiuliza masline maswali.

Katika misingi hii, juhudi ilikuwa imekwishafanywa ya kulinganisha Kimeroe na Kimisri au Kinubia kwa kutumia maneno ambayo maana yake ilijulikana au ingweza kubuniwa.

(c) Profesa Leclant alimaliza mada yake kwa kuelezea mikondo ya uchunguzi iliyokuwa ikifuatwa:

Profesa Hintze alikuwa akishughulikia muundo wa lugha;

Profesa Schaeukel alikuwa akiendeleza data ya kuingizwa katika kompyuta.

Profesa Abdelgadir M. Abdallah alikuwa akiendelea na utafiti ambao angetoa taarifa juu yake baadaye. Utafiti huu ulikuwa umetoa matokeo ambayo yalikuwa sawa na yale ya kundi la watafiti wa mataifa mbalimbali.

Juhudi zitakazofanywa hapo baadaye zitakuwa pamoja na kulinganisha lugha ya Kimeroe na lugha nyingine za Kiafrika ili kugundua nafasi yake kati ya lugha hizo hasa uhusiano wake na Kinubi. Juhudi nyingine za baadaye ni kufanya ulinganishi wa lugha hii na lugha zinazosenwa katika maeneo yanayopakana na Ethiopia. Mwisho ingekuwa vizuri kulinganisha Kimeroe na lugha za Kiafrika kwa ujumla.

Majadiliano

(2) Profesa Abdallah aliseina kwamba alikubaliana na utaratibu unaotumika kunukuu Kimeroe na mbinu iliyokuwa imeandaliwa ya kunakili matini. Aliseina kwamba kulikuwa na mapengo katika ujuzi waliokuwa nao. Mapengo yenyewe yalihusu: Kutojulikana kabisa kwa mfumo wa viwakilishi nafsi, matumizi ya

viwakilishi vionyeshi na maumbile ya viambishi awali na tamati. Ilikuwa muhimu pia kujua ni lugha nyingine zipi zilizokuwa na uhusiano na Kimeroe.

Profesa Abdallah alipendelea utaratibu wa kugawanya lugha ili kuchunguza vipengee vyake: Alionyesha jinsi vipengee vinavyotumika katika kuunda majina ya watu binafsi vinavyobadilikabadilika. Katika majina haya vipengee hivi vilikuwa na maana fulani kijamii. Vipengee vilivyokuwa vinabadilikabadilika vilirudiwarudiwa katika majina ya watu kadhaa wa familia moja; majina ya watoto fulani yalikuwa na vipengee kutoka majina ya mama na baba zao; majina fulani yalikuwa na maana ya vyeo na inengine yalikuwa majina ya inahali.

(3) Profesa Shinnie alieleza kwamba kulikuwa na uwezekano wa kutumia mbinu za namna tatu katika uchunguzi huu; kugundua matini iliyoandikwa kwa lugha mbili; uchambuzi wa muundo wa ndani wa lugha; na ulinganishi wa lugha hii na lugha nyingine za Kiafrika.

Ulinganishi wa moja kwa moja uliofanywa kati ya lugha mbili kuu za Sudani ya Kaskazini zisizo za Kiarabu na lugha za Kundi la M haukuleta matokeo yoyote mazuri. Lugha ya Kimeroe inaweza ikasaidia katika ulinganishi wa namna hii.

(4.) Profesa Kakosy aliyekuwapo kama msikilizaji tu alisisitiza umuhimu wa kuchunguza vyanzo vya nyaraka. Alisema kwamba huko Budapest kulikuwa na mabaki ya altare yaliyotoka katika machinibo karibu na Abu Simbel. Alipendekeza mabaki haya yawekwe mara moja katika Mikusanyo vitu vya nakshi vya Kimeroe.

(5) Profesa Cheikh Anta Diop alifurahishwa sana na maendeleo yaliyokuwa yamepatikana. Wakati ngunduzi wa maandishi yenye lugha mbili ukingojwa, alishauri zituniwe mbinu za kompyuta zilizowezesha kufunbuliwa kidogo kwa maandishi ya picha ya Maya na kundi la Leningrad lililoongozwa na Profesa Knorossov. Maandishi mengi yalikuwa yamefunbuliwa kwa kutumia matini za lugha mbili au zaidi. Utaratibu sahihi wa kuchunguza Kimeroe ungekuwa kutumia kwa pamoja lugha nyingi na uwezo wa kompyuta kwa namna ifuatayo:

- (a) Kana utaratibu tu wa kimbini uhusiano kati ya Kimeroe na lugha za Waafrika weusi ungedadisiwa ili kuunda hali ya kuwapo lugha nyingi.
- (b) Kwa kuwa kwa sasa hivi maneno 22,000 ya Kimeroe yanaweza kusomwa kwa uhakika mkubwa, orodha ya nisamiati wa msingi wa maneno 500 ingewekwa kwenye kadi za kompyuta kwa ajili ya kila moja ya lugha 100 za Kiafrika zilizochaguliwa na kundi la wataalamu wa lugha. Maneno yatakayochaguliwa yanaweza kuwa kwa mfano yale yanayoonyesha shemu za mwili, maneno yanayohusiana na ufalme, maneno ya kidini, maneno ya utamaduni wa kuonekana, na kadhalika.
- (c) Kompyuta iandaliwe ili iweze kutambua, kwa mfano, konsonanti tatu zinazofanana, konsonanti mbili zinazofanana, n.k.
- (d) Kutokana na matokeo yaliyopatikana, kufanywe ulinganishi wa miundo ya lugha zilizopungua kando kwa kando.

Njia hii ilikuwa nzuri zaidi kuliko ile inayolinganisha miundo ya lugha shaghala

baghala kwa sababu ni mainbo machache tu yanayofahamika katika sarufi ya Kimeroe. Njia hii ilikuwa mathubuti zaidi kuliko kungoja matokeo ya uchunguzi usio linganishi wa muundo wa ndani wa Kimeroe.

Profesa Leclant aliunga mkono njia hii ya uchunguzi na hatua ambazo zinapaswa kufuatwa. Alifikiri kwamba zingeweza kutoa habari muhimu sana. Alifikiri kwamba ingefaa sana kupanga orodha si tu ya maumbile yaliyopo bali pia na yale yasiyokuwapo (yaani kutokuwepo kwa miundo fulani au mfuatano fulani katika mpangilio).

Bw. Glélé' aliuliza ni kwa kiasi gani mbinu zilizotumika kufumbulia lugha nyingine zingeweza pia kutunika kufumbulia maajabu ya lugha ya Kimeroe. Alisema kwamba Profesa Knorossov na Profesa Piotrovski walikuwa wanaelikwa kwenye mkutano walivyokaribishwa Profesa Holthoer na Profesa Hintze ili watoe habari zinazohitajika.

Profesa Leclant alisema kwamba uchunguzi mkubwa sana kuhusu jambo hili ulikuwa umefanyika katika mikutano iliyofanyika Paris na London wakati wa kiangazi cha mwaka 1973. Uchunguzi kuhusu maandishi ya Kimohenjodaro na Kimaya ulikuwa haujapiga hatua kubwa ya kutuwezesha kuwa na msimamo thabiti.

Lakini Profesa Diop alitumaini kwamba wazo la kutumia mbinu za ulinganishi pamoja na uchunguzi wa miundo lisingeachwa. Pendekezo lake lilikubaliwa na Profesa Sauneron ambaye alichakua fursa hii kusisitiza umuhimu wa kazi ambayo ilikuwa imekwishafanywa na Kundi la Uchunguzi wa Meroe.

Majadiliano yaliyofuata yalihusu zaidi lugha za Sudani. Profesa Save-Soderbergh alisisitiza kwamba ilikuwa muhimu kwa lugha hizi kufanyiwa utafiti kwani hata ukiacha mbali haja ya kuzilinganisha na Kimeroe, ujuzi wa lugha hizi ungalisaidia kuendeleza utaalumu wa Kiisimu wa lugha za Kiafrika. Baada ya kusema haya, Profesa Save-Soderbergh alitoa multasari wa pendekezo lake kuhusu jambo hili. Alisisitiza pia kwamba ilikuwa inawezekana, hata kwa kutunika fedha kidogo sana, kuanzisha idara ya uandishi na kuharakisha ukusanyaji wa vitu, kuvichambua kwa kompyuta na kusambaza tena taarifa husika.

Mwisho kulikuwa majadiliano kuhusu mapendekezo yenyewe. Profesa Diop alitumaini kwamba kazi nzuri sana iliyokuwa imefanywa na Kundi la Uchunguzi wa Meroe ingeendelezwa kwa ushirikiano wa mataifa yote na kwamba uorodheshaji wa msamiati ungefanyika Sudan na kwamba uorodheshaji wa namna hiyo hiyo ungefanyika katika sehemu nyingine za Afrika kwa ushirikiano wa Profesa Obenga. Profesa Sauneron aliyakubali mapendekezo haya yote. Lakini kuwa haikuwa wazi kazi hii ingekuwa na umuhimu gani katika shughuli za kufumbua Kimeroe, alitumaini kwa utafiti wa lugha za Kiafrika ungeendelezwa peke yake hata kama utafiti huo ungekuwa schemu ya mradi wote. Yawezekana mradi huo ungeendelea kwa muda mrefu sana na ilikuwa muhimu kwamba mbinu madhubuti, ipatikane tangu mwanzo baada ya mradi kutathminiwa ipasavyo, Profesa Obenga aliunga mkono wazo hili na alitoa rai kwamba itayarishwe orodha ya maumbile ya sarufi ya Kimeroe

yanayojulikana mpaka sasa. Profesa Leclant alionelea kwamba rai hii ingeweza kutekelezwa mara moja. Profesa Habachi alitumaini kwamba umuhimu wa kufanya uchunguzi wa Kiakiolojia usingepuuzwa.

Akijibu pendekezo la Profesa Obenga kuhusu mbinu ya kutumika katika utafiti, Bw. Glélé' alisema kwamba mbinu ambazo zingetumika zingeamuliwa baada ya kukamilika kwa kundi la kimataifa litakalohusika na jambo hilo. Alieleza kwamba UNESCO ilikuwa inaweza kutoa fedha kusaidia uchunguzi huo kwa kufuata njia za kawaida za kutoa misaada hiyo. UNESCO ilikuwa ikigharimia na kuongoza mpango uliokuwa unachunguza utaalumu wa Kiisimu wa lugha za Kiafrika na ilikuwa imedhamini mpango wa miaka kumi kwa madhumuni hayo.

Mapendekezo

- (1)(a) Mkutano ulieleza kufurahishwa kwake na kazi iliyokuwa imefanywa na Kundi la uchunguzi wa Kimeroe hako Paris likishirikiana na wataalamu wa nchi nyingine nyingi. Mkutano unafikiri kwamba kazi hiyo ni ya kimsingi na yenye matumaini ya kuleta matokeo mazuri.
- (b) Mkutano umeamua kwa kauli moja kupendekeza hatua zifuatazo ili kuendeleza mradi huo:
 - (i) Kuharakisha uchambuzi unaotumia kompyuta kwa kutoa msaada zaidi wa fedha, na kusambaza taarifa kwenye vituo vyote vikuu vinavyochunguza Kimeroe. Habari zinazosambazwa ziwe zimehakikiwa na kufanywa za kuaminika zaidi;
 - (ii) Kila inapowezekana itolewe orodha ya majina halisi ya binafsi ya Kimeroe, majina ya mahali na ya yeye, na kuainisha miundo Kiisimu. Zifanywe pia juhudi za kuwashirikisha wataalamu wa Isimu ya lugha za Kiafrika.
 - (iii) Kupambana na kuchapisha mikusanyo yote ya matini za Kimeroe pamoja na orodha ya vitabu, picha, nakala halisi na unukuzi wa maandishi kwenye majalada yaliyopo.
 - (iv) Kutoa msamiati kamili wa Kimeroe.
- (c) Kwa kuwa matokeo ya mradi yaliyopatikana mpaka sasa ni ya kisayansi na yanatoa matumaini ya maendeleo mazuri, na kwa kuwa gharama kubwa zaidi ya mradi wote imekwishalipwa kwa fedha kutoka sehemu mbalimbali, mkutano huu unafikiri sasa kwamba ni lazima kuhakikisha mradi unaendelea hadi ukanulike kwa kupatikana fedha zaidi zitakazotumiwa ifuatavyo:
 - (i) Gharama za uandishi na malipo kwa wafanyakazi watakaokusanya nyaraka na uchapishaji wa mambo ya kisayansi;
 - (ii) gharama za utafiti katika sehemu zilipohifadhiwa mikusanyo ya vitu kwenye makumbusho;
 - (iii) gharama za kusafiria wataalamu;

- (iv) gharama za kutayarisha makadi ya kuingiza katika kompyuta na kukodi kompyuta.

(2) Hatua inayofuata katika utafiti ingekuwa uchunguzi unaolinganisha miundo na maneno ya lugha za Kiafrika kwa kuanza na lugha za Sudan na maeneo yanayopakana na Ethiopia; lugha ambazo baadhi yake zimeanza kutoweka. Kazi hii ingefanywa kwa kuwapa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Khartoum mafunzo katika isimu; ikiwezekana wanafunzi hawa wawe wale ambao lugha hizi ndio zao za asili.

Mafunzo haya yangekuwa ya manufaa katika malengo mengine mengi. Mradi kama huu ambao ungekuwa nyongeza kwa kazi ambayo imekwishafanyika tayari nchini Sudan ungefanywa kwa maafikiano na Chuo Kikuu cha Khartoum; na fedha zitahitajika za kuwasomesha wanafunzi.

(3) Zaidi ya hayo uchunguzi mpana zaidi wa kiisimu ungefaa ufanyike ili maneno muhimu yaweze kukusanywa. Uchunguzi kama huu unapaswa kufanywa kwa kushirikiana na Kundi la Uchunguzi wa Meroe na kuongozwa na wataalamu waliochaguliwa na UNESCO wakishirikiana na Kamati ya Kisayansi ya Kimataifa ya Historia ya Afrika. Uchaguzi wa maneno unapaswa kufikia kiwango cha inancno kama 500 ya makundi mbalimbali. Maneno hayo yachaguliwe kutoka lugha 100 hivi.

Maneno haya yaliyokusanywa yakiwekwa katika kompyuta yanaweza yakawa chombo muhimu sana si tu kwa kufumbulia lugha ya Kimeroc bali pia kwa kufumbuka matatizo mengine mengi ya Kiisimu katika Afrika ya leo.

2

Misri ya Mafarao

Mnamo mwisho wa kipindi cha barafuto huko Ulaya, kulitokea mabadiliko makubwa ya hali ya hewa katika nchi zilizo kusini mwa Bahari ya Mediterani. Kupungua kwa mvua, kulisababisha watu wanaoishi kwa kuhamahama katika jangwa la sahara upande wa Afrika kuhamia katika bonde la mto Nili, wakitafuta sehemu za kudumu za kupatia maji, makazi halisi katika bonde la mto Nili, huenda yalianzishwa mwanzoni mwa kipindi cha karibu cha Neolithiki, (kama mwaka - 7000). Baada ya kufanya maskani katika bonde la mto Nili, Wamisri wa kale waliyaingia maisha ya ufugaji na ukulima.

Muda mfupi kabla ya historia kuanza wamisri walijifunza matumizi ya metali katika kipindi kijulikana kama kipindi cha matumizi ya Shaba ambapo matumizi ya metali yalienea taratibu na kuchukua nafasi ya mawe. Dhahabu na shaba nyekundu vikaanza kuonekana kwa mara ya kwanza, ingawa shaba nyeusi haikutumiwa hadi Ufalme wa Kati. Inavyoonekana matumizi ya chuma hayakuwa yameenea sana hadi kipindi cha mwisho cha historia ya Mafarao.

Enzi kabla ya historia

Wakazi wa awali katika Misri, walikuwa na maisha magumu, na yumkini yalikuwepo mashindano kamambe kati ya makundi mbalimbali ya watu ili kujipatia ardhi kwenye kingo za mto Nili na katika eneo la Delta lililokuwa ua nafasi ndogo zaidi. Wakiwa wanutokea magharibi, mashariki na kusini, watu hawa bila shaka walikuwa wametokana na makundi mbalimbali yaliyojipambanua. Isingekuwa ajabu kwa vikundi kama hivi kuishi mbali mbali katika maeneo ya bonde kutokana na kuwapo kwa vizuizi tofauti tofauti vya asilia na pia kutokana na asili zao.

Makundi haya, ndiyo asili ya majimbo ya kale ya Misri, yaliyotokea kuwa msingi wa muundo wa kisiasa wa nchi hiyo katika vipindi vya kihistoria.

Mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi kabla ya historia ni udhibiti wa ardhi (tazama utangulizi). Wamisri wa kale walifanikiwa kufyeka mapori katika maeneo yao ya karibu kwa ajili ya kilimo, walikausha inabwawa na kujenga miambaduki ya kuzuia maji ya mafuriko. Polepole watu waling'amua manufaa ya kutumia mifereji kmmwagilia maji inashambani. Kazi ya namna hii ilihitaji juhudi ya watu wengi wakifanya kazi kwa pamoja, na hii ilisababisha kuchipuka kwa infumo wa kisiasa wa sehemu iliyohusika katika kila jimbo.

Baadhi ya kumbukumbu kuhusu kukua kwa umoja wa kisiasa katika Misri zinaweza kuonekana katika mabaki ya kale ya kimaandishi. Hii huonyesha kwamba muamo zania za kale majimbo katika Delta ni dhahiri yalikuwa yamekwisha kuungana. Majimbo ya magharibi ya sehemu hii, kwa desturi yalikuwa yameungana chini ya mungu Horus, ambapo yale ya mashariki mwa Delta yalikuwa yameungana chini ya mungu Andity, mtawala wa Djedu, ambaye baadaye madaraka yake yalimezwa na yale ya Osiris. Imewahi kutolewa fikra kwamba majimbo ya magharibi yaliyateka yale ya mashariki, na kuunda muungano wa Ufalme katika Misri ya Kaskazini. Hii ilifanya Horus aendelee knabudiwa katika sehemu zote za Delta, na hii ikaenea polepole katika Misri ya Juu, hadi nguvu zake kupita zile za Seth aliyekuwa mungu mkuu wa muungano wa Misri.

Kipindi cha enzi za kale (-3200 - -2900)

Tukio la kwanza lenye umuhimu wa kihistoria tunalolijua ni muungano wa hizi falme mbili za kipindi kabla ya historia au hasa kutekwa kwa Misri ya chini na mtawala wa Misri ya Juu ambaye masimulizi ya jadi yameintambulisha kwa jina la Menes, hali vyanzo vya kiakiolojia vimemwita Narmer. Huyu ndiye Mfalme wa kwanza katika Falme thelathini ambazo mwana-historia wa Misri, Manetho (-280) alizigawanya katika msururu mrefu wa watawala hadi kufikia wakati wa Alexander Mkuu, Familia ya Menes ilikuwa na makazi yake Thinis katika Misri ya Juu, ambayo ilikuwa wilaya iliyojulikana zaidi ikiwa na maji wakfu wa Abydos ndani yake. Ilikuwa karibu na nji wa Abydos, na hekalu la mungu Osiris, ndipo Petrie alipochimba makaburi makubwa ya Wafalme wa Falme mbili za mwanzo. Ni wazi kwamba ufalme wa kusini ndio ulitawala nchi nzima, na baada ya ushindi wao wa kwanza, ukaanzisha makao makuu yake huko Memphis karibu na mahali ambako sehemu hizi mbili ziliungana.

Habari za wafalme wa Falme mbili za mwanzo za kipindi cha enzi za kale hazijulikani sawasawa kwetu; Hata hivyo, ni dhahiri kwamba kipindi hiki kilikuwa cha kazi ngumu za kujiimarisha. Katika kipindi cha miaka 300 ya ufalme wa kwanza na wa pili utamaduni wa miaka ya baadaye ya kipindi kabla ya ufalme uliendelea. Lakini, wakati wa Ufalme wa tatu na wa nne umoja wa kisiasa ulifikiwa na nchi mpya ilikuwa imara kiasi cha kuweza kujieleza bayana katika taratibu za Kimisri.

Ufalme Mkongwe (- 2900 Hadi - 2280)

Ufalme wa Tatu

Imekwishonyeshwa kwamba Wafalme wa Falme mbili za mwanzo (kipindi cha enzi za kale) yaelekea walijihusisha zaidi na mapigano ya ushindi na kujiimarisha. Tunaamini kuwa imani mpya ya ufalme kuhusishwa na mungu, ilianza hasa katika kipindi cha Ufalme wa Tatu na ni hapo ambapo Misri ilikupokuwa taifa n moja lililoungana. Ufalme huo ulianzishwa na Mfalme Zoser, ambaye bila shaka alikuwa mtawala mwenye nguvu na hodari. Hata hivyo sifa zake zilifishwa kwa kiasi kikubwa na sifa za raia wake I-em-htp, mtu aliyekuwa mashuhuri tangu enzi zake hadi leo kama mjenzi, tabibu, kasisi, mwana-

mazingaombwe, mwandikaji na mtunzi mashuhuri wa methali. Miaka elfu mbili na mia tatu baada ya kifo chake aliabudiwa kama mungu wa madawa ambaye Wayunani (waliomwita Imeuthes) walimtambua, kwa upande wao kama Askelepios. Mafanikio yake makubwa kama mjenzi yamedhihirika katika Piramidi yenye ngazi, jengo kubwa na pana lililojengwa mahsusi kwa maziko ya Farao wake katika sehemu iitwayo Sakkara, kwenye eneo la hekta 15 katika mstatih wenye urefu wa meta 544 na upana wa meta 277. Alitumia kipaji chake kujengea Piramidi hii ukuta uliokuwa kama ngome na akaanzisha ujenzi wa kustaajibisha uhotumia mawe badala ya matofali.

Wafalme wengine wa Ufalme wa Tatu hawajulikani sana, kama walivyo wale wa Falme mbili za mwanzo, ingawa haram kubwa sana yenye ngazi ambayo haikumalizika kujengwa, ya Mfalme Sekhem-Khet (ambaye huenda alikuwa mtoto wa Zoser na mrithi wake) hapo Sakkara, ni ushahidi wa kutosha kuwa majengo ya Piramidi ya Zoser hayakuwa ya kipekee. Mfalme Huny, aliyekuwa wa mwisho katika Ufalme wa Tatu, ndiye aliyemtangulia Snefru ambaye ni mwanzilishi wa Ufalme wa Nne. Piramidi iliyoko Mcidum umbali wa kilometa 70 kusini mwa mji wa Cairo, ilijengwa kwa ajili yake. Jengo hili, ambalo tangu mwanzo ujenzi wake ulifanywa hatua kwa hatua lilipanuhiwa mara kadhaa na kufanyiwa mabadiliko ya kisani kabla ya kukamilishwa kuwa Piramidi kamili (labda na Snefru mwenyewe).

Ufalme wa Nne

Ufalme wa Nne ambao ulikuwa moja ya vilele katika historia ya Misri, ulianza na kipindi kirefu cha utawala mkakamavu wa Mfalme Snefru. Sehemu ya kumbukumbu zake zilizopatikana katika jiwe la Palermo zaelezea mafanikio ya kampeni zake za kijeshi dhidi ya Wanubi upande wa kusini na makabila ya Kilibya kwa upande wa magharibi kudumisha kupitika kwa njia za biashara (hasa ya mbao) pwani ya Syria, na shughuli nyingi za ujenzi zilizokuwa zikifanyika mwaka hadi mwaka zilizohusu mahekalu, ngome na majumba ya Kifalme kote nchini Misri. Snefru alitawala kwa miaka ishirini na miine na yasadikiwa kuwa pengine alikuwa mzawa wa tawi dogo la ukoo wa kifalme. Ili kuuhalalisha wadhifa wake alimuoa Hetep-Heres, binti rukubwa wa Huny na hivyo kuingiza damu ya kifalme katika ufalme huu mpya. Alijenga piramidi mbili Dahshur, ya upande wa kusini ikiwa na umbo la mstatili-dufu na ile ya upande wa kaskazini ikiwa na umbo halisi la piramidi na ikiwa na ukubwa ulioanza kukaribiana na ule wa Piramidi Kuu ya Khufu iliyoko Giza.

Wafalme waliomfuatia Snefru, yaani Khufu (Cheops), Khafre (Chephren) na Mankaure (Mycerinus) wanakumbukwa hasa kutokana na piramidi tatu walizozijenga kwenye mwinuko wa rasi ya Giza, umbali wa kilometa 10 kusini-magharibi mwa mji wa Cairo ya sasa. Piramidi ya Khufu ina sifa ya kuwa jengo kubwa kuliko yote yaliyopata kujengwa na binadamu, na ilijengwa kwa ufundi makini mno, mipango ilikuwa sahihi mno na uzuri wa ulinganifu wake umeifanya ibakie ya kwanza kati ya maajabu saba ya dunia. Piramidi za mtoto na mjukuu wa Khufu, ingawa ni ndogo kwa umbo, zinafanana na piramidi hiyo kiukenzi na katika mpangilio wa majengo madogo madogo yanayozizunguka.

Ufalme wa Tano

Ufalme huu ulijiimarisha kutokana na kukua kwa ukasisi katika Heliopolis. Ngano katika Mafunjo ya Westcar inaeleza kuwa Wafalme watatu wa kwanza wa ufalme wa tano walikuwa watoto wa mungu Re na bibi aliyecitwa Radjeded, ambaye alikuwa mke wa kasisi luko Heliopolis. Ndugu hawa watatu walikuwa Weserkaf, Sahure, na Neferirkare. Sahure anajulikana hasa kwa sababu ya ubora wa sanamu za kuchora ambazo zimepamba hekalu lenye kaburi lake kule Abusir, kaskazini mwa Saqqara. Inajulikana sana kuwa piranidi za kifalme za Ufalme wa Tano zilikuwa ndogo sana ukilinganisha na makaburi makubwa ya enzi za Ufalme wa Nne; ufundi wa majengo hayo pia ulikuwa wa hali ya chini. Hata hivyo mahekalu ya makaburi yaliyopakana na piramidi hizo yalikuwa majengo maridadi sana ambayo yalikuwa yamepambwa vizuri kwa sanamu za kuchora zilizopakwa rangi.

Wengi kati ya Wafalme wa Ufalme huu, walijenga karibu na piramidi, mahekalu makubwa kwa heshima ya Mungu-Jua. Kila hekalu lilikuwa limepitwa na mnara mrefu sana wa mawe yenye kung'ara juani.


Pamoja na ujenzi wa mahekalu mengi makubwa yaliyokuwa na mali kadhaa, ambayo yameorodheshwa katika Jiwe la Palermo, Mafarao wa Ufalme wa Tano walikuwa hodari katika kulinda mipaka ya Misri na katika kupanua uhusiano wa kibiashara na nchi majirani zake. Kumbukumbu za misafara ya mashambulizi dhidi ya Walibya na jangwa la magharibi, mabedui wa Sinai, na Wasemitiki wa Palestina ya kusini, ziliandikwa katika kuta za mahekalu yaliyokuwa na makaburi yao. Meli kubwa zilizuru pwani ya Palestina wakati wa enzi za Sahure na Issesi. Meli za Kimisri zilifika pia katika pwani za nchi ya Punt iliyo katika pwani ya Somalia, kutafuta bidhaa zilizothaminiwa sana kama, manemane, mpingo, wanyama, na bidhaa nyinginezo. Biashara ya mbao za mwerezi kati ya Misri na Syria iliendelea kushamiri. Bandari ya kale ya Byblos iliyokuwa pwani chini ya miteremko yenye misitu mingi ya nchi ya Lebanoni ilifikiwa na meli nyingi kutoka Misri zilizofuata mbao.

Ufalme Wa Sita


Hakuna ushahidi unaoonyesha kuwa kulikuwa na machafuko ya kisiasa katika kipindi cha mabadiliko kati ya Ufalme wa Tano na wa Sita. Ufalme wa sita ulionyesha nguvu zake wakati wa utawala wenye nguvu na uliodumu kwa muda mrefu wa Pepi I (mfalme wa pili). Kwa mara ya kwanza mfalme wa Kimisri aliacha kutumia mbinu za kujihami kijeshi, na kuongoza jeshi lake kwa nguvu zote kushambulia nchi ya adui. Jeshi kubwa likiwa chini ya mamlaka ya Uni, jemadari wa Kimisri, liliwarudisha nyuma maadui mpaka makwao kaskazini karibu na mlima Carmel, na kuwazingira katika mashambulizi matano ya mwisho, kwa kushusha majeshi toka kwenye manowari za Misri kaskazini kabisa mwa pwani ya Palestina. Pamoja na hayo, katika kipindi hiki hiki mfalme huyu aliweza kupanua na kuhami mamlaka ya nchi ya Misri katika Unubi.



2.1 Mto Nili ulivyotoka Poromoko la Tatu hadi Bahari ya Mediterani Kronolojia ya Historia ya Misri.



2.2 Kronolojia ya historia ya Misri (Mchoro na J.Vercouter)



Alipofariki mtoto wa Pepi I, Merenre, Peri II, mtoto wake mwenye umri wa miaka 6, alichukua madaraka ya ufalme na kuitawala nchi kwa muda wa miaka tisini na minne. Alikufa akiwa na umri wa miaka mia moja. Huyu ndiye mfalme aliyetawala kwa kipindi kirefu kuliko wafalme wote katika historia. Katika mwaka wa pili wa utawafa wa Pepi II, alirudi Herkhuf, mfalme wa Elephantine ambaye alikuwa amesafiri katika nchi ya Nubi na kufika katika jimbo la Yam ambako alipata bidhaa nyingi za thamani na mbilikimo mchezaji kama zawadi za mfalme. Kwa hamasa kubwa, mfalme ambaye wakati huu alikuwa na umri wa miaka minane tu alipeleka barua ya kutoa shukrani kwa Herkhuf akimwomba kuchukua kila hadhari kusudi yule mbilikimo aweze kufika Memphis salama.

Utawala wa Pepi II ulifikia kikomo kwa machafuko ya kisiasa ambayo yalianza mwanzoni mwa enzi za Ufalme wa Sita. Katika nyakati hizi wafalme wa Misri ya Juu walikuwa wakizidi kupata nguvu zilizowawezesha kujenga makaburi yao katika wilaya zao, badala ya kujenga karibu na piramidi ya mfalme katika eneo la Nekropolis. Madaraka aliyokuwa nayo mfalme yaligawanyika au kugawanywa kwa haraka kwa watawala wa mikoa. Matukio haya yalifanya jumba la kifalme kupoteza vitu vingi inavyoonekana kutokana na kukosekana kwa kumbukumbu baada ya zile zilizojengwa na Pepi II. Haijulikani kwa bakika kama matukio haya utengano hayakuweza kudhibitiwa na Mafarao au ikiwa utawala dhaifu uliodumu kwa muda mrefu wa Pepi II ndio ulioharakisha kuanguka huku. Jambo linalofahamika wazi ni kwamba Ufalme Mkongwe ulifikia kikomo chake mara tu baada ya kifo chake, halafu kikaanza kipindi cha machafuko na ghasia nyingi tunachokiita Kipindi cha Kati cha Mwanzo.

Kipindi cha Kati cha Mwanzo (- 2280 hadi - 2060)

Alipokufa Pepi II taifa la Misri lilitengana kutokana na mlipuko wa ghasia za kimwinyi. Kipindi cha ufutini wa kisiasa, ghasia, na vita vya wenyewe kwa wenyewe kilianza. Katika bonde zima la mto Nili, watawala wadogo wadogo, walishambuliiana katika machafuko haya hata Manetho akataja katika historia yake kuhusu Misri kwamba utawala wa Ufalme wa Saba ulijunuishwa Wafalme sabini waliotawala kwa muda wa siku sabini.

Zinajulikana habari kidogo tu kuhusu Ufalme wa Saba na hata kama tungekuwa na taarifa kuhusu majina ya Wafalme, mfuatano wa orodha hiyo ya majina kulingana na tawala mbalimbali zinazohusika, haukubaliki.

Baadaye ulitokea ukoo mpya wa kifalme huko Herkloopolis (katika Misri ya Kati) na lilifanyika jaribio la kuendeleza utamaduni wa Memphis. Wafalme hawa wa Ufalme wa Tisa na wa Kumi ni dhahiri walikuwa wamelidhibiti eneo la Delta, sehemu ambayo ilikuwa ikishambuliwa mara kwa mara na watu wanao hamahama jangwani. Lakini Misri ya Juu wakati huo, ilikuwa imekwisha gawanyika katika vitengo vyake vya zamani, kila jimbo likiwa chini ya mamlaka ya mtawafa mwenyeji wa hapo. Historia ya baadaye ya Misri inabainishwa na WaThebes kuwa na nguvu zaidi. Nguvu hii iliwawezesha kudhibiti katika enzi za Ufalme wa kumi na moja Misri ya Juu na baadaye kidogo nchi nzima.

Hali ya Misri baada ya kuvunjika kwa Utawala Mkongwe ambao ulikuwa umekwishapata mafarakiio makubwa ya vitu vya kuonekana na utaalamu imeelezwa vizuri

sana na mtu mmoja mwenye hekima aitwaye Ipu-wer. Maandishi yake ambayo yanaelekea kuyagusia pia matukio ya Kipindi cha Kati cha Mwanzo yamehifadhiwa kwenye mafunjo ya Ufalme Mpya ambayo sasa yapo katika Makumbusho ya Leiden. Katika fungu moja la habari hiyo, anaeleza kuhusu mapinduzi ya kijamii yaliyotokea mwanzoni mwa Kipindi cha Kati Mwanzo na kukosekana kwa utawala wa aina yoyote wenye nguvu katika nchi nzima.

Hata hivyo, kulipatikana mambo mengine ya manufaa katika kipindi hiki cha machafuko. Mojawapo ya mambo hayo mapya ni hadhi ya mtu binafsi kutiliwa mkazo zaidi, kwa mfano, kutambuliwa kwa haja ya usawa wa kijamii, na heshima kwa watu wa kawaida. Hivyo, katika kipindi cha machafuko Wamisri waliibua mwenendo wa maadili wenye lengo la kumlinda mtu binafsi. Hii inajidhihirisha katika maandishi kwenye mafunjo yanayojulikana sana kama Ukinzani wa Mkulima mwenye Ufasaha wa kusema yaliyoandikwa kuanzia enzi za Ufalme wa Kumi. Hii ni hadithi ya mkulima maskini ambaye baada ya kunyang'anywa mali yake na kabaila mmoja anaamua kutetea haki zake.


Ufalme wa Kati (- 2060 hadi - 1785)

Ingawa Wamisri walionja kidogo desturi za kidemokrasi, njozi yao hii haikudumu. Desturi hizi zilionekana dhahiri wakati wa matatizo lakini zikafifia wakati neema na nidhamu viliporejea tena katika enzi za Ufalme wa Kati. Hiki kilikuwa kipindi kikuu cha pili cha maendeleo ya kitaifa. Misri iliungana tena kwa nguvu za silaha. Thebes mji ambao hapo kabla haukuwa na umaarufu sana wala kujulikana, ulikomeshwa utawala wa Heracleopolis na kuwa na madaraka juu ya nchi nzima ya Misri. Baada ya ushindi katika vita sehemu mbili za nchi hii ziliunganishwa na kuwekwa chini ya utawala mmoja.

Mfalme Menthutep anajitokeza kama mtu mashuhuri sana katika Ufalme wa Kumi na moja. Jukumu lake kubwa lilikuwa kupanga upya taratibu za utawala wa nchi. Upinzani wowote dhidi ya Mfalme huyu ulikuwa umekwisha nyamazishwa, ingawa yawezekana palitokea maasi kidogo hapa na pale. Menthutep II ambaye pia alitawala kwa muda mrefu, alijenga hekalu lenye kaburi mahali paitwapo Deir el Bahari ambalo ndilo jengo kubwa sana la ukumbusho kuliko mengine yote katika kipindi hicho hapo Thebes.

Kuanzia kipindi kilichafuatia utawala wa Menthutep II, familia ilianza kupoteza nguvu zake. Katika utawala wa mfalme wa inwisho wa Ufalme wa Kumi na Moja mtu mmoja aliyetwa Amenemhet, ambaye alikuwa waziri wa mfalme, na huku akiwa pia na vyeo vingine yafikiriwa kuwa huenda ndiye aliyekuwa mwanzilishi wa Ufalme wa kumi na mbili. Mfalme wa kwanza katika mfululizo wa watawala wenye nguvu katika Ufalme huu alijulikana kwa jina Amenemhet.

Amenemhet I alichukuwa hatua tatu inuhimu ambazo zilizingatiwa kwa dhati na warithi wake. Alianzisha makao makuu mapya yaliyoitwa Ithet-Tawi (Mmiliki wa Nchi



2.3 Kiephren (*Historia ya Ustaarabu wa Misri ya Kale Juzuu la 1, Neuchâtel, Paris, 1961*)

Mbili) kusini kidogo mwa Memphis. Kutoka mahali hapo, aliweza kudhibiti vizuri Misri ya chini. Aidha, alianzisha desturi ya kumweka mtoto wake wa kiume karibu naye katika kiti cha ufalme kama naibu wake.

Senusret I alifuata nyayo za baba yake, na kwa juhudi zake mwenyewe, uwezo, na upana wa maono yake, aliweza kutekeleza mipango iliyotajirisha na kuipanua Misri. Mfululizo wa safari za kivita, zikiongozwa na mfalme mwenyewe au na wasaidizi wake hodari, uliimarisha utawala na namalaka ya Misri juu ya Unubi ya chini. Vitendo vya mfalme kwa upande wa magharibi yaelekea vilihusu tu misafara ya mashambulizi dhidi ya Walibya wa Temen na kuhifadhi mawasiliano na maoasisi. Sera yake kuhusu nchi za kaskazini-magharibi ilikuwa ni kulinda mipaka yake na kuendelea kufanya biashara na nchi za Asia magharibi.

Wafalme wawili walofuata, Amenemhet II na Senusret II yaonekana hawakupendelea kuimarisha na kupanua maeneo ya kigeni yaliyokuwa yametekwa na Misri. Hata hivyo, Senusret III anakumbukwa kwa kuiteka Unubi ya chini na knishinda hata kufanya iwe na hadhi ya jimbo la Misri. Utawala wa muda mrefu, na wenye neema wa mrithi wake Amenemhet III, ulijulikana kutokana na mipango yake kamambe ya umwagiliaji maji mashamba, iliyoleta upanuzi mkubwa wa shughuli za kilimo na za kiuchumi katika Fayyum.

Alipotawala Amenemhet IV, ukoo wa kifalme ulionekana dhahiri kuwa ulikuwa unapoteza nguvu zake. Utawala wake wa muda mfupi, na ambao haukuwa na mambo ya sifa, ukifatiwa na utawala wa muda mfupi zaidi wa Malkia Sobek Neferu, ukawa ndio kikomo cha Ufalme wa Kumi na mbili.

Kipindi cha Kati cha Pili (- 1785 hadi - 1580)

Majina yaliyotumiwa na Mafarao wa Ufalme wa Kumi na Tatu yanaonyesha kuwapo kwa jumuiya kubwa ya watu wa Asia katika Misri ya Chini. Bila shaka, jumuiya hii iliongezeka kutokana na uhamaji wa makundi makubwa ya watu kutoka sehemu za kusini-mashariki mwa Misri. Makundi haya yalilazimika kuhamia kusini, kutokana na uhamaji ulioenea huko Asia ya magharibi. Viongozi wa makundi haya waliitwa Hka-Hasut na Wamisri, kwa maana ya Watawala wa Nchi ya Kigeni. Kutokana na neno hilo ilitoholewa istilahi Hyksos aliyotumia Manetho katika maandishi yake ambayo ilitumika kwa jumla kuita watu wote.

Wahyksos, walianza tu upinzani wao dhidi ya mamlaka ya kisiasa ya Ufalme wa Kumi na Tatu mnamo mwaka - 1729. Hata hivyo kufikia mwaka - 1700 walikuwa wamekwishajitokeza kama watu waliojizatiti vycina, wenye silaha za kutosha na wapenda vita, na wakateka sehemu ya mashariki ya Delta ikiwa ni pamoja na mji wa Hat-Wert (Avaris) ambao waliujengea ngome upya na kuutumia kama makao yao makuu.

Hapana shaka yoyote kwamba uvamizi wa Wahyksos ulikuwa na athari kubwa katika taifa. Kwa mara ya kwanza walileta farasi, gari la farasi, na deraya la kulinda mwili katika nchi ya Misri. Wamisri ambao hapo awali hawakuwa na haja ya inatumizi ya vifaa



2.4 *Malkaa Hatshepsut akiwa amekaa*

hivi, polepole walivitumia kikamilifu na kwa ustadi dhidi yao na kuweza kuwafukuza nchini. Walianzisha vita vya ukombozi, ambavyo viliongozwa na watawala wa jimbo la Thebes. Nyaraka chache zilizosalia za kipindi hiki zinahusu vita walivyopigana wafalme wa mwisho wa Ufalme wa Kumi na Saba dhidi ya wakandamizaji wa Ki-Asia, baada ya karibu miaka 150 ya uvamizi wao. Ahmose alifanikiwa kabisa kuwafukuza wavamizi kutoka katika Delta, akateka makao yao makuu, Avaris, na akawafuata hadi Palestina ambako aliwazingira katika ngoime ya Sharuhen. Baada ya hapo, aliendelea kaskazini na kushambulia nchi ya Zahi (Pwani ya Foenesia). Kutokana na matukio haya nguvu za Wahykos zikawa zimevunjiliwa mbali kabisa.

Ufalme Mpya (- 1580 hadi - 1085)

Ufalme wa Kumi na Nane

Mfalme Ahmose I, alisifiwa na vizazi vilivyofuata kama baba wa Ufalme mpya, na mwanzilishi wa Ufalme wa Kumi na Nane. Amenhotep I alifuatwa na Thutmose I na II halafu na Malkia Hatshepsut aliyeolewa na ndugu zake wawili wa kambo Thutmose II na III kwa zamu. Lakini katika mwaka wa tano wa utawala wake Hatshepsut alikuwa na nguvu kiasi cha kuweza kujitangaza kuwa mtawala mkuu wa nchi. Miaka ishirini ya utawala wake ilikuwa ya amani na neema kwa nchi ya Misri. Alijihusisha sana na mambo ya ndani ya nchi, na katika miradi mikubwa ya ujenzi (hasa hekalu lake maarufu katika Thebes ya magharibi). Mafanikio yake makubwa aliyoyaonea fahari sana yalikuwa msafara wa mashambulizi huko Punt, na usimikaji wa minara miwili ya mawe katika hekalu la Karnak.

Baada ya kifo cha Hatshepsut, Thutmose III akaanza kutawala mwenyewe.

Kitendo chake cha kwanza alichofanya kama mfalme, kilikuwa ni kubomoa sanamu za Hatshepsut, na kufuta jina lake pamoja na sura yake mahali popote vilipoonekana. Baada ya kuridhika kiasi chake aliunda jeshi haraka haraka na kwenda kushambulia muungano wa serikali ya miji ya eneo la Palestina, Syria, Lebanon, ambazo zilikuwa zimeunganisha majeshi yake katika mji wa Megiddo zikijitayarisha kuuasi utawala wa Misri. Akishambulia kwa kasi ya kustaajabisha, Thutmose III aliwatia kishindo maadui na kuwafanya wakimbie kutafuta mahali pa kujificha katika kuta za mji. Baada ya Megiddo kusalimu amri, nchi nzima hadi kufikia Lebanoni ya kusini, iliwekwa chini ya mamlaka ya Misri. Kwa jumla, Thutmose III alifanya ziara ya mashambulizi kumi na saba ugerini, na silaha za Kimisri ziliwatia hofu watu wa Syria kwa miaka mingi iliyofuata. Misri ilijiimarisha barabara kama taifa lenye nguvu ulimwenguni, likiwa na himaya kubwa sana.

Thutmose III alifuatiwa na Mafarao wawili hodari, Amenhotep II na Thutmose IV. Hiyu wa mwisho alikuwa na ulusiano wa karibu sana na ufalme wa Mittani, kwani alikuwa ameoa binti kutoka katika nyumba ya ufalme huo. Binti hiyo ndiye bibi anayeonekana katika picha zilizoko katika majengo ya ukumbusho, kama Malkia Mkuu wa Farao na mama wa Amenhotep III.



2.5 Akhenaton akawa kwenye jua (G. Mokhtar)

Amenhotep III alipomrithi baba yake, huenda alikuwa amekwishamwoa malkia wake mkuu Teye. Kutawazwa kwa huyu mfalme kijana kulifanyika wakati nchi ilipokuwa imefikia kilele cha nguvu kisiasa, uchumi, na utamaduni wake ulikuwa uneendelea. Zaidi ya hayo kulikuwa na amani duniani hata kuwapa fursa Farao na watu wake kuendelea kuishi maisha ya starehe na anasa za kila namna. Karibu na mwisho wa utawala wa Amenhotep III, kama inavyodhihirishwa na nyaraka za Tell-el-Amarna, kukosekana kwa matumizi ya nguvu za kijeshi kuliwafanya baadhi ya raia wakakamavu wafikirie mipango ya kijitwalia madaraka na kuuasi kabisa utawala wa Misri. Licha ya maasi hayo kugundulika, Amenhotep III yaelekea hakuyajali kabisa. Kusifika kwake kunatokana na uhodari wake katika shughuli za ujenzi na udhamini wa sanaa mbalimbali. Ndiye mjenzi wa hekalu la Luxor, majengo mengine makubwa hapo Karnak, na katika sehemu nyingine nyingi katika Misri, na mahali pengine kama Soleb kule Nubia.

Ingawa madhehebu ya Aton yalianza katika utawala wa Amenhotep III, ukuaji wake haukuathiri taratibu za ibada kwa miungu wengine, mpaka baadaye katika kipindi cha utawala wake pengine katika mwaka wa thelathimi wa utawala huo. Huu ndio wakati ambapo mtoto wake, Amenhotep IV (ambaye baadaye alijulikana kama Akhenaton) alipokuwa naibu wake katika utawala wa nchi. Mtawala huyu mpya ambaye alionekana kuwa na mwili dhaifu, mnyouge, na mwenye kuwa na maumbile hafifu kama ya kike hakuwa na huika ya kiaskari, au mwana siasa mashuhuri. Alijijhusisha sana na mambo ya kiakili na kiroho.

Katika ushupavu wake wa wakati wa ujana, Amenhotep IV alianzisha inabadiliko makali ya sera yaliyofanya ukasisi wa Amon ushambuliwe moja kwa moja. Mfalme huyu mwanzoni aliendelea kuishi Thebes, mahali alipokuwa amejenga hekalu kubwa kwa ajili ya Aton, mashariki mwa hekalu la Amon huko Karnak.

Baada ya kukasirishwa na jinsi watu walivyopeka mabadiliko yake huko Thebes, aliamua kuondoka mjini humo. Alianzisha makazi mapya sehemu iitwayo Tell-el-Amarna, katika Misri ya Kati, ambayo aliyaita Akhet Aton, (upeo wa macho wa Aton) mahali ambapo aliishi hadi kufa kwake miaka kumi na minne baadaye. Alibadili jina lake na kuwa Akh-en-Aton (Yule-anayemtumikia Aton).

Akhenaton hakutosheka na kitendo chake cha kumtangaza Aton kama mungu wa pekee. Aliendelea kuwashambulia minngu wengine wa zamani. Wakati machafuko yakiendelea kila upande kumzunguka, Akhenaton aliishi katika makao yake makuu akimwabudu miungu wake wa pekee. Ibada hii ya nguvu za uumbaji wa jua iliyopewa jina la Aton, haikuhitaji sanamu zozote za miungu huyu, na iliendeshwa wazi hadharani katika uwanja wa hekalu.

Mapinduzi ya Kiaton, hayakudumu baada ya kifo cha Akhenaton. Naibu na mrithi wake Semnekh-Ka-Re, baada ya muda mfupi tu alianzisha juhudi za kuleta mapatano na ukasisi wa Amon. Semuekh-Ka-Re hakutawala kwa kipindi cha zaidi ya miaka mitatu, na alifuatiwa na Tut-Ankh-Aton, ambaye baadaye alibadili jina lake na kuwa Tutankhamun. Kwa kuwa tunafahamu ya kwamba Farao huyu kijana alifariki dunia alipokaribia miaka 18 hivi, na ya kwamba alitawala kwa kipindi cha miaka tisa hivi, huenda alikuwa na umri wa

miaka minane hivi wakati alipochukua kiti cha ufalme. Wakati wa utawala wa Tut-Ankh-Amon na hata baada ya kifo chake, kulikuwa na kusita kidogo katika kuachana kabisa na Aton, licha ya kumrudisha Amon. Aidha, Aton alikuwa na nafasi yake katika miungu ambayo iliendelea wakati wa kipindi kifupi cha utawala wa Mfalme Ay, aliyemfuata Tut-Ankh-Amon. Ilikuwa tu katikati enzi za Horemheb aliyekuwa mfalme wa mwisho katika Ufalme wa Kumi na Nane, yalipoanza mateso dhidi ya Aton kwa mkazo ule ule kama ilivyokuwa dhidi ya Amon hapo awali.

Horemheb alitoka katika ukoo wa nasaba ya watu wa majimboni katika mji mdogo uliokuwa katika Misri ya Kati. Uzoefu wake wa muda mrefu kama amiri-jeshi wa jeshi la Misri, na kiongozi katika utawala, ulimpa fursa ya kutathmini ufisadi wa kisiasa uliokuwa umeongezeka kwa kiasi cha kutisha tangu mwanzoni mwa utawala wa Akhenaton. Alipokalia kiti cha ufalme tu akaanzisha mara moja mabadiliko mengi yaliyokuwa ya manufaa kwa nchi. Pia, alitoa amri kuhimiza ukusanyaji wa mapato ya taifa, na akakomesha ubadhirifu jeshini na kati ya watumishi wa serikali.

Ufalme wa kumi na tisa

Horemheb alimpendelea sana kiongozi mmoja wa jeshi, aliyeitwa Pa-Ramesses, ambaye alimfanya waziri na kumteua kuwa mrithi wake. Katika kufanya hivyo akawa ameanzisha utawala wa Ufalme wa Kumina Tisa. Hata hivyo, Pa-Ramesses alipopata madaraka ya ufalme, alikuwa amekwishaazeka na alitawala kwa muda wa miaka miwili tu. Alifuatiwa na mwanae aliyekuwa mtawala mshiriki wake, Seti I. Mtawala huyu alikuwa wa kwanza katika ukoo wa wapiganaji shupavu walioonyesha juhudi zao katika kurudisha hadhi ya Misri katika nchi za kigeni. Mara baada ya kutwaa madaraka ya ufalme Seti I, alikumbana na tishio kubwa kutokana na muungano wa serikali za miji ya Syria, ambazo zilichochea na hata kupewa misaada ya Wahittaiti. Aliweza kuushinda muungano wa serikali hizi, na kuiwezesha Misri kuwa na mamlaka juu ya Palestina.

Baada ya kushinda shambulio la Walibya, Seti alielekea tena Syria ya kaskazini, mahali ambapo majeshi ya Misri yalilikabiliana na Wahittaiti kwa mara ya kwanza. Aliteka Kadesh na japo Wahittaiti walilazimika kurudi nyuma kwa muda, waliendelea kuwa na athari huko Syria ya kaskazini. Vita hivi viliendelezwa na mrithi wake, Ramses II.

Katika utawala wa Ramses II, makao ya kifalme na makao makuu ya utawala yaliamishiwa katika mji uliokuwa kaskazini-mashariki ya Delta, mahali palipoitwa Per-Ramesse. Mahali hapa palianzishwa kambi ya kijeshi iliyokuwa na uwezo wa kumudu vikosi vikubwa vya askari wa miguu na wa magari ya farasi. Katika mwaka wake wa tano wa kutawala, Ramses II, aliongoza majeshi yake manne kukabiliana na muungano wenye nguru wa watu wa Asia waliokusanywa pamoja na Mfalme wa Wahittaiti aliyeitwa Mutawallis. Hii ilikuwa katika juhudi za kuendeleza jitihada za baba yake za kutaka kutwaa tena sehemu zilizokuwa zimekaliwa na Misri katika Syria ya kaskazini. Ingawa katika vita maarufu karibu na Kadesh Ramses aliongoza vikosi vyake katika mtego wa maadui, aliweza tena kukusanya majeshi yake, na kugezuza hali ambayo dhahiri ilikuwa ya kushindwa na kuleta ushindi. Michoro na masimulizi maalumu kuhusu vita hivi na

mashambulio mengine ya ushindi huko Palestina na Syria yaliyotangulia kufuatia vita hivyo ilikuwa imechongwa kwenye kuta za mahekalu ya Ramses II yaliyojengwa katika miamba huko Abu-Simbel na El-Derr katika Unubi ya chini, na katika mahekalu yake kule Abydos na Karnak. Habari za picha hizo pia zilichongwa kwenye lango alilooongeza katika hekalu lake la Luxor, na katika hekalu la kaburi lake linaloitwa Ramesseum. Uhasama kati ya nchi mbili hizi uliendelea kwa muda wa miaka kadhaa. Ilikuwa katika mwaka wa ishirini na moja wa utawala wake, ndipo Ramses II alipoamua hatimaye kutia saini mkataba maarufu wa amani kati yake na Mfalme wa Wahittaiti Hattusilis. Baada ya hapo, ulikuwepo ulusiano wa kirafiki kati ya nchi hizi mbili na Ramses alinwoa binti mkubwa na Hattusilis, katika sherehe iliyotangazwa kila mahali kama alama ya amani na udugu. Alipofariki Hattusilis, hatari mpya ilizuka kutokana na nyendo za watu wa Baharini, ambao hawakakawia kuuvamia na kuushinda Ufalme wa Wahittaiti.

Miaka sitini na saba baada ya kutia saini mkataba wa amani Mfalme Ramses, ambaye sasa alikuwa mzee sana, hakuajali tena dalili za mkosi kutoka nchi za kigeni, na mrithi wake hodari, Merneptah alijikuta amekabiliwa na hali ngumu alipotwaa madaraka ya ufalme.

Wakati huo huo, idadi kubwa ya watu wa Baharini waliokuwa wakipenda vita, walikuwa wamekwishaingia katika eneo la pwani magharibi mwa Delta. Watu hawa waliungana na Walibya na kuwa tishio kubwa kwa Misri. Katika mwaka wake wa tano wa utawala Merneptah aliwakabili wavamizi hawa katika vita kuu sehemu za magharibi mwa Delta, akawapa pigo kali na kuwashinda vibaya sana. Kwenye jiwe lenye maandishi ya kumbukumbu la Merneptah, aliandika kuhusu slughuli zake za kijeshi katika sehemu za Syria na Palestina, na akaorodhesha miji na tawala alizoziteka ikiwa ni pamoja na Kanaan, Askalon, Gezer, Yenoam, na Israel. Hii ilikuwa mara ya kwanza Israel kutajwa katika kumbukumbu za Misri.

Ufalme wa Ishirini

Kifo cha Merneptah kilifuatiwa na migogoro katika Ufalme na kiti cha ufalme kilirithiwa na watawala watano mfululizo ambao mfuatano wao na uhusiano baina ya havijajulika sawasawa. Amani ilirudishwa tena na Sethnakhr ambaye alitawala kwa muda wa miaka miwili akiwa mfalme wa kwanza katika Ufalme wa Ishirini. Alirithiwa na mtoto wake Ramses III, ambaye katika muda wa miaka thelathini na moja ya utawala wake alifanya kila lili lowezekana kufufua utukufu na heshima ya Ufalme Mpya. Katika mwaka wa tano na wa kumi na moja wa utawala wake aliyashinda kabisa makundi ya wavamizi kutoka sehemu za Libya Maghribi. Aidha katika mwaka wa nane wa utawala wake alifaulu kuzima mashambulizi yaliyoandaliwa vizuri na watu wa Baharini kutoka nchi kavu na baharini.

Katika kukabiliana na maovu ya ndani ya nchi Ramses III hakuwa na mafanikio ya kuridhisha kama ilivyokuwa katika kuulinda nchi isivamiwe na majeshi ya kigeni. Nchi ilipata msukosuko kutokana na ghasia za wafanyakazi, machafuko ya watuinishi serikalini, bei kubwa sana za ngano, kushuka kwa thamani ya shaba nyeusi na shaba nyekundu.

Uchakavu uliota mizizi katika vipindi vya utawala wa wafalme waliofuata kuanzia kwa Ramses IV hadi kwa Ramses XI. Mamlaka dhaifu ya wafalme yaliendelea kuwa ya wasiwasi zaidi kulingana na jinsi nguvu za ukasisi wa Amon zilivyoongezeka, mpaka hatimaye alipochaguliwa kasisi mkuu Heri-Hor kuchukua madaraka ya Kifalme na kuanzisha Ufalme mpya.

Kipindi cha kupungua nguvu

Ufalme wa Ishirini na Moja hadi wa Ishirini na Nne (- 1085 hadi - 720)

Katika kipindi cha Ufalme wa Ishirini na Moja, utawala uligawanywa kwa makubaliano ya pamoja kati ya wana wa mfalme wa Tanis katika eneo la Delta na Ufalme wa Heri-Hor katika mji wa Thebes. Alipofariki Heri-Hor, Sniendes (mtawala wa Delta) inaelekea alijinyakulia madaraka ya nchi nzima. Kipindi hiki kilishuhudia kuchanua kwa utawala mpya wa familia yenye asili ya Libya kutoka Fayyum. Mmoja wa watu wa familia hii, aliyeitwa Sheshonq, alinyakuwa madaraka ya utawala wa kifalme wa Misri, na kuanzisha Ufalme uliodumu kwa muda wa miaka 200.

Ilipokaribia mwisho wa utawala wa Ufalme wa Ishirini na Mbili, Misri ilikuwa imegawanyika katika falme ndogo ndogo zilizokuwa zikigombana zenyewe na kutishiwa na Assyria, na nchi ya Sudan ambayo kwa wakati huu ilikuwa yenye nguvu na huru. Wakati huo, mtu aliyeitwa Pedibast alianzisha Ufalme pinzani ambao wafalme wake waliendelea kutumia majina ya ufalme wa Isirini na Mbili. Nyakati hizo, Misri ilidumisha uhusiano wa amani na Suleman kule Jerusalem, ambaye alidiriki hata kumwoa binti wa mfalme wa Misri. Hata hivyo katika mwaka wa tano wa utawala mrithi wa Suleman, Sheshonq aliishambulia Palestina. Ingawa Misri haikufanya jitihada ya kuikalia Palestina, lakini ilifanikiwa kurudisha mamlaka yake ya zamani katika sehemu hizo, na ilinufaika kutokana na kuongezeka sana kwa biashara na nchi za kigeni.

Ufalme wa Ishirini na Nne ulikuwa wa mfalme mmoja tu, yaani Bekenrenef, ambaye Wayunani walimwita Bocchoris mwana Tefnakht. Bocchoris alijitahidi kumuunga rakono mfalme wa Israel dhidi ya Mfalme wa Assyria Sargon II, lakini jeshi lake lilishindwa nguvu katika sehemu itwayo Raphia mwaka - 720. Utawala wa Bocchoris ulifikia kikomo wakati mfalme wa Sudan, Shabaka, alipoivamia Misri.

Ufalme wa Ishirini na Tano na Wasudani wa Waasiria (- 720 hadi -658)

Kulikuwa na mvamizi mwingine wa nchi ya Misri mnamo mwaka - 720 hivi, na safari hii kutoka kusini. Kutoka katika makao makuu yake yaliyokuwa katika Poromoko la Nne kwenye mto Nili. Piankhi, Msudani aliyetawala Sudan kati ya Maporomoko ya Kwanza na ya Sita, alijiona mwenye nguvu na uwezo wa kutosha kuwashambulia Mafarao na utawala wao. Ufalme wake ulidumu kwa muda wa miaka sitini, kabla ya Waassyria kufanikiwa kuukomesha kabisa baada ya mashambulizi mengi.

Ufalme Wakisait (- 658 hadi - 530)

Misri ilikombolewa kutoka kwa utawala wa Waassyria, na Mmisri aliyeitwa Psammetik. Mnamo mwaka - 658 alifanikiwa, kwa msaada wa Gyges wa Lydia pamoja na askari wa kukodiwa wa Kiyunani, kushinda mabaki yote ya ubwana wa Kiassyria, na kuanzisha Ufalme mpya wa Ishirini na Sita. Wafalme wa ukoo huu walijitahidi kishujaa kurudisha heshina ya Misri kwa kuendeleza utanukaji wa biashara. Misri ya Juu ilibadilika na kuwa sehemu yenye kutoa mazao ya kilimo kwa wingi ambayo yaliuzwa na Misri ya chini.

Kipindi cha Waajemi (- 530 hadi - 322)

Katika utawala wa Psammetik III, Misri ililazimika kuvumilia utawala wa Waajemi waliotokea nchi hiyo chini ya kiongozi Cambyses. Kutokana na uvamizi wake na utekaji wa nchi, historia ya nchi ya Misri kama taifa huru ilifikia kikomo. Ufalme wa Ishirini na Saba uliongozwa na Wafalme wa Kiajemi, Ufalme wa Ishirini na Nane, ulikuwa wa kienyeji ulioanzishwa na Amyrtaios, aliyepanga uasi wakati wa utawala wenye heka heka nyingi wa Darius II. Kwa kushirikiana na wafalme wa Athena na Sparta, wafalme wa Ufalme wa Ishirini na Tisa na wa Thelathini walifaulu kulinda uhuru wao waliopata kwa muda wa karibu miaka sitini.

Kipindi cha pili cha utawala wa Waajemi katika Misri kilianza chini ya Artaxerxes III, kauka mwaka - 341. Utawala huu ulikomeshwa na Alexander Mkuu, aliyeiyamia Misri mnamo mwaka - 332, baada ya kuishinda Uajemi katika mapigano ya Issus.

3

Misri ya Mafarao: jamii, uchumi na utamaduni

Uchumi na Jamii

Mashamba na Mabwawa

Kuanzishwa kwa dola ya Mafarao yapata mwaka - 300 hivi, na kipindi kilichofuatia ambacho habari zake hazijukani sana bila shaka viliandamana na maendeleo makubwa ya kiuchumi. Hatuna namna ya kujua kwa hakika kama mipango ya umwagiliaji maji mashambani ndiyo iliyokuwa sababu ya msingi ya kuanzishwa kwa taifa moja lililoungana, au ikiwa kuimarika kwa utawala wa kifalme wa Wathini kulikoambatana na maendeleo katika elimu ya maandishi, ndivyo vilivyorahisisha kazi ya kuratibu mipango ya uchumi mikoani kwa kuandaa kwa akili taratibu za ujenzi na za usambazaji wa chakula katika sehemu mbalimbali za ufalme. Kinachojulikana kwa hakika ni kwamba ufanisi na uhai wa Misri hadi kufikia karne ya kumi na tisa ya enzi zetu ulitegemea sana ukulima na nafaka, hasa ngano na shayiri.

Mfumo wa mabonde anibayo yalidhibiti wa kutawanya maji ya mafuriko pamoja na taka za mto ndani ya matuta ya udongo ulistahimili hadi zilipotengenezwa njia za kisasa za umwagiliaji kwa mwaka mzima. Upo ushahidi unaodhihirisha kuwa utaratibu huu wa umwagiliaji maji ulikuwa ukitumika tangu enzi za Ufalme wa Kati na pengine ulianza mapema zaidi. Ni dhahiri kuwa utaratibu kana huu uliwezesha kulima mazao mara moja tu kwa mwaka. Kwa upande mwingine inuda mfupi wa msimu wa kilimo, ulisababisha watu wengi wawe na nafasi kubwa ya kutumiwa shughuli za ujenzi wa majumba ya dini na ya kifalme. Watu wa kale pia walikuwa na ujuzi wa kumwagilia maji kwa mwaka mzima kwa kuchota maji kutoka miferejini au kutoka kwenye mashimo yaliyochimbwa. Lakini kwa muda mrefu, miguu ya watu na mabega ya binadamu yaliyofungiwa mikatale ndivyo vilivyokuwa nyenzo pekee za kuchota maji zilizofahamika. Na umwagiliaji maji kwa njia ya mitaro ulitumika tu katika kilimo cha mboga, miti ya matunda, na mashamba ya mizabibu.

Mkate na pombe vilivyotengenezwa kutokana na nafaka, ndivyo vilivyokuwa vyakula vikuu. Hata hivyo vyakula vya Wamisri wa kale vilikuwa vya aina nyingi sana. Inashangaza kuona wingi wa aina za keki na mikate zilizoordheshwa katika nyaraka za

wakati huo. Kama ilivyo wakati huu, bustani zilizawisha maharage, choroko na aina nyingine za jamii ya kunde, vitunguu, iliki, mboga za saladi na matango. Bustani za matunda zilitoa tende, tini, mbegu za mkuyu na zabibu za kuliwa. Ukulima wa kitaalamu wa mizabibu ulioendelezwa hasa katika eneo la Delta, na katika sehemu zenye maoasisi jangwani ulizalisha aina nyingi sana za mvinyo. Ufugaji nyuki uliwapatia asali. Walitengeneza mafuta kutokana na ufuta, na mnea uitwao "nabk". Miti ya mizeituni ambayo ilipandwa kwa mara ya kwanza katika kipindi cha Ufalme Mpya, ilikuwa adimu kupatikana, na ustawishaji wake haukuwa na mafanikio sana.

Misri ya enzi za Mafarao haikubadilisha bonde lote kuwa mahali pa kufaa kustawisha mazao. Lakini waliweza kutumia mabwawa, na maziwa yaliyoko katika kingo za kaskazini za Delta, na katika ufuko wa ziwa Moeris. Vile vile walitumia mabonde yaliyoko pembezoni mwa jangwa, na katika mizingo ya mto Nili. Katika sehemu hizi, ndege wengi wa kila namna wuliwindwa au kutegwa. Kwa kuwa mto Nili ulikuwa na aina nyingi za samaki, ambao walikuwa chakula muhimu kwa wananchi, ziliendeshwa shughuli za uvuvi wa kutumia nyavu, vyungu, ndoana na vikapu. Mabwawa naya yalitoa mafisho safi kwa ng'ombe.

Meza za Miungu na inatajiri zilijazwa nyama ya ng'ombe. Kulikuwa na ufundi maalum wa tikataji wa nyama. Mafuta katika nyama yalitumika kutengeneza uturi.

Tunajna kuwa Wamisri wa Ufalme Mkongwe walijaribu kufuga aina kadhaa za wanyama kama vile choroa, swala, korongo wenye vishungi kichwani, na hata fisi, lakini shughuli hii ilikatisha tamaa kutokana na mahitaji yake ya juludi nyingi za kazi. Badala yake walifanikiwa sana katika ufugaji wa kuku, na hasa bata wa into Nili. Nyama ya mbuzi, ambao walikuwa waharibifu wa miti iliyoota kwa uchache bondeni, nyama ya kondoo waliofungwa katika mashamba na kando kando mwa jangwa, pamoja na nyama za nguruwe (licha ya viziwi kadhaa) vilikuwa vyakula vilivyochukua nafasi muhimu katika milo ya kila siku ya wananchi. Kulikuwa na aina mbili za wanyama wa Kiafrika waliofungwa na Wamisri, ambao wanahusiana sana, katika mawazo yetu, na utawala wa zamani wa Mafarao. Wanyama hao ni punda ambao walitumika tangu kipindi cha enzi za kale si kwa kubeba watu, bali kwa kubeba mizigo. Mnyama mwingine alikuwa paka wa nyumbani walioanza kuonekana tu tangu mwishoni mwa Ufalme Mkongwe na mwanzoni mwa Ufalme wa Kati.

Uchimbaji Madini na Viwanda


Watu mashuhuri wenye nasaba bora, waliwinda sungura kama burudani, na kwa madhumuni ya kubadilisha chakula; lakini shughuli hii haikuwa na umuhimu mkubwa kiuchumi. Jangwa lilikuwa na madini aina kwa aina; rangi za kijani na nyeusi kutoka jangwa la Arabuni zilizotumika kupamba na kurembesha macho hata katika kipindi kabla ya historia. Aidha, palipatikana mawe mazuri na magumu yaliyotumiwa na wajenzi na wachongaji (chokaa, itale, alabasta, kwatzi, na mawe mengine ya thamani ya kadiri kama vile feruzi ya Sinai au akiki ya Unubi na amethisti. Utengenezaji wa vifaa vyenye uso wa

kioo uliendelezwa tangu mapema, hata ukasababishwa utengenezaji wa vyombo vyenye kufanana na madini ya thamani yenye rangi feruzi au kijani. Misri ya enzi za Ufalme Mpya, iliendeleza mbinu za utengenezaji kioo, na kuwa mafundi mashuhuri katika fani hii.

Mojawapo ya utajiri uliopatikana kutoka katika sehemu kaine zilizoizunguka nchi, ilikuwa dhahabu, ambayo alitoka Arabuni na Unubi, na ambayo ilikuwa na bei ghali zaidi kuliko fedha, ingawa fedha, madini ambayo yalikuwa safi zaidi na adimu sana ilikuwa na thamani kuhiko dhahabu katika enzi za Ufalme Mkongwe. Jangwa lilikuwa na madini ya shaba ambayo kwa junula yalikuwa ya hali ya chini isipokuwa yale ya Sinai, na hii iliifanya Misri kutegemea shaba kutoka Asia.


Ingawa Misri ililazimika kuagiza vyuma na mbao kutoka kwa majirani zake wa Asia, uwezo wake katika viwanda ulikuwa bora kabisa kushinda nchi nyingine katika fani mbili. Mafarao waliuza nchi za nje nguo na vitambaa, hasa nguo ya kitani ya Misri iliyokuwa bora kushinda zote kutoka nchi za majirani. Mafunjo ambayo yalitumika katika shughuli nyingi kama vile tanga, kamba, nguo, na viatu. Mafunjo haya yalifaa pia kwa utengenezaji wa aina fulani ya karatasi nyororo ya kuandikia iliyokuwa chanzo cha nguvu na madaraka ya maandishi. Aidha aina hii ya karatasi ilihitajika sana katika nchi za nje hasa baada ya kuenea kwa maandishi ya alfabeti katika sehemu za Mediterani ya mashariki. Kilimo cha hali ya juu cha mimea hii huenda kilikuwa mojawapo ya mambo yaliyosababisha kutoweka kwa inabwawa ambayo yalikuwa maskani ya ndege, mamba, na viboko, ambao kana watu wa kale walivyohisi, waliipamba mandhari ya Kimisri.

Undelezaji wa usafiri ulikuwa mojawapo ya fani yakinishi katika maendeleo ya utawala wa Mafarao. Ng'ombe hawakutumika kwa shughuli yoyote ile, isipokuwa kuvuta plau na jenezha wakati wa mazishi. Punda ambaye ni mvumilivu zaidi, na ambaye halitaji matunzo mengi, alikuwa mnyama hasa wa kubeba mizigo mashambani na katika njia ya jangwani (tunafahamu kuwa farasi, ambao walianza kutumika katika elfia ya pili walibakia kuwa anasa kwa wapiganaji na kwamba matumizi ya gurudumu katika shughuli za kiuchumi japo yalifahamika hata katika enzi za Ufalme wa Kale, hayakuwepo mpaka baadaye sana). Ingawa matumizi yake hayakuwa ya mafanikio makubwa na ingawa namna ya kuwatumia katika makundi ilijulikana, punda walitangulia ngamia na kufanya kazi ambazo zingefanywa nao. Ngamia wenyewe walianza kutumika zaidi vijijini baada ya Misri kutekwa na Waajemi. Kwa usafirishaji wa mizigo mikubwa mikubwa inayopelekwa mbali, Wamisri walitumia mto na mifereji yao. Vyombo vidogo vidogo, na mashua kubwa vilisafiri kwa wepesi na vilikuwa thabiti. Zaidi ya hayo hata mapema kabla ya kipindi hicho, mashua za tanga zilikuwa zikasafiri huku na huko katika bahari ya Sham na ya Mediterani. Katika kusafirisha mapande makubwa ya mawe yaliyohitajika hasa katika ujenzi wa mahekalu, walandisi wa enzi za Mafarao walikuwa wamevumbua mbinu stadi na rahisi sana za kufanyia kazi hiyo. Mathalan walitumia matope yenye sifa za kulainisha na kuteleza ili kusogeza rikwama (ambazo hazikuwa na magurudumu wala chao). Vile vile waliweza kutumia kujaa kwa maji ya mto Nili katika kufanya matishari yaliyokuwa yamepakiwa mapande makubwa ya mawe yaelee, au kutumia mukeka ya mafunjo kama matanga ya kuongozea mashua.



3.1 *Kuweka mahesabu* (J. Pirenne, Paris, 1961)

3.2 *Uvuvi* (J. Pirenne Paris, 1961)



Mfumo wa kichumi na kijamii

Uchunguzi wa nyaraka zilizopo waelekea kuonyesha kwamba kila kitu kilitokana na mfalme. Mfalme alikuwa na wajibu wa kidini wa kuhakikisha utaratibu unaowastahili wote ulimwenguni, usalama wa Misri na furaha ya watu wake katika ulimwengu huu na ujao. Wajibu huu ulitimizwa si kwa kutumia madaraka yake kama mfalme tu, bali pia kwa kuongoza ibada za kuabudu miungu, hali ambayo ilisababisha mfalme kugawana madaraka yake ya kisiasa na wakuu wa mahekalu. Kwa upande mwingine, katika kutunia madaraka ya mahekaluni na pia katika kumudu shughuli za nchi, Farao ambaye kinadharia alikuwa kasisi pekee, askari shujaa pekee hakimu pekee, na mzalishaji mali pekee, aliweza kugawa madaraka yake kwa utawala mzima. Njia mojawapo ya kuwalipa watumishi wake ilikuwa ni kuwapa ardhi, Mapato yaliyotokana na ardhi hii ilikuwa mali yao.

Kwa hakika, safari za kwenda Punt, Baiblosi, Unubi na katika majangwa kutafuta bidhaa za kigeni na mawe, kwa kawaida zilipangwa na mfalme na kuongozwa na viongozi wa serikali. Ujenzi wa mahekalu vile vile ulikuwa wajibu wa serikali, ambapo katika enzi za utawala wa kimwinyi, watu walioishi katika sehemu zilizotekwa kama vile Kush na zilizokuwa chini ya himaya kama Palestina Syria walinyonywa kwa kutoa sehemu ya mali yao moja kwa moja kwa mfalme. Pamoja na mali iliyomilikiwa na mfalme, vilikuwepo pia viwanja vilivyokuwa chini ya miungu, ambao vile vile walimiliki mashamba, makundi ya mifugo, karakana, na kadhalika. Aidha tuseme kuanzia utawala wa Ufalme wa Kumi na Nane na kuendelea, wapiganaji walipewa haki za kumiliki ardhi ambayo iliweza kurithishwa. Viongozi wa ngazi za juu walituzwa ardhi, ambazo walizitunza wenyewe. Hatufahamu namna watu binafsi walivyoweza kujilimbikizia utajiri lakini ni dhahiri kuwa kulikuwa na tabaka la matajiri na ukiachia mbali cheo alichokuwa nacho mtu, na ambacho angeweza kukirithisha kwa watoto wake ilikuwepo vile vile mali ya nyumbani ambayo ingeweza kurithishwa kulingana na matakwa ya mwenye mali hiyo. Yasemekana kuwa mashamba mdogo madogo yalikuwepo hasa katika enzi za Ufalme Mpya, wakati ambapo istilahi "mashamba ya watu fukara" ilitumika kueleza mashamba ya wakuliina makabwela waliokuwa huru, ambao walikuwa tofauti kabisa na wakuliina wapangaji waliokuwa wakifanya kazi katika mashamba ya mfalme au niungu. Watu kutoka nchi za nje waliohamia Misri katika enzi za vita vya ushindi mkuu, japokuwa walikuwa wachache ukiwalinganisha na wenyeji, walikuwa mabingwa wa kazi mbalimbali (kama vile watunza mashamba ya mizabibu wa Kipalestina, wachungaji na waswagaji wa mifugo ya Kilibya) au walowezi wa kijeshi. Watumwa waliochukuliwa na watu binafsi walitumika mara nyingi kama watumishi wa nyumbani tu, na ingawa kuna ushahidi kuwa watumwa walitumika katika shughuli za kawida za kiuchumi, watumwa hawa walikuwa sehemu ndogo sana ya wafanyakazi katika shughuli za kilimo.

Katika miji iliyokuwa na masoko, milki za mfalme, na mahekalu, ustadi katika nyanja maalumu za kiufundi ulikuwa wa hali ya juu. Vyama vya wafanyakazi, vingine vikiwa na mfumo azizi wa utawala, vilimtumikia mfalme, au kuyatumikia mahekalu, ufundi wao ukiwa wa kurithiwa kutoka kwa baba hadi mwana. Vyama hivyo vilijunisha wafanyakazi kama, waoka mikate, wafinyanzi, wapanga mtau, mafundi wa kusubu, wachonga mawe,

mafundi wachoraji, masonora, wateka maji, walinzi wa kila aina, watunza mbwa, wachunga kondoo, wachunga mbuzi, waangalizi wa bata na kadhalika.

Utumishi katika serikali

Mwenendo na mfumo wa uzalishaji mali, nangalizi wa amani na usimamizi wa shughuli zote, ulikuwa ni wajibu wa watumishi wa serikali chini ya mamlaka ya mwana wa Farao. Katika nyakati za mafarakano, waliowajibika na mambo haya ni mtawala wa sehemu inayohusika au viongozi wa mahekalu. Watumishi hawa walijajiriwa kutoka kundi la waandishi, elimu ya kuandika ikiwa ndiyo ufunguo wa maarifa yote na nbinu za ufundi wa hali ya juu. Waandishi hawa, wakiwa wameaminiwa na uongozi wa kidini na wa kiraia walikuwa na mamlaka juu ya shughuli zote za utaalum wa aina mbalimhali. Wataalamu hawa waliweza kuwa wahandisi, mabwana shamba, wahasibu, wajuzi wa ada au hata viongozi wa jeshi na wengine wengi walikuwa na ujuzi wa namna kadhaa kila moja. Mkubwa wao wote aliishi maisha mazuri ya neema katika ulimwengu huu na alitumaiiwa kuishi vivyo hivyo katika uliniwengu ujao. Utajiri wao, akiachilia mbali athari ya mali waliyokuwa nayo, uliwapa uwezo wa kuwa wafadhili.

Historia ya Mafarao yaelekea ilijengeka katika mapambano baina ya maofisa wa ngazi za juu ambao waliendesha mambo yao kaina kundi lenye uhuru na uwcozo wa kurithisha mamlaka yao kutoka kizazi hadi kingine, na mfalme wa nchi, ambaye aling'ang'amia haki ya kudhibiti uteuzi wa viongozi wa nchi. Hivyo Ufalme Mkongwe ulifikia kikomo wakati koo za "machifu wakuu" au wasimamizi, ambao walikuwa na desturi ya kurithisha madaraka walipojitwalia nguvu katika majimbo ya kusini. Katika kipindi cha Kati cha Pili, madaraka ya utawala katika ngazi za juu, yalifanywa kuwa mali ya mtu binafsi ambayo yangeweza kununuliwa au kuuzwa. Ufalme Mpya ulifikia kikomo wakati ukasisi wa Thebes pamoja na uongozi wa jeshi wa kusini walipoungamishwa na kuwa mali ya makasisi wakuu wa Amon.

Utaratibu wa kisiasa

Wazo lililowaridhisha jamii ya Kimisri ni kuwa na mfalme mwenye nguvu ambaye ndiye hasa aliyetoa msukumo uliohitajika katika kuhifadhi hali njema ya jamii hiyo. Mtawala alikuwa kitovu cha shughuli zote za umma. Istilahi "Farao" inatokana na neno "per-ao" ambalo Ufalme Mkongwe ulilitumia kwa maana ya "Nyumba Kuu" ya mwana wa mfalme, ikiwa ni pamoja na makazi yake na mawaziri wake. Katika enzi za Ufalme Mpya neno hili hatimaye lilitumika kwa maana ya mfalme mwenyewe. Huyu mfalme alikuwa tofauti kabisa na binadamu wengine. Mambo yaliyomtofautisha ni kama: ngano zilizoeleza kuteuliwa kwake kabla hajazaliwa, majina yake manne ya kisheria na sifa ambazo alijiongezea katika jina lake binafsi, itifaki iliyokuwa ikimzunguka, nfahari na mazingira yaliyoambatana na kuonekana kwake na pia maamuzi yake, sifa za kumfananisha zilizorudiwa rudiwa bila kikomo, sanamu na michoro yenye kueleza sifa na orodha ya vyeo

mbalimbali vilivyoko katika majengo matakatifu, sherehe zake za kumbukumbu za matukio muhimu, na mtindo wa kaburi lake (kama vile Piramidi ya Memphis, na kaburi lililochongwa katika mwamba lililoko Thebes.)

Kuna maajabu fulani kuhusu kurithishwa kwa ufalme. Ni wazi ilikuwa desturi kwa mtoto wa kiume kumrithi baba yake madaraka ya ufalme, kwa kulingana na mfumo wa masimulizi ya akina Osiris na Horus. Katika Ufalme Mpya, wadhifa au kutambuliwa kwa mfalme mpya, kwa nguvu za ubashiri wa Amon ilikuwa ndiyo thibitisho la uhalali wa mtawala huyo. Kwa namna hii, "haki ya moja kwa moja. kuhusu utawala kutoka kwa miungu", ilikuwa muhimu zaidi kuliko haki ya kuzaliwa katika ukoo wa kifalme.

Wanawake wanne walipata kuwa Mafarao. Ajabu yenyewe, wawili wa kwanza (Nitokris na Sebeknefru) walikuwa watawala wa mwisho katika Ufalme. Wawili wengine (Hatshepsut na Tauosre) walihesabiwa kama wanyang'anyi wa madaraka ya vizazi vilivyofuata. Heshima nyingi walinimumiwa mabinti mfalme katika kipindi cha Ufalme wa Kati, na hasa baadaye. Teye, mke wa kwanza wa Emeuhotep III, na Nefertari mke wa kwanza wa Ramses II, walipewa heshima za pekee. Ahnuotep akiwa chini ya mamlaka ya Amasis, au Ahmosis-Nefertari aliyekuwa chini ya mamlaka ya Amenhotep I yaelekea walikuwa na uwezo mkubwa wa kuathiri masuala ya kisiasa na kidini. Kuhusishwa kwa shughuli za ada za "mke wa Amon mwenye nguvu za kimungu" na mabinti wa wafalme au malkia, kunaonyesha dhima maarufu ya wanawake katika ibada ya mungu.


Uchunguzi wa orodha za vyeo vya viongozi wa ngazi za juu na chini, pamoja na matini chache za kisheria na uongozi ambavyo tumevipata, hutupatia picha ya karibu zaidi ya hali halisi ya taratibu za serikali. Taratibu hizi huhusu serikali za majimbo, ngazo za uongozi katika jumuiya ya makasisi na mgawanyo wa majukumu ya kidini kwa makasisi hao; uendeshaji wa ardhi inayomikiwa mifungo machimbo ya madini, maghala ya vyakula, usafiri katika mito, sheria, na kadhalika na wafalme au makasisi.

Katika kilele cha mfumo wa uongozi alikuwapo "tjaty" au "waziri" tukitumia istilahi ya kimapokeo ya wanataaluma ya Misri. Waziri Mkuu huyu alikuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa amani ilikuwapo na zaidi ya yote alikuwa na mamlaka ya juu ya kisheria katika nchi, akiwafuata tu Farao na Waziri wa Sheria. Hata hivyo "tjaty" huyu (katika cnzi za Ufalme Mpya walikuwa wawili) hakuwa mshauri pekee wala mshauri mkuu wa mfalme. Waliheshimiwa wengi walijivunia kuombwa ushauri na mkuu wa nchi kwa siri, wakiwa wamechaguliwa kufanya kazi maalum. Na katika cnzi za Umwinyi, Gavana wa Unubi aliyetumkiwa heshima ya kuwa "mtoto wa mfalme" aliwajibika moja kwa moja kwa Farao, na katika nchi yake alikuwa na mamlaka makubwa mno. Baadli ya watu waliotokea kuwa inashuhuri ni kama Amehotep, mwandishi wa watu waliokuwa wakiandikishwa kwa shughuli mbalimbali na mwana wa Hapi. Alikuwa msanifu majenzi ambaye alipandishwa cheo hatua kwa hatua hadi kuwa sawa na niungu kwa sababu ya hekima yake. Mwingine ni Khamois, kasisi mkuu wa Ptah, na mjawapo wa watoto wengi wa Ramses II. Kwa hakika watu hawa walikuwa na madaraka sawa na inawaziri wakuu wa enzi zao.

Taratibu za kijeshi

Mfalme aliwajibika kulinda usalama wa taifa. Kinadharia, sifa zote za ushindi zilimwendea mfalme. Ramses II alitumia propaganda kwa wiingi katika maneno na sanamu, kueleza jinsi alivyosimama peke yake akiwa na mlinzi wake huko Kadash ili kuthibitisha uwezo mkuu aliokuwa nao mfalme, ambaye pia ni mwokozi pekee kwa neema za miungu. Vile vile Ramses II alitumia propaganda hizo kuonyesha jinsi alivyokuwa na madaraka yenye kauli ya mwisho juu ya jeshi ambalo ndilo lilikuwa chimbuko la Ufalme wake. Hata mapema zaidi, muamano nyakati za ujenzi wa Piramidi nchi ilikuwa na utawala wa ngazi za juu wa kijeshi uliokuwa na ufundi maalumu, ikiwa na jeshi la nchi kavu na jeshi la majini; kwa wakati mmoja. Utawala huo ulikuwa ukiyaamini majeshi hayo ambayo yalikuwa na uzoefu wa mbimu za kivita, na yaliyoweza kujipanga kufuatana na vyeo kwa nidhamu. Katika elfia ya tatu watu wa nchi jirani hawakuwa tishio kubwa kwa Misri. Makundi ya wavamizi yalisababisha kupungua sana kwa watu wa Unubi, kwa manufaa ya Misri. Mashambulizi yaliyowafanya watu wa vijijini watozwe kodi kubwa bila huruma yalitoshia kuwatia hofu na kuwanyan'ganya nali wakulima walioishi kwenye mipaka ya Libya na Asia. Wakati huo huo "wapelelezi wa jangwani" walichunguza kwa makini mienendo ya Mabedui wenye tamaa. Tunachojua zaidi kuhusu majeshi ya Memphis, ni kujihusisha kwao katika shughuli za kiuchumi na nupango nukubwa ya ujenzi. Vikundi malususi vya askari-wanafunzi vijana vilitumika kama vikundi vya walinzi wa mfalme. Walisimamia vile vile uchukuzi wa mawe kwa ajili ya ujenzi wa piramidi na shughuli nyingine kubwa katika machimbo ya madini ya Sinai, au katika machimbo ya mashariki. Kindi maalum cha askari wa muda kilichoitwa *sementi*, kilitafuta na kuchimba dhahabu katika machimbo ya dhahabu ya Unubi na katika jangwa. Katika kipindi cha Kati cha Mwanzo kugawanyika kwa ufalme katika majunbo yaliyoshindana, kulisababisha muundo mpya katika majeshi. Wafnasi binafsi wa mwana wa mfalme, na vikundi vya askari kutoka katika majunbo, viliunganishwa na majeshi mengine ili kuyaimarisha zaidi.

Katika enzi za Ufalme Mpya kulipokuwapo na misukosuko mikubwa ya kinataifa, kulitokea upanuzi wa majeshi kwa kiwango ambacho kilikuwa hakijashuhudiwa. Majeshi haya yaligawanyika katika sehemu mbili; askari wa magari ya farasi na askari wa miguu. Sehemu hizi nazo pia ziligawanywa katika vikosi mbalimbali. Askari walipewa misaada midogo midogo ya ardhi; na katika utawala wa Ramses, mateka wengi wa Kiuubi, Kisiria Kilibya, na maharamia wa Baharini, waliingizwa katika majeshi, na kupewa misaada kama hiyo pia. Licha ya kuingizwa katika utamaduni wa Kimisri haraka haraka, Walibya walijiundia kundi lililokuwa na uhuru wao wenyewe, na hatimaye kumfanya mtawala wao kuwa Farao. Katika aina mpya ya himaya Wafalme wa Saite, walilazimika kutegemea wanajeshi wa kilowezi walioajiriwa kutoka kwa Waioni, Wakaria, Wafoeniki na Wayahudi. Katika vitu vya mwisho dhidi ya himaya ya Kiajemi, Mafarao, kama maadui zao, walikodi askari wa Kiyunani ambao walipatikana kutokana na wasafiri waolikuwa wakizunguka huku na huku.



3.3 Kujaza maghala ya nafaka (A Budawy, Los Angeles, 1966)

Dhana za kidini na uadilifu

Ngano

Kwa hakika, mojawapo ya mafanikio makubwa ya ustaarabu wa Kifarao, na labda mojawapo ya udhaifu wake pia, ulikuwa ni mtazamo wa kifahari kuhusu ulimwengu, na nguvu zinazoutawala. Huo ulikuwa mtazamo wa busara uliojitokeza katika ngano, ada, sanaa, lugha, na matendo ya busara. Katika kufahamu nguvu za asili na maunbo mengine ya kiasili, ngano zilikubaliana na mitazamo, taswira, na hadithi za kishujaa kama zilivyotolewa kutokana na napokeo. Baadhi ya ngano ni kama: uwezekano wa kuwapo miungu kadhaa wa pekee, anga ni dari ya majimaji tumbo la ng'ombe jike, mwili wa mwanamke, nguruwe dume, na kadhalika. Kwa na namna hii zilikuwa dhana kadhaa kuhusu chanzo cha ulimwengu ambazo zilijunilishwa pamoja kwa namna mbalimbali na kutoa usanisi mkubwa, Usanisi huu ulielezwa katika misingi ya kienyeji miaka nenda miaka rudi. Kila usanisi uliigizwa tena na tena kwa usafi wake huo huo katika maonyesho ya ada fulani ulikotoa mapana na marefu ya kilimwengu.

Ufalme wenye sifa za kimungu ulitawala dunia hii. Siku hizo, Seth alimwua Osiris. Baada ya kupata uhai tena kutokana na matendo ya Isis na Anubis mkausha maiti, Osiris ahibakia kuwa mfano azizi wa wafalme wote waliokufa, na pia mfano azizi wa wafu wote. Yeye pia ni taswira ya jua linalokufa kila jioni, na majimaji yaliyotiririka kutoka mwilini mwake, yaliaminiwa kuwa ndiyo maji yajaayo kila mwaka.

Baadhi ya mambo yaliyowiana na taratibu za kimungu ni muundo na inwendo wa ulimwengu yakini, na pia taratibu za uadilifu -Ma'at- ambao ndio kanuni ya ukweli ua haki inayojitokeza Ra anapowashinda maadui zake. Aidha taratibu hizi zapaswa kutawala katika shughuli za taasisi na tabia ya mtu binafsi. Kwa ajili ya furaha ya binadamu wote Ra mwenyewe hnishi kwa Ma'at. Thoth, mungu wa wasoni ambaye pia ni Mhasibu wa Ra na hakimu wa miungu naye hufurahi kwa Ma'at.

Minugu

Imani na taswira zote tulizozitaja, zinakubaliwa katika mahekalu yote. Nyimbo zilizoimbwa kusifu sifa za ulimwengu na majaliwa ya kustaajabisha na mungu-muunba, hutoa dhamira hiyohiyo ikiwa zinamhusu mungu wa kike wa kwanza Neith, au mungu wa dunia kama Ptah. Ngano kubwa kama zinazosimulia juhudi ya roho ya Osiris pamoja na ada za msingi, zilikuwa sawasawa katika makazi yote ya watu. Lakini miungu mbalimbali kila mmoja akiwa na jina lake, taswira za jadi, maurubo ya wanyama na miungu anaposhirikiana nao walikuwa "watawala" wa miji mbali mbali: Khnum katika Elephantine, Isna na mahali pengine; Min katika Coptos na Akhmin; Mont katika Hermonthis; Amon katika Thebes; Sebek katika Fayyum na mahali pengine; Ptah-Seker katika Memphis; Ra-Harakhte-Atun katika Heliopolis, Neith katika Sais, Bast katika Bubastis, Uadjit katika But, Nekhbet katika El Kah, na kadhalika. Aidha, kulikuwa na miungu wengi wa kienyeji waliojulikana kwa jina la Horus. Walikuwapo pia Miungu

wengi wa kike walioogofya kama vile Sekhments, au wenye huruma mithili ya Hathors. Dini ilielekea kupunguza idadi ya miungu kutoka katika wingi kwa kuhusisha miungu fulani fulani na niungu wengine hadi kufikia aina chache tu: mungu mkuu, kwa kawida mungu-jua, anihaye mara nyingi alihusishwa wazi wazi na Ra, (Amon-Ra, Horocris-Ra) alikuwa na mungu mwenziwe wa kike aliyejulikana kwa majina mbalimbali (Mut=Bast=Sekhmet=Hathor). Kilichofadhaisha kuhusu matatizo ya kinadharia yaliyotokana na maumbo mengi ya mungu ni uzushi wake wa udadisi wa kidini na wa kifalsafa. Msimamo wa Akhenaton ambaye alitambua tufe la jua linaloonekana kuwa ndiye mungu pekee wa kweli, ulikuwa bado ndicho kiini kikubwa cha maono ya Wamisri. Hata hivyo msimamo huo ulifarakana na mafundisho rasmi kwani ulivuruga desturi za kimila, anabazo zilizingatia kuwepo kwa mafumbo ya mambo yasiyocleweka kirahisi, na pia kukubali na kuafiki namna zote za utawa na fikra.

Hekalu

Kila mungu aliumba mji wake, na kuwa na utawala wake pake yake. Vile vile nchi yote ya Misri ilikuwa chini ya mamlaka ya miungu hao. Mfalme alijihusisha na miungu wote kwa pamoja. Ili kufanikisha shughuli hii, sayansi takatifu ilitumia mbinu za uchawi wa maneno na ishara, maandishi na sanamu na maumbo mbalimbali ya ujenzi. Shughuli zote zilitumika kuhakikisha kuwepo kwa maisha ya baadaye kwa mtu aliyekufa. Shughuli za kawaida zilizoendeshwa na makasisi wapya, ziliambatana na ada za kidini kwa kutumia kanuni mahsusi za maneno, hivyo wakikiza uwezo wao wa kulazimisha kwa kutumia ulozi wenye kukumbusha matukio yaliyotangulia. Ufafanuzi wa kanuni hizi za ibada, na uandikaji wa matini hizo katika kuta za mahekalu vilidumisha uwezo wao wa kutenda. Msanii majenzi alitengeneza hekalu tufano wa ulimwengu na hivyo kuipatia hali ya kitu kilichonuiwa kudumu milele. Lengo la hekalu lilikuwa mlima wenye jua linalopambazuka, sehemu ya ndani yenye giza ilikuwa mahali linapolala jua; minara iliwakilisha bwawa la kwanza ambalo ndani yake kulitokea viumbe vyote, ua misingi ya kuta zake iliwakilisha ardhi ya Misri. Ukuta mrefu wa matofali ulilitenga hekalu na bustani zake, pamoja na majengo mengine ya kudumu ili kuviweka mbali na uchafu ambao ungetia dosari katika mambo ya kimungu. Makasisi wenye kuendesha ibada na watu wengine waliotunukiwa fursa ya kuingia madhabahuni, waliwajibika kufanya ibada za kujitakasa, na kufuata masharti yanayohusu chakula, mavazi, na vitendo vya kutwaana kati ya mume na mke. Ili kuonyesha kuwa shughuli za ibada zinaendeshwa hasa na Farao, zilikuwepo sanamu katika kuta zikimwonyesha akifanya ibada mbalimbali, na akiwakilisha majimbo ya Misri katika mlolongo mrefu. Aidha, sanamu hizo zilionyesha hatua mbalimbali za mafuriko, na niungu wadogo wakisimamia shughuli mbalimbali za kiuchumi katika maisha. Katika kipindi chote cha siku nzima, sanamu ya kuabudiwa, au kitu chochote kilichotumika katika mawasiliano na mungu, kilitakaswa na kupewa fahamu, kilivishwa mavazi, kulishwa chakula na kaimbiwa nyimbo ndefu. Nyimbo hizi zilikuwa na shabaha ya kumsihi mungu aziuduke, kumhakikishia uwezo wake wa kimungu, na kumshawishi afanye ukarimu. Katika sherehe kubwa kubwa, mungu hutokca katika maandamano ili kupata nguvu mpya

za kimungu kutokana na mionzi ya jua, kuzuru makaburi ya wafalme na miungu waliopita, na kuamuru tena matukio yaliyo katika ngano, ambayo kwayo ulimwengu ulipata sura yake.

Sheria


Kama tulivyoona dini na maadili husisitiza kuwapo kwa nidhainu ya hali ya juu, kwa manufaa ya watu wote katika jumuiya, yaani ya watawaliwa na kwa shughuli pekee za mfalme katika kuendesha ada za kiserikali. Hivyo inazidi kustaajibisha namna sheria za Farao zilivyokusudiwa kubakia na ubinafsi. Kulingana na maamuzi ya mfalme na taratibu za kisheria na adhabu yaelekea watu wote, waume kwa wake wa tabaka zote, walikuwa sawa mbele ya sheria. Familia iliyotambuliwa ilikuwa ya baba, mama na watoto wao wadogo. Wanawake walikuwa na haki sawa katika kumiliki mali, na katika kupatiwa msaada wa kisheria. Kwa kawaida, uwajibikaji ulikuwa wa mtu binafsi tu. Uhisano wa karibu kati ya familia na ndugu wengi haukuwa ukitambuliwa kisheria. Hadhi ya mtu haikuwa na uhusiano wowote na ukoo wake.

Katika utawala wa kisheria, Misri ya enzi za Mafarao, ilikuwa tofauti kabisa na utawala wa asili wa Kiafrika na ajabu, ulikaribiana sana na hali ya maisha katika jamii za kisasa za Ulaya.

Imani na desturi za mazishi

Hali ile ile ya upekee yenye ubinafsi iliendelea kutawala imani na ada zinazohusu maisha baada ya kifo. Kila mtu kulingana na uwezo wake, alijiandalia maisha yake baada ya kufa, na aliwajibika pia kuwafanyia hivyo hivyo mke wake na watoto endapo watakufa kabla ya kufanya shughuli hizo zenye. Mtoto wa kiume hana budi kushiriki katika shughuli zote za mazishi ya baba yake, na ikilazimu hata kuhakikisha kuwa anazikwa. Binadamu pamoja na kuwa na mwili unaokufa na kuoza, pia ana michanganyiko mingine - mathalani Ka, Ba, na nyingine zaidi ambayo haijulikani sana - ambayo maunbo yake layaelezeki kwa urahisi na uhusiano baina yake si dhahiri kufahamika. Ada za maziko zinakusudiwa kuhakikisha kusalimika kwa "roho hizi" lakini, sifa moja inayojulikana sana kuhusu diini ya Wamisri, ni kuhusisha salama ya roho hizo na hifadhi ya mwili wa marehemu kwa njia ya kuukausha kwa madawa. Aidha ilitakiwa kufanyika mipango mahsus, ili watu waliofariki wapate neema katika maisha yao ya baadaye angalau kufikia kiwango alichokuwa akimudu mtu katika maisha yote katika ulimwengu huu tuujnao. Kaburi lina sehemu wazi kwa ajili ya ndugu wa marehemu waliobakia, na mwanandani ambamo hulazwa maiti ukiwa na vifaa vya uchawi au vya nyumbani. Matajiri walilipa ada kila mara kwa makasisi wa maandamano ambao waliwajibika kuleta sadaka za chakula, kama tahadhari ya mwisho walitumia vitisho mbalimbali kama vile uchawi na ushirikina kem kem, zikiwamo sanamu za kuchongwa au zilizochorwa. Ada za msingi za kufunga au kuzuia, pamoja na kafara, vilifanywa kuwa vya milele, katika kaburi la ndani kwa ndani lililokuwa katika hekalu dogo. Sanamu nyingine za matukio, ziliumbwa upya, iufumo wa kazi na starehe za ulimwengu bora. Sanamu kubwa na ndogo ziliunda viwukilishi vingi sana vya miili ya

watu. Kwenye mbao za sanduku la kuzikia, na katika mawe ya mwanandani, na pia katika "Kitabu cha Wafu" kilichotolewa ili mwili uliokaushwa kwa dawa ukitunze, palinakiliwa kanuni mahususi zilizotamkwa wakati wa mazishi, na manuizo ya uchawi ya kumwezesha marehemu kutumia vipaji vyake vyote, kuepuka hatari za Ulimwengu Mwingine, na kutimiza majukumu yake ya kimungu.



Uhusiano wa misri na sehemu nyingine za Afrika

Hivi sasa imekubaliwa na wengi kwamba utafiti wa kiakioloji haujaonyesha ushahidi wa kutosha kuhusu mawasiliano kati ya Misri na sehemu nyingine za Afrika kusini mwa Meroe. Miaka inichache iliyopita watu walikuwa wakizungumzia kugunduliwa kwa vifaa na zana za Kimisri katika sehemu za mbali katikati mwa bara kijisanamu kidogo cha Osiris ambacho ni cha karne saba kabla ya enzi zetu, kilipatikana huko Zaire kando ya mto Lualaba karibu na ndagano ya mto Kalme-ngongo. Aidha, sanamu iliyoandikwa majina na sifa za Thutmose III (-1490 hadi -1468) ilipatikana kusini mwa mto Zambezi. Hata hivyo uhakiki wa hali ambano vitu hivi viligunduliwa, hufanya isiwezakane kuvitumia wakati huu kufikia hitimisho kwamba vinaonyesha kuwapo kwa uhusiano kati ya Misri na sehemu zilizotajwa katika karne ya Saba, au ya kuni na tano kabla ya enzi zetu. A. Arkell alifikia hitimisho hilo kutokana ushahidi ambao hauaminiki sana, kwamba kulikuwepo mahusiano baina ya Misri ya Utawala wa Kiruini na nchi ambayo leo inajulikana kwa jina la Ghana.

Hata hivyo hoja hii isitufanye tufikie uamuzi kwamba hapakuwepo na uhusiano wowote baina ya Misri na sehemu nyingine za Afrika hapo zamani sana.

Kwa mfano wapo watu wanaofikiri kwamba ustaarabu wa Misri umeathiri mambo fulami katika ustaarabu wa nchi nyingine za Kiafrika. Eva Meyerowitz anachukulia matumizi ya tai na Waakan kama ishara ya kuyumba kwao kuwa uthibitisho wa athari za Kimisri. Anasisitiza pia kuwapo uhusiano kati ya mungu Ptah na mungu wa Wa-Akan Odemankoma. Miungu hao wote wana maumbile ya kike na kiume na kwamba walijiumba wenyewe kwanza ndipo wakaumbwa ulimwengu kwa mikono yao. Ingawa uhusiano huu ni wa kuvutia lakini bado haujapatikana ushahidi wa kutosha kuthibitisha kuwapo kwa mahusiano kati ya Misri ya kale, kwa upande munoja, na Akan ya kale au eneo la Ghuba ya Benin kwa upande mwingine.

Kwa namna hiyo, imani katika nyoka ambayo imejitokeza katika uchunguzi uliofanywa na wataalamu mashuhuri juu ya ustaarabu wa Kiafrika kwa jumla ilifikiriwa toka kale kwamba huenda ina asili ya Kimisri. Lakini oni hili linabatilisha ukweli kwamba tamaduni za kale zilitukuzwa kwa makini hali ya inazingira yao, na ziliweza kuunda imani zao kutokana na utukufu huo.

Majirani wa Magharibi: Wasahara na Walibya

Inakubalika kwa jumla kwamba katika kipindi kabla ya ufalme mabadilishano ya mara kwa mara kati ya watu wa Misri na watu wa Sahara yalipungua. Kuna habari kidogo sana kuhusu mabadilishano haya, na mara nyingine hudaiwa kwamba hayakuwepo kabisa. Katika kipindi cha Ufalme ni dhahiri kwamba Misri ilikuwa na athari kubwa sana huko Sahara japokuwa hapa napo hakuna ushahidi wa kutosha kuthibitisha jambo hili.

Kwa hakika kulingana na utafiti wa siku za karibuni, kwa Wamisri watu wa Sahara wakati wa kipindi cha ufalme walikuwa hasa Walibya waliojikusanya polepole kaskazini inwa jangwa mojawapo duniani, lenye ukubwa wa ajabu, na ambalo halikuweza kukalika. Hali ikiwa tofauti na hali katika enzi za Neolithiki wakati ambapo kuenea kwa haraka kwa jangwa kulikozidi katika kipindi cha ufalme kuliwalazimisha Walibya, wachunga kondoo na wawindaji kurejea katika makazi yao ya awali, au kuwafanya waende kwenye maeneo ya neena ya Wanailotiki kutafuta chakula ili wasife njaa. Wanailotiki nao waliamua kujiharaji dhidi ya watu hawa. Majaribio yao yaliendelea bila kusita, lakini hayakuleta mafanikio yoyote ya ushindi, isipokuwa labda katika sehemu za magharibi ya Delta, ambayo Wasahara walikuwa wameikalia toka zamani sana, na watu wake walikuwa wa namna moja. Mabwanyenye wa Kimisri waliwinda katika maeneo ya maoasisi makubwa yaliyozungukwa na jangwa kama vile Kharigali, Dakhilali, Farafirah, na Siwah. Ilikuwa lazima kuvuka maoasisi haya kabla ya kwenda kusini kuelekea Chad, au kaskazini kuelekea Fezzan na Niger. Hata hivyo, hadi leo hii hakuna uthibitisho kwamba njia hizi zilitumika mara kwa mara katika kipindi cha Ufalme.

Utafiti wa njia hizi hauna budi kufanywa hata bila kutilia maanani hali zake nyingi zenye kuvutia. Akiolojia na toponomia vinapaswa kufanya izezekane kujua kama kweli Wamisri walitumia njia hizi muhimu za Kiafrika kwenda Tibesti, Darfur, Bahr el Ghazal na Chad au kwenda Fezzan na Ghudamis; au la.

Kwa vyovyote vile, hasa kuanzia enzi za Ufalme wa Kumi na Tisa na kuendelea, Walibya walikuwa kama akiba ya wafanyakazi na askari nchini Misri. Mateka wa Kilibya, waliokuwa wakitambulika kutokana na manyoya ya ndege waliyoyayaa kichwani, walikuwa inaaskari hodari, hasa wale waendeshao magari ya farasi. Waliingizwa jeshini ambamo idadi yao iliongezeka kila karne zilivyokuwa zikipita. Kama wafugaji wa ng'ombe Walibya ndio waliotoa wanyama hawa nchini Misri. Wamisri waliwapata kutoka kwao kama ushuru, au kwa kunyanganya wakati wa mashambulizi. Hivyo umuhimu wa Walibya kiuchumi unaweza kuliganishwa na ule wa Wanubi.

Katika karne ya kumi na tatu na kumi na mbili kabla ya enzi zetu, Walibya, kutokana na hali zilizowakumba, walilazimika kujipenyeza nchini Misri. Seti I na Ramses II walijenga ngome dhidi ya Walibya na kuwateka baadhi yao waliokuwa wajasiri zaidi. Baada ya majaribio mawili ya kutaka kuzirudia sehemu za magharibi ya Delta walipokuwa wamekwishafukuzwa kushindwa katika karne ya kumi na mbili kabla ya enzi zetu, Walibya waliruhusiwa kuishi katika sehemu hizo na Ramses III. Kwa upande wao, Walibya hawa walishiriki kwa kiasi kikubwa katika shughuli za kijeshi za kulinda Misri, ili kulipa ukarimu wa wenyeji wao.

Katika karne ya kumi, ua kwa karibu karne mbili zilizofuatia, Walibya waliitawala Misri chini ya utawala wa ufalme wa ishirini na mbili ua ishirini na tatu. Hali hii mpya ya mambo ilizusha mrejesho mkali kutoka Misri ya Juu, ambako kulifanyika majaribio ya kutaka kuwaondoa Walibya kwa ushirikiano wa Ufalme wa Napata.

Wakati wa kuutafakari uhusiano kati ya Misri na mataifa mengine, yawe ya Kiafrika au menginyo, mchongo wa Delta, ambao inpaka hivi sasa habari zake bado hazijajulikana barabara, usisahauliwe.

Majirani wa Kusini

Kwa vile Misri ni taifa la Kiafrika, yawezekana watu wake walishawishika kujipenyeza ndani kabisa mwa sehemu za bara kwa kuufuata mto Nili, angalau kufikia Poromoko la Nne. Yawezekana walishawishika pia kwenda Chad wakipita katika mabonde ya kale yaliyoelekea katika ukingo wa kushoto wa mto Nili, na huko Ethiopia ambako kulikuwa na utajiri mkuhwa wa pembe za ndovu. Katika kuelekea kusini, labda pingamizi kubwa lingekuwa ni mabwawa makubwa yaliyoenea sehemu nyingi, ambayo yangewashinda Wamisri kuvuka au kufikia. Mabwawa haya, tangu nyakati za kale sana yalikuwa kinga madhubuti ya siri za mabonde ya juu ya mto Nili.


Ingawa leo tunaweza kufuatia kirahisi historia ya mahusiano kati ya Misri na majirani zake wa kaskazini, na pia ile misafara ya wapagazi kati ya Bahari ya Sham na mto Nili, hakuna data ya utafiti wa akiolojia juu ya uhusiano baina ya Misri ya kale na sehemu za kusini. Hali hii ni ya kusikitisha.

Tangu wakati wa utawala wa ufalme wa kwanza, Misri ilikuwa imekwishajenga ngome kadhaa ili kuhani mipaka yake ya kusini. Na katika kipindi kirefu historia yao nchi zilizoko kaskazini mwa Poromoko la kwa kwanza na zile zilizoko kusini mwa Poromoko la nne zilitengwa na tofauti za kisiasa na za kitamaduni pamoja na maslahi yaliyopingana. Hata hivyo, uhusiano huu uliokuwa changamano na wenye tofauti nyingi kati ya Wamisri na majirani zao wa kusini waliowaita Nehesi, haukukatizwa kabisa kabisa.


Kwa vyovyote vile, Wamisri walivutiwa sana na Nubia ya Chini kwa sababu ya dhahabu iliyokuwa ikipatikana hako. Walivutiwa pia na maeneo ya Wanailotiki yaliyokuwa kusini zaidi kwa sababu ya njia zierendazo ndani kabisa mwa Bara la Afrika kupitia Nili Nyeupe, mabonde ya Sahara, au Darfur. Katika kipindi chote cha historia ya Misri, nchi hii ilijishughulisha sana kupata njia ya kuwafikisha kusini. Labda sababu hii pia inaweza kueleza kwa nini ilikuwa ni muhimu kwa Misri kuzidhibiti oasisi za magharibi, ambako ilipitia njia nyingine iliyokuwa sambamba na Mto Nili.

Tangu mwanzo wa Ufalame Mkongwe Sudan kama ilivyokuwa Libya, nayo ilikuwa ikihesabiwa na Misri kuwa ni sehemu ya kujipatia wafanyakazi, mifugo na madini. Wanubi nao ambao walikuwa na sifa za kutupa mishale, walikuwa na nafasi muhimu katika jeshi la Misri.

Wamisri walianza kuandaa mawasiliano yao na nchi ya Sudan mnamo mwisho wa utawala wa Ufalme wa Tano. Katika kipindi hicho hicho kulianzishwa chao cha kisiasa



4.1 Hongo ya wafungwa wa Kilbya wa Himaya ya Kale (W. Smith, 1965)



na kiuchumi cha Gavana wa Kusini. Aliyekuwa na cheo hicho, aliwajibika kulinda lango la kusini la Misri, kupanga na kuongoza shughuli za kibiashara, na kuhudumia misafara ya wafanya biashara. Unas, aliyekuwa Gavana wa Kusini katika enzi za utawala wa Ufalme wa Sita, alikuwa na mamlaka ya kuwaamrisha askari-wanafuuzi kutoka sehemu mbalimbali za Unubi: mathalan, Nehesi (Wanubi) kutoka nchi ya Irhtet, Madja, Yam, Wawat na Kau.

Mwishoni mwa Ufalme Mkongwe uhusiano wa kibiashara kati ya Misri na Sudani ulivurugika. Hata hivyo, mwana wa mfalme wa Edfu, anaeleza kwenye ukuta wa kaburi lake huko Mealla kwamba nafaka zilipelekwa Wawat kwa madhumuni ya kuepusha baa la njaa. Huu ni ushahidi wa kuonyesha kwamba uhusiano kati ya Misri na Unubi ulikuwa ukiendelea katika nyakati hizo. Zaidi ya hayo askari wa Kinubi, walifanya kazi kubwa katika vita huko Misri ya Kati wakati wa Kipindi cha Kati cha Mwanzo. Kuna sanamu za mbao zilizopakwa rangi zionyesha kombania ya watupa mishale arubaini wa Kinubi, ambazo zinaonyesha umuhimu ambao askari hawa wa kisudani walikuwa nao kwa Wamisri.

Mwanzoni mwa enzi za Ufalme wa Kati yaelekea Wafalme wa Misri waliomba msaada kutoka kwa wananchi wa Sudani wakati walipokuwa wakitishwa na mabedui wa Kiasia. Jambo hili laelekea kuthibitisha kwamba uhusiano kati ya Misri na Sudan, ambao ulikuwa umevurugika wakati wa Kipindi cha Kati cha Mwanzo ulikuwa uncanzishwa tena. Kwa vyovyote vile, yamkini baadhi ya Wamisri walivuka mpaka na kuingia Sudan. Kutokana na jiwe la kaburi lililopatikana huko Buhen, tunajua kwamba familia kadhaa za Kimisri ziliishi Unubi kwa muda mrefu wakati wa enzi za Ufalme wa Kati. Watu hao walikuwa na majina ya Kimisri na waliabudu miungu ya kienyeji. Wafalme wa nyakati hizo walijenga ngome kumi na rue katika Nubia ili kuhamu nupaka yao na misafara yao ya kibiashara.

Wahyksos walipozikamata sehemu za kaskazini na za kati ya nchi ya Misri, nchi ya Kush ilijipatia uhuru zaidi na nguvu zaidi; na Ufalme wa Kush ulikuwa ni tishio kwa Mafarao.

Maandishi ya Kimisri yanaelezea kuwa wakati wa vita vya kuwaondoa Wahyksos madarakani, Komese, Farao wa inwisho katika Ufalme wa Kumi na Saba, alijulishwa habari za kukamatwa kwa injumbe wa mfalme wa Wahyksos ambaye alikuwa ametumwa kupeleka ujumbe wa mfalme wa Kush wenye madhumuni ya kumwomba huyo mfalme wa Kush amsaidie mfalme inwenzake katika kupigana na Wamisri. Katika enzi za utawala wa Ufalme wa Kumi na Nane, Sudan ilijikuta imezongwa tena, na uhusiano ukaongezeka kwa kiwango kikubwa ambacho kilikuwa hakijapata kufikiwa hapo kabla. Wakati huo huo uhusiano kati ya wakazi wa maeneo ya Maporomoko ya Pili na Maporomoko ya Nne, ulipata nguvu mpya. Wakati wa utawala wa Thutmose III, muundo ya makaburi katika maeneo haya ilibadilika. Makaburi yenye muundo wa Kimisri yaliengwa na mapiramudi madogo mfano wa yale yaliyoko Deir al Medina yaliengwa pia. Hii ndiyo iliifanya nji ya Buhen na Aniba kufanana na miji ya Kimisri. Vile vile vito vyenye umbo la indudu kama mende vilipatikana kauka makaburi huko Sudan. Majina na niichoro katika makaburi ya wana wa wafalme yalichorwa kama walivyofanya Wamisri. Kaburi la Heka-Nefer,

khamun, mwana wa mfalme wa Aniba wakati wa utawala wa Tutan limejengwa kama yale makaburi ya kuchonga katika miamba yapatikanayo Misri.

Kabla ya hapo, Nubia na Misri zilikuwa hazijapata kuwa na uhusiano wa karibu zaidi kama huo. Katika mwaka -1400, hekalu la Soleb lilijengwa. Watu wa Sudan walishiriki kwa kiasi kikubwa zaidi, kuliko hapo awali, katika shughuli za kijeshi na za kitawala huko Misri; na hayo yakafikia kilele wakati ufalme wa Ethiopia ulipoitawala Misri. Hata hivyo ingawa wakazi wa mabonde ya juu waliingizwa katika ustaarabu na utamaduni wa Kimisri, lakini hawakubadilika kuwa Wamisri. Mpaka wakati wa Ufalme wa Thelathini, utamaduni wa namna yake uliendelea kujionyesha japo ulikaribiana na ule wa Kimisri. Utamaduni huo uliirejeshea Misri hadhi ya Uafrika, ambayo imetajwa katika Biblia mara mbili: mara ya kwanza ni wakati Bwana Mungu anapowalinda Wayaludi kutokana na washambulizi ya Waassiria, kwa kumjia mfalme wao katika ndoto iliyomtia hofu kwamba mfalme wa Ethiopia Tir-hakani anataka kumdhuru. Pili, ni wakati mfalme wa Wayaludi, Hezekiali alipotaka kushirikiana na Farao na watu wake.

Kutekwa kwa Thebes na Waassiria kulitokea wakati mmoja na kuibuka kwa himaya ya Wameroe kusini. Hii ilifanya ulinzi wa sehemu hii dhidi ya mashambulizi toka kaskazini, kuwa wa lazima kabisa, kwa kuwa tokea wakati huo majeshi ya Misri yalikuwa na vikosi vikubwa vya mamlaki wa Kiyaludi, Kifoeniki na wa Kiyunani. Kutokana na kutokuwepo kwa utafiti, ambao yalazimu ufanyike hakuna habari nyingi zinazojulikana kuhusu uhusiano ambao bila ya shaka ulikuwa na matatizo kati ya dola mpya ya Kinailoti na Misri.


Punt

Kama ilivyo kuhusu matatizo mengine juu ya historia ya Afrika, yameandikwa inambo ambayo mengi hayana ukweli unaonyesha mahali ilipokuwapo nchi yenye kubuniwa ya Punt iliyokuwa na ulusiano na Misri, hasa katika enzi za Ufalme Mpya, na ambayo inaonyeshwa katika taswira zilizoko Deir al Bahri. Juludi zimefanywa za kuonyesha mahali nchi hii ilipokuwa, na hivi leo yakubalika kwamba Punt ilikuwa katika Pembe ya Afrika, ingawa bado kuna utatanishi kuhusu mipaka yake halisi. Nadharia mojawapo inayoelekea kuwa kweli, inadai kuwa nchi ya Punt, ilikuwa katika pwani ya Kiafrika inayoanzia kwenye mto Poitialeh katika Somalia ya kaskazini, hadi kufikia Ras Guardafui. Eneo hilo lina milima yenye mashamba ya ngaro yanayofanana na yale yaliyoko Deir al Bahri. Miti mingi, ikiwa ni pamoja na ile itoayo ubani, udi na mafuta ya dawa, huota katika ngaro hizi.

Yaelekea makubaliano yamekwishafikiwa kwamba vyombo vya baharini vya Kimisri vilisafiri kwenda Punt kutafuta ubani wenye thamani, na bidhaa nyingine. Yaelekea pia kwamba Ras Guardafui ndiyo ilikuwa sehemu ya kusini kabisa ambako meli zindazo Punt zilifikia na mipaka ya kusini ya nchi ya Punt ilikuwa karibu na Rasi hii. Kuhusu mipaka yake ya kaskazini, inaweza kuchukuliwa kwamba ilikuwa ikibadilika karne hadi karne.

Kutokana na dalili nyingine tunaweza kufananisha pwani mbili za nchi ya mungu na





kingo mbili za mlango wa bahari wa Bab-el Mandeb. Ushahidi zaidi unatokana na ukweli kwamba miti itoayo ubani ilitawi vizuri huko Arabia Felix na katika Afrika.

Tunaweza kufuatilia hatua kwa hatua uhusiano kati ya Misri na Put. Hatua ya kwanza ilitangulia utawala wa Malkia Hatshepsut. Wakati huo, Wamisri walikuwa na habari chache sana kuhusu Punt. Walipata ubani kutoka kwa walanguzi wa ubani ambao walieneza hekaya kuhusu nchi hii kwa madhumuni ya kupandisha bei ya ubani. Wamisri wachache wanaojulikana kuwa walifanikiwa kufika hadi Punt walikuwa watu majasiri. Hatua ya pili ilianza na Malkia Hatshepsut. Kulingana na maelezo ya picha ya Mchoraji aliyepamba hekalu la Deir al Bahri, msafara wa meli tano ulitumwa kwenda kuleta miti itoayo ubani.

Katika chumba kimoja ndani ya hekalu hili hapo Deir al Bahri kuna sanamu ionyeshayo kuzaliwa kimungu kwa Hatshepsut, wakati imake, Ahmose, anaamshwa kutoka usingizini na manukato ya ubani kutoka nchi ya Punt. Hapa, kuhusishwa kwa jina la Punt na asili ya kimungu ya malkia huyu ni ushahidi unaoonyesha urafiki kati ya Malkia wa Misri na Punt, nchi ambayo wakazi wake walimwabudu Amon.

Picha za msafara huu zimetunza juu ya hali ya maisha katika nchi ya Punt, mimea yake, wanyama, na wakazi wake na umbo la nyumba zake pia. Nyumba hizi zilijengwa juu ya malundo ya udongo katikati ya miti ya jamii ya mnazi, mpingo na miti itoayo mafuta ya dawa na udi.

Kwa kuangalia picha za Punt zilichorwa katika malekalu, hakuna jambo jipya linalosimuliwa baada ya utawala wa Malkia Hatshepsut. Kabla ya hapo zipo matini zinazotaja habari za kufika kwa watu wa Punt nchini Misri. Watawala wa Punt waliwajibika kumpelekea zawadi Farao, ambaye alimwamuru insaidizi wake kuwapokea wegeni hao pamoja na zawadi zao. Kuna ushahidi fulani kuhusu biashara katika bandari za Bahari ya Sbam kati ya watu wa Punt na Wamisri na kuhusu usafishaji wa bidhaa kutoka Punt kwa njia ya nchi kavu kati ya Bahari ya Sham na mto Nili (Kaburi la Amon-Mose huko Thebes na Kaburi Na. 143).

Mwishoni mwa utawala wa Ramses IV, uhusiano kati ya Misri na Punt ulikwisha. Lakini kumbukumbu za nchi ya Punt zilibakia katika fikira za Wamisri.

Labda ingefaa tuongeze katika orodha ya ushuhuda juu ya uhusiano katika nyakati za kale ukweli kwamba kifaa cha kugegemeza kichwa kinachoitwa "*barchi*" au "*barki*" kwa Kisoinali cha leo, kilikuwa na jina hilo hilo katika Kimisri cha kale. Zaidi ya hayo Wasomali huita Mwaka wao Mpya Karamu ya Farao.

Sehemu zilizobakia za Afrika

Juhudi za watu au viongozi wao za kuanzisha uhusiano na nchi nyingine hutokana na makusudio mbalimbali ambayo mwishowe huweza kuelezwa kwa wepesi. Mahitaji ndiyo husababisha safari za uvumbuzi na juhudi za kuanzisha uhusiano. Uhusiano kati ya Misri na sehemu nyingine za Afrika, aghalabu, hufikiriwa kuwa ulikuwa ukielekea upande mmoja tu kama ilivyokuwa kuhusiana na uenezaji wa utamaduni wake katika nchi za kigeni. Hoja hii haizingatii ukweli kwamba Misri ilitengeka uuzaji wa bidhaa fulani za

Kiafrika. Hii ingewezesha pande zote zihusikazo kuathiriana. Katika uwanja huu, kuna vitu vingi ambayo havijashughulikiwa, na uchunguzi bado ni ngumu sana.

Uvumbuzi wa pwani za Afrika kutokea baharini wakati wa utawala wa Farao Necho II mwaka -610 hadi -595 umewavutia watafiti wengi. Lakini si wote wanaokubaliana na usahihi wa kihistoria wa taarifa alizozitoa Herodotus karne moja baada ya kipindi hicho. Necho II, ambaye anakuja mwishoni katika orodha ya Mafarao, ndiye aliyefanya mambo mengine mengi.

Je tuyachukulie vipi maelezo juu ya safari ambayo Harkuf aliifanya kwa niaba ya Pepi II na ambayo imezaa mahitimisho yanayopingana na yasiyokubalika kwa urahisi? Je taarifa za safari hii ni udadisi tu au zilitungwa kuridhisha ladha za wale wapendao mambo kutoka nje? Itakavyoelezwa hapo baadaye aliporejea kutoka katika safari yake hiyo Harkuf alimletea Pepi II mbilikimo mcheza ngoma kutoka nchi ya Yam. Hitimisho limepata kufikiwa kwamba huyu mbilikimo alikuwa mpigmi, na kwamba mfano huu wa pekee unathibitisha kuwapo kwa uhusiano kati ya Misri, Nili ya juu na Chad.



Safari hii ya uvumbuzi ahyoifanya Harkuf ni ya kihistoria ambapo safari nyinginezo ni kama ngano au hadithi za kubuni tu. Kwanza zipo habari kidogo sana kuhusu makazi ya kale ya Wapigmi na ni hatari kuchukulia kwamba walikuwa wanapatikana kwa wingi sana katika sehemu za juu za mabonde ya mto Nili, Pili hakuna ushahidi wowote kwa kuonyesha kwamba mbilikimo anayehusika alikuwa mpigmi. Na mwisho, bado haijajulikana kwa hakika mahali nchi ya Yam ilipokuwa.

Hoja itolewayo mara nyingi kwamba wanyama wa Kiafrika huonekana katika usawiri wa Kimisri inakosa ushahidi wa kutosha, hasa kilingana na kiwango cha ujuzi uliopo wakati huu, kuthibitisha kuwapo kwa uhusiano kati ya Misri na sehemu zilizo katikati mwa bara la Afrika. Nyani, mnyama mtakatifu wa Toth na ngozi za chui zilizohitajika katika mavazi rasmi ya makasisi kwa ajili ya ada za madhehebu ya Osiris zilizofanywa na Horus, na pia kwa ajili ya mavazi ya Mafarao, huenda vilipatikana katika nchi zilizopakana na Misri, au kutokana na mabadilishano ya mara nojamoja kati ya wachuuzi.


Kabla hatujajenga wazo dhahiri kuhusu kiwango cha ujuzi wa Misri juu ya Afrika, utafiti kamambe lazima ufanyike ili kuchungua taratibu za matukio ya wakati pamoja na wingi na ubora wa maana za marejeo yahasuyo wanyama wapatikanao katika matini na taswira za Kimisri.

Hata kama uhusiano kati ya Misri na Afrika yalitokana na mahitaji maalum au na udadisi wa mambo tu, ushahidi uliokwishapatikana ni mdogo sana na fasiri yake huwa ngumu na yenye kuleta mabishano mengi hata kufanya iwe vigumu kufikia hitimisho lenye maana kulingana na hali ya ujuzi wetu leo hii. Hata hivyo kuna fursa nyingine za kuweza kufanya utafiti wenye kuleta matokeo ya kuridhisha.

Swali limezuka mara kwa mara ikiwa egemezo la kichwa lenye muundo wa mstatili lililovumbuliwa na Wamisri, halikuenea katika sehemu nyingine za Afrika pamoja na ustaarabu wao. Hapa pia lazima ichukuliwe hadhari; na vishawishi kwamba mambo yalianzia sehemu moja tu na kuenea sehemu nyingine, lazima viepukwe. Je, kiegemezo hiki, cha kichwa na vingine vilivyoonekana, ni vya kiafrika tu vikiwa na asili yake huko



4.3 · Hongo ya Punt



Hongo ya Punt (inuendelea)

Misri? Je, havipo katika tamaduni nyinginezo zilizo mbali na Afrika? Je, viegemezo hivi haviwezi kuwa vifaa vilivyokuwa vikitumika na ambavyo yawezekana vilivumbuliwa katika sehemu tofauti.

Je yawezekana katika uwanja mwingine, kucludukulia kama baadhi ya watafiti walivyoharakisha kwanba aina yoyote ya ufalme unaolusisliwa na utakatifu una asili yake Misri; hayo yakiwa matokeo ya uhusiano yakiniifu na ya kihistoria kati ya Misri ya kale na wale Waafrika walioanzisha dhana hiyo? Je, kwa nini tusifikirie uwezekano wa maendelo ya asili kutokea hatua kwa hatua katika muda fulani?.

Je, ni njia zipi zilizotumiwa na madhehebu ya kondoo-dume, ambaye alikuwa mnyama mtakatifu wa Amon, anayeheshimiwa luuko Kush, Sahara na kati ya Wayoruba na watu wa Fon? Kwa wakati huu hapana budi kuorodhesha matukio haya yanayofanana na pale yanapotokea kabla ya kufikia mahitimisho ya namna yoyote.

Katika nyanja nyingi inawezekana kuonyesha kufananafanana kati ya mbimu, desturi na imani za Misri ya kale na zile za Kiafrika ambazo zimezuka hivi karibuni. Mfano mmoja mzuri ni ule wa uwili (uliojulikana kama "*Kas*" katika Misri ya kale) wa mtu halisi ambao Wamisri na jamii nyingi za Kiafrika leo hii lutilia maanani. Mfano kama huu yafaa usitazaniwe juu juu. Maisha baada ya kifo kama sehemu ya uwili huo katika imani za Wabantu. Waule, au Waakani huweza kuwashawishi watu kwa urahisi kuhusisha na dhana za Kimisri katika enzi za Mafarao.

Ulinganishi pia umefanywa wa ada za mazishi za Kimisri na zile zilizoelezwa na Al-Bakr kwa ajili ya wafalme wa Ghana katika karne ya kumi na moja ya enzi zetu.

Haiwezekani kutoa orodha kamili ya ada na desturi zinazofanana fanana, ambazo zimekusanywa kwa miaka nuingi katika uchunguzi uliotumia au kutotumia misingi ya kisayansi. Taaluma ya lugha nayo ni uwanja mkubwa wa kuweza kufanyia utafiti. Katika uwanja huu, kwa muda huu tulio nao, makisio yamekuwa mengi zaidi kuliko ukweli halisi unaojulikana.

Mambo yote haya, yanaelekeza kwenye litimisho kwamba ustaarabu wa Misri yawezekana uhuikuwa na athari juu ustaarabu wa Kiafrika wa hivi karibuni, japo mapana na marefu ya athari hii hayajulikani. Katika jitihada za kutaka kupima ni kwa kiasi gani ustaarabu wa Misri uliathiri ustaarabu wa Kiafrika, litakuwa jambo la busara kutafakari pia ni kwa kiasi gani Misri iliathiriwa. Huu ni uchunguzi wa kuvutia ambao ndio kwanza umeanza.

5

Matokeo ya Utawala Wa Mafarao Misri

Mchango mkubwa wa Misri ya wakati wa Mafarao kwa dunia unaonekana katika fani mbalimbali ikiwa ni pamoja na historia, uchumi, sayansi, sanaa na falsafa. Wataalamu katika fani hizi na fani nyingine nyingi wameuona muhimu wa mchango huu ingawa mara nyingi ni vigumu sana kuonyesha jinsi Wamisri walivyoathiri utamaduni wa jamii za jirani na ule wa watu walioishi karne za baadaye.

Mambo waliyofanya Wamisri au tuseme ushahidi uliopo juu ya mambo hayo ni vitu vya maana sana katika historia ya binadamu. Mambo hayo yaliziathiri jamii za kale za Wayunani na Warumi kabla ya kuwafikia Waarabu. Lakini watu walioishi Uyunani kabla ya enzi za Wayunani na baadaye Wayunani wenyewe hawakushirikiana na Misri hadi ilipofika mwaka - 1600 hivi. Baada ya kuanzisha mahusiano yao waliendelea kushirikiana kikamilifu na Wamisri mpaka karne ya saba kabla ya enzi yetu. Kutokana na mahusiano haya Wayunani walianzisha safari za wavumbuzi na wasafiri na baadaye baadhi yao wakajenga makazi yao katika bonde la Mediterani na hasa katika Misri. Wakati huo huo, Wayunani wa kale na wale waliowafuatia katika miaka elfia ya kwanza au elfia ya pili kabla ya enzi zetu walikuwa wakiwasiliana na jamii za Asia Ndogo hivyo wakapata athari za ustaarabu wao. Aidha walipata athari za ustaarabu wa Mesopotamia kupitia kwa watu wa Asia Ndogo. Mara nyingi si rahisi kusema kwa yakini ni katika mazingira gani hasa ya utamaduni, iwe ni ya Asia au ya Misri, ambamo uvumbuzi au ufundi fulani ulibuniwa kwa mara ya kwanza. Hii ni kwa sababu mazingira ya nchi hizi mbili yalifanana sana.

Ugonu wa kuorodhesha iniaka wakati wa enzi za kale unatufanya tusijue kwa hakika mawazo mbali mbali yalibuniwa lini na wapi. Pia kuna uwezekano kuwa mambo mengine yalifanywa wakati mmoja sehemu mbalimbali. Mfano mmoja ni ule wa uvumbuzi wa maandishi. Kuna sababu za kutufanya tuamini kuwa maandishi yalivumbuliwa karibu wakati ule ule Misri na Mesopotamia bila utamaduni wa nchi hizo mbili kuathiriana.

Juu ya hayo yote mambo ya Misri yaliyorithiwa na jamii nyingine za baadaye na hasa hasa jamii za kale za Kiafrika ni mengi, ya muhimu na wala hayawezi kupuuzwa.

Mchango wa Misri ya enzi kabla ya historia

Mojawapo ya mambo ya maendeleo yaliyotokea Misri hapo zamani ni katika fauji ya uchumi. Mwishoni mwa kipindi cha Neolithiki, mwaka - 5000, Wamisri wa kale waliliguza polepole bonde la mto Nili na kuwawezesha wakazi wa bonde hilo kupiga hatua mbele na kutoka katika kutegemca uchumi wa kukusanya chakula hadi ule wa kuzalisha chakula wao wenyewe. Mabadiliko haya katika mazingira ya maisha ya watu katika bonde la mto Nili yaliambatana na maendeleo makubwa ya hali na mali. Maendeleo katika kilimo yaliwawezesha Wamisri wa kale kujenga makazi ya kudumu vijijini na hali hii iliathiri mali ya usitawi wake kijamii na kimaadili sio tu kwa wakati wa historia ya awali, bali pia hata hata nyakati za utawala wa kifalme.

Mojawapo ya matokeo ya kwanza ya mapinduzi haya ya kipindi cha Neolithiki katika bonde la mto Nili ilikuwa kuwafanya Wamisri wa kale kuanza kuchunguza nguvu za vitu vilivyokuwa katika mazingira yao. Walianza kuheshimu jua na mto kama miungu ambayo ilikuwa inaonekana katika maumbo tofauti hasa niaumbo ya wanyama na ndege wanaofahamika zaidi. Kwa kuendeleza kilimo, Wamisri walijenga moyo wa ushirikiano katika jamii yao. Bila ushirikiano wa nainna hiyo kati ya wanakijiji, uzalishaji wa mazao ungalipungua.

Ustaarabu wa enzi za Mafarao unashangaza kwa jinsi ulivyocnea na kuendelea. Janbo lolote lililoanzishwa katika jamii liliendelezwa na kurithishwa, baada ya kufanyiwa marekebisha, tangu mwanzo hadi mwisho wa historia ya Misri. Ndiyo maana ufundi wa enzi ya Neolithiki uliendelezwa na kukitwa wakati wa kipindi cha kabla ya ufalme (mwaka - 3500 hadi 3000) na kuhifadhiwa katika kipindi cha historia.

Mabadiliko haya ya kipindi cha Neolithiki yalionekana hasa katika ustawishaji wa miji huko Misri. Mfano uliojitokeza zaidi ni ule wa vijiji vya zamani kuliko vyote katika bonde la mto Nili viitwavyo Merinda, Beni, Salama, katika ukingo wa Magharibi wa Delta.

Kipindi cha Historia

Vitu viwili vinajitokeza katika ustaarabu wa Misri wakati wa historia ya enzi ya Mafarao. Kitu cha kwanza ni maendeleo ya vitu. Cha pili ni maendeleo ya utamaduni yaliyotokana na wakati wa kale na yaliyohusu hali ya watu. Vitu hivi viwili vinahusiana na ndivyo kwa pamoja hufanya kile kinachoitwa utamaduni wa Misri. Kwa upande wa maendeleo ya vitu, kuna ufundi (kazi za mikono), sayansi, aljebra, jometri, unajimu, kemia, hisabati-matumizi, tiba, utaalumu wa kupasua sehemu za mwili na sanaa. Kwa upande wa utamaduni, kuna vitu kama dini, fasihi na nadharia za falsafa.

Mchango katika sanaa na kazi za mkono

Mchango wa Wamisri wa kale katika sanaa na kazi za mkono unaweza kuonekana katika uchongaji wa mawe, metali, kioo, penbe za ndovu, mifupa na vitu vinginevyo.

Wamisri hao waligundua na kutumia kwa wingi vitu mbalimbali vilivyokuwa katika mazingira yao na walikuza ufundi uliohitajika katika kutengeneza zana za mawe na shaba kama vile shoka, patasi, nyundo na tezo ambavyo vilitengenezwa kwa ufundi mkubwa ili kutumika katika ujenzi na katika viwanda kwa kazi kama zile za kuchimba mashimo au kupasua mawe. Aidha walitengeneza pinde na mishale, mapanga, ngao na rungu.

Kwa muda mrefu na hata wakati wa historia, zana na silaha zilizorithiwa toka kipindi cha Neolithiki zilitengenezwa kwa mawe. Mawe ya chokaa yaliyoko kwenye kingo za mto Nili yana vipande vigumu na vikubwa sana; Wamisri waliendelea kuvitumia hata baada ya kugunduliwa kwa shaba.

Matumizi ya chuma kwa kutengeneza vyombo hayakuhitajika sana hadi karibu na mwisho wa enzi ya Mafarao. Kwa sababu hiyo ufuaji wa madini katika Misri ulihusu dhahabu, fedha na shaba tu. Uthibitisho kuwa watu walikuwa wakichimba madini na kutengeneza shaba nchini Misri, umeonekana Sinai na Unubi.

Hata katika kipindi cha mwanzo cha ufalme (mwaka - 3000) Wamisri walikwishafahamu namna ya kutengeneza zana kwa kutumia shaba. Walikwishapata ufundi wa msingi wa kutengeneza chuma kama vile kufua, kugonga, kumimina, kuponda, kuunganisha na kukasa. Walimudu vizuri sana ufundi huu. Panoja na picha, zimepatikana sanamu kubwa za shaba ambazo ni za mwaka - 2300. Maandishi ya kale zaidi, kwenye miaka ya -2900, yanaelezea kuwepo kwa sanamu hiyo. Mandhari kwenye makaburi ya zamani katika kipindi cha mwanzo kabisa zinaonyesha karakana ambamo johari zilikuwa zinatengenezwa kwa dhahabu mchanganyiko wa dhahabu na fedha.

Tumepata habari nyingi toka Misri kuhusu ufundi uliotumiwa na wachoraji. Katika karakana zilizochorwa katika picha zilizo juu na chini ya kuta za makaburi, tunaweza kuona, kwa mfano, seremala na mafundi wa kutengeneza kabati wakitengeneza vifaa vya nyumbani, misumeno, kekee, tezo, patasi na nyundo. Mafundi hawa wamechorwa kwa ustadi na kila kitu kuhusu utumiaji wa vifaa hivyo kinaonekana. Hivyo tumeweza kuona kuwa msumeno wa Wamisri ulikuwa wa kuvuta na siyo wa kusukuma kama misumeno ya kisasa.

Pamoja na michoro hii, Wamisri wa kale waliacha makaburini mwao picha halisi za karakana zilizoonyesha mafundi wakitengeneza vifaa mbalimbali.

Michoro hii inamsaidia sana mwana historia katika kueleza na kuelewa ufundi huu na jinsi ulivyokuzwa. Zaidi ya hayo, vifaa vingi ambavyo vimepatikana vinaonyesha aina tofauti za shughuli za viwanda katika Misri ya kale. Kwa mfano, katika utengenezaji wa johari, Wamisri walitumia mawe yenye thamani kubwa na mengine yenye thamani ndogo kama vile dhahabu, fedha, inawe ya kung'aa, feruzi na vito vyenye rangi ya samawi na akiki kwa kutengeneza vizibo, mikufu na vitu vingine vya urembo kwa ufundi mkubwa.

Ulimaji wa kitani ulileta ufanisi mkubwa katika usokotaji kwa mkono na utengenezaji wa nguo. Ufundi huu ulijulikana tangu mwanzo wa kipindi cha

neolithiki (mwaka - 5000). Wanawake walifuma nguo kwa ufundi mkubwa kwa vile mara nyingi walishikilia pia mbili kwa wakati mmoja. Kitu kinachojulikana sana katika usokotaji wa Wamisri ni urefu wa nyuzi zilizotengenezwa kwa kuweka pia mbali kidogo toka kwenye kitani. Ili kuongeza umbali huo, wanawake walikalia vigoda virefu. Mwanzoni mitando ilikuwa si wima lakini kuanzia kipindi cha Himaya ya Kati, mitandi hiyo ilikuwa ya kusimama wima. Hii ili wawezesha wanawake hao kutengeneza nguo pana za kuvaa kila siku pamoja na nguo za kufunikia maiti waliokaushwa au kwa matumizi ya sanda.


Utengenezaji wa nubao, ngozi na madini mbalimbali pia uliendelezwa na bidhaa zilizotoka katika viwanda hivi zimeendelea kuwa katika hali nzuri hadi leo.

Vifaa vingine vilivyotengenezwa na mafundi wa Misri vilikuwa ni pamoja na vyombo vya shaba, jeneza la mbao, machanuo na mipini iliyotengenezwa kwa pembe. Wamisri wa kale pia walikuwa na ufundi maalumi wa kusuka matete ya porini na kuteugeneza mikeka na walitumia usumba ili kutengeneza nyavu na kamba ngumu. Ingawa vyombo vya udongo vilivyoanza kutengenezwa kabla ya historia havikutengenezwa vizuri sana, baadaye vyombo hivi vilitengenezwa kwa rangi nzuri nyekundu vikiwa na mzingo wa rangi nyeusi. Baadaye zaidi, vyombo hivi viling'arishwa na kuwekewa michoro. Vyombo hivyo vilitumika kuhifadha vitu mbalimbali na vingine vilitumika kama mapambo.

Ingawa labda siyo Misri iliyovumbua ufundi wa kutengeneza vioo, nchi hiyo ilisaidia katika uenezaji wa ufundi huo. Ni kweli kwamba huko Mesopotamia na katika utamaduni wa Indus, ufundi wa kung'arisha vioo - kitu ambacho ni muhimu kujua kabla ya kutengeneza vioo - ulikuwa ukitumika tangu zamani lakini hakuna ushahidi wa kuonyesha kuwa nchi hizi zilisambaza ufundi huo nje ya maeneo yao. Tunaweza tu kufikiria kuwa vitu hivi vilifanyika na kukuzwa wakati mmoja katika nchi tofauti na kwamba utengenezaji wa vioo uligunduliwa bila watu wa Asia na wale wa bonde la mto Nili kuwasiliana.

Vioo vilitumika siyo tu kwa kutengeneza shanga bali pia kwa kutengeneza vyombo vya aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na kalisi ndefu na majagi yenye umbo la samaki. Mara nyingi vyombo hivi vilikuwa vyenye rangi nyingi na havikuwa viangavu kwa ndani. Vioo viangavu vilianza kuonekana wakati wa utawala wa Tutankhamun (yapata mwaka - 1300). Tangu mwaka - 700, majagi ya glasi yenye rangi nyingi toka Misri yakiwa na umbo lenye jiwe laini la kung'aa yalienea sehemu yote ya Mediterani.

Baadaye, maandishi ya picha yalichorwa ndani ya kioo cha rangi na kioo hicho kilitumika kuandika juu ya ubao au juu ya jiwe. Ufundi wa kutengeneza vioo katika kipindi cha mafurao ulirithiwa na mafundi wa wakati wa Wayunani. Kwa hiyo ni juu wa Alexandria ulikuwa kituo muhimu cha kutengeneza vyombo vya kioo na kuviuza nje hadi Uchina. Lakini watu wa Meroe waliagiza bidhaa za kioo kutoka Alexandria na kisha wakawaiga mafundi wa Alexandria na kuenza ufundi wao sehemu ya juu ya bonde la mto Nili.



5.1 Picha ya Giza: Mtumbwi wa Cheops ("Mtumbwi wa Jua")

Kiwanda kimojawapo muhimu kilikuwa kile cha kutengeneza mafunjo yaitwayo "papyrus". Utengenezaji wa karatasi hizi ulivumbuliwa na Wamisri wa kale. Mafunjo yalitumika kwa kazi nyingi kuliko mimea mingine yote. Nyuzi zake zilitumika kutengeneza mitumbwi, kukalafati, kutengeneza tambi za taa, mkeka, vikapu, kamba ndogo na kamba kubwa. Kamba zilizotumika kufungia nguzo za daraja ambalo Xerxes alijaribu kuweka juu ya mto Hellespont zilitengenezewa Misri kwa nyuzi za mafunjo. Katika ujenzi wa zamani, mashina ya mafunjo yalifungwa pamoja na kutumika kama nguzo. Baadaye, wakati wa Warumi na Wayunani, wajenzi waliyatumia mashina hayo kujenga nguzo zilizoungwa pamoja na kuonekana kwa jnu kama maua yaliyofungwa au yaliyofunguka. Lakini mafunjo yalitumika hasa kutengeneza karatasi au "papyrus", neno ambalo limechukuliwa katika Kiingereza kama "paper".

Mafunjo yalitengenezwa kwa kukingama chane nyingi zilizokatwa toka mashina ya mimea ambazo baada ya kugandamizwa na kukaushwa zilitandazwa na kuwa ukurasa mpana.

Kurasa ishirini za mafunjo ziliunganishwa wakati zikiwa bado na unyevunyevu na zikatengenezwa katika hali mviringo yenye urefu wa meta tatu hadi sita. Hati mviringo nyingi ziliweza kuunganishwa na kufikia urefu wa meta 30 au 40. Hati mviringo ya namna hiyo ndiyo iliitwa kitabu huko Misri.

Katika vitu vyote vilivyotumika kutengeneza vifaa vya kuandikia, mafunjo ndiyo yalikuwa rahisi zaidi kutumika kwa vile ni laini na mepesi. Kasoro yake moja ni kwamba yanakatika kwa urahisi na si magumu.

Mafunjo yaliyotumika Misri wakati wa ufalme wa kwanza (mwaka - 3000) mpaka mwisho wa kipindi cha Mafarao yalitumiwa pia na Wayunani, Warumi, Wakopti, watu wa Byzantium au Armenia pamoja na Waarabu. Yamegunduliwa maandishi mengi ya Kigiriki na Kilatini kwenye karatasi za namna hii. Mojawapo ya vitu ambavyo Misri iliuzwa kwa wingi nchi za nje ni hati mviringo za karatasi. Mafunjo ni mojawapo ya vitu vikubwa ambavyo Misri ya kipindi cha Mafarao ilieneza katika jamii nyingine za ulimwengu.

Viwanda vilivyokuwapo vilitegemea ufundi na ujuzi na viliwafanya mafundi kuungana ili kukua ujuzi wao. Kuna mamia na hata maelfu ya mifano ya vitu vya kale toka Misri katika majumba mengi ya makumbusho na hifadhi za watu binafsi duniani kote.

Ufundi mwingine ambao ni mdogo uliocenzwa na Misri ulimwenguni ni utumiaji wa mawe katika ujenzi. Haikuwa kazi rahisi kuchonga mawe makubwa na magumu au mawe ya chokaa na mawe meusi ili kutengeneza mawe yaliyo na umbo zuri na yenye kung'aa tayari kwa kutumika katika kazi za ujenzi.

Aidha utafutaji wa mawe ya kutengeneza sanamu ambao ulileta matumaini ya kupatikana kwa pamoja na juhudi za kugundua vitembwe na mawe yenye thamani na rangi ulisaidia sana kueneza ufundi wa Wamisri katika nchi za Asia na Afrika.

Wamisri hawakusita kutafuta mawe mbali jangwani. Mara nyingine walisafiri

umbali wa kilometa mia moja toka mto Nili. Jiwe lillilotumika kutengenezea sanamu maarufu ya Chephren iliyoko katika jumba la makumbusho la Kairo, lilichimbwa toka machimbo ya jangwa la Nubia yapata kilometa 65 Kaskazini Mashariki ya Abu Simbel. Machimbo haya yalianzishwa tangu mwanzo wa Historia ya Misri (yapata mwaka - 2800).

Vifaa vilivyotumiwa na mafundi waashi wa Misri vilikuwa nyundo za miti na patasi za shaba kwa mawe yasiyo magumu kama vile mawe ya chokaa; sululu, patasi na nyundo za mawe kwa aina mbalimbali za mawe magumu. Machimbo yalipopatikana mbali na mto Nili, watu wapatao 1,400 walitumwa kwenda huko wakiwemo viongozi, wanajeshi, wapagazi, wachimba migodi, makarani na waganga. Msafara wa namna hiyo ulikuwa unajandaa kukaa muda mrefu nje ya Misri na hivyo watu waliokuwemo walisaidia kueneza utamaduni wa Misri, hasa Afrika.

Ufundi wa kuchonga mawe uliopatikana mwanzoni mwa kipindi cha ufalme, uliwafanya Wamisri waweze kuchimba makaburi katika miamba wakati wa Ufalme Mkongwe (mwaka - 2400). Lakini, hata kabla ya wakati huo niwaka -3000 mpaka -2400, Wamisri walikuwa wakijenga makaburi kama makazi ya kudumu ya wafu. Hivyo waliweza kujenga majengo makubwa makubwa na baadaye utaalumu wa ujenzi ulipoendelea, waliweza kujenga piramidi ya vidato na baadaye piramidi hasa.

Ujuzi wa Wamisri katika kutumia mbao unaonekana hasa katika ujenzi wa meli. Katika bonde la mto Nili mto ndiyo njia pekee inayofaa kwa usafiri. Hii iliwafanya Wamisri kuwa na ujuzi wa uundaji meli tangu nyakati za zamani. Mitumbwi ilipewa nafasi muhimu katika kazi zao za sanaa tangu kipindi kabla ya Historia na kuendelea. Wamisri waliweka inifano ya mitumbwi katika makaburi na walichora katika kuta za makaburi sanamu za mito na ujenzi wa mitumbwi. Hii ni kwa sababu waliamini kuwa maisha baada ya kufa yanafanana sana na maisha kabla ya kufa. Wakati mwingine, walizika mitumbwi karibu na makaburi ili iweze kutuuniwa na wale waliokuwa wamezikwa. Hii ilitokea Herluan kwenye makaburi ya falme mbili za kwanza na Dahshur karibu na piramidi ya Sesostris wa tatu. Lakini hivi karibuni kumegunduliwa kitu kingine cha ajabu zaidi. Mwaka 1952, upande wa kusini wa Piramidi Kuu, kumegunduliwa mashimo mawili yaliyochimbwa katika mwamba na kufunikwa na vipande vikubwa vya mawe ya chokaa. Katika mashimo haya, kulionekana ile mitumbwi aliyotumia Cheops ikiwa imepanguliwa kidogo lakini ikiwa na kila kitu pamoja na makasia, vijumba na sukani. Mtumbwi mmoja kati ya hii umetolewa shimoni na kuhifadhiwa. Mwingine utatolewa baadaye.

Mtumbwi wa Cheops ambao sasa uko katika jumba maalum la makumbusho umejengwa upya. Wakati ulipogunduliwa, ulikuwa na vipande vya mbao 1224 ambavyo vilikuwa vimepanguliwa kidogo na kupangwa shiironi katika tabaka 13 zilizofuatana. Mtumbwi huu una urefu wa meta 43.4 na upana wa meta 5-9 na unaweza kubeba uzito wa tani 40. Mbao za pembeni zina upana wa sentimeta 13 na 14. Ni vigutnu kukisia mtumbwi huu uliweza kwenda chini ndani ya maji kiasi gani lakini ulikuwa mtumbwi mwepesi ukilinganisha na ukubwa wake. Ingawa huu

mtumbwi wa Cheops umeundwa kwa mbao ambazo hazikupangwa kwa ujuzi, hauna mkuku, lakini umechongoka vizuri na sehemu ya chini imesawazishwa. Kitu kinachostaajabisha ni kwamba mtumbwi huu ulijengwa bila misumari. Mbao zimeungwa kwanza kutumia ndimi na matundu yayotobolewa kwenye mbao. Mbao na miti ya mkingamo vilivyotumika kujenga mtumbwi huo vimefungwa pamoja kwa kamba. Kuna ukumbi mkubwa ambao una sehemu iliyofunikwa katika gubeti. Hauna mlingoti na uliendeshwa ama kwa kupiga makasia au kwa kuvutwa na kamba, ingawa matanga yalikuwa yakitumika Misri muda mrefu kabla ya utawala wa Cheops. Wanajeshi waliweza kupigana ndani ya maji huko Bahari ya Sham na kwenye mto Eufratesi mbali na Misri kwa kutumia ujuzi huu wa ujenzi uliowawezesha kuunda sehemu mbalimbali ambazo baadaye zilifungwa pamoja.

Mchango wa Wamisri katika Sayansi


Mchango wa kipindi cha Mafurao katika sayansi na hisabati umekuwa wa faida kubwa katika maendeleo ya fizikia, kemia, elimu ya wanyama, tiba, elimu ya madawa, jiometri na hisabati. Ama kwa hakika ulimwengu ulifaidika na uzoefu wao nikubwa katika nyanja zote hizi. Ujuzi wa niasomo mbalimbali ulitumika ili kutekeleza miradi maalum.

Ukaushaji Maiti

Mfano mmojawapo unaoonyesha utaalumu wa upeo wa juu wa Wamisri wa kale ni jinsi walivyohifadhi maiti wao. Kufanya hivyo kunaonyesha kuwa walimudu sayansi ya aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na fizikia, kemia, tiba na uganga wa kupasua viungo vya mwili. Utaalam huu katika kila somo ulitokana na uzoefu wa muda mrefu. Kwa mfano, Wamisri walikuza ujuzi wao wa madawa yaliyomo kwenye madini ya magadi yaliyokuwa sehemu fulani za Misri hasa sehemu ya Wadi el Natrun na kutumia madawa yaliyomo kwenye madini haya ili kutimiza matakwa ya inani yao juu ya maisha baada ya kifo. Wamisri wa kale waliamini kuwa kuna maisha baada ya kifo na walisisitiza kikamilifu imani hii kwa kuhifadhi mwili wa binadamu. Imegunduliwa hivi karibuni kwamba madawa yaliyomo katika magadi ni mchanganyiko wa aina mbalimbali za chumvi. Wamisri wa kale walikuwa wanaelewa madawa hayo na kazi zake. Ili kumhifadhi maiti, walimweka katika magadi kwa muda wa siku sabini. Walitoa ubongo kupitia puani na walitoa utumbo kwa kupasua pembeni mwilini. Upasuaji wa namna hii ulihitaji utaalumu mkubwa katika anatomia. Utaalamu huu unajidhihirisha katika namna maiti yalivyohifadhiwa vizuri.

Utaalamu wa kupasua viungo vya mwili

Bila shaka elimu waliyopata Wamisri kutokana na kuhifadhi maiti ndiyo iliawawezesha kuendeleza mapeina sana mbinu za upasuaji wa viungo vya mwili. Tunafahamu mengi kuhusu utaalumu huo huko Misri kutokana na maelezo ya kitaalamu ya Smith, nakala ya waraka ulioandikwa katika mafunjo wakati wa Ufalme



5.2 Mfano wa Kiwanda cha Ufumaji, nasaba ya kumi na mbili, kwenye –2000

Mkongwe kati ya mwaka - 2600 na - 2400. Makala haya yanaelezea juu ya upasuaji na utabibu wa mifupa kwa nje. Kuna maelezo kamili juu ya aina 48 za magonjwa. Kwa kila aina ya ugonjwa, niwandishi anaanza na maelezo yake chini ya kichwa cha jumla kisemacho: 'Maelezo hayo kila mara yanaonyesha hatua kwa hatua taratibu zote. Yanafuatiwa na uchunguzi wa ugonjwa wenyewe na kama mganga anaweza kumtibu mgonjwa, kuna maelekezo kamili juu ya kufanya hivyo.

Kuna namna za kutibu magonjwa ambazo zinaelezwa katika maandishi haya ya Smith ambazo bado zinatumika hadi leo. Uchunguzi wa maiti waliohifadhiwa umeonyesha matibabu yaliyotumika. Kwa mfano, taya linalokisiwa kuwa ni la enzi ya Ufalme Kongwe lina mashimo mawili yaliyotobolewa ili kuondoa usaha kwenye jipu. Kuna mfano mwingine wa fuu la kichwa lililopasuliwa kwa shoka au kwa upanga na kuwekwa sawa tena.

Hii yote inaonyesha utaalumu wa waganga wa Misri ya kale, utaalumu ambao tunaweza kusema ulienezwa Afrika, na Asia taratibu na waganga waliofuatana na misafara ya vikosi vya majeshi ya Misri yaliyokuwa yakienda nchi za nje. Aidha inajulikana kuwa watawala wa nchi nyingine za nje kama vile Bactria, mwana wa mfalme toka Bakhtan, asia, au hata Cambyses mwenyewe aliwaalika madaktari wa Misri kufanya kazi katika himaya zao. Tunajua pia kuwa Hippocrates alitumia maktaba ya hekalu la Imhotep lililoko Memphis. Waganga wengine wa Uyunani walifuata mfano wake baadaye.

Tiba

Elimu ya Tiba ilikuwa ni mchango mkubwa mmojawapo wa kisayansi ambao Misri ya kale iliutoa katika historia ya maendeleo ya binadamu. Kuna nyaraka zinazoonyesha kwa ukamilifu vyeo vya waganga wa Misri pamoja na masomo waliyohitimu. Watu wa Mashariki ya Asia na hata Wayunani walikiri uwezo na sifa za Wamisri wa kale katika tiba na elimu madawa. Mmojawapo wa watu wanaojulikana sana katika ulimwengu wa tiba ni Imhotep ambaye alikuwa ni afisa wa serikali, mtaalamu wa ujenzi na daktari wa Mfalme Zoser wa Ufalme wa Tatu. Umaarufu wa Imhotep ulivuma wakati wote wa historia ya zamani ya Misri mpaka wakati wa Wagiriki. Wamisri walimtambua mtu huyu kama mungu na kumwita Imouthes. Wayunani waliimtambua pia na kumfananisha na Askelepios, mungu wao wa tiba. Ama kwa hakika katika tiba na elimu madawa, tunaweza kuona kwa urahisi jinsi Wamisri walivyoathiri Wayunani katika maendeleo yanayohusu taratibu za kuponya na maelekezo ya dawa yaliyotolewa na mganga. Vifaa vingine vilivyotumika wakati wa upasuaji vimegunduliwa katika machimbo.

Ushahidi uliopo katika maandishi juu ya tiba wakati wa Misri ya kale unaonekana kwenye maandishi ya wataalamu wa madawa kama vile Elbers, Berlin na Edwin Smith; maandishi yaelezeayo utaalumu wa kupasua pamoja na maelezo mengine yanayoonyesha njia zilizotumika katika upasuaji zinazoonyesha kwa kinaganaga maagizo yaliyotolewa kuhusu njia za kuponyesha.

Kinyume cha maandishi ya Edwin Smith juu ya utaalumu wa kupasua ambao ni wa kisayansi, maandishi mengi juu ya tiba yalikuwa yakieleza zaidi taratibu za uchawi. Wamisri waliamini kuwa ugonjwa ulikuwa ni kazi ya miungu au ya mashetani. Hii iliwafanya waamini uchawi na udiyo maana maagizo mengine yaliyoko kwenye maandishi ya Ebera yanafanana na wimbo wa mchawi kuliko maagizo ya daktari.

Hata hivyo, madaktari wa Misri waliwapima wagonjwa wao na kuona dalili za ugonjwa. Halafu walifanya uchunguzi na kutoa maagizo ya tiba. Maandishi yale yaliyopo yanaonyesha hatua hizo na tunaweza kusema hatua hizi zilifuatwa na kila daktari. Mgonjwa alipimwa katika hatua mbili. Hatua ya pili ilifanyika baada ya siku chache kama chanzo cha ugonjwa hakikuonekana vizuri. Miongoni mwa wagonjwa yaliyoonekana, kuelezwa kitaalamu na kutibiwa na madaktari wa Misri ni pamoja na magojwa ya tumbo, kuvimba tumbo, kansa ya ngozi, ugonjwa wa kuumia kikoromeo, chemba ya moyo, ugonjwa wa kifua, kisukari, kufunga choo, bawasiri, ugonjwa wa mkojo kutotoka au kutoka bila mtu kujizuia, kichocho na wagonjwa ya macho n.k.

Madaktari wa Misri waliwatibu wagonjwa wao kwa kutumia vidonge vya kuweka mkunduni, dawa ya kupaka, dawa ya asili, aina mbalimbali za mafuta, kukanda, bomba la kuingiza dawa, dawa ya kubandika na hata dawa za kuvuta ambazo Wamisri waliwafundisha Wayunani. Vitabu vya Wamisri juu ya utengenezaji wa madawa vilivyonyesha pia namna mbalimbali ya mimea ifaayo kwa dawa. Kwa bahati mbaya, majina ya mimea hii hayawezi kufasiriwa. Kama Herodotus alivyosema, ufundi wa Wamisri na madawa yao vilisifika sana wakati wa kale. Kuna maandishi yanayoonyesha majina ya madaktari kama mia moja hivi wa Misri ya kale. Kati ya majina hayo, wapo pia waganga wa mifugo.

Hisabati (hesabu, Aljebra na Jiometri)

Hisabati ni moja ya nyanja muhimu za sayansi ambazo Wamisri walishughulika nazo. Ushahidi kuwa walizingatia kupina kwa uangalifu unaonekana tukiangalia vipiino sahihi vya majengo yao makubwa yaliyopimwa kitaalamu na michoro iliyoko kwenye majengo hayo. Hawangaliweza kupima kwa uangalifu hivyo bila ujuzi wa kutosha katika hesabu.

Ushahidi juu ya maendeleo yaliyokwishafikiwa na Wamisri unapatikana hasa katika nyaraka za kipindi cha Ufalme wa Kati (- 2000 hadi - 1750). Muhimu katika hizo hupatikana katika mafunjo ya Moscow na Rhind.

Wamisri walitumia mfumo wa desimali katika kuhesabu. Walirudia rudia alama za nambari (mamoja, makumi, mamia,) mpaka hapo walipofikia tarakimu waliyoitaka. Hawakutumia sufuri. Alama ambazo Wamisri walitumia ili kuonyesha sehemu za kumi kama vile $\frac{1}{2}$, $\frac{1}{4}$, n.k. zinatokana na hadithi ya Hourus na Seth isemayo kwa jicho la kipanga alilokuwa nalo Horus lililochomolewa na kukatwa vipande vipande na Seth. Vipande hivyo ndivyo vinawakilisha sehemu fulani za kumi.

Tunaweza kugawa hisabati za Wamisri katika vichwa vitatu - hesabu, aljebra na jiometri.

Mfumo wa utawala wa Wamisri ulihitaji ujuzi wa Hesabu. Haishangazi kuona kuwa makarani walitumia muda mwingi sana wakihesabu na kuorodhesha ukubwa wa ardhi iliyokuwa inalinimwa, wingi wa mazao yaliyokuwa yamevunwa na ugawaji wa mazao hayo, idadi ya wafanyakazi na ujuzi wao.

Matatizo yote yaliyojitokeza na kutatuliwa katika mada za hesabu za Wamisri yanafanana kwa kitu kimoja; ni matatizo ya vitu vinavyoonekana na ambavyo karani wa kijijini alipaswa kushughulikia kila siku - kama vile idadi ya matofali yaliyotakiwa kujenga ukuta ulioinama. Kwa hati hiyo hesabu za Wamisri zilishughulikia hasa maswala bayana kuliko maswala ya kinadharia.

Haieleweki kama tunaweza kuzungumzia kitu kama aljebra huko Misri wakati huo. Wataalamu wa historia ya sayansi wanatofautiana juu ya swali hili. Jibu linategemea kama inawezekana kufanya aljebra bila kutumia ishara kuwakilisha dhana.

Waandishi wawili wa Kiyunani, Herodotus na Strabo wanakubaliana kuwa Wamisri ndio walivumbua jiometri. Uvumbuzi huu ulitokana na haja ya kuhesabu kiasi cha ardhi iliyokuwa inamoinonyoka au inaongezeka kila mwaka wakati wa mafuriko ya mto Nili. Jiometri huko Misri, kama hesabu zao ilihusu vitu vinavyoonekana. Katika maandishi ya zamani, kazi kubwa na ya umuhimu wa kwanza ilikuwa kumwezesha karani kuwa na kanuni za kutafuta eneo la shamba, wingi wa nafaka katika ghala au idadi ya matofali yaliyohitajika katika mradi wa ujenzi. Zaidi ya hapo Wamisri walijua jinsi ya kutafuta eneo la pembe tatu au duara, ujazo wa mcheduara, piramidi au piramidi fupi na labda waliweza hata kupima kizio cha kitu. Walifaulu zaidi katika kutafuta eneo la duara.

Maarifa ya jiometri yaliwafaa sana Wamisri katika upimaji wa ardhi ambacho kilikuwa ni kitu muhimu sana kwao. Kuna makaburi mengi ambayo yana sanamu zinazoonyesha watu wakipima ardhi na wakijaribu kuhakikisha kuwa mawe yanayoonyesha mipaka ya mashamba hayakuondolewa. Sanamu hizo zinaonyesha pia watu wakipima eneo lililolimwa kwa kutumia kamba yenye fundo (badala ya minyororo watumiaio mafundi leo hii). Hii kamba waliyokuwa wakitumia wapimaji wa ardhi iliitwa "*nouh*" na inazungumziwa katika maandishi ya mwaka -2800.

Unajimu

Maandishi tuliyo nayo juu ya unajimu huko Misri si mengi kama yale yaliyopo juu ya hisabati na utaalumu wa upasuaji na tiba. Lakini kuna ushahidi wa kutuwezesha knamini kuwa kulikuwa na makala yaliyoandikwa juu ya unajimu. Waraka wa tisa wa Carlsberg ambao unaeleza njia mojawapo ya kuonyesha mabadiliko ya mwezi bila shaka uliandikwa wakati wa kipindi cha Warumi lakini inaonekana kuwa waraka huo unatokana na maandishi ya awali kwa vile mawaidha yaliyomo hayaonyeshi kuwa

ameathiriwa na maandishi ya Kiyunani. Hii inahusu pia waraka wa kwanza wa Carlsberg. Kwa bahati mbaya, hatuna mwanzo wa maandishi hayo na mchango wa Misri katika unajimu unaweza kujulikana tu kutokana na makisio kwa kuangalia vitu vilivyofanyika. Hata hivyo, mchango huu si mdogo.

Kama tulivyoona katika utangulizi mwaka wa Wamisri uligawanywa katika majira manne ya miezi minne. Kila mwezi ulikuwa na siku 30. Siku tano ziliongezwa mwisho wa mwaka na hivyo kufanya mwaka wa Misri kuwa na siku 365 ambao ndio mwanzo wa kalenda tunayotumia. Misingi hii iliyowekwa na Wamisri ilirithiwa na kuendelezwa na Warumi. Mwaka - 47 kwa mfano Mfalme Julius alifanyia mabadiliko kalenda ya Kimisri ambayo ilitumika mpaka ilipofanyika marekebisho tena mwaka 1582 chini ya Mfalme Gregory. Wamisri walikuwa na Kalenda ya kidini iliyotegemea mwezi.

Tangu nyakati za safari za Napoleon huko Misri, wazungu wameshangazwa na mpango mzuri wa majengo ya wakati wa Mafarao hasa piramidi ambazo pande za inbele zinaangalia kusini, mashariki, kaskazini na inagharibi. Mampiramidi maarufu yamecahana uelekeo wa kaskazini kwa sehemu ndogo ya digrii inoja. Usahihi wa namna hiyo uliweza tu kupatikana kwa kutumia maarifa ya unajimu. Wamisri waliweza kufikia usahihi wa kiasi hicho kwa sababu walikuwa na kikundi cha Wanajimu waliokuwa wakifanya kazi chini ya uongozi wa Waziri ambaye kazi yake ilikuwa ni kuangalia anga wakati wa usiku, kuangalia kuchomoza kwa nyota hasa nyota iliyoitwa Sirusi na zaidi ya yote kuonyesha jinsi saa za usiku zilivyotofautiana kufuatana na inajira. Usiku ulikuwa na saa 12 na ulianza jua lilipotua na kuisha jua lilipochomoza asubuhi. Tunayo majedwali yanayoonyesha kuwa kila saa ya usiku iliorodheshwa kila mwezi baada ya kila siku kumi kwa kuangalia kuchomoza kwa kundi la nyota au nyota moja kubwa. Maandishi haya yanaonyesha inakundi thelathini na sita ya nyota. Kila kikundi cha nyota kilikuwa ni mwanzo wa kipindi cha siku kumi. Kuna makaburi ambayo yana picha zinazoonyesha anga na nyota na picha hizi zimetuwezesha kuona makundi ya nyota ambazo zilitambuliwa na Wamisri. Kundi la "Dubu Mkuu" (Ursa Major) linawakilishwa katika michoro hiyo na "Gui la Fahali". Nyota zinazozunguka "Akuturusi" zimeonyeshwa kwa picha ya mamba na kiboko wakiwa painoja. "Awizi" inaonyeshwa kwa picha ya mwanaume aliyenyoosha mikono. "Jabari" imeonyeshwa kwa picha ya mtu anayekimbia akiwa amegeuza kichwa nyuma. Binti Kitini (kasiopea) imeonyeshwa kwa sanamu iliyo na mikono iliyonyoosha. Ghuli, Kilimira, Nge na Hamali zimeonyeshwa kwa sanamu nyingine.

Ili kuonyesha saa za mchana ambazo zilitofautiana kufuatana na majira, Wamisri walitumia kitu kilichoitwa "gnomon" (saa). Chombo hiki kilitengenezwa kwa kusimamishwa wima ufito wa kawaida kwenye ubao wenye vipiimo anibao uliunganishwa kwenye timazi. Chombo hiki kilitumika kupiina muda uliotumika kumwagilia maji mashambani kwa vile maji hayo yalipaswa kugawiwa kwa usawa. Pamoja na kipimo hiki, Wamisri walikuwa pia na saa zilizotembea kwa nguvu ya maji

katika mahekalu yao. Saa hizi zilichukuliwa na Wayunani na kutengenezwa vizuri zaidi kama saa za mezani za wakati wa kale.

Usanifu wa Majengo

Wamisri wa kale walitumia ujuzi wao wa hisabati katika kuchimba, kusafirisha na kupanga mawe makubwa yaliyotumika katika miradi yao ya ujenzi. Walikuwa na mazoea ya muda inrefu ya kutumia matofali ya udongo na namna mbalimbali za mawe tangu nyakati za zamani. Walianza kutumia mawe magumu na mazito yapata miaka elfu tatu kabla ya wakati wetu. Mawe hayo yalitumika kujengea sakafu za makaburi mengine ya nasaba ya kwanza huko Abydos. Wakati wa ufalme wa pili, walitumia mawe ya chokaa kujengea kuta za makaburi.

Walipiga hatua mpya wakati wa Ufalme wa Tatu. Kulitokea maendeleo makubwa katika historia ya maarifa ya ujenzi Misri. Kwa mara ya kwanza, jumba zima lilijengwa kwa mawe. Jumba hili ni lile la piramidi ya vidato iliyoko Sakkara ambayo ni sehemu ya jumba kubwa la mazishi la mfalme Zoser.

Wamisri walivumbua aina mbalimbali za mitindo ya ujenzi, ambayo piramidi ni mfano mmoja unaojulikana sana. Mapiramidi ya kwanza yalikuwa na vidato na ni mpaka wakati wa ufalme wa nne (mwaka - 2300) ndipo yalijengwa mapiramidi yenye umbo la pembe tatu. Tangu wakati huo, mafundi wa ujenzi waliacha kutumia mawe madogo waliyokuwa wakitumia wakati wa Ufalme wa Tatu na kuanza kutumia mawe makubwa.

Hadi wakati Warumi walipoivamia Misri, ujenzi wa majengo ya kawaida uliendelea kuwa wa matofali yaliyokaushwa juani. Hii ilihusu hata majengo ya kifalme. Majumba ya Ramses huko Thebes na boma kubwa la Unubi yanaonyesha jinsi matofali haya yalivyoweza kutumika kwa njia nyingi. Yaliweza kupendeza sana kama inavyoonekana kwenye jumba la mfalme Amenhotep wa nne lililoko Tell - el-Amarna likiwa na sakafu na dari vilivyopambwa kwa sanamu. Mchango mwingine katika maarifa ya ujenzi ulikuwa ni utengenezaji wa nguzo. Mwanzoni, nguzo hizi ziliunganishwa na kuta laini baadaye zilisimama peke.

Utaalamu huu uliendelezwa na Wamisri wa kale kutokana na mazingira. Kwa ufano, walifikiria utengenezaji wa nguzo kisha kuchunguza maumbo ya mimea ya porini kama vile mabua na mafunjo. Walijenga sehemu ya juu ya nguzo ikifanana na umbo la ua la yungiyungi, mafunjo au mimea mingine. Huu ulikuwa ni muundo mpya katika maarifa ya ujenzi. Wajenzi wa mataifa mengine waliiga kutoka kwa Wamisri wa kale nguzo za namna hii zenye umbo la yungiyungi au mafunjo au minazi.

Iuawezekana kuwa Wamisri wa kale walivumbua jinsi ya kujenga kwa kutumia zege wakati wa Ufalme wa Pili (yapata mwaka - 2900). Mwanzoni walitumia zege ya matofali lakini ilipofika mfalme wa sita, Wamisri walikuwa wakijenga zege ya mawe.

Piramidi kubwa ya Giza ilikuwa mojawapo ya maajabu saba ya ulimwengu wa kale. Jumba la ukubwa wa namna hiyo linaonyesha wazi kuwa Wamisri walikuwa na

utawala mzuri wa ujuzi katika usanifu ujenzi. Ujuzi huu unadhihirishwa na ujenzi wa vijia vinavyopanda juu kuelekea chumba cha mfalme kilichojengwa kwa mawe makubwa. Chumba ambacho kina matundu mawili ya kuingiza hewa yanayoangalia nje upande wa kaskazini na kusini mwa chumba cha mfalme.

Ustadi wa Wamisri wa kale unadhihirishwa pia na vipimo vilivyotumiwa katika kujenga vyumba na vijia vilivyoko kwenye mapiramidi licha ya ule ujuzi mkubwa wa kukata, na kusimamisha minara mirefu na mikubwa ya mawe.

Ufundi walioupata Wamisri katika ujenzi na umwagiliaji kwa mifereji na mahandaki au maboma ya kuzuia maji ulionekana katika mambo mengine yanayohusu ujenzi. Mwaka - 2550, walikuwa wamekwishapata ujuzi wa kutosha kujenga boma la mawe yaliyochongwa katika "oasisi" karibu na Kairo. Baadaye kidogo, wahandisi wao walitoboa njia ya maji katika mawe ya Maporomoko ya Kwanza yaliyoko Aswan na kuwezesha meli kupita katikati.

Vitu vingine vilivyojitokeza katika maarifa ya ujenzi Misri ni kulima bustani na kustawisha miji. Wamisri walipenda sana bustani. Hata maskini walipanda inti au miti michache katika uwanja mdogo wa nyumba zao. Bustani za matajiri zililingana na ufahari wa majumba yao makubwa na yenye kuvutia. Bustani ilizunguka bwawa la kuogelea na mara nyingine kulikuwa na mabwawa mengi. Mabwawa haya yalitumika kwa kufuga samaki au kutunza maji ya kumwagilia na pia kupoza hewa iliyozunguka nyumba. Mara nyingi bwana mwenye nyumba alikuwa na kibanda kidogo cha mti kilichojengwa karibu na bwawa ambamo alikaa kupunga hewa saa za jioni na kuwakaribisha rafiki zake kwenye vinywaji baridi.

Mara nyingine mabwawa yaliyochimbwa yalikuwa makubwa sana. Ziwa la Kasri ya Snefru lilikuwa kubwa la kutosha kumwezesha Snefru asafiri kwa intumbwi akiwa na wasichana waliovaa nguo nyepesi wakipiga makasia. Amenhotep wa tatu alikuwa na bwawa kubwa lililojengwa kwenye nyumba yake ya Thebes. Wamisri waliwaambukiza Warumi tabia hii ya kupenda bustani.

Kuna mifano ya zamani zaidi ya ustawishaji wa miji kuliko ile inayosemekana ilitokana na ujuzi wa Wayunani. Wakati wa ufalme wa Sesostri II yapata mwaka - 1895 mji wa Lahu ulijengwa kwa kuzungushiwa ukuta wa pembe tatu. Mji huo ulikuwa na majumba ya utawala na yale ya kuishi watu. Nyumba za wafanyakazi zipatazo 250 zimechimbwa zikiwa zimejengwa pamoja kando ya barabara yenye upana wa meta 4 ambayo ilikutana na kuu yenye upana wa meta 8. Kila nyumba ilikuwa imejengwa kwenye ardhi ya meta za mraba 100 hadi 125 na ilikuwa na vyumba 12 kwenye ghorofa moja. Katika sehemu nyingine ya mji kulikuwa na nyumba za viongozi. Hizi nyumba za mijini zilikuwa na vyumba vingi. Kuna nyumba zilizokuwa na vyumba sabini. Kulikuwa na nyumba za viongozi zilizokuwa pia zimejengwa kando ya barabara zilizonyooka zikienda sambamba na kuta za mji. Katikati ya barabara hizi kulikuwa na mifereji ya kuondoa maji machufu.

Ngome kubwa za Unubi zilikuwa pia zimejengwa kwa muundo huo huo. Wakati wa ufalme mpya, ramani hiyo ilitunika kujenga Tell - el - Amerna na sehemu

nyingine ambako barabara zilikutana kwenye pembe mraba ingawa mji wenyewe ulikuwa haukupangwa vizuri kama Lahun.

Ingawa ni ukweli usiopingika kuwa Misri ilitoa mchango mkubwa katika mambo ya ujenzi, ni vigumu kuona athari ya ujuzi huo duniani kote. Ama kwa hakika mafundi wengi wa ujenzi katika nchi mbalimbali wametumia na wanaendelea kutumia safu za nguzo, piramidi na nguzo ndefu ambazo zilitoka Misri. Ni rahisi kuona jinsi nguzo zilizojengwa pamoja huko Sakkara na huko Beni Hassan zinavyofanana na nguzo zilizojengwa baadaye Uyunani na Urumi. Kitu kinachojulikana ni kwamba sanaa ya ujenzi ya wakati wa Mafarao iliingia Afrika kupitia Unubi kwanza. Kutoka Unubi, ufundi wa kujenga piramidi, milango mikubwa pamoja na vitu vingine na ufundi wa kutumia vyombo vidogo vilivyochongwa kwa ujuzi ulienea sehemu nyingine.

Mchango wa Wamisri katika utamaduni

Sehemu hii ya mchango wa Misri ya wakati wa Mafarao katika fani ya utamaduni haiwezi kudhihirishwa katika kila hali. Wamisri walitoa mchango mkubwa katika sanaa, fasihi na dini.

Fasihi

Wamisri waliendelea namna ya kuandika kwa kutumia ishara na alama nyingi zitokanazo na mazingira ya Kiafrika. Hivyo tunaweza kusema kuwa walivumbua wao wenyewe maandishi hayo bila kuiga. (tazama Utangulizi).

Wamisri wa kale walijieleza kwa kutumia michoro ya picha. Baadaye ishara hizi zilipewa alama zilizolingana na sauti na alama hizi zilipofupishwa baadaye zikawa ndio mwanzo wa maandishi ya kutumia alfabeti.

Uhusiano wa kitamaduni na maandishi ya Kisemitiki ulianza Sinai, ambako kulijitokeza namna tofauti za kuandika kwa kutumia ishara zilizofanana na maandishi ya picha. Labda hii ndiyo ilisaidia uvumbuzi wa alfabeti ya sasa ambayo ilipokelewa na Wayunani na kuenea Ulaya. Licha ya hiyo, Wamisri wa kale walivumbua vifaa vya kuandika. Uvumbuzi wao wa karatasi za mafunjo ulipokelewa na watu wa jamii za kale. Hii ni kwa sababu karatasi hizo zilikuwa nyepesi na zenye kuweza kukunjwa na mtu aliweza kuviringisha pamoja hati nyingi. Uvumbuzi huu ulisaidia kueneza ujuzi na maarifa. Kuna maandishi mengi tangu nyakati za Mafarao juu ya kila sehemu ya maisha ya Misri kama vile nadharia za dini, fasihi, hadithi, michezo, ushairi na mazungumzo. Fasihi ni mchango muhimu wa Misri ya kale katika utamaduni.

Mifano mizuri ya fasihi ya Misri ni ile iliyoandikwa wakati wa kipindi cha kati cha mwanzo na mwanzoni mwa Ufalme wa Kati. James Henry Breasted, mtaalamu wa mambo ya Misri, anafikiria kuwa fasihi hii ilikuwa ni dalili ya mwanzo wa kukomaa kifika na kijamii huko Misri. Alikielezea kipindi luki kuwa ni mwanzo wa dhainira inayomfanya mtu aweze kujadiliana na nafsi yake juu ya asili na mwanzo wa

vitu. Mfano mwingine wa fasihi ya wakati huo ni kazi iliyoandikwa na “Mkulima Mwenye Ufasaha” ambayo inazungumzia hali ya kutoridhika na jamii na hali ya ardhi. Kazi hii inaweza kuchukuliwa kama hatua ya kwanza ya inapinduzi na demokrasia.

Mwisho, inaonekana kuwa kazi nyingine za fasihi ya Misri zipo mpaka leo. Hii imetokana na hadithi nzuri sana za fasihi ya Kiarabu. Misingi ya fasihi hii inaonekana katika fasihi simulizi ya Misri. Kuna vitu vinavyofanana katika hadithi ya Ali Baba na Wezi Arobaini iliyomo kwenye kitabu cha “*The Arabian Nights*” na katika hadithi mmoja ya wakati wa mafarao iitwayo “kuchukuliwa na Joppe.” Pia kuna mambo yanayofanana katika hadithi ya “Sindbad Baharia wa Baghdad” na katika hadithi ya “Baharia Aliyepotea Baharini” iliyoandikwa wakati wa Mafarao wa Ufalme wa Kati.

Sanaa

Katika uwanja wa sanaa, Wamisri wa kale walieleza hisi zao kwa kutumia njia nyingi ikiwa ni pamoja na kuchora sanamu, kupaka rangi, kufinyanga na kujenga. Walionyesha katika sanaa yao mambo ya dunia, matukio na imani yao ya matumaini katika maisha baada ya kifo. Sanaa yao ilieleza mambo mengi kwa vile iliwasilisha vitu ambavyo walikuwa wakiamini kwa dhati. Waliamini kuwa mtu hafi dalili za kuishi zinapoisha. Wanadamu huendelea kuishi kikamilifu hata baada ya hapo. Lakini ili kuendelea kuishi, binadamu alihitaji mwenzi wake. Ndiyo maana maiti walihifadhiwa au, kama haikuwezekana, walichonga katika sanamu zilizofanana na watu waliokufa. Sanamu hizi za wanaume na wanawake pamoja na picha za makaburi, zilitengenezwa ili kuendeleza maisha ya watu baada ya kufa. Katika sanamu, macho yalichongwa kwa ndani ili yaweze kuona vizuri zaidi na nyusi zilitengenezwa kwa shaba au fedha. Mboni za jicho zilitengenezwa kwa jiwe gumu jeupe lenye kung’aa na kiini cha jicho kilitengenezwa kwa utomvu wa miti. Hii ililitaji ufundi mkubwa na uzoefu katika utengenezaji wa chuma. Ufundi huu unaonekana katika sanamu nyingi za kila kipindi cha historia kilichogunduliwa katika machimbo mengi.

Katika sanaa za mambo madogo madogo, Wamisri wa kale walitengeneza hirizi, mihuri, mapambo na vitu vingine vya thamani ambavyo ni vizuri sana ingawa ni vidogo. Mara nyingi hivi vitu vidogo ndivyo vilienea na kupendwa Afrika, Mashariki na Asia na hata Ulaya. Ni kuenea kwa vitu hivi ndiko kumetuwezesha kujua uhusiano uliokuwapo kati ya Misri na nchi nyingine hapo zamani.

Dini

Dini ni mchango mmojawapo wa Misri katika fani ya falsafa. Wamisri wa kale walizua nadharia mbalimbali juu ya mwanzo wa maisha, nguvu ya vitu vilivyo

kwenye mazingira, imani ya jamii katika vitu hivyo, miungu na jinsi inavyoathiri fikra za binadamu, utakatifu wa mfalme, kazi za makasisi katika jamii na imani kuwa maisha hayana mwisho na kuendelea baada ya kifo.

Wamisri walikuwa na uzoefu mkubwa katika falsafa na waliathiriwa kiasi kikubwa na fikra za dini. Matokeo ya athari hiyo yanaonekana nje ya nchi yao mpaka leo. Wanahistoria wanaweza kuona kwa uralisi athari hiyo katika vitu fulani vya Wayunani na Warumi vinavyohusu mambo ya dini, kwa mfano jinsi Mungu Isis alivyopendwa na kuheshimiwa katika utamaduni wa Wayunani na Warumi wa kale.

Kuenezwa kwa Utamaduni wa Mafarao: Dhima ya ujia wa Wasiria na Wapalestina


Wafoeniki walikuwa na dhima maalum na muhimu katika kueneza utamaduni wa Mafarao.

Tunaweza kuona jinsi Misri ilivyoathiri Ufoeniki kwa kuchunguza uhusiano wa kiuchumi na kitamaduni kati ya nchi hizo mbili. Uhusiano huo ulianza kuonekana wakati biashara na uvumbuzi vilipoanza kukua kabla ya nyakati za ufalme ili kukidhi mahitaji makubwa ya wakati huo. Hata uvumbuzi wa kuandika ambacho ni chombo muhimu cha mawasiliano ulitokana na sababu za kiuchumi na dini. Wamisri walipaswa kushirikiana na Wafoeniki ili waweze kuagiza mali ghafi waliyohitaji sana kama vile mbao ambazo zililhitajika kwa ujenzi wa sehemu takatifu na sanamu za dini.

Pamoja na vitu vingine, athari ya utamaduni wa Misri katika elimu ya Biblia ni kubwa. Uhusiano wa biashara na utamaduni kati ya Misri na upande wa Mashariki wa Mediterani uliendelea elfia ya pili na ya kwanza kabla ya wakati wetu. Huu ndio pia wakati wa Ufalme wa Kati na Mpya na ndicho pia kipindi cha falme za mwisho mwisho. Uhusiano huo ulizidi baada ya Misri kupanuka kisiasa na kijeshi ua ruwaza ya sanaa ya Misri inaonekana katika sehemu nyingi huko Siria na Palestina katika sanamu za wanyama wenye umbo la binadamu na katika mapambo. Ubadilishanaji wa zawadi ulisaidia kukuza uhusiano wa kitamaduni na biashara katika sehemu inayopakana na bahari ya Mediterani na kueneza vipengele mbali mbali vya utamaduni wa Misri katika sehemu nyingine.

Maandishi ya ishara yameonekana katika maandishi ya Wasemiti wa Mashariki ya Mediterani. Wataalamu wamelinganisha alama maalumu za maandishi ya Wamisri (alama zilizotumika kabla ya kufika Sinai) na alfabeti ya Wafoeniki. Herufi nyingi katika maandishi hayo zilikuwa zimetokana na picha na ishara na zilirahisishwa kwa namna iliyofanya zifanane na herufi za alfabeti zilizofuata baadaye. Herufi hizo ndizo asili ya alfabeti ya Wafoeniki na ndizo pia asili ya herufi za alfabeti iliyotumika Ulaya.

Huu mchango mkubwa wa Misri ya Mafarao ambao ulienezwa kupitia jamii za zamani za Mashariki ya karibu, leo hii umeipa Ulaya utamaduni unaofanana na ule wa wakati wa Wayunani.



Misri wakati wa Wayunani

Wakati Alexander Mkuu alipofariki, himaya yake ilikuwa na nchi za Macedonia, sehemu kubwa ya Asia Ndogo, mashariki ya pwani ya Mediterani, Misri na upande wa Mashariki toka Asia hadi Punjabu. Baada ya kifo chake kilichotokea mwaka - 323, falme tatu ambazo zilikuwa zimeanzishwa na majemadari wake zilikwishakuwa imara kiasi cha kuweza kutawala dola hiyo: Ukoo wa Antigonid ulitawala Macedodia, ukoo wa Seleucid ulitawala Asia, sehemu iliyokuwa zamani dola ya Uajemi, na ukoo wa Ptolemy ulitawala Misri.

Ukoo wa Ptolemy ulitawala Misri kwa muda wa karne tatu na ulianzisha mambo ambayo yalikuwa tofauti na vipindi vingine vya historia ya nchi hiyo.

Serikali mpya nchini Misri

Wakati wa utawala wa ukoo wa Ptolemy ambao ulikuwa na zaidi ya watawala kumi na wawili, Misri iliathiriwa sana mwanzoni na vitendo vya watawala hao wa kigeni na siasa yao mpya. Baadaye watawala wa Delta walishirikishwa polepole katika utawala huo.

Ulinzi wa mji mkuni, ambao kwa mara ya kwanza katika historia ya Misri, labda tangu wakati wa utawala wa ukoo wa Ptolemy II na kuendelea, uliwekwa Alexandria kando ya bahari. Ulinzi huu uliwafanya watawala wajenge jeshi la nchi kavu na la majini lililokuwa kubwa zaidi kuliko mengine yote yaliyokuwa Mashariki ya Mediterani. Ili kupata mbao za kutosha kwa ujenzi wa meli walipaswa kuzuia ujenzi wa kiholela huko Misri. Aidha walianzisha mashamba ya serikali kwenye bonde la mto Nili na kuagiza mbao toka Ejjani na visiwani. Kitu kinachojulikana sana katika shughuli zao za mjini ni kuanzishwa kwa vituo vya kuwinda tembo kote pwani ya Afrika hadi Somalia na ujenzi wa meli za kusafirishia wanyama hao. Ujenzi wa meli hizo uligharimu kiasi kikubwa sana cha fedha. Wakati wa utawala wa Ptolemy wa tatu, Hippalus alivumbua jinsi pepo za kaskazi na kusi zinavyovuma. Hii ilifupisha safari za kwenda India na kuzifanya ziwe zenye gharama ndogo na zenye usalama zaidi. Uhusiano wa kibiashara uliongezeka, na ukoo wa Ptolemy ulifanya kila ulichoweza kukuza uhusiano kati ya Bahari ya Sham na Delta. Wakati wa utawala wa Ptolemy wa Pili, mfereji uliochimbwa na Darius wa kwanza tangu kingo za kushoto

ya mto Nili hadi maziwa ya Bitter uliongezwa urefu kwenda chini na hata meli kubwa ziliweza kupita. Katika jitihada za kukuza uhusiano huu Ptolemy wa Pili alianzisha pia njia-bahari kati ya Coptos iliyoko Thebaid na Berenice iliyoko Bahari ya Sham.

Siasa ya mambo ya nje ya ukoo wa Ptolemy iligharimu kiasi kikubwa cha fedha. Gharama hizi zilipaswa kufidiwa na mapato ya hazina ya mfalme. Njia moja ya kutatua tatizo hilo ilikuwa ni kulinda uchuni vizuri zaidi na kusimamia uuzaji wa vitu nchi za nje. Vitu vilivyouzwa nchi za nje viliorodheshwa na kushughulikiwa na wajumbe wa mfalme tu. Kwa vile uzalishaji wa vitu vya kuuza nchi za nje uliongezeka, kulizuka sera ya kuanza kulima sehemu ambazo zilikuwa hazijalimwa. Kazi zote hizi ziligharimiwa na mfalme. Lakini mfalme hakujishughulisha na ustawi wa jamii za wakulima wa Misri.

Njia nyingine ya kuweza kupata fedha za kutosha kununulia silaha na kuagiza bidhaa ilikuwa ni kuuza huko Mediterani bidhaa za Afrika kama vile pembe, dhahabu manyoya ya mayai na mbuni. Bidhaa hizi zilinunuliwa kusini mwa Misri, katika pembe ya Afrika na kuuzwa tena Mediterani. Bidhaa nyingine zilinunuliwa kutoka Bahari ya Hindi kama vile mbao ambazo zilikuwa hazipatikani kwa urahisi, rangi, hariri na inawe ya thamani na kuuzwa tena Uyunani na Mashariki ya Mediterani.

Wiwanda vya kusindika vilikuzwa sana katika sehemu ya Delta na katika mkoa wa Alexandria. Hatua zilichukuliwa kupata sufu na kuingiza nchini kondoo kutoka Uarabuni na wa Milesia. Alexandria ndio mji peke yake uliotengeneza karatasi za inafunjo. Ufundi wa kutengeneza kioo ulifikia kiwango cha juu sana na njia mpya za vioo hivyo ziligunduliwa wakati wa ufalme wa ukoo wa Ptolemy. Kwa muda wa karne nyingi, Alexandria ilisifika kama kituo cha kutengeneza vyonbo vya kioo. Hapo Alexandria palikuwa pia na ujuzi mwingi wa kushughulikia madini kama vile dhahabu, fedha na shaba. Vyombo vya kuwekea maji vilivyotengenezwa huko vilithamimiwa sana.

Ili kukabili matatizo yote haya ya fedha, ilihitajika fedha yenye thamani ya juu. Fedha hiyo ilipaswa kulinganishwa na viwango vya fedha nyingine za kimataifa ili kukuza biashara na sehemu nyingine za Uyunani. Hili lilikuwa jambo jipya Misri. Hivyo, sera mpya kabisa ya fedha ilianzishwa. Benki kuu ilijengwa Alexandria ikiwa na matawi katika miji mikuu ya wilaya na matawi madogo katika vijiji vikubwa. Kulikuwa pia na benki za watu binafsi ambazo zilisaidia uchumi wa taifa kwa namna fulani.

Wageni walikuwa na nafasi tofauti kijamii, kisiasa na kiuchumi ukilinganisha na wenyeji na walipendelewa zaidi. Wafanyakazi wa ngazi za juu wa baraza la mfalme, wajumbe wa serikali, maafisa wa jeshi na askari walikuwa wageni. Katika kilimo wageni waliweza kumiliki ardhi kwa urahisi zaidi kuliko Wamisri.

Kitu kilichoonekana zaidi katika serikali dini hii mpya kilikuwa ni hekalu la Alexandria lililoitwa "Serapeion" ambalo lilikuwa limejengwa mashariki ya mji. Hatuna habari nyingi kuhusu ujenzi wa hekalu hili lakini wanahistoria wa Kirumi wameeleza kuwa lilikuwa limejengwa sehemu ya juu na ili kulifikia kulikuwa na njia

ya ngazi yenye vidato mia moja. Tangu karne ya tatu kabla ya enzi zetu, imani kwa Serapis ilikuwa inaenea haraka kwenye visiwa vya ziwa la Ejiyani. Karne ya kwanza ilipofika, watu kila mahali walikuwa wakiwatukiza Serapis na Isis kama wakombozi. Miungu hao wawili waliabudiwa nchi za mbali. Isis aliabudiwa mpaka Uruk huko Babylonia na Serapis aliabudiwa mpaka India.

Mji maarufu pwani karibu na Misri

Alexandria ulijengwa wakati wa utawala wa ukoo wa Ptolemy. Ni mji uliostawi sana hata ukawa siyo mji mkuu wa Misri peke yake bali pia mji mkubwa kuliko yote Uyunani. Ingawa Misri ilikuwa imeshindwa katika vita na kuingizwa katika dola ya Makedoni, iliendelea kumvutia sana Alexander ambaye alitaka kuanzisha huko Misri miradi mikubwa ya ujenzi wa miji. Inasemekana kuwa Alexander alitaka kujenga mji mkuu wa dola yake Misri. Zaidi ya hayo, elimu ya Misri ilisifika sana hata wasomi wa himaya yote walikuwa wakienda kuishi Alexandria. Wakati wa utawala wa ukoo wa Ptolemy, Alexandria ulikuwa ndio mji wa wasomi sehemu ya Mediterani.

Mahali pa kujenga mji mpya palichaguliwa na Alexander Mkuu yapata mwaka - 331 wakati akitoka Memfisi kwenda katika oasisi ya Ammonium (Siwa) kupata ushauri wa nabii mashuhuri aliyekuwa katika hekalu la Anion. Alexander aliyutiwa na mahali pazuri kati ya Mediterani kaskazini na ziwa Mercotis upande wa kusini. Mahali hapa palikuwa mbali na inabwawa ya inatope lakini palikuwa karibu na sehemu ya rutuba ya mto Nili. Sehemu hii ilikuwa ina kijiji kidogo kilichoitwa Rakotisi. Mawimbi na dhoruba yalikuwa hayakifikii kijiji luki kwa vile kilikuwa kimekingwa na kisiwa cha Faros.

Msarifu majenzi inmoja alichora ramani ya kukiungisha kisiwa cha Faros na bara kwa kutumia ukuta inpana wa inawe ulioitwa Heptastadion kwa vile ulikuwa na urefu wa stadia saba (karibu meta 1200). Ukuta huu sasa umezaina chini ya matope pande zote mbili.

Ujenzi wa ukuta huu ulifanya ziwepo bandari mbili. Bandari ya mashariki iliitwa "Portus Magnus" ambayo ilikuwa kubwa kuliko bandari ya magharibi ambayo iliitwa "Portu Eunostos" au bandari ya "Rudi Salama." Kulikuwa pia na bandari ya tatu kwenye ziwa Mareotis iliyotumika kwa biashara ya ndani.

Chini ya utawala wa Ptolemy wa kwanza aliyeita Soter, mji mkuu wa shughuli za siasa ulikuwa Memfisi. Lakini inasemekana kuwa baada ya maiti ya Alexander kupelekwa mji mkuu mpya, Ptolemy wa pili alihamishia hapo makao makuu ya ufalme wake ambapo yaliendelea kuwa kwa muda wote.

Mji mkuu ulikuwa umegawanywa katika wilaya tano kila moja ikiitwa kwa herufi tano za kwanza za alfabeti ya Kiyunani. Kwa bahati mbaya hatuna maelezo mengi kuhusu wilaya hizi. Makazi ya mfalme yalichukua karibu theluthi moja ya mji yakiwa yanapakana na bandari ya mashariki. Sehemu hii ilikuwa ndiyo sehemu ya mji iliyovutia zaidi na makazi ya mfalme yalizungukwa na bustani na visiwa vizuri pamoja na mabanda ya kufugia wanyama ambao walikuwa wamechukuliwa toka

sehemu zote zilizojulikana wakati ule. Wilaya hii pia ilikuwa na maktaba, jumba maarufu la maonyesho na makaburi ya wafalme.

Lugha nyingi zilizungumzwa mitaani katika mji huo. Lugha iliyotumika zaidi ilikuwa ni Kiyunani pamoja na lahaja zake tofauti. Watu walioishi kwenye vitongoji vya wenyeji walitumia Kimisri. Lugha kubwa kwenye vitongoji vya Wayahudi zilikuwa ni Kiaramikiki na Kihibrania. Lugha nyingine za Kisemiti zilikuwa zinatumika pia.


Alexandria ilisifika pia kwa ajili ya baadhi ya majengo ya ukumbusho ambayo ni vigumu sasa kujua yalikuwa yamejengwa sehemu ipi. Baadhi ya sehemu muhimu za mji huu wa Kiyunani siku hizi zimo chini ya bahari na sehemu nyingine imo chini ya mji wa sasa. Kwa hiyo tunapozungumzia majengo ya ukumbusho ya mji wa zamani, tunategemea habari tulizopata toka kwa waandishi wa zamani pamoja na vitu ambavyo wanaakiolojia wameclumba.

Kusini ya kisiwa cha Faros, katika lango la bandari ya mashariki, kulikuwa na jumba la taa lililokuwa maarufu sana (*Faros*). Jumba hili lilikuwa mojawapo ya maajabu saba ya ulimwengu. Majumba ya taa mengine yaliojengwa zama hizo yalijengwa kwa kufuatisha umbo na jina la jumba la taa la Alexandria.

Jumba hilo liliharibiwa kabisa mnamo karne ya kumi na nne. Kwa hiyo tunaweza tu kukisia umbo lake na jinsi lilivyojengwa kutokana na maelezo machache ya kipindi cha Wayunani na maelezo ya wanahistoria wa Kiarabu. Pia sarafu za zamani na michoro iliyoko kwenye sanamu mbalimbali za mawe vinaonyesha kidogo umbo la jumba hilo. Umbo hili lilibuniwa na Sostratus wa Cnidus yapata mwaka -280, wakati wa utawala wa Ptolemy wa Pili. Jumba hilo lilikuwa na urefu wa karibu meta 135 na lilikuwa limejengwa kwa mawe ya chokaa zaidi na kupambwa kwa mawe ya kung'aa na shaba.

Jumba la Makumbusho lilikuwa na maktaba kubwa na ndilo lilikuwa kitu kikubwa kuliko vyote vilivyofanywa na ukoo wa Ptolemy huko Alexandria. Demetrius wa Phaleron, mkimbizi toka Athens, ndiye aliyemshauri Soter, Ptolemy wa kwanza, kuanzisha jumba hilo. Strabo anaeleza kuwa mpango wa majuniba ulikuwa kania ifuatayo: "makazi ya mfalme yana jumba la makumbusho ambalo lina njia na ukumbi mkubwa ambamo wanafilolojia wanakula pamoja. Kulikuwapo na fungu la fedha kwa ajili ya kutunza chuo na kasisi aliyeteuliwa na wafalme kuliifadhi jumba la makumbusho. Hii inaonyesha kuwa wataalamu waliishi katika taasisi hiyo. Walipata malazi na chakula bure na hivyo walitumia muda wao wote kufanya utafiti na kusoma bila kufanya kazi ndogondogo.

Demetrius wa Phaleron alikuwa pia amemshauri Soter, kuanzisha maktaba ambayo ingalijumuisha utamaduni wote wa sehemu hiyo kwa kununua na kunakili miswada kwa mpango maalum. Baada ya muda mfupi, zaidi ya majuzuu 200,000 yalikusanywa. Uongozi wa maktaba uliwekwa chini ya wataalam mashuhuri wa Kiyunani. Kulikuwa pia na maktaba ndogo zaidi katika hekalu la Serpeion iliyokuwa na vitabu 45,000. Jumba la Makumbusho la Alexandria lilikuwa ndiyo taasisi 6.1



6.1 *Mnara wa taa wa Alexandria*

iliyokuwa kubwa kuliko zote wakati huo huko Uyunani. Maktaba iliyoweza kushindana na ya Alexandria ilikuwa ni ile ya Pergamon. Kutoka maktaba ya Alexandria tumeweza kupata vitabu vya tamthiliya ya mada za tanzia iliyotungwa na Aeschylus, tamthiliya ya mada za ramsa iliyotungwa na Aristophanes, utenzi wa Pindar na Bacchylides na vitabu vya historia vya Herodotus na Thucydides.

Baadhi ya washairi walikuwa na nyadhifa mbili, kama makatibu na pia kama wasaidizi wa mfalme. Callimachus aliandika kazi zake nyingi wakati akiwa katika maktaba ya Alexandria. Kazi hizo ni pamoja na mashairi maarufu ya kuomboleza yaitwayo "Fungo la Berenice" (*The Lock of Berenice*). Katika mashairi hayo, Berenice, mke wa Ptolemy III aliapa kuwapa miungu fungo moja la nywele zake iwapo mume wake angerudi salama kutoka vitani huko Syria. Mfalme aliporudi, malkia alitimiza kiapo chake. Siku iliyofuata, fungo la malkia lilipotea toka hekaluni. Wakati huo huo, imajimu Canon alikuwa ndiye amevumbua kundi jipya la nyota ambalo aliliita "Fungo la Berenice" na akazua hadithi kuwa miungu wenyewe walikuwa wamechukua fungo hilo toka hekaluni na kuliweka mbinguni. Mpaka leo, kundi hilo la nyota bado linaitwa "Dhuaba" ("Coma Berenices"). Callimachus aliheshimu kitendo chema cha mtaalam huyo wa elimu ya nyota na kuandika shairi hilo ambalo lipo katika tafsiri ya Kilatini iliyofanywa na Catullus (aliyeishi mwaka - 84 mpaka -54).

Wanajiografia, wanakosinografia (wataalam wa mazingira ya ulimwengu) na wanajimu walitoa mchango mkubwa katika maendeleo ya sayansi huko Alexandria. Baadaye tutaona kuwa walivumbua vitu vingine kwa kujifunza kutoka kwa Wamisri na sio tu kutoka maktaba ya Alexandria.

Eratosthenes, ambaye ni mtangulizi katika uwanja wa sayansi ya jiografia, alizaliwa Krone yapata mwaka -285. Mnamo mwaka -245, Ptolemy alimpa kazi ya kuwa mkutubi kazi ambayo aliifanya mpaka alipokufa. Mafanikio makubwa aliyoyapata yalitokana na jaribio lake la kupima mzunguko wa dunia kwa kuangalia uhusiano kati ya kivuli kilichoonekana kwenye saa ya Alexandria wakati jua likiwa kaskazini zaidi mwa Ikweta na kutoweka kwa kivuli katika Syne (Aswan). Uchunguzi wake ulionyesha kuwa mzunguko wa dunia nzima ulikuwa stadia 252,000 (yaani kilometa 46,695). Vipimo hivi vinazidi kwa 1/7 ukubwa halisi wa mzunguko huo ambao ni kilometa 40,008. Ni Eratosthenes ndiye aliyerodhesha nyota 675.

Mwanajiografia, Strabo (mwaka - 63 mpaka + 24) ameandika historia ya kwanza iliyo na mpango mzuri juu ya Misri. Strabo alizaliwa Kappadocia na aliishi muda mrefu zaidi wa maisha yake huko Roma na Asia Ndogo. Mwishowe aliamia Alexandria. Ingawa Strabo aliishi wakati wa Warumi, kazi yake nyingi ilifanyika wakati wa Wayunani. Makala yake ya jiografia yapo katika vitabu 17 na kati ya hivyo theluthi mbili ya kitabu cha mwisho ni juu ya Misri.

Jiografia na unajimu vinahitaji ujuzi mkubwa wa hisabati. Kati ya watu mashuhuri waliofanya kazi katika Jumba la Makumbusho alikuwamo mwanahisabati mashuhuri aliyeitwa Euclid (aliishi mwaka -330 mpaka -275). Yeye ndiye alikuwa wa kwanza

kukabidhiwa idara ya hisabati na aliandika kitabu maarufu juu ya unajimu (kiitwacho “*Phaenomena*”) na kitabu cha msingi juu ya jiometri (kiitwacho “*Element*”) ambacho kilikuwa kitabu cha msingi juu ya somo hilo. Baadaye kitabu hicho kilitafsiriwa katika Kilatini na Kiarabu. Archmedes wa Syracuse (aliyeishi mwaka -287 mpaka -212) mmojawapo wa wanahisabati waliofundishwa na Euclid, aligundua uhusiano kati ya kipenyo na mzunguko, kanuni ya kuzunguka na kanuni ya mvutano. Mchango wake mkubwa katika hisabati na ufundi wa mashine ulikuwa ni uvumbuzi unaojulikana kama “rafadha ya Archimedes,” ambayo bado inatumika Misri kupandisha maji.

Apollonius wa Perga, mwanajiometri maarufu alikwenda Alexandria akitokea Palmyra mwaka -240 kufanya kazi katika chuo cha hisabati kilichokuwa Alexandria. Alionyesha ubingwa wake na akawa anatambuliwa Uyunani kama bingwa kuliko wengine wote katika hisabati.

Kuanzia karne ya tatu chu kikuu cha hisabati cha Alexandria kilipata sifa zake maalumu na kuwa kituo kikuu cha hisabati ya Wayunani.

Theophrastus ambaye aliishi wakati wa Ptolemy I anajulikana kuwa ndiye mwanzilishi wa elimu ya mimea kutokana na kazi zake juu ya historia na muundo wa mimea.

Mwanahistoria, Diodorus Siculus alitembelea Misri mwaka -59. Kitabu chake cha kwanza cha historia kinaitwa “*Maktaba ya Historia*” (Library of History) na kiliandikwa kwa Kiyunani. Kitabu hicho kinaeleza habari za ngano, wafalme wa Misri na desturi za nchi hiyo. Diodorus anasema kuwa binadamu alionekana kwa mara ya kwanza hapa duniani huko Misri. Anasema katika sura ya kwanza, aya ya kumi: “Katika mwanzo wa dunia binadamu wa kwanza alizaliwa Misri kwa sababu hali ya hewa ilikuwa nzuri na kwa sababu ya mto Nili.”

Waganga pia walienda kufanya kazi kwenye Jumba la makumbusho na katika maktaba. Uhuru waliokuwa nao katika masomo yao uliwawezesha kupiga hatua kubwa katika ujuzi wao juu ya umbo la mwili wa binadamu na katika utaalumu wa kupasua maiti.

Herophilus wa Asia Ndogo aliyekwenda Misri mwanzo wa karne ya tatu kabla ya wakati wetu ndiye alikuwa wa kwanza kugundua uhusiano kati ya mapigo ya moyo na kipigo cha mshipa wa damu na kutofautisha kati ya mshipa ya arteri na vena. Majina mengine aliyotoa bado yanatumika hadi leo kama vile “duodenum” na “torcular herophili”.

Erasistratus, intaalamu mwingine wa upasuaji naye alizaliwa Asia ndogo na alipokuwa Alexandria alifanya uvumbuzi juu ya umbo la moyo.

Sifa ya Chuo cha Tiba cha Alexandria ilivuma kwa muda mrefu. Kuna shairi la maombolezo ambalo limehifadhiwa, huko Milan linalomsifu mganga aliyehusika kwa inaneno yafuatayo: “Nchi yake ilikuwa ni Misri, nchi tukufu”.

Jinsi miaka ilivyopita, asili ya Misri ilizidi kuonekana. Manetho, Mmisri wa Samanud alikuwa mmoja wa wasomi mashuhuri. Aliishi mwanzo wa karne ya tatu

kabla ya enzi yetu. Kazi yake inayojulikana zaidi inaitwa “*Aegyptiaca*”. Kazi hii ingetuwezesha kujua historia ya kale vizuri zaidi kuliko maandishi mengine yote lakini kitabu kizima hakikupatikana. Sehemu za kitabu hicho ambazo zimepatikana zinaonyesha majina ya wafalme wakiwa wamepangwa kufuatana na nasaba zao na kuonyesha muda ambao kila mtawala ulidumu. Wanahistoria wa leo wanafuata mtindo huo huo wa kuorodhesha.

Athari ya Misri kwa utamaduni wa Kiyunani

Tumeona kuwa wafalme wa ukoo wa Ptolemy walifanya bidii kukuza uhusiano kati ya Misri na Bahari ya Hindi. Katika uvumbuzi wa nchi, wataalam hawakubaliani kama Wamisri walikuwa na scra maalum ya kujaribu kutafuta mto Nili unakoelekea na kujaribu kuutumia kusini zaidi kwa safari za mbali na pia kama njia ya kusafiria na ya biashara. Hata hivyo kuna uhakika kuwa upelelezi ulifanyika kusini ya Misri. Timesthenes, jeinadari wa jeshi la majini toka Philadelphia alitembelea Unubi; Aristo alikwenda kupeleleza pwani ya Arabia, Satyrus alifuata pwani ya Afrika mpaka sehemu iliyoko kusini ya Rasi ya Guardafui.

Kuna maandishi yanayoonyesha mambo yaliyotcndeka wakati wa safari hizi na maandishi haya yamewasaidia wasomi kama vile Agatharchides kupata habari zaidi wakati wa utafiti.

Wapelelezi hawa walikuwa wakifuata mfano wa watu mashuhuri. Mwaka -500, Hacatacus wa Miletus, inwana jiografia wa kwanza toka Uyunani kutembelea Misri aliandika kitabu cha kwanza kinachoeleza juu ya dunia. Kwa bahati mbaya, sehemu tu za kitabu hicho cha jiografia ndizo zimebaki. Akiwa Misri mtaalamu huyo alisafiri mbali hadi Thebes na inawezekana kuwa katika kitabu chake alizungumzia kwa kirefu juu ya Misri. Hacatacus alidhani dunia ni duara kama sabani na Uyunani ilikuwa katikati. Aliigawa dunia katika makotinenti mawili, Ulaya na Asia. Asia ilikuwa na Misri pamoja na Afrika ya kaskazini yote ambayo kwa wakati huo ilijulikana kama Libya. Alidhani kuwa kwa upande wa kusini, mto Nili uliunganika na mto Osceanus ambao ulizunguka dunia nzima. Herodotus wa Halikarnassus alikuwa ameishatembelea Misri mwaka -450. Aliteremka kusini hadi Elefantine ambapo alidhani ndio mpaka kati ya Misri na Ethiopia. Katika kitabu chake cha pili kati ya vitabu vyake tisa vya Historia, Herodotus anazungumzia Misri peke yake. Ndiye alikuwa mtaalamu wa kwanza wa jiografia kutaja jina la Meroe kwa vile yeye binafsi alikutana na Wameroc huko Aswan.

Herodotus pia alifikiri kuwa dunia ilikuwa duara lakini hakukubaliana na Hecatacus kuwa dunia ilikuwa mviringo ua kwamba ilikuwa inazunguka na mto Osceanus. Herodotus aliigawa dunia katika makotinenti matatu: Ulaya, Asia na Libya (yaani Afrika) na alisema kuwa Libya ilikuwa imezungakwa pande zote na bahari isipokuwa pale inapopakana na Asia.

Diodorus Siculus alieleza njia inayofuatwa na mto Nili katika kitabu cha kwanza cha kazi zake. Yeye alifikiria kuwa mto Nili ulikuwa unaanzia Ethiopia na ulikuwa

na visiwa vingi kimojawapo kikiitwa Meroe. Diodorus aliandika juu ya Ethiopia tu katika kitabu chake cha tatu. Nchi hiyo inaitwa Sudani siku hizi. Strabo kama Diodorus alisema kuwa Meroe kilikuwa kisiwa na alizungumzia kwa kirefu juu ya wakazi wa Meroe.

Inashangaza kuona kuwa Wamisri waliiga mambo ya Wayunani polepole. Inaonekana kuwa Wamisri hawakukubali kwa urahisi utamaduni wa kigeni. Uhusiano wao na wafalme wa ukoo wa Ptolemy ulikuwa wa namna ya pekee, ukilinganisha na Wayunani ambao walimhusudu sana mfalme. Hata hivyo wakati huo Kiyunani kilikuwa tayari ni lugha ya kimataifa na kwa kuwa ilikuwa rahisi zaidi kuiandika kuliko Kimisri, kilienea haraka sana ingawa Kimisri kiliendelea kutumika katika mambo fulani. Wanaakiolojia wameona kuwa kuna mafunjo mengi yaliyoandikwa katika Kimisri cha zamani na katika Kiyunani. Sheria ya Kiyunani iliathiri sheria ya Misri polepole sana. Kalenda ya Misri ilitumika badala ya ile ya Kiyunani. Zaidi ya hayo, kwa kutumia Kiyunani, urithi wote wa Misri ulienea katika sehemu za dunia ambako haungaliweza kufika kama lugha hiyo mpya haingalitumika.

Sanaa ndicho kitu pekee cha Misri na Afrika ya watu weusi ambacho kiliweza kuathiri utamaduni wa Wayunani. Hii ilishangaza sana. Wayunani waliendelea kupenda tamthiliya kama walivyokuwa wakifanya walipokuwa Athens na walipokuwa Misri walijenga majumba ambayo yalionyesha jinsi walivyopenda tamthiliya.

Kwa hivyo mwanzoni, mitindo ya sanaa na vitu walivyopenda Wayunani waliokuwa Misri vilifanana na vile vilivyopendwa na jamii nyingine za Wayunani wa dola hiyo kubwa. Ni kweli kuwa vitu vilivyozalishwa katika viwanda vidogo vidogo vya Alexandria vilifanana na vile vya Uyunani kwa namna fulani na vilionyesha kufanana na mitindo ambayo haikuwa ya Kiafrika. Kuna mifano mingi ya sanaa hii maarufu katika Jumba la Makumbusho la Alexandria ikiwa ni pamoja na sanaa mashuhuri ya kichwa cha Alexander ambayo ni ya mtindo wa wasanii waliokuwa wanafunzi wa Lysippus. Lakini kulikuwa na mitindo mipya iliyobuniwa Alexandria; mmojawapo ukiwa ule mtindo ambao wanaakiolojia waliuita kwa jina la Kitaliano "*sfumato*". Mtindo huu ni mchanganyiko wa rangi zenye kung'aa na rangi hafifu katika sehemu laini za mwili na uso bila kujali sana kuonyesha nywele au mashavu. Mara nyingi mashavu yalitengenezwa kwa mawe yanayong'aa ambayo ni rahisi kutumia kwa muundo usio mgumu walioupenda wasanii wa Alexandria. Nywele na mashavu vilipoongezwa, vilichorwa kwa rangi.

Katika Misri ya wakati wa Mafarao, mto Nili ulichorwa kama intu ninene mwenye matiti yaliyo na mimea inayoota majini pamoja na mafunjo. Mimea hii huota katika bonde la mto Nili. Wayunani waliuchora mto huu kama mtu mwenye nguvu na mwenye ndevu akiwa ama amekaa au ameinama pamoja na viboko, mamba au na sananu ya mtu aliye na mwili wa Simba na kichwa cha mwanamke. Hizo ni nembo za Misri. Michoro ya wafalme pia ilifuata mtindo luohuo. Upakaji wa rangi ulifanana sana na ule wa Wayunani wakati wote wa karne ya nne na ya tatu lakini karne ya pili, picha zilionyesha mitindo ya Kimisri pamoja na ya Kiyunani mathalani katika kaburi

mojawapo la Anfushi huko Alexandria. Chumba cha mazishi kimejengwa na kimepambwa tangu mlangoni kwa nchanganyiko wa mitindo ya Misri na Uyunani.

Sanamu zilizofanywa kwa mawe madogo zilionekana kwanza inashariki ya Mediterani na labda Alexandria penyewe. Njia nyingi za mawe zilizo na picha zimegunduliwa ndani ya Alexandria na karibu yake. Sanamu iliyo maarufu zaidi imechongwa jina la Sefhilos na katikati ya mraba kuna kichwa cha mwanamke akiwa na mlingoti na niti wa kushikilia tanga. Kichwa hiki kina taji la kitambaa cha kichwani kinachofanana na gubeti ya meli. Inadhaniwa kuwa hii inaonyesha jinsi mji wa Alexandria ulivyokuwa.

Bila shaka kati ya vitu na mitindo mipya inayoshangaza sana katika sanaa ambayo Wamisri waliiga kwa Wayunani ni kule kuenea kwa sanamu ndogo zilizokuwa za kuchekesha au zilizokuwa mbaya sana au za kweli. Sanamu hizo zilionyesha mambo yanayofanyika katika maisha ya kila siku na zilionyesha pia Wamisri na Waafrika weusi. Picha ndogo za watu zilizotengenezwa kwa shaba, mawe ya kung'aa, udongo mwekundu au plasta zilitengenezwa kwa ajili ya watu wa kawaida. Lakini picha zenye thamani kubwa zaidi zinaonyesha kuwa mada hizi za mambo ya kila siku zilipendwa.

Misri wakati wa Wayunani: uhusiano wa Libya

Manibo fulani fulani ya utamaduni wa Wayunani yaliingia Afrika ya kaskazini toka Misri kupitia Sarenaika (Cyrenaica) schemu ya mashariki ya Libya. Hii haikuwa mara ya kwanza kwa utamaduni wa Kiyunani kuonekana Kirenaika. Tunafahamu kuwa Wayunani toka kisiwa cha Dorian kilichoko Thera walihamia Sarenaika, ambapo mwaka -631 walijenga Kirene ambayo ilikuwa koloni la kwanza. Hii ilifuatiwa na makoloni mengine manne, bandari ya Kirene (ambayo baadaye iliitwa Apollonia) Taukira, Barka (ambayo sasa inaitwa Al-Merg) na Euthesperdes. Makoloni haya, hasa Kirene, yalitokana na utamaduni wa Wayunani na yalipitia mabadiliko ya kisiasa ambayo yalikumba kila mji wa Kiyunani. Kirene ilipojengwa, ndipo ulianza utawala wa ufalme wa Battiad ambao ulianguka mwaka -440 kwa sababu ya mizozo ya wenyewe kwa wenyewe. Baadaye kulikuwa na mzozo kati ya mabwanyenye na wapenda urasimu. Sarenaika iligeuka kuwa nchi ambamo watu walikuwa hawaelewani.

Dunia yote ya wakati huo ilikuwa inaingiliwa na matatizo wakati Alexander Mkuu alipoishambulia Misri wakati wa masika ya mwaka - 332. Alexander aliendelea magharibi mpaka Paraetoniuni iitwayo Mars-Matruh siku hizi akiwa njiani kwenda katika oasisi ya Siwa kupata ushauri kutokana na ubashiri wa Ammon¹. Kirene, na labda miji iningine pia ilijaribu kulinda uhuru wao kwa kupeleka mabalozi kumlaki Alexander huko Paraetoniuni na kumweleza kuwa miji yao ilikuwa ina utifu kwake. (Hii ni kwa vile watawala wa miji hiyo hawakuelewa Alexander alitaka nini hasa na

¹ Mwandishi wa sura hii akisaidiwa kuhusu somo juu ya Libya na Dk. Mustafa Kamal Abd Ek Alim.

walikuwa wakijaribu kumzuia asishanbulie Sarenaika). Lakini hawakuweza kulinda uhuru wao siku zote kwani mwaka -323 baada ya kifo cha Alexander, Ptolemy, alipokuwa bado gavana wa Misri, alitumia mizozo ya wenyewe kwa wenyewe iliyokuwapo Kirene ili kuiteka Sarenaika na hivyo kuanzisha kipindi cha utawala wa Wayunani katika nchi hiyo. Kulikuwa na kipindi kifupi tu cha uhuru mwaka -258 mpaka -246. Wafalme wa ukoo wa Ptolemy walitawala Sarenaika tangu mwaka -322 mpaka 96 wakati ambapo Ptolemy Apion (mtoto wa Ptolemy Euergetes II) aliyekuwa akitawala Sarenaika alipoitoa nchi hiyo kwa wananchi wa Roma na kuiunganisha na Krete na kuwa jimbo la Roma.

Chini ya utawala wa wafalme wa ukoo Ptolemy, miji ilipewa majina mapya. Majina mengine yalikuwa yale ya wafalme wa ukoo huo. Kirene ilibaki na jina lake lakini Taukira ulipewa jina jipya la Arsinoe (leo unaitwa Tokra) na baudari ya Barka ilipewa jina la Ptolemais (leo unaitwa Tolmeta) ambao hatimaye ulikuwa kitovu cha jiji badala ya bandari ya Barka. Badala ya Euhesperides, kulizuka mji mpya ambao uliitwa Berenice (leo hii unaitwa Benghazi) kwa heshima ya binti ya mfalme toka Sarenaika na mke wa Ptolemy III. Bandari ya Kirene ilipewa hadhi ya mji na kuitwa Apollonia (leo hii mji huo unaitwa Susa).

Watu wa Sarenaika walikuwa na mataifa mbalimbali. Mijini kulikuwa na Wayunani na watu wasiokuwa Wayunani wakiwemo Wayahudi na wageni wengine wengi. Nje ya miji, watu wa vijijini (*georgoi*) walikuwa Walibya, wazaliwa wa huko, pamoja na askari wa kukodiwa ambao walikuwa wamehamia huko kama wafanyakazi.

Watu wa vijijini (*georgoi*) walilima sehemu za Sarenaika zilizoweza kulimwa ikiwemo ardhi ya mfalme (gébasiliké) ardhi ya mji (gêpolitike) na ardhi ya wananchi wazaliwa wa Libya. Mfumo huu ulileta ugomvi kati ya wananchi wazaliwa wa Libya na wawezi wa Kiyunani.

Wakati wa kipindi cha Wayunani, Sarenaika ilikuwa nchi muhimu sana kiuchumi na ilihesabiwa kuwa ghala la dunia ya wakati huo. Wengine wamesema kuwa Kirene ilipeleka zawadi ya "*medimni*" 800,000 za nafaka huko makao makuu ya Uyunani kwa ajili ya kulisha wakazi wa mijini wakati wa njaa ya niwaka -330 mpaka -326. Mengi yamesemwa juu ya sufuri ya Kirene, juu ya uzalishaji wa farasi na "*silphium*" maarufu ya Sarenaika ambayo ilikuwa mali ya wafalme wa Battiad tu na baadaye ikawa mali ya wafalme wa ukoo wa Ptolemy tu.

Hii zawadi ya nafaka si ushahidi pekee wa uhusiano wa karibu uliokuwapo kati ya Wayunani wa Sarenaika na wale wa Uyunani kwenyewe. Inajulikana kuwa wanafalsafa na wataalamu mashuhuri wa Kirene walitoa mchango mkubwa wa kisomi huko Uyunani hasa wakati wa karne ya nne. Kutokana na uhusiano huu wa karibu wa kisomi kati ya Kirene na Athens, Kirene ilisaidia kuendeleza falsafa na elimu nyingine kusitawi katika nyanda Sarenaika. Hapo ndipo ambapo Shule ya mawazo ya wanafalsafa ijulikanayo kama "Cyrenaics" ilipositawi sana. Kikundi hicho cha wanafalsafa kilikuwa cha wafuasi wachache wa Socrates na kiliongozwa na



6.2 Cleopatra VII

Aristippus (mwaka -400 mpaka -365), mjukuu wa mzee Aristippus aliyekuwa rafiki na mwenzi wa Socrates. Hili vuguvugu la kisomo lililikuwa bado linaendelea wakati wa Wayunani. Kwa mfano Callimachus (mwaka -305 mpaka - 240) na Eratosthenes (mwaka -275 mpaka - 294) walikuwa kati ya watu waliohamia Alexandria toka Kirene kusaidia kuendeleza sayansi na fasihu huko Alexandria. Watu hao walishiriki kwenye kazi za chuo, Jumba la Makumbusho na Maktaba na waliongeza hadhi ya taaluma katika mji wa Alexandria na kuufanya mji huo kuwa kitu cha harakati za taaluma wakati wa Wayunani.

Sanamu nyingi za wanafalsafa, washairi na miungu tisa wa usanii zimegunduliwa Kirene. Imepatikana pia sanamu ya Demosthenes ingawa inafanana sana na ile iliyokuwa Roma. Hii inaonyesha jinsi Wayunani wa Kirene walivyomthamini msemaji huyu mashuhuri wa Kiyunani.

Mifano mizuri ya vinyago vya Alexandria imepatikana kati ya sanamu mbalimbali za mawe zilizoko Kirene. Sanamu zilizochongwa wakati wa Wayunani zinafanana sana na kile kinachoitwa sanaa ya Kiyunani ya Alexandria. Hatushangai kuona kuwa ufundi uliotumika Alexandria uliigwa kiasi fulani na Kirene. Tunaona pia kuwa vinyago vilivyochongwa na Wayunani wa Sarenaika vilifanana sana na vile vya Alexandria. Tukilinganisha sanamu za kuchonga zinazohusu uzazi toka Sarenaika na sanamu za maiti waliohifadhiwa Misri, tunaona kuwa zinafanana sana. Hata sanamu za wakati wa Warumi zinaonyesha kuwa zimeigwa kutoka zile za wakati wa utawala wa ukoo wa Ptolemy.


Vitu vilivyotengenezwa na wafuuzi pamoja na sanamu zilizotengenezwa kwa udongo mwekundu vilitoka Kirene. Sanamu hizi zilitengenezwa katika viwanda vidogo vidogo ambavyo vilikuwa vimeanza kwa kuiga na kutengeneza sanamu kama zile za Wayunani kwa kutumia udongo mwekundu lakini baadaye viwanda hivi vilivunbua mifumo ya aina ya peke yake. Uchunguzi wa sanamu hizi ni wa manufaa kwa vile unaonyesha mambo mbalimbali ya maisha ya kila siku ya wakazi wa Sarenaika, hasa wakazi wa mjimi.

Katika mambo ya dini, taratibu za heshima za ufalme wa ukoo wa Ptolemy ziliingia pia Sarenaika. Hii inaonekana tukichunguza maandishi mengi yanayowasifu wafalme na malikia wa ukoo wa Ptolemy. Miji ya Sarenaika pia ilichukua taratibu hizo za Serapis na mahekalu ya miungu Isis na Osiris yameonekana katika miji ya Kirene na Ptolemis.

Taratibu lizi za mchanganyiko toka Uyunani na Misri zilienea Tripolitania toka Sarenaika. Tripolitania haikutawaliwa na wafalme wa ukoo wa Ptolemy mpaka wakati uliotangulia kipindi cha Warumi. Hekalu la miungu Serapis na Isis liligunduliwa Leptis Magna na uchunguzi unaonyesha kuwa taratibu za heshima kwa miungu Isis na Isiacrites zilifuatwa pia huko Sabrato. Taratibu za heshima kwa Isis na Serapis zilienea magharibi. Isis alikuwa anajulikana zaidi na Serapis alianza kuwapa watu wa zamani tumaini jipya la maisha bora zaidi.

Mambo mengi yaliyoandikwa juu ya Sarenaika ya zama hizi yanawahusu

Wayunani peke yao kwa vile taarifa kuhusu Walibya, wenyeji na mahali hapo, jinsi waliyoathiriwa na utamaduni wa Wayunani si nyingi na hazipatikani kwa urahisi. Tunajua kuwa Walibya ambao walikuwa wenyeji walifukuzwa kutoka sehemu zenye rutuba pwani na kuzuliwa ndani ya nchi sehemu za shamba. Hivyo wenyeji hawakuwapenda Wayunani walioivamia nchi yao. Hata hivyo utamaduni wa Kiyunani ulistawi kwa karne tatu na kuenezwa sehemu nyingine Afrika ya Kaskazini.



Misri chini ya utawala wa Warumi

Jinsi Urumi ilivyoshirikiana na Misri hadi kuitawala

Misri ilitoka katika utawala wa wafalme wa ukoo wa Ptolemy na kutawaliwa na Warumi taratibu bila wao kujitambua. Kwa muda mrefu tangu utawala wa Ptolemy Philadelphus, uhusiano ulikuwa wa kirafiki sana. Ptolemy Philadelphus ndiye alikuwa mtu wa kwanza katika ukoo huo kutiliana sahihi mkataba wa urafiki na Roma na alianzisha ofisi ya Ubalazi huko Roma mwaka -237. Miaka hamsini baadaye, Ptolemy Philopator alikuwa upande wa Roma wakati wa vita kati ya Roma na Hannibal (mwaka -218 mpaka - 201). Roma pia ililipa fadhila hizo kwa kuokoa uluru wa Misri wakati Antiochus III alipovamia nchi hiyo mwaka -168. Hata hivyo, kisha kufikia hatua hii, Roma iliweza na ilizoea kuingilia wazi wazi mambo ya ndani ya Misri hasa wakati wa miaka ya mwisho ya utawala wa ukoo wa Ptolemy. Nia ya hila za Cleopatra VII na majemadari wa Kirumi kati ya mwaka -51 na -30 ilikuwa ni kuwafanya Wamisri wakubaliane na siasa ya Roma. Cleopatra wa saba alimuunga mkono kikamilifu rafiki yake Mark Anthony na hivyo alipoteza kabisa ufalme wake mara Octavian alipomshinda Mark Anthony mwaka -31.

Mambo ambayo mtawala mpya aliyafanya Misri yalionyesha waziwazi umuhimu ambao Roma iliweka kwa jimbo hili jipya la himaya yake. Roma iliweka Misri vikosi vitatu, vyenye askari takribani 15,000. Kazi ya wanajeshi hao ilikuwa ni kuidhibiti na kurudisha hali ya utulivu katika nchi hiyo ambamo ghasia ilikuwa imczagaa wakati wa miaka ya mwisho ya utawala wa ukoo wa Ptolemy, hata ikasababisha kuharibiwa kabisa kwa mji wa Thebes mwaka -88.

Mfalme wa Kirumi aliyetawala misri baada ya ukoo wa Ptolemy alijaribu kuchukua kikamilifu nafasi ya watawala waliointangulia. Pamoja na madaraka yake ya kiserikali alikuwa pia na wadhifa wa kuwa kiongozi wa dini na alijenga mahekalu mengi wakati wa enzi zake. Aliongoza pia mambo ya kila siku yaliyohusu ustawi wa jamii wa wauanchi na kutumia jeshi siyo tu kudumisha amani ila pia kutengeneza ufereji ambao ulikuwa umeharibiwa vibaya wakati wa fujo zilizotokea mwishoni mwa utawala wa ukoo wa Ptolemy.

Utawala wa Warumi

Mfalme wa Kirumi aliiga mfumo wa utawala wa ukoo wa Ptolemy huko Misri. Aliitawala nchi hiyo kama mali yake binafsi na mapato ya nchi nzima yalikuwa chini ya mfalme. Hali hii ambayo ilishamiri enzi za Augustus ndio ulikuwa msingi wa siasa ya unyonyaji alioanzisha Misri. Siasa hii iliendelezwa na wafalme waliofuata Augustus ingawa katika ukusanyaji kodi baadhi yao walionya juu ya madhara yanayoweza kutokea kwa sababu ya kutoza wananchi kodi kubwa. Mmoja wa wafalme hao aliwahi kumkemca msinainizi kuwa “kondoo hukatwa manyoya na siyo kuchunwa.”

Madaraka ya mfalme yalionekana wazi kwa vile yeye binafsi ndiye aliwateua wakuu wa majimbo. Mfalme pia ndiye aliyewachagua maofisa wengine (kama hakimu mkuu) ambao walitawala kwa jina lake. Kuna jumba dogo la kitawala linaloonyesha jinsi Misri ilivyokuwa na mtindo wa pekee. Ilikuwa ndiyo nchi peke yake katika himaya nzima ambako miaka ilihesabiwa kufuatana na utawala wa mfalme na haikupewa majina ya “inabalozi” waliokuwa wakitawala kwa kipindi fulani. Mtindo huu ulikuwa kama ule wa wakati wa utawala wa Ptolemy na Mafarao na inkuu wa nchi aliheshimika Misri kuliko alivyoheshimika mahali pengine popote katika himaya hiyo.

Kitawala, nchi ilikuwa imegawanywa katika wilaya, kila wilaya iligawanywa katika tarafa na kila tarafa ilikuwa na vijiji kadhaa. Mikoa ya Misri ya kaskazini ilikuwa ineunda kanda ambayo iliitwa Thebaid na kanda hiyo ililingana na Heptanomis au kanda ya mikoa ya Misri ya kati na sehemu ya ndomo wa mto Nili. Kila mkoa ulitawaliwa na rukuu wa nkoa ambaye aliitwa “strategos” na chini yake kulikuwa na mshauri wa mambo ya utawala ambaye alikuwa karani wa mfalme. Cheo hicho kilitunika pia katika mji wa Ptolemais. Maofisa wadogo zaidi waliongoza sehemu ndogo kama zamani.

Serikali kuu ilikuwa mpya. Makao makuu yalikuwa Alexandria, mji wa zamani wa wafalme. Watunishi hawa wa serikali walikuwa wote ni Warumi na waliteuliwa na mfalme. Cheo cha juu zaidi kilikuwa cha mkuu wa utawala ambaye alikuwa mkuu wa idara zote ikiwa ni pamoja na hazina, jeshi na mahakama. Uamuzi wake uliweza tu kubatilishwa kwa rufaa kwa mfalme mwenyewe. Ili kuinsaidia kutimiza wajibu wake, mkuu wa utawala alikuwa na Baraza ambalo lilikuwa na waheshimiwa wa Kirumi. Mwanasheria na Hakimu walimsaidia kusimamia sheria, Bwana Fedha alimsaidia mkuu wa utawala kuendesha mfuko wa mfalme na mheshimiwa mmoja aliongoza utawala wa mahekalu. Wilaya nyingi pamoja zilikuwa chini ya baraza la watu watatu ambao walikuwa waheshimiwa wakiwa na cheo cha hakimu. Gavana ndiye pekee aliyekuwa jaji na ofisa mwenye madaraka yote ya utawala na aliweza kumwachia madaraka mtu mwingine, hasa mkuu wa mkoa, lakini jaji ndiye aliyewajibika. Alitembelea nchi kila mwaka ili kuainua kesi ngumu. Ziara hii iliitwa “*conventus*”. Alitumia sheria ya Kirumi kwa wananchi wenye uraia wa Urumi lakini

kwa watu wengine alitumia sheria ya kigeni ambayo alizingatia mila na desturi za nchi ingawa sheria hiyo ilikuwa na hitilafu katika vipengele vyake vingi.

Mifano hiyo peke yake inaonyesha kuwa Warumi walikuwa na uwezo wa kubadilisha kwa kiasi fulani mfumo wa utawala uliokuwapo Misri wakati wa ukoo wa Ptolemy. Tangu mwanzo wa utawala wa Augustus, kulikuwa na sababu nyingine zaidi za kuweza kuleta mabadiliko. Utawala wa akina Ptolemy uliweka madaraka makubwa katika Serikali Kuu, na maofisa wengi walikuwa wakilipwa mshahara kutokana na kazi walizokuwa wakifanya za kusimamia mashamba. Mashamba hayo yalipitana ukubwa kufuatana na madaraka ya kila afisa. Jeshi pia lilikuwa na mfumo wa kurithi na lilikuwa na haki ya kurithi ardhi ya kulima ambayo ukubwa wake ulipimwa kufuatana na vigezo mbaliinbali (kama alikuwa Myunani au Mmisri; au kama alikuwa na farasi wa kulisha au la, n.k.).

Wakoloni wa Kirumi walipenda kuwagombanisha watu wa mukundi tofauti walioishi Misri kwa kufuata mila za zamani na kuwapendelea Wayunani kwa kuwapa nafasi bora katika jamii, si kwa mambo ya kila siku tu bali hata kisheria pia. Wamisri walilipa kodi ya kichwa iliyoitwa "*laographia*". Kila mtu anayeishi alitakiwa kulipa kodi hiyo isipokuwa Wayunani. Watu waliokuwa wakiishi katika miji mikuu ya mikoa walilipa kodi ndogo zaidi kuliko wale walioishi vijijini. Baadhi ya watu wa mashambani hawakumiliki ardhi ya kulima. Kwa hivyo jambo muhimu lilikuwa ni kwa mtu kutoka katika familia ya Kiyunani iliyosoma. Mtu aliweza kudai ametoka familia ya namna hiyo kama aliweza kuonyesha vyeti kuwa babu zake wawili walikuwa wamehudhuria shule ya Kiyunani. Hivyo, katika mfumo huo mpya, haki za Wamisri zilipuuzwa au kuondolewa kabisa. Nia ya siasa hiyo ilikuwa kuunda tabaka lenye nguvu la watu wa tabaka la kati waliokuwa wananufaika na kuimarika kwa dola hiyo.

Inafaa tuzungumze pia hadhi maalumu ya miji iliyokuwa ikijitegemea wakati wa utawala wa ukoo wa Ptolemy kama vile Ptolemais wa Misri ya Juu na Naucratis mji wa zamani na wenye sifa nyingi uliokuwa kwenye Delta ya mto Nili. Mji wa tatu ulikuwa Alexandria ambao ulikuwa bandari kubwa kuliko zote kwenye bahari ya Mediterani na ulishindana na Roma kwa wingi wa wakazi na umuhimu wake. Hata hivyo mji huu ulinyang'anywa bunge lake na ukawa ni kituo cha jeshi la majini lililjulikana kama jeshi la Augusta Alexandria. Jeshi la Warumi lilikuwa na kambi Nicopolis karibu sana na mji wa Alexandria. Watu wa Alexandria walijulikana sana kwa mbinu zao za kuelewana na watawala wavya na hawakuchelewa kuonyesha mbinu hizo.

Misri chini ya Warumi

Kwa muda mrefu vituo hivi vya dola ya Warumi viliachwa bila kuingiliwa. Gharama za utawala wa mikoa ambao ulihakikisha kuwepo kwa amani katika nchi zilitokana na kodi ya ngano iliyoitwa *annona* ambayo ilizusha migomo na maasi mara nyingi.

Tiberius (mwaka + 14 mpaka +37) alitawala baada ya Augustus na alipunguza vikosi vya jeshi vilivyokuwa Misri na kubakiza viwili tu. Wakati wa utawala wa mfalme aliyemfuata, machafuko yalitokea kwa mara ya kwanza kati ya Wayunani wa Alexandria na Wayahudi wengi waliokuwa wakiishi mjimi humo.

Uhusiano kati ya Serikali ya Wayahudi wa Misri uligeuka kuwa mbaya zaidi wakati wa maasi huko Uyahudi. Vespasian aliyekuwa mfalme wa Syria (kati ya mwaka +69 mpaka +79) alilakiwa kwa shangwe Alexandria. Vespasian aliyaita majeshi yaliyokuwa Nicopolis ili kushambulia Jerusalem. Baada ya mji wa Jerusalem kuharibiwa wakati wa utawala wa Traja (mwaka +98 mpaka +117) Wayahudi wa Misri waliasi na kuitoka Alexandria. Machafuko haya yalikumbukwa kwa muda mrefu na kuitwa “Vita vya Wayahudi”. Jemadari Marcus Turbo alipowashinda waasi, koloni la kiyahudi katika Alexandria lilitoweka.

Tukiachilia mbali machafuko haya, tunaona kuwa karne ya kwanza na niaka ya mwanzo ya karne ya pili ya dola hiyo ilikuwa ni kipindi cha amani na maendeleo ya kiuchumi. Mfalme Nero (mwaka +54 mpaka +68) aliwatuma wavumbuzi kwenda ufalme wa Meroe. Roma ilikuwa na uhusiano mzuri wa biashara na Meroe. Vespasian alipendwa sana Alexandria na watu walisema kuwa alikuwa anaweza kulanya miujiza. Trajan alipunguza vikosi vilivyokuwa Misri na kubakiza kimoja tu. Hii inaonyesha kuwa hali ilianza kuwa shwari. Alichimba mfereji kati ya Mto Nili na Bahari ya Sham ili kupanua biashara na sehemu za mashariki na kushindana na misafara iliyokuwa inaenda Syria kupitia nchi ambazo hazikuwa chini ya utawala wa Warumi. Hatua hizi zote zilinfuata Alexandria ambayo ndiyo ilikuwa bandari kubwa kuliko zote kwenye bahari ya Mediterani. Njaa ilipoingia, Trajan alipeleka msaada wa dharura wa ngano jambo lilikuwa kinyume cha utaratibu uliokuwepo kwamba Misri ndiyo ilipaswa kulipa kodi ya ngano kwa Roma.

Hadrian (mwaka +117 mpaka +138) alielekea kuipenda sana Misri na mwaka +130 na +131 alitembelea nchi hiyo kwa muda mrefu kidogo pamoja na mkewe. Hadrian ndiye aliyejenga upya sehemu za mji wa Alexandria ambazo zilikuwa zimeharibiwa wakati wa vita vya Wayahudi. Yeye ndiye aliyejenga pia mji wa Antinopolis huko Misri ya kati kwa ukumbusho wa Antinous. Kulikuwa pia na sababu halisi za kumfanya ajenge mji huo ambao baadaye ulipewa hadhi ya mji huru na ukawa ni kituo kilichokuwa ndani ya Misri ambacho kilikuwa na uhusiano mzuri na Roma. Kilikuwa pia ni kituo ambapo misafara ya biashara kati ya Bahari ya Sham na sehemu ya bonde la mto Nili ilianza.

Hali ya uchumi ya wakulima na watu wenye mashamba madogo, ambayo imeelezwa kwa kirefu kwenye nyaraka, ilionyesha wazi kuwa siasa ya Warumi ya kupendelea tabaka la kati ingeweza kuleta matunda mabaya. Watu wa tabaka la chini walikuwa maskini zaidi na machafuko yalianzia kwao. Tukio mojawapo lilikuwa ni kuuawa kwa kiongozi mkuu wa utawala huko Alexandria. Hii ilitokea wakati wa utawala mrithi wa Hadrian, Antoninus Pius (+139 hadi +131). Mkuu huyo alikuwa ametumwa Misri kuziua fujo. Mwana mrithi wa Antoninus Pius, Marcus Aurelius,


Mwanafalsafa na mwenye upendo mkubwa wa watu (+161 hadi +180) alikabiliwa na hali mbaya zaidi wakati wachungaji walioishi katika Delta walipoasi. Maasi hayo yaliongozwa na kasisi wa Kimisri aliyeitwa Isidor. Yasemekana kwamba waasi hao walipata ushujaa wao kutokana na tambiko lililofanywa kwa kula watu. Walipigana kishujaa kutetea haki zao za kutaka kuishi vizuri zaidi na kutaka kutambuliwa kama taifa. Watu wa Alexandria walikuwa upande wa Warumi kwa vile wao walikuwa wakipendelewa zaidi kuliko Wamisri.

Hali hii ya wasiwasi kati ya Roma na Misri iliendelea hata baada ya mabadiliko yaliyoletwa na Septimus Severus (mwaka +193 mpaka +211) ambaye aliwarudishia watu wa Alexandria bunge lao (*boule*). Bunge hili lililokuwa ishara ya madaraka yao ya ndani lilikuwa limevunjwa na mfalme Augustus. Caracalla, aliyetawala baada ya Augustus (+211 hadi +17) alipotembelea Alexandria alikasirika sana kwa vile wakazi wa mji huo walimzonea. Hivyo, kwa kiburi, alitoa amri vijana wote wakusanywe, akisingizia kuwa alitaka kuwaandikisha jeshini, wakati ambapo nia yake hasa ilikuwa kuamuru wauawe. Baada ya mauaji hayo majeshi yalihama kutoka makazi yao ya Nicopolis na kukaa Alexandria ili kuwalazimisha watu wajisalimisha.

Ukatili na umwagaji damu ulioendeshwa na mfalme Septimus Severus ulifunika hata yale mema aliyofanya. Kwa mfano ni wachache wanaokiri kuwa yeye ndiye alipitisha katiba ya Antoni mwaka +212. Kufuatana na katiba hii, watu wote waliokuwa wakiishi kwenye dola walipewa uraia na ubaguzi kati ya raia wa Roma na watu wa mikoani uliondolewa. Ukiacha maofisa toka ng'ambo raia wa dola ya Roma walikuwa wachache sana Misri kabla ya mabadiliko hayo ya katiba. Aghalabu hata lao maofisa wachache walikuwa ni Wamisri waliopata kulitumikia kwa muda wa miaka ishirini au ishirini na mitano na kutokana na utunishi wao mzuri waliporudi kwao Misri baada ya kustaafu walirejeshewa uraia wao na kurejea katika miji ya nyumbani kwao kama watu mashuhuri na wenye sifa kubwa.

Katiba mpya iliondoa huu uraia wa pande mbili kwa wakazi wa dola hii. Kila mtu alipaswa kufuata sheria ya Roma na mfumo wa jamii ulibadilika sana. Hata hivyo athari za mabadiliko hayo hazikujitokeza sana nchini Misri. Mabadiliko ya katiba yaliambatana na mfumo mpya wa utawala. Alexandria ilipoanzisha tena bunge lake, kulitokea mabadiliko ya hadhi ya miji. Miji mikubwa ikawa majiji na ikapewa madaraka ya kusimamia tawala za majimbo yake. Misri haikuwa tena ghala ya nafaka kwa dola nzima. Tangu mwisho wa karne ya pili na kuendelea, Afrika (ambayo sasa inaitwa Maghreb) ndiyo ikawa ghala ya chakula. Hii inaonyesha kuwa Misri ilikuwa imekwisha. Kulizuka mtindo ambao ulianza kuenea: wakulima walianza kuacha mashamba yao na kuenda kuishi jangwani kwa sababu hawakuweza kulipa kodi iliyodaiwa na Serikali.

Mnamo katikati ya karne ya tatu, kulikuwa na matukio makubwa mengi. Marcus Julius Aemilianus mmojawapo wa wakuu wa utawala Misri alijitangazia madaraka ya ufalme mwa +262. Baada ya kutawala miezi michache, alishindwa vibaya sana na Gallienus. Watu wa nje walivamia mpakani na kushikilia kwa muda selicnu chache



7.1 (a) Machimbo yaliyofanywa na watalamu toka Poland huko Kom el-Dikka, Alexandria: mahali pa kuogea pa Warumi.

7.2 Michoro ya Baonit



za Misri. Hii inaeleza kwa nini wakati wa utawala wa Claudius wa pili (mwaka +268 mpaka +270), Mmisri mmoja aliyetwa Thimegenes aliwaita Wapalmyria nchini. Hawa Wapalmyria walikuwa wafanyabiashara mashuhuri katika mji mmoja wa dola, wakiwa na uhuru wa kuendesha mambo yao wenyewe. Malkia wao, Zenobia, bila kuonyesha wazi kuwa amejitenga na Roma alipeleka kikosi cha askari 70,000 kumsaidia Thimegenes. Kikosi hiki kikiungwa mkono na wakazi kiliwasumbua sana askari wa Kirumi. Hata Aurelian alipozima uasi huo na kuwaondoa Wapalmyria, vikundi vya wananchi vilivyokuwa vinapinga utawala wa Warumi vikiongozwa na Firmus, viliendelea kuunga mkono Wapalmyria wachache waliokuwa wamebaki Misri, Wananchi hao walianza pia kushirikiana na Wablemmye, taifa ambalo lilikuwa linaogopwa sana. Wablemmye walikuwa wahamaji waliokuwa wamesambaa Unubi ya chini na walionekana Misri ya Juu wakitoka jangwani ambako walikuwa wakitawala na kuwasumbua wakulima.

Jemadari Probus (mwaka +276 mpaka +282) alifaulu kuwashinda Wapalmyria, Wablemmye na wapigania uhuru wa Misri. Probus alikuwa kwanza kiongozi wa najeshi ya Aurelian: na baada ya Aureliani kufa alishika madaraka ya kutawala. Alifanya bidii kubwa ili kurekebisha hali ya maisha ya wananchi ambayo ilikuwa inaanza kuzorota baada ya utawala wa jadi kulegalega na kufanya uvamizi nje au uasi wa ndani kushangiliwa kama vitendo vya ujasiri. Hii ilionyesha kuwa kulikuwa na unuhimu wa kuwapa wananchi imani inpya ambayo ingaliwafanya waungane zaidi. Probus alinua kufanya hivyo kwani mara tu baada ya kuwashinda maadui zake waliokuwa waneivamia nchi, aliwapangia askari wake kazi za kujenga mifereji na kuendeleza kilimo.

Probus alielewa hali ya nchi na aliiacha huru Unubi ambayo iliweza kushambuliwa kwa urahisi na Wablemmye na wahamaji wengine walioishi jirani na Unubi. Aliomba tu watu wa Unubi wawe tayari kulinda mipaka ya kusini ya dola yake. Kwa ulinzi huo walilipwa fedha kidogo ambayo wafalme wao wadogo walifurahia kupata kama ushuru.

Misri yenyewe iligawanywa katika majimbo matatu ambayo hapo awali yalikuwa epistratejia. Majimbo mawili ya kaskazini, jimbo la Delta na jimbo la Heptanomis (yote pamoja yakiwa na wilaya saba), yaliitwa Aegyptus Jovia na Aegyptus Herculia. Kila jambo lililwekwa chini ya gavana ambaye hakuwa na madaraka juu ya jeshi. Thebaid, jimbo la kusini ambalo lingeweza kushambuliwa kwa urahisi lilikuwa chini ya uongozi wa jemadari kiongozi ambaye alikuwa na madaraka juu ya raia na jeshi. Misri ilipoteza hadhi yake kama jimbo lililokuwa linajitegemea na ikaanza kutumia sarafu iliyokuwa inatumika katika sehemu nyingine zote za dola. Polepole jumuiia yote ilianza kuwa na mifumo iliyokuwa inafanana. Hii iliwafanya wananchi waanze kuepa kulipa kodi wakati kodi ilipoongezeka. Kwa sababu hiyo, serikali ilitoa amri kuwazuia watu wasihame. Hakuna mtu aliyeruhusiwa kubadilisha kazi. Wakulima walipaswa kubakia wakulima na kukaa katika ardhi walipokuwa ili waendeleo kuwa wakodishaji ardhi kwa makabaila wenye kuniliki ardhi. Waungwana nao kwa upande wao

walipaswa kulipa kodi ya kichwa isipokuwa walc tu waliokuwa na wadhifa maalum wa siasa. Hivyo maskini walijiunga na vikundi vya matajiri ili waweze kutetewa kwa maofisa wa kodi. Mara nyingi maskini waliwapa viongozi mali yao wawatunzie. Serikali ilijaribu njia zote za kisheria kuzuia mtindo huu wa watu wenye ardhi kuwagandamiza na kuwanyanyasa wengine lakiini sheria haikuweza kurekebisha mambo kwa vile haikuzingatia sababu zilizoleta mfumo wa namna hiyo. Watu waliomiliki ardhi kubwa walipopewa uwezo wa kukusanya kodi waliyopaswa kulipa kwa serikali? mfumo wa kumiliki mali ukawa umebadilika sana. Mashamba madogo ambayo yalikuwa yakiwapa nguvu watu wa tabaka la kati wakati dola ilipoanza yalitoweka na watu waliomiliki mashamba makubwa walianza kutwaa madaraka. Madaraka hayo yalivunja mfumo wa utawala wa halmashauri za miji na kuleta mfumo mpya wa tabaka tofauti kufuatana na uwezo wa watu kiuchumi.

Athari Ya Dini Ya Kikristo Kwa Jamii Ya Misri

Uzoefu katika mambo ya dini luko Misri ulisaidia kuenea kwa dini nyingine ya wokovu. Dini ya Kikristo ilionekana kama dini ya wokovu katika mambo yake mengi hasa katika nchi ambayo watu walikuwa wanaamini sana juu ya maisha baada ya kifo. Zaidi ya hayo, kwa muda wa karne nyingi, Misri ilikuwa na koloni la Wayahudi na ndiyo maana tangu wakati wa Ptolemy Filedelfa, Biblia ilitafsiriwa katika Kiyunani. Biblia hiyo iliitwa "*Septuagint*". Hivyo misingi ya dini ya Kikristo ilijulikana katika jamii nyingi za Misri tangu zamani na hii ilisaidia kueneza dini hiyo mpya ya Kikristo tangu mwanzo.

Hakuna mambo mengi yaliyoandikwa juu ya mambo hayo ya dini. Kitu cha maana ni kuwa dini ya Kikristo ilienea kama dini nyingine, kama vile dini ya watu walioamini kuwa walijua kila kitu juu ya Mungu au dini iliyoanzishwa na Manes ikiwa ni mchanganyiko wa imani za Zoroastres, Budha na Kristu. Wamisri wamehifadhi mambo ya dini hizi kwenye nyaraka zilizoandikwa kwenye mafunjo na karatasi za ngozi zilipopatikana katika machimbo. Inaonekana kuwa dini ya jadi ilikuwa imeanza kushindwa kukidhi inahitaji ya imani ya watu. Huko Misri, sheria ya dini iliamuru kuwa lugha ya nchi hiyo itumike kama lugha rasmi katika mambo ya dini. Dini ya Kikristo pamoja na dini nyingine mbili zilizotajwa hapo juu zilitumia lugha ya Koptiki na lahaja zake za majina au mikoa. Hii iliwafanya wahubiri wawasiliane na wanyonge ambao walikuwa hawakushirikishwa katika utamaduni wa Wayunani wa tabaka la juu. Hii ilionyesha pia kuwa katika dini, wananchi walipewa nafasi ya kwanza na kwamba utamaduni wa wananchi ambao ulikuwa haukuzingatiwa katika katiba ya Antonius na katika maisha ya tabaka zilizokuwepo ulikuwa unathaminiwa. Kwa upande wa serikali, niwenyeji wa Misri alikuwa ni mtu ambaye hakustahili kushiriki katika utawala. Kwa Wakristo, neno "*Hellena*" lilikuwa na maana ya mpagani au mtu ambaye alistahili kudharauliwa.

Wakristo walionekana kuwa wengi na watu muhimu kufuatana na jinsi wafalme walivyowaadhibu mara kwa mara. Hili lilikuwa ni jambo la kushangaza lakini

lilitokea mara nyingi. Mambo makubwa yaliyofanywa na Decius mwaka +249 mpaka +251 bado yanajulikana Misri. Decius alitoa vyeti kwa watu ambao walikuwa wametoa sadaka ya kipagani mbele ya wakuu wao kwa kuchoma ubani kama ishara ya heshima kwa mfalme. Wale waliokataa kufanya hivyo walidhaniwa kuwa ni Wakristo na waliweza kuadhibiwa kwa kusosa utii. Lakini adhabu kubwa kuliko zote iliyotolewa kwa watu wasioamini imani za kijadi ni ile iliyotolewa na Diocletian mwaka 303. Mwana wa mfalme Diocletian alitumia ukatili na nguvu yake yote. Mateso hayo ndiyo yaliyozusha kipindi cha Koptiki au mashahidi. Huo ndio ulikuwa ushahidi wa mwisho kuonyesha kuwa ilikuwa haiwezekani kupinga kitu ambacho kilikuwa tayari kimeishakomaa. Miaka michache baada ya tukio hilo Constantine alitambua haki ya watu kuwa Wakristo na alianza kazi ngumu na ndefu ya kuwashirikisha Wakristo katika shughuli mbalimbali za dola yake. Hii ilitokea Milan mwaka +313. Tangu hapo maendeleo ya dini ya Kikristo huko Misri yalitegemea uhusiano kati ya Alexandria na Constantinople, mji mkuu mpya wa dola hiyo.

Dhima Mahsusi ya misri katika himaya ya Kikristo

Tangu dola ilipoanza rasmi kuwa dola ya Kikristo, wakati wa utawala wa Theodosius, historia ya Misri iliathiriwa na maoni rasmi ya wafalme ambao walijichukulia madaraka ya kutoa amri kutoka mji wa Constantinople juu ya kanuni gani zifundishwe na zikubaliwe katika dola yote. Kwanza wafalme hao walitaka kuunganisha watu kisheria. Baadaye walitaka kuwe na imani moja kwa watu wote iliyoitwa Othodoksi.

Dini ya Kikristo ina misingi maalum ya imani na tangu karne za mwanzo wa dini hiyo, Wakristo wamekuwa wakikinzana kutokana na jinsi wanavyoelewa na kueleza misingi hii kwa namna tofauti.

Wakati ambapo mambo ya Kanisa yalikuwa yanaendeshwa kwa siri, ugomvi kati ya waumini haukuwa na maana kisiasa lakini jamii ya Kikristo ilipoanza kuwa na watu wengi zaidi katika dola, ugomvi kati ya Wakristo ulihusisha Serikali. Constantine mwenyewe alipaswa kuingilia kati mara nyingi ili kusuluhisha uhusiano mbaya uliokuwapo kati ya vikundi vya Wakristo. Uhusiano huo uliweza kuzusha machafuko kwa kusingizia kuwa chanzo kilikuwa ni tofauti za mafundisho ya elimu ya dini. Constantine alikuwa mtu aliyetaka amri zake zifuatwe, na kwa maoni yake, ubishi katika mambo ya dini ulipaswa kakoma na badala yake pawepo amani na makubaliano juu ya ukweli na sheria. Wale waliotawala baada ya Constantine walifuata siasa yake na siasa hiyo ndiyo ilikuwa kiini cha mvutano wa mara kwa mara kati ya wafalme wa Constantinople na inaaskofu wa Alexandria, kila mmoja akisema kuwa yeye ndiye alikuwa na jukumu la kulinda imani ya kweli.

Dini ya Kikristo katika mji wa Alexandria ilikuwa tofauti na sehemu nyingine za dola. Hii ilitokea mwanzoni kabisa dini hiyo ilivyoendelea kukua. Utamaduni wa Wayunani ambao ulikwishaathiri mji wa Alexandria ulijitokeza hata katika kupokelewa kwa dini hiyo mpya. Dini ya Kikristo haikuvingia kama imani ya

kimapinduzi ila watu walijaribu kutumia dini hiyo kuhalalisha mambo fulani na kuyaunganisha na fikira na falsafa ya zainani. Mawazo hayo hayakuwavutia wananchi wasio Wayunani ambao dini yao ilikuwa zaidi inahusu kuelewa bila kuidadisi. Askofu wa Alexandria alikuwa na uhusiano wa pekee na mapadri wake kwani walikuwa ni kikundi chenye nguvu kama ilivyokuwa wakati kanisa lilipoanza. Ili kudumisha madaraka yake, askofu wa Alexandria aliwategemea sana askofu wa mikoani, yaani askofu wa mikoani yote ukiondoa Alexandria, na yeye ndiye aliwaweka wakfu askofu hao.

Ugomvi mwingi ulitokea kutokana na maoni na matarajio mbalimbali. Ugomvi wa kwanza ulitokea wakati askofu Melecius wa Lycopolis (Asyut) alipowaunga mkono watu wenye msimamo mkali na kukataa kuwaingiza katika kanisa watu ambao walikuwa wamelegalega wakati wa mauaji ya dimi.

Ugomvi mwingine ambao ulikuwa mkubwa zaidi ulitokana na ubishi kati ya wasoni na wanafalsafa mbalimbali kuhusu Kristo kuwa binadamu na Mungu pamoja. Je, Kristo ana hali mbili zisizotengana au hali inoja ya kimungu, utu wake ukiwa tu kwa nje? Je, Kristo ana hali mbili tofauti? Padri Arius wa Sytis alisema kuwa Kristo alikuwa na hali mbili tofauti na Kanisa lilimlaumu. Mtu aliyetetea zaidi umoja wa imani katika mambo ya dini alikuwa ni mtakatifu Athanasius (aliyeishi mwaka +293 mpaka +373) na aliyekuwa Askofu Mkuu wa Alexandria. Wakati wa ugomvi huo, yeye aliwapinga hata wafalme waliokuwa wakimuunga mkono Arius kupinga imani ya nafsi tatu katika utatu intakatifu. Athanasius alitambuliwa na Warumi na Wayunani kama Mlinzi wa Kanisa. Nusu karne baadaye, Askofu Mkuu mwingine wa Alexandria, Cyril, (mwaka +412 mpaka +444) alipinga kanuni za Nestorius, Askofu Mkuu wa Constantinople na alifaulu kumpinga mfalme Theodosius wa pili. Juu ya suala la Kristo, Cyril alisahihisha maoni ya wataalam wa mabo ya dini na akasema kuwa Kristo ana nafsi moja na hali mbili. Baada ya kifo cha Cyril, mtawa Eutyches akisaidiwa na Disocurus, mtawa aliyemfuata Cyril, walipiga hatua zaidi kwa kusema kuwa Kristo alikuwa na hali moja tu. Baraza la Chalisdoni lilipinga kanuni hii mwaka 451. Watu wa Alexandria walijivunia kisomo na utakatifu wa askofu wao. Falsafa hii ilijulikana kama "imani ya hali moja".

Mwaka +451, Baraza la Chalisdoni liliamua kusuluhisha ugomvi huu kwa kutangaza kuwa Kristo alikuwa na hali mbili zilizoungana na hii ilipaswa kuwa kanuni ya imani. Hii ilileta hali ya msukosuko Alexandria. Msukosuko huo uliendelea mpaka Waislamu walipoivamia nchi.

Ugomvi mkali uliosababishga unuwagaji wa damu ulizuka kati ya waumini hasa katika mji wa Alexandria. Watu wa mikoani walisikia mambo mabaya na ya aibu yaliyokuwa yanatokea Alexandria, lakini dini ya Kikristo katika bonde la mto Nili ilifaulu kuonyesha kwa vitendo kuwa ilikuwa ikivutia. Hivyo ziliundwa jamii za dini kama zile za wapagani wa Misri na Wayahudi waliokuwa Misri ambao wameelezwa na Philo. Jamii hizi ndizo zilikuwa misingi ya dini mpya. Tunaweza kuona hatua mbalimbali za imani hiyo mpya ya utawa. Mtu wa kwanza mashuhuri kuanzisha

utawa alikuwa ni Paulo wa Thebes (mwaka +234 mpaka +347). Yeye, pamoja na mfuasi wake Anthony (mwaka +251 mpaka +336), waliyakimbia mambo ya dunia na kuunda kikundi cha watawa wanaojitenga. Mtu mwingine mashuhuri alikuwa ni Pachomius (mwaka +276 mpaka +349) ambaye alikuwa kiongozi na aliunda vikundi ambavyo vilishirikiana katika kazi na wajibu, vikiwa na sheria moja na kuishi pamoja katika maisha ya kijamii. Halafu kulikuwa na Shenout wa Atripa (mwaka +348 mpaka +466) ambaye huko Deir - el - Abyda aliwafanya wanaume na wanawake kuishi kwa nidhamu kali na alianzisha huko Misri mfumo ambao ulifuatwa Ulaya kati ya karne ya tano na ya kumi na tano.

Inaonekana kuwa yale maasi ya Alexandria yalihusu zaidi maswala ya dini. Maasi hayo yalitokea karne ya sita wakati ule ule wa vikundi vya watawa waliokuwa wanajitenga na watu. Constantinople ilikuwa inawalazimisha Wamisri kukubali kanuni za mtaguso wa Chalisidon na kanuni nyingine zilizotolewa baadaye na Constantinople. Kuna sababu nyingi zilizowafanya Wamisri wasipende kanisa lililokuwa tajiri na lenye madaraka makubwa na wakati huo huo likishughulikia imani ya watu. Watu wa Eutyches walioamini kuwa Kristo ana hali moja walikuwa wakiuawa kwa ajili ya imani yao na walipendwa zaidi na watu. Katika karne ya tano, Syria iliwaunga mkono, na karne ya sita, Wasyria, ambao pia walikuwa wanawindwa kwa ajili ya imani yao, walijiunga nao. Wamisri walianza kuchoka na mambo ya tabaka na walianza kuamini kuwa msimamo wao ndio ulikuwa wa kweli na haki. Walionyesha imani hiyo kwa kuandika mara nyingi katika biblia yao isiyotambuliwa na Wakristo na kuonyesha maisha ya Kristo huko Misri. Watu wa Byzantium walionekana kama wageni wasiotakiwa na ambao walikuwa wamekalia Misri bila kukaribishwa na wananchi.

Kuna nyaraka zinazoonyesha jinsi hali ya wananchi katika kila tabaka ilivyokuwa. Kila mahali watu walikuwa wanaogopa, wanaonewa na walikuwa wamechoka. Haishangazi kuona kuwa uchumi ulikuwa unalegalega kwa vile watu walikuwa wamechoshwa na utawala mbaya na usioridhisha. Nchi ilikuwa imegawanywa kwa magomvi na ilikuwa haina uhusiano mzuri na Constantinople.

Baada ya miaka michache, utawala wa Byzantium ulishindwa vitani mara mbili na udhaifu wa utawala huo ulionekana wazi.

Mfaline Chosroes wa pili wa Sassanida alikusudia kuudhofisha utawala wa nguvu ya Byzantine. Wasassanida walikuwa wakitawala sehemu ya kusini ya Arabia na walikuwa wakizuia biashara ya Byzantium katika bahari ya Sham. Walishambulia himaya ya Byzantine toka pande tatu, upande wa Anatolia na Byzantium, upande wa Aleppo na Antioch na upande wa Agaba na Misri na kufika upande wa kusini wa mto Nili mwaka +615. Waajemi nao waliposhambulia Wayahudi waliasi kwa vile walikuwa wamejinasuru kutoka utawala mrefu wa Warumi uliokuwa ukiwakandamiza. Kanisa la wale walioamini kuwa Kristo ana hali moja lilianza kujitokeza bila kujificha na kwa miaka mingi ndilo likawa kanisa rasmi peke yake.

Misri ilipotekwa na Heraclius mwaka +629, watu wa Byzantium walipumua tena

lakini kwa muda mfupi tu kwani walipaswa kulinda koloni ambalo wakati huo lilikuwa gumu sana kutawala. Hofu iliingia tena wakati wa Askofu Mkuu wa Melchite kwa vile Byzantium iliamua kutangaza kanuni mpya za kuunganisha waumini ambazo zilikuwa hazilingani na zile za mtaguso wa Chalisidoni au zile za Roma au hata zile za watu walioamini kuwa Kristo ana hali moja. Toka mwaka +639 na kuendelea, Waislamu walianza kuonekana kuwa tishio kubwa na mwaka +642 Misri ilijisalimisha kwa wavamizi hao wapya ambao waliahidi kuleta usawa zaidi katika hali ya uchumi. Uvamizi wa Waarabu ulianzisha kipindi kipya katika historia ya Misri.



Umuhimu wa Uubi: kiunganisho baina ya Afrika ya kati na Mediterani

Kwa kuitazama ramani ya sura ya nchi ya Afrika tu tunaweza kuona dhahiri umuhimu wa Unubi kama kiungo baina ya Maziwa Makuu na bonde la Kongo lililoko Afrika ya Kati kwa upande mmoja na Mediterani kwa upande mwingine. Sehemu kubwa zaidi ya bonde la Nili iliyo sambamba na Bahari ya Sham hadi "Ukumbi" wa Unubi pamoja na jangwa la Sahara kwa upande wa magharibi na jangwa la Uarabuni au Unubi kwa upande wa mashariki, imezileta pamoja tamaduni za zamani za Mediterani na za Afrika ya watu weusi.

Kuvumbuliwa kwa sanamu ya shaba nyeusi ya kichwa cha Agosto huko Meroe karibu kilometa 200 kutoka Khartoum, hakustaajabishi. Kwa hivyo Unubi imezagaa njia panda za Afrika na ni mahali zinapokutana tamaduni za mashariki, magharibi, kaskazini na kusini mwa Afrika pamoja na zile za Mashariki ya Karibu, Asia ya Mbali na Ulaya ya Mediterani.

Kihistoria, kama maandishi ya zamani ya Kimisri yanavyodhihirisha, wasafiri waliotoka kaskazini waliingia Unubi kusini kidogo mwa Al-Kab. Kwa muda mrefu, jimbo la Misri lililo katikati ya Thebe na Aswan liliitwa Ta-Seti, "Nchi ya Upindi" (kwa Kimisri cha zamani) na nyaraka za kale za maandiko ya picha yanatumia istilahi hiyo kwa lile eneo tunalolijua kama Unubi. Ndiyo kuserua Unubi Kuu ya awali kabisa ilianzia kwenye maeneo ya mchanga ya bonde la Nili ambapo "mchanga wa Unubi" hakutana na mawe ya chokaa kwa upande wa kaskazini. Hapo awali Maporomoko ya Kwanza yalikuwa katika eneo hili. Ni vigumu kutanubua mipaka yake ya kusini, lakini utafiti wa kiakiolojia unaonyesha kuwa kuanzia elfia ya nne kabla ya enzi yetu, utamaduni uleule au uliohusiana nao ulienea kote, kutoka nyanda za juu za Ethiopia kusini hadi sehemu ya Misri ya Nili kaskazini.

Historia na akiolojia ya Unubi ya Chini inajulikana vizuri, na wakati taarifa za uchunguzi wa historia, akiolojia na wa anthropolojia zitakapochapishwa, tutaweza kupata taswira sahihi ya dhima ya sehemu hii ya Unubi katika kuunganisha kaskazini na kusini. Hata hivyo, hali ya Unubi iliyo kusini mwa Batn al-Hadjar ni tofauti na hairidhishi. Tukiacha mikoa midogo midogo, sehemu kubwa ya nehi hii bado *ingali "Ardhi isiyojulikana"* kiakiolojia, na kwa hiyo, kihistoria pia.

Mbali na utafiti wa kiakiolojia, maandishi ya zamani ya Kifarao, pamoja na baadhi katika Kilatini na Kiyunani hutoa maelezo machache juu ya historia ya awali ya ustaarabu wa Unubi na hutupatia fikra fulani ya nafasi yake katika mabadiliko ya Afrika. Lakini

vyanzo hivi havitoshi kuwa badala ya maelezo ya akiolojia na maandishi kuhusu sehemu kubwa ya Unubi.

Kwa ufupi, Unubi iko mahali ambapo ingepaswa kutoa maelezo mengi zaidi yenye tarehe kuliko nchi nyingine yoyote ya Kiafrika kuhusu muungano wa kihistoria kati ya Afrika ya Kati na ya Kaskazini, na kati ya Mashariki na Magharibi ya Bara lili. Lakini maelezo tuliyonayo ni haba sana, isipokuwa kwa sehemu ya kaskazini ya nchi, kiasi kwamba kuelewa kwetu juu ya aina ya muungano wenyewe, umuhimu wake na muda wake ni kidogo mno.


Kuanzia miaka - 7000 hasa katika kipindi cha joto kuelekea mwisho wa Kipindi cha Neolithiki inaonekana palikuwa na utamaduni wa asili wa aina moja kwa Unubi nzima. Ni katika miaka ya - 3000 hivi tu ambapo tofauti dhaluri inaonekana kati ya utamaduni wa upande wa chini wa sehemu ya Misri ya bonde la Nili na ule wa upande wa juu wa sehemu ya Unubi. Hadi kufikia wakati huu, mila za aina moja au zilizofanana katika shughuli za matanga, ufinyanzi vyungu, ala za mawe na, baadaye, chuma zimepatikana, kuanzia Khartoum kusini hadi Matuar, karibu na Asyut kwa upande wa Kaskazini. Mila hizi zinaonyesha jinsi ambavyo sehemu mbali mbali zilifanana kijamii, katika imani za kidini, ada za mazishi, pamoja na desturi za maisha kwa jumla ambapo usasi, uvuvi na ufugaji wa wanyama vilihusishwa na kilimo ambacho kilikuwa bado duni.

Mnamo miaka ya - 3200 sanaa ya uandishi ilianza Misri wakati ambapo Unubi, iliyopo kusini mwa Maporomoko ya Kwanza iliendelea kudumisha mfuano wake wa kijamii wa kipekee pamoja na utamaduni wa kinapokeo. Ulipofikia mwaka wa - 2800 uandishi ulikuwa umeshazoea katika Misri. Wakati huo huo ni dhahiri kwamba kulikuwako na mawasiliano ya mara kwa mara kati ya Misri na Ukumbi wa Unubi, ambayo huenda yalikuwa muhimu zaidi kihistoria kuliko mashambulio ambayo Mafarao walizoea kuyafanya tangu mwaka wa - 3000 na kuendelea dhidi ya Ta-Seti, Nchi ya Upindi, iliyoko katikati ya Maporomoko ya Kwanza na ya Pili.

Hata hivyo, mashambulio haya ambayo yamesinuliwa katika maandishi ya Misri ya awali (tazama sura ya 9) yanaonyesha hali mbili za ushirikiano wa kijeshi na kiuchumi kati ya kaskazini na kusini mwa bonde la Nili. Ijapokuwa maandishi haya yanatataniisha, mahusiano hayo yanadhihirisha umuhimu wa Ukumbi wa Unubi katika kuunganisha Afrika na sehemu za Mediterani.

Hadi kufikia mwaka wa - 3200 Wamisri chini ya ufalme wa Kwanza walikwisha kuitambua nchi hiyo kiasi kwamba waliamua kupeleka kikosi cha majeshi yao mbali sana kunakoanzia Maporomoko ya Pili. Hivyo, tunaelezwa kwamba chini ya Shefru (mnamo - 2680) majeshi ya Farao yaliwateka nyara wafungwa 110,000 pamoja na mifugo 200,000 - Tarakimu hizi zinathibitisha ukubwa wa idadi ya watu na mifugo katika jamii yao.

Ugunduzi muhimu wa kiakiolojia uliofanyika katika +1961- 2 umesaidia kutupatia mwangaza kidogo juu ya historia ya awali ya Ukumbi wa Unubi. Makao ya Dola la Zamani ya Misri yamegunduliwa katika Buhén, ikiweko mihuri ya zamani ya Kifarao mingine ikiwa ya tangu ufalme wa Nne, lakini mingi ikiwa ni za zama za Ufalme wa Tano. Makao haya yalihusiana na tanuu kadhaa zilizotumiwa kuyeyushia shaba nyekundu.



8.1 Nubia ya Kale

Ugunduzi huu unadhihirisha kuwa, Wamisri hawakutegemea shaba iliyotoka Asia peke yake - hasa Sinai - na kwamba tayari walikwishapekua machimbo ya chuma ya Unubi katika Afrika. Pili, ugunduzi huo unadhihirisha jambo la umuhimu mkubwa: kuwa Wamisri waliweza au walilazimika kuanzisha mbinu za kuyeyusha madini katika bonde la juu la mto Nili. Ugunduzi wa Buhen unathibitisha kuwa shaba nyekundu ya Kiafrika ilizalishwa wakati huu. Nyaraka za Kimisri za ufalme wa mwisho wa ufalme Mkongwe zina maelezo kadha ya safari za kwenda Unubi ya Juu (tazama sura ya tisa). Katika mwanzo wa ufalme huo wa sita safari hizi zilikuwa hasahasa za kibiashara na za amani. Ni wazi kuwa biashara hizi zilisambaza mawazo na ufundi katika pande zote mbili. Jamii ya miungu wa Kimisri pia ilipata mungu mpya wa Kiafrika aitwaye Dedun, mungu wa ubani. Ili kustawisha mawasiliano yao na kusini, Wamisri walichimba mifereji ya maji ipitikayo kwa mashua katika Maporomoko ya Kwanza huko Aswan. Sera hii, iliyoanzishwa katika elfia ya tatu kabla ya enzi zetu, ilitakiwa iendelezwe na Mafarao wa Ufalme wa Kati na baadaye wale wa Ufalme Mpya.

Wamisri pia, katika safari zao, walizifuata njia kavu pamoja na zile zilizoko kwenye bonde la Nili. Kwa hakika, wakati huo hizi hazikuwa njia za jangwani kwa sababu kipindi cha joto cha enzi ya Neolothiki hakikuwa kimekwisha kabisa. Katika safari zao kwenda kusini, kama hawakupitia vivulini, bila shaka njia hizo zilijaa chemchemi na visiwa vya maji kwa sababu wanyama hamali kama vile punda ambao huhitaji maji safarini, walikuwa wakitumika.

Kama walifuata njia za bondeni au nchi kavu, yaelekea kuwa tangu zama hizo za zamani, Wamisri walikuwa tayari wanawasiliana na Afrika ya kusini mwa Sahara na kwamba Ukumbi wa Unubi ulikuwa wa muhimu katika mahusiano hayo. Chini ya Pepi II, kuelekea mwaka - 2200 safari za Wamisri zilileta “mbilikimo wa ibada” kutoka kusini ya mbali (tazama sura ya tisa). Neno lililotumiwa kumtaja mtu huyu tu *denegi*, ijapokuwa neno la kawaida la kumwita “mbilikimo” katika maandiko ya picha ni *nemu*. Twaweza kujiuliza na jibu laweza kuwa yakinishi, - kama kweli *deneg* ina maana ya mbilikimo. Kama hivi ndivyo na tafsiri ya *deneg* kuwa mbilikimo inakubaliwa na wengi, basi Wamisri wa Ufalme Mkongwe walikuwa na uhusiano wa namna fulani na hili kabila lililoteka katika misitu ya Ikweta. Kwa hivyo, tunaweza kusema kuwa Wamisri na Ufalme Mkongwe walikuwa na uhusiano na Afrika ya kati na kwamba Unubi na wenyeji wake walijitahidi kuanzisha uhusiano huo.

Kwa vyovyote vile, mahusiano kati ya Misri na Afrika ya Kati ni ya kale sana kwani neno *deneg* linapatikana katika maandishi ya zamani yaliyovumbuliwa katika piramidi. Inakubalika kwamba kuna mabishano makubwa kuhusu tarehe ya maandishi haya, lakini hata kwa kukisia maandishi haya hayawezwi kuwa yameandikwa baada ya Ufalme wa Tano na kwa kweli yanaweza kuwa ni ya zamani zaidi kuliko tarehe hiyo.

Kuanzia mwaka - 2200 hadi -1580 Wanubi walioishi katika ya Aswan na Batn al-Hadjar walidumisha uhusiano wao na Misri ama kwa kuwa Misri ilitawala sehemu hii moja kwa moja tokea mwaka - 2000 hadi - 1700 au kwa sababu Wamisri wengi waliishi katika nchi hii (tangu - 1650 hadi - 1580) wakiutumikia ufalme mpya wa Kusli. Kadri

waliyivoendelea kudumisha uhusiano na nchi yao wenyewe, Thebe, walisaidia kueneza siasa na ufundi wa Kimisri.

Kusini zaidi kutoka Batn al-Hadjar, ulikuwapo ufalme wa Kerma, jina ambalo lilitokana na kituo muhimu ambacho kilikuwa kimeshavumbuliwa. Utafiti wa akiolojia uliofanywa katika machimbo machache yaliyochimbuliwa mpaka sasa unaonyesha siyo tu uhusiano kati yao na Misri bali pia kuanzia - 1600 kati yao na Wahikso wa Asia ambao wanaonekana kuwa walikuwa na uhusiano wa moja kwa moja nao.

Ni rahisi kuonyesha mpaka wa kaskazini wa eneo lilitawaliwa na Kerma, yaani Batn al-Hadjar. Lakini mpaka wa kusini ni vigumu kuutambua. Hivi karibuni ugunduzi wa vyoimbo vya udongo vya Kikerma (1973) kati ya Nili Nyeupe na Nili Samawati kusini mwa Khartoum unaelekea kutokeza kwamba hata kama ufalme wa Kerma haukuwa umeenea mpaka Gezira ya Ico, athari yake ilienea na kwa hivyo ilieta sehemu hii karibu na nchi ya Kinailotiki yenye matete.

Kwa bahati mbaya hatuna uhakika kuwa ufalme wa Kerma uhenea kiasi gani kuelekea Afrika ya Ikweta kwa sababu ufalme huu, ambao huenda ndiyo iliyokuwa dola ya kwanza ya Kiafrika inayofahamika katika historia ya Afrika, ulikwisha kupata ustaarabu wa hali ya juu. Ustaarabu huo uliwezesha dola hii kuathiri sana nchi zilizo kusini mwake, kwenye Nili ya Juu na katika Afrika ya Kati pamoja na nchi zilizo Mashariki na Magharibi pia.

Tunawajibika kusisitiza kwamba ufalme huu uliathiri sana utamaduni wa nchi zilizopakana nayo hasa kwa mbinu za ufuaji vyuma. Kadhalika nguvu zake za kisiasa zinazodlulirishwa na ukubwa wa mji wake mkuu ni ushahidi kwamba huenda uliwezesha kueneza himaya yake mbali sana kwa bahati mbaya hatuna ushahidi wowote wa kiakolojia katika maeneo yanayouzunguka ufalme huu. Hivyo hatuwezi kufanya lolote ila kukisia tn juu ya nafasi ya ufalme wa Kerma katika kueneza fikra, ufundi au lugha.

Marekebishi yaliyofanywa na Wamisri katika njia ya safari ya kaskazini hadi kusini kuanzia mwaka wa - 2000 hadi - 1780 yamedhihirisha kuwa Ukumbi wa Unubi ulikuwa njia kuu kati ya Afrika, bonde la Nili ya kusini na nchi za Mediterani: njia za maji zinazopitika hadi katika Maporomoko ya Kwanza ziliwekwa wazi na chombo cha kuvutia mitumbwi kilichoitwa "*doiko*" kilijengwa sambamba na sehemu zisizopitika za Maporomoko ya Pili. Bwawa lilijengwa huko Semna ili kurahisisha usafiri kupita katika maporomoko madogo ya Batn al-Hadjar. Haya yote yanaonyesha kuwa Mafarao wa Ufalme wa Kumi na Mbili waliazimia kuufanya usafiri kwenda kusini uwe wa kuridhisha inavyowezekana.

Sesostri III aliweka mpaka wa Misri Semna na akaimarisha majeshi ya ulinzi ili kuzuia uwezekano wa kushambuliwa na mchokozi mwenye nguvu kutoka kusini. Lakini matini moja maarufu ina habari juu ya amri aliyotoa kwamba ngome zilizojengwa zisizue mawasiliano ya kibiashara ambayo yaliwanufaisha Wamisri na Wanubi.

Hatujui mengi kuhusu hiki kipindi cha mashaka kuanzia - 1780 hadi - 1580 ambacho wataalamu wa mambo yanayohusu Misri wanakiita Kipindi cha Kati cha Pili. Lakini kipindi hicho kinaonekana kama kilikuwa kipindi cha ustawi kwa Ufalme wa Kush

ambayo makao yake makau Kerma, yaliongeza kiwango cha biashara baina ya bonde la Nili ya Chini na ya Juu baada ya kudhoofika kwa mamlaka ya watawala wa Misri juu yao. Kerma ilifaidika sana kutokana na biashara hii.

Uhusiano baina ya Ufalme wa Kiafrika wa Kush na Misri unaelekea uliongezeka sana wakati wa Wahikso (- 1650 hadi - 1580). Katika sehemu yote ya Ukumbi wa Unubi sanaa ya vinyago vya mende pamoja na mihuri yenye majina ya wafalme wa Kiasia ambao walikuwa wakiitawala Misri zimekwishapatikana. Waafrika wa Nili ya Kati walikuwa na uhusiano wa karibu na Waasia walioishi katika Delta kiasi kwamba Mafarao wa Thebe wa Ufalme wa Kumi na Saba walipoanzisha mapigano ya kuitwaa tena sehemu ya Kati na ya Chini ya Misri, Mfalme wa Wahikso alioniba msaada kwa marafiki zake Waafrika na kupendekeza zichukuliwe hatua za pamoja za kijeshi dhidi ya adui wao wa pamoja Farao wa Misri (angalia Sura ya 9).


Kwa vyovyote vile, uhusiano baina ya Wathebe wa Misri ya Juu na Wakush wa Kerma ulikuwa na uhasama na pia wa kusaidiana. Kuanzia - 1650 hadi - 1580, Wathebe waliokuwa wakimtumikia mfalme wa Kush walileta utalamu wao wa kiufundi katika Unubi ya kati. Kuwako kwa Wamisri wengi waliokuwa katika ngome za Unubi ya chini kulihakikisha kwamba Kush ingeendelea kuwa na uhusiano na watawala wa Wahikso wa kaskazini. Vile vile, Mafarao wa mwisho wa Ufalme wa Saba waliwaajiri mamluki wa Medja katika mapambano yao ya ndani ya kutaka kuiunganisha Misri ya juu na katika vita vya kuwafukuza Wahikso.

Mafarao wa Ufalme wa Kumi na Nane, walioitwa Thutmosid, waling'amua kwamba ufalme uliougana wa Kiafrika uliokuwa upande wa pili wa mpaka wao wa kusini ungekuwa hatari kwa Misri: Urafiki kati ya Wahikso na Wakush ulikuwa umepunguza sana tamaa ya Wathebe ya kutawala.

Mafarao wa Thebe walifahamu pia kuwa kusini mwa Semna katika Afrika kulikuwa na utajiri mwingi wa mali-ghafi pamoja na wafanyakazi ambao Misri haikuwa nao na kwamba wasingeweza kutulia mpaka wameutwaa Ukumbi wa Unubi; njia pekee ya kuifikia sehemu hii ya Afrika ambayo mali zake za asili zilikuwa muhimu sana kwa sera yao ya Asia.

Hadi kufikia wakati wa Thutimosid I eneo lote lililo kati ya Maporomoko ya Pili na ya Nne lilikuwa linekwishatekwa. Wamisri sasa walikuwa wamezishika njia za jangwani za kwenda Darfur, Kordofan na Chad. Lakini pia wangeweza kuelekea kwenye sehemu ya Ziwa Kuu katika Afrika, ama kwa kufuata mto Nili kutoka Abu Hamad - maandishi kwenye mawe pamoja na sanamu za Thutimosid I na Thutimosid III zimepatikana hapa - au kupitia Jangwa la Bayuda kutoka Korti na kukutana tena na mkondo mkuu wa mto Nili, kwa kupitia Wadi Muqaddam na Wadi Abu Dom zilizoko kwenye Maporomoko ya Tano. Licha ya njia hii kuwa fupi, pia ilikwepa matatizo ya safari ya kupanda mto kutoka kusini magharibi hadi kaskazini mashariki baina ya Korti na Abu Hamad na pia safari za kupitia katika Maporomoko ya Nne na ya Sita.

Utafiti kidogo lakini makini wa anthropolojia ulokwisha kufanywa kuhusu watu walioishi katika bonde la Nili baina ya Maporomoko ya Pili na ya Nne, hata baada ya



8.2 Umniai ya Sudan

kutawaliwa na Mafarao, hakuna ushahidi wa kutosha wa kuonyesha kuwa kulikuwa na mabadiliko muhimu ya kikabila katika Unubi wakati huu. Badala yake, utafiti huu unaonyesha kuwa hali ya maisha ya watu walioishi katika sehemu hii ilifanana. Hii inamaanisha kwaamba, inpaka tutakapopata ushahidi zaidi tunaweza kukubali kwaamba watu weusi wanaonekana katika taswira za Ufalme Mpya walikutana na Wamisri katika nchi yao wenyewe; kufuatana na hayo tunaweza kuhitimisha kuwa kulikuwa na mahusiano ya pamoja kwa moja, hata lau kama yalikuwa ya misafara mifupi ya kijeshi, baina ya Wamisri na Waafrika Weusi katikati ya Afrika mnamo -1450 - 1200.

Uchunguzi huu mfupi unaonyesha kuwa nafasi hii maalumu ya Unubi kama kiungo ambayo ilitokana na nafasi yake ya kijiografia kati ya Afrika ya Kati na nchi za Mediterani, ilishaimarishwa ilipofikia mwaka - 1800. Pia uchunguzi huu unadhihirisha mambo kadhaa ya kudumu : kwanza, ukweli kwamba ilikuwa muhimu kwa Misri kupata njia ya kufikia maliasili ya Afrika na pili, kwamba Unubi ilitaka uhusiano na tamaduni za kaskazini. Hali hii iliendeleza uhusiano wa viwango tofauti vya ukaribiano katika vipindi vyote vilivyofuatana tangu - 1200 hadi 700.

Ufalme wa Napata (- 800 hadi - 300) na dola ya Meroc (- 300 hadi + 300), ustaarabu wa Ballana na Qustul (Kundi la X) (+300 hadi +600) na falme za Wakristo baada ya +600 zote zilihesabu Unubi kama kiungo muhimu baina ya Staarabu za Afrika ya Kati na za Mediterani. Kama Wahikso waliowatangulia, Waajemi, Wayunani, Warumi, Wakristo na Afrika ya watu weusi, Waislamu, wote waliuvumbua ulimwengu kwa kupitia Unubi.



Unubi kabla ya Napata (-3100 hadi -750 KK)

Kipindi cha watu wa Kundi A

Karibu na mwisho wa elfia ya nne kabla ya enzi zetu palizuka utamaduni katika Unubi unaojulikana na wataalamu wa akiolojia kama utamaduni wa watu wa Kundi - A. Zana za shaba na vigae vyenye asili ya Kimisri vilivyochimbuliwa katika makaburi ya watu wa kundi - A zinaonyesha kushamiri kwa utamaduni wao katika kipindi sawa na cha Ufalme wa Kwanza katika Misri (-3100). Utamaduni huu, kama ulivyo kwa tamaduni zingine za Unubi, hutajwa kwa kutumia herufi ya alfabeti kwa sababu wakati huo hapakuwepo na maandishi; hakuna maelezo au marejeo yoyote ya kimaandishi ya wakati huo. Aidha utamaduni huo hauwezi kuhusishwa na sehemu maalumu ya uvumbuzi au vituo fulani muhinu. Lakini hata hivyo kilikuwa kipindi cha maendeleo makubwa na chenye ongezeko kubwa la idadi ya watu.

Masalia asilia ya watu wa Kundi - A yamevumbuliwa katika Unubi kati ya Maporomoko ya Kwanza kaskazini na Batn al-Hadjar kusini. Lakini vigae vilivyofanana na vya watu wa Kundi -A vimepatikana sehemu zilizofanyiwa uchunguzi kaskazini mwa nchi ya Sudan.

Watu wa Kundi -A walifanana kimaumbile na Wamisri wa enzi kabla ya Ufalme. Walikuwa ni wafuagaji wa kondoo, mbuzi na ng'ombe. Kwa kawaida waliishi katika kambi na walihama hama kila malisho yalipokwisha.

Watu wa Kundi A waliishi katika kipindi cha Utamaduni wa Kineolithiki. Havi ni kusema kwamba walikuwa wakitumia zana za shaba, ijapokuwa ni kwa kiasi kidogo tu, zana ambazo ziliagizwa kutoka Misri. Muhimu mno katika mambo ya watu hawa wa Kundi A ni vile vyombo vya udongo vilivyopatikana katika makaburi yao. Vyombo vilivyopatikana kwa wingi ni vile vilivyong'arishwa, vyeusi ndani na vilivyo katwa nakshi nyekundu ifananayo na msuko wa vikapu. Pamoja na vyombo hivi vya udongo palipatikana pia magudulia ya mviringo yaliyochongoka shinani, vyungu vyenye mpiui wa matao na magudulia mengine mckundu yenye asili ya Kimisri.

Mintarafu desturi za maziko ya watu hawa wa Kundi A tunazijna kaburi za aina mbili. Aina ya kwanza ilikuwa ni ya shimo la mviringo lililokuwa na kina cha mita 0.8 na ile nyingine ilikuwa ni shimo la mviringo lililokuwa na kina cha mita 1.3 na ambalo lilikuwa na mwanandani. Kichwa cha maiti aliyefungwa sanda ya ngozi kilielekezwa magharibi ilihali mwili wake ukiwa umekunjwa kidogo.

Mwisho wa Kundi A

Utamaduni wa Kundi A ambao yafikiriwa uliendelea kiwako Unubi hadi kufikia mwisho wa utawala wa Ufalme wa Pili katika Misri (-2780) ulifuatiwa na kipindi cha ufukara na kudhili kwa utamaduni. Kipindi hiki kilidunua tangu mwanzo wa utawala wa Ufalme wa tatu katika Misri (-2780) hadi wakati wa utawala wa Ufalme wa Sita (-2258). Utamaduni uliopatikana katika Unubi katika kipindi hiki uliitwa utamaduni wa watu wa Kundi B na wanaakiolojia waliofanyakazi katika sehemu hizi. Wataalamu hawa walidai kwamba Unubi ya Chini, katika kipindi cha Ufalme Mkongwe wa Misri, ilikuwa na wakazi wazalendo waliotofautiana na wale wa Kundi A. Ijapokuwa wasomi wengine wamekubaliana na maoni haya, bado kuna wengine ambao hawajayaafiki.

Kuendelea kuwako kwa maumbo ya picha za watu wa Kundi A katika makaburi ya watu wa Kundi B kunayafanya makaburi haya kuonekana kuwa pengine yalikuwa ya watu wa Kundi A waliokuwa mafukara wakati utamaduni wao ulipokuwa ukidhili. Maumbile haya mapya, ambayo yanajibainisha katika watu wa Kundi B kwa namna fulani yalikuwa pengine niatokeo ya kudhilika kwa utamaduni na kuzagaa kwa umaskini katika jumuiya ya Unubi kwa jumla.

Utawala wa Misri katika Unubi

Tangu enzi za kale Wanisri wa kale walishangazwa na utajiri wa dhahabu wa vitu vingine vya anasa vilivyopatikana Unubi na wakataka kuitawala Unubi kiuchumi. Hivyo tunaona kwamba historia ya Unubi haiwezi kutenganishwa na ile ya Misri. Ubamba wa mpingo wa tangu zama za Hor-aha, mfalme wa kwanza wa Misri katika Ufalme wa Kwanza unaonyesha kushangilia ushindi wake katika Unubi. Sanaa za Kimisri za wakati wa utawala wa Djer na Ouadji, watawala wa Misri wakati wa Utawala wa Ufalme wa Tatu na wa Nne zilizovumbuliwa katika makaburi ya watu wa Kundi A katika Faras zinaonyesha kulikuwa na inwingiliano baina ya nchi ya nchi hizi mbili hata katika wakati huu wa zamani.

Hata hivyo, kumbukumbu za zamani sana zinazoonyesha ushindi wa Misri katika Unubi ni zile zilizomo katika Bustani la Maonyesho ya Sanaa za kale lililo katika eneo la jengo la hifadhi ya Sanaa za maonyesho mjini Khartoum. Haya yalikuwa ni mandhari asilia yaliyochorwa katika ubamba wa jiwe juu ya kilima kidogo kilichoitwa Jebel Sheikh Suliman, kilichoko maili saba kusini mwa mji wa Wad el Halfa katika ukingo wa Magharibi wa into Nili. Yalikusiana na utawala wa Mfalme Djer, aliyekuwa mfalme wa tatu wa Ufalme wa kwanza uliokwishatajwa. Mandhari hayo yana taarifa kuhusu vita katika Nili iliyoanzishwa na Mfalme Djer dhidi ya Wanubi.

Kumbukumbu nyingine ya Matendo ya uhasama katika Unubi inapatikana katika kipande cha ubamba wa jiwe kutoka Hierakonopoli kinachoonyesha Mfalme

Kasekhem aliyetawala katika Ufalme wa Pili akiwa amepiga magoti yake juu ya mfungwa kutoka Unubi. Jiwe la Palermo linatueleza kwamba Mfalme Snefru aliangamiza Ta-Nehasyu, nchi ya Wanubi na kuwateka nyara wafungwa 7,000, na ng'ombe na kondoo 200,000.

Ni dhahiri kwamba Misri haikupata taabu katika kunyonya mali asili ya Unubi. Uvumbuzi kutokana na utafiti wa maarifa ya mambo ya kale uliopatikana hivi karibuni katika Buhen, karibu na Maporomoko ya Pili, unaonyesha kuwako kwa koloni la Wamisri huko Buhen wakati wa utawala wa Ufalme wa Nne na wa Tano. Mojawapo ya viwanda katika makazi haya ya Wamisri ilikuwa inatengeneza shaba kama inavyodhihirishwa na kuwako kwa inatanuru ya kuyeyushia shaba yaliyopatikana huko. Majina ya walalme kadhaa wa enzi ya Ufalme wa Nne na wa Tano katika Misri yalipatikana hapo katika mafunjo na kwenye vizibo vya magudulia.

Kumbukumbu mbili za Mfalme Merenre zilizovumbuliwa katika Maporomoko ya Kwanza zinaweza kuchukuliwa kama alama ionyeshayo kuwa mpaka wa kusini wa Misri ulikuwa Aswan wakati wa Ufalme wa Sita (-2434, hadi -2242). Hata hivyo inaonekana kuwa hata katika kipindi hicho Wamisri walikuwa wakiiathiri Unubi kisiasa, kwa sababu kumbukumbu hizi zaonyesha kwamba Mfalme Merenre alizuru wilaya ya Maporomoko ya Kwanza ambapo alikaribishwa kwa taadhima na inachifu wa Medju, Irfet na Wawat. Amani ilikuwa kubwa Unubi wakati wa enzi za Ufalme wa Sita na Wamisri walitambua umuhimu wa nchi hii katika biashara ambayo ingeweza kutajirisha Misri kiuchumi. Harkhuf, kiongozi maarufu wa nusafara na aliyewatunikia wafalme Merenre na Pepi II aliongoza misafara minne hadi nchi ya Yam, Jimbo ambalo bado halijatambuliwa lakini kwa hakika lilikuwa ng'ambo, kusini mwa Maporomoko ya Pili.

Kipindi cha Watu wa Kundi C

Karibu na mwisho wa Ufalme Mkongwe wa Misri yaani kati ya miaka - 2240 na - 2150 kulitokea, katika Unubi ya Chini, utamaduni mpya wa pekee ambao unajulikana na wataalamu wa mambo ya kale kama utamaduni wa watu wa Kundi C. Kama ilivyokuwa katika kipindi kilichotangulia cha watu wa Kundi A, utamaduni huu pia ulikuwa ukitumia shaba sana. Ulidumu katika sehemu hii ya bonde la Nili hadi wakati ambapo Unubi yote ilipopoteza kabisa utamaduni wake na kufanywa eneo lililotawaliwa na utamaduni wa Misri. Hali hii yaseonekana ilitokea katika karne ya kumi na sita kabla ya enzi zetu.

Mojawapo ya hadharia zilizotolewa kuhusu asili ya kundi hili inasema kwamba yawezekana utamaduni huu ni maendeleo ya utamaduni wa Kundi A, kwani watu hawa walikuwa wanahusiana. Nadharia nyingine inadai kwamba utamaduni huo chimbuko lake ni athari zilizoletwa Unubi na wageni lakini hakukuwa na mwafaka baina ya wanataaluma wenye kuunga mkono nadharia hii hasa kuhusu asili ya wageni hawa na upande walikotokea. Kumbukumbu za kitamaduni na kinaumbile




zimetolewa kama uthibitisho wa madai mbalimbali. Baadhi yao wanapendekeza kwamba wageni hawa walihamia Unubi ya Kusini kutoka mashariki ya jangwa au katika sehemu ya mto Atbara. Wengine wanaamini kuwa wageni hawa walitoka magharibi, hasa Libya. Wazo hili sasa limeanza kupoteza nguvu yake. Wataalamu wengi wanaelekea kufikiri kwamba utamaduni huu ni matokeo ya maendeleo yaliyojengwa katika misingi ya utamaduni uliotangulia.

Imedhihirika kwamba watu wa Kundi C walikuwa hasa ni wafugaji ambao waliishi katika kambi ndogo au waliokaa kwa muda vijijini. Nyumba zilizovumbuliwa katika jimbo la Wadi el Halfa zilikuwa za aina mbili: moja ilikuwa na vyumba mvingi vyenye kuta za mawe zilizosakafiwa na udongo na ile nyingine ilikuwa na vyumba mraba vya mtofali.

Mazishi ya zamani sana ya watu wa Kundi C yanapambanuliwa kutokana na kuweco kwa mapambo ya mawe madogo juu ya mashimo mvingi au ya mvingi wa yai. Mwili uliokunjwa kidogo uliwekwa upande wa kulia huku kichwa kikielekea mashariki na kikiwa kimegemea mto wa majani makavu. Maiti, aghalabu, alivishwa sanda ya ngozi. Mahali pa kaburi la aina hii palichukuliwa na aina nyingine ya kaburi lililokuwa kubwa lenye mawe juu ya shimo mraba ambalo lilikuwa na pembe mwingi na wakati mwingine, zilizosakafiwa na bamba za mawe. Kaburi la aina ya tatu, mtindo ulioanzishwa baadaye kidogo, lilipatikana pia katika kipindi cha watu wa Kundi C. Tunaona makanisa madogo ya mtofali yaliyojengwa, aghalabu, kaskazini au mashariki, mkabala na mapambo ya mawe. Waliozikwa, aghalabu, walielekwa kaskazini. Vitu vilivyowekwa makaburini vilikuwa vya aina ya vigae vya vyungu, mawe, mifupa na bangili za pembe, vipuli, shanga na udongo laini, makubazi, bangili za visahani vya lulu na mende-inwigo wa Kimisri.

Ufalme wa Kati

Watawala wa Ufalme wa Kati wa Misri walielekeza utawala wao katika nchi ya Unubi. Hali hii ilianza wakati wa wafalme wa Thebe wa ufalme wa Kumi na Moja. Kipande cha ubamba wa jiwe kutoka katika hekalu la Gobein katika Misri ya Juu, Mentuhotep II anaonyesha akipiga maadui wake, miongoni mwao wakiwa Wanubi. Ubamba wa jiwe wa Mentuhotep III ulio katika Maporomoko ya Kwanza unaeleza habari za safari za meli hadi Wawat aubapo ni mwisho wa Nili katika Shellal-Wadi el Halfa. Zaidi ya hivyo, kuna maelezo ambayo huyamkinisha kuwa Wamisri wa Ufalme wa Kumi na Moja waliitawala Unubi kusini hadi kufikia Wadi el Halfa. Yapo kwa mfano, maandishi yaliyopatikana katika vilima viwili magharibi na kaskazini mwa kijiji cha Abdel Gadir kilichoko katika ufuo wa magharibi ya Nili karibu na Maporomoko ya Pili ambayo yanamtaja Antefu, Mentuhotep na Sebekhotep na ambayo yanasimulia kuhusu uchimbaji wa mawe, uwindaji pamoja na kazi za ukarani.



9.1 Vyungu vya Kundi C (Wizara ya Utamaduni na Habari ya Jumuiya ya Sudan)

Baadhi ya ushahidi huonyesha kwamba kutwaliwa kwa sehemu hii ya Unubi kulianzishwa na Amenemhet I, ambaye ni mwanzilishi wa Ufalme wa Kumi na Mbili. Anafikiriwa kuwa alikuwa na damu ya Kinubi.

Kutawaliwa huku kulikoanzishwa na Amenemhet I kulikamilishwa na mwanawe mrithi Senusret I. Ubamba wa jiwe wenye maandishi uliojengwa katika mwaka wa kumi na nane wa utawala wa Senusret I katika Buhen na Afisa aliyelitwa Mentuhotep, mungu wa vita wa Wathebe aliyelitwa Montu anaonyeshwa akimkabidhi mfalme mateka waliofungwa kutoka kata kumi za Unubi. Kush, jina lililotumiwa na Wamisri kutambulisha sehemu kubwa iliyokuwa kusini, lilimaanisha sehemu ambayo hapo awali ilikuwa ya Unubi na ambayo habari zake zilianza kusikika wakati wa Ufalme wa Kati

Ubamba wenye maandishi uliopatikana katika kaburi la Ameny, mtawala wa Beni Hassan katika Misri anatoa maelezo zaidi juu ya ushindi wa Senusret I wa Unubi ambao uliwapa mafarao wa utawala wa Ufalme wa Kumi na Mbili uwezo mkubwa juu ya nchi iliyoko kaskazini mwa Semna. Hii inatuonyesha kwamba Ameny alisafiri kuelekea kusini pamoja na mfalme mwenyewe na akapita "ng'ambo ya Kush hadi mwisho wa dunia".

Sababu zilizoifanya Misri iitwae sehemu ya Unubi zilikuwa za kiuchumi pamoja na kujihami. Kwa upande mmoja, kiuchumi, waliitaka Unubi ili waweze kupata ngozi, pembe na mipingo, na, kwa upande mwingine, ili wapate madini kutoka Unubi. Usalama wa ufalme wao uliwaniya kuihami mipaka yake ya kusini dhidi ya Wanubi na wakazi wa jangwani waliokuwako mashariki ya nchi yao. Hivyo, walihiifadhi na kuikimu sehemu hii ili iwe ni kama kinga yao wakati wa mashambulizi baina ya unipaka yao katika jimbo la Maporomoko ya Kwanza na nchi iliyo kusini mwa Semna ambayo ilikuwa ni chanzo cha hofu yao. Katika kufanya hivyo, wangeweza kuulinda na kuitawala na hivyo kuondoa kabisa tisho la kushambuliwa na Wakush.

Namna Wamisri walivyojihami katika kuiteka Unubi wakati wa Ufalme wa Kati inadhihirishwa wazi na idadi na nguvu za ngome ambazo wafalme wa utawala wa Ufalme wa Kumi na Mbili walikuwa hawana budi kuzijenga katika sehemu walizotwaa. Mafunjo ya enzi za Ufalme wa Kati yaliyopatikana katika kaburi la Remesseum lililoko Luxor unataja ngome kumi na saba zilizoko baina ya Semna katika kusini na Shellal ambayo iko kaskazini.

Nguvu za ngome hizi na juhudi zilizofanywa ili kuzifanya vigumu kutwalika zinaweza kuonekana katika ngome iliyoko Buhen ambayo ilikuwa ni mojawapo ya ngome zilizohifadhiwa sana katika Unubi kabla ya kugharikishwa na maji ya bwawa kuu la Aswan. Ngome hii ya kutisha ya Ufalme wa Kati iliongezewa nguvu na ngome nyingine ndogo zilizojengwa katika muundo wa mstatili na zilizokuwa na urefu wa mita 172 na upana wa mita 160.

Ufalme wa Kati ulipoanguka na kutokana na mashambulio ya Wahikso, Wamisri hawakuitawala tena Unubi. Ngome zilitekwa na kuchomwa moto na wenyeji ambao

wanaonekana walichukua fursa ya kuanguka kwa serikali kuu ya Misri ili kijipatia tena uhuru wao.

Kerma (-1730 hadi -1580)

Tayari tumekwishaona kwamba mpaka wa kusini wa Ufalme wa Kati wa Misri uliwekwa Semna na Senusret III. Lakini inachimbo yaliyofanywa na Mmarekani mtaalamu wa mambo ya kale, G.A. Reisner, baina ya 1913 na 1916 katika Kerma yameonyesha kile ambacho sasa kimekuja kujulikana kama Utamaduni wa Kerma. Tangu hapo wasomi wamehitilafiana sana juu ya jinsi wanavyofasiri utamaduni huu.

Mahali pa zamani palipoitwa Kerma palikuwa na majumba mawili makuu yaliyojulikana kama Dufufa ya Magharibi na Dufufa ya Mashariki. La kwanza lilikuwa la matofali yaliyokaushwa kwa jua na la pili lilikuwa kama kanisa, likiwa pia limejengwa kwa matofali na kuzungukwa na eneo la makaburi. Majengo yote mawili yalifanana na yale ya Ufalme wa Kati katika ujenzi wake. Kwa ushahidi huu, Reisner alifikia hitimisho kuwa: (a) kuta za chini katika Dufufa ya Magharibi zilikuwa za mahali palipofanyika biashara enzi za Ufalme Mkongwe; (b) Dufufa ya Magharibi ilikuwa, wakati wa Ufalme wa Kati, seheinu ya kusini kabisa iliyolindwa vizuri kwa kujengewa msururu wa ngome na Wamisri kati ya Aswan na Kerma. Ngome hizi zilijengwa ili kulinda maslahi yao katika Unubi: (c) Kerma ilikuwa ni makao makuu ya Magavana Wakuu wa Misri, wa kwanza pengine akiwa ni Hapidjefa; (d) Magavana wakuu wa Misri walizikwa katika makaburi yaliyokuwa karibu na Dufufa ya Mashariki kufuatana na desturi za Kimisri na (e) Wakati Wahikso walipoishambulia Misri, ngome zilizokuwa Kerma ziliharibiwa na Wanubi.

Tafsiri ya Reisner kutokana na ushahidi huu uliopatikana Kerma ilitiliwa shaka na Junker kwa sababu zifuatazo: Dufufa ya Magharibi ilikuwa ndogo mno kutosha kujengwa ngome na pia ilikuwa mahali pa hatari kwa jinsi ilivyojitenga ikiwa umbali wa maili 400 kutoka ngome ya Wamisri iliyokuwa karibu huko Semna. Zaidi ya hayo mali asili iliyopatikana katika vyumba mbalimbali inaonyesha kuwa Dufufa ya Magharibi ilikuwa ngome ya kituo cha biashara wala si kituo cha utawala.

Kuhusu makaburi, Reisner, aliona Dufufa ya Magharibi kama mahali pa kuzikwa magavana wa Misri kutokana na kupatikana kwa sanamu za Hapidjefa na mkewe katika kaburi mojawapo. Desturi za mazishi katika makaburi haya makubwa ilikuwa ya Kinubi. Hapa, maiti hakukaushwa na alizikwa pamoja na wakeze, watoto na watumishi wake katika kaburi moja. Sasa, licha ya kuwa makaburi haya hayakuwa ya Kimisri katika muundo wake na kwamba Wamisri walichelea kuzikwa ugenini ili mila zao za mazishi zisikiukwe, inakuwa ni vigumu kukubali kwamba Hapidjefa, mtu mwenye hadhi katika jumuiya na katika siasa angeweza kuzikwa ugenini kwa mtindo usiofungamana na ule wa dini ya kwao. Zaidi ya hayo, mojawapo ya vitu vilivyopatikana katika kaburi lililosemwa kuwa lake ni mchanganyiko wa vitu vya makaburini vilivyokuwa vya Kipindi cha Kati cha Pili au kipindi cha Wahikso. Kutokana na haya, Save-Soderbergh na Arkell walifikia hitimisho kwamba sanamu



9.2 Kumarishwa kwa Ngome ya magharibi ya Falme ya Kati huko Buhen (Wizara ya Utamaduni na Habari ya Jamhuri ya Sudani)

zilizopatikana mahali hapa zilikuwa zimebadilishwa na wafanyabiashara wa Misri kwa vitu vya Unubi kutoka kwa maliwali wa Kerma walioishi katika Kipindi cha Kati cha Pili. Kutokana na fikra hizi nadharia ya Reisner kuhusu Dufufa ya Magharibi na makaburi yaliyozunguka Dufufa hiyo imekataliwa na wengi. Badala yake, wasomi wengi wamekubaliana na maoni kwamba Dufufa ya Magharibi ilikuwa ni kituo cha biashara cha Wamisri ambapo sehemu ya makaburi ilikuwa ni mahali pa kuwazika wana wa Kifalme wa eneo hilo.

Hintze, alipokuwa akichunguza tena nadharia mbalimbali kuhusu suala la Kerma, aliona kuwa zimehitilafiana na kwa hivyo kufanya usahihi wake utiliwe mashaka. Kwanza kabisa anataja kwamba sababu zilizotolewa na Junker kukataa fasiri ya Reisner zinaweza kutumika pia kukataa oni la Junker mwenyewe kuwa, Dufufa ya Magharibi ilikuwa kituo cha biashara kilichoimarishwa kwa kujengewa ngome. Hintze pia anafikiri kuwa hakuna uwezekano kwamba ngome ya Wamisri katika kituo cha biashara ingekuweko katika Unubi wakati huu, hasa ikiwa Kerma ilikuwa Makao ya siasa ya Kush, nchi iliyokuwa adui wa jadi wa Misri, katika Ufalme wa Kati. Na kama ambavyo wasomi wengine ambao amewachunguza wanavyokubali, kwamba hili ni kaburi la kinubi na kwamba Dufufa ya Mashariki ni hekalu la maziko lililounganishwa nalo, Hintze anadokeza kutowezekana kwa Farao kunituma Afisa wa Kimisri kuingilia Kush kwa madhumuni ya kutengeneza hekalu la maziko ya Kinubi. Mwisho, Hintze amesisitiza yale yaliyoonyeshwa na Save-Soderbergh kwamba, kaburi hili lilikuwa la Kipindi cha Kati cha Pili, hivi ni kusema kwamba lilifuata Dufufa ya Magharibi katika ujenzi wake na kwa hivyo, magavana wa dufufa ya Magharibi hawangalikuwa wakizikwa humo.

Hii ni nadharia rahisi ambayo inakaribia ukweli, hasa kuhusu ushahidi kutoka makaburini. Tarehe ya vitu vilivyopatikana katika makaburi na jinsi vilivyokuwa vimcundwa pamoja na ada ya maziko inadhihirishwa wazi kuwa haikujengwa kwa ajili ya Magavana Wakuu wa Kimisri na Ufalme wa Kati. Lakini ushahidi mkubwa bado unahitajika ili kudhihirisha kwamba Dufufa ya Magharibi ilikuwa makao ya intawala mwenyeji wa Kush. Wazo la kuwako kwa kituo cha biashara cha kawaida cha Kimisri si la kupuuzwa haraka haraka kama anavyofikiri Hintze. Eneo alilolichimba Reisner ndilo tu lililochimbuliwa katika jimbo hili la Dongola ambalo ni maarufu katika eneo la Kerma na mpaka utafiti muafaka wa machinibo utakapokuwa unefanywa, mambo mengi yanayohusu utamaduni wa Kerma yatabaki bila kujulikana.

Utamaduni wa Kerma

Utamaduni unaofanana na wa Kerma umeonekana tu katika Unubi kaskazini hadi kufikia Mirgissa, na hivyo kuonyesha kwamba mpaka wa utamaduni wa Kerma na ule wa watu wa Kipindi cha Kundi C ulikuwa katika Maporomoko ya Pili. Kilichotambulisha utamaduni wa Kerma kilikuwa ni chombo kilichokwatuka vizuri na kupakwa rangi nyekundu juu na ambacho kilitengenezwa juu ya gurudumu la

mfinyazi. Imedokezwa kwamba zana nyingi za namna hii zilikuwa zikitengenezwa na mafundi wa Kimisri lakini hata hivyo zinaweza kuwa zilitolewa kwa mahitaji ya nyumbani na mafundi waliokuwa wamepata ujuzi huo wa Kimisri.

Ufalme Mpya (-1580 hadi - 1050)

Wakati Wamisri walipoanza kujiimarisha tena baada ya kuikomboa nchi yao kutoka kwa Wahikso, walianza kuelekeza mioyo yao katika mpaka wao kusini na hii ilisababisha ushindi mkubwa wa Misri juu ya Unubi katika historia yao ya awali.

Kutawaliwa kwa Unubi kulianzishwa na Amosis aliyemfuata Komose na mwanzilishi wa utawala wa Ufalme wa Kumi na Nane katika Misri. Maelezo haya ya harakati za kijeshi katika Unubi na yale ya waliomfuata Amosi tumeyapata katika maelezo ya Admeli Ahmose mwana wa Abana na ambaye alikuwa kapteni na mkuu wa meli yaliyokuwa yamenakiliwa katika kuta za kaburi lake huko El-kab katika Misri. Katika maandishi haya tunaambiwa kuwa baada ya Mheshimiwa kuwaangamiza Waasia, alikwenda hadi Khent Hennefer (mahali pasipotambulikana katika Unubi) na kuwapindua Wanubi. Amosis aliweza kujenga tena na kupanua ngome ya Buhen na akajenga hekalu huko. Inawezekana pia alifika katika Kisiwa cha Sai kilichoko kilometa 190 kutoka Buhen kwa sababu sanamu yake na maandishi mengine yaliyomhusu yeye na mkewe yalipatikana huko.

Hata hivyo, ilikuwa ni Tuthmose I (-1530 hadi -1520) ambaye alikamilisha kutwaliwa kwa Sudan ya Kaskazini na hivyo kutokomeza uhuru wa ufalme wa Kush. Alipofika Tambus kusini mwa Maporonioko ya Tatu, aliweka ubamba wa jiwe wenye maandishi yake makuu huko. Kutoka huko aliendelea kusini na kutwaa sehemu yote iliyoko katikati ya Kerma na Kurgus, maili 50 kusini mwa Abu Hamed ambapo aliacha maandishi yake na pengine kujenga ngome. Hivyo Unubi ikaja kutawaliwa na Misri na enzi mpya na yenye mambo makubwa katika historia yake ikaanza. Matukio katika enzi hii yaliacha athari za kudumu juu ya utamaduni wa sehemu hii kwa vipindi vyote vilivyofuata.

Unubi chini ya Utawala wa Ufalme wa Kumi na Nane

Kutokana na maandishi kwenye mwamba uliopo kati ya Aswan na Philae, yaliyoandikwa mnamo mwaka wa kwanza wa utawala wa Tuthmose II tunajua kwamba kulikuwa na maasi katika Unubi baada ya kifo cha Tuthmose I. Maandishi hayo yanatueleza pia kuwa maasi haya yalikomeshwa na kikosi kilichotumwa huko. Baada ya adhabu iliyotolewa na kikosi hiki amani ilirudi na kuimarishwa katika Unubi miaka kadhaa baadaye.

Amani iliendelea kudumishwa wakati wa utawala wa Malkia Hatshepsut aliyetawala baada tu ya Tuthmose II. Ukumbusho ukubwa na muhimu sana wa wakati wake katika Unubi ni lile hekalu lililojengwa ndani ya ngome ya enzi za Ufalme wa Kati, katika Buhen. Hekalu hili liliwekwa wakfu kwa Horus mungu

mwenye kichwa cha aliyekuwa Bwana wa Buhen. Umuhimu wa hekalu hii ni mambo ya kihistoria na sanaa yenye kuvutia iliyomo humo. Alijenga pia hekalu ya mungu wao Hathor huko Faras iliyoko katika ukingo wa magharibi wa Mto Nili karibu sana na mpaka wa sasa wa Misri na Sudan.

Matendo ya Tuthmose III yaliyoandikwa katika kuta za hekalu ya Amen huko Karnak yanaonyesha malipo ya kodi ya jimbo la Wawat kwa muda wa miaka minane na yale ya Kush kwa muda wa miaka mitano. Hii inaonyesha dhahiri kwamba kodi ya Unubi daima iliingia katika hazina ya mfalme na kwamba hali ya amani iliendelea kuwako wakati wa utawala wa Tuthmose III. Katika mwaka wake wa pili wa kutawala alijenga upya kwa mawe hekalu la Senusreti lililokuwa limejengwa kwa matofali na ambalo lilikuwa Semna Magharibi. Aliweka hekalu hili wakfu kwa miungu wa Wanubi walioitwa Dedwen, Khnum ana pia kwa mfalme wao aliyekuwa ukiabudiwa aliyeitwa Senusret III. Hekalu hili ni mojawapo kati ya yale mahekalu yaliyohifadhiwa kabisa kabla ya Ptolemy katika bonde zima la Nili.

Tuthmose III alifuatiwa na Amenophis II ambaye katika wakati wa utawala wake Unubi ilikuwa na amami. Alimaliza ujenzi wa hekalu ya Amada iliyoanzishwa na baba yake mfalme Tuthmose III. Katika maandishi yaliyoandikwa katika mwaka wa tatu wa utawala wake yaliyowekwa hekaluni, Amenophis II ameeleza marejeo yake yenye ushindi kutoka Asia pamoja na maiti za wana saba wa kifalme.

Kutoka katika utawala wa Tuthmose IV aliyemfuata tunapata maelezo katika Kisiwa cha Konosso karibu na Filai juu ya ushindi wa Msafara wa mshambulizi uliopelekwa kukomesha maasi yaliyofanywa Unubi. Maelezo haya yana tarehe ya mwaka wa nane wa utawala wa Tuthmose IV.

Tuthmose IV alifuatiwa katika utawala na mwanawe Amenophis III aliyeongoza mashambulizi huko Unubi hasa katika Karei katika mwaka wake wa tano wa utawala. Katika Soleb alijenga hekalu madhubuti sana kuliko yote katika Unubi nzima. Hekalu hili alilifanya kuwa la ukumbusho wake mwenyewe. Amenophis II pia alimjengea hekalu mkewe malkia Teye katika Sedeinga, maili kumi na tatu kaskazini mwa Soleb iliyoko katika upande ule ule wa Nili.

Mchafuko wa kisiasa katika Misri uliosababishwa na mapinduzi ya kidini ya Amenophis IV (-1370 hadi - 1352) haukuvuruga amani Unubi na ujenzi uliendelea kama awali. Katika Sesebi, kusini mwa Soleb, kutazamana na Delgo, Amenophis IV, kabla hajabadili jina lake kuwa Akhenaton, alijenga mahekalu matatu yenye maumbo sawa. Mahekalu haya yalikuwa ndani ya mji mdogo na yalikuwa ni pamoja na madhabahu ndogo iliyotengewa Aton, mungu wao mpya. Hekalu jingine lilijengwa huko Kawa na Tutankhamun aliyemfuata Amenophis III. Huko Faras, Huy, Kaimu Mtawala chini ya utawala wa Tutankhamun alijenga hekalu ndani ya makazi yaliyozingirwa kwa kuta.

Palitokea matata mwishoni mwa utawala wa Ufalme wa Kumi na Nane katika Misri lakini hayakuathiri sana amani na utengemanu katika Unubi na kuliendelea kuwa shwari katika kipindi hiki.

Unubi chini ya utawala wa Ufalme wa Kumi na Tisa

Kuanzia wakati wa Akhenaton na kuendelea Misri iliendelea kudhoofika nje na ndani ya mipaka yake. Akhenaton alikuwa mtu wa njozi na kwa mienendo yake ya kidini aliathiri sana himaya yote. Kulikuwa na kila sababu ya kuogopa vita ya wenyewe kwa wenyewe pamoja na machafuko ya kisiasa. Katika wakati huu wa hatari Misri ilipata bahati ya kukombolewa na Jenerali mmoja mwenye hekima na ujuzi wa kutawala aliyelitwa Horemheb.

Ramses I (-1320 hadi - 1318) aliyekuwa hasa mwanzilishi wa utawala wa Ufalme wa Kumi na Tisa alimfuata Horemhebu. Katika mwaka wa pili wa utawala wake aliweka ubamba wa jiwe la ukumbusho katika hekalu ya Hatshepsut, iliyoko Buhen ambapo anatuambia kuwa aliongeza idadi ya makasisi na watumishi wa hekalu hiyo na majengo mapya.

Baada ya kifo cha Ramses I, mwanaye Seti I (-1318 hadi - 1298) alirithi ufalme. Katika Unubi ya juu Seti I alijenga mji huko Amara Magharibi, karibu kilometa 180 kaskazini mwa Wadi el Halfa. Pia, labda ndiye aliyejenga hekalu kuu ya Amon iliyoko Jebel Barkal karibu na Kereima. Kuna ushahidi mdogo sana wa kuwapo shughuli za majeshi katika Unubi wakati wa utawala wa Seti I. Inaonekana hapakuwapo na haja kubwa ya kupeleka majeshi huko lakini hii si kusema kuwa hapakupelekwa vikosi vidogo huko Unubi.

Seti I alirithiwa na mwanawe Ramses II (- 1298 hadi - 1232) Tuna marejeo mengi juu ya kuwako kwa harakati za kijeshi katika Unubi wakati wa utawala wa Ramses II aliyetawala kwa muda mrefu lakini kwa sababu marejeo haya hayatoi tarehe wala kuonyesha mahali palipohusika hayana faida sana. Kwa jumla inaonekana amani ilikuwapo katika Unubi wakati wa utawala wa Ramses II na hii inadhihirishwa na harakati za ujenzi mwingi wa majengo zilizoendeshwa naye katika Unubi yote.

Katika mwaka wa tatu wa utawala wake, Ramses II tunamwona akishauriana na maofisa wake juu ya uwezekano wa kufunguliwa kwa Alaki ili iwezekane kustawisha migodi ya dhahabu ya huko, ambayo baba yake alikuwa ameshindwa kuitumia. Kaimu mtawala wa Kush aliyekuwapo alimweleza mfalme shida zilizokuwapo pamoja na kushindwa kwa baba yake kuwapelekea maji waliokuwa kwenye msafara. Hata hivyo, jaribio jingine lililofaulu liliamrisha na mfalme huyu, kwani maji yalipatikana dhiraa kumi na mbili tu katika mashimo yaliyokuwa yamechimbwa na baba yake, Seti I. Katika Kuban, ambapo njia panda iliyoelekea katika machimbo ya Wadi el Alaki ilitokea bonde la Nili, ubamba wa jiwe la ukumbusho ulijengwa kuadhimisha ushindi huu.

Ramses II alianzisha harakati kubwa za ujenzi katika Unubi. Moja ya uthibitisho wa juhudi zake ni hekalu la Abu Simbel moja ya majengo makubwa yaliyokatwa kwenye mawe duniani. Hekalu hili liko kando ya mto Nili. Inawezekana eneo hili lilichaguliwa kwa kuwa tangu zamani palidhamiwa kuwa mahali patakatifu. Hekalu hili liliwekwa wakfu kwa Re-Harakhte, mungu wa jua linalokucha, ambaye

anaonyeshwa kama mtu mwenye kichwa cha tai aliyevishwa kitu mithili ya mduara wa juu.


Kufanywa Kwa Unubi Kuwa Sehemu Ya Misri

Hatua za mwanzo za kutawaliwa kwa Unubi na Misri wakati wa Ufalme Mpya zilikabiliwa na upinzani. Lakini muda si muda Wanubi walisitirika chini ya utawala mpya wa Misri, wakawa na maendeleo yenye utulivu katika nchi yao ambayo walikuwa hawajawahi kuyapata. Tayari tumekwishaona kuwa mahekalu yalijengwa kote Unubi na wafalme wa utawala wa Ufalme wa Kumi na Nane na wa Kumi na Tisa. Miji iliyokuwa mashuhuri kidini, kibiashara na kitawala ilijengwa katika maeneo ya mahekalu hayo. Unubi ilirekebisha upya kabisa kama Wamisri waliyotaka na mfumo mpya wa utawala wa Misri ukawako uliodhihirishwa na kuwako kwa waandishi, makasisi, askari na wasanii, na matokeo yake yakawa ni kutawaliwa kabisa kwa Unubi na Misri. Wenyaji wakaiga mtindo wa dini za Kimisri na wakawa wanaomba miungu yao na desturi za maziko zikawa ni kama zile za Kimisri.

Mwisho wa Ufalme Mpya


Kwa sababu ya utajiri na unuhimu wa majeshi yake, Unubi, karibu na mwisho wa Ufalme Mpya, ilianza kuchukua nafasi muhimu katika mashauri ya ndani katika Misri yenyewe. Michafuko, unyonge, ufisadi na harakati za kutafuta vyeo vilikuwa mambo ya kawaida katika Misri ya wakati huo. Wapinzani katika harakati hizo, wakitambua umuhimu wa Unubi katika mambo hayo, walijaribu kushindania insaada kutoka utawala wa Unubi. Mfalme Ramses Siptah wa utawala wa Ufalme wa Kumi na Tisa alikwenda mwenyewe Unubi katika mwaka wake wa kwanza wa utawala ili kunitawaza Seti kama balozi wake katika Unubi. Mjumbe wake aliwaletsa maofisa wakuu wa Unubi hidaya na zawadi zingine kutoka kwa mfalme. Kutokana na hali hii, Mfalme wa mwisho na utawala wa Ufalme wa Kumi na Tisa, Memeptah-Siptah, aliwajibika kumpeleka mmoja wa maofisa wake kuchukua kodi katika Unubi ingawa kazi hii ilikuwa ikifanywa na Kaimu wa Unubi wakati farao alipokuwa na uwezo mkubwa wa kutawala na udhibiti wa himaya.

Wakati wa utawala wa Ufalme wa Ishirini hali katika Misri ilizorota kabisa. Kulikuwa na mashauri ya usaliti ya kumuondoa Ramses III (- 1198 hadi - 1166) katika utawala wake. Mmoja wa wasaliti, ambaye alikuwa dada wa nkuu wa kikosi cha watupa mishale katika Unubi, alimhimiza ndugu yake kusaidia katika utekelezaji wa hila hiyo. Lakini ni dhahiri kwamba, mwakilishi wa mfalme katika Unubi alikuwa bado ni mwanimifu kwa mfalme wake. Hata hivyo, chini ya utawala wa Ramses XI, ambaye alikuwa mfalme wa mwisho wa utawala na Ufalme wa Ishirini, kulizuka maasi katika jimbo la Asyut. Mfalme, akisaidiwa na Balozi wake wa Kush aliyetwa Pa-nchesi pamoja na majeshi yake alifaulu kukomesha maasi hayo na kuleta utengemano katika Misri ya Juu. Kutokana na maasi hayo, Heri-Hor akawa Kuhani



9.3 *Hekalu la Amenophis III huko Soleb*

Mkuu wa Amar huko Thebe. Inaonekana alitawazwa na Pa-nehesi pamoja na maaskari wake wa Kinubi na inaelekea alikuwa mmoja wa wafuasi wake. Katika mwaka wa 19 wa utawala wa Ramses XI, baada ya kifo cha Pa-nehesi, Heri-Hor alifanywa balozi wake katika Unubi na waziri katika Thebe. Hivyo akawa ndiye kiongozi katika Misri ya Juu na pia katika Unubi. Alipokufa Ramses XI, Heri-Hor akawa mfalme (- 1085) na akawa ndiye ameanzisha mlolongo wa watawala wapya huko Misri. Hata hivyo, machafuko yalianza tena katika Misri na utawala mpya wa maangamizi ukaanza katika Unubi - maangamizi yaliendelea hadi Karne ya Kumi na Nane, kabla ya enzi za Kikristo ambapo Kush ghafla ilitokea kuwa himaya yenye nguvu sana.



Utawala wa Kushi Napata na Meroe

Ingawa leo hii eneo la Dongola na bonde linalopakana nalo limetengwa kabisa na jangwa na Maporomoko ya Pili na ya Tatu ya Mto Nili, Mahali hapa palikuwa kituo cha mfumo wa kisiasa uliokuwa na nguvu na ukwasi. Katika nusu ya kwanza ya elfia ya pili utamaduni wa Kerma ulikuwa chini ya Ufalme wenye ukwasi na ufanisi. Ufalme huu ndio unajulikana katika kumbukumbu za Kimisri kama Kush. Machimbo kidogo ya kiakiolojia yaliyokwisha fanywa katika ukanda huu usiojulikana sana, hayatoshi kudlihirisha historia ya eneo hili baada ya kipindi kifupi na maarufu cha Utawala wa Kimisri wa Ufalme Mpya (-1580 hadi -1085). Kwa muda wa karibu karne tatu hivi, uhusiano kati ya Afrika na nchi za Mediterani yaelekea ulisitishwa na kukawapo na ukiinya mkubwa juu ya Unubi. Lakini kuanzia mwishoni mwa karne ya tisa ya enzi zetu kulitokea Uamsho mpya. Uchimbaji alioufanya G.A. Von Reisner huko El-Kurru karibu na Napata chini ya Poromoko la Nane umeonyesha kuwapo kwa makaburi ya wana wa mfalme waliofuatana, ambayo mwanzoni yalikuwa ya malundo ya udongo na baadaye yakawa ya mawe.

Utawala wa Kisudani Misri: Ufalme wa Ishirini na tano au Ufalme wa "Waethiopia"

Hawa walikuwa mababu wa ukoo wa kifalme walioleta muungano kati ya Misri na Sudan. Muungano huu unajulikana katika historia kama Utawala wa Ufalme wa Ishirini na Tano au Ufalme wa "Waethiopia" Misri. Kwa muda mrefu imekuwa ikifikiriwa kuwa utawala huu ulianzishwa na wakimbizi wa Kimisri waliotoka katika jimbo la Thebe kutokana na kufanana kwa majina fulani na cheo cha Mungu wao aliyeitwa Amon pamoja na ukuhani wake. Baadaye vigumba vya mishale vilivyofanana na vile vya Sahara vilifanya ifikiriwe kwamba utawala huu ulianzia Libya. Kusema kweli utawala huu ulianzia Kerma na luenda unawakilisha msururu wa watawala wa kale wa nchi hiyo.

Jiwe la Kaburi la Peye (Piakhi).

Kuingia katika sehemu kuu ya historia hii baada ya Piaukhi, ambaye siku hizi jina lake huandikwa 'Peye' kushika madaraka ya ufalme: mojawapo ya maandishi ambayo aliagiza yachongwe huko Napata na ambayo yaligunduliwa upya katikati ya karne

iliyopita, hivi sasa yametunzwa kwenye Jumba la Makumbusho la Kairo na yanafahamika kama Maandishi ya Ushindi. Maandishi hayo ndiyo marefu na yenye maelezo ya kina kuliko yote katika Misri ya Kale. Mbele, nyuma na pembeni kuna mistari 159 inayoelezea malengo ya mfalme kwenye Kasri yake na sentensi za kampeni dhidi ya watoto wa mfalme wa Libya ambao walimiliki Misri ya kati na delta. Maandiko mengine ya Peye yaliyogunduliwa mwaka 1920 yanaelekezea hali ya muungano wa himaya ya Kush pamoja na utukufu wa Mungu Amon.

Mfalme Shabaka

Kuelekea mwaka - 713 Shabaka, nduguye Peye alitawazwa kuwa Mfalme. Mfalme Shabaka alipanua mipaka ya ufalme wa Kush kwa kuliteka bonde lote la Nili hadi kufikia jimbo la delta. Yasemekana aliamrisha Bocchoris mfalme wa Sais aliyeshindana naye auawe kwa kuchomwa moto. Waandalizi wa orodha ya Wafalme wa Misri hufikiria kuwa Shabaka ndiye mwasisi wa Ufalme wa Ishirini na Tano, Hali ya Kisiasa huko Mashariki ya Kati uliwafanya Wakushi waingizwe kwenye mambo yaliyokuwa yakifanyika huko Asia ambako nguvu ya Waassiria ilianza kuongezeka, Kuongezeka huku kwa nguvu ya Waassiria kulifanya wana wa wafalme na miji ya Siria- Palestina na hasa Jerusalem waombe msaada wa haraka. Lakini Shabaka alianza kwa kuhifadhi uhusiano mzuri kati yake na Waassiria. Na huko Sudani na Misri alianzisha sera ya kujenga makumbusho. Kazi hii ya ujenzi aliyozanisha ilipanuliwa na Warithi wake, wana wawili wa Peye, mmoja akiitwa Shabataka (- 698 hadi - 690) na mwingine Mtukufu Taharqa (- 690 hadi - 664).

Mfalme Taharqa: Mapambano dhidi ya Waassiria

Jina la Taharqa linaonekana katika minara mingi ya ukumbusho iliyojengwa kote katika bonde la mto Nili. Alijenga madhabahu yake chini ya mlima mtakatifu wa Gebel Barkal unaopakana na bonde kubwa lenye rutuba la Napata. Jina la Taharqa liliandikwa pia katika makumbusho mengine yaliyotapakaa Unubi. Katika Jimbo la Thebe alijenga madhabahu katika pande zote nne za hekalu ya Karnak na ndani yake akajenga vikanisa vingine vingi ambapo ibada ya miungu Amon na Osiris ilifanyika. Tunao ushahidi wa kuwako kwake katika Mephis na katika sehemu ya delta. Maandishi kadhaa, hasa yale yaliyovumbuliwa na Griffith katika Kawa, yanatoa mwangaza zaidi juu ya sera ya mfalme; ujenzi wa madhabahu, makombe ya kafara, vifaa vya ibada, vituo vilivyowekwa wakfu na wafanyakazi wake. Mwaka wa sita wa utawala wake unakumbukwa kuwa ni wakati ambapo kupungua kwa maji yaliyokuwa yamefurika ya mto Nili kulitoa fursa kwa kazi nyingi za ufanisi kufanyika katika ufalme.

Mfalme Tanoutamon: Mwisho wa Utawala wa Sudani nchini Misri

Taharqa alirithiwa na mpwae aliyetitwa Tanoutamoni mwana wa Shabataka. Kile

kinachojulikana kama *Jiwe la Kaburi la Njozi* kinaonyesha baadhi ya matukio muhimu wakati wa ufalme wake. Kaburi hilo lina michoro ya nyoka wawili ambao ni kielelezo chenye kuonyesha uwili wa mungu Urao wa watawala wa Ethiopia. Michoro mingine kwenye kaburi hilo inaonyesha kutawazwa kwa Tanoutamoni huko Napata, safari yake ya kwenda kaskazini, kutekwa kwa Memphis, vita vyake vya jangwani na kusalimu amri kwa watawala wa maeneo yaliyoshambuliwa. Lakini, ushindi wa Waassiria dhidi ya Wakush uliwalazimisha kurudi nyuma na kuelekea kusini na huu ukawa ndio mwisho wa utawala wao katika Misri.

Ufalme Pacha

Itafaa kuchunguza kipindi cha miaka hamsini hivi ambapo Misri na Sudani zimeunganishwa na Utawala wa Kiafrika wenye nguvu. Huu ni Ufalme wa Kush ulioonyesha muundo wa ufalme pacha. Nembo yao ilionyesha uwili wa Urao (tazama juu). Katika mienendo yao kwa ujumla, na katika mavazi na fikra zao, Wafalme hawa wa Ufalme wa Ishirini na Tano waliwaiga Mafarao wa Misri waliowatangulia. Wenyewe walidai kwamba walikuwa warithi kama si vizalia wa hao Mafarao. Mitindo yao ya sanamu ilifanana sana na sanamu za Mafarao. Pia walivaa mapambo yaliyofanana na yale ya Sudan. Ushungi wao maarufu ulikuwa ni kama kofia iliyobana shingoni yenye ukanda uliozuilia kipaji cha uso ambao ulikuwa umeshikwa na utepe uliosukwa na ulioacha kanda mbili zikining'inia mabegani. Vipuli na vijebu vya mkuu vilipambwa na picha za vichwa vya kondoo-dume - nembo ya inayina mtakatifu wa mungu Amoni. Amoni kwa hakika ndiye aliyekuwa mungu mkuu wa ufalme huu na ambaye aliabudiwa katika madhabahu manne ya Napata, Tore, Kawa na Phubo (Tabo katika kisiwa cha Argo).

Sifa za Ufalme wa Ishirini na Tano zilikuwa kubwa, kutokana na maandishi ya watu mashuhuri na kwa kweli sanaa ya wakati huu inaonyesha bidii kubwa. Wakush waliporithi utawala waliupa ufalme huu nguvu na msisiziuko mpya wa baadhi ya mambo mazuri ya utamaduni wa zamani.

Napata, mji mkuu wa kwanza wa Dola ya Kush

Baada ya kurudi nyuma kwa Wakush kutoka Misri waliposhambuliwa na Waassiria imekuwa vigumu kuukilia historia yao na ntiririko wa matukio katika vipindi vilivyofuata si dhahiri. Kwa elfia moja serikali yao ilinusuika na kila muda ulivyopita taifa lao liliendelea kuwa la Kiafrika zaidi na kushikilia jina la ufalme wa Kush ambalo walilichagua wenyewe kutokana na jina la asili la nchi yao. Mintaarafu ya Elimu kuhusu Misri muda huu unawakilisha kirefu cha upoozi ambapo athari za Mafarao ziliendelea taratibu kuwa za kibadhirifu. Kusema kweli hali hii ilifanya utamaduni usiokuwa wa Kiafrika kupata fursa ya kujisimika au kujinasibisha na ule wa Kimisri. Utamaduni wa Kimisri wenyewe ulikuwa ukipokea mambo mengi kutokea Mediterania, hasa baada ya Alexandria kujengwa.

Mwanzoni, mji mkuu wa Ufalme huu ulibakia Napata iliyokuwa chini ya mlima

mtakatifu wa Gebel Barkal. Baadaye, mnamo karne ya sita kabla ya kizazi chetu, mji mkuu ulihamishiwa kusini zaidi hadi Meroe. Hatuna uhakika kamili kuhusu eneo la Ufalme wa Kush na tofauti kati ya majimbo yaliyoshirikishwa katika ufalme huu. Kwa upande wa kaskazini kabisa, Unubi ya Chini, nchi isiyokuwa na mwenyewe, iliendelea kugombewa baina ya wenyeji wa Meroe na waliokuwa wakitawala Misri kama vile Wasaite, Waajemi, Watolemi na baadaye Warumi. Kuhuishwa kwa maendeleo ya sehemu hii kulitokana na uvumbuzi wa magurudumu ya kusukuma maji yaitwayo "saqiya" kama tulivyoona awali. Katika kitovu cha dola, Unubi halisi iliyoambaa mto Nili (katika mabonde ya Napata, Dongola na Kerma) yaelekea ilikuwa tofauti na sehemu ya mbuga iliyojulikana kama "Kisiwa cha Meroe." Utafiti katika sehemu hii bado haujakamilika kutuwezeshwa kutoa msimamo thabiti kuhusu historia yake katika kipindi hiki. Kwa mfano huko Butana sehemu za mashariki kuna maeneo mengi ambayo hayajachimbwa; na hakuajafanyika utafiti wowote wa njia za misafara na sehemu za pwani ya Bahari ya Sham.

Huko Napata, makaburi ya Nuri ni miongoni mwa mambo muhimu yanayoweza kutumiwa kudhihirisha historia ya wafalme wa ufalme wa Napata ambayo inajulikana kidogo sana. Kama ilivyokuwa kwa Wafalme wa Ufalme wa Ishirini na Tano, mahali pao pa mazishi palikuwa na piramidi zilizofanana na za Kimisri ambazo mitindo yake ni kama ile ya waheshimiwa siku za mwisho za Ufalme Mpya kuliko piramidi ya kifalme za Ufalme wa Nne. Mapambo katika makaburi yao yanafanana sana na yale ya Kimisri kwa kila namna.

Hatuji lolote juu ya wafalme wa kwanza zaidi ya majina yao, kama vile, Atlanarsa aliyetawala kati ya - 653 na - 643 na mwanaye aliyetawala Seukamaniskeni aliyetawala kati ya -643 na -623. Habari kuhusu watawala waliofuata zinajulikana zaidi. Hawa walikuwa ni watoto wa Seukamaniskeni, Anlamani (-623 hadi -593) na Aspelta (-593 hadi -568). Katika jiwe la kaburi la Anlamani lililoo Kawa, zimeelezwa habari kuhusu safari za mfalme huyu majimboni na vitu alivyogawia mahekalu yaliyoko huko. Jiwe hilo lina habari pia kuhusu kampeni ya mfalme huyu dhidi ya watu waliofikiriwa kuwa Wablemye. Habari nyingine za husu kuwasili kwa Mama Malkia Nasalsa na kuhusu dada zake mfalme kuwekwa wakfu kama wacheza manyanga inbele za Mungu Amon katika madhabahu makuu manne ya mungu huyu.

Aspelta, ndugu na mrithi wa mfalme Anlamani aliyetawala kati ya -593 na 568 naye aliacha maandishi nakshi makuu mawili yaliyogunduliwa miaka michache iliyopita. Maandishi hayo yanaelezea matukio muhimu katika mfalme. Kwayo tunaielezwa tarehe za kutawazwa kwa wafalme tokea mwaka wa kwanza wa utawala wa mfalme huyu na kwaonyeshwa wanajeshi walivyokusanyika karibu na Qebel Barkal. Kuna habari pia kuhusu uamuzi wa viongozi kutafuta baraka za mungu Amoni wa Napata na uteuzi wa Aspelta na mungu. Uteuzi wake huu kwa kushuka kwake kupitia kwa "Dada wa Kifalme" kunapambanuliwa sana. Inaonyeshwa jinsi mfalme huyu alivyoehukua nembo za kifalme na jinsi alivyomshukuru Mungu na kutoa sala zake. Yaonyeshwa pia jinsi mfalme alivyopokea jeshi kwa furaha na jinsi

alivyotoa tuzo zake mahekaluni.

Jiwe la Ukumbusho wa kutukuzwa kwa dada zake katika niwaka wake wa tatu wa utawala limehifadhiwa katika Jumba la Makumbusho la Lure. Hapa zinaelezwa habari kuhusu jinsi dada zake walivyofanywa inakuhari. Matini ya ziada iliyogunduliwa na G.A. Reisner huko Gebel Barkal yanasimulia kutukuzwa kwa mfalame kwa nyimbo za heshima muda mrefu baada ya kifo chake. Matini hii hutoa pia bahari kuhusu Khahut mwanaye Peye. Kwa upande niwingine, maoni ya wanataaaluma wengine kwamba “Jiwe la Kuharimisha” nalo lilikuwa mchango wake Aspelta, mi ya kutokuwa mashaka, kwa sababu majina ya wafalme kwenye jiwe hilo yamefutika.

Msafara wa Mashambulizi ulioongozwa na Psammetik II na Kuanguka kwa Napata

Katika mwaka -591, yaani mwaka wa pili wa utawala wa Aspelta jimbo la Kush lilishambuliwa na majeshi kutoka Misri iliyokuwa chini ya Mfalme Psammetik II aliyetawala wakati mmoja na Aspelta. Majeshi ya Psammetik II yalisaidiwa na maniluki wa Kiyunani na Wakaria chini ya uongozi wa majemadari wawili, Amasir na Potasimto. Majeshi haya yalifanikiwa kuuteka mji wa Napata.

Makao Makuu Kuhamishiwa Meroe

Baada ya kutekwa kwa mji wao mkuu Wakush waliyahamisha makao yao ya ufalme toka Napata hadi Meroe, kusini zaidi na sehemu ambayo waliamini ingekuwa rahisi kuihami dhidi ya mashambulizi ya Wamisri. Meroe haikuwa mbali sana na Poromoko la sita. Tukio hili lina umuhimu mkubwa kihistoria ingawa halijapata kutiliwa maanani. Kutokana na tukio hili yawezekana ikasemwa kwa hakika kwamba Aspelta ndiye aliyekuwa Mfalme wa kwanza wa Meroe.

Mnamo mwaka -525 kulizuka hatari ya mashambulizi ya Waajemi. Akiwajibu mabalozi wa Kambise kuhusu tukio hili Mfalme wa Unubi alisema “ikiwa Waajemi wanaweza kujipinda kwa urahisi nifanyavyo mimi, na ikiwa wana nyuta kubwa niithili ya uta huu nilio nao, basi hebu na waje kwa wingi kupigana na Waethiopia” Kambise hukutilia maanani onyo hili na hivyo kufanya mashambulizi. Lakini majeshi yake walishindwa kuvuka Barm al-Hadjar na wakarejea nyuma baada ya kupata pigo kubwa. Baada ya kushindwa huku Waajemi waliamua tu kuwahesabu wananchi wa Unubi kama raia wa himaya yao. Kuna ngao iliyowekwa maalumu kwa ajili yao katika sanamu kubwa ya Darius iliyoapatikana hivi karibuni huko Susa. Katika sanamu hii kuna maandishi ya nakshi kulusu raia wote wa himaya ya Waajemi. Yaonekana kwamba sehemu ndogo ya nchi ya Unubi ilibakia chini ya utawala wao, na kulikuwa na vikosi vya Kikushi katika majeshi ya Darius na Xerxes.

Lakini inaezekana vilevile ikawa kwamba kuhamishwa kwa makao makuu ya Kush kutoka Napata kwenda Meroe kulifanywa baada ya kuzingatia sababu za kiuchumi hali ya hewa. Eneo la Meroe lilikuwa na mbuga pana zilizofaa sana kwa shughuli za kilimo na ufugaji. Hali hii ilikuwa tofauti na ile katika mabonde yaliyozunguka Napata ambayo yalizingirwa na majangwa. Kilimo kiliwezekana kwa

sababu ukanda huu una mvua za kutosha wakati wa kipupwe. Mabonde makubwa ya kumwagilia maji mashambani (*hafirs*) yalichimbwa karibu na sehemu muhimu. Biashara pia ilikuwa kubwa kwa sababu Meroe ilikuwa katika njia panda ya misafara ya biashara ya Bahari ya Sham, Nili ya juu na Chad.

Kutokana na karne nyingi ambazo habari zake hazijulikani sawasawa, Wanahistoria hawana vyanzo vingine vya historia ya Kush zaidi ya makaburi ya kifalme. Mchimbaji maarufu wa makaburi haya G.A. Reisner alianza kazi ya kulinganisha majina ya wafalme yaliyopatikana kwenye mapiramidi na yale yaliyopatikana kwa bahati na kufanywa marekebisho mengi. Marekebisho haya, hata hivyo, hayajakamilika. Inaelekea mfalme wa mwisho kuzikwa Nuri alikuwa Nastasen (muda mfupi kabla ya -300). Baada ya hapo mazishi ya wafalme yalifanyika katika makaburi huko Meroe.

Tunayo maandishi ya nakshi kadhaa juu ya Mfalme Amennoteyerike (ya muda mfupi kabla ya -400). Maandishi yaliyo mazuri kuliko yote ni yale yanayoeleza juu ya uchaguzi wa mfalme, "mtu mwenye nguvu, na umri wa miaka 41". Maandishi hayo pia yanaeleza juu ya misafara ya majeshi, tamasha za kidini, chale ya mwenge, ziara ya mama-malkia kazi ya kujenga upya majengo na utoaji sadaka katika madhabahu.

Kumepatikana pia habari kuhusu Harsioter ambaye maandishi yake naarufu ya nakshi huelezea juu ya tamasha za kifalme na vita dhidi ya maadui. Habari hizi zinafanana na zile zilizoko kwenye jiwe la kaburi la Nastasen lililopelekwa Berliu na Lepsius. Jiwe hilo kwa kweli linaweza kutupatia majina yaliyotumika kwa wakati mmoja hasa ikiwa kweli mojawapo ya maandishi hayo humtaja Khababash kama mfalme aliyetawala kwa muda mfupi huko Misri. Katika mojawapo ya kampeni zake, Nastasen aliteka nyara ng'ombe 202120 na mifugo mingine midogo 505,200. Ingefaa sana kama kulikuwa na uwezekano wa kupambanua kinaganaga habari kuhusu majina yote yaliyotajwa kwenye maandishi haya ya nakshi. Majina yaliyomo humu ya vitu na watu waliotekwa ni mengi mno na huenda itakuwa vema kuchunguza makabila yaliyoko katika ukanda wa nyasi kati ya Nili na Chad ili kujua chanzo cha majina hayo.

Philheliene Ergameno

'Kufufuka' kwa utamaduni huko Kush kunakoonekana kuwa chanzo cha miongo iliyofuata kunathibitishwa na maelezo juu ya "Ergameno" yaliyopo katika historia ya Wayunani. Baada ya kuandika juu ya nafasi ya makuhani wa Kikush wenye nguvu na walioweza kumshurutisha mfalme ajinyonge ikiwa hakupendeza watu, Diodorus wa Sisili anasimulia jinsi mfalme Ergameno aliyefundwa katika utamaduni wa Kiyunani, aliyowageukia hawa makuhani na kuamuru baadhi yao wauawe. Hata hivyo bado tuna mashaka juu ya mtu huyu Ergameno. Papo hapo tunakuta sanamu zenye mitindo halisi ya Kimeroe kama vile vilemba, mapambo na pia nembo za kifalme zilizokuwa za kienyeji na sura zilizokuwa tofauti na zile za Kimisri. Pamoja na kuendelea



10.1 : *Sanamu gramiti nyeusi ya Ethiopia ya Mfalme Aspelta*

kuabudiwa kwa mungu wa Mafarao, zilikuwapo pia ibada za Kimeroe. Hapana shaka uhusiano uliendelea kuwapo kati ya Misri na Kush kwani yapo madhabahu yaliyo wakfu kwa wote huko Philae na pia huko Dakka Unubi Kusini. Lakini, uasi uliofanyika huko kusini mwa Misri wakati wa utawala wa Ptolemy katika karne ya tatu kabla ya enzi zetu yaelekea uliungwa mkono na wafalme wa Kinubi. Ptolemy V alilazimika kufanya mashambulizi nchini na Ptolemy VI alianzisha makoloni huko *Triacontaschone*.

Lugha na Hati ya Wameroc

Wakati wa utawala wa Malkia Shanakdakhete (yapata -170 hadi -160) kulizuka utawala yenye uguvu ulioongozwa na mwanamke. Katika jumba lililojengwa kwa ajili yake huko Naga twakuta maandishi ya nakshi yaliyoandikwa kwa maandishi - picha ya Kimeroe.

Maandishi picha haya yaliigwa kutoka kwa Wamisri ila fasiri zake hutofautiana. Maandishi haya huandikwa na kusomwa kinyume cha yale ya Kimisri. Hii huenda ilifanyika kwa haja tu ya kuwa tofauti. Maandishi picha haya huandamana na maandishi ya kuapiza yaliyofupishwa. Alama zitumikazo kwenye maandishi haya yaelekea zimetokana na maandishi ya Kimisri ya kipindi hicho yaliyotumika katika nyaraka za kutawala na zile za watu binafsi. Kwa hali yoyte ile lugha hii ya Kimeroe ambayo unibo lake bado halijajulikana na yenye mfumo wa alama za maandishi ulio tofauti na ule wa Kimisri, kwa kawaida, hutenga kila neno kwa kutumia vikundi vya vituo (koloni). Lugha hii ina alama 23 zinazowakilisha konsonanti, baadhi ya irabu na silabi. Katika mwaka +1909, Mwanazuoni wa Kiingereza F.L. Griffith aligundua utaratibu wa unukuzi wa hati hiyo. Tangu wakati huo maandishi haya yamepangwa kwa muainisho wa aina kadhaa tofauti ambapo tafsiri zake zimekwewa sambamba, hasa kwa yale maandishi yaliyohusu mambo ya mazishi. Katika miaka ya karibuni mitambo ya kompyuta imeirahisisha kazi hii ya unukuzi wa maandishi yaliyotafsiriwa pamoja na maelezo yake kwa undani. Hata hivyo, kwa wakati huu, tafsiri ya hati zaidi ya 800 zilizopatikana haiwezekani kabisa. Matini ndefu za kwanza za lugha ya Wameroc inapatikana katika mawe mawili ya kaburi yenye sanamu ya Mfalme Taniydamani aliyetawala inwisho mwa karne ya pili kabla ya enzi ya Kristo.

Dola ya Warumi na Meroe

Baada ya Wameroc kufanya unyanganyi Aswan baada ya kuteka mji huo, Mtawala wa Misri iliyokuwa chini ya Warumi wakati huo alitwa Petrono. (Kuna uwezekanao kwamba sanamu ya Agosto ambayo kichwa chake kilipatikana chini ya jumba majowapo la kifalme huko Meroe, kilitekwa wakati wa mashambulizi haya). Mtawala huyu alipeleka majeshi yake na kuteka Napata mnamo mwaka -23. Warumi waliweka kikosi cha kudumu huko Primis (Gast/Ibrim) kilichowazuia Wameroc. Katika mwaka -21 an -20 mkataba wa amani ulijadiliwa Sainos ambapo Agosto alikuwa akikaa wakati huo. Yaelekea kikosi cha Warumi kilikuwa kimeondolewa; amri ya kuwatoza

kodi Wameroc kafutwa na mpaka baina ya himaya ya Kirumi na ile ya Kimeroc ukawekwa huko Hura Sycaminos (Muharraka).

Kilele cha Utawala wa Wameroc

Kilele cha utawala wa Wameroc kilifikwa katika miaka ya mwanzo ya kuenea kwa Ukristo kama majengo kadhaa yanavyodhihirisha. Majina ya Akinadad na lile la Malkia Amanishakheto yameandikwa katika Hekalu T huko Kawa na jengo la kifalme lililovumbuliwa miaka ya baadaye huko Quad ben Naga karibu na mto inasemekana lilijengwa na malkia huyu. Kaburi lake zuri bado linaonekana katika eneo la makaburi Kaskazini nwa Meroe. Piramidi, pamoja na lango la hekalu litokealo mashariki, ni mojawapo ya majengo makuu ya mji huo ambapo mnamo mwaka 1834 msafiri wa Kitaliano aliyetitwa Ferlini alipata vito vya anasa ambayo hivi leo vimehifadhiwa katika Makumbusho ya Munich na Berlin. Mapambo yanayofanana na haya yanapamba michoro ambapo malkia na wana wa kifalme walionyesha anasa ambazo kwa namna fulani zilifanana na za utamaduni wa mahali pengine katika nchi zilizokuwa zinatawaliwa na Wayunani, hususa Palmira.

Natakamani, mkwe na mriti wa Amanishakheto, pamoja na mkewe Malkia Amanitere (wa mwaka -12 hadi +12), walikuwa pia wajenzi maarufu na hapana shaka majina yao ndiyo yale yanayopatikana katika minara kadhaa ya Wakush. Mahali pengine katika miji mikubwa ya dola, minara hii inaonyesha nguvu za ufalme huu wakati ilipokuwa katika kilele chake. Kwa upande wa Kaskazini, Kusini inwa Maporomoko ya Pili, mfalme na malkia wake walijenga hekalu katika Amara ambapo sanamu zilizopo zilichongwa na Wamisri. Ukiacha tu michoro wa ushingi wa kifalme ambayo ilifanywa na Wameroc. Katika kisiwa kidogo cha Argo kilichoko karibu na Maporomoko ya Tatu, sanamu mbili zilizopo zimekwisha kubaliwa kuwa ni za Natekamani. Mfalme wa malkia wake pia walitengeneza upya Napata iliyokuwa imeharibiwa na majeshi ya Petrono; hasa lile hekalu la Amoni. Katika Meroe, majina ya Natekamani na mwandani wake yanapatikana katika hekalu kuu la Amoni pamoja na jina la Mwanamfalme Arikankharor. Kazi yao nyingine ya ujenzi inaonekana katika hekalu la kusini huko Quad ben Naga. Walichukua muda wao mwingi katika Naga sehemu iliyo katikati ya nchi hii ya mbuga kusini mwa Meroe. Mapambo ya mlango wa mbele wa hekalu la Amoni yamechanganya athari za Wamisri na zile za Wameroc. Jengo lenye sifa kubwa ni hekalu la simba la Naga ambalo michoro yake ni miongoni mwa ile inavyodhihirisha sana ya Wameroc.

Meroe na Mataifa yaliyoizunguka

Ni katika miaka michache iliyofuata ambapo tunyakuta matukio maarufu yalizonakiliwa katika kitabu cha Matendo ya Mitume (8:28-39) juu ya kuongolewa kwa Shamasi Philipo akiwa barabarani kutoka Jerusalem kwenda Gaza, na juu ya Muethiopia towashi, kasisi wa Kandase na Malkia wa Waethiopia akisimamia hazina yake yote. Yote haya yanaonyesha kuwa Meroe ilijulikana mbali.

Kuna upande mwingine ambao watafiti walikuwa wameshawishika kuutazama ili kuona Meroe ilivyofungamana na nchi za nje. Sanamu moja ya Apedemak, Simba-Mungu, inamwonyesha akiwa na vinyago vitatu vya simba na mikono minne. Hii inaashiria kuwa Meroe ilikuwa na uhusiano na India. Uhusiano kama huu huonyeshwa pia na sanamu zilizoko Naga zinazoonyesha ua la yungiyungi lenye joka lililotokeza. Shingo la joka linakuwa kiwiliwili cha mwanadamu pamoja na mkono mmoja ambao ni kinyago cha Apedemak akiwa amevaa taji ya utatu.

Nchi hii ya mbali iliendelea kuwapa shauku kubwa Warumi. Mnamo mwaka +60 Nero alituma vikosi viwili vya askari kusini mwa mto Nili. Waliporejea kwao waliseina kwamba nchi hiyo ilikuwa maskini sana isiyostahili kutwaliwa. Maandishi ya Kilatini yaliyoandikwa katika ukuta mmojawapo wa Mussawarat, ambapo sarafu za Kirumi, ijapokuwa chache nazo zilifikia sehemu fulani za Unubi na Sudan. Sarafu ya Klaudio imepatikana Meroe, moja ya Nero imepatikana Karanog, na nyingine ya Diokleta imepatikana Kordofan (El-Obeid). Sarafu nyingine iliyotumika katikati ya karne ya nne ya enzi zetu imepatikana huko Sennar.

Meroe iliendeleza uhusiano wa huduma na hekalu la Isis iliyoko Philae. Mabalozu walitumwa kila mara kupeleka tuzo inaridhawa kwenye madhabahu ya mungu wa kike. Maandishi mengi ya michoro yamehifadhiwa kwa lugha iliyotumika wakati huo Uyunani na kwa Kimeroe yakielezea haya. Maandishi haya yanatuwezesha kujua kwa hakika, jina jingine la mmoja wa wafalme wa mwisho wa Meroe aliyetwa Teqorideamani aliyetawala Meroe yapata +246 hadi +266 na ambaye alituma mabalozu huko Philae mwaka + 253. Tunazo habari kidogo sana juu ya Meroe katika karne za mwisho. Suala la utamaduni wa asili ndilo limeendelea kupata umuhimu zaidi katika utafiti. Lakini inaaminika kwanba wakati inakabiliwa na uhasama wa dola yenye nguvu kama ya Warumi Unubi haikuweza kudhibiti biashara iliyokuwa ikiendeshwa kati ya Bahari ya Sham na Ukanda wa Ngasi kati ya Nili na Chad.

Kudhoofika na Kuanguka kwa Meroe

Wameroe ambao hadi wakati huu walikuwa wameshinda uvamizi waliofanyiwa na makabila ya wahamaji waliendelea kushambuliwa mara kwa mara na majirani zao, Waaksumi walioko upande wa kusini, Wablemi walioko mashariki na Wanubi walioko upande wa magharibi. Yaelekea kuwa wazi kuwa hili kundi la mwisho ndilo lilifanikiwa kuuangusha utawala wa Meroe. Habari za kundi hili linetajwa kwa mara ya kwanza na Erastosthenes mnamo -200.

Tangu mwaka -330, ufalme wa Aksum ulikuwa unestawi sana katika nyanda za juu za Ethiopia ya leo ulikua haraka na kufikia kilele cha nguvu zake Ezana, mfalme wa kwanza kupokea Ukristo alifika kwenye ndagano ya Atbara na alijitapa kuwa yeye alikuwa ametuma majeshi yaliyomletea mafanikio makubwa dhidi ya Wanubi. Kutokana na haya tunaweza kusema kuwa ufalme wa Wameroe ulikuwa tayari umcanguka wakati wa mashambulizi ya Ezana. Tokea wakati huo na kuendelea 10..2



10.2 *Malkia Amanishakheto: kutoka kwenye piramidi ya Beg N 6 huko Meroe (J. Lectasnt)*

maandishi yaliyoandikwa kwa Kimeroe yalikoma. Yawezekana kuwa huu ndio wakati ambapo lugha ya Kimeroe iliacha kutumiwa na badala yake lugha za asili za Wanubi wa leo zilianza kutumiwa tena. Hata vyombo vya udongo ambavyo, ingawa viliendelea kuwa vya asili ya Kimero, vilianza kuwa na maumbile inapya.

Ingawa kupenya kwa athari za Wameroe kulikuwa na unuhimu katika sehemu nyingi za Afrika, nafasi ya Wakush haiwezi kudumishwa. Kwa zaidi ya miaka elfu moja, kwanza huko Napata na baadaye huko Meroe, palizuka utamaduni wa kiasili ambao ingawa ulishikiliwa na mtindo uliofanana na utamaduni wa Kimisri, ulibakia kuwa wa Kiafrika halisi.

Unubi baada ya kuanguka kwa Meroe: "Kundi X"

Inaaminika kuwa Wanuba wa magharibi au kusini magharibi ndio hasa walioeneza Kinubi ambacho hadi leo hii, lahaja zake zinazungumzwa katika majimbo ya milimani ya Darfur na pia katika sehemu kadhaa za Unubi ya Juu na ya Chini.

Anasa za kishenzi za Wafalme wa Kundi X zilidhihirishwa baina ya +1913 hadi 1933 wakati wanaikiolojia na Kiingereza Emery na Kirwan walipochimbua vichuguu vilivyokuwa Ballana na Qustil, maili chache kusini nwa Abu Simbel. J.L. Burckhardt, mchunguzi wa kwanza katika Unubi, alikuwa amekwishaviona katika karne iliyotangulia. Humo makaburini walizikwa wafalme wakiwa wanazungukwa na wake zao, watumishi wao na farasi wao wenye matandiko ya thamani. Maiti zao zililazwa katika machela kama ilivyokuwa ikifanyika katika Ufalme ukongwe wa Kerma. Taji zao na vikuku vya fedha vilivyopambwa na vito vinakumbusha mengi kuhusu Misri au Meroe. Athari za Alexandria zimedhihirika wazi katika hazina ya vyombo vya fedha vilivyotawanywa sakafuni. Miougoni mwa inabeseni, vikombe na visahani kulikuwapo na sahani ilinochongwa sanamu ya Hermes akiwa amekalia tufe na kando yake mnyama aliyefanana na simba mwenye kichwa na mabawa ya tai. Kulikuwa pia pana taa za shaba nyeusi na sanduku la mbao iliyonakshiwa kwa pembe za ndovu kwa upande wa ndani. Lakini vyombo vya udongo bado vilikuwa vya mtindo wa kale wa Kimeroe vikionyesha uzuri na afundi halisi wa Wanubi uliodumu kwa elfia kadhaa.


Wanabade au Wablemi

Hawa watu wa Kundi X walikuwa akina nani - Wanabade au Wablemi. Wablemi walikuwa wahamaji wapenda vita ambao kwa kawaida wanafananishwa na makabila ya Wabeja wa Mashariki mwa jangwa. Kwa upande wa Wanabade au Wanobate, imekubaliwa baada ya ubishani inwingi kwamba ni Wanuba. Inafikiriwa kuwa ndio waliokuwa watawala wa Ballana na Qustul. Kwa hali yoyote ile majina Wablemi na Wanabade hayana umuhimu mkubwa kwetu; pengine ingefaa kutumia mafungu ya maneno "Kikuni X au "Utamaduni wa Ballana" kikundi tunapozungunzia mambo yanayowahusu.

Ushahidi wa maandishi ya kale na nyaraka za uandishi wa nakshi zimetusaidia

kuunganisha vidokezo muhimu vya kihistoria. Mwanahistoria ajulikanaye kama Procopus anadai kwamba kuelekea mwisho wa karne ya tatu, wakati Mfalme Diocletian wa Rumi aliposogeza mpaka wa himaya yake nyuma hadi katika Poromoko la Kwanza, aliwatia Wanobate moyo wa kuhama kutoka kwenye maoasisi kwenda katika eneo la Nili, ili wakinge Misri dhidi ya mashambulizi ya Wablemi. Na kwa hakika wakati wa Utawala wa Theodosms yapata mwaka 450, Philae ilishambuliwa na Wablemi na Wanobade. Walirudhishwa nyuma na majeshi yaliyoongozwa na Maximinus na baadaye na majeshi chini ya uongozi wa Flarus.

Baada ya majilio ya Ukriksto waliruhusiwa kuendelea kuzuru madhabahu ya Isis huko Philae na wakati wa karamu muhimu waliruhusiwa kuazima sanamu ya mungu wa kike. Yaelekea Qasr Ibrim ndicho kilikuwa kituo cha safari hizi za hija, kwa sababu sanamu inayofanana na ile ya Isis iliyochorwa kwenye chungu cha udongo imepatikana huko. Ni mnamo wakati wa utawala wa Justinian, kati ya mwaka +535 na +537 ndipo jemadari wake Narses alipofunga Hekalu la Philae na kuwafukuza makuhami wa mwisho.



Ustaarabu Wa Napata na Meroe

Mfumo na Muundo wa Utawala

Chimbuko la Ufalme

Sifa kubwa ya muundo wa utawala katika Unubi na Sudan ya Kati toka karne ya nane kabla ya enzi zetu hadi karne ya nne ya enzi zetu, ilikuwa ni uimara wake. Kinyume cha falme nyingi za kale, nchi hii iliepukana na misukosuko inayotokana na mabadiliko ya ufalme kwa kutumia nguvu. Ukoo wa kifalme ule ule uliendelea kutawala kufuatana na desturi pasipo kukatizwakatizwa.

Mojawapo ya inambo ya kipekee ya mfumo wa kisiasa wa Meroe ulikuwa kumchagua mtawala mpya kwa kupiga kura. Waandishi mashuhuri wa kale, tangu Herodotus, mnamo karne ya tano kabla ya enzi za Ukristo, hadi Diodorus wa Sisili, mnamo karne ya kwanza kabla ya enzi za Ukristo, walishangazwa na mtindo huu ambao ulikuwa tofauti kabisa na ule uliokuwa katika falme nyingine za kale.

Kwa bahati nzuri tunaweza kukusanya na kuunda upya taratibu za kurithishana ufalme kutokana na maandishi ya Napata ambayo yanaeleza kwa undani zaidi, jinsi uteuzi na sherehe za kutawaza zilivyofanywa. Maandishi ya Napata kuhusu kutawaza ndicho chanzo chetu kizuri kwa kuelewa taasisi za kisiasa, hasa sifa za ufalme na taasisi nyingine zinazohusiana. Ingawa yameandikwa kwa kutumia maandishi picha yaliyofanana na yale yaliyotumika Misri katika kipindi hicho yanaonyesha tofauti kubwa katika mielekeo yake. Uandishi na usomaji wake ulifanywa kinyume cha vile ilivyofanyika kwa maandishi nakshi ya Ufalme mpya. Hivyo ni muhimu yachukuliwe kama zao la utamaduni wao.

Miongoni mwa maandishi nakshi haya matatu ya hivi karibuni, yaani yale ya Amani-nete-yerike (-431 hadi -495), ya Harsiotef (-404 hadi -369), na ya Nastasen (-335 hadi -310) yanaonyesha kwamba wafalme walikuwa na ari ya kutekeleza kikamilifu mila za jadi na kusisitiza mila na ada za wahenga wao. Kwa wakati huo huo, maandiko haya yanatoa maelezo zaidi kuliko yale ya awali, ingawa lugha iliyotumika humo ni ngumu kueleweka. Maandishi haya huonyesha uwiano katika mada zinazojadiliwa humo na pia katika utungaji wake wakati mwingine. Katika maandishi yote matatu tunaelezwa kuwa mfalme kabla ya kuteuliwa kwake, aliishi pamoja na ndugu zake wa kifalme huko Meroe. Alirithi ufalme akiwa Meroe na baadaye alisafiri kwenda kaskazini hadi Napata kwa

sherehe za kutawazwa kwake. Ama kwa hakika Amani-nete-yerike yanasema kwa dhiti kwamba aliteuliwa kuwa mfalme na viongozi wa majeshi yake alipokuwa na umri wa miaka 41 na kwamba alikuwa amepigana vita kabla ya kwenda Napata kutawazwa. Alipofika Napata alienda katika jumba la Kifalme alipopewa taji ya Ta-sti kama uthibitisho zaidi wa kuchukua ufalme. Baada ya hapo aliingia katika hekalu kwa sherehe, ambapo alimwomba mungu ampe ufalme wake; jambo ambalo kwa hakika lilifanyika kutimiza ada.

Maandishi nakshi ya awali yanathibitisha hitimisho lililopata kufikiwa kwamba kurithisha ufalme kulikamilishwa kabla mfalme hajaingia katika hekalu. Kwa hivyo kurithishwa ufalme Taharqa (-689 hadi - 664) kuliambuliwa na Shebitku (-701 hadi -689) aliyeishi Memphis nchini Misri. Taharqa alitwa kutoka miongoni mwa ndugu zake wa kifalme na akasafiri kuelekea kaskazini, kupitia Napata kabla ya kuendelea hadi Thebes.

Jiwe la kaburi la Mfalme Tanwetamani aliyetawala kati ya - 664 na - 650 yaonyesha aliishi mahali fulani nje ya Napata, pamoja na ndugu zake wengine wa kifalme na mama yake Qalhata. Hapo ndipo alipotangazwa kuwa mfalme na halafu akaanza maandamano ya sherehe akisafiri kuelekea kaskazini hadi Napata na kuendelea zaidi hadi Elephantine na Karnak. Hivyo yaonekana kwamba mahali hipokuwa kabla ya maandamano palikuwa kusini mwa Napata, yaani Meroe. Hii yaonyesha uamuzi juu ya urithi wa Ufalme, kwa kawaida ulifanyika nje ya Napata. Anlamani (-623 hadi -593) naye anaeleza matukio ya sherehe yake huko Gematon ambako jiwe la kaburi lilipatikana, kwa namna hiyo hiyo. Anaongeza kwamba alikuwa amemleta mama yake kuhudhuria sherehe hizi kama Taharqa alivyofanya kabla yake.

Mahitimisho kadhaa hudhihirika kutokana na maandishi haya. Moja ni kwamba safari ya kaskazini kuzuru mahekalu mbali mbali, ilikuwa ni sehemu muhimu ya sherehe ya kutawazwa mfalme ambayo ilimlaziinu kila mmoja kufanya wakati anapotwaa ufalme. La pili ni kwamba hekalu la Amon huko Napata lilikuwa na dhima maalum katika sherehe hii na kwamba jambo hili halikupingwa na mtu yeyote. Yote haya yanaathari kwa nadharia ya G.A Reisner, ya kuwepo kwa falme mbili zinazojitegemea katika Napata kama ilivyosemwa tena na Hintze hivi karibuni.

Nadharia hii ilitolewa na G.A. von Reisner katika kueleza idadi ya makaburi ya kifalme. Dhana yake ya msingi ilikuwa kwamba mazishi ya kifalme yalilusishwa sana na mji mkuu: Mfalme angezikwa mahali pasipokuwa mbali na makao yake ya kifalme. Kwa hali hiyo makaburi ya El-Kurru ambayo yalikuwa ya kale kuliko mengine, na makaburi ya Nuri, yaliyofuata ya El-Kurru, yalikuwa ni makaburi ya kifalme hadi wakati wa Nastasen ambapo mji mkuu ulikuwa Napata. Hatimaye makaburi mawili yaliyo Kusini na Kaskazini mwa Begrawiya yalikuwa makaburi ya kifalme wakati mji mkuu ulipohamishiwa Meroe katika miaka ya -300, baada ya utawala wa Nastasen. Hata hivyo, huko Gebel Barkal, katika Napata, kuna makundi mawili ya piramidi. Maoni ya kiakiolojia na ya kisanifu ujenzi yalimfanya Reisner kuamini kwamba kundi la kwanza ni la wakati wa utawala uliofuata mara baada ya Nastasen na kundi la pili linaonyesha kuwa lilianzia karne ya kwanza kabla ya enzi zetu na kumalizika wakati Warunu waliposhambulia Napata mnamo mwaka - 23 au mara baada ya hapo. Kila kundi lilipewa tawi la ukoo wa kifalme uliotawala

Napata mbali na ukoo mkuu ulipotawala Meroe.

Uchambuzi wa maandishi unaonyesha kwamba ofisi ya mfalme ilikuwa mi ya kurithiwa katika ukoo wa ufalme. Katika Napata na Meroe mfalme alichaguliwa kutoka kwa ndugu zake wa kifalme. Fikra ya kumchagua mfalme mpya ilitoka kwa viongozi wa kijeshi, maafisa waandamizi wa watemi (machifu) wa mbari. Mstahiki yeyote ambaye uwezo wake ulitiliwa mashaka au aliyekuwa hapendwi na wapiga kum aliachwa. Pamoja na hayo, ni wazi kwamba, kinadharia, ufalme ulirithiwa kwanza na ndugu wa mfalme kabla ya kwenda kwa kizazi kinachofuata. Kati ya wafalme ishirini na saba waliotawala kabla ya Nastasen, kumi na nne walikuwa ndugu za mfalme aliyekuwa anarithiwa. Kwa kweli, kulikuwepo na hali za kipekee ambapo mfalme huyu ama yule alinyakua kiti cha enzi kwa nguvu, lakini katika hali kama hizo alijaribu kuthibitisha na kuhalalisha kitendo chake. Pia kuna dalili nyingine kwamba haki ya kurithi kiti cha mfalme huenda ikategemea zaidi madai kutoka katika ukoo wa mama kuliko kutoka kwa baba. Dhima ya mke wa mfalme (mama malkia) katika uteuzi wa mfalme mpya inaonekana katika maandishi mengi. Tabia hizi nyingine zina mifano ya karibu katika falme na temi za sehemu mbali mbali za Afrika.

Sherehe zote za kutawazwa mfalme zinaonyesha wakfu mtakatifu wa ufalme katika Napata na Meroe: mfalme alichukuliwa kuwa mtoto wa kiume wa kulea wa miungu mbali mbali. Ni kwa kiasi gani yeye mwenyewe alichukuliwa kuwa Mungu, au kama mfano wa Mungu, haifahamiki, bali kwa vile yeye alichaguliwa na miungu matendo yake yaliongozwa na maadili ya sheria za kimila. Strabo na Diodorus Siculus wanaeleza matukio ambapo makuhani, wakiwa wanatekeleza maagizo ya kimungu walimwamuru mfalme ajiue. Wanasema kwamba mila hii iliendelea kuwapa hadi wakati wa Ergamenes (karibu - 250 hadi - 125), ambaye alikuwa amepata elimu ya Kiyunani iliyomfanya asifuate mambo ya ushirikina na ambaye aliwanyonga makuhani maarufu kutokana na uzushi wao. Baada ya wakati huo, mila ya wafalme kujiua ilitoweka.

Watawala wa Napata na Meroe walitumia majina ya kiasili ya Kifarao katika maandishi yao. Hakuna cheo chao chochote chenye jina linalotokana na neno la lugha ya Meroe lenye maana ya mfalme, Cheo kwr (linalosomeka *kere*, *ker au geren*) linaonekana tu katika maelezo ya Psemmetik wa II yanayohusu ushindi wake dhidi ya Kush anapomtaja mfalme Aspelta. Ingawa jina hili lazima lilikuwa namna ya kawaida ya kuwaita watawala wa Kikushi halikuruhusiwa kuingia katika kumbukumbu za Kushi.

Wakandase: Dhima ya Mama-Malkia

Dhima halisi iliyotekelezwa na wanawake wa kifalme katika nyakati za mwanzo siyo wazi kabisa, lakini zipo dalili nyingi kwamba walishika nafasi maalum na ofisi muhimu katika utawala. Wakati wa utawala wa Kushi katika Misri afisi ya kuhani mkuu wa kike (Dewat Nete) wa mungu Amon wa Thebe ilishikiliwa na binti wa mfalme na ilimpa uwezo mkubwa wa kuathiri mambo ya kiuchumi na kisiasa.

Dhima muhimu ya mama-malkia katika uchaguzi na sherehe za kutawazwa wana wake imetajwa na Taharqa na Anlamani kwa jnia ambayo haiachi wasi wasi wowote juu ya nguvu za athari zake na hadhi yake maalumu. Pia aliathiri mambo nchini kwa jinsi

alivyotumia mfumo wa humtwaa mwana ambapo mama-malkia akitumia cheo chake cha mama-mlezi wa Kushi, humtwaa mke wa mwanawe. Katika jiwe la Kaburi la Nastasen (-335 hadi - 310) sehemu ya juu inaonyesha mama yake Pelehhs na mke wake Sakhakh, kila mmoja akiwa ameshikilia manyanga ambayo yanaonekana kuwa ishara ya ofisi yao. Maandishi ya nakshi ya Anlamani yanasema kwamba alikuwa ametoa wakfu kila mmoja wa dada zake wanne, kwa kila hekalu kati ya mahekalu manne ya Amon, ili wawe wapiga manyanga na kumwomba kwa mungu huyu.

Katika kipindi cha baadaye malkia hawa - walikuwa mama au wake - wa mfalme walianza kupata nguvu za kisiasa na wakajitangaza kuwa watawala, hata wakachukua majina ya kifalme kama vile, Mwana wa Re, Bwana wa Nchi Mbili (*sa Re, neb Tawy*) au Mwana wa Re na Mfalme (*sa Re, nswbit*). Wengi wao walikuwa mashuhuri, na katika nyakati za Wayunani na Warumi, Meroe ilijulikana kwamba ilitawaliwa na ukoo wa *Kandase*, *Kandake* au *Malkia* wenye nguvu.

Jina lili linatoka katika neno la Kimeroc *Ktke* au *Kdke* lenye maana ya mama-malkia. Jina jingine - *gere* - linalomaanisha mtawala, halikutumiwa hadi maandishi ya Kimeroc yalipoonckana. Kwa kweli tuna malkia wanne tu wanaojulikana kwamba walitumia jina hili, nao ni Amanirenas, Amanishekhete, Nawidemak na Maleqereabar, wote wanaelezwa kuwa ni Wakandase. Inafaa kuzingatia kwamba katika makaburi ya kifalme ya Nuri, tangu Taharqa (aliyekufa - 664) hadi Nastasen (aliyekufa yapata - 310) hakuna uthibitisho kwamba malkia alifanyiwa mazishi kamili ya mtawala, na katika kipindi hiki hakuna malkia aliyetawala anayejulikana. Malkia wa mwanzo aliyethibitishwa kuwa alitawala ni Shanakdekheta mnamo karne ya pili kabla ya enzi ya Ukristo na ambaye alifanyiwa mazishi kamili ya kifalme kaskazini mwa Begrawiya. Huenda wakati wa mwanzo, jina hili na afisi havikuwa na maana zaidi ya mama-malkia. Kuanzia kwa Shanakdekhete na kuendelea tuna mfululizo wa Malkia watawala. Lakini kuanzia na Amanirenas katika karne ya kwanza kabla ya enzi zetu yaelekea kulikuwa na tukio jingine. Hili lilikuwa ni uhusiano wa karibu sana kati ya mke wa kwanza wa mfalme na, labda, mwana wao mkubwa wa kiume katika shughuli nyingi muhimu. Hii inaonyesha kiwango fulani cha ushirika katika utawala kwa vile mke aliyeachwa baada ya kifo cha mumewe mara kwa mara alikuwa ndiye kandase intawala. Hata hivyo, mpango huu haukudumu kwa muda zaidi ya vizazi vitatu na yaelekea uliisha baada ya Natakamani, Amenitere na Sherakarer mnamo nusu ya kwanza ya karne ya kwanza ya enzi zetu, Haya yote yanaonyesha desturi hii ilizuka na kukua miongoni mwao na wala haikuigwa kutoka nje kama walivyofanya Waptolemi wa Misri: mfano ukiwa ule wa Cleopatra. Kwa kweh tunaweza kuona nanina taasisi hizi zilivyokuwa kwa hali mbali mbali kwa muda wa karne nyingi.

Utawala wa Serikali Kuu na Tawala za Mikoa

Katika kitovu cha utawala alikuwepo mfalme, mtawala pekee mwenye nguvu zote ambaye kauli yake ilikuwa sheria. Hakutoa madaraka yake kwa mtu yeyote, wala hakushirikiana na mtu yeyote kutawala. Hapakuwa na taasisi iliyokuwa na mtawala mmoja. Kwa mfano hapakuwa na Kuhani mkuu kwa mahekalu yote au waziri ambaye alipewa madaraka

makubwa mno. Makao ya mfalme yalikuwa ndiyo kitovu cha mambo ya utawala. Kufuatana na ushahidi wa hivi karibuni inaelekea kwamba Meroe ulikuwa ndio mji pekee uliokuwa makao ya kifalme na kitovu cha utawala. Piankhi hakubainisha waziwazi makao yake halisi yalipokuwa; ingawa ni dhahiri kwamba Memphis ndio uliokuwa mji mkuu wa warithi wake wa mwanzoni katika Ufalme wa Ishirini na Tano wa Misri. Hata hivyo, Taharqa anaonyesha bayana kwamba alikuwa anaishi pamoja na ndugu zake wa kifalme na mama yake. Kutokana na maandishi mengine ni wazi kwamba ndugu hawa wa kifalme waliishi Moroe.


Utawala wa serikali kuu uliendeshwa na idadi ya maafisa waandamizi ambao majina ya vyeo vyao vya Kimisri yamehifadhiwa katika mawe mawili ya makaburi ya Asyelta. Miongoni mwao tunaona - mbali na makamanda wa kijeshi - wakuu wa hazina, watunza mihuri, wakuu wa makumbusho, maandishi wakuu wa Kushi na maandishi wengine. Viongozi wa kijeshi wanaonekana mara kadhaa katika maandishi haya hasa katika nyakati za shida. Walipewa jukumu la kutangaza urithi wa mfalme mpya na kuendesha sherehe za kijadi za kutawazwa mfalme. Kwa kweli huenda walikuwa na dhima maalumu katika uteuzi wa mrithi. Kutokana na maelezo haya, intu anaweza kusema kwa yakini kwamba wengi wao walitoka katika ukoo wa kifalme, na huenda walikuwa na wadhifa mkubwa. Ilikuwa ni kawaida kwa mfalme kutokwenda vitani, ila kubakia katika makao yake, akimwachia numoja wa majenadari kazi ya kuendesha vita.

Kwa upande wa utawala wa mikoja, zipo alama za majumba ya kifalme zinazopatikana katika sehemu nyingi. Kila makao ya mfalme yalikuwa na kitengo kidogo cha utawala kihichoongozwa labda na intunza mhuri nikuu aliyetunza bohari na mahesabu ya makao makuu ya mfalme.

Hata hivyo, katika kipindi cha baadaye, kunzia labda karibu na inwisho wa kame ya kwanza kabla ya enzi za Ukristo tuna kumbukumbu za kutosha za watawala wa mikoja, za kutuwezesha kuandika upya japo kwa uchache kuhusu mkoja wa kaskazini wa ufalme ambao unaelekea uliendelea kwa haraka sana kufuatia hali ya machafuko baada ya Waruni kuiteka Misri na kushindwa kwa jitihada zao za kutaka kuelekea kusini zaidi hadi Unubi. Ili kukabiliana na hali hii mpakani, utawala maalum wa Umubi ya chini ulianzishwa. Kiongozi wake alikuwa mtu mwenye cheo cha Paqar. Qar, alikuwa mtu mashuhuri wa kitala ambaye huenda alikuwa mwana-mfalme, iwapo huyu Qar alikuwa wa kwanza kushika madaraka haya basi yaweza kusemwa kwamba ndiye aliyecanzisha utaratibu huu wa utawala mikoani. Paqar wa kwanza alikuwa Akinidad, mwana wa Teritiqas na Amanirenas, aliyepigana dhidi ya uvamizi wa Kirumi katika Unubi. Cheo hiki pia kiliandamana na majina ya watu kama Arkankharor, Arikakhatani na Sherekarer (Mfalme wa picha za mawe za Jabal Qayli) na wana wa kiume watatu wa Nakatamani na Amanitere (- 12 hadi + 12). Majina yao yenye cheo cha pqr yamepatikana katika maandishi ya nakshi kutoka Napata, Meroe na Naqa.

11.1 *Piramidi ya*

*Mfalme Natekamani huko
Meroe na mabaki ya kamisa
mbele yake*



11.2 *Kondoo dume
aliyetengenezwa kwa
gramiti huko Naqa*

Vyeo vingine viwili maalumu chini ya peshte vilikuwa *pelmes-ate* (jemedari wa maji) na *pelmes-adab* (jemedari wa ardhi). Maafisa hawa wawili wanaonekana walikuwa na jukumu la kuangalia na kuhifadhi mawasiliano ya njia ya ardhi na maji ambayo japo yalikuwa ya kiwango kidogo lakini yalikuwa muhimu katika Unubi kuhakikisha kuwa biashara kati yake na Misri inaendelea, kudhibiti mipaka na kuchunguza mienendo hatari ya wahamaji waendao mashariki na magharibi mwa mto Nili. Maafisa hawa walisaidiwa na maafisa wengine wadogo, waandishi, makuhani na watawala wenyeji.

Maisha ya Kiuchumi na ya Kijamii

Ikologia

Ufalme wa Kush ulitegemea shughuli mbalimbali za kiuchumi ambazo zilitofautiana kulingana na hali tofauti za kijiografia za nchi iliyoenea kutoka Unubi ya Chini hadi kusini mwa Sennar na kuendelea hadi sehemu ya Gebel Moya katika nyanda za kusini za Gezira. Nchi hii ilienea pia hadi katika sehemu kubwa iliyo kati ya bonde la mto Nili na Bahari ya Sham. Vile vile sehemu kubwa za magharibi ya mto Nili huenda zilikuwa chini ya utawala wa Meroe ingawa kiasi chake bado hakijafahamika. Sehemu hii kubwa inaanzia katika sehemu kame hadi katika zile zinazopata mvua za msimu wa joto zinazoridhisha. Nchini Unubi shughuli za kiuchumi zilitengea sana kilimo katika bonde la Nili ambapo mkondo mmoja tu wa mto huu ulikuwa chanzo pekee cha maji. Ushahidi wa kiakolojia wa hivi karibuni umeonyesha kwamba kiasi cha maji ya mto Nili kilikuwa cha chini na kwa kuwa Unubi ipo nje ya ukanda wa mvua, hali ya ikolojia haikusadifu kilimo kilichotegemea kutosheleza idadi kubwa ya watu. Ama kwa hakika imedaiwa kwamba mwanzoni kabisa mwa kipindi cha Napata, Unubi ya Chini ilikuwa inahanwa na wakazi wake wengi kwa kitambo kirefu sana na kwamba ni kwanza tu katika karne ya tatu au ya pili kabla ya enzi za Ukristo na hasa kutokana na kuanzishwa kwa *saqiya*, ndipo wakazi wake walipoanza kurudi tena.

Mafuriko ya kila mwaka ya mto Nili yalifamkisha kilimo katika makonde ya Kerma, Letti na Nuri yaliyoko Unubi ya Juu. Sehemu nyingine wakuluna walimwagilia mashamba yao kwa kutumia vyombo vya kupandisha maji. Msingi huu wa uchumi imara ulisababisha kukua kwa miji maarufu kama vile Barkal, Kawa, Tabo, Soleb au Amara. Katika sehemu hii kilimo kilikuwa na dhima muhimu kiuchumi na mashamba ya mitende na mizabibu yanatajwa mara kadhaa katika maandishi ya nakshi ya Taharqa, Hersiotef na Nastasen. Kutoka katika ndagano ya mto Atbara na mto rukuu wa Nili kuelekea kusini, mto Nili hautiririki tena kwenye mkondo mmoja unaopita jangwani. Badala yake mto huu hugawanyika katika vijito vingine vingi ambavyo vimewezesha kustawi kwa kilimo katika ukanda huu. Baadhi ya vijito hivyo ni Atbara, Nili Samawati, Nili Nycupe, Dinder, na Rahad. Kila kimoja ya hivyo hutoa mchango muhimu katika maendeleo ya kilimo na uchumi kwa jumla kwa eneo kubwa zaidi.

Kilimo na Ufugaji

Wakati ufalme wa Napata ulipokuwa unajimarisha, ufugaji pamoja na kilimo vilikuwa

ndio msingi mkubwa wa uchumi wa himaya hiyo. Mbali na ng'ombe wenye pembe ndefu na wale wenye pembe fupi watu walifuga kondoo, mbuzi na farasi na punda, japo kwa kiasi kidogo. Ufugaji wa ngamia ulianza kunako mwishoni mwa karne ya kwanza, kabla ya enzi za Ukristo.

Umuhimu wa ufugaji wa ng'ombe katika dola ya Kushi unathibitishwa kwa njia nyingi. Kama vile, katika usawiri, katika ada za mazishi na katika sitiari. Mfano mmojawapo wa sitiari ni ule usemao: Jeshi hisilokuwa na kiongozi ni kama kundi la mifugo lisilokuwa na mchungaji.

Sadaka zilizotolewa katika mahekalu zilikuwa hasa ni mifugo na inaelekea kwamba utajiri wa wafalme, na makuhani wa mahekalu ulipimwa kwa idadi ya ng'ombe waliowamiliki. Kumbukumbu za waandishi za zamani, Strabo na Diodorus wa Sisili, haziachi wasiwasi wowote juu ya hali ya ufugaji katika jamii ya Meroe, ambayo kwa njia nyingi ilikuwa sawa na jamii za baadaye za wafugaji wa ng'ombe barani Afrika.

Katika historia yote ya Napata na Meroe, maendeleo ya kilimo katika sehemu za kaskazini yaliathiriwa na hali ya hewa pamoja na uhaba wa ardhi yenye rutuba katika bonde lile lile jeimbamba la mto Nili. Mitambo inuhimu ya umwagiliaji maji ya wakati huu ilikuwa *shaduf(u)*, mpaka ulipovumbuliwa mtambo mwingine ulioitwa *saqiya*. Choinbo hiki *saqiya* kinachoitwa *kole* kwa lugha ya Kinubi kilitokeza Unubi ya chini mnamo nyakati za Wamerote, ingawaje tarehe kamili haijulikana. Inakisiwa kwamba *saqiya* ilianza kutumika Dakka na Gamia katika karne ya tatu kabla ya enzi zetu. Kuanza kutumiwa kwa ntambo huu wa umwagiliaji maji kulikuwa na athari kubwa katika kilimo, hasa katika Dongola, kwa vile gurudumu hili hurusha maji mita 3 hadi 8 kwa kutumia nguvu na muda kidogo zaidi kuliko shadufu ambayo huendeshwa kwa nguvu za binadamu. *Saqiya*, kwa upande mwingine, huendeshwa na nyati au wanyama wengine. Nafaka kuu zilizolimwa zilikuwa ni shayiri, ngano na, mtama au *durra*. Wenyeji vile vile walilima dengu, matango, matikiti na mamumunya.

Pamba ilikuwa ni miongoni mwa mazao muhimu katika ufalme huu. Pamba ilikuwa haijulikani katika Misiri ya kale, lakini dalili nyingi zinaonyesha kwamba kulimwa kwake katika bonde la Nili kuliaza katika ufalme wa Kushi kabla ya mwanzo wa enzi zetu. Ushahidi wa nyakati za mwanzo ni kidogo sana lakini katika karne ya nne kabla ya enzi zetu kilimo cha pamba na maarifa ya kufuma na kushona nguo za pamba yalifikia kiwango cha juu katika Meroe. Inaaminika kuwa utzaji nje wa nguo ulikuwa ni mojawapo ya njia zilizotajirisha Meroe. Mfalme Ezana wa Aksum alijigamba katika maandishi yake kwamba aliharibu mashamba makubwa ya pamba ya Meroe.

Kulikuwa na bustani nyingi za natunda ya aina nibalimbali ikiwemo mizabibu iliyolimwa na watumwa. Nyingi kati ya bustani hizi zilikuwa ni mali za makuhani na wafalme. Licha ya hayo ufugaji uliendelea kushika nafasi kubwa katika uchumi wa falme za Napata na Meroe.

Madini

Hapo zamani za kale, inasemekana kuwa Ufalme wa Kush ulikuwa moja ya nchi tajiri sana

katika dunia iliyokuwa ikijulikana enzi hizo. Sifa hii ilitokana zaidi na utajiri wa madini yaliyokuwa yakipatikana sehenu za mashariki na kandokando ya bonde la mto Nili.

Madini yaliyoiletea sifa kubwa na utajiri mwingi yalikuwa ni dhahabu iliyokuwa ikichimbwa katika maeneo yaliyokuwa kati ya mto Nili na Bahari ya Sham. Uchimbaji wa hivi karibuni huko Meroe na Mussawwarat es-Sufra umeonyesha mahekalu yenye kuta na sanamu zilizofunikwa mkondo wa dhahabu. Dhahabu na uuzaji wake kwa nchi za nje haikuwa tu chanzo kikuu cha utajiri na ukubwa wa ufalme huu, bali iliathiri sana uhusiano kati ya Kushi na Misri pamoja na dola ya Warumi. Imekadiriwa kwamba hapo kale Kushi ilizalisha kilo 1,600,000 za dhahabu safi. Kwa upande mwingine, jangwa la mashariki lilikuwa na utajiri wa vito mbali mbali kama vile amethysti, kabanko, hayasinthi, kraisolithi, berili na vinginevyo. Baadhi ya migodi ilikuwa nje ya ufalme wa Meroe lakini madini yote yalipitia katika njia za biashara za Meroe, na hivyo yaliongeza umaarufu wa Meroe kama mojawapo kati ya nchi tajiri sana katika ulimwengu wa kale.

Ufuaji Chuma na Uhunzi

Malundo makubwa ya mavi ya chuma yaliyopatikana karibu na inji wa kale wa Meroe na kwingineko katika Butana vimekuwa chanzo cha udadisi juu ya umuhimu wa chuma katika ustaarabu Wameroc. Inasadikiwa kuwa maarifa ya kufua chuma na utengenezaji wa zana za chuma katika sehemu nyingi za Afrika kusini mwa Sahara yalienea kutokea Meroe. Hii inatokana na uvumbuzi uliofanywa na A.H. Sayce mwaka 1911 katika sehemu mbalimbali za ufalme wa Meroe. Mtaalamu huyo anamini kuwa kwa bara la Afrika Meroe ilikuwa kama Birmingham ilivyokuwa huko Uingereza. Hili ndilo oni lililokuwa likikubalika hadi hivi karibuni; na imekuwa nadharia iliyokubalika katika kazi nyingi zilizoshughulikia historia ya Afrika na Sudani. Lakini katika iniaka ya karibuni oni hili lililokubalika limepingwa na baadhi ya wanataaluma wakidai kwamba ushahidi uliotokana na zana za chuma zilizopatikana katika makaburi ni kigodo mno. Na kwa vyovyote vile si sahihi kuchukulia kwamba jamii fulani ina ujuzi wa kufua vyuma kwa kutazama tu mifano ya vitu vilivyotengenezwa kwa chuma.

Biashara na kustawi kwa miji

Inaaminika kwamba maendeleo ya miji katika Unubi ya Chini yalifuatia maendeleo ya siasa na kuongezeka kwa shughuli za biashara baina ya Wameroc na Wamisri. Biashara hii iliwanufaisha na kusababisha kukua kwa miji mikubwa karika sehemu muhimu kama vile Qasr Ibrim au Gebel Adda katika Nubia ya kusini. Maisha ya kisiasa na kidini yalikuwa yakitawaliwa na matajiri waliokuwa na nyadhifa mbalimbali katika serikali au jesluni. Watawala hao waliishi katika ngome kama ile iliyopo Karanog na katika majumba ya kifalme kama vile vile junba la Gavana huko Mussawarat es-sufra.

Pliny akiwakariri Bion na Juba kwa uthibitisho wa maelezo yake, amehifadhi majina ya miji mingi ya Wameroc iliyokuwa katika kingo mbili za Nili kwenye eneo lililoko kati ya Poroinoko la kwanza na mji wa Meroe.

Mji wa Faras, Pakhoras ulikuwa kituo kikuu cha utawala wa jimbo lililoitwa *Akin*,

ambalo linaelekeana na Unubi ya Chini. Majengo kadhaa yaliyotumika kwa shughuli za utawala yamechimbuliwa. Mojawapo kati ya majengo hayo ni lile lililoitwa Jumba la Kifalme la Magharibi ambalo huenda lilijengwa katika karne ya kwanza ya enzi zetu. Jengo hili limejengwa kwa matofali yaliyokaushwa juani na kuzungushwa ngome. Limejengwa ukingoni mwa mto. Makazi ya Wameroe huadimika kusini nuwa Faras. Sehemu hii ina bonde jembamba ambalo halikuweza kukidhi mahitaji ya kilimo na ufugaji wa watu mengi. Ni karibu na Dongola tu ambapo tunakuta ardhi pana na dalili nyingi za makazi ya watu hapo kale. Hakuna sehemu nyingine muhimu kati ya Kawa na Napata.

Nafasi ya Napata katika tafrija za kifalme na desturi za kidini imekwisha sisitizwa. Umuhimu wa Napata ulitokana na mahali pake mwishoni mwa njia kuu ya misafara kwa upande wa kaskazini. Njia hii imeyaambaa maporomoko matatu yasiyopitika kwa urahisi. Bidhaa zote kutoka sehemu za kusini na katikati mwa ufalme, pamoja na zile zilizotoka ndani ya bara la Afrika ilibidi zipitite Napata. Ingawa baadhi ya sehemu za mji wa Napata hazijalanyiwa uchunguzi wa kutosha, makaburi ya kifalme katika El-Kurru, Nuri na Gebel Barkal, pamoja na inahekalu ya Gebel Barkal na Sanama yamechunguzwa kwa makini. Kutokana na uchunguzi huo twaweza kuona unuhinu wa Napata kama kituo cha kifalme na kidini katika kipindi cha mwanzo cha historia ya Kush.

Kituo kingine muhimu katika eneo hili kilikuwa Dangeili iliyoko maili 5 kaskazini mwa Berber, ambapo masalia ya majengo na kuta za matofali vimevumbuliwa. Sehemu hii yenyewe inaelekea kuwa katika njia muhimu inayotoka Meroe kwenda kaskazini.

Katika kisiwa cha Meroe, ambacho kinaelekeana kidogo na nyanda za Butane ya sasa zilizoko kati ya Atbara na Nili ya samawati yamepatikana magofu ya makazi ya Wameroe.

Japokuwa inji wa Meroe unatajwa kwa mara ya kwanza katika robo ya mwisho ya karne ya tano kabla ya enzi za Ukristo katika maandishi ya nakshi ya Amannateeriko katika hekalu la kawa kwa jina la B. Rw. T. tabaka la chini kabisa la uchimbujaji linaonyesha kwamba makao makubwa yalikuwepo mahali hapa mnamo karne ya nne. Sehemu ambayo hadi sasa ilikuwa imechimbuliwa na kuchunguzwa inatosha kuonyesha kwamba Meroe katika kilele chake lilikuwa jiji kubwa lenye sifa zote za maisha ya kimji. Kwa sababu hii Meroe lazima iorodheshwe kati ya kumbukumbu muhimu za ustaarabu wa mwanzo wa bara la Afrika. Vitu muhimu vya sehemu za mji zilizochimbuliwa ni jiji la kifalme, birika la kifalme na majengo mengine, na hekalu la Amon. Karibu na hapa kulipatikana hekalu la Isis, hekalu la Simba, hekalu la Jua, inapiramidi mengi na makaburi yasiyokuwa ya kifalme.

Mahali ambapo si mbali sana kutoka Meroe kuna inakao ya Wad ben Naga yenye magofu ya mahekalu yasiyopungua mawili. Uchimbujaji wa hivi karibuni umeonyesha jengo kubwa ambalo huenda lilikuwa junba la kifalme na jengo lenye umbo la mzinga wa nyuki ambalo huenda lilikuwa ghala kubwa. Hii na miinuko mingi iliyosambaa karibu na hapa inaonyesha umuhimu wa mji huu uliokuwa makazi ya Wakandase na bandari katika mto Nili.

Kulikuwa na sehemu nyingine maarufu katika ufalme huo. Sehemu hizo ni kama Basa iliyoko Wadi Hawad, ambayo ina hekalu kubwa lililozungukwa na sanamu za simba zilizotengenezwa kwa inawe Jambo kubwa la kuzingatiwa ni kwamba mji huu haukukua

kiholelaholela tu, bali ulipangwa kwa uangalifu kufuatana na uwanda wa ardhi ambao kabla ya hapo ulikuwa na miti na vichaka. Mji mwingine uliokuwa na umuhimu wa pekee katika mambo mengi ni Mussawwarat es - sufra ulioko Wad el - Banat mbali kidogo kutoka mto Nili. Umbile lake maalumu ni Ua Mkuu ulio na majengo mengi ndani yake na nyua za kuta zinazozunguka hekalu lililojengwa mnamo karne ya kwanza kabla ya enzi zetu au mapema.

Meroe, ilisifika sana kwa shughuli za ufinyanzi. Sifa hiyo ilitokana na ubora wa vyombo vilivyotengenezwa na nakshi. Kuna mitindo miwili iliyo bayana: ufinyanzi wa mkono uliofanywa na wanawake ambao unaonyesha kuendelea kwa usanii na uzuri ambao unaakisi ufinyanzi uliojikita katika mtindo wa Kiafrika, na mtindo wa pili ulitumia gurudumu lililozungushwa. Ufinyanzi wa aina hii ulifanywa na wanaume, na uliruhusu mabadiliko mengi katika mitindo ya vyombo vilivyotengenezwa.

Usonara ulikuwa sana nyingine iliyoendelezwa sana. Vifaa vya madini vimepatikana kwa wingi katika makaburi ya kifalme. Kama ilivyo kwa vifaa vingine vya zamani, vito vya mwanzo vilitengenezwa kwa kufuatia mitindo ya Misri na ni baadaye sana wasanii walipoanza kubuni mitindo na mapambo yenye asili ya Kimeroe. Madini yaliyotumika yalikuwa hasa ni dhahabu, fedha, na vito vingine vya thamani ndogo. Madini hayo yalitumika kufulia mikufu, bangili, vipuli na pete.

Mafundi seremala nao walitengeneza aina mbalimbali za samani kama vile vitanda, vibweta, masanduku na hata ala za muziki, Wafumaji walitengeneza nguo za pamba na kitani. Walikuwepo mafundi waliopata umaarufu kwa kutengeneza vifaa mbalimbali kutokana na ngozi za wanyama.

Haya yote yanaonyesha kwamba huko Meroe kulikuwa tabaka kubwa la mafundi wa fami mbalimbali. Jinsi gani sanaa hizi zilifanywa haijulikani hadi sasa kwa vile majina ya sanaa hizi katika maandishi ya Kimeroe bado hayajafumbuliwa. Inaclekea kwamba kulikuwepo na karakana kwa ajili ya kuhudumia mahekalu kama ilivyokuwa huko Misri.

Dola ya Kushi ilikuwa kituo muafaka cha kuhifaidi na kusambaza bidhaa katika njia za misafara kati ya Bahari ya Sham, Nili ya Juu na Chad. Kwa hivyo siyo ajabu kwamba biashara ya nje ilichukua nafasi muhimu katika uchumi na siasa ya Meroe. Biashara ya nje ilielekezwa zaidi Misri na ulimwengu wa Mediterani na baadaye labda kwenda Arabia ya Kusini. Njia kuu ya biashara ilipitia kandokando ya mto Nili ingawa katika sehemu nyingine kulikuwa na njia nyingine zilizozagaa mbali zaidi. Kwa mfano inayumkinika kwamba kulikuwa na njia nyingi zilizoanzia au kuishia kisiwa cha Moroe na mji wa Napata. Misafara kutoka miji hii ilielekea jimbo la Bahari ya Sham, Ethiopia ya Kaskazini, Kordofan na Darfur. Jinsi ya kudhibiti biashara katika njia hizi nyingi lilikuwa tatizo kubwa lililowasumbua wafalme wa Meroe. Watawala walijenga ngome katika sehemu muhimu katika mbuga za Bajude - kati ya Meroe na Napata, ili kulinda njia za biashara. Vilevile walichimba visima kando kando ya njia hizi, kwa ajili ya matunizi ya wasafiri.

Mfumo wa Jamii

Ni vigumu kueleza bayana mfumo wa jamii ya wakazi wa Meroe. Mpaka sasa tunajua tu

juu ya kuwapo kwa tabaka la juu au tabaka tawala lililoundwa na mfalme na jamaa zake, tabaka tawala katika jimbo ambalo lilifanya kazi mbalimbali za kitawala na kijeshi, na makuhani maarufu walioishi katika mahekalu. Kwa upande mwingine wa kipimo cha kijamii, kumbukumbu zetu mara kwa mara hutaja kuwapo kwa watumwa waliochukuliwa kutoka kwa mateka wa vita. Kutokana na ushahidi usio dhahiri tunaweza kubahatisha kwamba ukiachilia mbali wakulima na wafugaji ambao ndio waliokuwa wakazi wengi zaidi wa Meroe, kulikuwapo na tabaka la kati la wasanii, wafanyabiashara na maafisa na watumishi mbalimbali wa ngazi za chini kaika serikali. Lakini hatujui chochote kabisa kuhusu hadhi yao ya kijamii. Hadi hapo ushahidi zaidi utakopatikana, jaribio lolote la kuonyesha aina ya mahusiano ya kijamii na ya uzalishaji haina budi kufanywa kwa tahadhari sana.

Dini

Maumbile yake kwa jumla

Watu wa Meroe walipata fikra zao nyingi za kidini kutoka Misri. Miungu mingi iliyoabudiwa katika mahekalu ya Meroe inafanana na ile ya Misri, na wafalme wa mwanzo wa Meroe walimtambua Amon, Mungu mkuu, kwani waliamini kuwa walipata haki zao za kiti cha enzi kutoka kwake. Makuhani wa mahekalu ya Amon walikuwa na ushawishi mkubwa, hadi wakati wa Mfalme Ergameno, ambaye inaelekea alivunja nguvu zao. Lakini hata wafalme waliofuata walionyesha heshima kwa Amon na makuhani wake. Waliwatunukia makuhani wa Amon zawadi za dhahabu, watumwa, ng'ombe na mali nyingine.

Pamoja na miungu wengi wa Kifarao, kama vile Isis, Horus, Thotli, Arcusnuphis, Satis, na ishara zao za mwanzo, miungu halisi wa Meroe waliabudiwa kama vile Mungu-Simba Apedemak au Mungu Sebewyemeker (*Sbomeker*). Mahehebu rasmi ya miungu hawa yalianza baadaye kama katika karne ya tatu kabla ya enzi zetu. Inaelekea kwamba wali walikuwa ni miungu wa sehemu ndogo tu ya sehemu za kusini na dola na walipata umaarufu tu wakati athari za Misri zilipoanza kufifia na nafasi yake kuchukuliwa na hati na lugha ya Meroe.

Apedemak, mungu mpiganaji, alikuwa mungu mwenye umuliimu mkubwa kwa Wameroe. Anasawiriwa na kichwa cha simba na simba walichukua nafasi fulani katika sherehe za hekalu, hasa huko Mussawarat es-Sufra. Naye Sebewyemeker aliabudiwa sana katika sehemu hii kwani alifikiriwa kuwa ni muumbaji. Mungu huyu hakujulikana kwa Wamisri. Miungu wengine wa kike nao wanaonyeshwa huko Naqa lakini majina yao na mahali pao katika jamii ya miungu ya Meroe bado havijulikani.

Mahekalu ya Amon

Kuwepo kwa makundi mawili ya miungu, moja la Misri na jingine lenye asili yake papa hapa, kunaonyeshwa pia katika usanifu majengo wa mahekalu.

Ishara za kidini zilichukua nafasi muhinu katika kusanifu mahekalu ya Misiri ya kale. Kitengo cha ibada kilionyesha kwa matambiko mengi yaliyochangamana na kila sehemu

ya hekalu ilikuwa na nafasi mahsusi wakati wa kutambika. Sehemu hizi mbalimbali, kama vile kumbi, nyua na baraza, zilipangwa katika msitari zikatoa mfano wa ujia mrefu wa maandamano. Mahekalu kama haya yalijengwa katika jimbo la Dongol na Piankhi na Taharqa, na wale waliowarithi. Hekalu muhimu zaidi kati ya haya lililotolewa wakfu kwa Amon-Re wa Napata lilijengwa Gebel Barkal.

Kwa upande mwingine maandishi nakshi ya mwanzo juu ya sherehe za kumtawaza mfalme hazionyeshi kama Meroe ilikuwa na hekalu la Amon.

Mahekalu ya Simba

Hekalu la simba limetokana na sanamu za simba zinazoonekana kila mahali karibu na jengo lenyewe. Baadhi ni sanamu zilizochongwa katika mawe yanayolinda lango la Hekalu. Sanamu hizi ni ishara inayomtambulisha Apedemak, Mungu mkuu wa Meroe. Hii haina maana kwamba kila hekalu la aina hii lililotolewa wakfu kwa Apendemak pekee. Yalikuwapo mahekalu mengine yaliyojengwa kwa ajili ya miungu wengine, kwa mfano kulikuwa na hekalu la Isis, hekalu la Sun, hekalu kuu - Augustus, Baraza la Fresco, na kadhalika. Matumizi ya istilahi hekalu la simba yalikusudiwa kuondoa mkanganyiko ambao umgeweza kutokea baadaye. Katika baadhi ya sehemu sanamu za kondoo dume ndizo zilizotumika badala ya simba hata pale ambapo Apedemak alikuwa miongoni mwa miungu walioabudiwa. Ingawa miungu wenye vichwa vya kondoo dume, Amon-Re na Khnum, wanaonekana nara nyingi katika kuta za juu za mahekalu haya ya simba hakuna wakati ambapo sanamu ya kondoo dume imehusishwa na mahekalu ya simba.

Mtawanyo na aina za mahekalu ya simba

Mbali ya mahekalu ya simba thelathini na mawili ambayo yamerekodiwa, zipo sehemu nyingine kumi na nne ambazo ni dhahiri zilikuwa na mahekalu ya simba. Tukiongeza katika idadi hii vyeo vya kikuhani vinavyohusiana na mahekalu kama yale yaliyopo Nalete na Teye, twaweza kupata idadi kubwa sana ya mahekalu huko Meroe. Yaonekana mahekalu haya yalisambaa kote Meroe. Kutokana na uchunguzi wa mtawanyo mambo mawili hudhihirika wazi: kwanza kwamba kuna maeneo manne ambako mahekalu kadhaa yamevumbuliwa. Maeneo haya ni Naga, mahekalu manne; Mussawwarat es Sufra na Meroe mahekalu sita kila mji, na Gebel Barkal, mahekalu matatu.

Pili, mahekalu ya simba yote yanaweza kugawanywa katika aina mbili kuu. Ya kwanza ni hekalu lenye baraza mbili, mifano ya awali kabisa ya aina hii ikiwa imejengwa kwa matofali ya udongo na yasiyo na lango lililonakshiwa. Aina ya pili ina baraza moja tu na mengi ya mahekalu haya yana lango la hekalu lililonakshiwa.

Kuna hali mbili za mahali hapo zinazoweza kutumiwa mahekalu ya simba yalivyozuka. Yaelekea ujenzi huu ulitokana na maendeleo ya kiufundi ya ujenzi wa aina ya kwanza. Hii yathibitishwa na ujenzi wa -900 baadaye ikiwa na usanifu wa aina ya pili. Kwa upande mwingine, kuna majengo kadhaa madogo yenye baraza moja huko Barkal na Kerma ambayo huenda ndiyo asili ya aina ya pili ya ujenzi. Mifano ya mwanzo ya aina hii inaweza kuonekana labda chini ya Meroe M 250 iliyojengwa enzi za Aspelta na chini ya hekalu

nambai 100 ya Mussarawat es-Sufra lililojengwa kabla ya - 500.

Japokuwa mtu anapoyatazama haya malekalu ya aina mbili aina ya Amon na aina ya simba-kwa mara ya kwanza lupata fikra za kuwepo kwa namna mbili za dini. Lakini baada ya kufikiria kwa makini inadhihirika kwamba kwa kweli kulikuwepo na dini moja tu luuko Meroe. Kwa sababu kuwapo kwa dini mbili kunamaanisha kwamba, kulikuwepo na uvumilivu wa hali juu wa tofauti za kidini hali ambayo si ya kutarajiwa katika nyakati hizo. Vinginevyo ingemaanisha kuwapo kwa mikinzano mikali na vita vya kidini vya mara kwa mara, jambo ambalo halionekani katika aina yoyote ya kumbukumbu. Kinyume na hivi, jamii ya miungu iliyoabudiwa karika mahekalu ya Amon yaelekea pia kuwa ndiyo iliabudiwa karika mahekalu ya simba, isipokuwa kwamba miungu mingine ilipewa umuhimu mkubwa katika hekalu moja kuliko ilivyokuwa katika jingine. Kwanza miungu wote ni inchanganyiko wa miungu wa Misri kama vile Amon-Re au utatu wa Osiri au Miungu wa wenyeji wa hapo kama vile Apedemak, Mandulis na Sebewyemeker. Tofauti ya michoro ya mahekalu inaonyesha tofauti katika matambiko zaidi kuliko tofauti ya dini. Matambiko yaliyofungamana na sherehe za kutawaza yalihatiji hekalu la aina ya Amon ili kuweza kuhimili maandamano na shamrashamra. Aina hii ya desturi ya kidini iliwezesha kujumuisha miungu mbali mbali na imani za kienyeji bila mikinzano na hivyo ikasaidia kuleta umoja kwa muda mrefu kwa ufalme uliotokana na vikundi tofauti.

12

Kuenea kwa Ukristo katika nchi ya Unubi

Mfumo wa kijamii na matukio ya kihistoria ya kipindi cha mwanzo cha Ukristo katika Unubi yalisababishwa na mambo mawili muhimu. Jambo la kwanza lilikuwa ni kushuka hadhi kwa ufalme wa Meroe. Jambo jingine lililikuwa ni kuingia kwa Warumi na Ukristo katika Misri, nchi iliyokuwa jirani yake kwa upande wa kaskazini. Baada ya kuanguka kwa ufalme wa Meroe, taifa la Nobade lilianzishwa katika Unubi ya kaskazini, kati ya Poromoko la kwanza na Dal, yaani sehemu iliyo kati ya Maporomoko ya Pili na ya Tatu. Taifa hili lilianzishwa baada ya mapambano ya muda mrefu kati ya Wablemi na Wanobade. Hatimaye hawa Wanobade walipata ushindi na nguvu katika bonde la Nili ua kuwafukuza Wablemi (Beja au - Buga) hadi katika jangwa la mashariki.

Uchimbujaji uliofanywa na Wapolandi katika Faras ulidhihirisha kwamba Pachoras ya zamani ilikuwa mji mkuu wa Ufalme wa Wanobade mnamo miaka ya mwisho ya ufalme huu. Hapa ndipo palipokuwepo jumba la kifalme ambalo lilibadilishwa kuwa kanisa kuu la mwanzo.

Masalia ya utamaduni wao wa kuonekana yanaonyesha kwamba tofauti katika hali zao za maisha zilikuwa kubwa. Umma ulikuwa maskini. Makaburi yao yalikuwa duni hata kumfanya mchimbujaji wa Uingereza, G.A. Von Reisner, atumie istilahi "Utamaduni wa Kundi X" kuwafafanua. Hakuona istilahi nyingine ambayo ingefaa zaidi kihistoria. Kinyume cha hali ya chini ya watu wa kawaida, matabaka ya watawala, wanamfalme na Kitala walidumisha mila za sanaa na utamaduni wa Meroe. Masalia muhimu ya kuonyesha vitu vya utamaduni wa tabaka dogo la juu la kijamii ni samani za fahari sana za makaburi maarufu ya malundo ya udongo ya huko Ballana, yaliyovumbuliwa mwaka 1938 na W.B. Emery pamoja na Jumba la kifalme la Unubi lililoko Faras na ambalo habari zake zimekwishatajwa.

Machiinbo ya Wapolandi huko Faras yalisaidia kugunduliwa chini ya Jumba la Mfalme Wanobade kanisa la Kikristo lililojengwa kwa mtofali ambayo hayakuchomwa, ambalo lazima lilijengwa kabla ya mwisho wa karne ya tano. Ni kweli kwamba tarehe hii ya zamani imepingwa hivi karibuni, lakini imedhihirika kwamba miongoni nwa makaburi ya 'Kundi -X' kumepatikana makaburi ya Wakristo na pia kwamba taa za mafuta na vyungu vya Wakristo vilivyopambwa kwa alama ya msalaba, vinaonekana katika makao ya 'Kundi -X', katika kisiwa cha Meinarti. Huu ni ushahidi mkubwa kwamba mapema sana, hata kabla ya kuingizwa kwa Ukristo nchini Unubi na Wamisionari walioongozwa na mhubiri

Julianos ambao walitumwa na Malkia Theodora wa Byzantium, imani ya Kikristo ilikuwa imewafikia Wanobade na ikawa imepata wafuasi kwa urahisi iniongoni mwa watu maskini. Hoja zaidi kulusu kuingizwa kwa Ukristo katika nchi ya Unubi mapema sana ni kuwepo kwa nyumba za watawa tangu mwisho wa karne ya tano. Kwa hiyo, inaweza kuelezwa kwa dhati kwamba dini ya Kikristo ilikuwa imepenyeza taratibu nchini Unubi kabla ya nchi hii kuongolewa rasmi mnamo mwaka +543 kulingana na maelezo ya Yohana wa Efeso.

Mambo mengi huelezea kuongolewa mapema kwa nchi ya Wanobade Dola ya Kirumi, ambayo ilikuwa bado ina uhasama dhidi ya Ukristo katika karne ya tatu, na dola ya Kikristo hadi karne ya nne, tano na sita, ziliwatesa wale ambao hawakutii amri rasmi zilizohusu dini. Tangu wakati huo Wamisri wengi na labda Wanubi pia waliokuwa wakitoroka kutoka Misri, huenda walileta imani yao kwa Wanobade waliokuwa wanaishi kusini mwa Aswan. Misafara ya wafanyabiashara ilipitia Aswan ikiwa njiani kuelekea kusini. Wafanyabiashara hawa walileta imani ya kidini pamoja na vitu vingine. Sera ya Byzantine, ya kuwa na uhusiano mzuri na nchi fulani ilikuwa na dhima kidogo katika kuenea kwa Ukristo mnamo karne ya tano na ya sita. Byzantine ilikuwa na shauku ya kubaki na uelewano mzuri na Aksum wakati walipokabiliwa na tishio la Waajemi katika Bahari ya Shamu. Katika mwaka wa +524 mkataba rasmi uliwezesha Aksum kuwepeleke Wablemi na Wanobade kushiriki katika msafara uliokuwa unepangwa wa mashambulizi huko Yemen. Ni wazi kwamba makasisi hawakusita kutumia fursa kama hii kueneza dini.

Kwa amri ya Malkia Theodora, mhubiri Julianos alitoa ubatizo wa imani juu ya hali moja ya Kristokwa watawala wa nchi pekee. Kutokana na athari ya Misri ya Kikristo, watu wake wengi walikuwa wamevutiwa na hii imani mpya na kuikubali mapema sana. Kanisa lililokuwa nje kidogo ya kiungo za Nili, lilikuwa linahudumia jumuiya ndogo ya Wakristo mapema katika karne ya sita. Kuongolewa kwa mtawala wa Wanobade kwenye Ukristo kulichukuliwa na watu wa nchi hiyo kama kitendo cha kisiasa. Hawukuwa tena na itikadi ya kidini iliyokuwa wazi ambayo ingewafungamanisha watu pamoja. Dini ya Kikristo sasa iliwapa fursa ya kufika Misri ambako aliishi Askofu katika kisiwa cha Philae tangu karne ya nne. Kwa kupitia Misri wangeweza kufika hadi Mediterani na katika kitovu cha ustaarabu wa enzi hizo, yaani, Byzantium.

Ufalme wa Wanobade (Nuba kwa Kiarabu), uliojulikana kama Nubadia, ulienea kutoka Philae hadi Poromoko la Pili. Mji wake mkuu ulikuwa Faras. Kwa upande wa kusini kuendelea hadi Moroe ya kale, ufalme mwingine wa Unubi uliibaka katika karne ya sita mji wake mkuu akiwa Dongola Kongwe (Dungula kwa Kiarabu). Ufalme huu baadaye uliitwa Makuria (Mauqurra kwa Kiarabu). Kinyume cha Unubi ya Kaskazini, ambayo ilikuwa imechukua imani ya hali moja ya Kristo Makuria iliongolewa katika dini ya Melkite na ujumbe ambao Mfalme Justinian alituma mnamo mwaka wa +567 hadi +570.

Kutokana na Matokeo ya uchinbuaji wa Wapolandi uliofanywa Dongola Kongwe tangu 1964, makanisa manne na Jumba la Mfalme wa Kikristo yamepambanuliwa. Mojawapo ya inajengo haya linafikiriwa kuwa lilijengwa ama mwishoni mwa karne ya saba au mwanzoni mwa karne ya nne. Chini yake masalia ya kanisa la inapema zaidi

lililojengwa kwa matofali ambayo hayakuclionwa limegunduliwa. Kanisa hili ambalo halikuwa kanisa kuu, lilikuwa na sehemu kubwa taro za kusali na lilihamiliwa na nguzo kumi na sita za mawe magumu, zenye urefu wa mita 5.20. Kutokana na wingi wa masalia yaliyochimbuliwa, ipo sababu ya kutosha kufikiri kwamba maelezo yenye kutia shauku yaliyotolewa na insafiri mmoja wa Kiarabu katika karne ya kumi na moja yalikuwa ni sahihi kihistoria: Dongola ulikuwa ni mji mkuu muhimu, hasa tunapotazama majumba yake ya kumbukumbu.

Hatimaye Wamakuria pia walichukna imani ya hali moja ya Kristo ya 660 na 700 na ukweli huu ulizusha matukio muhimu. Kuelekea mwaka 580, kwa msaada wa Wanobade ujumbe wa Byzantine ulikuja Alodia na kiongozi wake, Askofu Longinos, alikiri kwamba nchi hii ilikuwa imekwishaongolewa kwa kiasi fulani Waaksum. Ndiyo kusema kuelekea mwishoni mwa karne ya sita Unubi ilikuwa nchi ya Kikristo iliyokuwa na falme tatu: Nobade kwa upande wa kaskazini Makuria katikati na Alodia kwa upande wa kusini. Uhusiano na uelewanao kati yao bado haujadhihirika wazi hasa tukizingatia kwamba mwanzoni zilikuwa nchi huru.

Tangu utafiti wa Monneret de Villard, uvumbuzi nwingi wa kiakiolojia umeongezeka, hasa kutokana na Kampeni ya Unubi iliyoendeshwa kwa msaada wa Unesco mnamo mwaka 1960-5 ili kuchunguza ardhi ambayo ingemezwa na maji ya mto Nili juu ya Saad al-Aali na Bwawa Kuu. Katika sehemu nyingine za Unubi ya Kaskazini, kupanda pole pole kwa kiasi cha maji yaliyohifadhiwa katika bonde kumewezesha uchimbaji kuendelea hadi 1971, na katika Qasr Ibrim, ambayo haijafurika uchiimbaji unaendelea hadi sasa.

Matokeo ya utafiti wa miaka ya hivi karibuni, inara nyingi yamekuwa ni yenye manufaa makubwa na yamesababisha kudhihirika kwa matatizo ya Unubi ya Kikristo.

Ingawa Unubi, tofauti na Misri, haikuwa sehemu ya himaya ya Byzantine, hapana shaka kuwa kulikuwepo na ushirikiano mahsusi ulioendelezwa na mishihi za makasisi, Julianos na Longinos. Utaratibu wa serikali ya Unubi, kama majina yake yanavyoonyesha, ulipangwa kwa makini kwa kufuatia mfano wa utawala wa Byzantine. Ingawa Uajemi ulipoivamia Misri mnamo mwaka 616 waliishia katika mpaka wa Unubi, upo ushahidi kwamba ufalme wa kaskazini ulivamiwa na vikosi vya Sassanid vilivyokuwa kusini mwa Poromoko la Kwanza. Kwa vyovyote vile uvamizi wa Chosroes II ulivunja ushirikiano wa moja kwa moja kati ya Unubi na Misri, ambazo kwa wakati huo zote zilikuwa nchi za Kikristo. Uvamizi huu pia ulivunja mawasiliano kati ya viongozi wa kidini na Unubi na Uaskofu mkuu wa Alexandria ambao ulisimamia rasmi kanisa la Unubi Mnamo 641 Misri ilitwaliwa na Waarabu. Hii iliacha Wakristo wa Unubi kuhudumiwa kutoka Mediterani kwa muda mrefu sana baadaye.

Mwanzoni Waarabu hawakufikiri kwamba kulikuwa na umuhimu kuteka Unubi. Mashambulizi yao yalielekezwa kaskazini tu. Kwa hivyo, mara baada ya Misri kusalimu amri, walitiliana nikataba na Unubi. Katika mkataba huo ulioitwa *baqt* Wanubi waliwajibika kulipa ushuru kila mwaka wa watumwa na baadhi ya bidhaa kwa Waarabu, ambao nao waliwajibika kulipa Wanubi kiasi cha kutosha cha chakula na nguo. Katika muda wa karne saba za uhuru wa Unubi ya Kikristo pande zote mbili zilichukulia

mkataba kuwa halali kimsingi, lakini mapigano ya silaha ya litokea zaidi ya mara moja. Kwa hivyo, mara tu baada ya *baqt* kutiwa sahihi, Amiri Abdallah ibn Abu Sarh alishambulia Dongola mnamo 651-2; lakini shambulio hili halikuvuruga biashara iliyoendelea kati ya Unubi na Misiri ya Kiislamu.

Unubi ya Kaskazini na ya Kati zihungana kuwa nchi moja; bila shaka hii ilitokana na mkwaruzano wa kwanza kati ya Waarabu kutoka Misri na Wanubi. Maqrizi, akinukuu maandishi ya mwanzo ya Kiarabu, anasema kwamba katikati ya karne ya saba, Unubi ya Kati na ya Kaskazini yote hadi katika mipaka wa Alodia ilitawaliwa na mfalme mmoja, Qulidurut. Maandishi ya Kikristo yaelekea kuthibitisha kwamba muungano wa Unubi ulikuwa ni kazi ya Mfalme Mercurious, ambaye alitwaa ufalme mnamo 607. Yase nekana huyu mfalme ndiye ahiyeingiza imani ya hali moja ya Kristo huko Makuria. Alianzisha mji mkuu wa muungano wa ufalme katika mji wa Dongola.


Hadi leo hii suala la Uumini katika hali moja Kristo huko Unubi haliko wazi kabisa hasa kuhusu uhusiano wa ufalme wa nchi hii na kanisa la Melkite. Bado kuna uwezekano kwamba imani ya Melkite ilidumishwa kwa namna fulani katika inaceo ya ndani ya ufalme. Inafahamika kwamba hadi mnamo karne ya kumi na nne jimbo la Maris ambalo lilikuwa ufalme wa awali wa Unubi ya Kaskazini, lilikuwa chini ya Askofu wa Melkite ambaye, kama Askofu mkuu mkazi wa Tafa, alitawala jimbo lililojumlisha Unubi yote. Zaidi ya hayo kila wakati isipokuwa katika karne ya nane tu, Alexandria ilikuwa na maaskofu wakuu wawili, mmoja wa imani ya halimoja ya Kristo na mwingine wa Melkite.

Mfalme Kyriakos alipojua kwamba gayana wa Ummayyad alikuwa amemfunga Askofu Mkuu wa Aleksandria, aliishambulia Misri kwa kutumia tukio hilo kama kisingizio na akaingia hadi Fustat. Mara baada ya Askofu Mkuu kuachiliwa huru, Wanubi walirejea nyumbani. Shambulio la Kyriakos huko Fustat linadhihirisha kwamba Unubi haikuwa ikijithami tu, bali iliweza pia kuishambulia Misri ya Kiislamu.

Mashambulio ya kijeshi, hata hivyo, siyo ushahidi pekee wa nguvu za nchi ya Unubi katika miaka iliyofuatia karne ya nane. Uyumbuzi wa kiakiolojia umedhihirisha pia maendeleo makubwa ajabu katika utamaduni, sanaa na usanifu wa minara huko Unubi kwenye kipindi hicho. Mnamo mwaka 707 Askofu Paulos ahlijenga upya Kanisa Kuu la Faras na akalipamba kwa picha nzuri za ukutani.

Majengo muhimu kadha ya kidimi katika Dongola Kongwe yalijengwa katika kipindi hicho. Makanisa mengine ya Unubi kama yale ya Abdallah Nirgi na Al-Sabu'a, yalipambwa vizuri kwa picha za kutani ambazo zilikuwa unbo lenye mvuto wa kudumu katika mapambo ya sherehe.

Kipindi cha Kikristo kilikuwa ni wakati yalipopatikana maendeleo ya haraka ya uchumi. Idadi ya watu wa Unubi ya Kaskazini ilikuwa kama 50,000. Kuanzishwa kwa unwagiliaji inaji mashambani kwa *Sakiya* (gurudumu la maji), katika enzi za Ptolemi na Warumi, kulipanaua eneo lililolimwa kulimwagia inaji kati ya mafuriko mengi ya Nili ya wakati huo. Maeneo haya yalizalisha ngano, shayiri, mtama na mizabibu. Wingi wa myuno kutoka katika mashamba ya michikichi pia yaliongeza kiwango cha maisha ya watu nchi humo.



12.1 *Kanisa la Faras*

Biashara na nchi jirani iliongozeka na kuenea mbali. Wakazi wa Makuria waliuza meno ya ndovu kwa Byzantium na shaba nyekundu na dhahabu kwa Ethiopia. Misafara ya wafanya biashara wao ilienda hadi katikati ya bara la Afrika, hadi katika nchi ambazo zinajulikana leo kama Nigeria na Ghana, kwa kutumia mitumbwi ya makasia na ngamia. Matabaka ya matajiri yalipendela nguo za Byzantine. Wanawake walivaa kanzu ndefu, ambazo mara nyingi zilipambwa kwa nakslu za rangi.

Kama ilivyokwishasemwa, utaratibu wa utawala katika Unubi ya Kikristo ulifanana na ule wa Byzantium. Gavana wa kirai wa jimbo alikuwa Askofu Mkuu, ambaye mamlaka yake yalionyeshwa kwa ishara na taji yenye pembe ambayo aliivaa juu ya kofia ya chuma iliyopambwa kwa sura ya mwezi mwandamo. Kwa kawaida alivaa joho refu lililoshikwa kwa mshazamu. Tarazo za tepe za Maaskofu ambazo walizivaa juu ya mavazi yao ya fahari ya shughuli za kidini, zilipambwa kwa kengele ndogo.

Umaarufu wa Wanubi katika utupaji mishale umethibitishwa na waandishi wengi wa kale na wa Kiarabu. Zaidi ya upinde walitumia sime na mkuki.

Majengo ya wakfu, isipokuwa baadhi ndogo tu yalijengwa kwa matofali ambayo hayakuchoniwa. Makanisa makuu ya Qasr Ibrim, Faras na Dongola ndiyo pekee yaliyokuwa na kuta za mawe au matofali ya kuchoniwa. Makanisa inengi yalijengwa katika umbo la nyumba ya kanisa, lakini majengo yenye umbo la msalaba au makanisa yenye mpango wa kati nayo yameonekana wakati mwingine katika usanifu majengo wa Kinubi. Mapambo ya kipindi cha kwanza, yaani, hadi kufikia mwisho wa karne ya saba yanaweza tu kuchakuliwa kutoka katika makanisa ya kumbukumbu yaliyotajwa hapo juu.

Mapambo kwenye majengo yalifanywa kwa mawe ya mchanga uliogandamana isipokuwa kwenye sehemu za majengo ya wapagani walioongoka kama yale yaliyokuwa huko Faras. Mapambo hayo yalirudia rudia sulubu za kuviringa zilizokopwa na sanaa ya Wameroc kutoka kwa sanaa ya Kiyunani ya mashariki ya himaya ya Warumi. Ilikuwapo pia michoro mizuri inayopindapinda ya miji mikuu iliyopambwa. Sanamu za utakatifu ambazo zilichorwa kwenye vipande vya mbao au kuchongwa huenda zilitumiwa wakati huo kama sanamu za ibada.

Kumbakumbu za kale za sanaa ya Kikristo huko Unubi zimeathiriwa sana na Misri ya Kikoptiki. Hii inadhilurishwa zaidi na vitu vilivyochorwa mumo kama vile mapambo ya njiwa viambazani au tai wanaojikumbusha taswira za waliochorwa kwenye mawe ya Kikoptiki.

Kuanzia karne ya nne na kuendelea makanisa ya Unubi yalipambwa kwa michoro ya nakshi. Uvumbuzi uliofanyika Faras mwaka +1961 hadi +1964 wa michoro ya kutani zaidi ya 120 iliyo katika hali nzuri zikiwaino picha za Maaskofu ambao tarehe zao za uongozi zinaweza kuonekana katika orodha ya Maaskofu, umefanya iwezekane kufasiri maendeleo ya jumla ya mtindo wa michoro ya Unubi. Fasiri hizi zinathibitishwa na michoro michache ya kutani itokayo katika makanisa inengine ya Unubi.

Bila shaka Faras ilikuwa wakati huo, kituo kikuu cha sanaa hasa katika Unubi ya Kaskazini. Mtindo wa michoro iliyopatikana kaskazini mwa Faras huko Abdallah Nirqi na Tawit na kusini mwake huko Songi Tino, ni dhahiri ulikuwa wa huko huko jimboni hasa



12.2 Kichwa cha Mtakatifu Anne: Kaskazini ya Aisle ya Kanisa la Faras



12.3 Ufinyanzi wa Unubi ya Kikristo

michoro hii ikilinganishwa na sanaa maarufu zilizopo Faras.

Tangu mwanzo wa karne ya nane hadi katikati ya karne ya tisa, wachoraji wa Unubi walipendelea katia rangi za urujuani katika picha zao. Kipindi hiki cha uchoraji wa Kinubi kiliathiriwa sana na sanaa ya Kikoptiki, sanaa ambayo imetokana na mtindo wa picha za Fayum. Mojawapo ya kazi zinazowakilisha kipindi hicho ni ile ya kichwa cha Mtakatifu Anne wa Faras (ambacho sasa kipo katika jumba la makumbusho la Warsaw) lakini athari za sanaa ya Byzantine na maudhui yake yaweza kuonekana pia.

Baadaye mtindo ule uliendelea, na hadi kufikia katikati ya karne ya kumi picha za rangi nyeupe ziliongezeka sana. Huenda hii imetokana na athari ya michoro ya Kisiria na Kipalestina ambayo inabainishwa waziwazi na mikunjo miwili ya mavazi na maumbile mengine ya usawiri. Yawezekana nafasi ya Jerusalem kama mahali ambapo watu wengi kutoka nchi zote za Kikristo za Mashariki walifanya ziara za kidini wakati huo ndiyo sababu ya maendeleo haya ya uchoraji wa Unubi katika kipindi hicho.

Uhusiano mkubwa kati ya ufalme uliozingatia imani ya hali moja ya Kristo na waumini wengine wa imani hii wa madhehebu ya Yakobo wa Antiokia, uliendelea wakati huo, Shemasi John na Abu Salih, wote wameeleza kwamba wakati wa utawala wa Mfalme Kyriakos, Askofu Mkuu wa Alexandria wa madhehebu ya Yakobo alikuwa Mkuu wa kanisa la Unubi. Mwelekeo mkubwa wa kiyakinifu ulionekana kwa mara ya kwanza katika uchoraji wa Unubi; mfano wake mzuri ukiwa ni picha ya Askofu Kyros wa Faras (ambayo sasa ipo katika jumba la makumbusho la Khartoum).

Uchumbuaji umetoa vitu vingi ambavyo kati yake vyombo vya udongo ni vingi zaidi. W.Y. Adams amefanya uchunguzi muafaka wa vitu hivi. Ainegundua kwamba vinatoa ushahidi wa maendeleo mazuri ya mtindo wa ufundi na uchumi wa kijamii.

Hata kabla ya mwaka +750, Aswan ilizipelekea nchi za kusini vyombo vya udongo vya kutosha vilivyotumika hako. Biashara hii haikuingiliwa wakati Waislamu walipotamamani Misri.

Hadi karne ya tisa Unubi ilifurahia kipindi cha ufanisi ambacho kiliendelea pasipo kuingiliwa sana na majirani wao Waislamu ambao kwa kawaida walikuwa watu wa amani. Ni vigumu kupambanua ikiwa Unubi ya Kikristo ilikuwa na utamaduni mmoja. Huko Faras maafisa tawala walizungumza Kiyunani kama walivyofanya wastahiki wa kanisa. Vongozi wa dini pia walielewa Kikoptiki, ambacho huenda ilikuwa lugha ya wakimbizi wengi. Ingawa Kinubi kilizungumzwa sana na watu, kumbukumbu pekee zilizoko za maandishi ya lugha hii ni za kipindi cha baadaye ambacho huenda ni cha miaka ya katikati ya karne ya tisa.

Kipindi cha ustawi wa Unubi ya Kikristo, mnaino mwaka +800 kilikuwa hakijawadia.

Mikoa ya kaskazini mwa Ethiopia haielekei kama ilikuwa na idadi kubwa ya watu katika miaka ya awali. Taarifa chache tulizonazo zinaonyesha kwamba makundi ya watu walianza kuongezeka huono kama ilivyofanyika katika sehemu nyingine za Pembe ya Afrika.

Katika kipindi cha karibu elfia kumi kabla ya enzi zetu, yaelekea wafugaji waliishi katika eneo hili. Watu hawa walichora picha za ng'ombe wao wenye pembe na wasio na nundu katika sehemu zenye miamba mingi iliyoanzia kaskazini mwa Eritrea mpaka Hareri. Mifugo yao ilifanana na ile iliyofugwa katika kipindi hicho hicho huko Sahara na katika bonde la Mto Nili. Watu hawa walikuwa na uhusiano na watu wa Misri tokea miaka mingi ya nyuma.

Kwa upande wa lugha Kikushi pia kilikuwa na umuhimu. Lugha hii ilikuwa na asili yake mahali hapa na ilianza kujulikana katika sehemu nyingine. Ugunduzi wa hivi karibuni huko Gobedra karibu na Aksum unaonyesha kwamba kilimo cha mtama na matumizi ya vyonibo vya udongo vilianza katika elfia ya tatu au ya nne. Kwa hiyo zipo sababu za kutufanya tuamini ya kuwa, pamoja na kuwepo kwa shughuli za uchungaji wa mifugo, shughuli za kilimo kama zile zilizokuwa zikifanyika Ethiopia zilianza kuendelezwa katika kipindi hiki. Mbinu hizi mpya huenda zilizhusiana na maisha ya utulivu katika makazi ya kudumu. Maisha ya namna hii yalijenga hali muafaka za kukuza ustaarabu wa hali ya juu.

Ingawa kuanzishwa kwa jiji la Aksum na kuinukia kwa Ufalme wa Aksum vyafikiriwa vilitokea mnamo karne ya pili kabla ya enzi zetu kulingana na ushahidi wa mwanajiografia Claudis Ptolemy alioungwa mkono miaka mita moja baadaye na "*Periplus Maris Erythraei*" na ugunduzi wa kiakiolojia, Waandishi wa kale wa Kiyunani na Kilatini hawatuelezi lolote kuhusu karne zilizotangulia matukio haya.

Jambo pekee wanalotueleza ni kwamba mnamo katikati ya karne ya tatu kabla ya enzi za Ukristo, Ptolemy II alijenga Philadelphus na bandari ya Adulis. Bandari hii ilipamuliwa na mrithi wake Ptolemy III na mnamo mwaka +75 Pliny alieleza kwamba hii ilikuwa mojawapo ya bandari muhimu katika Bahari ya Sham. Pliny vile vile anataja habari kuhusu makabila mengi ya Asachae ambayo yaliishi kwa kutegemea uwindaji wa tembo katika

milima iliyokuwa umbali wa mwendo wa siku tano kutoka baharini. Uhusiano ambao mara kwa mara umefikiriwa kuwepo kati ya jina la makabila haya na lile la Aksum ni wa kubahatisha.

Mbali ya masimulizi ya ngano, taarifa muhimu lazima zitafutwe kutoka kwenye mfululizo wa ugunduzi wa kiakiolojia uliokwihafanyika tangu mwanzoni mwa karne ya ishirini. Ugunduzi huo unatuwezesha kuunda na kupanga upya kipindi cha kabla ya utawala wa Aksum ambacho kutokana na utafiti W.F. Anfray, kina sehemu mbili: kipindi cha kusini mwa Bara Arabuni na kipindi cha mabadiliko.

Kipindi cha Kusini mwa Bara Arabuni

Hiki ni kipindi ambapo athari ya kusini mwa Uarabuni ilikuwa kubwa mno kaskazini mwa Ethiopia. Ishara kuu ya athari hizo ni kuwapo kwa minara ya ukumbusho na maandishi nakshi huko Eritrea na Tigre yanayofanana na yale ya huko kusini mwa Bara Arabuni wakati wa utawala wa ufalme wa Saba. Utafiti wa J. Pirenne maandishi ya kale na mitindo yake umetuwezesha kutambua kwamba mifano iliyoonekana kusini mwa Bara Arabuni ilikuwa ya karne ya nne na ya tano kabla ya enzi za Ukristo. Kwa jumla inakubaliwa kuwa tarehe hizi pia zinaweza kutumika kwa ugunduzi uliofanyika huko Ethiopia, ingawaje nadhari tete iliyotolewa na C. Conti-Rossini kuhusu kupishana kwa nyakati kati ya pwani mbili za Bahari ya Sham haiwezi kupuuzwa. Kwa maoni ya F. Anfray, "ipo sababu ya kufikiri kwamba hapo baadaye kutakuwa na haja ya kupunguza kipindi hicho cha muda, na pengine kusogeza mbele tarehe za kipindi cha kusini mwa Bara Arabuni".

Jengo pekee la kihistoria lililobakia katika kipindi hiki ni hekalu la Yeha. Hekalu hilo limejengwa kwa mapande makubwa ya mawe ambayo yameunganishwa kwa ustadi mkubwa sana, na huku yakiwa na marembo na nakshi inbalimbali. Pia kuna chumba cha pembe mraba chenye ukubwa wa mita 18.6 kwa mita 15, kilichogemezwa kwenye sakafu ya kipiramidi yenye rusu nane. J. Pirenne anasema ya kwamba sura za mbele za jengo hilo ambazo zimehifadhiwa hadi kiasi cha mita 9 hivi, zimetengenezwa kwa namna iliyosawa na majengo mengine mengi yaliyoonekana huko Mârib, mji mkuu wa Ufalme wa Saba. Hata hivyo muundo wa jengo hili la Yeha haulingani na ule wa madhabahu mengine ya kusini mwa Bara Arabuni tunayoyafamu. Jengo jingine ambalo limeharibiwa vibaya sana huko Yeha lina nguzo za mawe za pembe mraba zilizosimama kwenye matungazi ya juu. Jengo hilo liko Grat-Beal-Guebri na hivi sasa linachimbuliwa. Yaelekea jengo hili ni la kipindi kinachojadiliwa. Nguzo kama hizo zipo katika maeneo mengine mawili. Baadhi ya nguzo hizo zinaonekana kwenye kilele cha kilima cha Haoulti, kusini mwa Aksum zikiwa zimesimama bila mpangilio maalum, na luenda hazipo kwenye mahali pake pa asili. Huko Kaskase, kwenye barabara ya kutoka Yeha kwenda Adulis, kuna nguzo sita ambazo mpangilio wake bado haujaeleweka, kwani eneo lenyewe bado halijachimbuliwa. Nguzo hizi zinafanana na safu za nguzo kubwa zenye pembe nne zinazopamba madhabahu na Marib (Awwam, Bai'an) na Tinuna (hekalu la Ashtar).

Sanamu za kuchongwa zilizopatikana Yeha pia zinaashiria kuwa zimetoka Marib. Baadhi yake ni sanamu za aina ya mbuzi wenye pembe ndefu, zilizochongwa kwenye

vipande vya bati, ambazo pia huonekana katika jimbo la Melazo mjimi Haoulti na Enda Cerqos. Michoro hiyo huenda ilitumika kama nakshi za ukutani. Eneo la Melazo limetokea kuwa na mabaki mengi ya sanamu hizo ambazo ni za kipindi cha kusini mwa Bara Arabuni. Pamoja na mawe ya Haoulti na vipambo vilivyokwishatajwa, kuna kazi nyingine zilizotumiwa tena baadaye baada ya kufanyiwa marekebisho. Mifano mingine maarufu zaidi ni sehemu za ndani za mahekalu na sanamu zilizogunduliwa huko Haoulti.

Mnara wa ukumbusho unaitwa 'naos' kutokana na pendekezo la J. Pirenne umechongwa kutokana na kipande kimoja cha jiwe la chokaa lenye urefu wa kama sentimeta 140 hivi. Una miguu minne inayofanana na miguu ya ng'ombe dume. Miguu hii huegemeza msingi uliopambwa kwa fito mbili zilizokaa juu ya shubaka lenye mapambo kote isipokuwa upande wa nyuma ambao ni laimi. Juu ya shubaka hilo kuna jukwaa lililo na umbo la tao lililo inamishwa lenye upana wa sentimeta 67 na kina cha sentimeta 57. Katika pembe zake ambazo zina kimo cha sentimeta 7 kuna safu mbili za michoro ya mbuzi mwitu inayokutana mwishoni na kuunda kitu kinacho fanana na mti uliosimama kwenye ncha ya sehemu ya ndani ya "naos". Hali kadhalika michoro mingine ya mbuzi mwitu huelekea upande wa shubaka na huenea katika kingo za pande zote mbili za fito zenye upana wa sentimeta 13 zilizowekwa juu yake.

Schemu ya nje ya kila upande imerembwa kwa sanamu nakshi za namna moja zionyeshazo sura ya mtu asiye na ndevu aliyeshika gongo mbele ya sura ya mtu mnene mwenye ndevu aliyeshika namna ya upepeo. Pua zao zimekunjika kidogo ikitoa sura ya Kisemitiki, na nywele zao zimewakilishwa kwa michoro ya umbo lenye pembe nne. Sanamu ndogo imevalishwa joho linalofika hadi kwenye kifundo cha mguu na mtandio mabegani. Upande wa kulia wa "naos" limeandikwa jina halisi la kiume juu ya kichwa cnake kwa maandishi ya Ki-saba: 'RFS' (*Rafash*). Sanamu kubwa imevalishwa kikoi kilichopwaya chenye kipande cha nguo kinachoning'inia kwa nyuma. Kiunoni vazi hilo limeshikiliwa na mkanda uliofungwa kwa nyuma na ncha yake moja ikining'imia. Juba iliyotupwa mabegani hushikizwa mahali pake kwa pembe zake mbili kufungwa kwenye fundo kubwa kifurani mwake. Katika sanamu nakshi iliyoko upande wa kushoto ameshika kitu kinachoelezwa kuwa ni upepeo kwa mikono yake miwili. Lakini katika sanamu ya upende wa kulia amevaa bangili ya pembe mraba katika mkono wake wa kushoto huku akiwa ameshika rungu kwa mkono wake wa kulia.

Eneo hilo huko Habulti limetoka sanamu kadhaa zinazofanana na ambazo, kati yao, ni moja tu iliyokaribia kuwa kamili. Sanamu hiyo ni ya sura ya mwanamke aliyekaa chini na mikono yake ameiweka magotini. Amevaa joho refu lenye mikunjo iliyosimama ikifuatilia umbile lake. Juu ya joho hilo mwanamke hnyo amevaa mkufu wenye kamba tatu nene zilionakshiwa. Katika kamba hizo imefungwa tasbihi. Hivi vimeshikiliwa kwa nyuma na pambo mfano wa pembea lenye vishina sita linaloning'inia katikati ya mabega. Sanamu hiyo ilikusudiwa kuenea kwenye kiti kwani sehemu ya nyuma ya miguu imekuwa bapa, na una mburuto wa wima ulioharibika katikati.

Mbali ya vipande vipande vya sanamu mbili hivi zinazofanana, kulikuwa na sanamu nyingine isiyo na kichwa iliyotengenezwa kwa ufundi mdogo kuliko ile iliyoelezwa juu.

Sanamu hii hutofautiana na hivyo nyingine kwa sababu lina pambo la mkufu wenye kamba tatu zilizopakishwa na imekaa kwenye kibago kulichopambwa kwa ufito.

Namna sanamu za Houlti zilivyokaa inakumbusha mkao wa sanamu iliyovumbuliwa, kwa bahati tu, ikiwa pamoja na vitu vingine vya kale huko Addi Galamo, pembe ya magharibi ya uwanda wa Tigre. Sanamu yenyewe ina kimo cha sentimeta 40. Mikono yake imekaa magotini ikiwa inashikilia vikombe viwili vya miringo ambayo vilikusudiwa kuwa vyombo vya kuwekea sadaka. Nywele zimewakilishwa kwa michoro ya maumbo yenye pembe nne. Nywele hizo pia zina michoro ya mfuo wa mkufu pamoja na bangili ambazo huenda zilitengenezwa kwa madini ya thamani. Vazi lenyewe halina pindo lakini lina marembo marembo mfano wa mana ya waridi, na linaishia ukingoni. Kiti cheneyewe kimepambwa kwa ufito.

F. Anfray alipochimbua eneo la Matara, eneo muhimu karibu na Kaskase, alifukua sehemu ya kichwa kilichofanana sana na kichwa cha Haoulti katika tabaka la kilima B la kipindi kabla, ya utawala wa Aksum. Lakini ufundi uliotumika katika kazi hiyo ni ule wa mwanzoni mwanzoni na inambo mengi kwenye sanamu hii huonekana katika sehemu za kuchongwa zilizotokeza.

Sanamu nyingine iliyopo katika Jumba la Makumbusho huko Roma (MNR 12113) ina mambo mengi yanayofanana na yale ya sanamu za Haoulti. Sanamu hiyo inaonekana kuwa ni ya mwanamke aliyekaa chini, miguu yake imevunjika na kichwa kimevunjika pia. Kimo chake ni sentimeta 23.7. Mwanamke huyo amevaa vazi refu na jembamba. Pia amevaa mkufu wenye kamba mbili zilizopakishiwa. Katika mkufu huu huning'inia shanga, tasbihi na kidani. Sehemu ya chini ya sanamu imechongwa kitu mfano wa pembea, na juu ya pembea hiyo kumeandikwa jina la kusini mwa Bara Arabuni la Kanan. J. Pirenne anafikiri maandishi hayo ni ya mwisho wa karne ya nne kabla ya enzi za Ukristo.

Kusini mwa Bara Arabuni mpaka sasa imetoa tu vitu vyenye unibo la kuka, baadhi yake vikiwa vya maumbule ya kike; huonyesha, wanawake waliokaa katika sanamu nakshi za mazishi zinazopatikana Marib, Haz na katika Jumba la Makumbusho la Aden. J. Pirenne huchukulia sanamu ya Bibi Barlat akiwa Timna, kama mungu mkuu wa kike wa kusini mwa Bara Arabuni.

Mapema katika karne ya tisa na ya nane kabla ya enzi za Ukristo aina ya sanamu ya mwanamke aliyekaa au mungu, ambaye mara nyingi alishika chombo cha kunywa, ilipatikana sana katika eneo lililotawaliwa na Wasiria na Wahiti.

Inaelekea kuwa kuna uhusiano halisi kati ya sanamu za Ethiopia na zile za Asia Ndogo za kipindi cha mwishoni mwa karne ya saba na mwanzoni mwa karne ya sita kabla ya enzi zetu. J. Pirenne tayari alikwishafanua baadhi ya uhusiano kati ya sanaa za Kiyunani zenye athari za Mashariki ambazo ni za karne ya sita au mtindo uliotokana na mtindo ya karne ya tano na sanaa ya kusini mwa Bara Arabuni.

Wakati mifano ya sanamu inayofanana inapatikana hasa katika Mashariki ya karibu ya Wasemitiki na ulimwengu wa Kiyunani wenye athari za Mashariki upo ushahidi wa athari za ki-Misri, na hasa pia zile za Meroe kwenye mikufu. Ushahidi huu umeanzishwa na 'mankhit' na kama alivyogundna J. Pirenne, majoho yenye pindo yanakunibusha kanzu

fupi za malkia wa Meroe na unene wa mwili aliorithi kutoka kwa Ati wa Punt, aliyeishi wakati mmoja na Hatshepsut.

Ulinganisho kama huu unaonyesha tofauti za athari zilizoonekana kwenye sanamu hizi za wanawake waliokaa wa Tigre. Hata hivyo sanamu hizi hazionyeshi kwamba zinawakilisha nini hasa. Haiwezekani pia kufikia hitimisho lolote juu ya msingi ulionakshiwa uliopatikana huko Addi Galamo ambayo yaelekea inahusiana na sanamu hizi. Ni vigumu kusema kama hawa walikuwa malkia au watu mashuhuri, au ikiwa wanawakilisha miungu wakuu wa kike anavyoamini J. Pirenne.

Kwa msingi huo tutaelekea kuikataa nadharia tete juu ya kiti cha kifalme kilichopatikana Phoenicia, Adulis au Tacazze. Kisha kulikataa nadharia tete hiyo twapaswa kurejea kwenye mtazamo wetu wa awali wa kuchukulia, alivyofanya sema J. Pirenne, kwamba sanamu hiyo ni aina ya 'naos' iliyotengenezwa kwa jiwe ambako sanamu ya ibada iliegeshwa. Mbali ya vipande vipande vya sanamu vilivyopatikana huko Haoulti, ambavyo huenda vilitoka kwenye mnara wa makumbusho wa aina moja "naos" hii ni ya kipekee kabisa.


Inagwa hakuna kitu chochote cha mfano wake kilichopatikana huko kusini mwa bara Arabuni - ambacho kimetokana na uchunguzi wa sasa wa kiakiolojia nchini Yemen - baadhi ya maumbile yake yamepatikana huko, na kuna majaribio ya kuyaweka pamoja ili kuyapambanua.

Kwato za n'gombe dume yule yule zimeonekana katika samani za mawe zilizoainishwa na G. Van Beek, na katika sanamu ya marumaru ya Marib. Sanamu za mbuzi-pori walioinana kidogo, na ambao wamepangwa katika vyumba vya pembe mraba vilivyowekwa moja juu ya nyingine na katika ukingo jiwe bapa ambao mfano wake umegunduliwa hivi karibu huko Matara, huonekana mara kwa mara katika jimbo la Saba (Marib, Haz).

Vile vile tunakuta sanamu za rubuzi pori zinazohusishwa sanamu za mti uliochongwa kwa mtindo maalum ambazo yaelekea matunda yake yanaliwa na mbuzi mwitu hao. Sanamu hizi zinaonekana katika madhabalu ya Marib. Umuhimu wa kidini wa mbuzi hao wawe wanahusiana na "mti wa uhai" au la, waelekea kufahamika vyema. Grohmann yaelekea aliweza kuthibitisha kuwa mbuzi hao ni alaina ya mungu wa mwezi ajulikanaye kwa jina la Almaqah. Ng'ombe dume pia alikuwa ametolewa wakfu kwa mungu huyu wa mwezi.

Wakati ufundi wa michoro ya sanamu nakshi za pembezoni unakaribiana sana na ule wa Achemenide wa Uajemi kuliko ule katika kazi za kusini mwa Bara Arabuni zinazojulikana kwetu leo hii na ambazo zilitengenezwa baadaye; kuna kufanana kati ya michoro hii na sanamu ya shaba nyeusi ya Marib. Kufanana huko kunajitokeza katika macho, nywelc, masikio, vikoi na kandambili.

Sanamu ya kipindi cha kusini mwa Bara Arabuni pia inawakilishwa na umbo la simba mwenye kichwa cha niwanamke, ingawa mbali ya kipande kidogo kilichopatikana Melazo, nyingine zote zimekwishapatikana tu huko Erythrea. Moja ya sanamu kama hizi iliyohifadhiwa vizuri zaidi inatoka huko Addi Gramaten, kaskazini mashariki ya Kaskase.



13.1 Madhabahu ya ubani ya Addi Galamo

Nywele zake zimesukwa kama ilivyo katika vichwa vya baadhi ya sanamu za udongo za Aksun za kipindi cha baadaye. Aina hii ya sanamu bado huvaliwa na wanawake wa Tigre siku hizi na shingoni mwake kuna mkufu wenye kamba tatu. Mkufu pia hupatikana kwenye miguu ya mbele ya sanamu mbili za aina hii, zenye nyuso zilizo gongwa na mipigo ya nyundo ambazo zinajitokeza kwenye jiwe lililopo Matara. Sanamu nyingine ya aina hii iliyoharibika vibaya imegunduliwa Dibdib, kusini mwa Matara, J. Pirenne anaeleza kuwa sanamu za simba hawa wenye vichwa vya binadamu hazihusiani na sanamu zile zenye mwili wa simba na kichwa cha tai au zile zenye mwili wa mnyama wenye mbawa zilizoko katika jadi ya Wafoeniki na zilizotengenezwa kusini mwa Bara Arabuni katika kipindi cha baadaye. Pengine itatupasa tutufute mifano kutoka Misri au Meroe, ambapo pamekwisha pendekezwa kuwa chimbuko la sanamu ya kichwa chenye nywele zilizosukwa na mkufu iliyopatikana huko kusini mwa Bara Arabuni.

Aina moja ya sanamu zilizochongwa kwenye jiwe, ambayo hupatikana sana sehemu za kaskazini mwa Ethiopia ni ile ya madhabahu yenye ubani. Hizi sanamu ni za aina moja na zile zinazojulikana sana kusini mwa Bara Arabuni. Madhabahu yenyewe yana umbo la pembe mraba sita na mapambo ya Kisanifu ujenzi ambayo inara nyingi husimama kwenye sakafu ya kipiramidi. Kulingana na maoni ya J. Pirenne, mfano mzuri sana kupita ile ya kusini mwa Bara Arabuni ni madhabahu ya Addi Galamo. Lakini madhabahu kadhaa yaliyohifadhiwa kwa namna mbalimbali yamepatikana huko Gobochela mjini Melazo. Mengine kadhaa yamepatikana huko Yeha na vipande vipande vyake vimepatikana huko Matara na katika sehemu ambazo hazijapambanuliwa. Kundi la madhabahu manne lililopatikana Gobochela linawakilisha aina ambayo kabla ya hapo haikujulikana. Kundi hili lina madhabahu ya ubani yenye umbo mviringo yahiyouekwa kwenye sakafu yenye umbo la pia. Mapambo katika madhabahu haya ni yale tu ya alama ya kimungu yenye umbo la mbalanwezi, yenye duara juu yake, iliyotumika kusini mwa Bara Arabuni. Alama hii iliwekwa juu ya mapambo ya picha ya pembe tatu. Kuhusu madhabahu madogo yenye umbo la pembe mraba sita yaliyoko kusini mwa Bara Arabuni tunavyo vitu viwili tu vinavyoelekea kuwa vya kipindii cha kusini mwa Bara Arabuni. Kati yazo cha kwanza ni kile kilichochimbuliwa Matara ambacho ndicho cha kwanza kujulikana nchini Ethiopia kama madhabahu ya kuchomea uturi yaani *mqr*. Cha pili ambacho kilipatika karibu na eneo lililotangulia huko Zala Kesedmai, kinatofautishwa na sanamu za nakshi zilizopambwa pembezoni mwake. Upande munoja una alama ya kimungu ya duara na umbo la mbalanwezi; na upande mwingine una picha ya “mti wa uhai” unaofanana na “mti wa uhai” wa Haoulti. Wale mbuzi-pori kwenye pande mbili zilizobakia wameelekezwa kwenye mti huo.

Kama ilivyo huko kusini mwa Bara Arabuni mbali ya madhabahu haya ya kucliomea ubani tunakuta pia madhabahu ya sadaka ya kumimina. Madhabahu haya yanaweza kutambuliwa kwa kimfereji kinachoruhusu sadaka hiyo ya mvinyo kutiririka wakati inapomwagwa kama sadaka. Huko Yeha kulionekana majukwaa kadhaa yanayofanana na yale ya Hureidha au jimbo la Marib, yakiwa na kimfereji. Kwenye madhabahu mengine kuna maandishi nakshi mazuri kwenye sanamu na mapambo ya picha ya kiambazani kama

ile ya madhabahu ya kuchomea ubani. Aina ya kwanza iliyotajwa, moja katika kikundi cha pili na madhabahu ya kipekee sadaka ya kumimina ya Matara, yote yana jina la kienyeji kwa ajili ya mfululizo wa vitu hivi, lijulikana kama “*mtryn*”. Jina hali halijathibitishwa kuwapo huko kusini mwa Bara Arabuni. Katika eneo la Matara pia kulipatikana meza nene za kutolea sadaka zinazofanana na ile ya kwanza kutoka Yeha. Madhabahu ya sadaka ya kumimina yahiyo Addi Gramaten yanafanana sana na aina ya madhabahu yenye mapambo ya picha ya kiambazani na msingi wa marusu. J, Pirenne anasema kuwa madhabahu ya Fikya, karibu na Kaskase, yenye umbo la bakuli na sanamu zenye maumbo ya wanyama au sima, yaelekea kukumbushia maunibo yaliyokuwa ya kawaida katika sanaa ya Kimeroc.

Machimbo yote ya kiakiolojia yametupatia, mbali ya sanamu hizi, aina ya vyungu ambavyo havijulikani sana. F. Anfray anasema kuwa vyombo vyote vyenye umbo la maua ya mtakawa na magudulia makubwa yenye vishikio na inatutamata yaliyolala yaliyotokea Matara na Yeha ni vya kipindi hiki cha kusini mwa Bara Arabuni. Yeye analingamisha vyombo na vifaa hivi na vile vilivyopatikana Es-Soba, maili chache kutoka kaskazini ya Adeni ambavyo viuaelekea kuwa vya karne ya sita kabla ya enzi za Ukristo.

Nyaraka za uandishi wa maneno ya nakshi ambayo elimu ya machimbo ya vitu vya kale huturuhusu kuhusisha na kipindi cha kale kabisa, zote zi katika hati za kusini mwa Bara Arabuni. Lakini kulingana na maoni ya A.J. Drewes nyaraka hizo zinaweza kugawanywa katika makundi mawili. Kundi la kwanza ni la maandishi nakshi kwenye minara ya kumbukumbu yaliyoandikwa kwa lugha rasmi ya Saba ikiwa na hali chache za pekee mahali hapo. Kundi la pili lina maandishi nakshi yaliyo kwenye miamba, yaliyoandikwa kwa hati zinazoigiza zile katika kundi la kwanza ambazo kwa kweli zina nukuu lugha ya Kisemitiki inayofikiwa kuwa na uhusiano na Kisaba tu. Maandishi hayo hayataji tu isilahi zinazotumika kwa vitu vilhusavyo imani za kidini, kama vile vitu vya kuchomea uturi au meza za kutolea sadaka, kama tulivyoona hapo awali, bali pia yanataja majina mengi ya miungu katika hekalu la miungu wote linalofanana na lile la ufalme wa Saba. Orodha iliyo kamili kuliko zote zinazojulikana leo hii ni ile inayoonekana kwenye jumba moja ambalo lilitumika tena kwenye kanisa la Enda Cerqos huko Melazo. Majina yaliyomo ni kama vile “Astar na Hawbas na Almaqah, na Dat-Himyan na Dat-Ba’dan...”

Jina la Astar linaonekana katika maandishi nakshi mengine inawili, moja kutoka Yeha, na ya pili kutoka mahali pasipojulikana. Jina hilo ni la umbo la Ki-Ethiopia la jina la mungu nyota Athtar, anayehusishwa pia na Almaqah katika matini tatu, moja ya Yeha na mbili za Matara. Huko Matara kuna madhabahu yaliyowekwa wakfu kwa Shron ambayo ni sifa ya mungu huyo anayehusishwa na sayari ya Zuhura.

Mungu mwezi ambaye yaelekea aliheshimika sana nchini Ethiopia na Saba ni Almaqah. Pamoja na maandishi nakshi ya Matara, Yeha na Enda Cerqos, tuliyokwisha yataja, matini za Gobochele huko Mlazo, na pia madhabahu ya huko Addi Galamo, na madhabahu ya sadaka ya kumimina ya huko Yeha; yote yamewekwa wakfu kwa mungu huyu peke yake.

Ibada ya Jua inawakilishwa na jozi la miungu wa kike Dat-Himyan na Dat-Ba’dan,

ambao wanaelekea kulingana na jua la majira ya kiangazi na jua la majira kipupwe.

Wakati ambapo matini zilizowekwa wakfu kwa kawaida hueleza juu ya uhusiano wa watu mashuhuri, zile za Gobochela zinatunyeshwa ya kwamba watu wake waligawanyika katika mbari. Matini nne kutoka eneo hili na moja kutoka Yeha, huwataja watu wa 'Lhy' wa ukoo wa Grb, wa familia ya (au mwana wa) Ygdm 'I Fgmm wa Marib. Mtu huyo anahusiana na kaka yake SBHHMW katika baadhi ya kazi zilizowekwa wakfu kwa ajili yao. Huko Yeha, mtu huyo hutoa sadaka vitu vyake vyote pamoja na mwanaye, Hyrnh kwa 'Astar na Almaqah.' Inawezekana ikiwa kwamba maneno haya YQDM'L na FOQMM ni majina ya makabila. Lakini tuna uhakika kuwa GRB ni jina la kabila. Misemo "ya Marib" na "ya Hadaqan" katika matini mbili za Matara ni toponimia (majina ya mahali) na siyo majina ya makabila. Huenda yanahusu sehemu zilizojengwa kaskazini. Lakini kufuatana na mawazo ya L. Ricci, maneno haya yanaelekea kuonyesha kuwa makundi haya ya watu yalitokea Bara Arabuni.

Utaratibu wa kisiasa huko kaskazini mwa Ethiopia wakati wa kipindi cha kusini mwa Bara Arabuni yaelekea ulikuwa wa ufalme wa kurithiwa. Wafalme wawili wa ufalme huu Rbh na mwanaye Lmm, wanajulikana kwa cheo kimoja cha 'mfalme Sr'n wa kabila la Yg'd *mukarrib* wa D'iamat na wa saba' Wa kwanza kati ya liawa watawala wawili, aliongeza maneno 'kizaliwa kabila la W'rn la Raydan' katika madhabahu ya Addi Galamo. Mtawala wa pili pia anatajwa kwenye madhabahu ambayo asili yake haijulikani yaliyowekwa wakfu kwa 'Anstar'. Huyohuyo Lmm au mtawala mwingine mwenye jina hilo anatajwa katika matini mbili za huko Matara. Katika matini mojawapo anahusishwa mtu fulani ajulikanaye kwa jina Sum'alay, jina linalotumiwa na *mukarrib* wa saba. Wa kwanza kati ya hawa watawala wawili, aliongeza maneno: 'akizaliwa kabila la W'rn la Raydan' katika madhabahu ya Addi Galamo. Mtawala wa pili pia anatajwa kwenye madhabahu ambayo asili yake haijulikani yaliyowekwa wakfu kwa 'Anstar'. Huyohuyo Lmm au mtawala mwingine mwenye jina hilo anatajwa katika matini mbili za huko Matara. Katika matini mojawapo anahusishwa na mtu fulani ajulikanaye kwa jina Sum'alay, jina linalotumiwa na *mukarrib* wa Saba. Kutajwa kwa uhusiano na kabila la Waren wa Raydan kunaonyesha unuhimu ambao wafalme hawa waliwekea ukoo wao wa kusini mwa Bara Arabuni.

Usanifu ujenzi, kazi za sanaa, sayansi ya maandishi ya nakshi na data iliyotokana na matini juu ya imani za kidini na muundo wa kijamii kaskazini mwa Ethiopia-zote hutoa ushahidi juu ya kuwapo kwa athari kubwa ya kusini mwa Bara Arabuni katika karne ya nne na ya tano kabla ya enzi zetu. Kama anavyotukumbusha F. Anfary, utamaduni huu ambao kwa sehemu kubwa ulikuwa wa Kisemitiki uliibuka baada ya karne nyingi ya kujipenyeza kimya kimya. Makundi mdogo ya wahamiaji yalieneza utamaduni wa kusini mwa Bara Arabuni bila shaka kutokana na hali ya kiuchumi na za idadi ya watu ambazo bado hatujazielewa. Yawezekana afikirivyo mwandishi huyu, kwamba wakoloni hawa walianzisha mbinu mpya za kilimo, hasa uatumizi ya plau na kuwa wahjenga vijiji vya kwanza vya mawe huko Ethiopia.

Kujitokeza kwa utamaduni ambao ni dhahiri ulikuwa na ushikamano katika sehemu

yote ya kaskazini mwa nyanda za Ethiopia, lazima kulitokea wakati mmoja na kuibuka na kujidumisha kwa tabaka moja la watu wenye madaraka. Lakini huenda hatutajua ikiwa kikundi hicho kilikuwa na vizalia vya wakoloni wa kusini mwa Bara Arabuni au wenyeji halisi waliokuwa wamezama barabara katika utamaduni huu uliokuwa umeendelea zaidi na hatimaye kuukubali kuwa ni wa kwao.

Kipindi cha Kati

Kuwapo kwa utamaduni wa kienyeji uliopokea athari za kigeni kunajitokeza katika vitu vya kuonekana vya kuanzia kipindi cha pili kabla ya utawala wa Aksum. Kipindi hicho ndicho kinajulikana kama kipindi cha kati.

Bila shaka maumbile fulani yenye asili ya kusini mwa Bara Arabuni yanaendelea kuonekana katika kipindi hiki. Lakini kama alivyokwishadhihirisha F. Anfray athari zilizopo si za moja kwa moja, bali ni maendeleo ya ndani yaliyokuwa kutokana na imichango ya awali. Maandishi nakshi yaliyoandikwa kwa hali mbaya mbaya hutumiwa kunukuu lugha ambayo ulusiano wake na lahaja za kusini mwa Bara Arabuni unazidi kupungua. Wamakarrib hawatajwi tena, lakini matini iliyopatikana Kaskase hutaja habari za mfalme aliyekuwa na jina la kusini mwa Bara Arabuni. Jina lilo ni Waren Hayanat (W'RN HYNT), Kizalia wa Salamat. Ukoo wa GRB ulioheshimika sana huko Gobochea katika Melazo, kwenye kipindi cha kusini mwa Bara Arabuni bado upo, ingawa ulusiano wake na Marrib haupo tena, kwani mmoja kati ya watu wa ukoo huo anatoa wakfu madhabahu ya ubani yenye umbo la pembe mraba sita kwa Almaqah. Sanamu ya ng'ombe dume pia inatolewa wakfu kwa mungu huyu. Huko Addi Gramaten, mkono mwingine umeongezwa kwenye madhabahu ambayo hutolewa wakfu kwa mara ya pili kwa Dat-Himyan na sanamu yenye mwili wa mnyama na kuwa cha mwanaruke hupewa jina Wa hab Wadd. Waraka wa uandishi wa maneno nakshi hukamilishwa kwa maandishi nakshi yaliyoungana ya herufi za kusini mwa Bara Arabuni.

Usanifu ujenzi wa kipindi hiki cha kati haujitokezi sana isipokuwa katika majengo ya kidini yaliyochimbuliwa katika jumba la Melazo. Vitu vyote vilivyogunduliwa na J. Leclant katika jengo moja la pembe mraba lililojengwa kwa niwelekeo wa mashariki na magharibi, huko Gobochea, ama vilikuwa vimetumiwa kwa madhununi inengine au vilikuwa mahali peke pa asili. Jengo hilo lina ukuta wa mita 18.1 kwa 7.3, unaozunguka jukwaa linaloelekea kwenye chumba kidogo chenye mita 8.9 kwa mita 6.75. Chumba hicho kina mlango wa katikati upande wake wa magharibi, na upande wake wa mashariki kuna ubao ambako vitu vilivyowekwa wakfu hutunzwa.

Umbile jingine la kipindi hiki ni mkusanyiko ukubwa wa vitu vilivyoko chini ardhini, kama vile makaburi ya visima ya Yeha na Matara au maslumo ya Sabea na Haoulti. Vifaa vya chuma ambavyo huenda vilianza kutengenezwa katika awamu hii, vinaonekana sana huko Yeha, na vifaa vinavyolusika ni kama pete, mikasi, panga, na sime. Upanga na pete fulani vimepatikana pia huko Matara. Masalia mengi ya vifaa vya chuma pia vimekusanywa kutoka kwenye mahekalu ya Haoulti.

Hata hivyo shaba nyeusi inaonekana zaidi kuliko chuma, pengine kwa sababu haiozi

kwa urahisi. Idadi kubwa ya pete nene zilizo wazi zikiwa na sehemu iliyo na umbo la pembe mraba zimepatikana huko Saba, na kitu kingine cha namna hii kilionekana kimewekwa juu ya ubao kwenye madhabahu mojawapo huko Haoulti. Pete hizi huenda zilivaliwa kama bangili mkononi au mguuni kwa kufata mitindo ya Kimeroe. Lakini huenda vitu hivi vilitumika pia kama fedha. Silaha zinaonyeshwa kwa shoka lenye umbo la mbalamwezi au shoka iliyowekwa pamoja na mkuki kwenye mpini mrefu na sime mbili zilizounganishwa kutoka Haoulti. Vile vile kuna visu viwili kutoka Matara, kimoja kimeunganishwa kwa msumari, na kingine kina mpini wenye umbo la mbalamwezi. Makaburi ya Yena yametoa pia vyungu vya kupikia, vyombo vya kukaangia na kengele ndogo. Mabaki ya vyombo vya kuwekea sadaka vile vile yanepatikana kutoka sehemu ya juu ya kilima huko Haoulti. Sindano na pini zimepatikana Haoulti, Yeha na Matara. Shanga ndogo ndogo shaba nyeusi zimeonekana huko Saba, Haoulti na Yeha.

Kuna aina ya mwisho ya vitu vya shaba nyeusi inayoonyeshwa kuwa vimetoka kusini mwa Bara Arabuni. Hiyo ni vipambe vinavyoitwa "tepe za utambulisho." A. J. Drewes na R. Scheneider wanapambanua aina mbili ya vitu hivi. Aina ya kwanza ina shanga ndogo za marembo kutoka Saba na Haoulti na baadhi kubwa kutoka Yeha. Aina ya pili inayopatikana katika eneo la Yeha tu ni shanga kubwa na nene, zilizounganishwa na kishukio na kutengenezwa katika umbo la innyama; ng'ombe dume, mbuzipori, simba au ndege. Shanga za aina hii zina majina maalum halisi yaliyoandikwa kwa herufi zilizoungana za kusini mwana Bara Arabuni.

Tukizingatia kiwango cha juu cha ufundi unaoonekana katika vitu hivi ni dhahiri kwanba nichango huu ulitokana na wasanii wa madini ya shaba nyeusi wa Ethiopia wa kipindi hiki cha kati. Na anavyopendekeza F. Anfray kazi nyingine kama vile sanamu ndogo ya jozi la kwato za ng'ombe dume zilizoonekana karibu na mahekalu ya Haoulti, na kisanamu cha ng'ombe dume kutoka Malabre Dyogwe hutoa ushahidi zaidi juu ya madhehebu ya Almaqah.

Dhahabu hutunika kwa kutengeneza mapambo kama vile pete za vidole zilizoonekana huko Yeha na Haoulti, hereni, shanga na nyaya zilizokunjwa mviringo, za kule Haoulti. Vipande vingi vya nukufu ya rangi inbalimbali iliyotengenezwa kwa kioo au kigae vinapatikana katika sehemu zote za machimbo ya kipindi hiki.

Vitu vingine vilivyotengenezwa kwa mawe ni pamoja na vinu au viteso vya mviringo au vya pembe mraba vilivyopatikana Yeha, Matara na Haoulti, na muhuri uliopatikana Saba chombo cha marumaru na pete za michoro iliyoindikapindika iliyopatikana Yeha.

Mwisho, machimbo ya Haoulti yalikuwa na hirizi iliyowakilisha kichwa cha Ptah-patec na kichwa cha Hathor. Katika maeneo ya bonde huko Matara kulipatikana hirizi ya akiki yenye kuonyesha Harpokrat. Kati ya vitu vilivyopatikana huko Addi Galano ni vyombo vinne vya kuwekea sadaka vilivyotengenezwa kwa shaba nyeusi, ikiwamo bakuli lililopambwa kwa picha za maua na vyura, na kipande cha chombo kilichopambwa kwa picha za ng'ombe. Vitu hivi vina asili ya Meroe na vinatoa ushahidi wa kuwapo kwa uhusiano kati ya Ethiopia ya kale na bonde la mto Nili. Athari nyingine za Kimeroe huonekana katika vyombo vya udongo vya kipindi hiki.



13.2 *Fahali wa shaba nyeusi wa Mahabere Dyogwere*

Ingawa vitu vingi vilivyopatikana huko Haoulti vinaonyesha kuwa msingi wa uchumi wa kipindi hiki ulikuwa ni kilimo na ufugaji lakini maendeleo ya haraka katika uhunzi wa shaba nyeusi, chuma na dhahabu, na vitu vingi vilivyotengenezwa kwa mawe na kioo, pamoja na vyombo vya mfinyanzi, vyote hivi vinaonyesha ya kwamba tabaka maalum la mafundi lilikwishajitokeza. Inaonekana dhahiri kwamba taratibu zilikuwapo za kuendeleza miji iliyojengwa katika kipindi cha kusini kama vile Melazo, Yeha na Matara, au katika miji iliyojengwa baadaye kama Adulis. Ingawa kumbukumbu ya utamaduni na mila za kusini mwa Bara Arabuni zilikuwa hazijapotea, lakini msisimko mpya yaelekea ulitokea ufalme wa Meroe, ambao ulieneza uhunzi katika Afrika.

Inawezekana kabisa kwamba kudidimia kwa Meroe, kwa upande mmoja, na kufifia kwa nguvu za falme za kusini mwa Bara Arabuni kwa upande mwingine, kuliwawezesha Waethiopia kumiliki biashara zote za dhahabu, ubani; pembe na bidhaa nyingine zilizoagizwa kutoka Bahari ya Hindi.



14

Utawala wa Aksum tangu karne ya Kwanza hadi ya saba

Kwa mujibu wa kumbukumbu za msingi, historia ya ufalme wa Aksum imeanzia karne ya kwanza ya kipindi chetu hiki, karibu miaka elfu moja hivi. Historia hii ni pamoja na uvamizi wa mara mbili dhidi ya kusini mwa Bara Arabuni katika karne ya tatu, ya nne, na ya sita, msafara wa kuingia Meroe kwenye karne ya nne, na kuingia kwa dini ya Kikristo katika kipindi cha nusu ya pili ya karne ya sita.

Wafalme kadhaa, wengi wao wakijulikana kutokana na sarafu zao tu walitawala Aksum, mmoja baada ya mwingine. Mfalme wa awali kabisa aliyetajwa katika kumbukumbu ni Zoscales. Jina hili limetajwa kwenye matimi ya Kiyunani ya mwisho wa karne ya kwanza. Lakini hata hivyo bado kuna mashaka kama jina hilo Zoscales ndiyo lile la 'Za-Hakale', jina ambalo linaonekana kwenye orodha ya watawala wa asili.

Maarifa yetu juu ya ustaarabu huu wa Aksum yanatokana na vyanzo mbalimbali, kwa mfano kutoka kwa waandishi wa mambo ya zama za kale, kama vile Pliny aliyetaja Adulis. Vile vile habari zilipatikana kutoka kwa wasimulizi wa Kiarabu wa mambo ya kale, kama vile Ibn Hischam na Ibn Hawkal. Sehemu kubwa ya ushahidi wetu unatokana na maandishi na vitu vingine vya kale vinavyoendelea kuchimbuliwa. Maandishi nakshi ambayo ni machache, yalianza kukusanywa kuanzia karne ya kumi na tisa. Kugunduliwa kwa maandishi nakshi mengine zaidi yaliyoandikwa na Ezana, Kaleb, na mmojawapo wa watoto wa Kaleb, Waazelia, katika lugha ya Kiyunani, Kige'ez na Kisaba, kumewezesha kupatikana kwa habari za aina mbalimbali. Habari hizo ni nyongeza iliyopatikana katika miaka ishirini iliyopita kutokana na ushahidi wa namna iliyokwishatajwa, pamoja na maandishi kwenye mapango na makala za tabaka za miamba zilizopatikana huko Eritrea. Makala hizo ni za kuanzia karne ya pili, na ni maandiko ya awali kabisa ya kipindi cha utawala wa Aksum.

Eneo

Akiolojia inaonyesha ufalme wa Aksum kama umbile la pembe-mstatili wenye upana wa karibu kilometa 160 na urefu wa kilometa 300. Eneo hilo liko katikati ya nyuzi za latitudo 13 na 17 kaskazini, na nyuzi za longitudo 30 na 40 mashariki. Eneo hili lilienea kuanzia kaskazini mwa Keren mpaka Alagui, iliyopo kusini; na kutoka Adulis iliyoko pwani hadi

kwenye vitongoji vya Takkaze upande wa magharibi. Addi-Dahno ndiyo hasa eneo lililogunduliwa mwisho kabisa katika sehemu hii; na likokaribu kilometa 30 kutoka Aksum.

Kipindi cha Wazaa - Waaksum

Jina la Aksum linaonekana kwa mara ya kwanza kwenye kielelezo cha safari za meli na biashara kitiwacho *Periplus Maris Erythraei* kilichoandikwa na mfanyabiashara mmoja kutoka Misri. Kitabu hicho kiliandikwa mwishoni mwa karne ya kwanza. Mwana-jiografia wa karne ya pili aitwaye Ptolemy, vile vile anataja jina hili la Aksum.

Kitabu cha *Periplus* pia kinaeleza kuwa Adulis ni 'kijiji kikubwa kilichoko umbali wa safari ya siku tatu kutoka Koloe. Mji wa Koloe uko hara na ni soko kuu la pembe za ndovu. Kutoka Koloe hadi kwenye mji wa watu wanaoitwa Waaksum ni safari nyinginc ya siku tano. Pembe zote za ndovu zitokazo bara katika nchi iliyo nyuma ya Mto Nili, lupitia eneo la Cyenum na hatimaye kufikishwa Adulis.' Kwa hiyo kijiji hiki kilimmika kama mlango rukuu wa Aksum, hasa kwa pembe za ndovu. Makala zenyewe zinaeleza kuwa pembe za faru, ng'amba na marumaru nyeusi pia ziliuzwa hapa. Vitu hivi ni baadhi tu ya bidhaa zilizosafirishwa kwenda nchi za nje kutoka Adulis vilivyotajwa na Pliny kabla ya *Periplus*. Hapa jina la 'Adulis' linatajwa kabla ya lile la Aksum. Kwa mujibu wa Pliny, Adulis ilikuwa katika nchi ya Watroglodaiti. Waruni na Wayunani walijua habari za kuwepo kwa Waaksum na 'miji' yao katika mrima wa Adulis tangu karne ya kwanza.

Akiolojia inatupatia habari chache sana kuhusu utamaduni wa kuonekana wa karne za awali za kipindi hicho. Maandishi machache ya karne ya pili na ya tatu ndiyo ushahidi pekee unaoweza kukisiwa tarehe yake. Maandishi hayo yanaelezea maumbo ya zamani sana ya alfabeti za Kihabeshi. Matumzi ya alfabeti hizo yameweza kudumu hadi leo hii. Hata hivyo maandishi hayo si ya zamani sana kati ya yote yaliyopatikana kwenye eneo la Waaksum. Kuna maandishi mengine mengi ya kusini mwa Bara Arabuni ambayo ni ya nusu ya pili ya elfia ya mwisho kabla ya enzi zetu. Hati za maandishi ya kusini mwa Bara Arabuni ulikuwa ndio mfano uliofuatwa na Waethiopia. Maumbo ya herufi yalibadilika sana katika karne ya pili ya enzi zetu yakitengana kabisa na hati za kusini mwa Bara Arabuni. Kwa mujibu wa 'Periplus' Adulis na Aksum, ni miji iliyokuwa mwanzo na mwisho wa njia iliyotumika hapo kale na ndiyo mji muhimu kuliko yote katika maeneo haya. Hii pia ndiyo mji ambayo majina yake ya kale yaliyotokeza katika matini na maandishi nakshi yanichifadhiwa hadi leo. Adulis ni mji ambao umehamwa kabisa na watu lakini wale wote waishio kwenye vijiji vya karibu bado wanayaita magofu ya mji huu Azuli. Maeneo mengine yote, au tuseme, karibu maeneo yote yaliyobaki yana majina ambayo kwa hakika hayafanani na yale ya enzi za Waaksum.

Aksum

Kwa mujibu wa matini ya kipindi cha Mani, Aksum ulikuwa maarufu sana katika karne ya tatu ya enzi za Ukristo. Matini hii hueleza kwamba Ufalme huu ulikuwa 'wa tatu duniani'

Na ni kweli katika mji huu kuna majumba makubwa na mabaki ya vitu yanayotoa ushahidi wa kipindi muhimu mno cha kihistoria.

Mwanzoni mwa karne hii ujumbe wa Kijerumani ulichora na kupiga picha majengo yote yaliyoweza kuonekana. Upande wa magharibi wa miji waligundua magofu matatu yenye utanzu wa usanifu majenzi. Magofu hayo yametambuliwa kikweli kuwa ni mabaki ya jumba la Kifalme. Utafiti uliofuata, hususa ule wa Taasisi ya Akiolojia, umedhihirisha majengo mengine na habari nyingine nyingi kuhusu mji wa kale wa kifalme.

Katika majumba matatu yanayojulikana kama 'Enda-Semon,' 'Enda-Mikael,' na Taakha-Maryam' yamebakiwa tu na sehemu zake za chini; lakini leo hii yanaweza kuonekana tu katika michoro na picha za ujumbe wa Kijerumani.

Magofu ya jumba jingine la fahari yako chini ya kanisa la Mryam-Tsion ambalo kwa upande wake wa mashariki, chini ya usawa wa ngoro, kuna mabaki ya sehemu ya chini ya nyumba yenye upana wa kati ya mita 30 na 42.

Kwa upande wa magharibi ya mji Taasisi ya Akiolojia ya Ethiopia mnamo mwaka 1966 hadi 1968 iligundua na kufanyia uchunguzi majengo mengine yaliyojengwa kwa ufundi mkubwa wa usanifu majenzi. Magofu ya majengo haya yaliyoko huko Dongour, kaskazini nwa barabara ya Gondar, ni ya ngone nyingine ya karne ya saba hivi.

Makundi nuanne ya majumba ambayo hayalingani yenye vyumba arobaini hivi pia yamejipanga kwa namna ambayo yameunda pembe mraba kuzunguka eneo kuu la ngoine hiyo. Taniuu tatu zilizotengenezwa kwa matofali ya kuchoma zilingunduliwa katika sehemu ya magharibi ya eneo hili. Katika chumba kimoja kwenye jengo lililoko upande wa nje kuelekea kusini mahali palipojengwa kwa matofali ambalo kutokana na alama ya ndimi za moto yaelekea palikuwa jiko la kupashia moto chumba.

Eneo hili la Dongour ndio mfano mzuri mno wa utaalumu wa usanifu majenzi wa ustaarabu wa Aksum unaoweza kuonekana leo hii. Huenda hapo waliishi watu mashuhuri wa nchi hiyo.

Jumba jingine la kuvutia ambalo kwa masimulizi ya wenyeji hulihusisha na Kaleb na mwanac Guebra-Masqal, wakati mmoja lilikuwa limesimama kwenye kilima, kaskazini-mashariki mwa Aksum. Jozi la majengo ambayo huenda ni kanisa, ilijengwa juu ya vyumba vya chini vyenye makaburi kadhaa yaliyojengwa na kufunikwa kwa mabamba ya mawe.

Huko Bazen, kwa upande wa mashariki wa mji, baadhi ya makaburi yenye umbo la tanuu yamechimbwa kwenye kilima cha miamba. Baadhi ya makaburi hayo yana shimo na vijumba vidogo kila upande kwa chini. Sehemu hiyo hiyo ina makaburi kadhaa na ngazi zipatazo kumi na saba ambazo zimechimbwa kwenye mwamba na kupitwa na mawe ya kaburi ambayo hapo kale hayakuwa yakisimama pake yake.

Mji wa kale ulienea kwenye eneo kati ya jiwe kubwa la kaburi na sehemu ya Dongour; ua magofu yameenea kila mahali chini ya ardhi. Wakati uchimbuaji zaidi utakapofanyika katika maeneo ya Addi-Kilte na Tchaanadong habari nyingi sana za kale Aksum zitaweza kupatikana.

Adulis

Kuna mabaki machache katika eneo hili ambalo liko yapata kilometa 4 kutoka pwani kuelekea bara. Kutokana na ushahidi uliopo juu ardhini, mabaki hayo yako katika eneo lenye urefu wa karibu meta 500 na upana wa karibu meta 400. Kunako mwaka 1868 msafara wa kikundi toka Uingereza uliofikia hapo karibu ulichimba baadhi ya mabaki ya majumba. Lakini tokea kazi ya uchimbaji ianze huko hakuna kitu kikubwa kilichobakia zaidi ya kuta zilizofukuliwa na ujumbe wa pembeni mwaka 1906 na kuta nyingine zilizogunduliwa na wataalamu wa Taasisi ya Akiolojia Ethiopia mnamo mwaka 1961-2.

Mwanzoni mwa 1906, Mswidi mmoja kwa jina Sundstrom aligundua jengo kubwa upande wa kaskazini, na muda mfupi baadaye, Periberu aligundua magofu mawili inadogo kwa upande wa mashariki na magharibi. Magofu yote haya yana vyumba vya chini, vyenye safu na ngazi nyingi. Vyumba hivyo vina maumbo mstatili na vimezungukwa na majengo mengine pambeni. Sundstrom aliita jumba moja alilogundua "jumba la kifalme".

Chumba cha chini kilichogunduliwa upande wa magharibi mwa jengo hili na Peribeni unaonyesha maumbile ya namna moja ya usanifu majenzi. Chumba hicho kina urefu wa meta 18½. Sehemu yake ya juu imefunikwa na sakafu ya mawe. Sakafu hii ilikuwa na mabaki ya nguzo za sehemu ya kanisa. Mwishoni mwa upande wa mashariki chumba cha nusu mviringo kilichokuwa katikati ya vyumba viwili vilionyesha dhahiri kwamba magofu hayo yalikuwa ya chumba maalum cha mikutano ya kanisa.

Upande wa mashariki ya eneo lililogunduliwa na Sundstrom, Peribeni aligundua chumba cha chini cha kanisa jingine. Ndani ya chumba hicho mlikuwamo vitu viwili vya kuvutia: tangi la maji ya ubatizo kwa upande wa kusini mwa kile chumba kidogo na katikati mwa jengo kulikuwa na mabaki ya nguzo nane zilizojiipanga katika umbo la pembenane. Muundo wa pembe mraba na muundo wa mstatili umetumiwa kwa pamoja katika jumba hili moja.

Upande wa nyanda za Eritrea, kama kilometa 135 kusini mwa Asmara, karibu na Senafe, kuna eneo moja la zamani sana la kiakiolojia nchini Ethiopia. Tabaka za chini kabisa ni sehemu ya jengo kubwa la kipindi cha kusini mwa Bara Arabuni.

Taasisi ya Akiolojia ilifanya uchumbuaji wa kutafuta mambo ya kale katika eneo la Matara, kati ya mwaka 1959 na mwaka 1970. Machimbo hayo yamiegundua majumba manne makubwa, makanisa matatu ya Kikristo, na sehemu ya kawaida ya kuishi yenye nyumba zipatazo thelathini. Majumba hayo manne makubwa ni ya aina inayojulikana yakuwa na ukumbi nkuu uliojengwa juu ya chuma kilichopo chini, na kuzungukwa na nyumba kadhaa pembeni. Kama ilivyo kila mahali, nguzo za mawe zilizo chini ya vyumba vya jumba kuu zilitunika kama msingi wa nguzo za kushikilia sebule.

Nyumba za kawaida zina vyumba viwili au vitatu. Unene wa kuta za nyumba ni kiasi cha sentimeta 70 hivi. Mabaki ya sehemu za kuotea moto, tanuu za kuchoma matofali na vyombo vingi vimctuwezsha kujua kuwa sehemu hiyo ilikuwa ni sehemu ya kuishi. Kuna aina nyingine ya nyumba yenye ukubwa wa kati iliyopo katikati ya majumba makubwa na nyumba za kawaida.

Upande wa kusini na mashariki mwa mji kulikuwa na majengo ya kidini ambayo kwa

nje yanaonekana kufanana na majengo mengine. Yalikuwa na jengo la kati lililozungukwa na nyua na nyumba za pembeni. Nanna ya ujenzi ni ile ile.

Kohaito

Katika eneo hili linaloonekana kaskazini mwa Matara, katika urefu wa meta 2,600 kwenda juu kuna magofu mengi ya majengo yenye umuhimu kwa taalauma ya usanifu majenzi. Kuna vilima kama kumi hivi vilivyotapakaa kwenye eneo kubwa lenye mabaki ya majengo makubwa ya wakati wa mwisho wa kipindi cha Aksum. Na upo uwezekano wa masalia ya majengo haya kuwa ya zamani zaidi. Zipo nguzo kadhaa ambazo bado zimesimama kwenye vilima hivyo. Inafikiwa ya kuwa mengi ya mabaki haya yalikuwa ya makanisa yaliyokuwa na ukubwa uliolingana na ukubwa wa makanisa ya Matara. Kuta zote kwenye vilima zinaonyesha maumbile ya ufundi uashi wa Aksum, na yamewekwa katika maumbo ya mstatili kama yale yanayoonekana katika maeneo mengine ya kipindi hiki. Pamoja na majengo yaliyoharibika, kaskazini ya kaskazini-mashariki kulikuwa na bwawa la maji lililojengwa vizuri kwa mpande ya mawe. Kazi ya bwawa hilo ilikuwa ni kukinga maji kutoka upande wa kusini mashariki ya bonde asili liljulikanalo kwa jina la 'Bonde la Safra'.

Kwa upande wa mashariki kuna kaburi la mawe lenye vyumba viwili vya kuzikia. Upo msalaba wa aina ya Kiaksum uliochongwa kwenye mwamba. Msalaba huo unaremba upande mmoja wa kaburi. Kwenye intaro karibu na eneo hili lipo jiwe lililochorwa na kuchongwa picha za ng'ombe, ngamia na wanyama wengine.

Miji na Masoko

Makazi makubwa yaliunda jumuiia zilizojaa watu na nyumba zilizojengwa karibu karibu kuzungukia majumba makubwa, yaliyojengwa kwa ajili ya kazi mbalimbali. Machimbo ya huko Aksum, Adulis na Matara yameonyesha kwamba sehemu hizi zilikuwa kamili. Kwenye makazi ya mji wa Matara yaliyokaliwa na watu wa kawaida kuna kichochooro kidogo kinachopindapinda kati ya nyumba. Yote hayo yanaonyesha kuwepo kwa idadi kubwa ya watu ambao hawukuwa wakiishi kwa kutegemea kilimo tu. Kuwepo kwa sarafu kunadhihirisha maendeleo makubwa ya uchumi wa jamii.

Ushahidi zaidi unajitokeza kwenye aina mbalimbali ya vitu vilivyochimbuliwa, kama vile vyombo vilivyotengenezwa kwa kioo na mabirika ya Kimediterani. Kazi za sanaa (kama vile taa za shaba nyeusi na vitu vingine kadhaa vilivyotengenezwa kwa dhahabu) vinathibitisha ya kwamba mambo ya anasa yalikuwepo pia.

Usanifu majenzi wa Aksum: maumbile yake kwa jumla

Sifa kuu za usanifu majenzi wa Aksum ni matumizi ya mawe, maumbo ya pembe mraba au mstatili, minara midogo midogo inayojitokeza sehemu ya juu ya majengo, misingi yenye ngazi na majengo makubwa kujengwa juu yake. Vilevile kuna uashi utumiaio ufundi wa kujenga kwa mawe kwa kutumia udongo wa mfinyanzi. Aidha kuna ukweli uonyeshao kwamba maumbile haya maalum hujitokeza karibu kila mahali. Yote yamesimama kwenye

masingi yenye safu kufikiwa kwa ngazi za minara. Ngazi hizi kwa kawaida huwa na vidato saba. Majengo yote haya makubwa huzungukwa na majengo ya pembeni yaliyotengwa na nyua ndogo ndogo.

Ni jambo lenye uhakika kwamba ngome na majumba makubwa yalikuwa na walau ghorofa moja juu. Kutokana na kimo chake chumba hiki cha kwanza tunaweza kukiita ni ghorofa ya kwanza. Kutokana na udogo wa nyumba katika maghorofa haya na kutokana na ukweli na nguzo kuna, uwezekano kuwa sehemu ya kuishi ilikuwa ile ya juu. Bado hajajafahamika kama ngome za Aksum zilikuwa na ghorofa za juu au la.

Waaksum walitumia pia mbao katika ujenzi wao. Fremu za milango na madirisha na sehemu fulani za kuta, hasa kwenye kona za vyumba, zilikuwa ni za mbao. Fremu nyingine zilipitishwa kwenye sakafu ya mawe kuimarisha zaidi sakafu hiyo. Boriti zilizoshikilia sakafu za vyumba vya ghorofa za juu nazo pia zilikuwa za mbao.

Pia ilikuwa tabia ya Waaksum kufanya vyumba vya chini vya majumba makubwa kuwa migumu na imara zaidi kwa kuweka au kulaza mapande makubwa ya mawe yaliyokatwa vizuri katika kona au juu kwa safu. Mawe mengi ya aina hii yanaonekana katika majengo ya wakati wa mwisho wa kipindi cha Waaksum. Baadhi ya mapande hayo ya mawe yalionekana kiroa yalikuwa yametumika katika ujenzi wa majengo ya awali.

Nguzo za mawe

Nguzo za mawe za Aksum ni za aina kadhaa. Nguzo hizo zimetawanyika kila mahali na bila shaka hapo zamani zilitumika kama alama za makaburi. Baadhi yazo zilikuwa na urefu wa meta 20. Nguzo za aina hii zinapatikana kwenye maeneo mengi, ingawa nyingi zaidi zinapatikana karibu na lile kundi la maguzo makubwa. Kuna nguzo saba katika kundi hili. Nguzo hizi zinavutia kutokana na mapambo ya kuchongwa. Moja kati yazo bado imesimama. Tano zimeanguka na kuvunjika. Guzo la saba lilichukuliwa na kupelekwa Roma ambako mnamo mwaka 1937 lilisimamishwa karibu na Ukumbi wa Caracalla ambako bado linaonekana limesimama.

Michongo huigiza majengo yaliyokuwa na ghorofa nyingi. Nguzo ndefu kuliko zote iliyokuwa na urefu wa karibu meta 33 inaonyesha ghorofa tisa zilizopangwa moja juu ya nyingine katika upande wake mmoja. Michongo hii inaonyesha jengo zuri la ghorofa lenye mlango na madirisha, na boriti. Jengo hili limechorwa kwenye jiwe gumu. Maana halisi ya usanifu najenzi luu wa kidhahania bado haijulikani. Kwa hakika jengo hili haliwezi kulinganishwa na jengo jingine lolote lile. Kwenye mojawapo ya mawe haya kumechongwa namna ya mkuki katika sehemu ya mbele ya nyumba. Nguzo nyingine ambayo haionyeshi mambo yoyote ya ufundi majenzi, inaonyesha namna fulani ya ngao.

Huko Matara na Anza, katika uwanda wa mashariki, kuna nguzo mbili zenye urefu wa meta 5 hivi na ni miviringo juu. Nguzo hizo zina sifa mbili bainifu: alama ya mbalamwezi ambayo ni alama ya diini ya kusini mwa Bara Arabuni na maandishi nakshi ya Kigèez. Maandishi kama haya kwa kawaida yana maana ya kumbukumbu fulani. Jambo hili linethibitishwa huko Matara. Vipengee vya maandishi ya kale vinaonyesha kuwa maandishi hayo ni ya karne ya tatu au mwanzoni mwa karne ya nne. Ufundi unaojitokeza

kwenye nguzo hizi ni sawa na ule wa nguzo za mawe laini za huko Aksum.

Viti vya enzi vimekuwa vikionekana kwa wingi sana katika utamaduni wa Aksum. Viti hivyo vinatajwa katika maandishi nakshi mawili ya Ezana. Katika karne ya sita Cosmas aligundua ya kwamba kulikuwa na kiti cha enzi karibu na jiwe la kaburi huko Adulis. 'Kiti hicho cha enzi kina msingi wa pembe mraba'. 'Kimetengenezwa kwa marumaru nyeupe na safi sana' na 'kimekatwa kutoka kwenye pande moja kubwa la jiwe.' Hicho kiti pamoja na jiwe la kaburi 'vimejaa herufi za Kiyunani.' Maandishi yaliyokuwa kwenye kiti cha enzi yalitungwa na mtawala wa Aksum aliyetawala wakati wa karne ya tatu hivi. Umuhimu wa vitu hivi vya kumbukumbu haujaeleweka bado. Je, ni viti vya enzi kwa ajili ya kumbukumbu za ushindi katika vita? Au viti hivyo vilikuwa alama ya kuonyesha ya kwamba ahadi fulani zilizotolewa kwa mungu zimetimizwa? Au viti hivyo vilikuwa alama ya uwezo fulani au mamlaka ya utawala? Vitu hivyo vimekuwa bado ni fumbo kubwa kama yalivyo yale maguzo makubwa.

Kundi lililopo karibu na Maryam-Tsion limepangwa kwa namna ambayo viti vyote vya enzi vinatazama upande wa mashariki ambao ni upande uliotazama zile nguzo zilizochorwa. Kama mpango huu wa vitu ni wa asili, basi inawezekana ya kuwa vilielekezwa kwenye hekalu anubalo huenda lilikuwako wakati huo mahali anubapo kuna kanisa leo hii. Eneo hilo lina magofu mengi sana.

Maandishi nakshi yenyewe yameandikwa kwa kuchongwa juu ya jiwe gumu. Matini majawapo ya Ezana iliyoandikwa kwa hati za aina tatu tofauti: Kiethiopia, Kiarabu cha kusini mwa Bara Arabuni na Kiyunani, imechongwa pande zote mbili za jiwe kwenye urefu wa zaidi ya meta mbili.

Kupendelea kutengeneza minara hii mikubwa ya mawe kumcejitokeza pia hata katika utengenezaji wa sanamu. Mwanzoni mwa karne jiwe bapa liligunduliwa huko Aksum. Na jiwe hilo lilionyesha sanamu za nyayo zilizokatwa humo zenye urefu wa sentimeta 92. Jiwe hilo lilitumika kama msingi wa sanamu, ambayo huenda ilikuwa ya chuma. Ezana, katika maandishi yake, anasema kuwa alitengeneza na kusimamisha sanamu kwa heshima ya utakatifu wake Mungu. Mojawapo ya matini hizo husema. "Kwa shukrani zake Mungu aliyetuumba, Arca Asiyeshindwa, tumeweka sanamu luizi, moja ya dhahabu, na nyingine ya fedha, na tatu za shaba nyeusi, kwa heshima yake."

Hakuna hata sanamu moja ya Kiaksum iliyogunduliwa mpaka sasa, lakini uchunguzi wa kiakiolojia bado haujakamilika. Michoro michache ya wanyama iliyoko kwenye inawe au chuma imegunduliwa. Cosmas anatuambia kuwa 'aliona sanamu nne za shaba nyeusi' za wanyama wanaofanana na farasi (yawezekana ni vifaru) katika jumba la kifalme.

Ufinyanzi

Kwenye maeneo ya Aksum kumepatikana vyombo vingi vilivyofinyangwa, vingine vikiwa vimevunjika na vingine vikiwa bado vizima. Vyombo hivi vilivyofinyangwa vilikuwa vya kulia chakula. Kulikuwapo na vyombo vyekundu na vingine nyeusi lakini vingi vilikuwa vyekundu. Schemu ya nje ya baadhi kubwa ya vyungu imepakwa rangi iliyofifia ya

dhahabu. Baadhi yao vimepakwa mstari mwekundu uliochorwa. Hakuna ushahidi wa kuonyesha kuwa gurudumu la ufinyanzi lilitumika.

Vyombo vyenyewe vinatofautiana kwa ukubwa na vingi vimerembwa. Vinaporembwa basi marembo hayo kwa kawaida huwa ni michoro ya kijiometri iliyochongwa kwenye chombo chenye au kupakwa, kufinyangwa au kupigwa chapa. Ni mara chache sana michoro hutokana na maumbile ya vitu. Mara chache hutokea masuke machache ya mahindi, na ndege na nyoka waliofinyangwa. Msalaba wa Kikristo unaonekana inara nyingi kwenye kingo, na kwenye sehemu za nje au za chini za vyombo.

Ipo tofauti kati ya vyombo vilivyofinyangwa kutoka mashariki ya uwanda na vile vya kutoka magharibi. Kwenye eneo la Aksum tunapata chombo chenye mikato ya mistari katika pande zake, lakini mchoro au mtindo huu hauonekani sana upande wa mashariki ya uwanda. Kuna bakuli kutoka Matara, lenye pambo la vinundu chini ya kingo zake, lakini hakujapata kuonekana chombo cha mfano wake upande wa Aksum. Lakini hapo Aksum tunapata birika lenye mdomo wenye umbo la kichwa cha nutu. Birika la namna hii halijawahi kuonekana mahali pengine popote.

Habari zilizopatikana kutokana na utafiti unaoendelea zinatuwezesha kutenganisha makundi mbalimbali ya vyombo hizi vya ufinyanzi, kufuata mfululizo wa kikronolojia. Lakini uchimbaji zaidi unahitajika kufanywa ndipo tuweze kupata tarehe sahihi ya matukio haya.

Vyombo vya ufinyanzi vilivyotoka nchi za nje, hasa yakiwamo magudulia yenye vishikio na mapambo ya vinundu kwenye pande zake vinapatikana pia katika tabaka la Aksum kwenye inaeneo yote yaliyochimbwa Magudulia haya, ambayo yanaonekana kwa wingi huko Adulis, yana asili ya Mediterani. Magudulia haya hayapatikani kabisa kwenye matabaka yaliyolitangulia lile la Aksum. Kwenye tabaka la Aksum kunapatikana mabaki mengi ya chupa ndogo za glasi, vikombe vingine vya glasi ya rangi ya buluu. Vyombo hivi vyote ni vya kutoka mwishoni mwa kipindi cha Aksum, na ambavyo vingi vilitoka Bahari ya Hindi. Vipo vikombe vidogo vinavyoonekana kama vimetengenezwa kwa udongo mweupe wa ufinyanzi na huenda viliingia kutoka Misri.

Vitu vichache maalum

Utafiti wa kiakiolojia umesababisha kugunduliwa kwa vitu kama vile mihuri iliyotengenezwa kwa mawe ya udongo mwekundu na kuchorwa michoro ya kijiometri au sura za wanyama; zana ndogondogo za chuma, dadu za udongo mwekundu, vipande vya nyembe, picha za wanyama, sanamu za wanawake zilizoshabihiana na sanamu za kizazi za wakati wa kale, na kadhalika. Vitu vya kuvutia hasa ni taa ya shaba nyeusi na kasha la kuwekea fedha vilivyochumbuliwa huko Matara.

Kitu cha kwanza kina bakuli la mstatili lililokaa juu ya kishina kinachofanana na sanamu ya kuchongwa ya miti ya mitende. Sehemu ya juu ya bakuli hilo kuna kifundo mfano wa mbwa aliyevaa kola fulani shingoni akiwa katika harakati ya kukamata mbuzi-pori. Nyuma ya bakuli pameumbwa sanamu ndogo. Urefu wa taa hiyo ni sentimeta 41.

14.1 *Shingo ya chupa*



14.2 *Tawa ya manukato, mitindo wa Aleksanda*

Bakuli lina urefu wa sentimeta 31. Kutokana na infano wake ambao yaelekea ni nakshi ya kiibada, taa hii huenda ilitoka kusini mwa Bara Arabuni ambako vitu vya namna hii vimegunduliwa.

Hazina hii ihpatikana kwenye chombo cha shaba nyeusi chenye urefu wa sentimeta 18. Ndani yake mlikuwa na misalaba miwili, minyororo mitatu, bangili sitini na nane, shanga za mikufu sitini na nne, sarafu kumi na nne za wafalme wa Roina wa karne ya pili na ya tatu (hasa Waantoni). Vitu vyote hivi ni vya dhahabu, na vimehifadhika vyema. Kwa kutazama mahali ambapo vitu hivyo vilipatikana, mi lazima vilikusanywa pamoja mnamo karne ya saba.

Wakati mwingine matabaka ya Aksum hutoa maandishi nakshi, na vipande vya viteso vya manukato vya kusini mwa Bara Arabuni vya karne ya tano kabla ya enzi zetu. Kwa kawaida mawe huwa yamevunjika na kwamba yalitumika tena na wajenzi wa Aksum. Matabaka haya ya Aksum pia hutoa vitu vichache vilivyoagizwa au kuingizwa kutoka Misri au Unubi. Na kama ilivyoonekana pia huko Haoulti, sanamu za udongo mwekundu ambazo, kulingana na mawazo ya Henri de Contenson, mgunduzi wa eneo hili 'yaelekea kuhusiana na vile alivyoviona huko India katika nyukati za utawala wa Mathura na Gupt.a' Vile vile anaonyesha kuhusiana na oni lilo juu kwamha karne mbili za kwanza na enzi zetu zilikuwa na ufanisi kwa wafanyabiashara waliokuwa na uhusiano na watu wa India na Mediterani, kupitia Bahari ya Sham.

Utaalamu wa Sarafu

Sarafu za Aksum zina umuhimu wake mahsus. Ni kwa kutuniia sarafu hizo peke yake ndipo tulipoweza kujua majina ya wafalme kumi na nane wa Aksum.

Maelfu kadhaa ya sarafu yamegunduliwa. Maeneo yaliyoliimwa kuzunguka Aksum yametoa sarafu nyingi sana, hasa wakati mvua nyingi zinapoosha udongo wote na kubakiza sarafu ambazo huonckana kwa urahisi. Sarafu nyingi ni za shaba nyeusi, na zinatofautiana kwa ukubwa kati ya milimeta 8 na milimeta 22. Sarafu hizi zina alama kadhaa. Zile sarafu za wafalme wa awali (Endybis, Aphilas, Ousana I, Wazeba, Ezana) zote zina picha ya duara na umbo la mbalamwezi. Sarafu zote zilizotengenezwa baada ya mfalme Ezana kuingia katika dini ya Kikristo zinaonyesha msalaba ukiwa katikati kwenye upande mmoja wa sarafu au imongoni mwa herufi za ngano zilizonakishiwa kwenye kingo za sarafu. Katika sarafu zingine picha ya mfalme imezungukwa na masuke ya mahindi yaliyokunjwa. Au wakati mwingine suke moja tu lililonyooka ndilo luwekwa katikati ya uso wa sarafu. Masuke haya ya mahindi yamo kwenye sarafu za mfalme Aphilas na Ezana. Huenda masuke haya ya mahindi yalikuwa nembo ya uwezo wa kuhakikisha kuwa ardhi ina rutuba tele.

Uandishi ulifanywa kwa hati za Kiyunani au za Kiethiopia. Hati za kusini mwa Bara Arabuni hazikutumika kabisa. Kiyunani kimeonekana kwenye sarafu za awali kabisa. Kiethiopia kilianza kuonckana kwenye sarafu za kuanzia wakati wa utawala wa mfalme Wazeba.

Maneno yaliyotumika kwenye maclezo hutofautiana Baadhi yake ni kama vile 'Kwa

Utukufu wake Mungu, 'Afyā na amani kwa watu wote,' 'Amani kwa watu wote,' 'Atashinda kwa njia ya Kristo,' 'Mfalme wa Waaksum', au 'Mfalme wa Aksum.'

Hati na lugha

Alfabeti za awali kabisa zilizotumika nchini Ethiopia, tangu karne ya tano kabla ya enzi zetu, zilikuwa za kusini mwa Bara Arabuni. Alfabeti hii imetumika kunukuu lugha inayofanana na lahaja za Kisemitiki za kusini mwa Bara Arabuni.

Mifano ya mwanzo ya hati za Kiethiopia ni ya kuanzia karne ya pili ya enzi zetu. Hati hizo zina maumbo ya konsonanti. Herufi zake bado zinakumbusha asili yao ya kusini mwa Bara Arabuni. Lakini polepole maandishi hayo yalibadilika na kupata maumbo yake maalumu. Mwelekeo wa maandishi ambo hapo awali ulitofutiana, ulikuwa mmoja, na baadaye ukawa wa kutoka kushoto kwenda kulia. Maandishi yaliyochongwa kwenye kipande cha chuma cha kuanzia karne ya tatu yamegunduliwa. Maandishi hayo yanamtaja Mfalme Gadara, na ndiyo maandishi nakshi ya kwanza ya Kiethiopia yenye jina la Aksum. Maandishi mengine yalikuwa yameandikwa kwenye mawe. Maandishi nakshi muhimu za mfalme Ezana ni za karne ya nne. Ni katika maandishi haya ndipo matumizi ya kwanza ya silabi yanajitokeza na baadaye kidogo yakawa ni kanuni mojawapo ya mwandiko wa Kiethiopia. Alama za irabu ziliunganishwa na mfumo wa konsonanti, na hivyo kukatoka lafudhi tofauti ya lugha ya mazungumzo.

Lugha hii, kama ilivyoonyeshwa katika maandishi nakshi inaitwa Kigeez. Ni mojawapo ya lugha za kisemitiki za kundi la kusini. Hii ndiyo lugha ya Waaksum. Katika karne ya tano Biblia ilitafsiriwa katika Kigeez.

Kuanzishwa kwa ustaarabu wa Aksum

Karne tano kabla ya enzi za Kikristo, muundo maalum wa ustaarabu uliojaa athari za kusini mwa Bara Arabuni ulianzishwa kaskazini mwa uwanda wa Ethiopia. Sehemu kubwa ya ustaarabu huo ulikuwa ni wa kilimo, na ulistawi sana katika karne ya nne na ya tano kabla ya enzi zetu. Baadaye katika karne zilizofuata, ustaarabu huo ukaanza kiufikia. Twafikia oni hili kutokana na ukosefu wa nyaraka za kiakiolojia. Lakini utamaduni huo haukufa kabisa. Baadhi ya maumbile yake yalilifadhiwa kwenye ustaarabu wa Aksum. Yafaa ikumbukwe pia ya kwamba majengo mengi ya Aksum yanesimama kwenye eneo lile lile yalipokuwa majengo ya zamani ya kipindi Aksum. Hii huonyesha kwamba mambo yaliendelea kudumu.

Hata hivyo, ugunduzi wa kiakiolojia wa kuanzia karne za mwanzo za enzi za Ukristo unadhihirisha vitu vingi ambayo ni vipya. Ingawa mwandiko uliotumika kwenye maandishi ulitokana na maandishi ya kusini mwa bara Arabuni, lakini kuna mabadiliko ya kutosha ambayo yanaonekana. Dini pia ilibadilika. Majina yote ya niungu wa kale yametoweka, isipokuwa jina la Astar.

Kama inavyoonekana kwenye maandishi ya mfalme Ezana, majina ya wafalme watatu: Mahrem, Beher na Meder, yameshika nafasi ya majina yale yaliyotoweka. Kwa upande wa

usanifu majenzi, ingawa matumizi ya mawe na mbao, na misingi yenye ngazi nyingi katika majengo bado yanaendelea, namna mpya ya ujenzi hujitokeza vizuri sana. Vyombo vya ufinyanzi vinaonyesha fundi mpya kabisa, kama vile katika maumbo ya urembeshaji. Mbinu mpya za kutoka nchi za nje, za uokaji wa vyombo vya ufinyanzi pia zinaonekana. Vyombo vya kioo vinaonekana katika maeneo yote ya uchimbaji. Jina la Aksum linatoka (kwa mara ya kwanza katika kumbukumbu za historia za kipindi hiki). Na huenda ni muhimu kwamba eneo hili la Aksum yaelekea halikuwa na historia ndefu kabla ya karne ya kwanza.

Vipengee vya kiuchumi

Katika kipindi cha Aksum, kama ilivyoonekana katika karne zilizopita, kilimo na ufugaji vilikuwa ndiyo msingi wa uchumi. Lakini wakati wa kipindi cha Aksum, hali hii iliendelea kawa namna ya kipekee kabisa, kwa sababu mbili maalum.

Vyanzo vyote vya kale vinaonyeshesha ya kwamba shughuli za biashara kwa njia ya baharini kwa Bahari ya Sham ziliongezeka katika kipindi cha karne mbili za kwanza. Hali hii ilitokana na kupanuka kwa ufalme wa Warumi katika eneo hili. Upanuzi huu ulisaidiwa na maendeleo ya safari za baharini. Tunajua ya kwanza mbinu za kusafiria baharini ziliendelea kupanuka mwanzoni kwa karne ya kwanza. Nahodha Hippalus alionyesha jinsi mabaharia walivyoweza kutumia upepo kwa manufaa makubwa ya usafiri, hivyo basi mbinu hiyo iliongeza wasafiri wengi baharini. Strabo ameonyesha kwamba, 'kila mwaka, katika nyakati za Agosto, meli mia moja na ishirini zilianza safari kutoka bandari ya Myos Hormos.'

Safari za kibiashara ziliongezeka maradufu, Meli zilileta bidhaa mbalimbili na ziliwezesha kufanyika kwa biashara na India na nchi za Mediterani. Adulis ndicho kilikuwa kituo kikuu cha biashara zilizofanyika kwa njia ya bahari, na kulikuwa na hadhi hiyo pia kwa biashara ya ndani ya nchi. Aksum ilikuwa ndiyo sehemu kuu ya kukusanyia pembe za ndovu kutoka sehemu mbalimbali. Na Pliny na mtunzi wa Periplus wanaweka bidhaa hii kama bidhaa ya kwanza katika orodha ya vitu vilivyosafarishwa nje kutoka Adulis. Pembe hizo za ndovu zilikuwa bidhaa muhimu sana kwa Warumi waliopenda sana mambo ya starehe na anasa. Katika kipindi cha WaPtolemi, tembo wa Ethiopia tayari walikuwa wamethaminiwa sana. Majeshi yaliwatumia tembo kama namna ya vifaru. Baadaye tembo hao waliwindwa ili kupata pembe zao. Wakati wowote ule watunzi wa mambo ya kale wanapozungumzia habari za Adulis, Aksum au Ethiopia (Afrika ya Mashariki) hawakusahau kutaja umaarufu wa tembo na pembe zao. Watunzi lutaja pia bidhaa nyingine kama vile ngozi za kiboko, pembe za faru, ng'amba dhahabu, na viungo vya chakula, lakini kamwe hawakusahau habari za tembo. Kunako mwaka 1962, ujumbe wa kutoka Taasisi ya Akiolojia ya Ethiopia uligundua pembe moja ya ndovu kwenye magofi ya Aksum huko Adulis. Na mwaka 1967 ujumbe huo uligundua vipande vya sanamu ndogo ya tembo iliyotengenezwa kwa udongo mwekundu wa mfinyanzi, katika kuta za junba la kifalme la Dongour.

Asili ya Kiafrika

Ustaarabu wa Aksum ulikua sana katika karne za mwanzo za enzi zetu, lakini chanzo chake huanzia mbali sana katika kipindi kabla ya historia. Ustaarabu huu ulifunikwa na utamaduni wa karne tano za mwisho kabla ya enzi za Ukristo. Utaalamu wa akiolojia unajaribu kuelezea maumbile yake maalumu, lakini ni jiha chache za mada hii zilizokwisha fanyiwa utafiti.

Upangaji wa data za mambo ya kale haujamalizika. Kazi kubwa inayofuata ni kutaka kujua ni athari gani zilizotaka nje na zipi zilikuwa za asili ya ustaarabu wa Aksum yenyewe. Kama ilivyo katika nchi nyingine, ustaarabu wa Aksum ni matokeo ya maendeleo ya mabadiliko ya kawaida yakisaidiwa na hali za kijiografia na kihistoria. Mchango wa asili kwa kawaida ni muhimu sana kwani hapana shaka ya kwamba ustaarabu wa Aksum, mbali ya yote, ni matokeo ya watu wenyewe ambao kitambulisho chao cha kitaifa kimeibuka kutoka kwenye taaluma ya maandishi, lugha na desturi. Utaalamu wa akiolojia polepole unadhihirisha tabia ya kipekee sana ya mafanikio ya vitu ya Aksum. Bado hata hivyo kuna mambo mengi ya kufanya, na utafiti wa baadaye utazingatia zaidi tafsiri za maana za ushahidi uliochimbuliwa ardhiini. Lakini tayari tunafahamu ya kuwa ustaarabu wa Aksum unazo sifa zenye asili ya Kiafrika.

15

*Aksum:
mfumo wa siasa, uchumi na diculture,
utamaduni Kuanzia karne ya kwanza
hadi ya nne*

Kumbukumbu za kihistoria za karne ya pili na ya tatu zinaelezea kuinukia kwa haraka kwa utawala mpya wa Kiafrika: Aksum. Claudius Ptolemi, alikuwa wa kwanza kutamka kuwa Waaksum walikuwa ni mojawapo ya makundi ya watu wa Ethiopia. Hali hii ya kaskazini mashariki ya Afrika inafanana na ile iliyoelezwa kwenye riwaya inayoitwa *Aethiopia* iliyoandikwa na Heliodoros, mtunzi wa Kiyunani na Kifoeniki wa karne ya tatu. Heliodoros anaelezea kuwasili kwa mabalozi wa Aksum kama marafiki na wenye mfungamano wa kushirikiana na mfalme wa Kimeroe. Katabu cha *Periplus Maris Erythraei*, ambacho kina kumbukumbu za vipindi vya kuanzia kabla ya mwaka 105 hadi mwanzoni mwa karne ya tatu ya enzi zetu kinataja 'mji mkuu wa watu walioitwa Waaksum' kuwa ni mji usiojulikana sana, na kwamba ufalme huo uliotawaliwa na Zoscales ulikuwa bado mchanga sana. Zoscales alitawala pawani yote ya Bahari ya Sham ya Erythrea lakini jangwa la Beja lilikuwa chini ya mamlaka ya Wameroe. Ulinganifu baina ya tawala hizi mbili - Mji mkongwe wa Wameroe na mji mpya wa Waaksum - unakumbushia riwaya ya Heliodoros. Vyanzo vya kale kabisa vilivyotaja juu ya kupanuka kwa Aksum hadi kusini mwa Bara Arabuni ni maandishi nakshi ya Kisaba ya mwishoni mwa karne ya pili na mwanzoni mwa karne ya tatu. Maandishi haya yanaeleza juu ya "Wahabeshi" au Waaksum waliopigana vita nchini Yemen na kuteka baadhi ya maeneo yake. Mwishoni mwa karne ya tatu na mwanzoni mwa karne ya pili, 'Azabah, mfalme wa Aksum alipigana vita pia huko kusini mwa Bara Arabuni.

Hatimaye, Wahimaria waliunganisha nchi yote lakini wafalme wa Aksum walidai ya kwamba utawala huo ulikuwa wa kwao, inavyoweza kuonekana katika vyeo vilivyotumika.

Vita vilivyoendelea kusini mwa Bara Arabuni vinaelezwa pia katika maandishi nakshi mawili ya Kiyunani yaliyoandikwa na wafalme wa Aksum ambao majina yao na vipindi vya utawala wao havijulikani. Mtunzi wa maandishi nakshi marefu zaidi alitwaa maeneo ya pwani ya Yemen 'mpaka nchi ya Wasaba'. Vile vile alikamata maeneo makubwa ya Afrika 'kutoka mipaka ya Misri' mpaka nchi ya ubani ya Somalia.

Kunako mwaka 270 umaarufu wa nchi hiyo mpya ulisikika Uajemi. 'Kephalaia' ya mtume Mani (aliyeishi tangu mwaka 216 hadi 276) aliita Aksum kuwa mojawapo kati ya falme kubwa nne duniani. Aksum ilikuwa na rasilimali kiasi gani, na mfumo wa namna gani vilivyoitea mafanikio yote hayo?

Kazi

Idadi kubwa ya Waaksum walijihusisha na kilimo na ufugaji, kama wanavyofanya wakulima wadogo wadogo wa Tigre leo hii. Sehemu za bondeni na kwenye tambarare kulijengwa mabwawa makubwa ya kuhifadhi injaji ya mvua kwa ajili ya unwagihaji. Mifereji ilichimbwa kwa ajili ya kupitishia maji hayo hadi mashambani. Maandishi nakshi yanaonyesha ya kwamba ngano na nafaka nyinginezo zilipandwa. Kilimo cha mizabibu pia kilikuwapo. Plau za kukokotwa na ng'mbe zilitumika. Makundi makubwa ya ng'mbe, kondoo na mbuzi yalifugwa. Wanyama wengine waliofugwa ni punda na nyumbu. Kama walivyokuwa Wameroc, Waaksum walijifunza kukamata na kufuga tembo, lakini tembo hawa walilifadhiwa kwa matuuzi ya shughuli maalumu za kifalme.

Stadi za sanaa zilikuwa za hali ya juu; wahuzi na wafanyakazi wengine wa madini walikuwa wamefikia kiwango cha juu cha kazi zao. Uvumbuzi mkubwa sana wa kiteknolojia ulikuwa wa inatumizi ya zana za chuma. Uvumbuzi mwingine ulikuwa wa upigaji lipu katika inajengo ambao ulileta maendeleo ya ujenzi wa kutumia mawe na mbaao.

Muundo wa kisiasa

Hapo awali huenda Aksum ilikuwa eneo lililokuwa chini ya utawala wa mtawala mdogo wa kawaida, lakini baadaye ikawa mji mkuu wa utawala wa milki ya kimwinyi. Historia iliwakabilisha viongozi wake na majukumu mbalimbali, lakini jukumu kubwa zaidi ya yote lilikuwa ni kuimarisha tawala za maeneo ya kaskazini mwa Ethiopia, na kuyakusanya chini ya ufalme mmoja. Wakati mwingine ilitoka kwamba mtawala mpya mara baada ya kutawazwa aliwajibika kufanya kampeni katika nchi nzima, ili kuwalazimisha watawala wadogo wakubali rasini kwamba wako chini ya utawala wake.

Kuanzishwa kwa ufalme kulitumika kama msingi wa kujenga himaya. Kuanzia mwishoni mwa karne ya pili mpaka mwanzoni mwa karne ya nne, Aksum ilishiriki katika mapambano ya kijeshi na ya kibalazi, yaliyofanyika kati ya nchi za kusini mwa Bara Arabuni. Baada ya mapambano haya Waaksum waliyateka majimbo au mikoa iliyokuwa katikati ya uwanda wa Tigre na bonde la mto Nili.

Dola hiyo iligawanywa katika ufalme wenye wa Aksum, na falme zilizokuwa chini yake. Watawala wa falme hizi walikuwa chini ya mamlaka ya mfalme wa Aksum na waliulipa kodi. Wayunani waliinwita mtawala wa Aksum mfalme (ni Athanasius Mkuu na Philostorgius tu ndio waliinwita 'mdhalimu'). Wafalme waliokuwa chini ya marulaka yake waliitwa mahakimu wakuu, machifu na wadhalimu. Waandishi wa Kisyria kama vile Yohana wa Efeso, Simeon wa Beth-Arsaw na nuwandishi wa 'Kitabu cha Walumyari' walimtunakia cheo cha Ufalme (malk) "mfalme wa wafalme" wa Waaksum na pia wafalme wa Kihimiyari na 'Alwa ambao walikuwa chini ya mamlaka yake. Lakini neno la Kiaksum kwa vyeo vyote hivi ni 'negus'. Wanetajwa pia viongozi wa kijeshi ambapo waliitwa 'ma-negus' (*nagasta sarawit*). Mbali ya kazi yao ya kuongoza majeshi wakati wa vita, viongozi hawa walisimamia pia miradi ya ujenzi. Na kati ya 'ma-negus' maandishi nakshi yanataja wafalme wa makabila inanne ya Bega (Beja), ambao kila mmoja wao

aliwaongoza raia wasiopungua 1100. Maandishi hayo humtaja pia mtawala wa jimbo la Agabo ambaye raia wake walikuwa kati ya 1000 na 1500 kukiwamo watu wazima wanaume kati ya 200 na 275. Falme zilizokuwa chini ya mamlaka ya Aksum zilikuwa kwenye uwanda wa Tigre na kwenye jimbo la Ghuba ya Zula; nyuma ya Taqqaze. Vile vile falme hizo zilikuwa katika majimbo yenye ukame yanayozunguka nyanda za juu za Ethiopia, na katika mkono wa nchi wa Bara Arabuni. Baada ya ushindi wa mfalme Ezana tawala hizi ziliongezeka na kuenea hadi Unubi ya Juu, kati ya Poromoko la Nne ya Nili na Sennar. Kwa hiyo kukawa kumeundwa ngazi za mamlaka, kuanzia ngazi ya juu kabisa ya mfalme wa wafalme wa Aksum mpaka kufikia ngazi ya chini kabisa ya machifu wa jumuiia ndogo ndogo.

Kulikuwa na njia mbili za kutoza kodi kutoka kwa watawala wa ngazi za chini. Njia ya kwanza ni kwamba watawala hao wadogo walituma kodi zao kwa mfalme wa Aksum. Njia ya pili ni kwamba mwenyewe mfalme wa Aksum, akiongozana na watumishi wake pamoja na maafisa wake, alikwenda kwa watawala hao wadogo na kukusanya kodi, ikiwa ni pamoja na posho ya watumishi wake.

Watawala hawa vibaraka nao walifuata utaratibu huo huo wa kutoza kodi kwa watawala waliokuwa chini yao. Maafikiano kati ya njia hizi mbili yalipatikana wakati watawala wadogo walipoamua kulipa kodi zao katika sehemu maalumu zilizoteuliwa kwenye njia aliyopitia mfalme.

Hakuna habari zozote zinazoeleza juu ya mfumo wa utawala wa Aksum. Ndugu wa karibu wa mfalme walishika madaraka makubwa ya kuendesha shughuli mbalimbali. Kwa hiiyo si jambo la ajabu kuona kwamba Mfalme Constantine II wa Urumi alipoandika barua kwa Ezana hakumtaja Ezana peke yake bali alitaja pia jina la ndugu yake. Se'azana. Shughuli za kijeshi ziliongozwa na ndugu yake mfalme au jamaa zake wengine. Majeshi mengine ambayo hayakuwa na umulimu mkubwa yakiongozwa na wafalme wa kijeshi, yalikuwa na wapiganaji walitoka kwenye jumuiya au makabila.

Watawala wa Aksum waliwalazimisha watu wa makabila yaliyokuwa shupavu katika mambo ya vita kuishi kwenye mipaka ya nchi. Kwa mfano Wahabeshi waliwekwa kusini nwa Bara Arabuni, na makabila manne ya Bega katika jimbo la Matlia au katika eneo la Byrn (ambalo yawezekana liko Begendir).

Kuna taarifa chache mno zihusuzo historia ya ufalme huu ambazo zingetuwezesha kujua maendeleo ya mfumo wake wa kisiasa. Inawezekana muundo wa siasa ulijengeka na kuimarika wakati Aksum ilipokuwa imestawi sana kimaendeleo.

Kanuni za kawaida za sheria zilizotumika katika ufalme huu zinaweza zikafanyiwa uchunguzi kwenye taarifa za mahakama za mwanzo zilizomo kwenye sheria nnc za Safra (Drewes, uk. 73).

Biashara na Sera yake

Ufalme wa Aksum ulishika nafasi ya kwanza katika ulimwengu wa biashara. Kuna ushahidi kwamba Aksum iliweza kujitengenezea sarafu za dhahabu, shaba na fedha kwa madhumuni ya kukidhi mahitaji ya wafanyabiashara. Ilikuwa nchi ya kwanza katika eneo

la Afrika ya tropiki kutengeneza sarafu. Utengenezaji wa sarafu haukuwa tu kipimo cha uwezo wa kiuchumi bali hata wa kisiasa. Uwezo huu ulidhihirishia dunia nzima uhuru na maendeleo ya taifa la Aksum. Mfalme wa kwanza wa Aksum kutumia sarafu alikuwa Endybis, (kunako nusu ya pili ya karne ya tatu). Sarafu za Aksum zinafanana sana na sarafu za Byzantine za wakati huo.

Ukiacha dhahabu za zumaridi, bidhaa nyingine za biashara zilizoordheshwa zilipatikana kutokana na uwindaji, utegaji mitego na ukusanyaji. Bidhaa zilizopatikana kutokana na kilimo na zile za wanyama kama vile maziwa, na bidhaa nyingine zilizotengenezwa kwa mikono hazikutajwa katika maandishi ya kipindi hiki. Hii pengine inaonyesha kwamba bidhaa hizo hazikupewa umuhimu katika biashara na mataifa mengine. Yawezekana ngano maarufu kutoka Ethiopia ndiyo ihuzwa katika nchi za jirani. Habari za awali kabisa kuhusu biashara ya ngano, japo haziaminiki sana, zinaanzia karne ya kumi. Kinyume cha maelezo haya *Periplus* hutaja kuwa Adulis ambayo ni sehemu ya ufalme wa Aksum iliagiza kutoka nje vyakula na kiasi kidogo cha mvinyo pamoja na mafuta ya mizeituni kutoka Siria na Italia. Bandari za Pembe ya Afrika zilipata nafaka, mvinyo na maji ya zabibu kutoka Misri. Pia zilipata ngano, mchele, mafuta ya ufuta na miwa kutoka India. Bila shaka baadhi ya bidhaa hizo kama vile miwa huenda zilipelekwa Adulis pia.

Kwa jumla data za akiolojia zinathibitisha na kujaliza maelezo yaliyoandikwa kwenye kitabu cha *Periplus*. Uchimbuzi wa vitu vya kale katika matabaka ya kuanzia kipindi tunachokizungumzia cha Aksum, Adulis na Matara, na mabaki yaliyopatikana Hawila-Asseraw na Debre-Damo, vyote vineonyesha kuwepo kwa vitu vingi ambayo si vya asili ya Uhabeshi. Huenda baadhi ya vitu hivyo viliingizwa nchini humo kwa njia ya biashara. Vitu vingi vya kigeni vilitoka himaya ya Warumi na Byzantine, hasa Misri. Vitu hivyo vilikuwa ni pamoja na aina za birika zenye mikono miwili ya kushikia, ambazo inaonekana zilitumika kwa ajili ya kuwekea mvinyo au mafuta. Vitu vingine ni vipande vya vyombo vya kioo, mapambo ya dhahabu na vidani vya sarafu za fedha kutoka Urumi vilivyoonekana huko Matara. Vile vile kulionekana vito vya thamani (huko Adulis), taa za shaba nyeusi na mizani ya shaba nyeusi (huko Adulis na Aksum).

Vitu kutoka India pia vimepatikana huko, Vitu vyenyewe ni kama: muhuri uliopatikana huko Adulis, sanamu za udongo unwekundu huko Aksum, sarafu 104 za dhahabu za enzi ya utawala wa wafalme wa Kushana kabla ya mwaka +200 luko Debre-Damo.

Bara Arabuni kabla ya Uislamu ilitoa sarafu za shaba nyeusi na fedha ambazo zilionekana kwa bahati tu huko Erythrea na Aksum wakati wa uchimbuzi. Taa ya shaba nyeusi ilipatikana huko Matara. Mifano ya ufundi wa watu wa Meroe iko iningi. Vipande vya vyombo vya udongo vilivyovunjika vimepatikana katika sehemu nyingi. Sanamu - hirizi zilizopakshiwa zimepatikana Hathor na Ptah huko Aksum, na Horus huko Matara. Jiwe la kuchongwa likionyesha sanamu ya Horus akiwa juu ya mamba limeonekana Aksum. Vile vile bakuli za shaba nyeusi zilipatikana Hawila-Asseraw. Baadhi ya vitu hivi huenda vilifika Ethiopia kutokea Sudani kwa njia ya biashara. Lakini huenda vitu hivi vilitwaliwa wakati wa vita au vilitolewa kama kodi kwa mfalme.

Kuunganishwa kwa sehemu kubwa ya kaskazini mashariki ya Afrika kulikofanywa na Waaksum kuliwaongezea heshima na umaarufu. Miongoni mwa hawa Wakwasi, walikuwapo wafanyabiashara wa Kirumi Kiarabu na Kihindi ambao walipata wateja wa bidhaa zao za anasa zilizokuwa na faida kuliko bidhaa nyingine zote.

Faida iliyotokana na kuanzishwa kwa ufalme wenye nguvu iliwanufaisha jamii ya kifalme pamoja na kundi lote la Waaksum raia wa nji mkuu waliokuwa wamebahatika. Bidhaa nyingi zilizoorodheshwa kwenye *Periplus* ziliangizwa kutoka nje ili kuwatosheleza wananchi wengi. Bangili za shaba kutoka nje zilizotengenezwa na mafundi wa kienyeji, mikuki ya chuma kilichoagizwa toka nje, na vifaa vingine vya chuma kwa matumizi nchini na pia nguo zilizotengenezwa kwa vitambaa vilivyoagizwa kutoka nje vyote viligeuzwa na kufanywa bidhaa kwa jili ya masoko ya mumo nchini. Bidhaa hizi zilipatikana kwa wakazi wa mjini na wale wa vijijini. Mwishowe wafanyabiashara na makundi mengine ya kigeni waliamua kufanya maskani yao ya kudumu katika miji ya Adulis, Aksum na katika miji mbalimbali ya Ethiopia, na walileta bidhaa nyingi kutoka nje. Ni wakazi kama hawa ndio walionunua kwa wingi mvinyo na mafuta ya mizeituni. Vitu vilivyochinbuliwa kama vile inizani na mawe yake, mihuri, na sarafu za Kirumi na za Kikushana ni wazi viliachwa na wafanyabiashara wa Kirumi na Kibyzantine na wale wa Kihindi walioishi Adulis na Aksum. Miongoni mwa watu waliofanya biashara na Ufalme wa Aksum ni kama Banu-Kuraish kutoka Maka anayetajwa katika masimulizi ya Kiarabu. Wengine ni watu wa visiwani kutoka Socotra wanaotajwa na Cosmas Indicopleustes, na Wahindi wanaotajwa na 'Pseudo - Calisthenes'. Umuhimu wa miji na nchi za ngambo kwa biashara ya Ethiopia inamo mwanzoni mwa karne ya sita huonekana kutokana na idadi za meli zilizotia nanga katika bandari ya nchi hiyo ya Gabaza katika majira ya kiangazi ya mwaka +525. Orodha ya meli hizo hupatikana katika kitabu *Martydom of Aretha* na uchambuzi wa ndani wa orodha hiyo umefanywa na N. V Pigulevskaya.

Kama ilivyokuwa katika falme nyingine za zamani barani Afrika, mifugo ilikuwa alama ya utajiri mkubwa sana nchini Aksum, lakini ilikuwa vigumu kubadili mifugo kuwa bidhaa inayoweza kuuzika. Haikuwzekana kusafirisha mifugo kwenda nchi za nje kwa kutumia meli zilizokuwapo, ingawaje Waaksum waligundua namna ya kusafirisha mnyama mmoja mmoja kukiwamo hata tembo kadhaa wa jeshi la Abraha. Lakini kulikuwa na uwezekano wa ng'ombe kuswaga kuelekea ndani barani Afrika ambako waliuzwa kwa wakazi wa huko. Cosmas Indicopleustes anataja kwamba misafara ya Waaksum waliswaga ng'ombe hadi Sasu. Lakini sehemu kubwa ya ng'ombe hawa walitumika kama chakula kwa misafara hiyo.

Watumwa walikuwa bidhaa iliyohitajika sana karne nenda karne rudi. Katika maandishi nakshi ya Ezana na katika vyanzo vingine vihusavyo vita vya Waaksum - Wahimiyari, zipo taarifa kuhusu wafungwa waliotekwa wakati wa vita ambao walinunuliwa na wafanya biashara watumwa kutoka nchi za kigeni. Dhahabu na niadini ya fedha zilizotekwa vitani au kutolewa kodi na Unubi, Beja, Agaw, Himyar na nchi nyingine zilisafirishwa kutoka Sasu kwenda Aksum, ili kutengeneza sarafu ambazo zilitumika kununulia bidhaa za kigeni zilizohitajiwa na mfalme na maafisa wake.

Ingawa nchini Aksum viwanda havikutoa sehemu kubwa ya bidhaa zilizoweza kuuzwa bidhaa nyingi sana za kilimo na mifugo zilitoa mizigo ya kutosha kwa vyombo vya biashara na misafara. Hivyo ina maana ya kwamba Waaksum waliweza kuzalisha chakula chao wenyewe na bidhaa za kutosheleza mahitaji yao ya nchini, na vile vile kuuza nchi za nje.

Maelezo kuhusu jinsi Waaksum walivyokuwa wakiendesha shughuli zao yamefanywa na Cosmas Indicopleustis wakati akizungumzia jinsi Sasu ilivyopeleka Aksum dhahabu kutoka kwenye machimbo yake. Asema: Mwaka hadi mwaka mfalme wa Aksum, kwa kupitia kwa hakimu mkuu wa Agaw, alituma watu kwenda kuchukua dhahabu. Watu wengine wengi waliongozana na ujumbe huu maalumu kwa madhumuni yale yale ya kwenda kuchukua dhahabu. Hivyo, kwa pamoja, misafara hiyo huweza kuwa na jumla ya watu mia tano.' Dhahabu zilizopatikana zilikuwa katika vibumba vyenye ukubwa wa maharage yaliyojulikana kama tankara. Yaelekea kiini hasa cha msafara kilikuwa mawakala wa mfalme. Watu wengine waliojiunga nao huenda walitumwa na maafisa wa ngazi za juu au na matajiri wenyeji wa nchini Aksum. Wageni hawakurusiwa kujiunga na misafara hiyo.

Mamlaka ya Ufalme wa Aksum juu ya njia za biashara uliuletea faida kama vile kushiriki moja kwa moja katika shughuli za biashara. Alipoteka Unubi ya Juu, kusini mwa Bara Arabuni jimbo la Mto Tana, na makabila ya jangwani kuzungukia Ethiopia, mfalme wa Aksum alidhibiti njia zote zilizounganisha Misri na Syria na Bahari ya Hindi na nchi za bara ya kaskazini inashariki ya Afrika. Kama nulango ya bahari ya Malacca na Gibraltar, mlango wa Bab-el-Mandeb uliokuwammojawapo kati ya milango mitatu mkuu ya bahari katika ulimwengu wa kale, nao ulidhibitiwa na Aksum. Hapo kale Ba-el-Mandeb ilikuwa njia maarufu ya bahari iliyounganisha Bahari ya Sham na Ghuba ya Uajemi, India, Sri Lanka Mlango wa bahari wa Malacca, na nchi za Kusini-Mashariki na mashariki mwa Asia. Kuanzia Ghuba ya Aden, ilitokeza njia nyingine iliyopitia pwani ya Somalia hadi Afrika Mashariki. Njia hii ilivumbuliwa na kutumiwa na mabaharia kutoka kusini mwa Bara Arabuni. Na katika karne za awali za enzi zetu njia hii ilivumbuliwa na kutumiwa na mabahari kutoka India na pia wale kutoka katika himaya ya Warumi.

Katika kipindi tunachokishughulikia sasa hivi biashara katika Bahari ya Sham ilisitawi vyema, ingawa kuna hadithi nyingi za uharamia uliokuwa ukifanywa mara kwa mara wakati huo. Makabila kutoka pwani ya Afrika na yale yaliyoishi pwani za Bara Arabuni yalijihusisha na uharamia wa aina hiyo. Watunzi wa vitabu wa Kirumi walihusisha matukio ya uharamia katika enco hili na mabadiliko katika mitazamo ya kisiasa ya Aksum na nchi nyingine za Bahari ya Sham kwa Warumi.

Wafanyabiashara wa Kirumi walikuwa na nia na shauku kubwa ya kuhakikisha kuwa kuna usalama wa kutosha katika njia zote za biashara katika enco lililokuwa chini ya mamlaka ya Aksum. Kutokana na sababu hii wafanyabiashara hao waliunga mkono muungano wa himaya za Urumi na Byzantine na ifalme wa Aksum. Isingekuwa sahihi kuwatazama wafalme wa Aksum kama wakuzaji tu wa sera ya Urumi na Byzantine. Ukweli ni kwamba pande zote zilifuata msimamo tofauti kabisa ya kisiasa hadi wakati nia

Ingawa nchini Aksum viwanda havikutoa sehemu kubwa ya bidhaa zilizoweza kuuzwa bidhaa nyingi sana za kilimo na mifugo zilitoa mizigo ya kutosha kwa vyombo vya biashara na misafara. Hivyo ina maana ya kwamba Waaksum waliweza kuzalisha chakula chao wenyewe na bidhaa za kutosheleza mahitaji yao ya nchini, na vile vile kuuzwa nchi za nje.

Maelezo kuhusu jinsi Waaksum walivyokuwa wakiendesha shughuli zao yamefanywa na Cosmas Indicopleustes wakati akizungumzia jinsi Sasu ilivyopeleka Aksum dhahabu kutoka kwenye machimbo yake. Asema: Mwaka hadi mwaka mfalme wa Aksum, kwa kupitia kwa hakimu mkuu wa Agaw, alituma watu kwenda kuchukua dhahabu. Watu wengine wengi waliongozana na ujumbe huu maalumu kwa madhumuni yale yale ya kwenda kuchukua dhahabu. Hivyo, kwa pamoja, misafara hiyo huweza kuwa na jumla ya watu mia tano.' Dhahabu zilizopatikana zilikuwa katika vibumba vyenye ukubwa wa maharage yaliyojulikana kama tankara. Yaelekea kiimi hasa cha msafara kilikuwa inawakala wa mfalme. Watu wengine waliojiunga nao huenda walitumwa na maafisa wa ngazi za juu au na matajiri wenyeji wa nchini Aksum. Wageni hawakurusiwa kujiunga na misafara hiyo.

Mamlaka ya Ufalme wa Aksum juu ya njia za biashara uliuletea faida kama vile kushiriki moja kwa moja katika shughuli za biashara. Alipoteka Unubi ya Juu, kusini mwa Bara Arabuni jimbo la Mto Tana, na makabila ya jangwani kuzungukia Ethiopia, mfalme wa Aksum alidhibiti njia zote zilizounganisha Misri na Syria na Bahari ya Hindi na nchi za bara ya kaskazini mashariki ya Afrika. Kaina milango ya bahari ya Malacca na Gibraltar, mlango wa Bab-el-Mandeb uliokuwammojawapo kati ya milango mitatu mikuu ya bahari katika ulimwengu wa kale, nao ulidhibitiwa na Aksum. Hapo kale Ba-el-Mandeb ilikuwa njia maarufu ya bahari iliyounganisha Bahari ya Sham na Ghuba ya Uajemi, India, Sri Lanka Mlango wa bahari wa Malacca, na nchi za Kusini-Mashariki na mashariki mwa Asia. Kuanzia Ghuba ya Aden, ilitokeza njia nyingine iliyopitia pwani ya Somalia hadi Afrika Mashariki. Njia hii ilivumbuliwa na kutumiwa na mabaharia kutoka kusini mwa Bara Arabuni. Na katika karne za awali za enzi zetu njia hii ilivumbuliwa na kutumiwa na mabahari kutoka India na pia wale kutoka katika himaya ya Warumi.

Katika kipindi tunachokishughulikia sasa hivi biashara katika Bahari ya Sham ilisitawi vyema, ingawa kuna hadithi nyingi za uharamia uliokuwa ukifanywa mara kwa mara wakati huo. Makabila kutoka pwani ya Afrika na yale yaliyoishi pwani za Bara Arabuni yalijihusisha na uharamia wa aina hiyo. Watunzi wa vitabu wa Kirumi walihusisha matukio ya uharamia katika eneo hili na mabadiliko katika mitazamo ya kisiasa ya Aksum na nchi nyingine za Bahari ya Sham kwa Warumi.

Wafanyabiashara wa Kirumi walikuwa na mia na shauku kubwa ya kuhakikisha kuwa kuna usalama wa kutosha katika njia zote za biashara katika eneo lililokuwa chini ya mamlaka ya Aksum. Kutokana na sababu hii wafanyabiashara hao waliunga mkono muungano wa himaya za Urumi na Byzantine na ufalme wa Aksum. Isingekuwa sahihi kuwatazama wafalme wa Aksum kama wakuzaji tu wa sera ya Urumi na Byzantine. Ukweli ni kwanba pande zote zilifuata insimamo tofauti kabisa ya kisiasa hadi wakati nia

na sababu za kiuchumi za nchi hizi ziliposadifiana. Mfano mzuri ni wa karne ya sita wakati ambapo Wabyzantine, licha ya safari nyingi walizozifanya kwenda India bado walifikiri kwamba Waethiopia ndio walikuwa na uhusiano mzuri na nchi hiyo kuwapita.

Katika karne ya nne na mwanzoni mwa karne ya tano, bandari za Adulis na Pembe ya Afrika hazikuwavutia sana wanajiografia wa Kirumi. Lakini kati ya karne ya tano na ya sita Adulis ilikuwa bandari yenye kuongoza miongoni mwa bandari maarufu kuliko zote kati ya Clysmo na bandari za India. Umaarufu huu ulifanya majina ya bandari nyingine za Afrika yasisikike tena katika kumbukumbu za maandishi.

Adulis ilifikia kilele hiki cha umaarufu ambacho haikuweza kukifikia hapo kabla au baadaye kulitokana mno na ulinzi wa dhati uliotolewa na serikali ya awali ya kimwinyi ya Aksum. Kutokana na hali hiyo ilieleweka wakati huo ni kwa nini Adulis iliitwa soko lililositawishwa rasmi, katika *Periplus*.

Utamaduni

Maendeleo ya himaya ya awali ya kimwinyi yalionekana kwenye itikadi na utamaduni wa Aksuni, katika kipindi kilichodumu kuanzia karne ya pili hadi ya nne. Maandishi nakshi mafupi yaliyohusu miungu yalibadilika pale pale hadi kuwa maelezo ya undani zaidi yaliyolusu usliindi alioupata mfalme wa wafalme katika vita. Maandishi nakshi yenye mvuto maalum ni yale ya Ezana yaliyoandikwa kwa Kiethiopia na Kiyunani. Ezana alifikia kilele cha mtindo wa uandishi wa maneno ya nakshi katika uandishi uliotoa maelezo kamili juu ya mashambulizi yake huko Unubi. Maandishi nakshi hayo yanaonyesha ustadi mkubwa wa kutumia lugha, hisia za kidini, na matumizi mepesi ya dhana ngumu sana. Kutokana na maandishi hayo mfalme Ezana anaonekana kuwa mtu mwenye busara na ukarimu. Maandishi nakshi haya yanaweza kuonekana kuwa ni mafanikio ya uandishi. Maandishi nakshi hayo yana vitu vyenye kufanana na ushairi na fasihi ya nchi ya Ethiopia katika kipindi kilichofuata.

Mabadiliko yaliyokuwa sambamba na hayo yaliyoelezwa juu yanaonekana kwenye maneno yaliyoandikwa katika sarafu za Aksum. Sarafu za kuanzia karne ya kwanza hadi katikati ya karne ya nne zilikuwa na majina yasiyo ya kweli kwa kila mtawala. Majina yenyewe yalikuwa na neno *'be'esi* (mtu), na neno jingine lililohusu jina mojawapo la 'majeshi' ya Aksum. Hali hii ilihusiana na muundo wa kikabila na kijeshi na taifa la Aksum, na huenda ilitokana na demokrasi ya kijeshi ya Waethiopia wa kale. Sarafu zilizotengenezwa wakati wa utawala wa mfalme Ezana na wafuasi wake, zilikuwa mwito wa shime wa Kiyunani uliosema 'Nchi Na Iridhike.' Inaonekana ya kwamba mtindo huu ulikariri na kuonyesha itikadi rasmi ya nchi, na mifano ya kwanza inaweza kuonekana kwenye maandishi nakshi ya mfalme Ezana.

Katika mabadiliko yaliyotokea mara kwa mara ya miito hii ya Shime iliyoandikwa kwenye sarafu na katika maandishi nakshi ya kifalme ya Aksuni, mielekeo miwili



15.1 Sarafu ya dhahabu wakati wa utawala wa Mfalme Endybis



15.2 Maandishi nakshi ya Kiyunani kutoka Ezana (karne ya nne)

inayokinzana inajitokeza katika itikadi za watawala. Mielekeo hii ni: wazo la kifalme lililofungamana na umoja wa Ukristo na wazo lililojikita katika imani ya watu iliyotokana na mapokeo ya mila.

Wazo la kujenga himaya liliandamana na maendeleo ya mambo makubwa ya usanifu majenzi na uchongaji sanamu, kama vile mwamba mkubwa uliosimikwa, wenye urefu wa meta 33.5, uliojengwa kwenye msingi wenye urefu wa meta 114. Pia kuna bamba kubwa la mawe meusi yenye vipinio vya meta 17.3 kwa meta 6.7, kwa meta 1.12. Pia zipo sanamu kubwa za chuma na majumba makubwa ya kifalme ya Wafalme wa Aksum, Enda-Mikael na Enda-Simeon. Na vile vile majengo mengine ya kifahari kama vile Taaka-Maryam, lililojengwa kwenye eneo la meta 120 kwa 80. Vitu vyote hivi havikuweza kulinganishwa na vitu kama hivi mahali popote pale katika nchi za Afrika ya tropiki. Utiaji nakshi na marembo mbalimbali ulionekana wazi kabisa katika usanifu majenzi wa majengo. Mchanganyiko wa mawe na mbao katika ujenzi, zikipiskana na mapande ya mawe, yalitumika kwa kiasi kikubwa au kidogo katika sehemu mbalimbali za jengo moja. Katika ujenzi huo maboriti ya mbao na kokoto zilichanganywa na kuunganishwa na dawa maalumu ya kugandisha. Ujenzi wa aina hii ulirahisisha kazi ya wajenzi, na hivyo kufanikisha afundi na ustadi mkubwa sana wa utiaji nakshi na marembo. Katika kipindi hiki ufundi wa ujenzi na uchongaji nchini Ethiopia ulionyesha uasili wake mkubwa na papo hapo bila kupoteza athari na marekebisho mbalimbali ya utamaduni kutoka ufalme wa Kirumi, kusini mwa Bara Arabuni. India na Meroe. Athari zilizojitokeza sana ni zile za kutoka Siria ambazo zilitokana na kuenea kwa dini ya Kikristo.

Junba la kifalme, lenye minara minne la mfalme wa Aksum, limetajwa na Cosmas Indicopleustes. Kwa mujibu wa ujenzi mpya uliofanywa na Dk. Krenker, jumba hili lilikuwa ni jumba la kifalme, na mpangilio wa majengo mengine ya kando, kama vile majumba ya kifalme, mahekalu na mengineyo yote hayo yalifanya jumba hili kutofikiwa na kutoonekana kwa urahisi katika mji mzima.

Upagani wa Waaksum ulifanana sana na dini ya kale ya kusini mwa Bara Arabuni. Imani hiyo ilikuwa na mambo ya kutatanisha na yasiyoweza kueleweka kwa urahisi ikiwa na maumbile ya madhehebu yahasuyo mambo ya kilimo na ufugaji. Miungu iliyoabudiwa ilikuwa Astar, taswira ya sayari ug'andu na miungu wengine wawili waliojulikana kwa majina ya Beher na Meder, wakiwa wanawakilisha ardhi. Beher na Meder (miungu ya ngazi ya chini) walifuata Astar katika maandishi nakshi. Masalia ya muundo huu wa ibada ndio huonekana katika neno Egzi'abher, linatotumiwa na Wakristo wa Ethiopia kwa maana ya mungu au mungu Beher au mungu wa ardhi.

Mungu mwezi Hawbas aliabudiwa kusini mwa Bara Arabuni na Ethiopia kabla ya wakati wa utawala wa Aksum. Conti-Rossini alitoa ushahidi ulioonyesha ya kwamba mungu aliyeitwa Gad na madhehebu yake ambayo watakatifu wa enzi za kati walipanbana nayo, hakuwa mungu mwingine yoyote isipokirwa mungu mwezi. Conti-Rossini aliihusisha madhehebu haya na mwezi kutokana na ukweli uliosema ya kwanba paa wakubwa waliwekwa wakfu katika sehemu tunayojua leo kama Eritrea.

Alama ya jua na mwezi zimeonekana kwenye mawe ya makaburi huko Aksum, Matara

na Anza, na vile vile kwenye sarafu za wafalme wa Aksum waliotawala kabla ya kuingia kwa dini ya Kikristo. Huenda alama hizo zinaashiria mungu Mahrem, mungu wa ufalme na kabila la Waaksum. Katika inaelezo ya kipagani ya mfalme Ezana yaliyoandikwa kwa lugha mbili, Mahrem aliyeko katika matini ya Kiethiopia amepewa jina la Kiyunani la Ares. Maandishi nakshi yote ya Kiyunani yaliyohusu wafalme wa Aksum, ukiachilia mbali maandishi nakshi ya Sembrythes ambayo hayakuwa na jina la mungu, yanatumia jina la Ares. Inajulikana sana kwamba Ares wa Athenia aliabudiwa kama inungu wa vita. Kwa hiyo yafaa kuchukulia kwamba uwili wake, Mahrem, uliabudiwa pia kama mungu wa vita. Katika maandishi ya Aksum Ares-Mahrem, katika hadhi yake kama mungu wa vita, alijulikana na maadui wake kuwa ni 'shujaa,' 'asiyeshindwa na mwenye kushinda daima. Katika maandishi yaliyotoka Abba-Pantalewon, Ares, akijulikana kuwa ndiye mhenga wa kabila lake, aliitwa 'mungu wa Waaksumiti.' Akiwa kama mungu wa ufalme, wafalme walimwita Mahrem-Ares kuwa ni 'mungu wao mkubwa,' mhenga wa wafalme wote.

Ni dhahiri kuwa Mahrem, mungu wa vita na ufalme alikuwa na uwezo mkubwa wa kimadaraka ulingana na miungu wengine wote wa hapa duniani na huko mbinguni, kama vile wafalme waliotawazwa walivyokuwa na uwezo juu ya watu wao. Wakati huo huo shughuli za vita ambazo ziliwakilishwa na Mahrem, zilitukuzwa zaidi kuliko kazi nyingine za wakati wa amani. Hivyo, vita vilionekana kuwa ni jambo tukufu na lenye sifa ya kipekee kuliko kazi za shambani, ingawa shughuli hizi huenda zilikuwa takatifu kwa wahenga wao. Jambo jingine linaloonekana wazi katika dini ya Aksum ni maumbile ya itikadi ya matabaka ya awali, yaani yale ya jamii ya kimwinyi iliyokuwa ikiambika.

Waaksum walitoa sadaka kwa miungu wao. Sehemu kubwa ya sadaka hizo ilikuwa ya wanyama wa kufungwa. Mojawapo ya maandishi nakshi ya Ezana yameandikwa kwamba ng'ombe kumi na wawili walitolewa sadaka kwa mungu Mahrem kwa wakati mmoja kama sadaka. Kutokana na unila ya kale ya Kisemitiki, baadhi ya sadaka zilikuwa zikiwekwa na kufungwa katika vitambaa vya nguo safi ya ibada lakini kwa wengine haikuwa lazima kufanya hivyo. Lakini katika kipindi kabla ya utawala wa Aksum, nafasi ya mnyama hai aliyetolewa kama sadaka ilichukuliwa na sanamu yake wakfu. Sanamu za shaba nyeusi na za mawe, za ng'ombe dunie, kondoo na wanyama wengine, waliotolewa sadaka zikiwa na maandishi nakshi zilikuwa zimehifadhiwa.

Madhehebu ya Wathenga, hasa wafalme waliokwisha kufa yaliendelea kupewa nafasi kubwa katika ibada za Waaksum. Ilikuwa ni mila na desturi za Waaksum kutoa wakfu mawe ya karibu yaliyochongwa vizuri kwa ajili ya wahenga hao. Neno 'hawelt,' likiwa linatokana na mzizi wa *h-w-l*, likiwa na maana ya kutentbea huku ukizunguka kitu fulani au 'kuabudu'. Dhana hii inalinganishwa na ibada za Kiislamu za Kaaba (*Qaaba*). Sadaka zilipelekwa kwenye madhabahu na kwenye ngazi za minara ile mikubwa ya mawe ya makaburi iliyochongwa mfano wa madhabahu. Damu ya mnyama atolewaye sadaka ilichuruzikia kwenye mashimo yaliyochongwa mfano wa makabuli. Makaburi ya wafalme wa Aksum yaliheshimika kuwa ni mahali patakatifu katika mji. Vyombo na vifaa kadhaa wa kadha vilivyopatikana kwenye makaburi ya wafalme hao vinadhihirisha imani ya Waaksum ya kuwapo maisha baada ya kifo. Kuwa kumbukumbu zisizo za wazi

zinazoonyesha kuwa yalikuwepo madhehebu ya 'Mabwana wa milima'. Madhehebu haya hulingana na madhehebu ya namna hiyo huko Bara Arabuni.

Katika kipindi cha awali cha Waaksum mawazo ya kidini kutoka nchi jirani na za mbali zilingia nchini Ethiopia. Katika kitabu *Monumentum Adulitanum* kumetajwa jina la Poseidon. Huyu alikuwa mungu wa Bahari aliyeabudiwa na wakazi wa Adulis pamoja na watu walioishi sehemu ya kusini ya pwani ya Bahari ya Sham. Sehemu takatifu za Almaqah, mungu wa 'taifa' wa Wasaba na mfalme Gadara wa Aksum aliyeabudiwa, zilikuwa Melazo, na pengine huko Hawila-Asseraw. Pande kubwa la mwamba wa jiwe lililogunduliwa Aksum, likiwa na alama ya uhai 'ankh' ya Misri, na vitu vingine vilihusiana na madhehebu ya Hathor, Ptah na Horus pamoja na mende udongo, linaonyesha kwamba waumini wa dini ya Misri na Meroe, wakati fulani waliishi Aksum, Adulis na Matara. Sanamu ndogo za dini ya Buddha zilizopatikana Aksum huenda zililetwa na wafanyabiashara wa Kibudha kutoka India.

Kutokana na athari za utamaduni wa kigcni, schemu fulani ya utamaduni wa watawala wa Aksum haukuwa wa kitaifa, tu, bali wa kimataifa vile vile. Pamoja na Kige'ez, lugha ya Kigiriki ilitumika pia kama lugha ya taifa na ya kimataifa. Wafalme kama vile Za-Hekale na Ezana walifahamu Kiyunani (*Periplus* lueleza ya kwanza 'mfame Zoscales' alijua kusoma na kuandika kiyunani na kuwa mshauri wa Ezana, alikuwa Mfoeniki-Myunani, aliyeitwa Frumentius na anubaye baadaye alikuwa Askofu wa kwanza na Aksum). Wafalme wengi wa Aksum, wa karne ya tatu na ya nne walitengeneza sarafu ambazo zilikuwa na maandishi ya Kiyunani. Tunajua kuwa yapo maandishi nakshi sita ya kifalme yaliyoandikwa kwa Kiyunani huko Aksum.

Hatuna sababu ya kutufanya tufikiri kwamba Kisaba kilikuwa lugha mojawapo rasmi ya ufalme wa awali wa Aksum. Makala mojawapo kati ya matini tatu za Ezana ambazo kwa kweli zilikuwa katika lugha mbili za Kige'ez na Kigiriki imeandikwa kwa hati za Kihimiyari na ina maumbile fulani maalum ya hati za maandishi za Kisaba na Kihimiyari. Hati hiyo hiyo ilitumiwa katika maandishi nakshi ya kifalme ya Aksum na Ezana, Kaleb na Wa'azab. Kwa hiyo, pamoja na maandishi ya Tsehuf-Einni (Erythraea) tunazo matini tano za Kihimiyari cha kubuniwa kutoka Ethiopia. Lugha yao ni Kige'ez chenye maneno machache sana ya Kinasaba.

Haiieleweki kwa nini wafalme wa Aksum walitunzia matini za Kihimiyari cha kubuni pamoja matini za kawaida ya Kiethiopia katika maandishi nakshi yao yaliyokuwa rasmi. Lakini pote janbo hili lilipotokea laonyesha ni ushahidi wa athari ya kusini mwa Bara Arabuni.

Pengine matumizi ya hati za Kihimiyari na zile za Kiethiopia zenye irabu na kuanzishwa kwa matumizi ya michoro ni ugunduzi uliofanyika wakati wa utawala wa Ezana. Namna hizi zote za ugunduzi zilihusiana.

Fikra kwamba Kiyunani kiliathiri uundaji wa alfabeti za Kiethiopia hajathibitishwa, ingawa asili ya Kiyunani ya mfumo na alama kuu za michoro Kiethiopia kama yalivyoonekana kwa mara ya kwanza katika maandishi ya Ezana, inajitokeza wazi.

Alfabeti za Kiethiopia zinahusiana sana mfumo wa fonimu za Kige'ez na huu ni

uthibitisho kwamba herufi hizi ziliundwa tu na Waethiopia peke yao. Alfabeti hizi, zikiwa zimeongezewa alama nyingine zikitumika kwa muda mrefu mpaka leo hii. Alfabeti hizo livi sasa zinatabuliwa kuwa ni mafanikio makubwa sana ya ustaarabu wa Aksum.

Mara tu baada ya kuundwa hati hizi Kiethiopia zilianza kuathiri hati za Transcaucasia. D.A. Olderogge alipendekeza kwamba Mesrop Mashtotz alitumia hati huo wa Kiethiopia alipovumbua alfabeti za Armenia. Si muda mrefu kabla ya wakati huu (mwishoni mwa karne ya tano) hati za Kiethiopia huenda ziliingizwa nchini Armenia na Askofu Daniel wa Siria.

Aksum na Anenia zilikuwa na uhusiano wa kitamaduni wakati huo kupitia Siria. Tuna ushahidi juu ya kuwapo kwa Wasiria Aksum na wa athari katika usanifu majenzi wa Waaksum. Ushahidi huo unajitokeza kwenye mapande makubwa ya mawe yaliyokuwa kwenye muundo wa majengo yenye ghorofa kadhaa. Iko mifano pia inayoonyesha kufanana kwa usanifu majenzi wa Aksum na ule wa kusini mwa Bara Arabuni na India. Tunaweza pia kupendekeza kwamba katika karne ya pili na ya tatu athari za Meroe zilitawala Aksum. Vitu vyote vya Meroe vilivyotengenezwa kwa mkono na kupatikana nchini Ethiopia ni vya kipindi hiki. Athari za Kihindi na zile za Meroe huenda ndizo zilizosababisha kutumiwa kwa tembo katika ibada za kifalme nchini Aksum.

Ufalme wa Aksum ulikuwa na nguvu za kibiashara kwenye njia kutoka Dunia ya Warumi kwenda India, na kutoka Bara Arabuni kwenda kaskazini-mashariki ya Afrika. Ufalme huu pia ulikuwa makao makuu ya utamaduni ambao ulienea kwenye njia hizo. Nchi nyingi za kale za kaskazini mashariki ya Afrika na kusini mwa Bara Arabuni nazo ziliukilia maunbile mengi ya tamaduni wa Aksum zilipotawaliwa nayo.



Aksum ya Kikristo

Madhehebu ya Aksum kabla ya Ukristo

Hadi kufikia karne ya kumi na nane, dini ilishika nafasi muhimu katika jamii mbalimbali. Vituo vya dini ya Kikristo hivi leo yilikuwa makao makuu ya upagani hapo zamani. Hakuna taifa lolote lile lililopokea na kuukubali Ukristo kabla ya kupitia kipindi cha upagani.

Ethiopia ni nchi mojawapo iliyoanza na upagani kabla ya kuingia kwa dini ya Kikristo. Hapo awali nchi hii ilikuwa na aina mbalimbali za kuabudu. Katika nchi kama Ethiopia lilikuwa ni jambo la kawaida kuwepo kwa madhehebu mbalimbali na yaliyorithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Kati ya watu wa Ethiopia ya kale makundi ya Kikushi, kinyuune kabisa na matabaka tawala, yaliweza kuepuka kabisa kusilimishwa katika utamaduni wa Kisemitiki. Makundi haya ya Kikushi pia yaliabudu vitu vya kudura kama vile miti mikubwa, inito, maziwa, milima mirefu au wanyana. Vitu vyote hivi viliaminiwa kuwa na pepo wabaya na wazuri, hivyo basi watu hawa waliwajibika kutoa sadaka na makafara ya kila mwaka au kila msimu fulani.

Makabila yenye asili ya kisemitiki ambayo hayakurithi madhehebu ya Kikushi na Wakushi, walioathiriwa na Wasemitiki, walikuwa wamepiga hatua mbele wakilinganishwa na makundi ya watu tuliowataja hapo juu. Wao waliabudu kudura katika maumbo ya angani na ardhini (jua, mwezi ua nyota, ardhi ua udongo) yakijulikana katika utatu kwa majina ya Mahremu, Beher na Meder. Kulikuwa na upinzani kati ya miungu hawa na miungu wa kigeni au wa kitaifa wa kusini mwa bara Arabuni au Assyro-Babylonia kama vile Almagah, Awbas, Astart, ambao hapo baadaye walisilimishwa katika miungu ya Kiyunani Zeus, Ares na Poseidon.

Usilimishaji huo ambao kwa kiasi fulani haukufuata kanuni maalum uliruhusiwa na baadhi ya wafalme wa Aksum ambao utamaduni wao ulikuwa ni wa Kigiriki. Lakini usilimishaji huu haukaharibu kabisa misingi ya umungu wa Mahremu, ambaye aliabudiwa kama mungu wa taifa. Mungu Mahremu wa Waaksum angeweza kuitwa Zeus na Wayunani, na angeweza kuitwa Amon na Mnubi mwenye utamaduni wa Kimisri, kwa kuwa kila mtu alizungumza lugha yake. Itakumbukwa ya kwamba Alexander Mkuu, alipoingia Misri baada ya kushinda mwaka -332, alipokelewa na makasisi kama mwana wa Amon.

Matini za Ethiopia Kongwe za tangu wakati wa Mfalme Amde Tsion (+1313 +

1342), hueleza habari zihusuzo kuwepo kwa madhehebu ya nyoka mkubwa aliyeitwa 'arwe', pamoja na inatumizi ya Sheria za Musa. Nyoka huyo wakati mwingine alijulikana kama mungu-joka, na wakati mwingine alijulikana kama mfalme wa kwanza kutawala, Arwe-Negus, baba wa malkia wa Sheba. Imani hii maarufu na iliyoenea sana ilitokana na simulizi za kihistoria za Ethiopia ya kale, kabla ya kuanza masimulizi ya namna hii kabla ya historia ya kweli. Nchi zote zina hadithi za namna hizi kabla ya historia zao za kale na za kati.

Wasemiti waliotoka kusini mwa Bara Arabuni na ambao ni wahenga wa Watigre na Waamara waishio kwenye nyanda za juu, walisemekana ya kwamba walileta madhehebu mengi ya kusini mwa bara Arabuni. Kuwepo kwa kanuni hizi ambazo hazikudondolewa vyema na wasafiri, kunathibitishwa na makala zinazohusu sarafu na maandishi ya kale.

Kufanyika kwa ibada za madhehebu hayo kwenye jumba la kifalme la Aksum, kabla ya kuingia kwa dini ya Kikristo kunathibitishwa na hekalu la Yeha (ambalo bado limesimama hadi leo hii), minara mikubwa ya mawe ya kaburi yaliyotawanyika karibu na hekalu hilo, maeneo ya ngome na vitu vya kutolea sadaka.

Hata hivyo, hoja ya kufafanuliwa ni kama dini hii ambayo ilionekana kuwa na maendeleo kuliko nyingine, ilikuwa dini ya jamii ya kifalme na watu wengine wakubwa tu, au iliwashirikisha pia watu wote kwa jumla. Kama ushahidi unavyoonyesha kulikuwa na kikundi cha watu waliokuwa waumini wa dini ya Kiyahudi nchini Ethiopia. Kitabu cha *Tarike Neguest* kinachozungumzia historia ya wafalme, kinaeleza jambo hili kwa muhtasari tu. Huenda hiki kilikuwa ndicho kikundi kile kilichopata kutawala kwa muda fulani.

Hata kama tukiweka kando hadithi ya kuvutia ya *Kbre Neguest* (sifa za Wafalme) ambayo makasisi wa Ethiopia wanaitambua kuwa ndiyo kazi ya msingi ya historia na fasihi na ambamo, kwa makosa, wafalme wote wa Aksum wanasemekana walihusiana na Suleman na Musa, baadhi ya mila za zamani kabisa zinaonyesha kuwapo kwa waumini wa imani za dini ya Kiyahudi.

Lakini kutokana na kuingia kwa dini ya Kikristo, ambayo ama ilitangulia au ilikuja baada ya madaraka kuchukuliwa na vikundi vya watu wengine (Wasaba, Wahabesan na wengineo), Wayahudi, kama ilivyo, mahali pengine, walichukiwa sana na kufanyiwa vitendo viovu na hivyo kulazimika kuishi katika maeneo yaliyojitenga na watu wengine.

Kuingia kwa dini ya Kikristo nchini Aksum

Dini mpya iliyoanzishwa na Yesu Kristo huko Palestina, na kuenezwa na mitume wake katika falme zote za mashariki na magharibi, nayo pia iliingia Aksum na kukuta madhehebu yenye imani katika miungu wengi waliokuwa wakiabudiwa na Wakushi na dini za Uarabuni ambazo waumini wake walikuwa Wasemitiki na Wakushi walioathiriwa na Wasemitiki.

Kutokana na inatini ya Agano Jipya ambayo si ya kuaminika sana juu ya matendo

ya Mitume, yaliyoandikwa na Abdia, kuna baadhi ya watu wanaoamini kwa makosa ya kwamba Mtakatifu Mateo alikuwa Mkristo wa kwanza kuingiza dini ya Kikristo nchini Ethiopia. Hata hivyo, hoja hii haithibitishwi na maandishi yoyote ya kuaminika.

Historia ya wafalme, *Tarike Neguest*, inatambua ya kwamba mtu mashuhuri, Frumentius ndiye aliyeingiza dini ya Kikristo nchini. Frumentius huyo huyo baadaye aliiitwa 'Mkombozi' (Kessate Brhan) au Abba Selama, kwa maana ya Baba wa Amani. Kuwasili kwa Frumentius, nchini Ethiopia kuondoka kwake kwenda Alexandria, na kurejea kwake Aksum kunaelezwa kinaganaga na Eusebius na Rufinus.

Kwa mujibu wa maelezo ya Rufinus, mtu aitwaye Meropius wa Tyre alitamani kwenda sehemu za India akifuatana na jamaa zake wawili, Frumentius na Aedesius. Katika marejeo yao mtumbwi wao ulishambuliwa na wakazi wa bandari moja. Meropius alifariki na hao ndugu wawili walipelekwa kwa mfalme wa Aksum. Aedesius, aliyekuwa indogo zaidi, alipewa kazi ya kushikilia kikonobe, na Frumentius, kwa kuwa alikuwa na utamaduni wa Kiyunani, akawa mshauri wa mweka hazina wa mfalme. Vile vile akapewa kazi ya kuwafundisha masomo watoto wa mfalme. Mfalme huyo aliyetawala wakati huo yaelekea alikuwa Ella Amida, baba wa mfalme Ezana. Baada ya kifo cha Ella Amida, mkewe akawa mtawala wa Aksum, na akawaomba ndugu hao wawili kuendelea kuishi nchini ili kumsaidia kuendesha nchi hadi hapo mwanaye atakapokuwa mtu mzima kuweza kushika madaraka ya kuongoza nchi.

Kwa hiyo Frumentius alimlea mwana huyo wa mfalme kuipenda dini mpya ya Kikristo. Baadaye, Frumentius na nduguye Aedesius waliondoka. Wakati Aedesius anarudi Tyre kwenda kuwasaidia wazazi wake ambao walikwisha kuwa wazee, Frumentius alikwenda Alexandria kumtembelea baba yake mlezi, Askofu Athanasius. Huko alisimulia juu ya ukarimu na upendo wa familia ya kifalme ya Aksum kwa dini ya Kikristo. Hivyo alimshauri Athanasius apeleke askofu huko Aksum. Kwa kuwa Athanasius hakupendelea kumpeleka askofu ambaye hajui lugha wala mila na desturi za nchi ya Aksum, aliamua kumpa Frumentius uaskofu wa kanisa la Aksum, na hivyo kumrejeshwa nchini Ethiopia. Frumentius alirejea Aksum na kumbatiza mfalme wa Aksum na familia yake yote. Ni kuanzia wakati huu ndipo dini ya Kikristo ilipoanza kuenea nchini Aksum.

Mfalme wa kwanza wa Kikristo, aliyesoma na kubatizwa na askofu Frumentius yaelekea alikuwa Ezana, mwana wa Ella Amida. Na zipo sababu za kutosha kabisa kuamini ya kuwa mfano huu ulioonyeshwa na mfalme na familia yake uliigwa na kufuatwa na watu wengi wa nchi hiyo.

Wakati tunatambua vyema kazi iliyofanywa na Frumentius, tunapendekeza ya kwamba badiliko la dini lapaswa kuhusishwa na sababu zingine. Kutokana na makala na maandishi yalusuyo mambo ya kale na maandishi yaliyoandikwa kwenye sarafu za zamani, na taarifa za wasafiri, tunajua kwamba ukoo wa kifalme wa Aksum ulikuwa na uhusiano mzuri na wa kirafiki na nchi ya Constantinopo. Kati ya nchi hizi

mbili kulikuwa na ushirikiano wa kibiashara na kitamaduni. Katika kitabu chake cha *Vita Constantini*, Eusebius ametaja kuwapo kwa Waethiopia nchini Constantinopo wakati wa utawala wa Constantine. Matumizi ya hati na lugha ya Kiyunani katika jumba la mfalme wa Aksum pia yanatibitisha ukweli huu. Mfalme Zoskales alijua kusoma na khandika kwa lugha ya Kiyunani kama Mfalme Ezana. Mambo yote haya yanaonyesha kutapakaa kwa utamaduni wa Kiyunani katika nchi ya Aksum.

Mfalme wa Constantinopo, Constantine Mkuu, alikuwa ndiye Mfalme aliyetawala wakati wa enzi za akina Ella Amida na Ezana. Uzuri wa jumba la kifalme la Constantine na mapenzi yake kwa dini ya Kikristo kulielezwa tena na kupanuliwa zaidi na wasafiri wengine, mbali na huyo Frumentius; ambao kamwe hawakutajwa katika maandishi. Mambo yote hayo yaelekea yaliwapendeza sana watu wa jamii ya kifalme huko Aksum. Pia yaelekea yalimpendeza Frumentius, ambaye vile vile alimkuta mfalme na familia yake wakiwa tayari kabisa kuikubali dini hiyo mpya ya Kikristo ambayo ilikwisha enea katika ufalme wa Constantinopo.

Mabadiliko ya kutoka dini moja hadi nyingine kwa hakika hayawi rahisi kamwe, na pengine mabadiliko hayo yalikuwa magumu zaidi kwa wafalme, ambao walimpenda mungu wao kama baba yao. Heshiina na hadhi ya mfalme wakati wowote ule ilihusishwa na mungu wake. Matakwa na mapenzi ya mfalme kila wakati yalifanamishwa na yale ya viongozi wa dini. Wakati mfalme, kama vile Ezana, alipomwita mungu wake 'asiyeshindwa' ukweli ni kwamba alikuwa anajifikiria yeye mwenyewe. Kwa kutumia jina la mungu wake, alikuwa anatafuta nguvu zake mwenyewe.

Kwa hiyo tunaweza kuwazia matatizo yaliyompata Ezana, kama yale yaliyompata mfalme mwenzake, Constantine Mkuu. Kwa hakika ingawa mfalme wa Constantinopo aliendesha mabaraza ya Kikristo na kuwa mpatanishi wa matatizo ya kidini kwa viongozi wa dini, lakini yeye mwenyewe alibatizwa wakati wa kifo chake. Alifanya hivyo kwa kuogopa kusalitiwa na waunini wa madhehebu ya kale ya Zeus na Ares.

Na hivyo hivyo kama Guidi na Conti-Rossini walivyoeleza, Mfalme Ezana na familia yake hawakuacha mara moja imani zao za kale na kukubali zile za dini ya Kikristo kwa sababu ya kuogopa au kwa majiyuno yao. Maandishi mashuhuri yaliyogunduliwa na ujumbe wa Kijerumani nchini Aksum (DAE), kwenye juzuu la pili, yalianza na maneno haya: 'kwa msaada wa Mfalme wa Mbinguni na Duniani...' na ambayo yanakubaliwa na Waethiopia wote kuwa hizo ndio dalili zake za kwanza za Ukristo, yanaonyesha wazi shauku yake ya kutaka kusilimisha dini mpya katika imani za kale za miungu Beher na Meder. Alifanya hayo yote kwa kukwepa kabisa kutaja jina la Kristo, umoja wa Kristo na Mungu wa Utatu Mtakatifu unaoundwa na Kristo mwenyewe, Baba na roho Mtakatifu. Msemo wa 'ufalme wa Mbinguni na Dunia' *Igzi Semay Wem* uliotamkwa kwa mara ya kwanza kwenye karne ya nne na mfalme wa kwanza wa Kikristo - umebaki na kutumika hadi leo hii.

Hakuna maandishi wala maelezo yoyote ya nje au ya ndani ya nchi ambayo

yanaonyesha mwaka maalum wa kuingia kwa dini ya Kikristo nchini Aksum. Kitabu cha historia ya Wafalme, '*Tarika Neguest*,' pamoja na '*Guedel Tekle Haymanot*,' vyote vinaeleza ya kwamba ndugu hawa wawili Frumentius na Aedesius waliwasili mwaka +257, na kwamba Frumentius alirejea Aksum akiwa askofu mwaka +315. Habari nyingine zinatoa tarehe za mwaka +333, + 343, + 350 na kadhalika. Tarehe zote hizi zinaelekea ni za kubuni tu. Baadhi ya habari kutokana na maandishi ya nje zinaeleza ya kwamba Mfalme Ella Amida, baba wa Ezana, alifariki kati ya mwaka +320 na + 335. Ukiichukulia miaka hiyo kumi na tano kama umri wa walio wengi, na kuacha nafasi ya kutosha kwa ajili ya tarehe ya kuondoka na kurejea kwa Frumentius, inaonekana ya kwamba ubatizo wa Mfalme Ezana ulifanyika kati ya mwaka +350 na +360.

Kwa kweli kuna maandishi ya Kigiriki yaliyogunduliwa huko Philae, yanayoelezea ziara ya mtawala mdogo wa Aksum mwaka 360. Mtawala huyo aliyekuwa Mkristo aliitwa Abratoeis. Alitembelea Urumi na kupokelewa na mfalme wa Urumi kwa heshima kubwa iliyolingana na cheo alichokuwa nacho. Yaelekea mfalme huyo alikuwa anaitwa Constans II (aliyetawala kati ya mwaka +341 na + 368) na ambaye alikuwa mwana wa Constantine Mkuu. Ingawa mfalme huyu alikuwa Mkristo lakini alipokea imani za Arius, aliyekataa umoja na imani ya kuwepo kwa pamoja kwa watu watatu katika Utatu Mtakatifu, na hali kadhalika usawa wa Yesu Kristo na Baba. Baraza la Nicaea, lililokutana mwaka +325 na kuendeshwa na baba yake Constantine II, lililaani imani hii.

Adui mkubwa wa Arius alikuwa Athanasius ambaye alimpa Frumentius naskofu wa Aksum. Askofu Mkuu huyu mwenyewe aliondolewa baadaye kwenye madaraka yake na mtawala ambaye alimteua George badala yake. George alipendelea sana imani za Arius.

Habari za kuwasili kwa Frumentius nchini Aksum, mfuasi mkuu wa Askofu mkuu Athanasius aliyempa uaskofu, hazikumpendeza mfalme wa Constantinopo. Mfame huyo mara moja alituma barua kwa mfalme Aizanz (Ezana), na kwa ndugu Saizana. Katika barua hizo, Constantine aliwaita ndugu hawa 'ndugu zangu waheshimiwa sana.' Kwa njia ya kirafiki kabisa, aliwaomba wamrejeshe Frumentius kwa askofu mkuu mpya George, huko Alexandria, ili shauri lake lichunguzwe na yeye, George, na wenzake, ambao ndiyo pekee walikuwa na uwezo wa kuamua kama Frumentius angestahili kuongoza uaskofu wa Aksum.

Kwa bahati mbaya hatuna maandishi wala taarifa zozote ambazo zingeyonyesha majibu yaliyotolewa na ndugu hao wawili baada ya kupokea barua hii. Ingawa kutokana na manufaa ya kitaifa, ndugu hawa wawili waliwajibika kuendeleza uhusiano inwema na mtawala shupavu wa Constantinopo, lakini inaelekea hawakuafiki ombi lake. Habari zote zilizopatikana nchini Aksum zinadhihirisha ya kwamba Frumentius aliendelea kufanya kazi zake za kidini kwa amani akiwa kama askofu mpaka alipofariki.

Kuenea kwa dini ya Kikristo

Kuingizwa na kuenezwa kwa dini ya Kikristo kulikofanywa na Frumentius pamoja na ndugu wawili waliokuwa wafalme (Abraha na Atsbaha) kunajulikana sana. Kumbukumbu za habari za ndani ya nchi ya Aksum zinathibitisha ukweli huu. Jambo moja la kushangaza ni kwamba katika matini mengi yaliyoandikwa juu ya historia ya Aksum, ya kuanzia kipindi hiki na kuandikwa kabla ya mwisho wa karne ya kumi na tisa, hamna kabisa jina la Ezana ambalo laelekea kuwa la kipagani. Na wala hakuna maandishi yoyote katika vitu vya kale, pamoja na sarafu, yanayotaja jina la Abraha, ambalo linashukiwa kuwa jina la ubatizo la mfalme. Kwa hiyo tunayo majina mengi kwa mtu mmoja, ambaye kama Constantine Mkuu, kwa bahati mbaya au nzuri, alikuwa nusu Mpagani na nusu-Mkristo wakati wa utawala wake.

Athari za ndugu hawa wawili, na hasa ya Abraha, ilikuwa kubwa nchini kote. Yeye alijenga mji wa Aksum na kanisa lake kuu la kwanza. Makanisa kadhaa pamoja na jumuiya za watawa, yote haya yanasenekana yalianzishwa naye. Hata hivyo hatulasahau msaada mkubwa uliotolewa na kaka yake, Atsbaha na askofu Frumentius, na viongozi wengine wa dini ambao hawatajwi popote.

Watu wa kwanza kuongolewa na ambao waliipenda dini mpya inaelekea walipokelewa vyema na watu waliohusika kiukoo na kitamaduni na jumba la kifalme na familia yake. Watu hawa walikuwa Wasaba, Wahabesan, Wahimiyari wa Kisemitiki, wahenga wa Tigre na Wamhara, ambao walikubali dini ya mabwana zao bila matatizo.

Baada ya kuingia kwa dini ya Kikristo, na waumini wake kuongezeka, misafara ya kwenda mahala patakatifu iliongezeka pia. Katika barua iliyopelekwa kutoka Yerusalemi mwaka 386, Paola alimwandikia rafiki yake Marcella aliyeshi mjini Roma maneno yafuatayo: 'Tuseme nini juu ya Waarmenia ... Wahindi na Waethiopia wanaokuja hapa (Jerusalem) na kuonyesha wema usio kifani ...?' Mtakatifu Jerome, daktari wa kanisa la Kilatini, vile vile anaelezea kuwasili niara kwa mara kwa Waethiopia mahali patakatifu.

Kuenea kwa dini ya Kikristo katika ufalme wa Aksum katika karne ya tano na ya sita ilikuwa ni kazi ya wazee wa kanisa, ambao kutokana na maandishi ya niapo keo wametajwa kama *Tsadkan* (Waadilifu) au *Tesseatou Kidoussan* (Watakatifu tisa). Lakini kuwasili kwao katika utawala wa Aksum kuliingiza Aksum katika ugomvi wa kidini uliokuwa umeenea wakati huo katika miji mikubwa ya ufalme wa Byzantini.

Baada ya kulaaniwa kwa Arius mwaka 325, ikawa zamu ya Askofu mkuu wa Constantinopo, Nestorius, kuzusha mgogoro mkubwa kwa kutangaza hadharani ubinadamu wa Kristo dhidi ya imani iliyoanzishwa huko Nikea juu ya maumbile ya kimungu ya Kristo. Kufuatana na maelezo ya Nestorius, maumbile ya aina mbili ya Kristo (ya mungu-mtu) yalikuwa mbalimbali na yaliyojitenga kabisa. Bikira Maria alikuwa mama wa Kristo, kama binadamu, na wala siyo kama Mungu, na kwa hiyo sio Mama wa Mungu bali Mama wa Kristo.

Hoja hii ilipingwa vikali sana na Cyril, Askofu Mkuu wa Alexandria, na baba Mtakatifu Selestini wa Roma. Nestorius akalaaniwa sana huko Ephesus mwaka 431, kama mwasi wa dini na akafungwa jela.

Mrithi wake, Flaviani, Askofu Mkuu wa Constantinopo, naye aliweka maelezo mapya kuhusu maumbile mawili ya Kristo (binadamu na mungu), bila kukanusha ya kwamba Kristo alikuwa binadamu wa kweli na Mungu wa kweli. Kwa mawazo ya Flaviani, maumbile ya Kristo ambayo ni mawili, yote ni kamili na ya kipekee, na yameunganishwa tu katika utu wa Kristo. Bila kuchelewa Dioscoros, Askofu Mkuu wa Alexandria, aliipinga hoja hii. Yeye alisema kwamba Kristo alikuwa na umbile moja tu, ambalo kwa wakati mmoja umbile hilo lilikuwa mtu na mungu. Mmetezi mkuu wa imani hii ya kuwepo kwa hali moja tu ya Kristo alikuwa mtaalamu Eutyches. Mabishano makali yalibadilika kuwa machafuko katika Baraza lililofanyika Ephesus mwaka 442. Dioscoros na Eutyches wakawa washindi katika mabishano hayo, na yule mpinzani wao aliyeshindwa baada ya kupigwa mijeledi alifariki baada ya muda mfupi. Dioscoros hatimaye alirejca Alexandria kwa ushindi mkubwa.

Baraza la wakuu wa dini na maaskofu wakuu pamoja na wakuu wengine wa kanisa wapatao 636 lilikutana Chalsidon mwaka 451, chini ya uongozi wa mfalme Marciani. Majadiliano hayo yalijaa ubishani na kutoelewana inno kiasi ambacho haikuwa rahisi kujua nani alishinda na nani alishindwa katika majadiliano hayo. Kwa hali hii, suala hilo ikabidi lipelekwe kwa Papa wa Roma, aliyeainika kuwa ndiye kiongozi mkuu wa makanisa yote. Papa Leo Mkuu, katika barua yake, alitangaza kuwa yeye aliunga mkono imani ya kuwepo hali mbili tofauti za Kristo. Kwa hiyo baraza likamlaani sana Dioscoros. Wapinzani hao wa Dioscoros, wakiwa wanzejihami na maoni ya kiongozi mkuu wa kanisa la Kikristo duniani, kwa upande mmoja, na kuungwa mkono na mfalme Marciani, kwa upande mwingine, walithubutu kumfanyia visa vingi na hata kumpiga Dioscoros. Walifanya hivyo kulipa kisasi cha matendo yake aliyomfanyia Askofu Flaviani. Baadaye Dioscoros alifukuzwa na kwenda kuishi katika kisiwa cha Galatia.

Tangu wakati wa Frumentius, utawala wa Aksum, kama tunavyojua, ulikuwa chiri ya mamlaka ya uaskofu mkuu wa Alexandria. Mji huo ndio uliotewa askofu na kutoa amri za kanisa.

Kwa hiyo wafalme na maaskofu wa Aksum walikuwa waumini waliofuata imani ya kuwa Kristo ana hali moja ambayo baadaye ilipata jina la *Tewahdo* nchini Ethiopia. Habari za vitendo viovu alivyofanyiwa askofu mkuu wao zilipowafikia, waliona chaki na kuanza kuwachukua sana waumini wa imani ya hali mbili za Kristo. Maisha ya Waumini wa hali moja ya Kristo yakawa magumu sana katika nchi nzima ya Constantinopo, kwani wale walioteka Chalsidoi waliwanyanya sana na kuwakebehi mara kwa mara. Ili kuepuka hali hii ngunu waumini wa imani ya hali moja ya Kristo walikinbilika Misri na Uarabuni. Ni katika wakati huu ndipo wale Watakatifu tisa maarufu walipowasili kwenye ufalme wa Aksum na kuoniba kuishi na waumini wenzao waliokuwa na imani kama yao.

Watakatifu hao waliendesha kazi zao za utume katika sehemu mbalimbali. Abba Aregawi alikwenda mpaka Debre-Damo, ambako imani ya Joka kuu ilishamiri sana kwa watu wake. Abba Guerima alikwenda kuishi Mettera (madera) karibu na Senafe. Abba Aftse aliishi Yeha, mahali ambapo hadi leo unaweza kuona hekalu la kale lililojengwa kwa heshima ya mungu wao Almaqah katika karne ya tano. Penteleon na Likanos walibaki katika jiji la Aksum, wakati ambapo Alef na Tshima walikwenda Bhazan na Tseden Tsedeniya. Ym'ata na Gouba waliishi katika mkoa wa Guerealta.

Majengo ya watawa na makanisa yahiyojengwa kwa heshima zao bado yanaweza kuonekana leo hii katika sehemu walizoishi. Baadhi ya majengo haya yalichongwa kwcnye miamba mikubwa ya mawe na yanaweza kufikika tu kwa kamba. Katika jengo la watawa la Abba Ym'ata ambalo nalo limechongwa kwenye mwamba huko Goh (Guerealta) kuna mchoro wa mvingo unaonyesha Watakatifu hawa Tisa.


Watakatifu hawa waliimarisha zaidi dini ya Kikristo kama ilivyoingizwa katika karne ya nne na Frumentius. Kwa kweli watakatifu hawa walisaidiwa na warithi wa Mfalme Ezana, kama vile Kaleb na Guebre Meskel ambao walikuwa wafuasi imara wa dini ya Kristo. Katika mafundisho yao ya Injili, Watakatifu Tisa hao waliitangaza kwa nguvu imani ya kuwapo kwa hali moja tu ya Kristo. Imani hii iliwafanya Wakristo wengi kuteswa na kufanyiwa maovu mengi hadi kuzikimbia nchi zao na kwenda ugenini.

Hata hivyo, kuenea kwa dini ya Kikristo haikuwa kazi ya watawa hawa tisa peke yao, waliotoka kwenye himaya ya Byzantine. Wakiwa wanaongozwa na maaskofu kama vile askofu maarufu sana, Abba metta'e, mamia ya wenyeji na watawa wa kigeni walisaidia sana kuenea imani ya Kikristo, ingawaje hawakuwa na hadhi ya kutajwa kwa majina, kama watakatifu Tisa, katika taarifa za historia. Dini ya Kikristo iliingizwa katika majimbo mengine kama vile Beguemdr, Gogian na Choa kwa Wabeja na Waamhara, kuanzia kwenye mikoa ya kaskazini. Dini ya Kikristo ilinufaishwa na imani na kuungwa mkono na wafalme, malkia, wana wa wafalme, magavana na wakuu wa makanisa. Wote hao walikubali yajengwe majengo ya watawa na inakanisa katika maeneo ambamo imani za kimila zilistawi mno.

Sasa na tuangalie snala la lugha iliyotumiwa na watawa hawa walitokea sehemu mbalimbali huko Byzantine. Watu wa matabaka ya juu karibu na familia ya kifalme walijua lugha nyingi na kuzungumza lugha ya Kigiriki, Kisiria au Kiarabu. Kwa upande wao hakukuwa na tatizo la lugha. Lakini watawa wa kutoka nchi za kigeni walilazimika kujifunza lugha ya wenyeji kwanza kabla hawajaweza kuwafundisha watu. Inawezekana baadhi ya waumini waliokwenda Jerusalem, Constantinopo na Alexandria walizungumza Kiyunani au kisiria, na wangeweza kuwa wakalimani, au wenye uwezo wa kufundisha watu moja kwa moja.

Ufalme wa Aksum na Kusini mwa bara Arabun

Kwa muda mrefu inekuwa ikifahamika ya kwamba watu wenye asili ya Kisemitiki walivuka bahari ya Sham na kuishi kaskazini mwa Ethiopia wakitafuta ardhi yenye



16.1 Debre Damo (Tekle Tsadik Mekouria)

rutuba kuliko maeneo ya jangwa kama ya nyumbani kwao. Wageni hao walikuwa na ustaarabu wa hali ya juu kuliko ule wa wenyeji (Wabeja, Waaguewi na wengineo wa asili ya Kikushiti). Hatimaye wageni hao walitwaa madaraka na kuanzisha miji ya Yeha, Matara, Aksum na Sehemu nyingine.

Vikundi vingine vya watu wenye asili hiyo hiyo ya Kisemitiki (Wasaba, Wahimyari) walibaki katika maeneo yao ya asili. Wale waliovuka Bahari ya Sham wakawa watu wenye nguvu na uwezo mkubwa kiasi ambacho serikali kuu ya Aksum ilikuwa na uwezo mkubwa hata kufikiriwa kuwa ni nchi ya tatu kati ya nchi zenye nguvu duniani. Utambulisho wa watu hawa wa aina mbili walioishi pande zote mbili za Bahari ya Sham unathibitishwa na alama za majumba makubwa ya kifalme, inahekalu, miduara na umbo la inbalamwezi, vitu ambavyo viliwakilisha miungu Marhem na Almaqah.

Hadi mwanzoni mwa karne ya nne watu wa Kisemitiki wa ng'ambo ya pili ya Bahari ya Sham, walifuata dini zile zile za kimila ambazo ni za kuabudu mwezi wakitumia mwezi, mwandamo kama alama ya imani hizo. Alama hii hadi leo ingali inaheshimiwa hivyo na mataifa ya Kiarabu yafuatayo Uislamu. Pengine mtume Muhammadi hakuwataka waumini wake kuacha kabisa kutumia alama hii, lakini maaskofu wa Aksum walihakikisha ya kwamba wafalme wa Kikristo hawatumii kabisa alama hiyo na badala yake watumie alama ya Kikristo ya msalaba.

Mapambano kati ya Wakristo na Wayahudi Kusini mwa bara Arabuni Makundi mengine ya watu wa dini ya Kiyahudi walikuwa wakiishi katika eneo ili la Kusini mwa bara Arabuni kwa muda mrefu sana, pengine tangu Nebukadnezza alipouharibu mji wa Jerusalem mwaka -587, na kukaliwa kwake na Walagidae. Lakini idadi yao iliongezeka sana baada ya mji wa Jerusalem kuharibiwa kwa mara ya tatu, na mfalme Titus, mwaka +70. Wakati Wayahudi walipofukuzwa na Warumi, walikaribishwa na jamaa zao waliokuwa wakiishi Kusini mwa bara Arabuni.

Zaidi ya hapo, waumini wengi wa imani ya kuwapo kwa hali moja tu ya Kristo walihama Byzantine na kwenda kuishi Arabuni baada ya mkutano wa Baraza la Nikea na wengine zaidi baada ya lile la Chalsidoni, ambapo Waaria walilaaniwa na kufukuzwa kabisa. Walipofika huko, na kwa msaada wa wafalme na Wakristo wa Aksum, walijenga jumuiya imara sana. Chini ya utawala wa mfalme Justini I, kati ya mwaka +518 na +527, waumini wengi wa imani ya hali moja ya Kristo, wa Kisiria, walifukuzwa kwa amri ya mfalme, na kukiinbilika Hira (Najaf, ambayo sasa iko Iraq) na kutoka huko walifika Kusini mwa bara Arabuni na kuishi Najran.

Lakini Wakristo wakisaidiwa sana na Waaksunui waliongezeka idadi na kuweza kuanzisha na kuimarisha jumuiya yao. Makanisa inengi yalijengwa. Kwa mfano Miji ya Najran na Zafar (Tafar) ikawa miji mikuu ya utamaduni wa Kikristo, na vituo muhimu vya biashara.

Vilevile Wayahudi, wakiwa na ujuzi mkubwa wanaouonyesha katika kazi zao, nao waliunda jumuiya zao huko Saba na Himyar na wakataka kuniiliki biashara katika

sehemu hizo. Kwa hiyo kukazuka ushindani mkubwa sana kati ya Wakristo na Wayahudi.

Mauaji ya Wakristo wa Najran yaliyofanywa na Wayahudi

Wakati mfalme Justin I alipokuwa akitawala Byzantine, kati ya mwaka +518 na +527, Kaleb alikuwa mfalme wa Aksum. Huu ulikuwa ndio wakati ambapo wakisaidiwa na Wahimiyari, Wayahudi walipowaua Wakristo wa Zafari na Najran. Tukio hili limerekodiwa na waandishi wa mambo ya dini wa kipindi hicho, Procepius na Sergius.

Sergius anayedai ya kwamba alikusanya habari zake kutokana na watu walioshuhudia kwa macho yao wenyewe, anaelezea kama ifuatavyo tukio anabalo Conti-Rossini amelifasiri katika lugha ya Kiitalia katika kitabu kiitwacho '*Storia di Ethiopia.*' Dhu-Nuwas, mfalme wa Wahimiyari, akisaidiwa na Wayahudi na Wapagani aliwatesa Wakristo. Hivyo askofu Thomas alikwenda Ethiopia kuomba msaaada na akaupata. Wakiongozwa na Haywana, Waethiopia walivuka bahari ya Sham na kujiandaa kumshambulia Dhu-Nuwas. Kwa kuwa alikuwa hana jeshi lenye nguvu, Dhu-Nuwas aliandikiana mkataba wa amani na kiongozi wa Ethiopia, Haywana, ambaye baada ya kuacha sehemu ya jeshi lake nyuma, alirejea nyumbani. Sehemu kubwa ya majeshi ilipoondoka, Dhu-Nuwas kwa hila aliwaua Wakristo wa Zafar na kuteketeza makanisa yao yote, pamoja na kuanganiiza askari wote 300 wa Wakristo waliobaki nyuma kama walinzi. Lakini mauaji inabaya zaidi yaliyoelezwa na waandishi wa habari za kipindi hiki, yanasemekana yalitokea mwaka +523 mjini Najran, moja ya makao makuu maarufu ya Wakristo.

Safari ya kiyita ya baharini ya mfalme Kaleb

Baada ya mauaji ya mwaka +523, mtu mmoja mlishimiwa, aliyelitwa kwa jina la Umayyah, aliweza kurejea Aksum na akamwambia Mfalme Kaleb na askofu yale yote waliofanyiwa Wakristo. Wakristo wengine walikimbilia Constantinopo kwenda kumuarifu mfalme Justin juu ya yaliyotokea. Kwa kupitia kwa Askofu Mkuu Timothy wa Alexandria, Justin alimpelekea barua Kaleb na kumtaka alipize kisasi cha damu iliyomwagika ya Wakristo. Kwa hiyo Mfalme Kaleb alikusanya haraka majeshi ambayo yangehakikisha kupatikana kwa ushindi. Inasemekana alipata askari 120,000 na meli za kiyita 60 kutoka kwa mfalme Justin. Hata hivyo kuna habari zisemazo ya kwamba aliondoka na meli zake mwenyewe na kutia nanga njini Adulis, na kwamba jeshi lake lilikuwa na askari wasiozidi 30,000.

Kuelekea mwishoni mwa mwezi Mei, +523, Kaleb aling'oa nanga meli zake na kuelekea kusini mwa bara Arabuni mahali ambapo mfalme wa Himyariti alikuwa akimsubiri. Kwa kweli mfalme huyu Kaleb alipowasili alikuta bandari ya adui imezibwa na minyororo na kulindwa na askari waliokuwa tayari kujihami.

Bila kusubiri mwisho wa vita, Mfalme Kaleb alitafuta mahali pazuri pa kuyashushia majeshi yake yaweze kufika nchi kavu. Kwa bahati nzuri mtu mmoja

aliekamatwa katika hekaheka hiyo ya vita alikuwa ndugu wa mfalme Dhu-Nuwas. Hivyo aliweza kuwaonyesha mahali pazuri pa kushushia askari, na mfalme mwenyewe, pamoja na mitumbwi kama ishirini hivi wakafaulu kufikia nchi kavu.

Mafanikio haya yalimwezesha Kaleb kuwachapa barabara askari wa mfalme wa Himrar na kuwatawanya ovyo. Wakati sehemu kubwa ya majeshi yanaendelea kuchapana Mfalme Kaleb akisaidiana na askari wake saba walifaulu kumkamata Dhu-Nuwas. Akiwa amejawa na mori na uchungu kutaka kulipiza kisasi cha damu ya Wakristo, Kaleb, bila ya kusita, alimwua Dhu-Nuwas pale pale.

Mjini Najran, mfalme Kaleb alikuwako kwenye sherehe za kuadhimisha ushujaa wa Wakristo waliopoteza maisha yao kwenye inauaji. Na kabla ya kurejea Aksum, mfalme alijenga mnara mjini Marib ili uwe kumbukumbu ya ushindi wake katika vita hiyo. Kaleb pia alijenga mnara mjini Marib ili jina lake lisisahaulike na vizazi vya baadaye.

Kabla ya kurejea Aksum mfalme alimwacha Summyapha Awsa mjini Zafar, kwa amri ya Abraha. Summyapha Awsa alikuwa mkuu maarufu sana wa majeshi ya Kikristo, katika jumba la mfalme wa Aksum, na vile vile kusini mwa bara Arabuni.

Kikosi cha askari 10,000 kilibakizwa kuwa jeshi la ulinzi. Baada ya vita hivi Kaleb aliporejea nyumbani alipokelewa kwa shangwe kubwa! Lakini badala ya kukaa na kufaidi matuuda ya ushindi wake, mfalme ambaye alikuwa mcha mungu na mpenda vita, alianua kwenda kuishi kwenye nyumba ya utawa ya Abba Penteleon, na kuendesha maisha ya utawa, na kuapa kwamba kamwe hataachana na maisha hayo ya utawa. Mfalme Kaleb alipeleka taji lake la ufalme huko Jerusalem, na kumsihi askofu Yohanna alitundike taji hilo mbele ya mlango wa Kaburi Takatifu, kulingana na kiapo alichopa kabla ya kwenda kupigana vita.

Ikiwa taarifa zilizotolewa na makala za wenyeji ni za kweli basi uamuzi wa mfalme wa kuacha madaraka yake ya uongozi ni wa kustaajibisha. Lakini matini nyingine zinasema ya kwamba Kaleb aliendelea na uongozi hadi mwaka 542. Inawezekana kabisa kwamba mfalme aliendelea kutawala kwa muda wa miaka kumi na saba mingine, baada ya kurejea Aksum, ikiwa vita vyake dhidi ya Dhu-Nuwas vilifanyika huko Uarabuni mwaka 525, ikiwa hapana kosa katika tarehe.

Fasihi andishi

Aksum ilikuwa na alfabeti nyingi zilizotumika na watu walioelimika na utawala wa ufalme. Baadhi ya minara mikubwa ya mawe ya kaburi iliyochongwa nchini Aksum ipo ambayo ina maandishi ya lugha ya Kisaba tu, au Kige'ez, au wakati mwingine Kiyunani. Lakini hakuna hata mnara mmoja uliokuwa umeandikwa kwa lugha zote tatu pamoja. Kisaba kilikuwa na alfabeti za makabila ya Kisaba ambayo yanadhaniwa kuwa ni mababu au wahenga wa Waaksumi, kama inavyoelezwa katika matini ya mapokezi kama vile Neguede Yoktan (kabila la Yoktan) ambalo lilizaa makabila ya leo ya Amhara, Tigre, Gouraghe, Argoba na Harrari (Aderes).

Kama kilivyo Kiingereza leo hii, Kiyunani kilikuwa ndiyo lugha ya kipindi hicho.

Lugha hiyo ilikuwa ni ya kigeni iliyoingizwa nchini Aksum kutokana na uhusiano wake wa kitamaduni, kiuchumi na kisiasa na himaya ya Byzantine. Hatimaye ni Kige'zi, ambacho mwanzoni kabisa kikiwa hakina irabu na baadaye kutiwa sauti, kilichokuwa lugha rasmi ya taifa la Waaksumi. Lugha hii pia iliitwa lugha ya Aga'izyan, neno lililotumiwa na wenyeji, lenye maana ya wakombozi.

Kwa jumla, lugha huwapa watafiti ishara nyingi muhimu lakini haisaidii kuwawezesha kugundua kikundi cha kabila lililohusika. Kwani wenyeji wanaweza kuwa ni wenye asili ya Kisemitiki, wa taifa la Kiaksumii na utamaduni wao ukawa ni ule wa Kiyunani. Na wengine huenda wakawa ni Wabeja au Wablemi; Wanubi kwa kuzaliwa au kwa taifa, na wenye utamaduni wa Kimisri. Kwa hiyo intu aliyezungumza au kuandika Kige'zi si lazima awe Mwaksumi.

Baada ya Waarabu kukamata na kuteka Mashariki ya Kati na Afrika ya Kaskazini, wakati wa karne ya saba, lugha za Kiyunani na Kisaba zikapotea na badala yake Kige'zi kikaanza kutunika katika shughuli mbalimbali za kiraia, kijeshi na kidini. Kiyunani kiliendelea kuwa na athari tu katika tafsiri ya Biblia, yaani kutoka Kiyunani na kuingizwa katika Kige'zi. Vilc vile, athari za Kiyunani zilidumishwa tu kutokana na baadhi ya maandishi ya Mapadre wa kanisa kama vile Cyril na Alexandria au Mtakatifu John Chrysostom.

Maandishi ya kwanza yanayoonyesha mwanzo wa fasihi audishi ya Aksum ya Kikristo ni yale ambayo ujumbe wa Ujeruni uliotcmbelea Aksum ulirckodi chini ya nambari 11, ambamo kwamo Mfalme Ezana, akiwa ndiyo kwanza amebatizwa, alieleza historia yake na juu ya watu wa Noba (Wanubi). Wanoba walithubutu kususia uwezo wa inadaraka yake ng'ainbo ya Mto Takazi na kuwaua wajunbe wake aliwatuma huko. Tunaweza kuelewa maadili ya mfalme huyo aliyewalaumu Wanoba kuwa ni "... wenye tabia mbaya za kuwanyanyasa na kuwakandamiza watu wa Mengourto, Hasa na Baria, watu wa rangi nyeusi na nyekundu (*Seb'a Tselime, Seb'a Que'yh*), kwa kuvunja kiapo walichoapa..." Je, hii ilikuwa ni matokeo ya dini yake mpya?

Athari ya dini ya Kikristo inajitokeza pia katika sarafu nyingi za wafalme wa Aksum. Katika sarafu hiizo alama ya mwezi mwandamo ilitoweka na badala yake kukawa na alama ya msalaba, alama ya dini ya kale ya Kikristo. Badhi ya wafalme wa Aksum waliopenda sana kujulikana na watu au kuungwa mkono na watu wake walikuwa na maandishi ya kushangaza katika sarafu zao. Sarafu za Mfalme Wazed au Wazeba (mwana wa Mfalme Kaleb, wa karne ya sita) zilikuwa na picha yake upande mmoja, na maandishi ya 'wananchi wawe wa furaha,' upande wake wa pili. Sarafu muhimu sana ni zile za Mfalme Lyouel, ambazo zilikuwa na kichwa chake kilichovikwa taji. Upande wa kulia wa taji kuna msalaba mdogo. Upande wa pili wa sarafu ulikuwa na alama ya msalaba. Alama hii ya msalaba inaonyesha ya kuwa mfalme huyu alikuwa Mkristo imara. Katika sarafu nyingine ya mfalme huyu huyu kuna maandishi yasemayo 'Kristo yupo nasi.' Pia kuna maandishi ya Kige'zi yasiyo na irabu. Hii ndiyo mara ya kwanza jina la Kristo limetajwa.

Agano la Kale pole pole lilifasiriwa kutoka Kiyunani katika Kige'ezi katika karne ya tano na ya sita. Biblia iliingia Ethiopia na kuanza kutumika, na mafundisho yake yalikuwa maarufu sana katika jumba la mfalme na viongozi wote wa dini. Hatimaye Biblia ikawa ndiyo kiini na msingi wa sayansi na falsafa bila ya kufifisha kazi za mapadre wa kanisa.

Agano la Kale pole pole lilifasiriwa kutoka Kiyunani katika Kige'ezi katika karne ya tano na ya sita. Biblia iliingia Ethiopia na kuanza kutumika, na mafundisho yake yalikuwa maarufu sana katika jumba la mfalme na viongozi wote wa dini. Hatimaye Biblia ikawa ndiyo kiini na msingi wa sayansi na falsafa bila ya kufifisha kazi za mapadre wa kanisa.

Baada ya Baraza la Chalsdony kukutana mwaka +451, Watakatifu Tisa na mitume wao waliwasili nchini Ethiopia na kuimarisha athari ya imani ya kuwapo kwa hali moja tu ya Kristo, kwa baadhi ya viongozi wa dini wa Ethiopia. Hii ndiyo maana kanisa la Ethiopia liliepuka kwa tahadhari maandishi yote yenye thamani au la, yaliyotokea magharibi. Makubaliano yaliyofanyika kati ya Amr Ibn Alas, sahaba wa Mtume Muhammadi kwa upande mmoja, na Maaskofu Wakuu Benjamin na Chenouda wakati mji wa Heliopolis ulipokuwa ukishambuliwa, mwaka 640 kwa upande mwingine, wakati Misri ilipokuwa ikitekwa, yatakumbukwa sana. Chuki zao dhidi ya Maaskofu Mukaukis na wengine wote waliohubiri imani ya hali mbili za Kristo yaliwafanya Wamisri wote walioshika imani ya kuwapo kwa hali moja tu ya Kristo kuwaunga mkono Waislamu.

Watawala wa Kiamhara wanaosemekana kuwa walitokana na ukoo wa Solomon na kwamba walikuwa warithi halali wa wafalme wa Aksum, waliwaheshimu sana wafalme hawa wawili: Daudi na mwanee aliyetitwa Suleman. Halafu akafuata Alexander Mkuu, Constantini Mkuu na Theodosius II. Hawa wawili waliheshimika sana kwa sababu ya msaada waliotoa kusaidia dini ya Kikristo. Hawakuwa na habari zozote kuhusu Charlemagne, Charles Martel au Charles mnene. Watu mashuhuri waliomo kwenye biblia na aubao walifahamika kwa watawa ni Joshua, Samson na Gidion. Maandishi kama vile winbo wa Nyimbo, Vitendawili, Kitabu cha Busara za Solomoni, Busara ya Mwana wa Sirach, na kadhalika, vilitambuliwa kuwa ni maandishi ya falsafa ya kweli kuliko maandishi ya Plato au Aristotle. Mabingwa kama Virgil, Seneca na Cicero na wataalamu wa kale wa Magharibi hawakujulikana kabisa.

Jamii ya Kikristo ya Ethiopia inapenda kumsifu Daudi zaidi kuliko mtu mwingine yoyote yule kwani wanamtambua kuwa ndiye babu wake Maria na Ufalme wa Suleman. Muethiopia mcha Mungu huiheshimu zaburi na kuamini kuwa kusoma zaburi hizo kila asubuhi kutamsaidia kuepukana na maovu yote. Kama alivyokuwa ameamini Daudi, wao pia waliamini ya kwamba kusoma zaburi hizo kila mara kulifanya Mungu Mwenye Uwezo Mkubwa awe nao wakati wote.


Kuna baadhi ya waumini ambao huzitumia zaburi hizo kama sala, wengine huzitumia kama dawa za kidini. Mwanazuoni hufahamu moyoni zaburi inayofaa

katika kila mazingira. Zaburi hizi huimbwa kimoyomoyo kwa madhumuni mbalimbali, kama vile kupata furaha au kuepuka balaa, kujikinga na maafa ya kutisha, au kujikinga na bunduki. Kwa jumla wanazuoni hao hudondoa zaburi nambari 6, 7, 10, 57, na nyinginezo.

Sehemu ya urithi ambayo Ethiopia imepata kutoka Aksum ya Kikristo ni sala zilizokusanywa na kujulikana kama Dgoya. Kwa mujibu wa habari za kutoka wa wenyeji wa karne ya kumi na nne mtunzi huyo alikuwa mwenyeji wa Aksum aliyemitwa Yared ambaye alitawala wakati sawa na Mfalme Guebre Meskel na wa Abba Aregawi, mmoja wa Watakatifu Tisa.

Kama utasoma nyimbo za dini katika kitabu hiki kwa makini unaweza kuona ya kwamba matini zimetolewa kwenye Biblia, kutoka kwenye maandishi ya maaskofu wakuu wa awali, wataalamu maarufu wa mambo ya dini wa karne ya tatu hadi ya nane, na kutoka vitabu vya agano la kale. Matini zenyewe zimepangwa kimashairi na kwa ufasaha, na kuunda mkusanyiko mkubwa wa maandishi yaliyogawanywa katika vitabu, sura na beti kadhaa. Halafu beti zenyewe zimetenganishwa (na instari wa kwanza ulioandikwa kwa rangi nyekundu). Na kuna ubeti mmoja kwa kila siku ya kila mwaka na mwezi. Beti hizo zimeandikwa kuwasifu malaika, watakatifu, mashahidi, Bikira Maria na Mungu. Zote hizo hutumika katika ibada za asubuhi na jioni.

Maandiko ya biblia ya nyimbo za dini yana historia ndefu za kimila. Nyingine ni za kweli na nyingine ni ngano, ambazo sikuzishughulikia sana. Nimeamua tu kufanya muhtasari. Haya yote hufanya sehemu ya urithi ambao Aksum ya Kikristo imerithisha kwa Waethiopia kwa karne na karne.



Wazaa - Waberiberi

Makabila yaliyounda taifa la Libya yalikuwa yameishalowea Afrika kabla ya kuwasili kwa Wafoeniki katika pwani lizo mnamo elfia ya kwanza kabla ya enzi zetu. Makabila hayo hayakubadilika katika wakati wote huo wa kale kwa kuwa yaelekea kwamba kuongezeka kwa Wafoeniki na Warumi hakukuwa na matokeo yoyote juu yao. Aidha, athari zinazotokana na idadi ya Wafoeniki katika Afrika kaskazini haziwezi kupimwa kwa usahihi. Lakini haielekei kama Wakariteji walikuwa wakioniba msaada wa namluki wakati wa vita ikiwa wale askari wa asili ya Kifoeniki walikuwa wengi. Athari iliyotokana na idadi ya Warumi pia nayo ni vigumu kupimwa.

Mnamo elfia kumi na tatu kabla ya enzi zetu ulikuwapo utamaduni ambao uliitwa kwa makosa 'Ibero-Maurusia'. Utamaduni huu ulikuwa wa taifa la Mehta - el - rbi. Walikuwa warefu (mita 1.72 kwa wastani) na wenye vichwa vyembamba na virefu. Walikuwa na komo la uso na miguu na mikono mirefu. Watu hawa walikuwa pia na mazoea ya kung'oa meno yao ya chonge. Hali inayodokeza umbo la kati na lenye kichwa kifupi na kipana na dalili za wembamba ziligunduliwa katika baadhi ya makao hasa katika Koluninata, magharibi mwa Algeria mnamo mwaka -6000. Utamaduni wa Ibero-Maurusia ulitoweka mnamo mwisho wa elfia ya tisa. Hata hivyo haikutokea mara moja kila mahali. Mahali pake palichukuliwa na utamaduni wa Kapsia katika sehemu za Sarenaika lakini ulizidiwa nguvu na utamaduni wa sehemu za magharibi mwa Algeria na Moroko. Hakuna dalili kwamba kulikuwepo na utamaduni huo wala kama uliacha alama chache katika eneo la Tangiers. Haiwezekani kwamba utamaduni huu ulitokea Ulaya kwa kuwa ulikuwapo kabla ya kuanzishwa kwa safari za baharini kupitia mlango bahari wa Gibraltar kwenda na kurudi Sisili. Yawezekana kwamba utamaduni huo ulitoka Mashariki lakini huenda pia ulitoka kaskazini ya Sudan ya Kinailoti kama anavyodai J. Tixier. Baadaye walipozidiwa na watu waliokuwa wakihamia sehemu hizo, hao Wa-Ibero-Maurusia, bila shaka walikimbilia vilimani na yawezekana kuwachukulia kama sehemu ya watu wa kwanza wa Jebeli.

Mnamo mwaka wa -7000 walitokea watu warefu, wa taifa la Mediterani lakini waliokuwa na tabia za Kinegro. Walijulikana kama Wakapsia kutokana na mahali

palipoitwa Kapsa (Kafsa ya sasa). Waliendelea kuishi vizuri katika eneo ambalo halijaelezwwa vizuri lakini bila shaka zilikuwa sehemu za bara ambazo hazikuenea hadi mipaka ya Magharibi ya Afrika Kaskazini wala katika kusini mwa Sahara. Kwa kawaida walikaa katika vilima au miteremko karibu na maji, lakini wakati mwingine walikaa katika nyanda zenye maziwa au kinamasi. Miongoni mwa vyakula vyao vilikuwa ni konokono. Utamaduni huu pia ulitoka mashariki na haiwezekani kwamba ulienezwwa kwa njia ya bahari. Yadhaniwa kwamba ulifikia kikomo chake mnamo mwaka wa -4500. Ingawa umbo la kichwa la Wakapsia lilifanana na la watu wengine wa wakati huo, yafikiwa kwamba wazaa Waberiberi hawakutokeza hadi enzi za Neolithi. Hii ni kwa sababu ibada za matanga za Wakapsia hazikuwepo katika nchi za Walibya na Waberiberi. Hata hivyo itaonekana kwamba desturi ya kutumia na kupamba inayai ya mbuni ambayo ilipendwa sana na Wakapsia, kama alivyosema Camps-Fabre, ilidumu wakati wa Neolithiki hadi wakati watu wa Libya wanaotajwa katika kumbukumbu za kihistoria, kama Wagaramante. Hawa Wagaramante kama asemavyo Lucian, waliyatumia mayai hayo kwa madhumuni mengi sana na hii yathibitishwa na machimbo yaliyochimbwa huko Abou-Njem (sehemu za bara za Tripolitania). Hata hivyo mtu wa Neolithiki katika Afrika ya Kaskazini aweza kuchukuliwa kama binamu wa Mkapsia. Kwa hali yoyote ile historia ya watu wa Maghreb bila shaka yatokana na mwungano wa aina tatu za watu; Waibero-Maurusia, Wakapsia na Waneolithiki. Uwiano wa idadi zao haujulikana bado.

Kwa ujumla inakubalika kwamba enzi ya Neolithiki ilianza kulipozuka vifinyange. Vipimo vya Kaboni 14 vyaonyesha kwamba matumizi ya vifinyange yalienea kutoka Sahara ya kati na ya mashariki. Katika eneo hili la kutoka Ennedi hadi Hoggar, fahali walianza kufugwa mnamo mwaka 4000. Yawezekana kwamba ng'ombe walianza kufugwa mapema zaidi huko Akakusi. Ushahidi wa kuwepo kwa utamaduni wa Neolithiki katika mila za Wakapsia unaanzia nyuma karibu mwaka -5330 katika ngome ya Elatta, hata mapema kidogo katika bonde la Sawura na hauelekei kushamiri katika sehemu ya kaskazini ya eneo la Kapsia kabla ya mwaka -4500. Katika eneo lililoko kati ya tamaduni hizi mbili zinazoathiri maghreb ya nyanda za juu na Sahara ya kaskazini, utamaduni wa Neolithiki haujitokezi mpaka baadaye kabisa.

Kipindi cha unyevunyevu cha Neolithiki kilimalizika katikati ya elfia ya tatu kama inavyodhihirishwa na tarehe za kinyeri cha ndege wa bahari kutoka Taessa (Atakor katika eneo la Hoggar). Kazi ya Arkell juu ya mabaki ya wanyama na mimea katika makao ya Mesolithiki na Neolithiki katika eneo la Khartoum inathibitisha uvumbuzi huu kuhusu bonde la Nili ya juu. Kutokea wakati huo Afrika kaskazini, ambayo ilikuwa kama imetengwa kabisa na sehemu nyingine za Afrika na jangwa, ilikuwa kisiwa kilichoweza kuwasiliana kwa urahisi na sehemu nyingine za Afrika kupitia njia wa Tripolitania.

Mnamo mwisho wa elfia ya tatu kabla ya enzi za Ukristo magae ya Gar Kahal yaliyo katika eneo la Scuta yanafanana na vifinyange vya Chalkolithi vya Los

Millares. Kwa hiyo lazima tukubali kwamba safari za baharini zilikuwapo na ambazo labda zitatupeleka nyuma hadi elfia ya nne.

Tangu mwaka wa -2000, pembe za ndovu na mayai ya mbuni viliingizwa Hispania, ilihali vyombo vya asili ya Kiiberia vilianza kuonekana katika sehemu za Seuta na Tetua. Kuelekea mwaka wa -1500, vigumba vya fedha na shaba vilianza kupatikana katika Afrika ya kaskazini, bila shaka viliingizwa huko kwa mara ya kwanza na wawindaji wa Kiiberia; lakini yaonekana kwamba havikuenea magharibi kupita eneo la Algiers. Kutokana na ukosefu wa bati, hakuna dalili zionyeshazo kwamba shaba nyeusi ilitumika Afrika kaskazini. Katika upande nwingine wa Afrika ya Kaskazini, kutoka Korba hadi Biserta mabainba ya volkano kutoka visiwa vya Lipari, ambayo yalitengenezwa huko Sisili na Pantellaria, yanatoa ushahidi wa mwanzo wa safari za meli katika mlango bahari wa Messina. G. Camps ametaja mambo mengi yaliyoigwa kutoka wakati huo na watu wa Afrika ya Kaskazini mashariki kutoka kwa jirani zao wa Ulaya. Makaburi ya mstatili yenye vijia vifupi na hori zenye pembe za mraba zilizochimbwa katika magenge yanayoitwa Honeti, yalikuwamo nchini Sisili kuanzia mwaka -1300. Majengo ya zamani ya mawe ya Algeria na Tunisia ni sawa na yale yanayopatikana kwa wingi katika Sardinia na Italia. Vifinyange vya Kastelusio ambavyo vilipatikana kwa wingi nchini Sisili katika miaka kabla ya -1500, pamoja na michoro ya rangi ya hudhurungi na nyeusi, iliyochorwa mahali pasipo na rangi ya kug'aa, ndivyo vilivyokuwa vyombo vya mwanzo vya udongo. Athari nyingine ya mbali kutoka Kupro na Asia Ndogo ilipitia Malta, Pantellaria na Sisili mara tu baada ya mabaharia wa Ejeni na baadaye Wafoeniki walipoanza kufika katika visiwa hivyo.

Uasili wa Afrika ya kaskazini, iliyoko kwenye mipaka ya bara hili, kutokana na akame wa Sahara na kuanzishwa kwa safari za majini, walitaji kusisitizwa. Hata hivyo si mawasiliano yote kati ya Afrika kaskazini na sehemu za ndani za Afrika yaliyovunjwa. Ingawa hali ya hewa ya Afrika kaskazini wakati huo ilikuwa kama ilivyo sasa, eneo linaloizunguka Sahara liliendelea kupata maji kwa muda mrefu na pia iliendelea kuwa na miti katika sehemu za vilima zilizokuwa na miamba-maji iliyokuwa karibu sana na ardhi. Miamba-maji hii ilifanya maji yaweze kupatikana kwa urahisi. Kwa hali hiyo farasi waliweza kutumiwa kusafiri katika Sahara. Huko Fezzan maji yalikuwa yakibubujika kutoka katika miamba-maji kwa muda mrefu sana. Twaweza kuchukulia kama ushahidi dhahiri wa asili ya umoja wa Afrika, kule kuwapo kwa mawasiliano hapo kale kati ya watu wenye ngozi nyeusi, ambao Wayunani waliwaita Waethiopia hapo baadaye kwa maana ya "wenye nyuso zilizoungua" na watu wa eneo la Libya na Berber, kwenye inaoasisi mengi ya Sahara, huko Fezzan na kwenye miterenko ya milima ya Atlas. Waliishi kwa amani wakijishughulisha sio tu na ukusanyaji wa vyakula na uwindaji bali pia katika kilimo kilichotekelezwa kwa kutumia njia za kale za kumwagilia maji mashambani.

Litakuwa kosa kufikiria kuwa Sahara yote ilikuwa ya Waethiopia katika enzi za Neolithiki na katika enzi za historia ya awali hata tukiwa waangalifu katika kufafanua

maana kamili ya Muethiopia yaani 'Mtu wa rangi' na kuepuka kumtaja kama Mnegro. M.C. Chamla amependekeza hivi karibuni kwamba inawezekana kuthibitisha kwamba thuluthi moja tu ya mifupa yote ya wakati huo ilikuwa ya watu weusi, ilihali zaidi ya asilimia 40 haina dalili za kingroidi. Kwa upande mwingine, masalia ya mtoto yaliyogunduliwa katika mwamba huko Akakus na kukadiriwa kuwa cha kipindi kati ya mwaka -3446 na -1800 yalikuwa ya kingegro. Katika makaburi ya Puniki, masalia ya kingroidi yalikuwa mengi na kulikuwepo na wasaidizi katika jeshi la Karithegi ambao bila shaka hawakuwa Wanailotiki. Walibya-Waberiberi (Wamaurin na Wanumidi katika sehemu za pwani na Wagetule katika sehemu tambarare) Wasahara weupe au machotara katika mipaka ya jangwa - kama vile Wafarusi, Wanigrite au Wagarainante, 'Waethiopia' waliotawanyika kutoka Sous hadi Jeridi, ndio waliokuwa watu wa Afrika ya kaskazini katika nyakati za safari za mwanzo za baharini za Wafoeniki na walibaki vivyo hivyo wakati huo wote wa kale.

Wazaa - Waberiberi na uhusiano wao na Wamisri na watu wa baharini

Kumbukumbu za kihistoria za Libya mnamo elfia ya pili kabla ya enzi za Ukristo zikiwa ni za maandishi au za vitu vilivyochongwa, zina asili za Kimisri na zinawahusu walibya waliokuwa na uhusiano na Misri na ambao waliweza kukaa kaskazini-magharibi ya delta kabla ya mwungano wa bonde la Nili.

Tokea enzi kabla ya ufalme, kuelekea katikati ya elfia ya nne, mpini wa kisu cha Jebel-El-Arak uliotengenezwa kwa pembe ya ndovu labda ulikuwa na sanamu ya Walibya wenye nywele ndefu wakiwa uchi isipokuwa tu mkanda ulioshikilia kipande cha kufunikia tupu. Hata hivyo jambo hili limepingwa na hatuwezi kuwa na uhakika na utambulisho wa Walibya katika usawiri kabla ya Wamisri kuwapa Walibya jina la kwanza, yaani Tehenou. Kama aliyoandika W. Hoscher, jina hili linaonekana katika kipande cha jiwe cha kuchanganyia rangi cha mfalme Scorpio na pia katika mcheduara wa pembe ya ndovu kutoka Hierakopolis kilichotunika wakati wa utawala wa Narmer (mnamo elfia ya tatu). Hiki kitu cha pili kinaonyesha nyara na wufungwa wa Farao. Lakini sanamu nakshi ya hekalu ya inatanga ya Sahoure (ya wakati wa ufalme wa kwanza yapata -2500) ndiyo inayotufahamisha juu ya inaumbo na mavazi ya Tehenou.

Watu hawa walikuwa warefu wenye inaumbo mazuri na midomo minene, ndevu ndefu na mtindo wa nywele ambao ulikuwa na nywele ndefu upande wa nyuma ya shingo. Shungi nyingine zikiningi'nia kwenye mabega na nyingine ndogo juu ya paji la uso. Walivaa tepe pana maalum kuzunguka mabega yao. Tepe hizo zilikutana kifuani. Pia walivaa mikufu yenye majebu yaliyoning'inia. Waliishi katika jangwa la Libya na maoasisi yake katika elfia ya tatu.

Watu wa Temehou wametajwa wakati wa ufalme wa sita, katika miaka iliyokaribia mwaka -2300. Hawa hawakuwa sehemu ya Watchenou, kama alivyofikiria C. Bates, bali walikuwa kabila jipya lililokuwa na ngozi zisizong'aa na macho ya samawati.

Wengi wao walikuwa na nywele nyororo. Imependekezwa kwamba walikuwa sawa na watu wa kundi C ambao walilowea katika Unubi wakati wa ufalme wa kati na mwanzoni mwa Ufalme Mpya. Fikra hii inaongezewa uzito mfanano kati ya vyombo vya udongo vya kundi hili na vile vilivyopatikana katika Wadi Howar, kilomita mia nne kusini-magharibi ya Poromoko la Tatu.

Mara nyini walitia manyoya katika nywele zao na wakati mwingine walikuwa na nembo. Silaha yao ilikuwa upinde, au wakati mwingine sime au gongo. Herodotus aliandika juu ya Walibya wa Syria ambao alisema walikuwa na tabia kama hizo katika karne ya tano.

Mashambulizi ya Watemehou yalikuwa ya kutisha zaidi wakati wa Ufalme wa kumi na tisa. Baada ya Seti I kuwarudisha nyuma mnamo mwaka wa -1317, Ramses wa pili aliwaingiza wanajeshi wa Kilibya katika jeshi la Misri na akaweka mstari wa ulinzi kando kando ya bahari ya Mediterani hadi kufikia El-Alamein. Mawe ya kaburi yaliyopatikana El-Alamein yathibitisha kwamba Ramses II alipateka mahali hapo na hicho ndicho kitu cha kwanza kinachotaja habari za Libou. Kutokana na jina la watu hao, Wayunani walipata Libya. Istilahi hii waliitumia kijografia kuita maeneo waliyokuwa wakiyatembelea lakini kidogo kidogo jina hili lilitumiwa kwa Afrika yote. Chini ya utawala wa Merneptah mnamo mwaka wa -1227, Meshwesh wanatajwa kwamba walikuwa majirani wa magharibi wa Libou. Libou na Meshwesh wanaonekana ndio waliounda kundi moja kubwa la Temehou. Baada ya kutwaa nuaosisi ya Bahari ya na Farafra, mwungano huo wa makabila ulishindwa na Wamisri kaskazini-magharibi ya Memphis.

Vita viwili vinavyojulikana sana baina ya Misri na Libya, vilitokea kati ya mwaka -1194 hadi -1188 wakati wa utawala wa Ramses III. Kumbukumbu zake zilinakiwa katika Mafunjo Makuu ya Harris na katika maandishi nakshi na sanamu kwenye hekalu la kaburi la Farao katika Medinat-Habou. Kwanza Walibou kisha Wameshwesh walitjaribu bila inafanikio kuwashinda nguvu Wamisri kwenye mto Nili lakini wote walishindwa.

Tokeo mojawapo ya ushindi wa Ramses III lilikuwa na umuhimu mkubwa, kwa kuwa aliweza baada ya hapo, kudhibiti maoasisi ya magharibi. Katika maoasisi haya hasa lile la Siwa, madhehebu ya Amon yalikuwa yakienea. Madhehebu hayo yakaenea polepole hadi kufika Tripolitania kwenye maeneo ya kuu; na katika kipindi cha Puniki yalikuwa na athari kubwa juu ya madhehebu yenye jina lenye kufanana ya Ba'al Ammon.

Huo ndio ushahidi wa mwanzo unaotueleza kuhusu Walibya katika sehemu ya mashariki kabisa ya eneo lao kubwa la nakazi. Yafaa kuzingatia kwamba Watu wa Baharini kwa upande wao, wanatajwa tu mara moja katika maandishi nakshi yaliyoko Karnak kuwa walikuwa wakiwasiliana mara kwa mara na Walibya wakati wa utawala wa Mernepta mwaka -1227. Na yaelekea maandishi nakshi haya yalikuwa matokeo ya mashambulizi kadhaa. Lakini hata tukikubali kwamba kulikuwako kikosi cha Watu wa baharini miongoni mwa Walibya, je twaweza kusema kwamba hao ndio watu

waliowafundisha Walibya kutumia magari ya farasi, kwanza nchini Misri na baadaye kote katika Sahara?

Pendekezo hili linaungwa mkono na baadhi ya mabingwa wa mambo ya Sahara, ingawa kuna mifanano michache kati ya picha za magari ya farasi ya huko Efeani na Sahara inavyoonyeshwa pia na mwanakiolojia wa zama za kale kama G. Charles-Picard na bingwa wa mambo ya farasi kama J. Sprutte. Magari haya ya Farasi ya Sahara yanaonekana kama alivyoyachora inpanda-farasi na wala sio kama yalishuhudiwa. Jukwaa la magari hayo halikuinuliwa na linakaa katikati ya ekseki ya mbali na magurudumu yenyewe na hivyo kutoa nafasi kwa abiria tu ambaye kwa kawaida ndiye mwendeshaji na ambaye hushika aina ya mjeledi mfupi na wala sio silaha. Farasi hawa, wengi wakiwa ni wa aina ya Barbary, Iijamu zake zilikuwa nira za ukosini na wala hazikuwekwa shingoni. Ijapokuwa wanaonyeshwa kama wanakwenda shoti, magoti yao hayaonekani. Katika hati za ejeani, msimamo wa farasi kama huo wa pichani huwa siyo farasi waliotiwa Iijamu wanavyosimama. Kwa hivyo magari haya ya farasi ya Sahara yaonekana kuwa ni magari hafifu ya michezo.

Kwa hivyo labda tungetofautisha magari ya Sahara na magari mengine ya kivita yaliyotambuliwa miongoni mwa maadui wa Ramses III na baadaye Wagaramenti (Magari ya farasi wanne), Waaribita, Wazoosi, Walibya walipokuwa katika utumishi wa Agathocles, jirani ya Kariteji, Waferusia na Wanigreti. Badala ya kuchukulia kwamba waliyaazima magari hayo kutoka kwa Watu wa Baharini, tutakuwa tumekaribia ukweli tukikubaliana na W. Holcher kwamba Walibya waliyaazima magari haya kutoka kwa Wamisri ambao walikuwa wameyatumia tangu uvamizi wa Haiksos mnaino karne nne au tano kabla. Chanzo cha magari haya ya Sahara kingali hakijulikani. Magari hayo yalitengenezwa kwa mbao tupu. Usanifu wake ulikuwa rahisi sana na huenda yalitengenezwa kulingana na ufundi wa mwanzo. Zaidi ya hayo farasi wa aina ya Barbary (au Mongol) waliokuwa na kinuo kidogo wenye uso wa mviringo, infupa wa mgongo uliokuwa wazi ndani na wenye vipande vitano vya mifupa na sehemu za nyuma za inwili wake zilizoteremka, haiwezekani kusema walitokana na mbegu ya Farasi wa Kiarabu na wa nchi za mashariki ambao walikuwa na maumbo inazuri na walioendesha na waikso na Waejeani. Labda walienea kutoka Afrika mashariki na Sudani, lakini huku ni kudhanja tu. Twaweza kuona kwamba katika sanamu za Sahara zilizochongwa na mwamba, na zile zilizochongwa wakati wa enzi ya Warumi, picha za farasi wa kiarabu na Kiasia ni haba sana ijapokuwa zilikuwapo. Hata kama tukidhani kwamba katika hali hii hatukabiliwi na tatizo la kuingiza dhana ngeni katika Afrika, ukweli unabakia kwamba hadi kuwasili kwa Waarabu, farasi wa Kibarbari ndio waliokuwa wengi katika Afrika Kaskazini.

Maisha ya Waberiberi kabla ya Kuanzishwa kwa Kariteji

Kama H. Basset na G. Camps, wanavyoeleza kwa usahihi Waberiberi wa Libya hawakufundishwa kilimo na Wafoeniki, bali walikuwa wakulima tangu mwisho wa enzi za Neolithiki. Nakshi na michoro ya 'enzi ya chuma' inaonyesha plau kwa

mchoro tu huko La Cheffia (jimbo la Konstantini mashariki) na katika milima ya Atlas, magharibi ya Tebessa, katika jimbo la Douar Tazbent. Kifani cha miraba ndiyo mabaki yaliyoko sasa ya mitambo ya maji iliyotumiwa mwanzo ambayo ni ya kipindi cha mapema zaidi kuliko enzi ya falme za kikabila. Watumiaji wa mitambo hii walikuwa na vifaa ambavyo baadhi ya sehemu zake zilitengenezwa kwa mawe.

Kwa muda mrefu walikuwa wamekwishazoea kutia lijamu mafahali. Hayo yanaonyeshwa katika mchoro ya Kimisri na maandishi katika milima ya Atlas. Kwa upande mwingine wanaonekana hawakujua mbinu ya kupukuchua mazao yao kwa mitambo kabla ya wakati wa Puniki (15) na walitosheka tu na nafaka yao kupondwa kwa kukanyagwa na ngo'mbe wazito.


Wataalamu wa elimu ya mimea wameonyesha kwamba ngano nguunu (labda iliyoletwa kutoka Abbyssinia) na shayiri vilipandwa Afrika kaskazini muda mrefu kabla ya kuwasili kwa Wafoeniki. Maharagwe ma njegere pia zilifika wakati huohuo ijapokuwa kwa Kiberiberi njegere huitwa *Ikiker*, neno lililotokana na jina la Kilatini la *cicer*.

Utafiti wa kiakiolojia katika minara ya makaburi unathibitisha kuwapo kwa makundi makubwa yaliyokuwa yakiendesha kilimo katika Afrika ya Kaskazini.

Samani ya makaburini huthibitishwa kama ilivyodhihirishwa na G. Camps kwamba Waberiberi walikuwa na utamaduni wa kale sana katika sehemu za vijijini. Twaweza kukubaliana na mtaalamu huyu kwamba ramani inayoonyesha kuenea kwa makaburi ya historia ya awali yenye vifinyange itatupatia habari sahihi juu ya kuenea kwa kilimo kijiografia. Uchunguzi wa umbo la vifinyange hivyo umemwezesha G. Camps kudokea juu ya maisha ya Waberiberi wa Libya wakati huo. Aina hiyo inafanana sana na vifinyange vya siku hizi: bakuli, beseni na makopo ya kuwekka vitu vilowevu na mchuzi wa nyama, sahani na madishi kama yale yanayotumiwa kuokea mikate na keki siku hizi.

Aina ya sahani ya matunda yenye kitako kama shina la mti pia ilipatikana tokea nyakati za historia ya awali hadi sasa. Machimbo yaonyesha kwamba tokea nyakati za mwanzo, Waberiberi walikuwa wakivining'iniza vyombo vya vya kulia chakula kwenye ukuta. Kwa upande mwingine, siku hizi hakuna vyungu vya kuchujia vinavyoweza kulinganishwa na vya zamani. C. camps alijiuliza iwapo vyungu hivyo vilitumiwa kwa kuchujia asali au kwa kutayarisha madawa.

Wanaakiolojia pia wamethibitisha kwamba wahamaji waliokuwa wakikaa sehemu za kusini walibeba silaha zilizopambwa na kuvaa bangili, vipuli au shanga za udongo na metali zaidi kuliko wenyeji wakazi wa sehemu hiyo. Vipande vya nguo vyaonyesha kwamba nguo zenye misitari zilikuwa zikitumiwa. Maandishi kwenye miamba yaliyopatikana karibu na Sigus yalidhihirisha kwamba zamani sana kulikuwapo na juba ambayo labda ndiyo chanzo cha hekaya kuhusu watu ambao hawakuwa na vichwa au watu waliokuwa na nyuso zao vifuani mwao. Ni dhahiri pia kuwa mavazi kama hayo yalivaliwa na Wablemi wa jangwa la Bara Arabuni kwenye mipaka ya Misri ya Juu.



17.1 Kushoto. Jiwe la kaburi la Libya kutoka Abiza (Kusini-mashariki ya Tizirt).

Chanzo muhimu cha utajiri wa wahamaji hao kilikuwa ufugaji wa kondoo, mbuzi, na ng'ombe. Mchoro uonyeshao mtu akikamua maziwa umepatikana Jerif Torba, magharibi ya Koloinbo Bechar katika eneo ambalo sasa halina kitu. Kwa mujibu wa Ellien (NA, VII. 10.1) wahamaji hao hawakuwa na watumwa, lakini badala yake walitumia mbwa. Maoni kama hayo yametolewa kuhusu wakazi wa mapangoni wa zamani wa Bahari ya Sham na Waethiopia waliokaa katika vinamasi vya Mto Nili. Uwindaji ilikuwa shughuli ya kawaida, na Ptolemy anawataja wawindaji wa Oreipase waliotoka kusini mwa Tunisia karibu na mpaka wa Ethiopia ambao walikuwa majirani wa Waethiopia wa Naibgenite waliokuwa wakitangatanga sehemu za kusini ya Djerid.


Tunajua machache sana kuhusu mfumo wa kijamii wa Waberiberi wa Libya katika nyakati zilizotangulia zile zilizoelezwa katika maandishi ya kale hasa ikiwa tutapuuza juhudi zinazofanywa mara kwa mara inara kueleza jinsi hali ya niambo ilivyokuwa kutokana na ushahidi uliopatikana baadaye. Ukubwa wa kupendeza wa vilima vya Rharb katika Moroko au kaburi la Medracen katika jimbo la Konstantini unaonyesha kwanba zile sehemu za magharibi na inashariki za Maghreb ambazo hazikuwa zikitawaliwa na wafalme wa Kariteji zilijitokeza tangu karne ya nne. Mengine zaidi hayawezi kusemwa kwa kuwa yale yote ya kuvutia kuhusu mfumo wa kijamii wa Libya ambayo yameandikwa na mtakatifu Gsell, yalitokana na hati za Kirumi za enzi ya kifalme na pia kutokana na ushahidi wa mshairi Koruppus ambaye alikuwa rika la Justimian.

Imani za Kidini za Waberiberi wa Libya

Ni vigumu kufahamu vizuri imani za kidini za Waberiberi wa Libya kabla ya athari ya Wafoeniki wa Puniki na baadaye ile ya Warumi. Akiolojia ya historia ya awali haitusaidii zaidi ya kutudokezea juu ya ibada zao ambazo hata kwa wakati huo, huko Afrika ya Kaskazini, zinahusu ibada za mazishi tu.

Miongoni mwa Walibya, fikra ya utakatifu inaelekea kuwa ilidhihirishwa katika vitu vingi sana. Mara nyingi ilifikiriwa kwamba ruhani ilikuwepo katika eneo lilowazunguka. Kwa hiyo maandishi nakshi ya nyakati za Kirumi yanaonyesha kuwa majini wa maji au wale wa milima waliabudiwa. Watu hao waliani kwamba uwezo wa kiroho ulikuwepo katika vitu vya kawaida. Mawe ya mviringo au yenye ncha, kama kokoto na mbwe zenye sura ya uso wa binadamu au sanamu ya uume, vilikuwa vikiabudiwa.

Kwa kawaida wanyama waliokuwa ishara ya uwezo wa kuzaa- fahali, simba, na kondoo dume-ndio walioheshimiwa na Walibya. Athanasius (*Contra Gentes*, 24) anatueleza kwamba kondoo dume alifikiriwa kuwa mungu wa Walibya ambaye walimwita Amon. Yatubidi tutaje madhehebu yaliyomwabudu samaki ambayo yalika katika eneo ambalo sasa ni Tunisia. Kwa kiasi fulani hii inafafatua kuwepo kwa picha nyingi za samaki zilizoonekana katika michoro ya picha za rangi za Tunisia. Samaki ambaye ni ishara ya uume, alikuwa kinga dhidi ya kuonewa kijicho. Samaki



17.2 *Kulia. Simba kutoka Khor Roumii*

mwenye umbo la uume akijamiiana na samaki wawili wa kike yaonyeshwa katika michoro ya picha za rangi zilizoko Susa. Pamoja na samaki huyo, kome zilitumiwa sana kama ishara ya wanawake katika Afrika ya kaskazini nzima. Ilitumiwa kama hirizi kwa walio hai na kuwatuliza wafu makaburini mwao.

Dhabihu kwa heshima ya wafu zilifanywa mbele ya makaburi yao katika eneo lililotengwa ambalo lipo kabili na jua linapochomozea. Wakati nwingine nguvu muhimu za mfu zilionyeshwa kwa mnara mrefu wa mawe wenye pande nne au jiwe la kaburi. Herodotus (IV, 172) anaeleza kwamba Wanasamonia walikuwa wakiomba ushauri kutoka kwa babu zao kuhusu siku za baadaye kwa kulala kwenye makaburi yao. G. Camps anaamini kwamba kanuni hii ndiyo sababu ya kuwepo kwa Bazina na Tumuli zenye umbo la jukwaa, lakini minara ya kumbukumbu ya Sahara iliyokuwa pamoja na kanisa dogo na chumba, kinaelekea kuambatana vizuri zaidi na desturi hii. Pengine desturi hii ilienea sana miongoni mwa watu wa Sahara kwa kuwa walishangazwa na ukweli kwamba Waatlante (Herodotus IV, 184) kamwe hawakuwa na njozi katika usingizi wao.

Haelekei kuwa Walibya waliabudu miungu wenye maumbo kama ya binadamu. Kwa mujibu wa Herodotus (IV, 188) walitoa sadaka kwa jua na inwenzi. Hata hivyo wale wa eneo la Djerid walikuwa na mazoea ya kutoa dhabihu kwa Athena, Triton na Poseidon, ambapo Waatarantia (IV, 184) majirani wa Wagaramante kwa upande wa magharibi, walililaani jua. Cicero anaeleza kwamba (Rep., VI, 4) Wamasinisa walitoa shukrani kwa jua na miungu wengine wa mbinguni. Jua liliendelea kuabudiwa katika miji kadha ya Afrika iliyokuwa chini ya utawala wa Kirumi kama Makta, Althiburos, Thugga, na Sufetula, lakini athari ya Puniki huenda ilionekana hapa na pale.

Mbali ya viumbe hivi viwili vya mbinguni, kumbukumbu za mashairi na maandishi zinaonyesha kuwapo kwa miungu wengi ambao mara nyingi walitajwa mara moja tu na wakati mwingine hutajwa kwa pamoja kwa mfano, Dii Mauri. Sanamu iliyopatikana karibu na Baja inaonyesha aina ya jamii ya miungu saba. Lakini hii inaonyesha aina ya dini yenye kuamini miungu wengi walioingizwa kutokana na ushawishi wa Kipuniki. Ushawishi huu uliwafanya Walibya kuufanya uwezo huo wa kimungu uwe wa kibinafi. Wakiachwa peke yao, Walibya walikuwa wakivutiwa zaidi na vyombo vitakatifu kuliko miungu.

18

Kipindi cha Wakariteji

Historia ya Maghreb ilianza kuandikwa baada ya mabaharia na walowezi kutoka Ufoeniki kufika katika pwani zake. Kuandikwa upya kwa historia ya wakati huu kunatatiza kwa sababu karibu kumbukumbu zote za historia yake ni za Kiyunani na Kirumi, na kwa mataifa haya mawili Wafoeniki wa magharibi hasa wale waliokuwa chini ya uongozi wa Kariteji, walikuwa maadui wakubwa. Kutokana na haya, habari zinazopatikana kutokana na kumbukumbu hizo ni za uadui. Hakuna maandishi ya Kikariteji yaliyoko wakati huu. Habari zilizotokana na akiolojia pia nazo ni haba kwa kuwa miji mikubwa ya Kirumi ilijengwa kwenye maeneo yale yale yaliyokuwa na makazi mengi ya Wafoeniki hapo awali. Hata hivyo mnamo miaka ishirini iliyopita, maendeleo fulani ya kiakiolojia yamepatikana. Kustawi kwa utamaduni wa asili wa Kilibya kabla ya karne ya tatu pia nako si dhahiri. Maelezo ya kiakiolojia ya elfia ya kwanza yanaonyesha mfululizo wa mabadiliko ya pole pole, lakini ushawishi wa Wafoeniki ulianza kusikika zaidi innamo karne ya nne. Kuenea kwa makaburi yaliyojengwa kwa mawe hakuonyeshi kuhusiana na utamaduni wa zamani wa kujenga nyumba kwa mawe makubwa kama ilivyokuwa kawaida ya watu wa Ulaya kaskazini. Makaburi makubwa mno kama yale ya vichuguu vya Mzora na Medrasen, huenda yanahusiana na kuongezeka kwa makundi makubwa ya kikabila katika karne ya nne au ya tatu. Waandishi wa Kiyunani na Kirumi hutaja idadi kubwa ya makabila tofauti. Lakini katika kipindi hiki, wakazi wa Maghreb wasio Wafoeniki waligawanywa katika makundi matatu. Kwa upande wa Magharibi, kati ya Atlantiki na Muluka (Moulouya) walikuwepo Wamauri. Jina la Mauretania ambalo zamani lilikuwa Maurousia, lilipewa eneo hilo. Lakini baadaye jina hilo lilituniwa kuita sehemu kubwa zaidi ya mashariki hadi Chelif. Kati ya Mauri na sehemu za magharibi za eneo la bara la Wakariteji, walikuwepo Wanumidi ambao nchi yao iliitwa Unumidi. Kundi la tatu lilikuwa Wagetuli, jina lililopewa wahamaji halisi kwenye mipaka ya kaskazini ya Sahara. Majina haya ya kale kwa vikundi hivi na kwa kila kabila yametumiwa katika sura yote hii.

Makazi ya Mwanzo ya Wafoeniki

Tiro na miji mingine ya Wafoeniki (katua Sidon na Biblus) kuanzia mwaka wa -1000

ilikuwa miji mashuhuri sana kwa biashara, katika pwani ya mashariki ya Bahari ya Mediterani bila kuingiliwa na ukuaji wa dola ya Assyria. Wafanyabiashara wa Kifoeniki walikwenda magharibi mwa Bahari ya Mediterani, kutafuta chuma na hasa dhahabu, fedha, shaba na bati. Hii iliwafikisha mapema sana katika Uhispania ambayo iliendelea kuwa mashuhuri kwa utoaji wa fedha katika sehemu hizi hata wakati wa Warumi. Uwezo wao pia uliongezeka kutokana na biashara hii, iliyoendeshwa kwa muda nrefu, na waliweza kuwatuma mawakala wengi wa kuanzisha makoloni huko Sisili na katika visiwa jirani, Afrika, Sardinia na Uhispania kwenyewe. Kwa kawaida makazi ya mwanzo ya Wafoeniki huko magharibi yalikuwa mahali ulipo mji wa Kadiz leo hii. Jina Kadiz lilitokana na Kifoeniki *Gadir*- yaani ngoine, labda kwa sababu mwanzoni kilikuwa kituo cha biashara. Wafoeniki walitumia njia ya kaskazini iliyopita kwenye pwani za kusini ya visiwa vya Sisili Sardinia na Balcariki, na njia nyingine ya kusini iliyopitia kando kando ya pwani ya Afrika kaskazini. Kwenye njia hiyo ya mwisho, imekisiwa kulikuwako na bandari kila baada ya maili thelathini hivi zilizotumiwa na Wafoeniki. Hata hivyo kukua kwa bandari kuwa makazi ya kudumu kulitegemea mambo kadhaa. Sehemu nzuri zilizopendwa enzi hizo ni visiwa vilivyokuwako mbali na pwani, au rasi zenye mahali pazuri pa kutia nanga kila upande. Aidha, uwezekano wa mahali kutumiwa kwa mbinu fulani ulipafanya paendeleo zaidi ya pengine. Umuhimu wa miji hii mitatu - Kariteji na Utika (Utique) katika Afrika kaskazini na Motya (Mozia) katika Sisili hutokana na kuwapo kwake mahali pazuri kwenye sehemu nyembamba kutokea mashariki hadi magharibi mwa bahari ya Mediterani na hutawala njia za kusini na magharibi.

Kuanzishwa kwa Kariteji

Jina la 'Kariteji' (Kilatini: *Certhegio*) linatokana na neno la Kifoeniki 'kart Hardasht' lenye maana ya 'Mji Mpya.' Hii yaweza kumaanisha kwamba mahali hapo penyewe, tokea mwanzo palinuiwa kuwa makazi muhimu ya Wafoeniki katika sehemu ya Magharibi, lakini tunajua machache sana kuhusu akiolojia yake kuweza kuthibitisha jambo hili. Kuanzishwa kwa Kariteji kulifanyika mwaka -814, muda mrefu baada ya kuanzishwa kwa Kadiz (-1110) na Utika (-1101). Tarehe hizi zote zimehakikishwa na nyaraka mbalimbali. Kwa tarehe ya Kariteji, ushahidi wa kiakiolojia ambao haujazua upinzani ni wa vitu vya katikati ya karne ya nane kabla ya enzi zetu. Hakuna taarifa ya kihistoria yenye uzito iwezayo kutolewa kutokana na masimulizi tuliyoachiwa kwa njia mbalimbali na waandishi wa Kiyunani na Kirumi kuhusu makazi hayo. Vitu ambavyo vilikuwa takribani vya wakati mmoja vilitoka Utika, na vya karne ya saba au sita vilitoka Leptis Magna (Lebda), Hadrametum (Sousse), Tipasa, Siga, Likasa na Mogador mji uliokuwa makazi ya mbali zaidi ya Wafoeniki yanayojulikana. Vitu vya kale vyenye umri kama huo vilipatikana Motya huko Sisili Nora (Nuri), sulsos na Tharros (Mnara wa Mtakatifu Giovanni) katika Sardinia na Kadiz na Alumunekar katika Uhispania. Lazima isisitizwe kwamba tofauti na makazi ambayo wayunani

waliyaanzisha Sisili Italia na kwingineko mnamo karne ya nane na saba, makazi yote ya Wafoeniki yakiweino Kariteji yenyewe, yaliendelea kuwa mahali padogo penye walowezi wasiozidi mia kadha, kwa vizazi vingi. Aidha, kisiasa walibakia chini ya Tiro kwa muda mrefu kama ilivyotazamiwa, kwa kuwa shughuli zao muhimu zilikuwa kutoa nafasi za kutia nanga na kununua bidhaa.

Uongozi wa Kariteji kwa Wafoeniki wa Magharibi

Kuibuka kwa Kariteji kama jiji huru, kulikofuatiwa na uongozi wake wa Wafoeniki wote wa Magharibi, na kuundwa kwa himaya yenye makao yake Afrika Kaskazini, iliyokuwa na inatokeo muhimu ya kihistoria kwa eneo lote la magharibi mwa Mediterani, kulianza mnamo karne ya sita kabla ya enzi zetu. Mnamo karne ya saba yaonekana hakukuwepo na migogoro mikubwa baina ya Wafoeniki na Wayunani, na kuna vitu vingi vya Kiyunani vilivyoonekana katika makazi mengi ya Wafoeniki ya Maghareb. Lakini mnamo mwaka -580, wakazi wa inji wa Selinus (Selinunte) pamoja na Wayunani wengine wa Sisili, walijaribu kuwafukuza Wafoeniki kutoka katika makazi yao ya Motya na Palermo. Kariteji yaelekea ndiyo iliyoongoza kupinga shambulio hilo ambalo kama lingalifaulu, lingaliwafanya Wayunani wawe tishio kwa inakazi ya Wafoeniki ya Sardinia na kuanzisha biashara na Uhispania ambayo hadi kufikia wakati huo walikuwa hawashiriki. Kufuatia mafanikio haya, makazi ya Wafoeniki ya Sardinia yaliimarishwa. Ushindi wa mwisho katika kipindi hiki ulikuwa katika Afrika yenyewe. Msparita inmoja (Myunani) aliyeitwa Dorieus alijaribu kuanzisha inakazi kwenye mlango wa mto Kinyps (Oued Oukirri) ulioko Libya. Kariteji iliichukulia hatua hiyo kuwa ya kuingilia mambo yao, na katika miaka mitatu, iliweza kuwafukuza Wayunani hawa, ikisaidiwa na wazalendo wa Libya.

Inaelekea kuwa wajibu wa kuwaongoza Wafoeniki wa magharibi uliuzidi uwezo uongozi uliokuwepo Kariteji. Hadi kufikia karne ya sita, waliwategemea raia wao wenyewe. Mnamo katikati ya karne ya sita sera ya kuwatumia mamluki kwa wingi, ilianzishwa na uongozi wa Mago. Sera hii ilifuatwa kwa muda wote uliobaki wa historia ya Kariteji. Baadhi kubwa ya mamluki hao walikuwa Walibya. Hawa walitumiwa sana kama askari wa nchi kavu. Jeshi la Wakariteji lilikuwa pia na Wanumidi na Wamauritania kutoka sehemu za kaskazini za nchi zijulikanazo leo hii kama Algeria na Moroko. Hawa walikodishwa kama mamluki mwanzoni, lakini baadaye walijaribiwa chini ya inikataba ya ushirikiano. Watu wengine waliohudumia jeshi la Wakariteji nyakati fulani fulani kama inamluki walikuwa Wahispania, Wagaul, Wataliani na Wayunani.

Kizazi kilichofuata baada ya ushindi dhidi ya Dorieus kilishuhudia mabadiliko makubwa katika miji ya Kiyunani ya Sisili ambayo iliipinga vikali Kariteji. Gelon, mtawala wa Gela ambaye kuanzia mwaka -485 alitawala pia Sairakuse alianzisha vita vya kulipiza kisasi kushindwa kwa Dorieus na akapanga kutwaa eneo la inakazi ya Wafoeniki karibu na ghuba ya Gabes. Kutokana na hayo, Kariteji ilianzisha urafiki na baadhi ya wakazi wa Sisili walioimpinga Gelon. Na mnamo mwaka -480, Kariteji

iliingiza jeshi kubwa la mamluki kisiwani humo. Labda Kariteji ilichukua fursa hiyo kwa sababu mnamo mwaka huo huo Uyunani ilikuwa imeshambuliwa na Uajemi. Wakati huo Kariteji ilikuwa na meli mia mbili za kivita, idadi iliyoifanya iwe na nguvu sawa na Sairakuse na knpitwa kidogo tu na Afini. Hata hivyo hatua hiyo iliishia kuwa maangamizi makubwa kwani jeshi lote na meli zote ziliharihiwa katika vita kubwa vilivyopiganwa Himera. Gelon hakuweza au hakutaka kuendeleza ushindi huo na hivyo akaruhusu kuwepo kwa amani kwa kulipwa fidia ndogo.

Upamuzi Kaskazini mwa Afrika

Kushindwa huko kulifuatiwa na miaka sabini ya amani wakati ambapo Kariteji iliepuka ugomvi na Wayunani lakini iliweza kuendelea kuhodhi biashara yote iliyokuwa ikiimiliki. Cha muhimu zaidi ni kuwa Kariteji ilianza kujipatia ardhi katika Afrika yenyewe. Badiliko hili lilitokea wakati Kariteji ilipokuwa inaendelea kutengwa kutokana na ushindi wa Wayunani katika sehemu nyingine, kwanza dhidi ya Waajemi ambapo Wafoeniki walishiudwa vibaya, na pili dhidi ya Waetrusi katika Italia. Sera hii mpya inahusiana na ukoo wa Magonid, ambao wakati huo uliongozwa ua Hanno, mwana wa Hamilicar ambaye alikuwa ameshidhwa katika vita vya Himera. Mwandishi mmoja wa Kiyunani Dio Chrysotom amemweleza Hanno kuwa ndiye aliyewageuza Wakariteji kuwa Waafrika badala ya kuwa Watiro.

Ingawa eneo la ardhi lililotekwa mnamo karne ya tano, na idadi ya makazi yaliyokua na kuwa miji midogo haijulikani kwa hakika, ni dhahiri eneo hili lilifikia kiwango kikubwa kabisa ambacho Kariteji ilipata kudhibiti. Muhimu zaidi ilikuwa ni kutekwa kwa musoma ya Cap Bon na eneo kubwa la ardhi kusini mwa Kariteji hadi kufikia Dougga. Hii ilikuwa pamoja na sehemu zenye rutuba nyingi za Tunisia, eneo lililokuwa na makazi mengi ya baadaye ya Kirumi. Eneo hilo lilikuwa na chakula muhimu kilichohitajika na lilitoa nafasi ya kuwapo kwa watu wengi zaidi katika mji. Wakariteji wengine baadaye walikuwa na mashamba huko Cap Bon. Ardhi katika eneo hili ilihesabiwa kama ardhi ya mji na wenyeji wa hapo yaonekana walifanywa manokoa. Wenyeji wa sehemu nyingine zilizotekwa walilazimishwa kulipa ushuru na kutoa askari. Idadi ya makazi ya Wafoeniki katika pwani iliongezeka baada ya wahamiaji wengine kuingia toka Kariteji yenyewe. Makazi hayo yalikuwa madogo ambamo mamia kadhaa ya watu waliishi na kufanya biashara na makabila ya wenyeji. Kwa Wayunani makazi hayo yalijulikana kama magulio.

Mpaka kati ya milki ya Kariteji na koloni la Wayunani la Sairenaika ulikuwa kwenye ghuba ya Sidra, lakini makazi yaliyokuwa pwani ya Libya yalikuwa machache. Makazi yaliyokuwa muhimu ni yale ya Lepsis ambayo yawezekana palifanywa makazi ya kudumu wakati safari ya Dorieus hadi karibu hapo, ilionyesha kulikuwapo ua hatari ya uvamizi wa Wayunani. Sabratha, ilikaliwa kuanzia karne ya nne. Lepsis ilikuwa makao makuu ya utawala kwa makazi yaliyokuwapo karibu na ghuba ya Gabes na panajulikana kuwa palikuwa uahali penye utajiri mwishoni mwa kipindi cha Wakariteji, na utamaduni wake wa Kifoeniki uliendelea kushamiri hapo

kwa zaidi ya karne moja chini ya utawala wa Kirumi. Utajiri huo ulitokana na biashara iliyofanywa kupitia Sahara, kwa kuwa eneo hilo lilikuwa mwisho wa njia fupi iliyopitia Sidamus (Ghadames) hadi Niger. Hata hivyo hatujui ni bidhaa zipi zilizokuwa zikiuzwa, isipokuwa kwamba mawe yenye thamani kidogo yametajwa. Utajiri kutokana na kilimo katika eneo hilo wakati wa Kirumi ulitokana na walowezi wa Kikariteji. Lepsis na Hadrumetum zilianzishwa na Ufoeniki na wala sio na Kariteji, na Hadrumetum baadaye ilikua na kuwa mji mkubwa zaidi katika pwani ya mashariki ya Tunisia. Kutoka Neopolis (Nabeul) kulikuwapo na barabara iliyotoka Cap Bon hadi Kariteji. Magharibi ya Kariteji ulikuwepo mji wa Utika ambao ulikuwa wa pili kwa umuhimu kwa Kariteji, na kama ilivyokuwa Kariteji, ulikuwa bandari, ingawa sasa iko maili saba kutoka pwani.

Himaya ya Kariteji

Kariteji ililaumiwa na maadui wake kwa kuwadhulumu na kuwanyonya raia wake; na bila shaka kulikuwepo na aina kadhaa za watu nuongoni mwa watawaliwa hao. Wale ambao walinufaika zaidi walikuwa wale waliokuwa katika makazi ya Wafoeniki na katika makazi yaliyoanzishwa na Kariteji yenyewe ambao Wayuani waliwaita wakazi wake Walibya-Wafoeniki. Inaelekea kuwa walikuwa na maafisa na taasisi sawa na Kariteji kwenyewe. Waliwajibika kulipa ushuru kwa bidhaa walizoingiza kutoka nje au bidhaa walizouza nje na wakati mwingine wanajeshi walichangishwa kutoka kwao. Baada ya mwaka -348, yaonekana walikatazwa kufanya biashara na watu wengine wowote isipokuwa Wakariteji. Hali ya watu wa Sisili waliokuwa wakitawaliwa na Kariteji ilikuwa tofauti kutokana na kuwepo kwao karibu na miji ya Kiyunani. Waliruhusiwa kuwa na taasisi zao wenyewe na kuwa na sarafu zao kwa muda wote wa karne ya tano, muda ambao Kariteji yenyewe haikuwa na sarafu. Biashara zao zaonekana kuwa hazikuwa na vikwazo kulingana na utaratibu wa Kirumi, ambapo Sisili ilipotekwa na Warumi, kiasi cha moja kwa kumi ya mazao kilitozwa. Walibya waliokaa sehemu za ndani yaonekana ndio waliogandamizwa zaidi ingawa miundo yao ya kikabila yaelekea iliruhusiwa kuendelea. Iuaelekea kwamba maafisa wa Kikariteji ndio walisimamia moja kwa moja, ukusanyaji wa ushuru na kuandikishwa kwa askari. Kiasi cha kawaida cha ushuru huo chaonekana kilikuwa robo ya mazao na mnamo wakati wa vita vya kwanza dhidi ya Warumi asilimia hamsini ilichukuliwa kama ushuru.

Biashara na Uvumbuzi wa Kariteji

Afrika Magharibi

Kwa jumla kulikuwa na kukubaliana miongoni mwa Warumi na Wayunani kwanba Kariteji ilitegemea zaidi biashara kuliko mji mwingine, na kila walipomfikiria Mkariteji halisi, walimfikiria kama mfanyabiashara. Aidha iliaminika kwamba Kariteji ulikuwa mji tajiri zaidi katika eneo la Mediterani. Hata hivyo lazima

isisitizwe kwamba biashara hiyo ya utajiri unaodaiwa haukuacha masalia yoyote kwa wanaakiolojia kama yale ya miji mingine mikubwa ya Kiyunani na Kitruskan ya wakati huo huo. Bila shaka sababu moja iliyofanya hali hiyo ni kwamba biashara zake nyingi zilikuwa za bidhaa ambazo hazikuacha mabaki, hasa vyuma ambavyo havikuwa vimesanwa. Bidhaa muhimu katika safari za upelelezi za Wafoeniki zilikuwa nguo, watumwa na chakula kilichotoka kwenye eneo kubwa la ardhi yake lililolimwa. Faida iliyotokana na biashara kati ya makabila mbalimbali yaliyowauzia dhahabu, fedha, bati, na pengine chuma kwa kubadilishana na vitu rahisi, inadhihirishwa na ukubwa wa jeshi la mamluki waliokuwa nao innamo karne ya tatu na ya nne na utengenezaji wa sarafu za dhahabu kwa wingi hata kufikia kiwango cha kushindana na zile za miji iliyostawi.

Uongozi shupavu katika nchi hiyo kwenye shughuli za biashara waonyeshwa katika kumbukumbu zetu, hasa zile zihusianazo na Afrika magharibi. Kwa mujibu wa Herodotus (karne ya -5), mfalme Necho wa Misri (c. -610 hadi -594) aliwatuua mabaharia wa Kifoeniki waizunguke Afrika kuanzia bahari ya Sham. Inasemekana kuwa walisafiri kwa miaka miwili, njiani walisimama mara mbili ambapo walipanda na kuvuna ngano. Herodotus aliamini kwamba safari hiyo ilifaulu na ilikuwa hatua iliyowezekana, lakini haikuzusha ubishi wowote wakati huo. Kaina safari hiyo iliwezekana, basi ukubwa wa bara hili uliogunduliwa wakati wa safari hiyo, uliondoa mawazo yoyote ya kuwepo kwa njia ya kutoka bahari ya Sham hadi Mediterani. Wakariteji ambao, kwa mujibu wa Herodotus, waliamini kwanba Afrika iliweza kuzungukwa wakati huo, lazima walijua safari hiyo na nyingine iliyofanywa mapema mnamo karne ya tano. Mwana mfalme wa Uajemi alinunua meli kutoka Misri kwa lengo la kujaribu kufanya safari ya kuizunguka Afrika kupitia upande wa magharibi. Inaonekana kuwa alipita pwani ya Moroko, umbali mrefu kutoka rasi ya Spartel lakini alilazimika kurudi. Herodotus pia anatoa maelezo kuhusu biashara ya Kikariteji kwenye pwani ya Moroko. Hayo ndiyo maelezo ya zamani zaidi kuhusu biashara ya kubadilishana bidhaa kimyakimya. Biashara ya dhahabu inasimuliwa katika maandishi ya Kiyunani ambayo imedaiwa ni tafsiri ya taarifa juu ya safari ya Hanno iliyofanywa pwani ya Moroko mnamo katikati ya karne ya tano. Hanno, anadhaniwa kuwa alikuwa kiongozi wa jamaa ya Magonid na kuwa ndiye aliyehusika na kupanuka kwa Kariteji katika sehemu nyingine za Afrika.

Makao ya kusini zaidi yaliyotajwa kwenye ripoti hii yanaitwa Cerne, ambayo kwa jumla yanahusishwa na kisiwa cha Hern mwanzoni mwa Rio de Oro:

'Huko Cerne, Wafoeniki (yaani Wakariteji) walitia nanga *gauloi* (jina lililotumika kuita meli zao za biashara) na wakapiga mahema yao kwenye kisiwa hicho. Baada ya kupakua bidhaa zao walizichukua hadi nchi kavu kwa kutumia mashua ndogo. Hapo waliishi Wahabeshi ambao walikuwa wakifanya biashara nao. Kwa kubadilishana bidhaa zao, walipata ngozi za paa, simba, na chui, ngozi na pembe za ndovu, hali nao Wafoeniki waliwapelekea manukato, mawe ya Misri (faience) na vyombo vya udongo kutoka Afini na magudulia.

Hapa pia dhahabu haitajwi. Inaelekea kuwa Cern palikuwa mahali pa kutia nanga tu na siyo makazi.⁷

Ikiwa dhahabu ndiyo iliyokuwa sababu ya safari hizo, inashangaza kuona kuwa habari kuhusu biashara hiyo ilitoweka mara Kariteji ilipoanguka, ijapokuwa makazi mengine katika pwani ya Moroko yaliokoka. Mwanahistoria mmoja wa Kiyunani aliyelitwa Polybius, alifanya safari kupitia Cerne baada ya mwaka -146, lakini hakugundua chochote cha thamani na katika karne ya kwanza ya wakati wetu, mwandishi mmoja wa Kirumi aliyelitwa Pliny aliandika juu ya taarifa iliyomhusu Hanno. Kutokana na taarifa hiyo, Wayunani na Warumi wengi wameeleza kuhusu vitu vingi vizuri, na kuanzishwa kwa miji mingi ambayo haikumbukwi wala hakuna mabaki yake popote. Ajabu ni kwamba Mogador ilianza tena kutembelewa na mabaharia kutoka nchi ya Mauritania iliyokuwa inshirika wa kibiashara na Roma, lakini yaonekana kwamba sababu kubwa ya ziara hizo ilikuwa samaki wala siyo dhahabu.

Atlantiki

Taarifa kuhusu safari nyingine inayosimuliwa ni ile iliyoongozwa na mtu mmoja aliyekuwa rika la Hanno aliyelitwa Himilko. Safari hiyo ilimchukua hadi pwani ya Atlantiki ya Uhispania na Ufaransa na bila shaka alifika Brittany. Labda madhumuni ya safari hiyo yalikuwa kuongeza usimamizi wa moja kwa moja wa biashara ya bati iliyopatikana katika sehemu mbali mbali karibu na pwani za Atlantiki. Waandishi kadhaa wa zamani walikuwa na hamu ya kuifahamu biashara hiyo lakini Wakariteji hawakuwa tayari kutoka maelezo mengi kuhusu biashara yenyewe. Kwa kweli kipindi cha Wakariteji ndicho kilichokuwa cha mwisho katika biashara ya bati kwenye pwani hii ambayo ilianza zamani sana kati yake na sehemu ya kusini-magharibi ya Uingereza, ambayo ilikuwa chanzo muhimu cha bati. Hata hivyo hakuna ushahidi wowote kwamba Mfoeniki yeyote aliwahi kufika Uingereza. Hakuna chombo chochote cha Kifoeniki ambacho kimepatikana huko wala katika Brittany. Ikiwa bati kutoka Uingereza ilipatikana, labda ilikuwa kwa kupitia makabila mengine huko Brittany. Yawezekana kwamba bati nyingi kutoka Uingereza ilisafirishwa kupitia Gaul hadi bonde la Rhone na Mediterani na kwamba Wakariteji walipata kiasi kikubwa cha bati kutoka Uhispania ya Kaskazimi. Hata hivyo madini ya thamani zaidi yaliyopatikana huko Uhispania yalikuwa fedha. Twajua kwamba namo karne ya tatu uchimbaji wa fedha uliongezeka sana na bila shaka fedha hiyo ilikuwa muhimu zaidi kuliko bati.

Biashara katika Bahari ya Mediterani

Kama iliyokwisha kuelezwa, Kariteji ilikuwa inahodhi biashara katika milki yake. Iliweza kufanya hivyo kwa kuzamisha meli yoyote iliyokaribia au kwa kuwekeana mikataba ya kibiashara na wale ambao wanalishindana nao kama miji ya Etruskan na Roma. Kwa kawaida wafanyabiashara wa kigeni hawakuruhusiwa kufanya

biashara magharibi ya Kariteji. Hii ilimaamisha kwamba bidhaa walizozileta mjini humo zilisafirishwa na kuuzwa katika meli za Kariteji. Ilikuwa ni kwa kupitia njia hii ambapo bidhaa nyingi kutoka Etruria, Campania, Misri na miji mingine mbalimbali ya Kiyunani zilizifikia sehemu nyingi za Afrika Kaskazini. Ni vigumu kuwatambua watengenezaji wa bidhaa wa Kariteji kiakiolojia kwa sababu hawakuwa na mitindo yao binafsi ya kutengeneza bidhaa. Hata hivyo mnamo karne ya nne Kariteji ilianza kutengeneza sarafu zake, baada ya biashara kati yake na mataifa yaliyostawi kuongezeka na pia mabadiliko ya kiuchumi wakati huo, yaliwataka kuwalipa mamluki kwa sarafu.

Biashara Katika Jangwa la Sahara

Uhusiano wa kibiashara kati ya Kariteji na watu wa Sahara na watu walioishi kusini zaidi si dhahiri. Iwapo kulikuwapo mawasiliano basi lazima yalikuwa katika Leptis Magna na Sabratha, kwa kuwa ni katika eneo hilo ambapo kulikuwako na vizuizi vichache vya kimaumbile. Wasiwasi wa Wakariteji wa kutaka kuwazuia Wayunani wasiingie katika sehemu hiyo, umetajwa kama ushahidi kwamba kulikuwapo na biashara katika sehemu za ndani kwa sababu ardhi iliyofaa kwa kilimo ilikuwa haba. Kwa bahati mbaya, biashara hiyo kama iivyokuwa, haikuacha mabaki yoyote ya kiakiolojia na katika maandishi na vito vyekundu tu ambavyo vimetajwa kuwa bidhaa zilizokuwa zikifanyiwa biashara katika jangwa. Wagaramante wascemkana waliwafukuza Wahabeshi yaani Waafrika kwa magari yaliyovutwa kwa farasi wanne. Pembe na ngozi zimetajwa japokuwa bidhaa hizo zilikuwa zikipatikana kwa urahisi katika nchi za Maghreb. Kuhusu dhababu kutoka Sudan, bado kingali ni kitendawili japokuwa ni janibo linalowezezana. Ushahidi wa hivi karibuni wa kiakiolojia uliopatikana Germa waonyesha kwamba kuongezeka kwa idadi ya watu wa kwanza katika eneo hilo kulianza karne ya tano na kwamba katika karne zilizofuata, watu waliokuwa na makao ya kudumu huko, waliokuwa wakitegemea kilimo walianza kuongezeka. Hii yaweza kuwa inatokana na kuenea kwa utamaduni kutoka makazi ya Wakariteji katika pwani. Baada ya kuharibiwa kwa Kariteji, Warumi waliingia ndani hadi Germa na wakati mwingine, kusini zaidi. Upo ushahidi wa bidhaa ziizoingizwa huko kutoka sehemu za Mediterani, ingawa hizi si nyingi. Kutokuwepo kwa ngamia wakati huo katika Afrika ya kaskazini kunaonyesha jinsi safari kupitia Sahara zilivyokuwa ngumu na za mashaka.

Mji wa Kariteji

Ingawa Kariteji ilikuwa na sifa za kuwa na utajiri mwingi, mabaki ya mji huo hayatupi dalili za utajiri huo, hasa inapofahamika kwamba mji huo uliharibiwa kabisa na Warumi. Hii haimaanishi kwamba mji huo haukuwa na majengo muhimu kama yalivyokuwa katika miji mingine ya kale yenye ukubwa wa mji huo. Kariteji ilikuwa na bandari kubwa ya kujengwa, iliyokuwa na sehemu mbili. Sehemu ya nje ilikuwa ya kutumiwa na meli za kibiashara lakini haijulikani ni meli ngapi zilizoweza kuitumia

kwa wakati mmoja. Na sehemu ya ndani ya bandari hiyo ilikuwa na magati na inabanda kwa ajili ya meli 220 za kivita pamoja na jengo la kuongezea lililokuwa refu zaidi ya mengine yaliyokuwapo bandarini hapo. Kuta za inji huo zilikuwa ndefu na ukubwa usio wa kawaida ambazo zilizahimili mashambulizi ya Warumi hadi mwisho. Ngome ya ndani ilikuwa na ukubwa wa karibu maili mbili, nayo ilizunguka kilima kilichoitwa Byrsa, ambayo bila shaka ndiyo sehemu ya kale zaidi ya mji huo.

Kati ya Byrsa na bandari hiyo kulikuwepo na eneo wazi la unma lililokuwa sawa na mahali pa inakutano pa Wayunani, lakini haionekani kwamba eneo hilo lilikuwa na mtindo wenye minara ya ukumbusho kama ilivyokuwa kawaida katika miji ya Wayunani. Mji huo waonekana ulijengwa bila mpango ukiwa na barabara nyembamba, na tumeelezwa habari juu ya majengo yenye maghorofa hata kufikia sita, kama Tiro kwenyewe na katika Motya huko Sisili. Kwa upande wa mahekalu, ingawa inasemekana kuwa yalikuwa mengi, huenda ikawa idadi yake ilianza kuongezeka baadaye katika historia ya Kariteji wakati ambapo athari ya utamaduni wa Kiyunani ilipozidi kuwa kubwa. Ushahidi mwingi unaonyesha kwamba Wakariteji walikuwa watu wasiopenda mabadiliko katika masuala ya dini na kwa muda mrefu waliendelea kuwa na viwanja vya kawaida vilivyozungushiwa uzio au bila majengo ya ukumbusho.

Taasisi za Kisiasa za Kariteji

Jambo la pekee la Kikariteji ambalo lilisifiwa na Wayunani na Warumi lilikuwa katiba yake ya kisiasa ambayo yaonekana ilihakikisha uthabiti wa kisiasa ambao ulitukuzwa sana zamani hizo. Mtindo wa kurithisha ufalme ulikuwepo katika miji ya Kifoeniki hadi wakati wa Kiyunani, na kumbukumbu zetu zote zinataja juu ya ufalme uliokuwepo Kariteji; kwa ufano Hamilkar aliyeshindiwa Himerra, na Hanno kiongozi aliyepanua dola yake katika Afrika, wanaelezwa hivyo. Inawezekana kwamba kwa kuwaita wafalme, waandishi walikuwa wakifirikiria juu ya uwezo wao mtukufu na wa kisheria, kisiasa na kijeshi. Cheo hicho kilikuwa cha kuchaguliwa wala si cha kurithiwa, lakini vizazi kadhaa vya familia ya Mogonid vilikishikilia.

Mnamo karne za tano na nne familia ya Mogonid ndio waliokuwa viongozi wa kijeshi wakati ulipowadia. Mnamo karne ya tano utaratibu ulianzishwa ambapo uwezo wa kifalme ulipunguzwa. Hii yaonekana ilihusiana na kuanzishwa kwa utawala wa Wasufet, istilahi pekee ya kisiasa ya Kikariteji ambayo tuliandikiwa na waandishi wa Kirumi. Neno hilo lina maana ya hakimu na gavana na kwa kuwa tangu mnamo karne ya tatu (Wasufeti wawili au zaidi) walikuwa wakichaguliwa kila mwaka. Ilikuwa rahisi kuwafananisha na magavana wa Kirumi, na neno Sufet liliendelea kutumiwa katika Afrika Kaskazini katika sehemu zenye utamaduni wa Kikariteji kwa muda usiopungua karne moja baada ya ushindi wa Roma, kama cheo cha hakimu mkuu wa mji. Kupunguzwa kwa madaraka ya wafalme kulikuwa sawa na matukio katika miji ya Kiyunani na katika mji wa Roma. Wakati huo huo uwezo wa watawala wakwasi uliongezeka. Pamoja na uanachama wao pekee katika baraza la taifa kama seneti la Roma, utawala huo ulianzisha baraza la wanachama 100 kwa nia ya

kusimania idara zote za serikali. Ingawa baraza la raia lilikuwa na uwezo fulani katika kuwachagua wafalme, Wasufeti na maafisa wengine, ni dhahiri kwamba siasa za Kariteji zilitawaliwa na matajiri na koo bora. Haikufikiwa kwamba utajiri ulikuwa na athari mbaya kisiasa huko Kariteji. Kuzaliwa kwenye ukoo wenye hadhi na utajiri vilikuwa vitu muhimu kwa mtu kuchaguliwa kwenye ngazi za uongozi.

Dini ya Kariteji

Japokuwa taasisi zao za kisiasa zilisifiwa, maisha ya kidini ya Wakariteji yalilaumiwa vikali na waandishi wa kale hasa kwa sababu ya kuendelea kuwatoa binadamu kama kafara. Nguvu za imani ya kidini pia zilijadiliwa. Kanuni za kidini za Kariteji zilikuwa sawa na zile za Wafoeniki ambao ndio waliokuwa asili ya kanuni hizo. Heshima kubwa waliyonayo wanaume wa Kifoeniki ilijulikana katika Afrika kama Baal Hammon, inayomaanisha tabia ya Hammon, iliyokuwa kali na yenye kueleza hali yake Hammon. Ilifaninishwa na sayari ya Saturn wakati wa Kirumi. Katika karne ya tano umashuhuri wake ulishindwa na mungu wa kike aliyeitwa Tanit.

Jina Tanit ni la Kilibya, na kukua kwa madhehebu yake kunahusiana na kuchakuliwa kwa ardhi katika Afrika kwa sababu ilikuwa na rutuba nyingi, ambayo ilitokana hasa na miungu wa kike wa Kiyunani walioitwa Hera na Deineter. Michoro isiyodhihirika ya mwanamke akiwa ameina mikonu juu inaonekana katika mabamba kutoka Kariteji na kwingineko. Miungu hawa wawili waliwashinda uguvu wengine, ingawa pia twajua juu ya Astarte, Eshimoun (ambaye alihusishwa na Aesculapus - Mponyaji wa Kiroho) na Malkart, mlinzi wa mji wa Tire. Utaratibu wa binadamu kama kafara umethibitishwa kiakiolojia kutokana na kugunduliwa kwa masalia yao huko Kariteji, Hadrumetum, na Girta, katika eneo la Libya ambayo iliathiriwa sana na utamaduni wa Kariteji, na idadi ya makazi mengine nje ya Afrika. Uvumbuzi huo ulikuwa wa maeneo matakatifu yaliyozungushiwa ua ambayo yalikuwa na vyombo vyenye inajivu ya mifupa ya watoto. Mawe ya kaburi yalikuwa na maandishi yenye kueleza kuwa kafara, kwa kawaida, zilitolewa kwa Baal Hammon. Hata hivyo ilionyeshwa pia kuwa Tanit naye alitolewa kafara mara kwa mara. Kwa mujibu wa kumbukumbu zetu (ambazo hazina uhakika) kafara zote zilikuwa wanaume, nazo zilifanywa kila mwaka, na zilikuwa za lazima kwa familia mashuhuri. Tabia hiyo ilipungua lakini tukio la mwaka -310, linaonyesha kwamba ingeweza kufufuliwa wakati ukitokea mkasa. Kusahauliwa kwake kulifikiriwa kuwa ndiko kulikoikasirisha miungu. Ni dhahiri kwamba msisitizo wa mawazo ya kidini ya Wakariteji ulikuwa na nia ya kuifurahisha miungu ambao uwezo wake ulikuwa unabadilikabadilika. Licha ya kukutana kwao na Wamisri, Wakariteji wanaonekana kuwa hawakutilia maanani sana fikra ya maisha baada ya kifo kama walivyofanya Wayahudi wa mwanzo. Ukutili kwa binadamu ulikuwa tukio la kawaida na bidhaa zilizotiwa makaburini hazikuwa nyingi. Makaburi mengi yalikuwa na vifuniko vya uso wa kuchekesha vilivyotengenezwa kwa udongo mwekundu na vilivyofikiwa kuwa vilikuwa vya kukawambuka wafu.

Mizozo na Wayunani wa Sisili

Kipindi cha upanuzi katika Afrika kilichoambatana na kipindi cha amani katika sehemu nyingine kilidumu hadi msiba wa Himera ulipomalizika mnamo mwaka -410. Jiji la Segesta, lililokuwa na wakazi wenye asili ya Kisisili lilikuwa na uhusiano na Kariteji. Jiji hili ambalo lilihusika kwa kiasi fulani na uingizaji wa Waathene Sisili lilianza kushambuliwa vikali na mji wa Kiyunani wa Selinus hadi likalazimika kuomba msaada Kariteji. Ombi hilo lilikubaliwa labda kwa sababu kwamba, iwapo Segesta ingalishindwa, mamlaka ya Wayunani yangelipunguza sana hadhi ya inakazi ya Wafoeniki magharibi ya kisiwa hicho. Aidha, kiongozi wa Wakariteji, Hannibal, aliifanya safari hiyo kuwa vita ya kulipiza kisasi cha kushindwa kwa Himera ambapo babu yake alikufa. Mnamo mwaka -409, jeshi la mamluki wapatao elfu hamsini lilizingira jiji la Selinus na kisha kuliteka siku tisa baadaye baada ya vita vikali.

Muda mfupi baadaye Himera ilitakwa na kuangamizwa kabisa na wakazi wake wote ambao hawakuwahi kutoroka waliuawa. Kisha Hannibal, alirejea na kulivunja jeshi, hatua iliyoonyesha kwamba hakuwako na wazo jingine la kutaka kupanua ardhi yake. Tangu wakati huo Wafoeniki wa Sisili na wale walioishi katika ardhi walizoteka waliunda jimbo la Kariteji. Hata hivyo katika mwaka wa -406 Kariteji ilijaribu kwa mara ya kwanza na ya mwisho kuteka kisiwa chote, baada ya ardhi yake kushambuliwa na Wasairakusi wengine. Vita hivi viliipatia Kariteji ardhi kubwa kuliko iliyokuwa nayo na ilipata kodi zaidi. Zaidi ya hayo iliondoa hali ya kutengwa kwa Kariteji iliyokuwa imedumu kwa muda mrefu katika karne ya tano. Na tokea wakati huo tunakuta kwamba bidhaa zilinunuliwa kutoka Uyunani na biashara kwa jumla na nchi hiyo ilifufuliwa, licha ya kutokea vita vya mara kwa mara. Afrika yenyewe haikukabiliwa na uharibifu, ila twasikia juu ya uasi uliotokea mnamo mwaka -368/7 ambao ulivunjwa kwa urahisi. Wakati fulani mnamo miaka ya -340, mtu mmoja aliyelitwa Hanno alijaribu kufanya mapinduzi kwa kuwaita watumwa, watawaliwa wa Kiafrika na makabila ya Mauretania kujiunga naye, lakini haionekani kwamba kulikuwapo na tishio kubwa.

Hali ilikuwa tofauti kabisa kati ya miaka -310 na -307 wakati Kariteji ilipokuwa inapigana vita na Sairakusi, iliyokuwa ikitawaliwa wakati huo na Agathocles. Wakati mji wake ulipokuwa umezingirwa, Mgriki huyo alifanya kitendo cha ujasiri wenye hatari kubwa. Hali akikwepa meli za kivita za Kariteji aliweza kuvusha askari wake elfu kumi na wanne katika Cap Bon, akazichoma meli zake za kivita na kuclekea Kariteji. Hata hivyo Kariteji kwenyewe hakukuwepo na vituo thabiti vya kijeshi wala makao ya kijeshi, na uharibifu mkubwa ulifanywa katika eneo la Wakariteji katika muda wa miaka mitatu kabla ya kulazimishwa kwake kuondoka Afrika.

Vita vya kwanza baina ya Kariteji na Roma

Mizozo hiyo haikuwa mikubwa ikilinganishwa na mapinduzi ya mashai wakati huo huo, wakati Aleksander Mkuu alipoanzisha dola ambayo ilienea hadi India. Lakini

punde Kariteji yenyewe ilipigana vita vya kihistoria ulimwenguni na Roma. Mkataba ulikuwapo kati yao mnamo -508 wakati Roma ilikuwa mojawapo tu ya jamii nyingi za Italia zilizokuwa na ukubwa wa wastami. Mkataba mwingine ulitiwa sahihi mnamo mwaka -348 ambao ulirekebisha biashara kati ya nchi hizo na ingawa kufikia wakati huo Roma ilikuwa imepata nguvu, mkataba huo ulipendelewa na Kariteji kwa sababu maslahi ya kibiashara ya Roma hayakuwa mengi. Mnamo miaka iliyofuata, Roma ilitawi haraka na kuwa yenye nguvu katika Italia yote. Pengo lililokuwapo kati ya sehemu ambapo nchi hizo mbili zilizokuwa na uwezo na maslahi, lilipungua hasa zaidi mnamo mwaka -293 wakati adui wa zamani wa Kariteji Agathocles alipoendesha shughuli zake kusini mwa Italia. Miaka michache baadaye, Mfalme Pyrrhus wa Epirrus alialikwa Italia ili kujaribu kuikomboa miji ya Kiyunani kusini mwa Italia, ambayo wakati huo ilikuwa ikiongozwa na Tarantum kutoka utawala wa Kirumi. Ijapokuwa alishindwa, aliendewa na Wasisili na kuombwa awe mlinzi wao dhidi ya Kariteji. Ili kuzuia jambo hilo, Kariteji ilipeleka msafara mkubwa wa meli za kivita Roma ili kuitia moyo Roma iendelee na vita dhidi ya Pyrrhus. Roma ilifaulu lakini Pyrrhus alikwenda Sisili na kujipatia uslundu usio mkubwa sana kabla ya kurejea Uyunani katika mwaka -276.

Kwa hiyo hadi kufikia wakati huo Kariteji na Roma hazikuwa na tofauti zozote katika maslahi yao. Lakini miaka kumi baadaye kulizuka mzozo mkubwa kati ya nchi hizi uliosababisha hasara kubwa kwa pande zote mbili. Hasara hiyo ilikuwa haijapata kutokea katika vita hapo kabla. Ingawa matokeo ya vita hivyo yalikuwa muhimu kijiografia na kisiasa, ni dhahiri kwamba sababu ya kuzusliwa kwa vita hivyo haikuwa ya maana sana na kwamba kila upande haukuwa na madhumuni mahusi. Katika mwaka -264, Roma ilikubali kusafimu ainri kwa Messana (Messina) ambayo ilipigana vita upande wa Kariteji katika vita yake na Sairakusi. Wanasiasa wa Kirumi wakati huo walikuwa wanajiamini sana. Yaonekana ilitazamiwa kwamba Kariteji haingeyajibu mashambulizi hayo, na kwamba kulikuwepo nyara ambazo zingelipatikana kutoka miji ya Kiyunani katika Sisili. Wengine pia walitilia maanani hofu za Roma kwamba ikiwa Kariteji ingetaka Messana, ingeitawala Italia, jambo ambalo Kariteji haikuwa na nia yoyote ya kulifanya. Kariteji ilidhamiria kupinga mwingilio wa Kirumi kwa sababu ungalibadilisha kabisa uwiano wa nguvu katika kisiwa hicho uliokuwa umedumu kwa karne moja na nusu, na pia kwa sababu walifikiria kwamba maongozi ya Kirumi yalikuwa ya kubahatisha sana. Vita iliyofuata (vita vya kwanza vya Kipuniki) iliendelea hadi mwaka -242 wakati meli za Kariteji ziliposhindwa nje ya visiwa vya Egates. Hii ilimaanisha kwamba Sisili isingeweza kupata bidhaa. Na kutokana na amani iliyosababishwa na uchovu iliofuatia, Kariteji iliamua kuiacha Sisili na ikakubali kulipa fidia kubwa.

Hannibal na vita ya pili na Roma

Hali mbaya ya kiuchumi iliyotokana na vita ilifanya iwe vigumu kwa Wakariteji kuwalipa mamluki ambao nusu yao walikuwa Walibya. Uasi ulitokea Afrika

uliosababisha vifo vingi kwa pande zote. Mamluki wapatao elfu ishirini walihusika kaika uasi huo na mmoja wa viongozi wao stadi zaidi alikuwa Mlibya aliyetwa Matho. Kariteji yenyewe ilikuwa hatarini na kwa wakati fulani waasi hao walishikilia sehemu za Utika, Hippo, Acra na Tunis. Waasi hao walijiandaa vizuri sana hata wakaweza kutoa sarafu zao zenye maandishi, Libyon, (inaana yake Walibya) kwa Kiyunani. Ukali wa mapambano hayo yaliyokwisha mnamo mwaka -237 yalidhihirisha jinsi Wakariteji walivyokuwa makatili wa Walibya. Wakati huo huo Warumi waliteka Sardinia wakati Kariteji ilipokuwa haijiwezi.

Mnamo mwaka -220, Roma ilianza kuwa na wasiwasi kuhusu jinsi Kariteji ilivyokuwa inaanza kupata nguvu na ikaanzisha njania ya kuizuia dola hiyo isiimarisha au kueneza mamlaka yake hadi Uhispania. Hannibal (na serikali yake) alikataa vitisho vya Roma na akaamua, kutokana na maongozi hatari ya Roma mnamo mwaka -264 na -237 kwamba vita haviwezi kuepukwa. Mnamo mwaka -218 Hannibal alivuka Ebro akiwa njiani kuelekea Italia. Hatua hii ilichukuliwa kutokana na fikra kwamba ushindi wa mwisho dhidi ya Roma ilikuwa lazima upatikane huko huko Italia. Ilikuwapo pia fikra kwamba kulikuwa na umuhimu kuizuia Roma isishambulie Afrika kwanza. Mashambulizi kama haya yangeweza kufanyika kwa urahisi kwa kuwa Roma ilikuwa ikitawala bahari. Vita hivi (vita vya pili vya Puniki) viliendelea hadi mwaka -202, na Roma ilipata hasara kubwa kwa mara nyingine. Ushupavu wa kijeshi wa Hannibal ulilisuka vizuri jeshi ambalo askari wake wengi walikuwa Wahispania, lakini wakiwamo pia Waganli na Waafrika. Ushindi mkubwa ulipatikana kwenye ziwa Trasimeme (217) na Cannae (216), ambapo Roma ilishindwa vibaya sana. Huko Italia wakati sera ya kujihami ya Fabius Maximus ilikuwa ikifuatwa, Hannibal hakuruhusiwa kuendelea kuonyesha ushupavu wake uwandani. Uhispania ilichukuliwa na Roma chini ya uongozi wa kijana Scipio Africanus katika mwaka -206. Baada ya hapo ndipo Roma ilijitayarisha kuishambulia Afrika.

Katika shambulio hilo Roma ilisaidiwa na hali ilivyokuwa katika Numidia. Makabila ya sehemu hiyo wakati huo yalikuwa yamekwishaathiriwa na ustaarabu wa Kikariteji kwa kame kadhaa. Kulikuwapo na vikundi vikubwa vya kisiasa kuliko ilivyokuwa hapo awali; na kushiriki niara kwa inara katika vita vya Kariteji, kulikuwa kumewaongezea nguvu na werrevu. Syphax aliyekuwa jumbe wa kabila kubwa zaidi katika Numidia Masaesyli ambaye eneo lake lilienea kutoka Ampsaga (Qued el Kebir) mashariki hadi Mulucha (Moulouys) upande wa magharibi. Alikuwa amejitenga kutoka Kariteji katika mwaka -213, lakini akajiunga nayo tena mnamo mwaka -208 alipomwoa binti wa mtu mmoja mashuhuri wa Kariteji. Kwa upande mwingine, Gaia, jumbe wa Massyli, ambaye eneo lake lilikuwa kati ya Masaesyli na Kariteji, alikuwa mwaminifu kwa Kariteji wakati wa kujitenga kwa Syphax, naye mwanaye Masinissa alitoa huduma nzuri kwa Uhispania. Wakati Uhispania ilipojipatia ushindi, Masinissa alijiunga na upande uliolekea kupata ushindi hivyo akafanya mapatano ya amani na Scipio. Masinissa aliporejea Afrika hakuweza tena kuchukuliwa kama kiongozi wa

kabila lake kwa hivyo akajikusanyia kikosi chake binafsi, na baada ya miaka miwili, alikuwa akimngojea Scipia awasili ili apigane upande wake. Alitekeleza wajibu mkubwa katika ushindi wa mwanzo katika mwaka -203 kabla ya Hannibal kuitwa kutoka Italia. Mapigano ya mwisho yalitokea Zama (Sab Biar) katika mwaka wa -202 wakati Hannibal aliposhindwa. Mesinissa ambaye wakati huo huo alikuwa amemtorosha Syphax kutoka eneo lake, alitoa askari wapanda farasi elfu nane, hatua iliyosaidia sana katika ushindi wa Roma. Kwa mujibu wa mkataba wa amani uliofikiwa baada ya vita hivi, Kariteji iliacha meli zake zote na ardhi yake katika Afrika ikapunguzwa na kuishia katika mstari kutoka Thabraca hadi Thaenae.

Lakini alipaswa pia kumrejeshea masinissa ardhi yote iliyokuwa ya babu zake iliyokuwa imetwaliwa. Kuendelea kushikwa kwa ardhi hii kungezidi kuzua mizozo. Kariteji pia ilipigwa marufuku kupigana vita nje ya Afrika, na hata Afrika kwenyewe bila idhini ya Roma.

Masinissa na Ufalme wa Numidia

Kariteji ilinusurika kwa miaka mingine hamsini, lakini kipindi hiki cha historia ya Maghreb, kilikuwa na maendeleo ya haraka katika uchumi na jamii ya makabila mengine yaliyokuwako karibu na Mediterani. Ilikuwa fumbo la kihistoria kuona kwamba mtu aliyehusika sana na maendeleo hayo, ambayo yalihusu kuenca kwa haraka kwa ustaarabu wa Kariteji kuliko ilivyopata kutokea wakati mwingine wowote, hakuwa mwingine bali adui mkubwa wa Kariteji, Masinissa. Haiba yake ilikuwa kwamba badala ya kuchukuliwa kama mkimbizi tu wa manufaa na Warumi baada ya mwaka -206, baadaye alianzisha uhusiano mkubwa na wanasiasa wenye uwezo mkubwa katika Roma. Baadaye ya Zama alitunukiwa sehemu za mashariki, zenye rutuba zaidi kati ya ardhi ya Syphax, na kwa hivyo akatawala kutoka Cirta (Constantine) eneo lililoenea kutoka mahali fulani Magharibi ya mji huo hadi kwenye mpaka mpya wa Kariteji. Biashara ya bidhaa nyingine iliwekewa vikwazo na sarafu zilizotolewa zilikuwa na shaba nyekundu na nyeusi. Mji mkuu wa Masinissa waonekana ulistawi na kuwa jiji kubwa. Akiolojia ya mji huu haijulikani sana lakini yaaminika hali yake ya kimji ilikuwa sawa na ya Kariteji. Minara mingi ya mawe ya makaburi imepatikana zaidi huko kuliko katika sehemu nyingine za Afrika isipokuwa Kariteji kwenyewe, na bila shaka lugha ya Kariteji ilizidi kutumiwa katika Numidia na Mauretania.

Kuharibiwa Kwa Kariteji

Katika muda wa miaka hamsini Masinissa aliendelea kuidai ardhi ya Kariteji na labda alitumaini kwamba Kariteji yenyewe ataiteka kwa idhini ya Roma. Mwanzo, Roma haikuwa na uia ya kuidhoofisha zaidi Kariteji ambayo ilikuwa yaitegemea na kufikia mwaka -170 Masinissa hakuwa amejipatia eneo kubwa. Tokea mwaka -167, hata hivyo, Roma ilianza kufuata sera za kikatili, sio tu katika Afrika, bali pia kwingineko

na ilimuunga mkono Masinissa. Ingawa ni kweli kwamba Kariteji ilikuwa imeimarika baada ya vita vya pili vya Kipuniki, wazo kwamba lingelikuwa tishio kwa Roma lilikuwa la kipumbavu. Wakariteji walipewa nafasi ya kuamua baina ya mambo mawili: ama wauache mji wao na kuingia ndani zaidi au wakabiliwe na vita. Walipoamua kupigana vita, jeshi la Kirumi lilipelekwa Afrika mwaka -149. Licha ya jeshi la Roma kuwa na nguvu zaidi, Kariteji ilipigana hadi mwaka -146. Walibya wengine walikuwa wangali wakiiunga mkono, na Masinissa mwenyewe hakupendezwa na hatua hiyo ya Roma ambayo ililivunja tumaini lake, lakini hata hivyo hatimaye hakuwa na jingine ila kukubali. Makazi mengi ya zamani ya Wafoeniki kama Utika, Hadrrumentum, Thapsus na mengineyo yaliijisalimisha kwa Roma na kuepuka kuangamizwa. Kariteji yenyewe ilivunjwa kabisa na enco hilo likalaaniwa katika sherehe, kitendo kilichofanywa na Roma kudhihirisha hofu na chuki ambazo walikuwa nazo kwa zaidi ya karne moja kwa nchi yoyote ambayo ilipinga vikali utawala wake katika eneo la Mediterani.

Mataifa yaliyofuata Kariteji

Numidia

Ilikuwa zaidi ya karne moja kabla ya Roma kuizidi nguvu Kariteji kaina nchi yenye uwczu katika Maghreb. Kwa sababu mbalimbali Roma ilitwaa sehemu ndogo tu ya kaskazini-mashariki ya Tumsia baada ya kuangamizwa kwa Kariteji. Hata hivyo, hawakujali sana sehemu hiyo. Katika sehemu nyingine za Afrika kaskazini, Roma ilizitambua falme marafiki ambazo ziliachiwa kufuata mambo yao wenyewe. Katika falme hizi, utamaduni wa Kikariteji uliendelea na hata kuongezeka wakati makazi ya zamani ya pwani yalipoendelea kustawi, na wakiinbizi wengi waliotokana na vita vya miaka ya mwisho mwisho ya Kariteji walikiimbilia luuko. Lugha ya Kifoeniki katika mtindo wake wa baadaye ulioitwa *Puniki mambo leo* ilienea sana. Huko Numidia, Masinissa alikufa muamo mwaka -148 akiwa na umri wa karibu miaka tisini. Mahali pake palichukuliwa na Micipsa (-148 hadi -118). Wakati wa enzi yake, biashara kati ya Numidia na Roma, na Italia ziliongezeka na tunasikia juu ya wafanyabiashara wa Kitaliano katika inji wa Cirta. Micipsa alipokufa, ufalme wake ulitawaliwa kwa pamoja na ndugu zake wawili, pamoja na Jugurtha aliyekuwa mjukuu wa Masinissa aliyeyungwa mkono na kiongozi wa Roma Scipio Aemilianus, kama vile Masinissa alivyoyungwa ukono na Scipio wa hapo awali. Jugurtha alikuwa mtu mwenye nguvu nyingi na alitaka awe mtawala peke yake. Baadaye Warumi walijaribu kuugawanya rasmi ufalme huo lakini wakati Jugurtha alipoteka Cirta kutoka kwa inmoja wa wapinzani wake na akawaua wakazi wa Kitaliano, Roma ilitangaza vita. Jugurtha alijitahidi sana katika vita hiyo na kuwaaibisha kijeshi Warumi hadi aliposalitiwa kwa Warumi na Bocchus, mtawala wa Mauretania. Baada ya hapo Roma ilimtawaza mtu mmoja katika ufalme wa Masinissa aliyeitwa Gauda kuwa mfalme. Gauda alirithiwa na mwanawe, Hiempsal. Inasemekana kuwa Hiempsal aliandika kitabu kuhusu Afrika

katika lugha ya Kipuniki, na huenda aliendeleza shughuli ya kueneza ustaarabu wa ufalme wake. Mwana wa Hiempsal Juba (-60 hadi -46) ambaye alikuwa ametukanwa hadharani na Julius Kaisari alipokuwa kijana. Alijiunga na shirika la Pompei katika mwaka -49 na akalisaidia sana shirika hilo katika shughuli zake Afrika. Kutokana na juhudi hizo aliaminika kwamba alikuwa amehidiwa jumbo la Roma katika Afrika iwapo Wapompei wanalishinda. Juba alijinyonga baada ya ushindi wa Kaisari huko Thapsus. Ushindi huu ulifuatiwa na kuanzishwa kwa utawala wa moja kwa moja katika Numidia kutoka Roma.

Mauretania

Ufalme wa Mauretania wafikiriwa ulistawi pole pole zaidi kuliko wa Numidia, lakini hii huenda ilitokana na ukosefu wa habari. Bila shaka mlima Massif wa Atlas haukufikiwa na Wafoeniki. Pia haukufikiwa na ustaarabu wa Warumi, lakini kulikuwepo na wakazi katika maeneo yenye rutuba kama bonde la Moulouva na kwenye pwani ya Atlantiki. Ilikuwa katika sehemu za milima ambapo makabila yalidumisha utafu wao wakati wa enzi za Warumi na hata baadaye Wamauri wanatajwa mapema wakati wa safari ya Cicily inwaka -406, katika maasi ya Hanno mnamo miaka ya -350 na katika uvamizi wa Warumi katika Afrika mwaka -256, Mfalme mmoja wa Mautri alimsaidia Masinissa alipokuwa katika hali ya hatari lakini pia walikuwapo Wamauri katika jeshi la Hannibal kule Zama. Katika tarehe ya baadaye, Bacchos wa kwanza alimsaidia Jugurtha katika vita yake dhidi ya Roma, lakini baadaye akamsaliti, na akatunukiwa ardhi kubwa inashariki ya Moulouya. Katika kizazi kilichofuata, eneo hilo laonekana kama liligawanwa. Bocchus wa pili alitawala sehemu ya inashariki na kwa kushirikiana na Taliano innoja aliyetwa P. Sittius, walipigana dhidi ya Juba kwa manufaa ya Kaisari ambaye pia aliungwa mkono na Bogud wa pili, ambaye alitwaa magharibi ya Moulouya. Wote wawili walitunukiwa; Bocchus aliongezewa ardhi yake, badala ya Numidia. Miaka michache baadaye Bogud wa pili alimuunga mkono Mark Anthony dhidi ya Octavian katika vita vya wenyewe kwa wenyewe vya Roma, na akafukuzwa kutoka ardhi yake na Bocchus wa pili kwa niaba ya Octavian. Bocchus alipokufa katika mwaka wa -33, naye Bogud akauawa mnamo mwaka wa -31, sehemu hiyo yote kubwa ilibaki bila mtawala. Mnamo mwaka wa -25 Augustus alimtawaza Juba mwana wa Mfalme wa mwisho wa Numidia kuwa mfalme. Juba aliishi nchini Italia tangu alipokuwa na umri wa miaka minne na alikuwa ametengewa ufalme wa Numidia kwa muda kati ya mwaka -30 na -25. Akitawala kwa zaidi ya miaka 40 akiwa mfalme kibaraka inwaminifu, Juba alitendea Mauretania yale ambayo Masinissa alitendea Numidia. Alikuwa amebobea kwenye utamaduni wa Kiyunani na aliandika vitabu vingi (ambavyo sasa vimepotea) katika lugha ya Kiyunani. Hapana shaka kwamba mji wake mkuu lol ambao baadaye ulipewa jina la Kaesarea (Oherchell), na labda nji mwingine mkuu wa pili, Volubilis, ulikuwa na maendeleo yote ya kimji wakati wa enzi yake. Mahali pake palichukuliwa na mwanawe Ptolemaus aliyetawala hadi mwaka +40 alipoitwa Roma na Mfalme

Gaius na kuuawa bila sababu yoyote kutolewa. Katika mwaka +44 Mauretania iligawanywa katika majimbo mawili, na hivyo kukamilisha mipango ya utawala wa Kirumi huko Maghreb.

Urithi wa Wafoeniki Katika Maghreb

Kwa jumla, wakati wa falme huru za Numidia na Mauretania ulikuwa wakati wa kukua na kuanzishwa kwa utamaduni mseto wenye vionjo vya Kilibya na Kifoeniki. Utamaduni wa Kifoeniki ndio ulioshamiri zaidi katika mseto huo ingawa uliwakilisha watu wachache katika jumla ya idadi ya watu wa huko. Nguvu za utamaduni huo wa mseto zadhihirika kutokana na ukweli kuwa maandishi ya Kipuniki - mamboleo yaliendelea kutumiwa hadi karne ya pili ya enzi zetu na kwamba wakati huo huo, neno Sufer lilitumika katika miji mbalimbali isiyopungua thelathini, baadhi yake ikiwa Volubilis uliokuwa magharibi mwa Moroko na Leptis Magna uliokuwa Libya. Kudumu kwa dini ya Maghreb na Libya wakati wa enzi za Warumi ni uthibitisho bayana wa jinsi dini hiyo ilivyoenea sana. Kihistoria, kuanzishwa kwa makazi ya Wafoeniki katika Maghreb ndiyo hatua pekee iliyoeenea ustaarabu mkongwe wa nchi za kalc za Mashariki katika eneo la magharibi la Mediterani. Kariteji ya karibu na ya kati ilidumu katika vipindi vyote vya ustaarabu huo. Ustaarabu huu pamoja na kuenea wa Wayunani upande wa magharibi, ulikuwa ni sehemu ya harakati ambazo zilikutanisha ustaarabu wa Ejeani na ule wa Mashariki katika eneo lote la magharibi mwa Ulaya, ambalo hadi kufikia wakati huo lilikuwa linakaliwa na watu wa makabila mbalimbali. Katika historia ya Afrika, wakati wa Wafoeniki uliileta Maghreb katika historia ya eneo la Mediterani, ikitilia mkazo uhusiano wake na pwani za kaskazini na inashariki mwa Afrika. Sababu za kijografia ambazo hadi hii leo zilikwisha husisha Maghreb na eneo la Mediterani nazo zilisisitizwa. Kwa sababu ya uhaba wa kumbakumbu zetu za kihistoria, akuaji wa maarifa zaidi juu ya kuendelea kwa utamaduni wa wazalendo wa Libya na jinsi ulivyokua kulingana na kuanzishwa kwa ustaarabu wa Kifoeniki lazima ungojce utafiti zaidi wa wanaakiolojia.*

* Taarifa ya Kamati ya Kimataifa ya Sayansi: Taarifa kamili zaidi inakusudiwa kutolewa kuhusu urithi na dhima ya Libya kwa kipindi kilichozungumziwa kwenye juzuu hili katika nakala itakayofuata. Kuna mpango wa kuandaa Kongamano juu ya mchango wa Libya katika kipindi maarufu cha kale kwa kurejelea hasa dhima ya Sirenaika katika enzi za Wagiriki Libya katika kipindi cha Wafoeniki na ustaarabu wa Wagaramante.

19

Kipindi cha Warumi na Baada ya Warumi Afrika ya Kaskazini

SEHEMU YA 1: Enzi za Warumi

Uvamizi wa Warumi Pwani ya Afrika Kaskazini na upinzani wa Wazalendo

Baada ya kushindwa kwa Kariteji katika mwaka wa -146, na kupunguzwa kwa eneo lake hadi kuwa sawa na jimbo la Urumi, hali ya Afrika kaskazini ilikuwa mikononi mwa Warumi na falme za wenyeji wa hako. Ingelikuwa vizuri kuandika sura maalumu kuhusu falme za wenyeji tokea falme za Numidia hadi mwisho wa utawala wa mfalme wa mwisho wa Mauretania katika mwaka +40. Tangu wakati huo eneo lote la Afrika ya kaskazini lilikuwa chini ya Warumi hadi uvamizi wa Waharabu.

Maumbile maalum ya vita vya Kiafrika huonekana hasa kutokana na taarifa za ushindi. Wakati wa robo ya mwisho ya karne ya kwanza kabla ya enzi za Ukristo, majemadari wa Kirumi walifanya sherehe nyingi kufurahia ushindi wao dhidi ya Wamaurusia, Wamuslamii, Wagaetuli, na Wagaramante, sherehe ambazo zinatoa ushahidi bayana kwamba wenyeji wa huko hawakushindwa kabisa licha ya ushindi wa Warumi.

Vita inayojulikana sana ni ile ya Watakarfarina wa Numidia ambavyo vilieleleka kwa muda wa miaka minane chini ya utawala wa Tiberius, na ikaenea hadi katika mipaka ya kusini mwa Afrika kaskazini kutoka Tripolitania mpaka Mauretania. Madai yaliyotolewa na Tikitus kwa Watakarfarina yanadhihirisha kwa nini wazalendo walikuwa wakipinga kuwapa kwao. Kiongozi wa Wanumidia alitangaza vita ili kumfanya mfalme wa Warumi mwenye nguvu kutambua haki za watu wake kumiliki ardhi, kwa kuwa ushindi wa Warumi ulifuatiwa mara moja na kutwaliwa kwa ardhi yote yenye rutuba. Mashamba ya Wanumidia yaliachwa bila kuhudumiwa na maenco ambayo kwa kawaida yalituniwa na wahamaji yaliendelea kupunguzwa na kuwa haba. Wajuzi wa kivita na wakoloni wengi wa Kirumi na Kitaliano walianzisha makazi kila mahali wakianzia na sehemu zenye utajiri mwingi. Makampuni ya kukusanya kodi, na makabaila wa Kirumi walijitwalia maenco makubwa ya ardhi. Huku nchi yao ikitumiwa hivyo, wahamaji na wenyeji wengine waliokuwa na makazi ya kudumu ambao hawakuishi katika miji michache iliyookoka

kutokana na vita vilivyofuatiwa na kuchukuliwa kwa mali, walifanywa ama kuwa maskini sana ama wakimbilie nyanda kame na jangwani. Tumaini pekee walilokuwa nalo lililikuwa kuchukua silaha na kupigana, na lengo lao kubwa la kivita lilikuwa ni knikomboa ardhi yao.

Mashambulizi ya kijeshi yaliendelea wakati wote karika karne mbili za kwanza za enzi za Ukristo. Kusonga mbele kwa mashambulizi ya Warumi kuelekea kusini-magharibi kuliyavuruga makabila ya sehemu hizo ambayo yalijikusanya na kutawanyikia katika eneo linaloanzia bonde la Moulouya hadi Jebeli Amour na Kuarisenia. Baada ya kujiimarisha kwa urahisi katika ukanda wa pwani na kaskazini-mashariki, Warumi walisonga mbele hatua kwa hatua katika sehemu ya kusini ya mahali ambapo siku hizi tunapaita Tunisia, na pia katika nyanda za juu na Atlas ya Sahara. Wakati wa utawala wa wafalme Julio na Claudian, mpaka wa eneo lililotekwa ulienea kutoka Cirta upande wa magharibi hadi Tacape upande wa kusini na ulijumuisha Ammaedara, ambayo yalikuwa makao makuu ya kikosi cha Tatu cha Augusta, Thelepte na Kapsa. Wakati wa utawala wa wafalme wa Flavian, kikosi hicho kilijiimarisha Theveste na mpaka ulisogezwa mbele hadi kufikia Sitifis. Sehemu ya Nemechta iliwekwa chini ya Trajan na koloni la Tingad lilianzishwa katika mwaka +100. Hatimaye mnamo mwaka +128, kikosi hicho, kilianzisha makao ya kudumu huko Lambaesis ambayo yalilindwa dhidi ya makabila ya wenyeji na kambi iliyokuwa Gemellae. Kati ya majimbo ya Kirumi, na sehemu za jangwa zilizokuwapo kusini ambapo ndipo makabila yalipofukuziwa, ukanda wa mpaka ulianzishwa; ukanda huu ulisogezwa mbele polepole kuelekea kusini-magharibi ukiwa na mitaro na barabara zenye vituo (vyenye umbali wa kilomita 50 hadi 100) na ambavyo vililindwa na vikosi vya kijeshi. Vituo hivyo pia vilikuwa na ngome ndogo ndogo. Uchunguzi wa kiakiolojia uliofanywa na J. Darades kutoka angani umegumdua pamoja na mambo mengine kwainba sehemu za ngome zilizungushwa ukuta ua kulindwa katika sehemu mbalimbali na minara ya miraba au ya mistatili.

Hata hivyo Urumi haikuwa na nguvu za kuiwezesha kuushinda upinzani wa Waberiberi, na kamwe haikufaulu kulanya doria daima katika sehemu za kusini na magharibi ili kuchunguza nyendo za wahamaji. Licha ya juhudi za Trajan na Hadrian, na licha ya sera thabiti iliyofuatwa na Septimius Severus katika mipaka ya Tripolitania, mzozo wa karne ya tatu uliuharibu mpango huo. Jangwa, uwezo wa wanamaji kusafiri kwa ngamia, na urahisi wa kufanya mawasiliano kati ya Mashariki na magharibi kwenye milima ya Atlas ya Sahara, viliiwawezesha Waberiberi kusafiri bila kipingamizi. Kutokana na haya, makabila yaliyoweza kukabiliana na nguvu za Warumi yaliwapata watu wa akiba kwa majeshi yao katika Mauretania Tingitana, na baadaye katika jangwa kubwa kwenye bara la Tripolitania. Hadi robo ya kwanza ya karne ya tatu, sehemu za kati na kusini za nchi hiyo zililindwa dhidi ya mashambulizi ya watu wa sehemu hiyo na kikosi cha Augusta III, ambacho nguvu zake za kijeshi zilidhaniwa kuwa na watu wapatao kati ya 5,000 na 6,000 ambao waliongezewa nguvu kama kawaida na askari wengi wa kusaidia. Imefikiriwa kwamba jumla ya wanajeshi wote huenda ilikuwa kati ya 25,000 na 30,000 katika karne ya pili. Hii si idadi kubwa, ijapokuwa ni muhimu kufikiria juu ya askari waliokuwa

wamepigana zamani na ambao walikuwa na uwezo wa kupigana ambao walikaa katika ardhi ambayo ilikuwa imefyekwa ili ilimwe. Ilipokuwa hapana budi wanajeshi waliletwa kutoka vikosi vilivyokuwa katika majimbo mengine ya himaya hii.

Utaratibu wa Utawala na Matatizo ya Kijeshi

Tarehe 13, Januari, mwaka -27, Oktavian alipewa cheo cha Augustus, na siku tatu baadaye, aliyagawa majimbo ya ufalme huo kulingana na mpango ulioidhinishwa kati yake na baraza la seneti. Afrika ambayo kwa muda mrefu ilikuwa imekwishatekwa na kutulizwa na kuhushishwa tabaka la kiseneti kulingana na desturi za kiuchumi na kisiasa, ilikuwa mojawapo ya majimbo yaliyotawaliwa na baraza la Seneti. Jimbo la Afrika ambalo kwa kawaida ya maongozi ya Kirumi lilitawaliwa na magavana wa Kirumi, lihunganisha majimbo mawili ambayo yalianzishwa na Warumi katika Afrika kaskazini: Jimbo moja lilikuwa lile la eneo la Wakariteji lililotekwa mnamo mwaka -146, na kuitwa Afrika Vetus, na Jimbo jingine lilianzishwa na Kaisari baada ya mashambulizi yake katika Afrika dhidi ya Wapompei na mshirika wao, Mfalme Juba wa kwanza wa Numidia na lilitwa Afrika Nova. Mbali na majimbo haya, yalikuwapo makoloni ya Cirta ambayo Kaisari aliyakabidhi kwa Mtaliano mmoja aliyetwa P. Sittius.

Kama ilivyokuwa wakati wa jamhuri, baraza la seneti la Kirumi liliendelea wakati wa utawala wa kidola kupeleka gavana katika Afrika. Gavana huyo alikuwa mmoja kati ya mabalozi wawili wakuu waliokuwapo Roma wakati wa kutayarisha mipango ya hali ya baadaye kwa majimbo. Kwa hiyo, alikuwa na cheo cha 'Gavana' na ikiwa muda wake wa kazi haukuongezwa kama hatua isiyo ya kawaida, alishikilia kazi hiyo kwa muda wa mwaka mmoja. Mbali na majukumu yake ya kisheria ambayo kutokana nayo alikuwa hakimu mkuu wa jimbo hilo katika kesi za jinai na za madai, pia alikuwa ni mtawala na mdhibiti wa utawala na wa fedha. Gavana alisimamia ujenzi wa miradi mikubwa ya umma na kuidhinisha matumizi ya fedha; alikuwa na mamlaka ya juu kwa idara iliyokuwa ikisimamia upelekaji ngano Roma kutoka Afrika na kwa shughuli za utaratibu wa mapato, ya serikali ambayo yalipelekwa *Aerarium Saturni*, iliyokuwa hazina ya seneti. Gavana alisaidiwa na wawakilishi ambao mmoja wao alikaa Kariteji kwenyewe na mwingine alikaa Hipone. Afisa mmoja pia alisimamia masuala ya fedha. Aidha, kama ilivyokwishatajwa, alipewa kikosi kidogo cha wanajeshi wapatao 1,600 kwa kuhifadhi sheria na utangamano.

Mfalme aliweza kuingilia kati, inashauri ya jimbo, moja kwa moja au kama ilivyokuwa mara nyingi, kupita kwa balozi mkazi, ambaye alikuwa afisa wa mfalme aliyesimamia miliki za mfalme na ukusanyaji wa kodi nyingine ambazo hazikuwa za moja kwa moja kama '*vicesima hereditium*' ambayo ilitoa pesa kwa hazina ya kijeshi iliyosimamiwa na mfalme mwenyewe. Mwakilishi alikuwa na uwezo fulani wa kisheria wa kusuluhisha mizozo iliyotokana na kodi. Tokea mwaka 135, alisaidiwa na msaidizi kutawala miliki za mfalme, naye mwakilishi wa nne *Publicorum Africae* (procurator 111 *Publicorum Africae*) alimsaidia kudhibiti mapato ya serikali.

Wakati huo huo, Afrika iliyokuwa ikitawaliwa na gavana wa Kirumi haikunyimwa haki ya kuwa na majeshi kama ilivyokuwa katika majimbo mengine ya kiseneti. Wakati sehemu ya kaskazini-mashariki iliyofanana na jimbo la zamani la Afrika Vetus ilikuwa tulivu hali haikuwa hivyo katika sehemu za kusini ambapo watawala wa Kirumi walihitaji kikosi cha kijeshi kuilinda na kisha polepole (labda) kupanua mipaka ya kanda ambayo walipaswa kuilinda. Majeshi haya ambayo mengi yake yalikuwa ya kikosi cha Augusta III yaliongozwa na balozi wa mfalme aliyefanya kazi chini ya gavana, na ambaye alikuwa na uwezo wa kutumia nguvu za kijeshi kwa magavana wa Jamhuri waliosimamia Seneti. Hata hivyo, hali hiyo isingeweza kuendelea hivyo kwa muda mrefu bila kumfanya mfalme aanze kungiwa na wasiwasi. Haukupita muda mrefu Caligula aliamua, kwa kuzingatia sera ya kuwazuia magavana wa kiraia kuwa na uwezo mkubwa na kupunguza mamlaka na uhuru wa seneti kufanya mabadiliko muhimu ya kisiasa na kijeshi katika uendeshaji wa Afrika iliyokuwa chini ya utawala wa Kirumi. Usimamizi wa jeshi uliondolewa kutoka kwa serikali ya kiraia, na hatua hii ilisababisha kuanzishwa kwa utawala wa kijeshi katika Numidia chini ya uongozi wa balozi aliyesimamia kikosi cha Augusta III. Mnamo mwaka +39 cheo cha afisa huyo aliyepewa uwezo huo maalumu kilikaa kati ya cheo cha mabalozi waliokuwa magavana wa majimbo na cheo cha wale waliokuwa manaibu wa majemedari wa vikosi.

Hatimaye Septimius Severus alirekebisha hali hiyo kwa kupandisha hadhi ya eneo hilo la kijeshi na kuwa jimbo kamili. Hilo ndilo lililokuwa jimbo la Numidia lililoundwa labada katika mwaka wa +198 had +199. Jimbo lilisimamiwa na balozi wa kikosi aliyelitwa pia '*Praeses*' na aliyeteuliwa na kuhamishwa na mfalme mwenyewe, na mpaka wake wa magharibi bado ulifuata ukingo wa kushoto wa Ampsaga (Oued-el-Kabir), kupita magharibi ya Kuikuli na Zarai na kuvuka nyanda za Hodna kuelekea kusini, upande wa Laghouat.

Kati ya Ampsaga na Atlantiki palikuwapo na ufalme wa Mauretania ambao ulikuwa umerithishwa na ufalme Bochas Mdogo kwa dola ya Kirumi mnamo mwaka -33. Oktavian, Augusto wa baadaye alikubali urithi huo na akatumia fursa hiyo kuanzisha makoloni saba ya kijeshi katika nchi hiyo. Lakini mnamo mwaka -25 alimwachia Juba wa pili ufalme huo ambaye naye alirithiwa na manawe Ptolemy katika mwaka +23. Katika mwaka +40 Caligula aliamua kwamba wakati ulikuwa umewadia wa kutawala moja kwa moja bila wawakilishi na akasababisha Ptolemy kuuawa. Mwishowe Claudius aliamua, mnamo mwisho wa mwaka +42 kupanga vizuri hayo majimbo mawili ya Mauretania: Kulikuwapo Caesariensis upande wa mashariki na Tingitana upande wa magharibi yakitenganishwa na Mulucha (Mouloya). Kama iliyokuwa Numidia, majimbo hayo mawili ya Mauretania yalitawaliwa moja kwa moja na mfalme.

Kuundwa upya kwa mipango ya kijeshi katika Afrika kaskazini kulikuwa ni lazima wakati jeshi la Afrika, Augusta III, lilipovunjwa chini ya Gordian III. Uongozi wa Kijeshi ulipewa Mwinyi wa Afrika aliyetawala majeshi yote kutoka majimbo yote ya Afrika. Jeshi lili la karne ya nne lilikuwa tofauti sana na lile la ufalme wa hapo awali. Mashambulizi ya makabila ya jangwani (Wainoor) yalisababisha haja ya kuunda jeshi jepesi lililokuwa tayari

kuchukua hatua za haraka katika maeneo ambayo hayakuwa na usalama. Nalo liliundwa na askari wa farasi na wa miguu walioandikishwa kutoka kwa wakulima walioathiriwa na Warumi ambao walikuwa wakikaa karibu na kambi. Hata hivyo, kazi ya jeshi polepole ilianza kuwa ya kurithi na ya lazima kwa mapato ya serikali. Hali hii, pasipo kukuudiwa ihiathiri ubora wa jeshi. Mbali na jeshi kuwa jepesi, kali na jasiri, lilikuwa na askari-wakulima pia (*walimitanei*) waliopewa mashamba. Wanajeshi hawakulipa kodi, lakini nao walitakiwa walinde sehemu za mpakani na wakabiliane na uvamizi wowote ambao ungetokea. Kama wale waliokuwako Mashariki, hao Walimitanei wa Mauretania Tingitana walipangwa katika vikundi vya Jadi ilihali majimbo mengine ya Afrika yaligawanywa kulingana na mazingira ya kijografia. Kila sehemu ilipokea amri kutoka kwa afisa aliyeitwa 'Praepositus Limitis'. Ushahidi mbalimbali wa kiakiolojia hasa ule uliopatikana sehemu ya mashariki unaonyesha kwamba Walimitanei walikusanywa kando kando ya mashamba yaliyozungushiwa ngoine na walitegemea kilimo. Mara kwa mara walimwagilia mashamba yao kwa mifereji. Kwa hivyo walihusika katika ustawishaji wa kilimo na makazi kwenye mipaka ya Sahara wakapafanya pawe mahali pa biashara na makutano ya kiutamaduni badala ya msitari wa kutenganisha majimbo ya Kirumi na sehemu huru ya nchi hiyo ambayo ilibakia chini ya Waberiberi.

Wakati ambapo mabadiliko ya kijeshi yalikuwa yakifanywa, marekebisho muhimu ya usimamizi wa majimbo yalikuwa yakifanywa pia. Sasa imefahamika kwamba mageuzi hayo yalifanywa polepole kwa kuzingatia mahitaji na hali zilizokuwapo katika kila jimbo. Ili kuimarisha uwezo wa kifalme, na wakati huo huo kuondoa uwezo wa magavana ambao mara kwa mara ulikuwa mikononi mwa wale waliojitwalia bila haki, na ili kuongeza mapato kutokana na kodi ili kugharamia shughuli za ulinzi dhidi ya vitisho vya mashambulizi mipakani, Afrika iliyotawaliwa na magavana wa Kirumi iligawanywa katika majimbo matatu yaliyojitegemea. Kwa upande wa kaskazini, Zeugitana au kwa maana kamili ya jina hilo - jimbo la gavana, lilienea kusini hadi kufikia msitari ulio kati ya Ammaedara na Puppit karibu na Hammamet; kwa upande wa magharibi ilijumuisha Kalama, Numidarum ya Thubursi na Theveste. Hata hivyo, gavana aliyekuwapo Kariteji alikuwa afisa muhimu sana. Alikuwa - Klarissimas - ambaye baada ya muda wake wa kazi, alikuwa amefikia upeo wa kazi ya kibalози na alikuwa mmoja wa watu maarufu. Magavana hawa wa karne ya nne walikuwa, mara kwa mara wa ukoo wa Kiafrika. Kila wakati walisaidiwa na mabalozi wawili ambao kwa kawaida walikuwa na unasaba nao, mmoja wao alikaa Kariteji na mwingine alikaa Hippone.

Jimbo la Byzacium lilitokana na jimbo la gavana. Lilienea kutoka mstari wa Ammaedara-upput hadi kufikia malango ya Tacape. Kwa upande wa magharibi, lilijumuisha maeneo ya Maktar, Sufetula, Thelepte na Kapsa. Hata hivyo, upande wa kusini, vituo vya ulinzi havikuwa chini ya utawala wa gavana wa jimbo la Byzacium, ambalo kama jimbo liliilotawaliwa na gavana, halikuwa na majesli. Kwa hivyo vituo vilivyokuwako karibu na Chott el-Jerid vilikuwa chini ya Numidia, ambapo vile vilivyokuwako kusini-magharibi vilikuwa chini ya usimamizi wa Tripolitania. Gavana wa Byzacium ambaye aliishi katika Hadriinet, kwanza alikuwa wa daraja la wajuzi wa

wapanda farasi maarufu na alikuwa na cheo cha hakimu wa Kirumi. Labda wakati wa enzi ya Constantine na baada ya mwaka 340 alifikia hadhi ya balozi.

Katika upande wa kusini-mashariki, jimbo jipya la Tripolitania lilikuwa na sehemu mbili tofauti: mwambao wa pwani ulioenea kutoka Tacape hadi madhabahu ya Philaeni, ambao ulikuwa chini ya gavana na pengine hakimu wa Kariteji; na katika sehemu za bara, eneo la Tripolitania, hadi kufikia karne ya tatu lilikuwa chini ya utawala wa amiri wa jeshi la Augusta III, gavana wa jimbo la Numidia. Eneo hili lilikuwa ni pamoja na Jeffera na Matimatas, na lilienea hadi ncha ya kaskazini ya Chott-el-Jerid. Jimbo la Numidia lilikuwa na kijia chembamba cha kuelekea baharini kati ya milima ya Edough, kwa upande wa mashariki na mdomo wa mto Ampasa, kwa upande wa inagharibi. Lakini kuelekea kusini, eneo lake lilipantuka kuanzia sehemu ya mashariki kabisa ya Chott-el-Hodna hadi malango ya Thevesta. Mwanzoni eneo hili liligawanywa katika kanda mbili; moja ikiwa na eneo tulivu la miji ya shirikisho la zamani la Cirta lililozunguka mji mkuu wa Cirta na kanda ya pili iliyokuwapo milimani na ambayo ilikuwa na misukosuko katika sehemu ya kusini. Lambaesis ndiyo yaliyokuwa makazi yake makuu, lakini iliunganishwa tena katika mwaka wa 314. Hata hivyo, iliendelea kutawaliwa na gavana mwenye cheo cha mpanda farasi aliyekuwa na uwezo wa kiraia na kijeshi na aliyekuwa na cheo cha 'praeses' hadi mwaka 316. Katika mwaka huo serikali ya kiraia ilikabidhiwa maseneti wakiwa na majina mapya ya 'Consularis Provinciae', wengi wao walikuwa wa tabaka tawala la Kirumi. Hii ilitokana na masilahi ya hili tabaka tawala ambayo yalilihusisha na jimbo hilo tajiri. Cirta ulikuwa mji mkuu wa pekee na ulipewa jina la Constantine kwa heshima ya mfalme.

Tatizo la kutengeneza upya mipango ya utawala wa majimbo ya Mauretania katika karne ya nne lakabiliwa na swali lenye umuhimu mkubwa: Je, Diocletian aliwahamisha watu wa bara ya Tingitana na sehemu yote ya magharibi ya Casariensis kabla ya kuchukua hatamu za uongozi? Kwa mujibu wa utafiti wa hivi karibuni, kuna wasiwasi mkubwa kama eneo lililoko magharibi ya Mauretania Caesariensis lililihamwa. Kwa upande mwingine yakubalika kwamba Diocletian aliwahamisha watu wote kutoka eneo lililokuwako kusini mwa Oued Loukkos katika Mauretania Tingitana katika mwaka 285. Hata hivyo, Urumi inaonekana kuwa ilidumisha tu uhusiano wa shughuli za meli pamoja na miji ya pwani, na hiyo ndiyo sababu sehemu kama Sala ziliweza kuendelea kuwa chini ya Konstantine, na kuendelea kuwa katika dola ya Kirumi. Aidha, Diocletian aliitenga sehemu ya mashariki ya Mauretania Caesariensis ili kuunda jimbo jipya: hili lilikuwa Mauretania Sitifensis na mji wake mkuu ulikuwa Sitifis ambao sasa unaitwa Setif. Mwisho, Mauretania Tingitana ilitenganishwa na sehemu nyingine za Afrika kwa sababu za kiutawala na kuunganishwa na dayosisi iliyoungwa na majimbo ya Kihispania.

Ukoloni na Upangaji wa Miji

Kama ulivyokuwa ustaarabu wa Kigriki, ustaarabu wa Kirumi ulihusu hali ya miji tu. Kiwango ambacho jimbo lilikuwa limestaarabika na kuchukua utauaduni wa Kirumi kilipimwa kwa kuangalia kuwepo kwake karibu na miji, Katika majimbo ya Afrika na hasa



19.1 *Sanamu kutoka Sousse: Msichana akiandika Aeneid (Picha, Makumbusho ya Bardo, Tunisi)*



19.2 Sanamu kutoka Chebba. ushindi wa Neptuni (Picha, Makumbusho ya Bardo, Tunis)

Afrika iliyotawaliwa na magavana maisha ya mijini yalistawishwa sana. Majiji yasiyopungua mia tano yamehesabiwa katika Afrika Kaskazini yote.

Katika kipindi cha Jamhuri, hakuna mji uliokubaliwa kuwa na uraia wa Kirumi. Kulikuwako na miji saba tu yenye asili ya Kifoeniki, iliyokuwa na kiwango fulani cha kujitegemea lakini haikuweza kuepuka mabadiliko ya kisiasa. Hii ilikuwa miji ambayo iliunga mkono Roma wakati wa vita vya Puniki. Asasi za kimapokeo zilitambuliwa rasmi na pia hazikutakiwa zilipe kodi ya ardhi iliyoitwa - *Stipendium* (Ijara). Wakati huo huo utawala wa Kirumi ulizivumilia ingawa haukuzilinda kisheria tasasi za miji mingine ya Afrika ambayo iliendelea kutumia mfumo wa utawala wa Kifoeniki na kuongozwa na masufeti na mabaraza ya watu mashuhuri na huku ikiendelea kulipa kodi ya ardhi. Kwa hiyo, hakuna uwezekano kuwa wakoloni waliishi katika Kariteji tu. Baadaye walitawanyika katika miji kadha. Bila shaka ilikuwa muhimu pia kuwanyang'anya mashamba wale waliokuwa nayo na kuwahamishia kwingineko. Matokeo ya majaribio ya mwanzo ya Urumi ya kuanzisha koloni katika Afrika yanajulikana sana. Kwa sababu za kisiasa zilizotokana na chuki waliyokuwa nayo wafalme wa Kirumi dhidi ya G. Graskusi, kiongozi aliyependwa na watu na ambaye aliongoza juhudi za kuleta mabadiliko na pia kwa sababu za kiuchumi zilizotokana na ufukara wa walowezi na kwa kiasi fulani umasikini wa wakulima, mpango huo ulishindwa. Kwa hiyo, ilikuwa ni dhahiri kwamba mpango wa ukoloni, ulikuwa ni kisingizio cha kukipindua chama kilichopendwa na watu na kuwaruhusu matajiri, maseneti na makabaila kujinyakulia ardhi kubwa ya sehemu zilizokuwa zimetekwa na Jamhuri hiyo.

Kwa kufufua mipango ya baba yake wa kambo, Julius Kaisari, Augusto Oktavius alianzisha kipindi kipya katika historia ya Afrika yaani utaratibu mpya wa kisiasa na mpango mkubwa wa utawala wa kijeshi na kidini. Kwa mujibu wa orodha iliyotolewa na Pliny, ambayo chanzo chake bado kinabishaniwa sana, kulikuwa na makoloni sita ya Kirumi, *Oppida Giviun Romanorum* kumi na tano, *Oppidum latimum* moja, *ippindum immune* moja, na *oppida libera thelathini* baada ya muda mfupi.

Wafalme waliomfuatia Augusto waliendeleza sera yake. Wakati wa utawala wa Marcus Aurelius, kulikuwapo zaidi ya makoloni 35 yaliyoawanyika katika majimbo yote ya Afrika. Kama ilivyo kawaida, wahamiaji walikuwa wapiganaji waliotumika katika vikosi vilivyovunjwa kutokana na kuundwa upya kwa jeshi. Walikuwapo pia Wataliano waliofukuzwa au kuhasiriwa na mgogoro wa kilimo katika peninsula. Hata hivyo, idadi ya Wataliano hao haikuwa kubwa sana, kuweza kuyafanya majimbo ya Afrika yawe makazi ya kuishi tena. Lakini njia ya busara iliyotumiwa kuyaanzisha makoloni hayo ilizingatia masuala ya kiulini na kiuchumi.

Hali ya Kiuchumi

Idadi ya Watu

Wakati huu hatuna makadirio ya idadi ya watu waliokuwa wakiishi katika dola la Kirumi

wakati huo hata kama tungefanya makisio. Ilikuwa muhimu kuwahesabu watu mara kwa mara kwa ajili ya mipango ya mapato ya serikali, lakini hatuna takwimu sahihi za hesabu hizo. Kwa hivyo, hatuna la kufanya katika jambo hili, ila kutumia njia zisizo kamilifu katika kujaribu kupata hesabu hizo na idadi ya watu: Njia hizo ni kama vile matumizi ya kizio cha wastani wa wingi wa wakaaji katika kukokotoa idadi ya watu na pia kwa kutumia sababu za kijografia pamoja na sababu nyingine kadha katika juhudi ya kutaka kujua idadi ya wakazi wa mji fulani.

Hivi karibu, A. Lezire anetoa maoni kuhusu idadi ya watu katika miji, anbayo yanatofautiana na yale ya G. Charles-Picard. Akichukua msimamo sawa na G. Charles-Picard, Lezire amedai kwamba hari za maisha na wingi wa watu katika Sahel ya Tunisia zilikuwa sawa karika Enzi za kati na zile zilizokuwapo enzi za kale. Amejariibu kuhesabu idadi ya watu wa Sousse kufikia mwisho wa karne ya kumi, na ile ya watu wa Kariteji kati ya 150 na 238. Hatimaye anepata jumla ya wakazi milioni moja na laki tatu wa mijini. Ikiwa tutakubaliana na idadi hii, huku tukiishikilia idadi ya jumla ya watu wote, iliyotolewa na C. Courtois, basi ni dhahiri idadi ya wakazi wa sehemu za mashambani zingekana sahihi zaidi. Hata hivyo, njia mpya ya kukabiliana na matatizo haya ya idadi za watu imependekewa na utafiti wa hivi karibuni. Badala ya kutegemea tu matokeo ya hesabu za watu wa nyakati za kale, wingi wa watu, nambari zinazofanana za Bomus na Insulae, na idadi ya wapokeaji wa misaada ya nafaka, sasa tunahesabu pia idadi ya makaburi kwa kila kizazi na malipo yaliyoitwa Summae Honorariae yaliyolipwa na mahakimu wapya kwa viwango vilivyotofautiana kulingana na vyeo vyao na ukubwa wa mji.


Kilimo

Ni dhahiri kwamba kilimo kilikuwa msingi wa uchumi wa nyakati za kale. Katika Afrika wakati wa utawala wa Kirumi, ardhi ndiyo iliyokuwa chanzo muhimu zaidi na chenye thamani sana cha utajiri na hali ya kijamii. Ni dhahiri pia kwamba Afrika ndiyo iliyokuwa ghala la nafaka la Roma. Maneno haya wakati mwingine yametumiwa kuonyesha kwanba kwa wakati fulani, Afrika ilikuwa na chakula kingi sana ikilinganishwa na ufukara na siku hizi ili kudhihirisha babari za kupotosha kuhusu hali mbaya inayowasibu Waafrika, bila kuzingatia matatizo makubwa ambayo yamesababisha hali hiyo ya kutoendelea. Hapa hatuna budi kukariri ukweli ambao hauwezi kupuuzwa na wanahistoria. Ni kweli kwamba Afrika ilikuwa ghala ya nafaka kwa Urumi kwa sababu, ikiwa mshinde, ililazimika kutoa nafaka ya kutosha kwa mshindi wake kama ushuru. Chini ya utawala wa Augusto, kwa mfano, Warumi wapatao laki mbili walipokea bila inalipo, posho ya lita 44 za nafaka kila mwezi ambazo zilifikia jumla ya pishi milioni kumi na sita. Kwa vyovyote vile nadharia kuhusu ustawi wa hali ya juu na mavuno makubwa sana ya ngano wakati wa utawala wa Kirumi imepotoshwa sana na mwanajografia J. Despoia.


Wakati wa mwanzo ushindi wa Kirumi ulisababisha kuzorota kwa kilimo katika uchumi wa Afrika kwa jumla. Chora za Kikariteji zilipuuza na utamaduni wake wa Arbori ukaachwa, kwa kuwa Italia ambayo ndiyo iliyokuwa ikisimamia masoko ya divai na

mafuta ilihakikisha kwamba hakukuwako na ushindani wowote katika shughuli hizi zenye faida. Ukuzaji wa nafaka ndio pekee ulioendelezwa, na, katika enzi ya Augusto, ulianza kupanuliwa kwa sababu za kisiasa na uliendelea hadi mwisho wa utawala wa Kirumi hususa kwa madhumuni ya kuhakikisha kwamba Warumi wa kawaida wanapata chakula cha kutosha. Baada ya Roma kupanna zaidi mipaka upande wa magharibi na kusini, wakati ambapo ilikuwa imeanza kutekeleza sera ya kuwazuilia watu wa makabila mbalimbali katika sehemu zilizotengwa, huku ikitekeleza sera ya kustawisha ardhi, hasa kwa kupanua miradi ya nguvu za maji, kulikuwako ongezeko kubwa la zao la mahindi. Kufikia wakati Nero alipokuwa akitawala, tunafahamu kuwa Afrika, ilikuwa ikitoa nafaka ya kutosha kwa makao makuu ya dola hiyo kwa miezi minane kwa mwaka. Kwa hiyo, imehesabiwa kwamba Afrika ilikuwa ikitoa pishi milioni 288 au kilo 1,260,000. Wakati wa ustawi mkubwa katika Afrika, tokea katikati ya karne ya pili hadi mwaka 238, hali hiyo iliimarika, kutokana hasa na kulimwa kwa ardhi mpya katika Numidia na pia zile sehemu za majimbo ya Mauretania. Lakini Afrika ilibidi ilipe kodi mpya za serikali, wakati *annona* za kijeshi zilipogezwa katika enzi za utawala wa Septimus Severus, na kuwa malipo ya mara kwa mara. Tokea karne ya pili na kuendelea mbele, rasilimali nyingi katika majengo ya umma ni dalili ya usitawi miongoni mwa watu wa matabaka ya juu na hasa miongoni mwa tahaka la kati katika miji. Ukweli ni kwamba, wakati huo, serikali ya kifalme iliruhusu shughuli mbalimbali za kustawisha uchumi wao, ambapo Italia ilikuwa ikikabiliwa na mzozo ambao tayari ulikwishakuwa tatizo wakati wa utawala wa wafalme wa Claudia. na ambalo lilikuwa bado halijasuluhishwa.

Tokea mwanzo Afrika ilipokaliwa na Warumi, alama ya ukoloni wa Kirumi ilikuwa ngwe za miraba. Ardhi ya Afrika iligawanywa katika miraba ya mita 710 toka upande mmoja hadi mwingine ambayo ilitoa mfano wa ubao wa sataranji. Baada ya ardhi kuwa mali ya Warumi kutokana na ushindi wao, ziligawanywa katika makundi kadha chini ya sheria ngumu za umilikaji mali ambazo zilikuwa zikibadilika mara kwa mara. Mauretania ndiko pekee ambako hakukuwako vizuizi, na kwa hali hiyo, mali ya kikabila ilipotea kutokana na wakoloni kuongeza kila mara maeneo ya ardhi waliyomiliki. Mpango mkubwa uliodhamiria kuyazuia makabila katika sehemu fulani ulianzishwa wakati wa utawala wa dola ya kwanza na kuendelezwa zaidi katika nyakati za Severan, wakati mipaka iliposogezwa mbele hadi Tripolitania, Numidia na Mauretania. Operesheni hii ilisababisha unyang'anyi mkubwa wa mali ya makabila yaliyofukuziliwa jangwani. Hata hivyo, wazalendo wenye mashamba waliokuwa wawakilishi mijini, ambao mali zao hazikutwaliwa kwa manufaa ya walowezi wa Kirumi na Kilatini, kwa jumla waliendelea kuwa na mashamba yao alimradi tu walipe ushuru ambao ni miji michache sana ya kiasili iliyosamelewa kutolipa. Aina nyingine za mali zisizoondoshewa ilikuwa ardhi iliyogawiwa raia wa Kirumi, askari wa zamani, wahamiaji wa Kirumi au wa Kitaliano wenye mapato madogo ambao walilowea katika makoloni hayo, *Oppida Civium Romanorum*, Pagi. Hata hivyo wakati huo, hali za kisheria za ardhi lizo za miji ya kiasili na zile za mali za miji ya Kirumi hazikutambulika wakati katiba za manispaa zilipoanzisha mtindo wa kushirikisha jumuiya za Autochthonous.



19.3 *Mfereji wa maji wa Cherchell, Algeria (P. Salama)*



19.4 *Tripoli (mji wa kale wa Qea, Libya) tao la ushindi la Marcus Aurelius (P. Salama)*

Hadhi na mipango ya miliki za huo ufalme mkuu twazijua kutokana na maandishi manne muhimu na ushahidi mwingine uliotolewa na waandishi wa maneno ya nakshi wa Kiafrika wenye maelezo mengi. Maandishi hayo yametufahamisha mambo muhimu sana, kama vile *Lex Manciana* na *Lex Hadriana* ambazo hazikuwa "sheria" kwa maana ya sheria za Kirumi, bali ni kanuni za kazi. Katika maoni ya waandishi wengi, kanuni hizi ziliwahusu watu wote (ager publicus) waliokuwapo katika ufalme huo. Habari tulizo nazo za kutosha ni zile tu zinazohusu jinsi miliki za mfalme zilivyotawaliwa. Miliki zote zilikodishwa kwa watu waliozisimamia waliojulikana kama "Conductores" ambao walijiri mameneja (villioi) wa kuziendesha. Meneja alistawisha mwenyewe miliki hiyo au sehemu yake. Pengine aliwatumia watumwa na vibarua wa mashambani, pamoja na kazi za lazima zilizodaiwa kwa walowezi waanzilishi. Walowezi hao waanzilishi walikuwa watu huru ambao walilima sehemu kubwa ya miliki kama wapangaji wadogo wa "conductores." Lengo kubwa la *Lex Manciana* na *Lex Hadriana* lilikuwa kujua haki na wajibu wa "conductores" na mameneja wao (villioi), kwa upande mmoja na zile za wakulima (coloni) kwa upande mwingine. Kanuni ya msingi ilikuwa kwamba, kwa kufuata utaratibu wa malipo ya kutoa thuluthi moja ya mavuno ya kila mwaka na kufanya kazi bure kwa siku fulani katika shamba lililokuwa chini ya usimamizi wa Meneja, wakulima wangekuwa na haki ya kutumia vishamba vyao wapendavyo kama vile kuwaachia warithi wao na hata kuvuza, mradi tu yule aliyenziwa anaendeleza utaratibu huo wa kilimo kwa miaka miwili mfululizo. Uongozi wa miliki hizo ulisimamiwa na kundi maalumi la maafisa wa kifalme.

Viwanda na Biashara

Kwa jumla imeonekana kwamba maandishi wa maneno ya nakshi na michoro iliyochorwa katika minara ya ukumbusho inatupa taarifa kidogo sana kuhusu Afrika kuliko katika majimbo mengine ya magharibi juu ya maisha ya mafundi mchundo na wafanyakazi wengine wa kuajiriwa. Hata hivyo, japokuwa ufuaji wa metali unaelekea kuwa haukuenea sana katika majimbo ya Afrika, hatuna budi kuepuka kutoa maelezo ya ujumla. Inaweza kudokezwa, kwa mfano, kwamba kumbukumbu za mashairi zinaeleza habari chache sana kuhusu wasanifu majenzi na wajenzi, ingawa kazi zao ziliacha mabaki mengi sana katika sehemu nyingi za kiakiolojia za Afrika. Kwa bali yoyote, kurvia kwa tekuolojia wakati wa utawala wa Kirumi hakukusaidia kuleta maendeleo nukubwa katika viwanda vya zamani. Katika hali hii, viwanda mashuhuri vilihusika katika utayarishaji wa bidhaa za kilimo na hasa utengenezaji wa mafuta ya mizeituni. Mabaki ya vinu vya kukamulia zeituni ambavyo vilipatikana kwa wingi sana katika eneo lote kuanzia Sefetula hadi Thelepte na Tebessa, yanadhahirisha umuhimu wa mafuta katika uchumi wa zama za kale, kama mafuta muhimu kwa matumizi ya binadamu tu bali pia kama mafuta ya pekee ya kutumiwa kuwaslua taa na kutengeneza sabuni za kuogea.

Kiwanda cha kutengeneza bidhaa za udongo, ambacho kimehusiana kwa kiasi fulani na shughuli za utengenezaji wa mafuta ya mizeituni, kilitosheleza mahitaji ya taa na vyombo, mbali na kutengeneza vyombo vya matumizi ya nyumbani. Katika nyakati za Puniki, viwanda vya selemu hiyo vilijishughulisha na utengenezaji wa bidhaa za kila siku, na

mifano mizuri zaidi ya usanii wa mfanyanzi iliingizwa nchini kwa mara ya kwanza kutoa Ugriki, na Etruria na baadaye kutoka Italia ya Kusini.

Kwa hiyo, Afrika ilifanikiwa kujikomboa dhidi ya kutawaliwa kiuchumi, na biashara zake za nje zilipata tena umuhimu wake wa nyakati za Puniki. Zana na huduina za bandarini zilipanuliwa ili kukabiliana na kuongezeaka kwa bidhaa za kuzwa nje kutoka bara na kuweza kukabiliana na kiasi kikubwa cha nafaka na mafuta ya kusafirishwa kwa meli hadi Italia. Biashara kubwa zilifanywa katika bandari ya Ostia, ambayo ilikuwa mlango wa bahari wa Urumi. Katika eneo la Ostia kumepatikana majengo yapatayo tisa miongoni mwa ofisi za mashirika ya meli, yaliyokuwa mali ya mashirika ya Kiafrika ya Mauretania Caesariensis, Musluyum, Hippo Diarrytus, Kariteji Kurubis, Missus, Gummi, Sullektum na Sabratha. Hawa *domini navium* au navioularii, waliounda mashirika, walihusika kwa pamoja na usafirishaji wa bidhaa hadi Italia, walipewa upendeleo maalum kuanzia enzi ya Klaudius, na walikuwa na mipango mizuri hadi kufikia nyakati za Septimius Severus, kulingana na kanuni za uhusiano huru.

Maandishi ya zama za zama ambayo bado yanaonekana pamoja na masalia ya akiolojia na maandishi ya nakshi yanatoa maelezo mengi kuhusu biashara ya ndani ya Afrika. Tunafahamu kutokana na kumbukumbu kama hizo kwamba - *nundinae* - ambazo zilikuwa aina ya maonyesho, zilifanywa katika vituo vya vijijini nnamo siku mbalimbali za juma, kama masoko ya sasa. Katika vijiji, masoko ya vyakula (macela) yalianzishwa katika sehemu ya mraba iliyozungukwa na baraza yenye vibanda vya wafanyabiashara mbalimbali. Makao kadha kama hayo yanechiimbuliwa, hasa Leptis, ambapo vibanda mbalimbali vilikuwa na zana za kupimia urefu na ujazo ambazo zilikuwa zikikaguliwa na maafisa wa manisipaa. Shughuli nyingine za kibiashara zilifanyiwa katika baraza au katika maduka na masoko yenye paa yaliyokuwa katika miji (ambamo walikuwapo wenye mabenki, wabadilisha fedha, wauza vileo, wafanyabiashara wa nguo na kadhalika). Barabara ambazo awali zilijengwa kwa madhumuni ya kufanikisha ukoloni, mara zilianza kuwa na manufaa makubwa kwa biashara hizo kwa kuwa zilirahisisha usafirishaji wa bidhaa. Wakati wa utawala wa Augusto na wale waliotawala baada yake, barabara mbili muhimu sana ziliunganisha Kariteji na sehenu za kusini-magharibi, kupitia bonde la Miliana, na sehemu za kusini-mashariki kupitia pwani. Sehemu ya tatu ya pembe tatu hii ilijumuisha barabara kuu ya Amnaedara-Tuoape, ambayo ilikuwa njia ya kwanza kuwa na alama za kuonyesha umbali au urefu. Chini ya utawala wa Flavian, na Waantonines wa kwanza, barabara zilipanuliwa sana hasa kwa ujenzi wa barabara kuu ya Kariteji - Theveste. Kando ya vituo vya zamani vya kijeshi vya Theveste na Lambaesiz barahara zilijengwa kuzunguka milima ya Aures na Nementacha na kwenda kaskazini kuelekea Hippo-Regius.

Utafiti mwingi unefanywa juu ya masuala kadha ya kiufundi kuhusu barahara za Kirumi: kama vile kuhusu jinsi zilivyojengwa, madaraja, na ulalo mrefu (unaovuka korongo la kupitisha reli ya gari la moshi), na nyumba za wageni. Watawala wa Kirumi walitanibua umuhimu wa kipekee wa barabara kuu, dhima yake kiutawala, na pia dhima yake ya kiuchumi na hivyo kutilia maanani, kwa mfano, njia ya biashara ya Marmar kati ya

Simitthu na Thabraca na uchunguzi umekwishafanywa mahali ambapo maghala ya nafaka na maghala mengineyo yalikuwapo katika njia panda na katika sehemu nyingine katika barabara ambapo nafaka na mafuta vilitolewa kwa wakusanya kodi.

Uhusiano kati ya Majimbo ya Kiafrika na watu wa Sahara

Imejulikana kwa muda mrefu kwamba Warumi walikuwa na ngome tatu kubwa katika Sahara kwenye mipaka ya jangwa, kusini ya Tripolitana. Ngome hizo zilikuwa Bu-Njem, Gheria el-Gherbia na Ghadames ambayo iliitwa Gidamus nyakati za kale. Zilikuwa katika mpaka kati ya jangwa na sehemu moja iliyokuwa chini ya utawala wa Warumi na iliyokuwa ikikaliwa na wakulima ambao mashamba yao yalizungukwa na ngome, na walikuwa wakikuza mizeituni katika mabwawa ya maji ya Wadis. Katika eneo hili, ustaarabu wa kiasili ulikuzwa, ukiwa na alama kubwa ya mila za mapokeo ya sehemu hiyo ambazo zilikuwa zimeathiriwa na mila za Puniki. Mila za asili zilizochanganyika na tabia za Puniki, zilionyeshwa hasa kwa maandishi mengi katika alfabeti za sehemu hiyo, na kudumu kwa lugha ya Puniki hadi usiku wa kuamkia uvamizi wa Waarabu, kulithibitisha kwamba yalikuwa ya kuweza kuigwa, kwa maisha mapya yaliyoanzishwa na Warumi. Ngome hizo zilistimamia njia muhimu zilizounganisha pwani na Fezzan, nchi ya Wagaramante. Mwaka wa -19, Korlelius Balbus aliwashambulia hawa Wagaramante, na kwa inujibu wa Pliny, Kornelius aliishinda miji na ngome zao kadha zikiwa ni pamoja na Garama na Cidamus. Baadaye, labda wakati wa utawala wa Domitian, safari iliyoongozwa na Julius Maternus ilianza Leptis Magna na ikafika Garama. Akiwa pamoja na mfalme wa Garamante na jeshi lake, safari hiyo iliendelea hadi nchi ya Ethiopia na eneo la Agisymba ambapo tunaambiwa kuwa vifaruu walionekana. Hii inaonyesha kuwa Warumi walitaka zaidi Fezzan, mradi tu hiki kituo cha kudumu cha msafara kinawawezesha kuufikia mpaka wa eneo la Sahara katika Afrika. Msafara luo wa kibiasham ulirudi na watuniwa wa Kiafrika, manyoya ya mbuni, wanyama wa mwinu, zumaradi na vito vyekundu kutoka sahara. Kwa kubadilishana, majimbo ya Kirumi yalitoa divai, vyombo vya chuma, vyombo vya udongo, nguo, na vyombo vya vico, kama ilivyodhihirishwa na vitu vilivyochimbuliwa, hasa katika makaburi ya Fezzan.


Kujitokeza kwa Waberiberi wa Kirumi na matatizo ya Jamii ya Kiafrika

Wakati wa utawala wa Augusto na wale waliotawala baada yake, kulikuwapo na aina tatu za watu katika majimbo ya Afrika zilizotofautiana kutokana na sheria ambazo ziliwatawala, na pia desturi na lugha zao. Hawa walikuwa wahamiaji wa Kirumi au Kitaliano. Wakariteji, na wakazi wa Kilibya ambao walikuwa wameshirikisha asasi na desturi za ya Puniki katika mila zao japokuwa mila zao zilikuwa nyingi zaidi; wahamaji wa Kilibya ambao walikuwa wamezuliwa katika sehemu fulani au walikuwa wamefukuzwa kabisa kutoka sehemu zao zilizokuwa na rutuba ambazo walikuwa wamelazimishwa kuziacha. Imesemwa mara nyingi, na kwa usahihi kabisa kwamba majimbo ya Afrika hayakuchukuliwa kama makazi. Wakati wa utawala wa Hadrian, makoloni ya askari wa



19.5 Timgad mji wa kale wa Thamagudi, Algeria: Barabara kuu na tao la Tryjan

19.6 Lebda mji wa kale wa Lepts Magna, Libya: uwanya wa michezo ya kaugiza wa Kirumi.



zamani hayakuanzishwa tena katika Afrika. Yale yaliyokuwapo Numidia, kuanzia wakati huo yalianzishwa kwa manufaa ya wanajeshi walioandikishwa katika miji ya Afrika. Kama tulivyooona hapo juu, hadhi za wanajeshi hao zilizidi kuimarika hadi walipofanywa Warumi kamili. Wazalendo wote waliokuwa wakazi wa miji walishirikishwa, na hasa wale waliokuwa tajiri zaidi ambao walitaka, kwa njia hiyo kujiepusha na kudhalilishwa kijamii, kiuchumi, na kisheria kulikotokana na ushindi wa Warumi, wakati katiba ya Antonina ilipotangazwa rasmi katika mwaka 212. Katiba hii ilitoa uraia wa Kirumi kwa wakazi wote waliokuwa huru katika ufalme huo waliokuwa hawajaupata isipokuwa Wadeditici. Septimius Severus alikuwa amekwishafuata mfano wa Antonine kwa kuipandisha vyeo, miji mingi kufikia cheo cha manisipaa au hata Koloni (*colonia*). Hivyo, watu ambao hawakuwa raia wakawa wachache kiasi kwamba kuwepo kwa haki duni za kisheria kuliendelea kupungua, kukilinganishwa na haja ya kurahisisha utaratibu wa utawala na ukusanyaji wa mapato ya serikali na niwelekeo unaopendelewa kisiasa, kisheria, kimaadili na kidini. Tofauti za kitaifa zinaelekea kutoweka katika miji ambapo zilikuwa nyingi sana hasa katika Afrika kabla ya wakati huo. Tofauti za kijamii zihendelea kuwepo mijini. Matabaka mawili ya juu zaidi ya Maseneta na wapanda farasi maamfu yalifurahia hadhi iliyotokana na mali aliyokuwa nayo intu na zilizoashiria uwezo na vyeo. Ingawa sifa ya mtu kuwa na unali ilihitajika, hii yenyewe haikutosha kwani kanuni ya kurithi ilikuwa ikifuatwa kila mara. Isipokuwa pale infaline anapoamua kumtuza mtu cheo cha Seneta au Umwinyi kama upendeleo maalum, vyeo na hadhi hizi hupatikana tu kwa haki ya kuzaliwa. Seneta wa kwanza mwafrika alitoka Cirta ambako aliishi wakati wa utawala wa Vespasian. Karne moja baadaye, karibu mwaka wa 170, idadi ya maseneta Waafrika ilikuwa imeongezeka kufikia karibu mia moja. Kundi hilo la maseneta Waafrika ndilo lililokuwa la pili kwa ukubwa likifuatiwa na kundi lile la Wataliano. Mwinyi wa kwanza Mwafrika anayejulikana katika historia, ambaye alitoka Musti, alipewa pete ya dhahabu na Tiberius. Ilipofikia wakati wa Hadrian kulikuwepo Mamwinyi elfu kadha katika Afrika na Numidia. Hivyo tunaona kwamba kujitokeza kwa Waberiberi wa Kirumi kulikuwa tukio muhimu katika wakati wa Antonine-Severan, wakati ambapo Waafrika walikuwa wakitekeleza wajibu muhimu huko Roma na katika dola nzima.

Nguvu muhimu za kijamii zilizowezesha himaya ya awali, na kwa manufaa ya Wafalme wenyewe, kutia damu mpya katika kanuni za utawala na kuhakikisha kwamba kanuni ya mpanda farasi nahifadhiwa katika ufanisi wa hali ya juu. Pia sifa binafsi zinazohitajika kwa utekelezaji wa wajibu wake kwa pande zote mbili yaelekea zilikuwa za watu wa tabaka la kati katika miji, ambao wanaitwa mabwanyenye.

Tabaka la kati la Decurion ndio lililokuwa kiini cha jamii zilizochukua kabisa utamaduni wa Kirumi katika Afrika. Chini ya ufalme wa zamani, matabaka hayo yaliandikisha wanachama wake kutoka matabaka fulani tu ya makundi ya wenye kumiliki mashamba mtu wa tabaka la Decurion, aliishi mjini kutokana na mapato yaliyotokana na mali yake lakini hakawa na - *latifundium* - wala hakawa mkulima na hata ikiwa aliishi kutegemea ardhi yake, alipendelea zaidi maisha ya kibwanyenye. Aghalabu alitajirika. Ili kujipatia sifa mjini pake kwa kutaka apate shukrani kutoka kwa wakazi wenzake mjini



19.7 *Haidra, Tunisia: Picha ya jumba ya ngome ya karne ya Byzantine*

19.8 *Haidra, Tunisia: Picha ya undani ya ngome ya Byantine*



hapo. Hivyo ilimbidi atoe zawadi ambazo alizigawanya kulingana na kiasi cha sifa alichohitaji apewe na pia kiasi cha ukarimu wake. Alitayarisha michezo ya manisipaa, kutoa zawadi ndogo ndogo za chakula, na pesa kwa maskini ama kutunza majengo ya umma. Wote walikuwa na dhamira ya kuwa na baraza leo kamili likiwa na sanamu, zikiwa kwenye viweko vyao, nyumba yao ya Seneti, ukumbi wao maalum kwa mahakama za sheria, bafu, maktaba, majengo mazuri ya gharama kubwa kwa michezo ya manisipaa, pamoja na hekalu nyingi sana kwa heshima ya miungu rasmi au ya asili.

Hata ikiwa nadharia kuhusu kudhoofika kwa miji katika karne ya nne lazima ichunguzwe tena kwa kuwa kuna ushahidi wa maandishi unaoonyesha kwamba kulikuwepo na shughuli nyingi za ujenzi. Akiolojia imeonyesha kwamba kulikuwapo na majengo mazuri ya gharama kubwa mno hata wakati wa karne ya tatu, hali ya maisha ya kijamii katika miji ilikuwa tofauti sana chini ya ufalme wa mwisho na ile aliyokuwako katika ufalme wa awali. Kilimo kilikuwa bado ni chanzo cha mapato ya watu mashuhuri katika miji, lakini "*decurion*" waliwakilisha watu wa tabaka la kati ambalo hadi kufikia wakati huo lilitawala kupitia halmashauri za majiji, lakini mahali pake palichukuliwa na kundi dogo la watu wenye mashamba, maaskofu, au watu wengine mashuhuri waliojitajirisha kwa kuuza nchi za nje nafaka na mafuta na kutoka mashamba yao na kwa hiyo basi kukubaliwa kuwa na vyeo katika ufalme. Watu hawa mashuhuri walifikia vyeo vikubwa zaidi katika serikali za manisipaa au majimbo. Walijenga upya majengo ya umma yaliyoharibiwa katika karne ya tatu au wakatengeneza yale yaliyokuwa yanabomoka kwa ukuukuu na kuiremba miji yao, wakijua kwamba shughuli kama hizo ziliwafungulia njia ya kupewa vyeo vikubwa zaidi. Wafalme walibadilisha maongozi yao ili yaoane na mabadiliko haya ya kijamii. Lengo muhimu lilikuwa kuhimiza ukuaji wa miji, sio tu kwa kuwa ilikuwa mojawapo ya sababu muhimu ambazo utaratibu wa utozaji kodi ulitegemea, lakini muhimu zaidi ni kwa sababu miji ilikuwa maboma thabiti dhidi ya vitisho vya watu waliodhaniwa kuwa maharamia.

Katika sehemu za mashambani, ilikuwa si kawaida katika karne ya nne kwa Waafrika mashuhuri wenye mashamba kuishi mashambani mwao peke yao. Waliendelea kushiriki kuipamba miji na kula starehe mijini. Lakini ilipofikia mwisho wa karne hiyo ya nne dalili za mwanzo za kilimo cha kikabaila zilianza kuonekana. Watawala ambao walikuwa wamezidi kujitegemea katika mashamba yao, walizidi kuzitumia haki za nchi hiyo iliyokuwa ikidhoofika, kwa kulinda mashamba yao na hata kutekeleza shughuli za kisheria katika mashamba hayo. Kuanzishwa kwa utaratibu mpya wa utozaji kodi wa *Ingatio-capitatio* kuhinufaisha zaidi hazina ya kifalme na wale waliokuwa na mashamba makubwa. Walihakikishiwa pia kwamba hapangekuwa na mabadiliko yoyote Juu ya umilikaji wa mali katika vitengo mbalimbali vya kuzalishia mali. Hivyo wale waliomiliki mashamba makubwa wawe watu wa dini au wasio na dini waliweza, kutokana na msaada wa utawala wa kifalme, kuwazuia wakulima wasijaribu kuendelea hali zao na walifaulu kuwatumikisha katika mashamba.

Maisha ya Kidini na Majilio ya Ukristo

Tawala za Kirumi hazikuzuia kuabudiwa kwa miungu ya jadi iliyoheshimiwa na

wazalendo. Madhehebu ya Kiberiberi ya 'genii' mara nyingi yaliendelea katika sehenu takatifu zilizoko mashambani ambapo yaliabudiwa katika hali zao za kizamani na za kimasikini. Lakini wakati mwingine yalichanganywa katika madhehebu ya miungu ya Kiyunani, Kirumi. kwa mfano madhehebu ya *genii* ya -urutubishaji- au maji ya afya wakati mwingine yalishindwa nguvu na yale ya Neptune, Aesculapius, au Serpis. Katika sehemu zilizokuwa na falme za Numidi, ambapo nguvu za Puniki zilikuwa kubwa na za kudumu, jamii ya miungu ya huko ilishindwa nguvu. Lakini watu wengi katika majimbo ya Kiafrika walifuata madhehebu ya Saturn na ya Kiyunani - Kirumi yaliyokuwa sawa na miungu ya zamani ya Kariteji, Dini hii ya Saturn wa Kiafrika ilikuwa ni ya kuendeleza ile ya Baal Hammon, kama vile Juno-Caelestis, Mungu mkuu wa Kariteji ya Kirumi, alikuwa, Tamit-mungu mkuu wa kike wa Kariteji ya Puniki.

Mintaarafu madhehebu rasni ya dola hiyo haikuchukua muda mrefu kabla ya kuanza kuheshimiwa katika majiji utii kwa Roma ilibidi udhihirishwe hasa kwa kuzingatia maadili ya dini ambayo yalikuwa sehemu ya ustaarabu wa Kirumi. Katika kila jiji, madhehebu ya Capitoline Traid, Jupiter, Juno, na Minerva, yale ya Mars - baba na mlinzi wa Warumi, Venus, Ceres, Apollo, Mercury, Hercules na Bacchus zilikuwa baadhi ya dini rasmi za ufalme huo na maisha ya kiroho ya Kiyunani-Kirumi. Hekalu, sanamu, minara na dhabihu zilikuwepo kila mahali kwa heshima ya miungu hiyo.

Miungu ya sehemu za mashariki za ufalme huo iliyokubaliwa bila pingamizi katika Roma, pia ililishimiwa katika Afrika ambapo ilianzishwa na maafisa, askari, na wafanyabiasham ambao walieneza madhehebu ya Isis, Mithra au Cybele. Wakati mwingine miungu hii ililingarishwa na miungu wa sehemu liizo kwa mfano Isis na Demeter au Cybele na Caelestis.

Lilikuwa jambo la kustaajabisha kwamba Kilatini kilitambuliwa kuwa lugha ya Ukristo katika Afrika kutoka mwanzo, ilihali kanisa la Kirumi lilikuwa bado linatumia Kiyunani. Kwa mujibu wa Tertullian aliyeishi kuanzia mwisho wa karne ya pili hadi mwanzoni mwa karne ya tatu, walikuwapo Wakristo wengine katika Afrika wakati huo waliokuwa wa tabaka na kazi mbali mbali. Iliwezekana kufanywa mkutano wa maaskofu sabini na mmoja katika Kariteji mnamo mwaka wa 220. Maaskofu tisini walihudhuria mkutano mwingine uliofanywa mwaka 240. Hii inadhihirisha kwamba jamii ndogo za Wakristo zilitapakaa katika miji mingi ya Kiafrika, na hii ilizusha hali ambayo ufalme huo uliifikiria kuwa ya hatari kubwa kwake. Ilikuwa kweli kwamba kwa kuikataa itikadi ya kifalme na hasa kwa kukataa kushiriki katika madhehebu ya mfalme, Wakristo walikuwa wanachukua msimamo wa chama cha upinzani. Mbali na mtazamo wake wa huruma, na uvunilivu kwa madhehebu mapya, Roma haikuweza kuafikiana na madhehebu yenye lengo la kuanzisha utaratibu uliokuwa ukizidi kupanuka, madhehebu ya vikundi vilivyoknwa vikifuata maongozi yaliyokuwa nje ya utaratibu wa taasisi rasmi. Hivyo adhabu kali, zilichukuliwa dhidi ya Wakristo waliofuata maongozi hayo yaliyokuwa nje ya utaratibu wa taasisi rasmi.

Hatuna nafasi katika maelezo haya mafupi, ya kuchunguza historia ya Ukristo katika Afrika ambayo ilifikia kilele chake katika kipindi kilichokuwa katikati ya wakati ambapo kanisa lilishinda amani mmamo karne ya mie na wakati wa kuwasili kwa Waarabu katika

Afrika kaskazini. Uchunguzi maalumu huenda ukafanywa kuhusu suala hili gumu, lihusulo utengano wa 'donatist' na pia kwa maandishi ya kikristo kuanzia Tertullian hadi Mtakatifu Augustine, ambao Hadhi zao na kazi zao zilikuwa matunda azizi ya mwisho yaliyoceleza juu ya maisha ya Kirumi katika Afrika.

Utamaduni wa Kiafrika

Baada ya kupuuzwa kwa muda mrefu na waandishi wa historia ya Kirumi, sanaa za majimbo na utamaduni uliokuwapo jirani, sasa umeanza kuzingatiwa zaidi. Hii inatokana na kuifahamu vizuri zaidi mipaka ya utawala wa Kirumi na hali zake tofauti ilizozitumia kuwasiliana na jamii za kizalendo. Aidha haiwezekani kukanusha ukweli kwamba sanaa ya jimbo lolote haiwezi kutengwa na maisha ya kiuchumi, kijamii na kidini ya jimbo hilo.

Kutokana na haya, ilikuwa muhimu, ili kuchunguza na kufahamu sanaa zilizostawishwa katika majimbo ya Afrika ya utawala wa Kirumi, kufikiria juu ya kuendelea kwa misingi ya Walibya na Kipuniki iliyoendelea kufuata utaratibu wa peke yake wa maisha na mabadiliko kwa karne nyingi.

Baadaye utamaduni wa Kifoeniki na Kipuniki, ulichanganyika na ule wa Kimisri na wa Asia na kujazwa na athari za Kiyunani baada ya kuharibiwa kwa Kariteji. Mwishowe mchango wa utamaduni wa Italia - Urumi, ukiwa ni muhimu na ambao ulipachikwa kwao, ulizusha mchanganyiko wa tamaduni ambao ni vigumu hata kuzifafanua. Imekuwa ni desturi kutofautisha tamaduni mbili katika Afrika, mmoja ukiwa rasmi yaani Kirumi na mwingine ukiwa ule uliopendwa na watu wengi, yaani wa kiasili na wa majimbo. Lakini kuna minara ambayo tamaduni hizo mbili hukutanikia na kuingiliana. Mwingiliano huo hupoteza utambulisho wa upekee wa kila moja.

Mitindo ya kazi za usanifu majenzi ya Afrika ilitoa minara ya makumbusho kama ile iliyoenea pote katika dola ya Warumi; nayo ilikuwa imechota maarifa na uzuri wake kutoka katika usanii wa Kirumi. Sanamu za mapambo na zile za miungu, wafalme na watu mashuhuri hazikutofautiana sana na zile za Italia na majimbo mengine. Hata hivyo usanifu majengo na uchongaji vinyago uliohusiana na desturi za dini au za matanga ya watu pamoja na usanii wa ujenzi fulani maalumu au mapambo unaonyesha mfano wa sifa za sehemu hizo. Hii inadhihirika katika hekalu ambamo sanamu za miungu zilibakia na hali zao za kiasili na kibinafsi licha ya kuhusishwa na miungu wa Kirumi, katika makaburi fulani ya mawe, katika utaalamu maalumu wa ujenzi wa ukuta uliojulikana kama '*Opus Africum*', katika ujenzi wa nyumba za kuishi na mwisho katika wakfu wa minara ya kaburi iliyoonyesha athari za enzi ya kabla ya wakati wa Kirumi.

Sanamu nyingi sana zilizofinyangwa kwa kupanga vigae vya rangi anuwai ambazo zimevumbuliwa tangu mwanzo wa karne hii nazo pia zinaonyesha tabia na sifa za sehemu zinazohusika. Hapa twaweza tu kumshauri msomaji asome majarida maalumu na kitabu ambacho kimetajwa hapo juu kilichoandikwa na G. Charles-Picard ambaye anakamilisha sura yake kulusu "Vishauifu vya Kiafrika" kwa maneno yufuatayo: "Kwa kusema machache sana, Afrika ililipa kikamilifu deni lake kwa Urumi, na ikaonyesha kwamba

ilikuwa na uwezo wa kujinufaisha kutokana na mambo iliyokopa katika moyo ambao haukuwa wa Kiyunani wala ule wa nchi za mashariki mwa Uyunani (Levant ya kihellen”).

SEHEMU YA II: Kutoka Roma hadi Uislam

Wakati wa utawala wa Kirumi ulipokwisha katika Afrika kaskazini baada ya kuwepo kwa karne nne katika baadhi ya sehemu na hadi karne tano katika sehemu nyingine, hali ya ndani ilikuwa ngumu sana. Maasi katika majimbo, mizozo ya kidini, misukosuko ya kijamii, yote haya yalizidi kuifanya hali kuwa mbaya, lakini uzoefu wa utawala na sifa za utamaduni wa kilatini ulitoa nafasi ya kuunusuru ustaarabu huo wa kigeni.

Ikiwa imegawanywa katika kanda zilizoshindwa au kanda huru kulingana na mabadiliko ya ushindi wa kigeni au upinzani wa sehemu zilizohusika, Afrika kaskazini baada ya Warumi na kabla ya Uislamu, ilishuludia nyakati za pekee kabisa katika historia yake.

Majimbo yaliyokaliwa na Wageni

Katika kipindi kinachokaribia karne tatu, wavamizi wa aina mbili wa kigeni, mmoja baada ya mwingine waliitwaa Urumi bila kufanikiwa kuibadilisha mipaka yake.

Tukio la Waharabu

Hakuna jambo ambalo halikutazamiwa zaidi katika Afrika ya Kaskazini kuliko lile la washindi wenye asili ya Kijerumani. Utawala huo haukuambatana kamwe na hali iliyokuwako katika nchi hiyo. Katika mwaka +406 Wavandal waliwashinda watu wengine wa Kijerumani, waliokuwa wametapakaa katika Ulaya magharibi kote. Waharabu hao wakalowea kwanza kusini ya peninsula ya Iberia ambayo yaonekana imeliendeleza jina lao. (Vandalusia = Andalusia).

Walivuka mlango-bahari wa Jibralta, idadi yao ikiwa 80,000 wakiougozwa na Mfalme wao Gaiserik (au Geneserio) mnamo mwaka +429. Waliendelea kusonga mbele kwa mafanikio makubwa. Katika mwaka +430, walikuwa tayari wameuzingira mji wa Hippone na Warumi walikiri kuwa Waharabu walikuwa wamelitwaa eneo la Konstantine katika mwaka +435. Miaka mitatu baadaye waliiteka Kariteji na baada ya kuondoka huko kwa muda mfupi mwaka +442, walianzisha mashambulizi makubwa matatu katika mwaka +455. Hiyo ndiyo iliyokuwa hatua ya mwisho ya kutwaa kabisa sehemu yote ya mashariki ya Afrika iliyokuwa chini ya Warumi. Kuvishinda visiwa vingi vikubwa vilivyokuwa magharibi mwa Mediterani na safari ya kijasiri ya kuitwaa Roma yenyewe. Ufalme wa mashariki ukiwa na matumaini ya kuwaondoa wavamizi hao, ulishindwa vibaya sana katika vita vya baharini katika mwaka +468. Hatimaye ni mkataba ulioafikiwa mnamo mwaka +474 ulianzisha ulusiano mwema kati ya Byzantium na Waharabu hao ambao walikuwa na nguvu nyingi za baharini katika bahari ya Mediterani.

Istilahi ya "Uharabu" (*Vandalism*) ikiwa na maana sawa na moyo wa uharibifu, ilibuniwa mwishoni mwa karne ya 18, na leo hii, kutokana na ushahidi wa kiakiolojia,

inaonekana dhahiri kwamba katika utawala wao mbaya wa koloni lao, Waharabu hao walifanya madhambi kwa kukosa kutenda yaliyostahili na wala hawakufanya hivyo kwa kukusudia.

Inaelekea kwamba wakati huo, kilimo na biashara havikutetereka. Uhusiano na nchi za nje unaonekana ulistawi nyakati mbali mbali na eneo lote lililokuwa katika miliki ya Waharabu hilitwa "dola ya ngano." Vito vya thamani na mitindo ya Kijerumani iliyoonekana katika nyakati mbali mbali huko Hippone, Kariteji, Thuburbo Mains na Makta inaonyesha utajiri uliokuwa mikononi mwa matabaka yenye uwezo. Kwa upande wa kisiasa na kidini, hali haikuwa nzuri sana. Upande wa kusini na magharibi mwa miliki yao ya Afrika ya kaskazini Waharabu hao walikabiliwa na mashambulizi kutoka kwa Wamoor, jina la jumla walilopewa waasi wa Afrika, kaskazini. Hadi leo imekuwa vigumu kuweka mpaka sahihi na miliki yao. Bila shaka ulikuwa wa kubadilikabadilika na labda haukuenea kabisa magharibi kuvuka eneo la Djernila Guicul.

Dini nayo ilikuwa na migogoro mingi sana ya mara kwa mara. Waharabu walikuwa Wakristo, lakini walisema walikuwa na imani ya Arian ambayo ilikuwa aina ya imani ambayo haikuweza kuvumiliwa na viongozi wa kanisa Katoliki. Hii ilisababisha kudhuluniwa kwa viongozi hao wa Kikatoliki na baraza la utawala ambalo halikuweza kuvumilia upinzani katika miasuala ya imani. Chaki dhidi ya Wakatoliki ilifikia kilele chake baada ya mkutano wa bandia uliofanyika mwaka +484.

Hali hii ya mgogoro wa kinaadili wa kijamii ilisababisha kuanguka kwa ufalme kulikoharakishwa na uzembe na ubadhifu uliokithiri miongoni mwa watawala baada ya Gaiseric. Katika mwaka wa +530, hatua ya Geline ya kumwondoa mamlakani mfalme Hilderic aliyekuwa mshirika wa Justinian, mfalme wa Ufalme wa mashariki, ilianzisha ushinde wa Byzantina (dola ya Kirumi ya Mashariki).

Tukio la Byzantina

Kitala katika Constantinople, kikijichukulia kama mrithi halali wa ufalme wa kirumi, kiliamna kuzifukua nchi mpya za Kijerumani zilizokuwa upande wa magharibi kutoka katika ardhi ambazo zilikuwa zimetwaliwa kwa nguvu. Lakini Afrika kaskazini hatua hii haikuwa na nguvu sana.

Katika mwaka +533, kwa amri ya Justinian, kikosi cha askari kilichoongozwa na Belizarius kiliumaliza kabisa utawala wa Waharabu katika muda wa miezi mitatu na Waharabu wakatoweka katika historia. Hatua ya kwanza ya Byzantina ambayo ilikuwa amri mashuhuri ya mwaka +534, ilipanga upya shughuli za utawala wa nchi hiyo na ikatoa utaratibu uliofuatwa. Sera hiyo ilikuwa ya maongozi ya kijeshi na kisheria, ambayo yalihusiana sana na yale ya Kirumi. Watawala hawa wapya hawakutambua kwamba baada ya miaka mia moja na zaidi ya ukosefu wa nidhamu imara, wakazi wa sehemu za mashambani hawangeweza tena kukubali sheria ngumu za utawala zisizokubali mabadiliko. Jambo ambalo utawala wa dola wa Byzantina ulilofanikiwa katika muda wa karne moja na nusu wa utawala wake huko Afrika ya kaskazini ni mafanikio katika

utaalamu wa ujenzi uliositawi katika mazingira ya ghasia na mashaka yaliyoendelea kwa muda mrefu.

Ukitazama ramani ionyeshayo ngome za Byzantina Afrika kaskazini, utaona kwamba mkakati wa kujenga ngome za kuzuia njia za uvamizi, kukaliwa vituo vyote vya kuvukia na kuilinda nchi hiyo hadi sehemu za ndani kabisa za nchi ulikuwa ushahidi bayana unaohitibisha kwamba kulikuwa na hali ya hadhari wakati wote kwa kuwa maadui walikuwapo kila mahali. Mtindo wa kizamani wa kushanibulia adui kwao uliachwa na badala yake mbimu za kujihami zilitumika kwa ajili ya hali ya wasiwasi iliyokuwepo.

Miji ya Kirumi wakati wa zamani iliendelea kudhoofika na idadi ya wakazi wake ikapungua katika ngome kubwa ambazo ziliwekwa kwa ajili ya ulinzi wao, kama katika Tebessa, Haidra au Timgad. Majimbo hayo ya zamani wakati mwingine yalifufuliwa kwa muda tu na yalipata inagavana waliokuwa chini ya amri ya afisa wa kisleria aliyekuwa Kariteji. Lakini utaratibu huu ulikuwa tofauti sana na uwezo wa kijeshi. Mnamo mwisho wa karne ya sita, kiongozi mkuu, kabaila alianua ajichukulic karibu uwezo na mamlaka yote.

Sera ya ndani ya nchi iliyotokana na utaratibu wa Kirumi ilimuiwa kurejesha mtindo wa zamani wa kutoza kodi. Hivyo Annona iliyokuwa kodi ya kila mwaka iliyotolewa kwa ngano ilianzishwa tena. Baada ya kutwaliwa kwa falme za Waharabu na kufilisiwa, mashamba ya binafsi yalirejestewa wenyewe wa zamani. Haya yanatokana na uchunguzi uliofanywa hata ikibidi kurudi nyuma hadi kizazi cha tatu cha watoto wao ili kuwatafuta waliokuwa wenye mashamba hayo. Twaweza kufikiria idadi ya mizozo ya kisheria na ihusuyo mali iliyozushwa na hatua hiyo. Katika kila miliki utoaji kodi ulichukuliwa kuwa mzigo mkubwa nino. Hata hivyo hali ya kiuchumi ilikuwa ni nzuri kwa kiasi fulani.

Kuendeleza uchumi wa fedha kwa ajili ya shughuli zote na kwa kuwakabidli wakala rasmi biashara, kuliipa Kariteji na sehemu za bara zinazopakana nayo, sifa ya kuwa na utajiri mkubwa katika nchi za Mediterani, hasa kwa sababu pande zote mbili za ulango-bahari wa Sisili zilikuwa chini ya utawala wa Byzantina. Kuna tashwishi iwapo wakazi wa selemu za mashambani hawakunufaika kutokana na hali hiyo.

Kuhusu masuala ya dini, watawala hao walianzisha tena madhelebu ya kinapokeo yaani akatoliki wa Othodoksi na wakapiga marufuku madhelebu ya Arian. Jaribio la kufufua madhelebu ya Donati ambayo yalikuwa yameenea sana katika Afrika iliyokuwa chini ya utawala wa Kirumi, lilikomeshwa kabisa. Uamuzi huu ulikuwa sahili kwani madhelebu hayo yalikuwa chanzo cha ingogoro wa kijamii. Byzantina ilijihusisha hata na ingogoro wa kiitikadi kama ule uliohusu suala la mungu mmoja tu. Majadiliano kuhusu Mungu na hali ya ubinadamu wa Kristo na tukio la ushindi wa Mohamed hayakuleta mafanikio yoyote na badala yake yalizusha mfarakano miongoni mwa viongozi wa dini.

Kuanzia wakati huu na kuendelea, kuongezeka kwa utovu wa nidhamu katika jeshi au utawala, kutunika vibaya madaraka na ufasidi katika ofisi za ngazi za juu, na vitisho vya mara kwa mara vya Waberiberi, vilikuwa ni dalili za kuanguka kwa utawala huu. Ilichukua miaka hamsini, toka mwaka +647 hadi +698, kwa mgeni ambaye hakutazamiwa, mshindi wa vita wa Kiarabu, kufajilia mbali utawala wa Byzantina milele.

Majimbo huru

Ikikumbukwa kwamba Afrika iliyokuwa chini ya Warumi ilikuwa imekwishapitia katika mabadiliko kadha ya kisiasa na kijamii, twaweza kutambua jinsi kuwasili kwa Waharabu hao kulivyotumika kama njia mojawapo na kujikomboa dhidi ya tabia hizi za kizamani. "Afrika ya Milele" ilipata tena haki zake, na kuwapo kwa wageni, karibu au mbali hakukuchukuliwa kuwa mzigo. Itakuwa ni kujidanganya, kutofautisha kisaikolojia kati ya sehemu zilizotawaliwa na wana wa kifalme wa Kiberiberi ambao walikuwa wakiheshimu utawala wa Waharabu au Byzantina, na zile sehemu zilizokuwa na uhuru kamili. Kundi la kwanza lilikuwa mbali na makao makuu na sehemu hizo zilikuwa chini ya utawala wa kigeni, zilipewa inadaraka ya kujiamulia mambo yao, jambo ambalo mara kwa mara lilizifanya kujitenga na serikali kuu. Watawala wa Byzantine walikubali kutambua Lavdas katika Aurae, Guenfän, Antalas na Coutzina katika milima ya mbuga za Tunisia, na kwa Carezani katika Tripolitania. Watawala hao wote walizitawala bila kipingamizi sehenu walizokuwa wanazikalia, na wala wasingelinyang'anywa sehemu hizo.

Kuhusu kanda zilizokuwa huru ambazo hazikuingiliwa na mataifa ya nje, baadhi yao zikiwa mbali sana kutoka kwa Waharabu au Byzantine, kanda zilizokuwa katika sehemu ilipokuwa Mauretania Caesariensie, na Mauretania Tingitana ya awali, zilikuwa na uhuru kanili tokea mwaka +429 na kuendelea na watawala wao hawakuingilia mashauri ya majirani wao isipokuwa kama walitaka kupata manufaa ya kibinafsi. Hapa tunakabiliwa na tatizo linalojitokeza mara kwa mara katika historia ya Maghrib ya zama za Wayunani - tabia ya kugawana na kugombania makoloni mara tu utawala wa serikali kuu unapotoweka. Sehemu zilizogawanywa kisiasa zilitawaliwa kulingana na mahali zilipo kijografia. Kwa bahati mbaya tunafaharau mambo machache sana kuhusu jinsi Afrika kaskazini ilivyokuwa baada ya utawala wa Kirumi. Falme nyingine ziliundwa huko kwa ushirikisho mkubwa wa kijamii na kisiasa, ambao habari zake zimetajwa kidogo sana katika maandishi au uvumbuzi wa kiakiolojia. Kwa mfano, katika miaka ya mwanzo ya karne ya sita katika eneo la Altaya na Themcen, kulikuwapo serikali ya Masuna "Mfalme wa Wamoor na Warumi" nuda mfupi baadaye katika Aures, kulikuwa na utawala wa Masties fulani "Dux kwa miaka 67 na Imperator kwa miaka 40", ambaye hakukana imani yake "kwa Warumi na kwa Wamoor". Vartaia, mtawala mwingine alitoa ushuru kwa mtawala mkuu kama shukrani zake, labda alikuwa mtawala wa sehemu ya Hodna. Hakuna shaka yeyote kwamba mji wa Tiaret ambao zamani ulikuwa ngome ya Kirumi uliokuwa katika njia panda ya wahamaji na wakazi, ulikuwa pia, katika karne ya tano, mji mkuu wa ufalme ambao nguru zake bado zadhihirishwa na Jordas ya Frenda ambayo ni makaburi makubwa ya utukufu mkubwa. Mfalme Garmul wa Mauretania aliyekuwa na uwezo mkubwa na ambaye aliliharibu jeshi la Byzantina katika mwaka 571 pia naye anastahili kufikiriwa katika hali hii. Hatimaye katika karne ya sita na ya saba, kulikuwapo na nchi ya wenyeji iliyokuwa katika nchi ya Tingitana kaskazini mwa Moroko ya sasa anubayo nguru zake zinadhihirishwa na maandishi katika Volubilia na katika kaburi la Souk el Gour.

Mara nyingi, mipango ya kijamii na kisiasa luonyesha muundo ambao hankuwa hafifu

au wa kiimla. Taasisi za mwanzo zilishirikisha mapokeo ya kiberiberi na kifani cha utawala wa Kirumi. Wamoor na Warumi walikuwa na uhusiano, jambo ambalo bila shaka linaonyesha kuwa kulikuwako na ushirikiano kati ya wakulima, watu ambao hawakufuata tabia za Kirumi na wakazi wa mijini karne kadha baada ya ushawishi wa Kilatini. Kwa hiyo hakukuwako na upinzani kwa urithi wa utawala na utamaduni ambao asili yake ilikuwa ya kigeni, na ambao wakati mwingine ulikuwa chanzo cha majivuno. Ramani ya kihistoria ambayo tunaeichora kwa sehemu hizi imeonyesha kuendelea kuwepo kwa miji midogo midogo kama Tiaret, Altaya, Tlemcen na Volubilia, ambayo ilikuwa haijafuata tabia ya Kikristo ingawa lugha ya Kilatini ilikuwa ingali ikitumiwa hadi karne ya saba.


Baada ya inatukio yaliyozusha ghasia za muda mrefu hadi wakati uthabiti uliporejeshwa, tunaweza kufikiria hali ya kijamii na kiuchumi ambayo kwa jumla iliwafanya watu kuwa maskini. Takwimu tulizo nazo, kwa mfano, idadi ya dayosisi katika mwaka +484 katika Mauretania Gaesariensia, zilikuwa bado na majina ya miji mingi ya wakati Afrika ilipokuwa chini ya Warumi. Hata ikifikiriwa kwamba miji iliyokuwa mingi ilikuwa imeshushwa hadhi yao hadi kufikia hadhi ya vijiji, lakini iliendelea kuwapo. Kwa kuwa makanisa yalikuwa bado yanajengwa, mara nyingi yakipambwa na sanamu za vigae vya rangi mbali mbali kama ilivyo huko Al Asnam, na hii inadhihirisha udadisi wa kisanaa uliotokana na utajiri uliosalia. Bila shaka manufaa yaliendelea kupatikana kutokana na kipindi kilichopita cha kihistoria. Hata hivyo akiolojia haijatao chochote katika karne ya sita au ya saba kilicho cha maana. Kuhamwa kwa miji kuliendelea na wakati huo huo jamii hii ya watu wa sehemu za mashambani - ambayo ilitapakaa kila mahali katika miaka ya mwanzo ya kipindi cha kati iliimarika.

Ni mabaki ya aina gani ya minara tuliyoachiwa na kipindi hiki cha mwisho? Wilaya zilizokuwako karibu na pwani za Mauretania, ambapo Wabyzantina walikaa, zilikubali bila pingamizi, ushawishi wa kigeni. Kwa mfano, vilango vizuri vya shaba vya tangu karne ya sita vilipatikana katika mabaki ya Mouzaiaville kuelekea kusini ya Tipasa. Mahali ambapo Tenes ilikuwapo, palifanywa mashuhuri kutokana na uvumbuzi wa hazina kubwa ya dhahabu na fedha za nyakati za kale, na muhimu zaidi kati yao yakiwa mapambo ya watu mashuhuri wa kifalme. Kuwapo kwa hazina hii mbali kiasi hiki bado ni kitendawili kikubwa. Mwandishi huyo anaamini kwamba vito hivyo vyote viliibiwa sehemu fulani na labda vyahusiana na kuporwa kwa Roma kulikofanywa, katika mwaka +455 na majeshi ya Waharabu yaliyokuwa na askari wahalifu wa jangwani kwa mujibu wa maandishi.

Lakini kadri tunavyotoka sehemu za pwani na wilaya zilizokuwa chini ya utawala wa kigeni, tunaona kwanza shughuli za ujenzi ziliendelea hadi mwisho wa karne ya tano. Hata hivyo kuna mambo mawili muhimu ambayo hayafuati sheria hii, yanayoonyeshwa na makaburi maarufu ya Collossus, ambapo maarifa ya ujenzi yalirudia uzuri wake wa zamani bila kuathiriwa na mambo ya kigeni. Kwa hivyo, huko Moroko, kaburi la Souk-El-Gour ambalo yawezekana lilijengwa katika karne ya saba, na huko Algeria, Jedars ya Frenda, ilifuatana mwaka baada ya mwingine tokea karne ya tano hadi ya saba (?) inaonyesha aina ya usanifu majengo ambao hauwezi kuelezeka ikiwa hali ya sehemu hiyo ilikuwa ya kifukara. Si ajabu kwamba falme za kwanza za Kiislamu za Maghreb ya kati na Magharibi,

ufalme wa Rostemides wa Tiaret, na kisha Idrisside wa Walili (Volubilis), ziliota mizizi sana katika sehemu hizi.

Kwa hivyo enzi ya zama za zama iliishi katika sehemu hizo, mchanganyiko wa matukio ambapo mabadiliko ya kijamii na ya kisiasa yalipata mageuzi ya taratibu ambayo yalifuta ushawishi wa Kilatini na kudhihirisha hamu kubwa ya uhuru na uthabitiwa dhamira ambayo imebakia kama kumbukumbu ya historia ya Afrika ya Kaskazini.



Sahara katika zama za kale za wakati wa Wayunani

Wazo la kawaida kuhusu 'Zama za Kale za Wakati wa Wayunani' huenda likaonekana kuhitilafiana na uchunguzi wa matatizo ya Sahara. Matatizo haya yana muainisho maalumu. Kwa mfano, akiolojia ya Mediterani, mambo ya kale ya wakati wa Wayunani yanajumulisha kipindi cha miaka takribani elfu moja, tokea karne ya tano kabla ya enzi zetu hadi karne ya tano ya wakati wetu. Lakini katika historia ya awali ya Sahara, inajumlisha kipindi cha mwisho cha 'Caballine' na sehemu ya kipindi cha Waberiberi wa Libya; nyakati ambazo hazawezi kuwekewa tarehe. Kwa hiyo utaratibu wowote wa miaka hauwezi kuhusishwa katika hali hii.

Hata hivyo wakati wa elfia hiyo hiyo, ulimwengu wa Sahara ulikuwa mahali palipotokea matukio muhimu sana ambayo yalikusiana kwa sehemu kubwa na historia ya ulimwengu wa Urumi na Uyunani. Kwa hiyo siwezi kusita kutumia vigezo vya kikronolojia ya kale ambavyo vinakubaliwa katika ulimwengu wote unaojulikana.

Wanahistoria wanalikabili vipi swala la Sahara ya kale? Kwanza kumbukumbu za maandishi ya Kiyunani - Kilatini lazima zichunguzwe: Japokuwa habari zilizokusanywa si za kuaminika wakati wote, na huenda zikapotosha ukweli, kwa ujumla, zina umuhimu mkubwa. hatua ya pili ni kutumia njia za kisasa za usomi ili kusahihisha kumbukumbu za zamani kidogo kidogo ili kufafanua matatizo hayo kwa jumla. Baada ya kufanya hayo, Sahara ya kale haitapimwa kutoka nje bali itajitokeza katika hali yake yenyewe.

Kumbukumbu za maandishi ya wakati huo na jinsi zilivyofafanuliwa kupita kiasi

Twazifahamu njia za uchambuzi zilizotumiwa wa wanajiografia wa wanahistoria wa kale. Waliposhindwa kuzifikia sehemu ambazo hazikuweza kufikia, walikusanya habari zisizo sahihi. Wayunani na baadaye Warumi walizungumzia juu ya 'Libya ya Ndani' istilahi ya kijiografia yenye utata sana inayoelezea kuhusu nchi zilizopo mbele ya Afrika ya kaskazini, au 'Ethiopia ya ndani' - eneo lililo kusini zaidi ambalo jina lake lilitokana na weusi wa ngozi za watu wanaoishi huko. Masimulizi ya sehemu hizi ambayo yaliwaogofya wanahistoria na wanajiografia wengine wa wakati huo kwa jinsi yalivyotisha yana maelezo

ya uwongo. Katika masimulizi hayo watu na wanyama mara kwa mara huonyeshwa kama vitu vya kuchekesha au madubwana ya kutisha.

Ingawa haikuwa rahisi kuepukana na hekaya, waandishi makini walinakili kumbukumbu muhimu; na wakati unavyoendelea, tunagundua kwamba kazi yao inazidi kuwa bora zaidi kwa uwiano ambao bila shaka uliwiana na maendeleo ya ukoloni wa Kiyunani - Kirumi katika Afrika uliwafanya watu watambue ukweli.

Katika karne ya tano kabla ya enzi za Ukristo, Herodetus alipata habari sahihi. Katika maandishi yake tunawaona Wagaramante wakiwawinda wakaa pangoni wa zamani kwa kutumia magari ya farasi wanne (IV. 183). Tunawaona Wanasamonia (IV 172-5) wakisafiri kupita jangwa ili kwenda kugundua katika nchi ya watu wenye ngozi nyeusi, mto mkubwa kama Nili uliojaa mamba. Twazidi kufahamishwa (IV. 43) juu ya kitendo cha kijasiri kisicho cha kawaida cha mabaharia wa Kifoeniki waliowuhi kulizunguka bara la Afrika tokea mashariki hadi magharibi kwa ajili ya Farao katika mwaka - 600, na kisha kushindwa kwa Waajemi kuzunguka Afrika tokea magharibi kuelekea mashariki baada ya kuingia katika bahari ya Atlantiki (IV, 43). Mwishowe twafahamishwa juu ya Wakariteji wakibadilisha bidhaa zao kwa mavumbi ya dhahabu katika ukingo wa magharibi wa Afrika. (IV, 196).

Hapa katika kumbukumbu zetu yaja hati moja mashuluri sana ambayo labda ni ya nusu ya kwanza ya karne ya nne kabla ya enzi za Ukristo iitwayo *Scylax Periplus* ya Hanno, ikieleza juu ya safari ya baharini ya Mkariteji mmoja aliyeamriwa kuvumbua na kuanzisha koloni katika pwani hiyo hiyo. (*Geographici Graeci Minores I*). Mandhari ya sura ya nchi inayovutia, imejaa majahili, mamba na viboko. Masimulizi haya mafupi yanadokeza mambo mawili muhimu. Kisiwa cha Cerni, kilichojulikana kutokana na kumbukumbu nyingine kama ghala la pembe za ndovu na ngozi za wanyama-mwitu (*Scylax periplus*, karne ya nne kabla ya wakati wetu, kifungu cha 112), na volkeno kuu iliyoitwa 'Gari la farasi la miungu', sehemu ya mwisho ya safari hiyo ya Hanno kwenye pwani ya Afrika. Kuwepo kwa mahali hapa pawili kulithibitishwa katika karne ya pili kabla ya enzi za Ukristo, na safari ya baharini ya mwanahistoria mmoja wa Kiyunani ahycitwa Polybius, ingawa masimulizi yake yanajulikana tu kupitia kwa maandishi mengi (Pliny Mkubwa, *Historia ya Asili*, V, 9-10).

Maandishi ya thamani kubwa ya Pliny Mkubwa (*Historia ya Asili*, V, 5) yaeleza juu ya uvamizi katika mwaka wa -19 uliofanywa na balozi wa Afrika, Cornelius Balbus dhidi ya ufalme wa wakorofi wa Wagaramante wa Fezzan. Pamoja na toponimia chache ambazo zatambulika wazi, kama Rhapsa (Gafsa) Cidamus (Ghadames) au Garama (Jerma), orodha ya ushindi wa Warumi ina toponimia nyingine nyingi ambazo zinakanganya na hukumbusha matamshi ya majina ya mahali pa sasa pa Sahara. Hii ilichukuliwa kama uthibitisho kwanza Warumi walifika Niger.

Mwandishi marinus wa Tiro (mwisho wa karne ya kwanza ya enzi za Ukristo na msimulizi wake, mwanajiografia mashuhuri Claudius Ptolemy ambaye kumbukumbu zake kuhusu Afrika zilianzia mwaka +110 hadi 120) anasema kwamba gavana Septinius Flaccus, akiendeshea shughuli zake kutoka kituo kimoja katika Libya alisafiri nmbali wa

kutoka kwa Wagaramante hadi kwa Waethiopia katika miezi mitatu kuelekea kusini; hali kwa upande mwingine Julius Maternus akitokea Leptis Magna na akisafiri kutoka Garama akiandamana na mfalme wa Wagaramante ambaye alikuwa akisafiri dhidi ya Waethiopia alifika Agisymba, ardhi ya Waethiopia ambapo vifarū walikuwa wengi sana, baada ya miezi minne mfululizo ya safari kuelekea kusini (Ptolemy, *Jiografia* I, 8, 4). Hadithi hii ilikuwa muhimu zaidi kwa kuwa Ptolemy aliongeza maarifa yake mengi ya jiografia ya Afrika kwa mfumo wa mahesabu, Longitudo na latitudo kuthibitisha mahali alipoyataja. Ramani yake ya sehemu za bara iliimarishwa kwa insaada wa kuandika maneno jinsi yalivyotamkwa. Kazi yake ilivutia sana na kwa mara nyingine tena watu waliamini kuwa na uthibitisho kwamba Warumi walifahamu kabisa sehemu za joto za Afrika hasa Niger na Chad.

Leo hii maoni haya yaliyotiwa chumvi sana hayakubaliki tena. Njia za kisasa za uchambuzi zatulazimisha kufikiria tena historia ya Sahara.

Mkabala wa uanazuoni wa siku hizi

Uhakiki mpya wa matini

Wanahistoria wa kisasa wametambua kwamba vitabu muhimu vitatu vilihusika: *Scylax Periplus* cha Hanno, matukio ya Cornelius Babus *Jiografia* ya Ptolemy.

Kwa miaka kadhaa tofauti za *Scylax Periplus* zimekuwa zikilaumiwa. Kwanza imethibitishwa kwamba mcli za kale zilisafiri kupita rasi ya Juby, lakini ikagunduliwa kwamba kwa safari ya kurudi wakati wa upepo mkali wa kusi, hazingaliweza kurejea vituoni nkwao. Kwa hiyo hii imepunguza kijiografia, umbali wa safari ya Hanno hadi pwani ya Atlantiki ya Moroko, ambapo utafiti wa marabo ya kale umetambulisha kisiwa cha Cern na kisiwa cha Essaouira-Mogador. Aidha, njia bora zaidi ya kufaninisha lugha yaonyesha kwamba *Scylax Periplus* ni nakala ya kitabu cha Herodotus, na kwa hivyo ni udanganyifu ulio dhahiri.

Wa pili: Hadithi ya Pliny kuhusu uvamizi uliofanywa na Cornelius Balbus. Uchambuzi wa miswada unaifanya isiwezekane kukanusha moja kwa moja ubainishaji wa kitoponimia na kusini ya Sahara. Kwa hiyo ushindi wa Warumi ulikuwa tu kusini ya Maghreb; na Fezzan. Aidha, balozi ambaye ofisi yake ilikuweco tu kwa mwaka mmoja haiwezekani kwamba alikwenda mbali zaidi.

Mwisho iligunduliwa kwamba *Jiografia* ya Ptolemy kazi iliyoonekana kuwa ya ajabu ilihusu tu sehemu chache. Longitudo na Latitudo zake ambazo zilipimwa kulingana na kanuni za marabo ya kale kama milima, mito, miji, na makabila zatufikisha katika mipaka ya kusini ya Maghreb; na Niger aliyochora, kwa nifano sio kitu bali ni mfumbi uliokuwa kusini mwa Algeria. Fezzan basi ingalikuwa sehemu ya kusini zaidi kujulikana na Warumi, tatizo la Agisymba kwenye nupaka ya *terpae incognitae* bado lingalipo.

Kwa vile sasa tumecondolewa viziuzi vya maandishi ambavyo kwa wakati mwingine vilikuwa tatizo, twaweza kujaribu kuona kila tunachoweza kujua kutokana na Sahara ya zamani.

Mambo ya kiakiolojia, kianthropolojia na kisosiolojia yalikuwaje? Masalio ya kiakiolojia yametudokezea kitu gani?

Matatizo ya kiakiolojia

Kwa hali ya hewa, Sahara yajulikana kwamba ilifikia hali yake ya mwisho ya ukame katika muda ambao sasa twaifikiria. lakini lazima tuithibitishe. Mabaka ya hapa na pale bado yalihifadhi unyevu kwa maisha wakati huo zaidi kuliko ilivyo wakati wetu. Ahaggar, Fezzan, Tibesti na kaskazini mwa Sahara kulikuwapo na wanyama wa porini ambao sasa wametoweka: mamba katika visiwa vya muda na vya kudumu, na paka katika nyanda za juu. Lakini kuna shaka kwamba wanyama wakubwa wanaokula nyasi kama ndovu na vifaruu wangaliweza kuendelea kuishi katika sehemu hiyo ya Tibesti au hata katika nchi ya Kuar, sehemu ya mbuga za joto katika Chad, ambapo walikuwa wengi sana.

Wanyama wa kufugwa pamoja na watu waliwekwa katika sehemu salama kwa kuishi. Kulikuwako aina mpya za wanyama kama ng'ombe, mbuzi, na kondoo. Lakini ni ajabu kwamba punda ambaye ndiye mnyama wa kazi zote katika maoasisi ya Sahara hayumo miongoni mwa picha zilizochorwa katika miamba.

Tatizo la Anthropolojia

Kutokana na ukosefu wa kanuni za kisayansi, ilifikiriwa kwamba kuwepo kwa watu weupe katika Sahara lilikuwa tukio la hivi karibuni tu; matokeo ya ushindi wa mara kwa mara ya Warumi yalikuwa ni kufukuzwa kwa Waberiberi wa mbugani nje ya Maghreb.

Hapa pia hali inafanuliwa zaidi kutokana na kazi ya hivi majuzi huko Fezzani na Algeria. Sasa yafikiriwa kwamba wakati wa historia ya kwanza ambayo ukale ulikuwa tu sehemu ya mwisho, eneo la kati na kaskazini la Sahara mlikuwa na watu weupe. Inaonekana kwamba asili ya watu hawa wenye nguvu haiwezi kutafutwa katika Maghreb bali kutoka kaskazini-mashariki mwa bara la Afrika. Tutaweza kujua zaidi wakati wa matokeo kamili ya utaratibu wa kuchambua aina za damu za watu. Kwa upande mwingine inawezekana kwamba watu wengi wa Sahara ya kusini walikuwa wenye ngozi nyeusi kutokana na mbuga za tropiki.

Ustaarabu

Kutokana na kutokuwapo kwa kronolojia inayoaminika inaonekana kuwa ni vigumu sana kutathimini maendeleo ya ustaarabu wa kalc, hasa kwa kuwa hakuna uhakika kwamba sehemu zote za koloni hilo kubwa zilistawi kwa usawa. Njia nzuri ya kuchunguza tatizo hilo ni kuanzia hali ya utamaduni wa Sahara mnamo mwisho wa kipindi cha Neolithiki na kwa msingi huo kufuata utaratibu wa maendeleo katika sehemu mbalimbali.

Lugha na Maandiko

Lugha ya mama ambayo ilikuwa mchanganyiko wa lugha mbali mbali iliitwa 'Berber' na ni ya asili ya kundi la Hamitiki-Semitiki lakini ilitofautiana na kundi hilo muda mrefu uliopita. Katika hali yake ya asili 'Kilibya' kinadhibirishwa katika nchi za Afrika katika

enoco la Mediterani na katika visiwa vya Canary, kwa mifano ya maandishi. Hakuna shaka kwamba lugha hii ilipelekwa katika Sahara toka kaskazini au kaskazini-mashariki na wahamiaji weupe. Wakati wa tukio hilo haujulikani lakini maandishi ya Kisahara yaliyoitwa '*Tifinagh*' yaliyotokana na alfabeti ya Kilibya ya Maghreb, ni tukio la baadaye. Katika nchi za kaskazini inaonekana hakuna ushahidi wa maandishi yoyote ya Kilibya yenye uhakika kabla ya karne ya tatu au ya pili kabla ya enzi za Ukristo na inakubalika kwamba Waberiberi walianza kuandika lugha yao chini ya ushawishi wa Kikariteji. Neno '*Tifinagh*' ambalo katika herufi za lugha ya Kifaransa ni '*Tifinar*' latokana na shina la FNR ambalo katika lugha zote za Kisemitiki lina maana ya Wafoeniki.

Huko Sahara, maandishi ya '*Tifinagh*' pole pole yaligeuka kutoka hali yake ya awali ya Kilibya, '*Tifinagh* ya zamani' ambayo bado ingali inafanana nayo. Kwa hiyo lazima tujihadhari na tarehe za imichoro inayoitwa 'Libya - Beriberi' ikiwa na maandishi juu yake. Makosa makubwa sana yaweza kufanywa. Aidha, lugha na alfabeti za Kiberiberi huenda pia zilitumiwa na watu weusi.

Mpango wa Kijamii na Kisiasa

Taratibu za kikabila, ambazo zilikuwapo wakati huo wa mabadiliko, ndizo zilizotumiwa kwa kanuni za kisiasa, lakini zilizusha mfululizo wa vita vilivyoolezwa kwa ulalisi katika Herodotus na Ptolemy.

Katika majimbo mawili, tuna mambo yenye uhakika zaidi: ukanda wa Ahaggar na Fezzan.

Katika Ahaggar mnamo nusu ya pili ya karne ya enzi za Ukristo, utaratibu msonge wa kijamii na kisiasa uliongozwa na mwanamke. Wakati kaburi lake lilipogunduliwa likiwa zima kabisa, lilihusishwa mara moja na mapokeo ya sehemu hiyo ya Malkia Tin Hinan. Katika nchi ya Waberiberi kulikuwepo na mifano kadhaa ya uwezo mkuu uliosemekana ulitokana na mwanamke mtakatifu. Hata hivyo wanawake katika jamii ya Tuareg waliheshiiniwa. Vifaa vya inatanga vya huyu Binti nifalme; kama vile bangili saba za dhahabu, nane za fedha, vito kadhaa vya thamani - yaweza kukisiwa kwamba vilitokea wakati sawa ua sarafu ya Kirumi ya mfalme Constantine mwaka +315 hadi +324. Na kuhusu kitanda cha mbao ambapo maiti alilazwa wakati akitolewa kwa majaribio na Redio-kaboni kilionyesha tarehe ya mwaka +470 (+130). Kwa tutakavyoona, mali ya mtu huyo mashuhuri yaweza tu kuelezwa na cheo chake kijamii na katika biashara ya kupitia Sahara. Eneo mashahuri lililoitwa 'Ufalme wa Wagaramante' - uliotajwa na Herodotus katika karne ya tano kabla ya enzi za Ukristo, lilipinga Warumi wasiisogelce mipaka ya kusini ya Maghreb. Baada ya kushindwa na Cornelius Balbus katika mwaka -19 na mwishowe na balozi Valerius Eestus katika +69, wanaonekana walianzwa kuwa na uhusiano nweema na himaya. Utafiti wa kiakiolojia karibu na Garama unonyesha karibu karne kumi za ustaarabu ambao sehemu yake ilianzishwa kwa uhusiano na nchi za kigeni, tokea wakati wa mwisho wa Puniki hadi kufikia kuwasili kwa Waarabu.

Kwa hiyo katika Ahaggar na Fezzan na pia kote kaskazini mwa Sahara, katika Taasili n'Ajjer mnamo muda wake wa mwisho na labda hata katika Adrar des Iforas, uwezo

mkubwa wa kisiasa katika nyakati za kale ulikuwa katika mikono ya tabaka tawala la watu weupe au wale ambao asili yao ilikuwa karibu na ya weupe.

Kutokana na kutokuwepo kwa hati, haiwezekani kusema kuwa hali ilikuwa sawa kwenye mipaka ya Sahara, nyanda za Niger na Chad. Yawezekana kwamba ushawishi wa watu weupe haukuwa umepenya hadi katika sehemu hizo.

Kuhusu dini, hapana shaka kwamba sehemu yote ya kati na kusini mwa Sahara iliendelea kuamini kwamba vitu vyote vilikuwa na roho. Ni watu wa Sahara kaskazini tu, waliokuwa katika mawasiliano ya moja kwa moja na sehemu za Mediterani, ambao huenda walibadili dini na kuwa Wakristo mnamo mwisho wa nyakati za kale. Mwandishi wetu anasema kwa msisitizo kwamba Wagaramante na Wa-Macurita waliingia Ukristo mwishoni mwa karne ya sita, lakini utafiti kuhusu mambo ya kale haujathibitisha hayo.

Sanaa ya Sahara ya Kale

Katika jumba kubwa la Abalessa linalohifadhiwa Ahaggar, lililopo kando kando ya kaburi la Tin Hinan ulikuwepo mtindo wa usanifu majenzi uhofanana na ule wa Kiafrika. Katika mji wa Tin Alkoun katika lango la kusini-mashariki la Tassilin'Ajjer, mlikuwamo makaburi mengi ya mtindo wa kawaida wa Sahara, ambayo tarehe zake zaweza kujulikana kutokana na vifaa vya mazishi vya Kirumi vya karne ya nne, sawa na vile vilivyoko katika makaburi ya Ghat yaliyoko karibu.

Kaskazini magharibi mwa Sahara, katika makaburi ya Jorf karibu na Bechar ambayo bahati mbaya yaliharibiwa na watalii, yaliweza kuonekana katika majengo makubwa ya kushangaza; bamba zilizochongwa au kuchorwa, nyingi kwa niaandishi ya Kilibya au michoro ya farasi au binadamu, kwa mtindo sawa na ile ya mwisho wa nyakati za kale katika Maghreb na bila dalili za Kiislamu.


Lakini kwa sanaa ya kuvutia sana ya Sahara lazima tutazame michoro iliyo katika miamba. Kulingana na mwainisho wa kawaida wa waandishi wa historia ya awali, sanaa ya kale ni ile ya Walibya na Waberiberi ya wakati unaofuata kipindi cha mwisho cha sanaa ya miamba, kabla ya ile ya wakati ya Waberiberi na Waarabu. Japokuwa nifululizo huu ni sahihi, unakosa misingi ya kronolojia sahihi na kusema kwamba wakati wa Waberiberi wa Libya ulikuwa kati ya mwaka -200 na +700 bado hakuna uhakika. Kuwepo kwa dalili za maandishi ya Tifinagh kongwe labda ndio kipimo kisicho na uhakika ingawa mwandiko huo uliendelea hadi wakati wa Kiislamu. Kwa kuwa farasi na magari ya magurudumu yalikuwa yakitumika yote kwa pamoja ni vigumu kuvitofautisha kikronolojia. Je magari ya kivita ya farasi yaliyokuwa Fezzan na Tassili ni ya jadi ya Kimisri ambayo huenda yalikuwepo katika karne kumi na nne kabla ya enzi za Ukristo au ya jadi ya Wayunani - Wakrene iliyoigwa mnamo karne ya sita hivi. Michoro ya ngamia iko katika maeneo yote ya Sahara, lakini pia ni vigumu kukadiriya umri wao. Yawezekana kwamba michache kati yao imo katika muda wa kihistoria tunaouchunguza. Michoro ya Waberiberi - Kilibya, na kazi za sanaa za kuvutia za Kineolithiki ambazo zilichota mitindo yake kutoka kwa michoro ya Waberiberi na Walibya, inadhihirisha jinsi sanaa za picha zilivyozingatiwa katika Sahara, wakati ambapo zilikuwa zikififia katika sehemu za kaskazini.



20.1 ◀ Kaburi la Malkia Tin
Hinan huko Abalessa mlango mkuu.



20.2 ◀ Kaburi la Malkia Tin
Hinan huko Abalessa: mawe
yaliyotumika kuziba mitara



20.3 ▼ Mifupa ya Malkia Tin Hinan

Maisha ya Kiuchumi. Mawasiliano ya ndani na uhusiano wa nchi za nje: mapinduzi ya ngamia?

Tangu zama za kale, maisha ya kiuchumi katika Sahara yamehusishwa na tatizo la mawasiliano. Katika zama za kale za wakati wa Wayunani, kutajirishwa kwa sehemu fulani kama Fezzan kwahusiana na kiwango cha uwezo wao, ikiwa tutachukulia pasipo uthibitisho kwamba kulikuwako na biashara nzuri. Kwa kuwa twajua kwamba safari za ndani mwa nchi hiyo zilikuwa haba, chanzo cha utajiri huu lazima kitafutwe katika uhusiano wao ua nchi za nje. Hali hii mpya ilikuwa ua tofauti muhimu na ile hali ya Sahara yenye unyevunyevu ya nyakati kabla ya historia.

Kwa maoni yangu, uwindaji wa wanyama ndio uliokuwa shughuli muhimu ya faida kwa nchi hiyo. Wakati huo Afrika kaskazini ilikuwa ingali na simba, dume, paa na mbuni; lakini Urumi iliwahitaji sana wanyama hao hivyo kwamba ilibidi uwindaji huo uendelezwe hadi sehemu za ndani za Afrika. Tunazo takwimu sahihi kuhusu suala hili. Wakati wa kufunguliwa kwa Ukumbi wa Flavian katika mji wa Roma mnamo mwisho wa karne ya kwanza, wanyama hao elfu tisa walipiganishwa. Kutokana na ushindi wake uliotokea mwaka 106, Mfalme Trajan aliwaonyesha watu wanyama elfu kumi na moja. Wengi wa wanyama hao walikuwa wa aina ya 'Libyaca' au 'Africanae' maana yake walitolewa Afrika kaskazini. Katika kundi hilo la wanyama, ndovu na vifarū walitolewa sehemu za kusini zaidi za Sahara au hata kutoka Ciud na Bahr el Gazal. Kwa vyovyote vile, pembe za ndovu lazima zilikuwa baadhi ya bidhaa zilizofanyiwa biashara katika biashara zilizopitia Sahara kwa kuwa ndovu wa Afrika kaskazini walitoweka kabisa katika karne ya pili ya enzi zetu Haitasahauliwa kwamba Unubi ilikuwa ikitoa kiasi fulani cha wanyama wa mwinu kwa Urumi.

Naona vigumu kuamini kwamba Ulaya ilikuwa ikifanya biashara ya watumwa weusi na sehemu hiyo ya Afrika. Nchi za magharibi ya Ulaya hazikuhitaji watumwa weusi. Imesemekana mara kwa mara kwamba misafara iliyobeba mavumbi ya dhahabu kutoka Mali na ghuba ya Guinea ilitoa bidhaa kwa masoko ya Ulaya, na kubashiri hali ya kibiashara itakavyokuwa katika Enzi za Kati. Maoni haya ni nadharia tete tu.

Uhusiano huu kidogo wa kibiashara, ambao haujafahamika vizuri, wazusha wasiwasi kuhusu matumizi ya kumbukumbu za safari za Sahara. Hapa tena lazima mtu ajihadhari. Kumbukumbu pekee ambazo twaweza kuzitumia tunapojaribu kujenga tena utaratibu wa mawasiliano na mahali kama vile Ghadames au Phazania ambapo mito mikuu ilikuwa na hori zake. Kutawanyika kwa bidhaa za Kirumi kutoka Sahara, na mwishowe kulinganisha njia za misafara kabla au baada ya muda tunaoufikiria sasa. Kumbukumbu mbili za mwisho ndizo zinazotuletea matatizo.

Inaonekana kwa ujumla kwanza njia za mawasiliano ya biashara za kigeni kwa wakati mwingi zilikuwa za kuelekea kaskazini na kaskazini-mashariki, huku Wagaramante na washirika wao wakizielekeza njia hizo upande wa Fezzan. Kutoka hapo njia sahihi zilielekea bandari za Syrtic (Sabratha, Osa, na Leptis Magna) ambayo ilikuwa miji yenye utajiri kuanzia wakati wa Kipuniki. Kutoka Garama ungeweza kufikia bonde la naili, kwa

kutumia njia ya kaskazini kupitia Oasisi za Zuila, Zella, Aujila, na Siwa, zote zikiwa sehemu zilizofahamika kwa waandishi wa nyakati za kale; au ingewezekana kupitia njia ya kusini zaidi ambapo Kifra ilikuwa ni njia panda. Katika sehemu hizi za mashariki, hapana budi kurejea tena katika tatizo kongwe la mawasiliano ya Kincolithiki na la mawasiliano ya historia ya mwanzo ambapo Tibesti ilikuwa ndicho kituo. Lakini yaonekana kwamba uhusiano ulifika kwanza na Uyunani na baadaye na Misri ya Kirumi. Biashara zilizidi kuelekezwa pwani ya Mediterania.

Labda mashariki mwa Sahara ndipo ambapo tungetafuta kiungo kilicholeta chuma katika nchi za watu weusi, kwa kiwa tukio hili halikutendeka peke yake. Tatizo la kipindi cha mpito kuanzia wakati wa utumiaji wa mawe budi wakati wa utumiaji wa chuma katika sehemu za Sahara na Niger ni la umuhimu mkubwa. Hapa pia hapana mlingano wa Kijiografia.

Suala la tasnia ya chuma ni tofauti. Kwa hivyo tatizo la jinsi ya kutenganisha chuma na udongo lilivyofika katika nchi za watu weusi lina ubishi mkubwa; wengine wanasema kwamba huo ulikuwa uvumbuzi wa Kiafrika, wengine wanasema kwamba ulipeleka huko na wageni. Wenye kutoa sababu ya pili wanegawanyika katika makundi mawili: wengine wanasema kwamba ulitokana na ishawishi wa Kiinediterani katika sehemu za kati ya Sahara; na hao wengine wanasema kuwa utaalim huo ulitokea nchi ya Kush na wanauchukulia kwamba ulifuata njia ya asili iliyounganisha Niger na bonde la Nili kupitia Kordofan na Darfur. Licha ya hayo yote tarehe za kaboni -14 zinaonyesha kwamba utaalim huo wa kutenganisha chuma na udongo ulikuwako katika nchi ya Chad na kaskazini mwa Nigeria katika karne ya pili na ya kwanza kabla ya enzi za Ukristo. Uwezekano kwamba utaalim huo ulikuwa uvumbuzi wa sehemu hiyo hauwezi kukataliwa, lakini ikiwa ilikuwa hivyo, ulitokana na ustaarabu wa Kimeroc; hivyo basi njia za kati za Sahara hazikuhusika.

Uchunguzi wa njia za usafiri waweza pia kusaidia vizuri zaidi kugundua njia za Sahara na kuchunguza nadharia tete fulani. Tunajua kwamba farasi walikuwa wakituniwa jangwani kabla ya ngania kuanza kutuniwa. Hapa, kama mahali pengine matoko ya awali ya kipindi cha "Caballine" yalikuwa ni magari yenye magurudumu. Hatujni ni lini inagari ya Farasi yalipokwisha, lakini kulingana na Herodotus, Wagaramante walikuwa wangali wanayatumia. Akiolojia imethibitisha jambo hili. Michoro mingi sana mbali mbali ya magari yenye magurudumu ilikuwako katika Sahara. Uchambuzi wa wazi uhofanywa kwa mpango umewezeshwa kuchora upya ramani za njia za magari ya farasi kupitia Saham. Inafaa kususitiza kwamba njia za safari zilizotumiwa na farasi waliokuwa na lijamu au la, zilihitaji utaratibu wa kupata maji, ambao twajna Wagaramante walikuwa nao, vinginevyo wangelazimika kubeba akiba kubwa ya mahitaji yao.

Ngamia, na hasa yule mwenye munda - ambaye asili yake ilikuwa Mashariki ya Karibu - alianza kuonekana katika enco la Sahara baadaye. Tukio hili limejadiliwa bila kikomo. Katika bara la Afrika lenyewe ngamia waliwasili tu baadaye. Hawakuwemo Misri hadi wakati wa Waajemi na Wayunani (karne za tano za nne kabla ya enzi za Ukristo) na yawezekana kwamba walienea katika Sahara kutoka bonde la chini la Nili. Takio hilo linaonekana gunu kuliweka tarehe ya kutokoa kwake. Tuliyo nayo ni michoro katika

miamba ya Sahara ya Waberiberi na ya Kilibya ambayo msaada wake ni kidogo sana katika utaratibu sahihi wa kronolojia, na idadi kubwa ya maandishi na uumbaji kutoka Afrika kaskazini iliyokuwa chini ya Warumi ambayo ilikuwa baada ya karne ya pili ya enzi za Ukristo.

Nitataja kwa ufupi tu kuhusu alama ya ngamia katika sarafu mashuhuri za Kirumi zilizoitwa '*Spintrian*' ambazo labda zilikuwa zikitumiwa na makahaba, na watu wa zamani walifikiria kwamba ngamia walikuwa na silika za ukware ambazo hazikuwa za kawaida.

Napenda kukubaliana na wanahistoria wanaotilia maanani sana kuongezeka kwa matumizi ya ngamia katika Sahara, matumizi ambayo yalimaanisha kwamba watu binafsi na makundi ya watu waliwahi kusafiri zaidi; jambo lililokuwa limetambuliwa zamani huko Bara Arabuni. Inafikiwa kwamba kubadilishwa kwa mahali pa kuweka lijamu na hasa kubadilisha mahali pa matandiko kuliwezesha kuwafunza '*Meharis*' - yaani ngamia wa kutumiwa kwa mashindano au kwa vita.

Sera ya Roma katika Sahara,

Kutokana na ukosefu wa kumbukumbu, hatujui ikiwa Kariteji ya Kipuniki ilishtushwa na kuwako kwa makabila yenye nguvu katika mipaka yake ya kusini. Machimbo ya Garama yanathibitisha kwamba katika karne ya pili na ya kwanza kabla ya enzi za Ukristo bandari za pwani za Syrtic ambazo wakati huo zilikuwa mali ya ufalme wa Numidia, zilikuwa na uhusiano wa kibiashara na Fezzan, uhusiano ambao utajiri wake uliutegemea kwa kiasi kikubwa.

Historia ya Kirumi inajulikana sana. Mikondo muhimu ya sera ya Kilatini yaweza kuelezwa kwa ufupi kama ifuatavyo: kukaliwa kwa ardhi za kilimo za Maghreb kulihitaji ulinzi katika sehemu za kusini. Katika sehemu hizo, wahamaji wa Sahara walikuwa wasumbufu sana. Uhamaji wao wa msimu katika makoloni haungeepukika kwa kuwa ulikuwa muhimu kwa uhai wao, na wao walikuwa na manufaa kwa kuwa waliwezesha bidhaa za nyika na jangwa kuwafikia walowezi. Lakini daima kulikuwapo na hatari ya kuzusha mzozo na makabila yasiyohamama. Hata Wagaramante walioishi mbali walionekana kuwa hatari kwa kuwa wangiweza kuongeza uwezekano wa kuwachokoza hawa wanaohamama. Uwezo wao ulikuwa tishio kubwa pia.

Kwa hivyo kama tulivyokwisha kuona tuna taarifa fulani kuhusu Sahara ya kale, hata ingawa habari tulizo nazo si kamulifu. Mambo fulani ni hakika. Ukavu wa hali ya hewa haukuua jangwa. Shughuli za kibinadamu ziliendelea. Lugha na maandishi yalianzishwa huko. Kuongezeka kwa matumizi ya ngamia kulipunguza matatizo ya usafirishaji na mawasiliano. Eneo hilo lilitokeleza wajibu wake katika historia ya nchi kuu za Mediterani. Je hivyo ndivyo mambo yalivyokuwa pia katika Afrika ya Tropiki? Ni katika nukta huu wa maendeleo ya kudumu ndipo twapata chanzo cha Ufufuo wa Kati.

21

Madokezo ya mwanzo ya historia ya awali ya baadaye ya Afrika kusini mwa Sahara

Habari zitokanazo na akiolojia

Moja ya mafanikio makubwa ya utafiti wa hivi karibuni wa akiolojia ya Afrika kusini mwa Sahara ni utambuzi kwamba watu katika hatua tofauti za maendeleo ya kiteknolojia walikuwa wakiishi kwa wakati ulcule katika sehemu tofauti za Afrika. Hakukuwa na mwisho mmoja wa enzi ya mawe, kilimo kilianza katika nyakati mbalimbali na jamii nyingi tutakazoziona katika sura chache za mbele zilikuwa bado zinaishi kwa kuwinda na kukusanya chakula kwa kutumia teknolojia ya enzi ya mawe hadi mwisho wa nusu ya kwanza ya elfia ya kwanza ya enzi yetu. Haiwezekani kupata tarehe kamili kinapoishia kipindi tunachokijadili katika eneo ambamo hatuna tarehe yoyote ya kihistoria iliyoandikwa. Tunazo tarehe kadha, lakini nyingi ya tarehe hizo zimetokana na uchunguzi wa kutumia rediokaboni (Kaboni 14). Badala ya kuweka tarehe kamili ya mwisho wa kipindi, sura kuhusu Afrika, Kusini mwa Sahara zinashughulikia zaidi kile kinachojulikana na wengi kama kipindi cha Niolitiki na enzi ya kale ya chuma. Kipindi hiki, kufuatana na ufafanuzi huu, katika sehemu nyingi kinaishia takribani mwaka -1000.

'Niolitiki' katika Afrika, Kusini mwa Sahara ni istilahi ambayo imekuwa ikitumika hapo nyuma kwa njia mbalimbali zisizo na upataiisho aina kwa maana ya uchumi wa kilimo au kuonyesha mikusanyiko ya zana inayojumlisha zana za mawe ya kuchongwa za kakatia, vyombo vya udongo na mara nyingi vijaa. Jamii za kwanza za wakulima si lazima kwamba ziliambatana na mikusanyiko ya zana zinazofanana na hizi. Utafiti wa hivi karibuni katika sehemu nyingi za Afrika unaoonyesha hali ya kuvuka mpaka wa muda wa zana kama vile shola la mawe lililochongwa ambalo lilionekana kwa mara ya kwanza katika sehemu kadha za Afrika baina ya zana za wawindaji na wakusanyaji wa chakula zaidi ya miaka 7000 hadi 8000 iliyopita, lakini zana kama hizi huenda zilikuwa bado zinatumika katika baadhi ya sehemu za bonde la Zaire (ueliani) labda miaka isiyozidi elfu moja iliyopita. Hali kadhalika yaelekea vyombo vya udongo vilikuwa vikitumiwa na wawindaji - wakusanyaji kwa mashirikiano na majitani zao wakulima muda mrefu kabla ya watumiaji wenyewe hawajawa wakulima. Vijaa vilianza kuonekana mara kwa mara kwenye maeneo ya enzi ya mawe na baadaye katika sehemu kadha za Afrika na zinaonyesha matumizi makubwa zaidi ya masalia ya mimea. Tunapozungumzia enzi ya mwanzo ya chuma tuna maana ya kipindi ambapo kulikuwepo na utumiaji wa mfululizo

wa teknolojia ya chuma kinyume na matumizi ya nadra ya zana za chuma. Kwa ujumla, enzi ya chuma ya mwanzo katika Afrika Kusini mwa Sahara ilijipambanna kwa kuwepo na makazi madogomadogo ya watu yaliyotawanyika hapa na pale na sio kwa ukuaji wa mataifa ambayo yalifunuka kwa mara ya kwanza kwenye enzi ya chuma ya baadaye.

Kwa bahati mbaya, ufahamu wetu wa maumbile ya wakazi wa Afrika Kusini mwa Sahara ni finyu sana. Huko Afrika ya Magharibi bila shaka kulikuwepo na watu waliokuwa na maumbile yanayofanana na wakazi wa siku hizi katika eneo hili tokea elfia ya kumi kabla ya enzi zetu (Waiwo-Eluru huko Nigeria) na wamepewa jina la "Mame-Wanegro". Huko Afrika ya Kusini mababu wa Wakhoisani wawindaji - wakusanyaji chakula na wafugaji wa Namibia na Botswana (Wasani na Wakhoikhoi) wa siku hizi walikuwa na maumbile makubwa zaidi kuliko wazawa wao na waliishi katika maeneo yaliyotapakaa hadi Zambia na pengine hata kufikia mto Semliki mashariki mwa Zaire. Ushahidi mzuri kabisa wa jambo hili umepatikana kwenye maeneo ya Gwisho nchini Zambia ambako mkusanyiko wa zana na vyakula vilivyoonakaan vinaonyesha waziwazi kuwa wakazi wa eneo hili walikuwa Wasani wa kale. Uchunguzi wa kibiojenetiki uliofanywa na Singer na Weiner umeonyesha kwamba Wasani na Wanegro wana uhusiano mkubwa sana baina yao kuliko walinganishwapo na kundi lolote la nje, jambo ambalo linaonyesha kuwa wao ni wazawa wa kiasili wa enzi ya mawe wa Afrika. Aidha wataalam hawa wameonyesha uhomojeni wa kibiolojia wa Waafrika wanaoishi kuanzia Afrika ya magharibi hadi Afrika ya Kusini. Ni katika maeneo madogoinadogo tu, k.v. misitu ya Zaire waishiko mbilikino au kaika mazingira ya Kalahari ya Wasan ndiko kulikuwepo na wakazi waliotofautiana sana na hii lazima ifafanuliwe kutokana na mwachano wa kijenetiki. Katika sehemu kama vile ukanda wa Sahel na pembezoni kaskazini - mashariki ya Afrika na huko Madagascar kuna mchanganyiko baina ya idadi kubwa ya watu walio Wanegro na wakazi wa kusini waliojitokeza na kukua kwa wakati wao bila kuwategemea watu wengine kama vile Wamalyo-Polynesia wa Madagascar na watu wauaofanana na wale walioishi kandokando ya Mediterani na kusini-magharibi mwa Asia walioko huko kaskazini-mashariki ya Afrika na Sahara.

Mchango wa Isimu

Jambo la muhimu katika kuielewa enzi ya chuma ya mwanzoni katika Afrika Kusini mwa Sahara ni utambuzi wa thamani ya usuli wa kiisimu. Matukio mawili makubwa yanahusu tu katika kipindi hiki tunachokijadili: kwanza, mgawanyiko wa vikundi mbalimbali katika familia ya lugha ya Kongo - Kordofani, tukitumia istilahi ya Greenberg, na pili, mtawanyiko wa watu wazungumzao Kibantu, ambao sasa idadi yao ni zaidi ya asilimia 90 ya wakazi wanaoishi kusini mwa msitari uliochorwa kutoka Ghuba ya Biafra hadi pwani ya Afrika Mashariki karibu na Malindi. Tunajua machache sana kuhusu tukio la kwanza. Linaloweza kusemwa juu ya lugha hizi ni kwamba lugha za Kordofani ni za zamani sana, ni uyingi za kutosha na aghalabu huzungumzwa na vikundi vidogovidogo sana, vya watu, na pengine vidogo kabisa; kila kijikundi kimoja cha lugha kikijipambanua kutoka lugha za jirani zake. Vikundi vyote hivi vilikusanyika katika jimbo la sasa la Kordofani lililoko

katika jamhuri ya Sudan na mkusanyiko mkubwa umezunguka katika Milima ya Unubi. Lugha za Kordofani zilitawanyika hasa kutoka kwenye lugha za Kinaija-Kongo na zimejitenga kutoka kwa makundi mengine ya lugha ya karibu nazo. Hakuna la maana linaloweza kusemwa kuhusu kiwango cha muda kilichochukuliwa katika kuitenga lugha ya Kordofani kutoka kwenye lahaja za Kinaija-Kongo za familia ya Maine-Kordofani isipokuwa kwamba kujitenga huko kwaweza kuwa kulitokea kati ya mwaka - 10,000 hadi - 8,000.

Kugawanyika kwa lugha za Naija-Kongo kunaweza kuhusishwa na kusambaa polepole kwa watu kuelekea kusini kutoka Sahel kadiri Sahara ilivyozidi kuwa kame. Painter anadhani kuwa mgawanyiko huu ulitokea takriban kati ya mwaka -6000 hadi -3000 lakini kuna mitazamo mingine pia. Armstrong anafikiria kuwa lugha za Nigeria ya kusini zina umri wa kufikia miaka 10,000 -jambo ambalo linamaanisha kwamba mwelekeo wa watu kwenda kusini ulianza mapema zaidi. Yawezekana mitazamo yote hii miwili ikawa sawa kukiwa na baadhi ya wazungumzaji wa lugha ya Kinaija -Kongo waliojitenga kutoka kwenye kundi kuu na baadaye wakaishi peke yao katika mazingira ya porini. Pengine hawa ndio wenzi, wa lugha ya Waiwo-Eluru wa Mame-Negro. Wazungumzaji wengine wa Kinaija-Kongo walitapakaa baadaye kutoka Sahel mara baada ya kuanzishwa kwa hali ya maisha ya ukulima. Tatizo la mtazamo huu ni kwamba wazalishaji wa mwanzoni kabisa wa chakula katika Sahel yaelekea walikuwa ni wafugaji na wala sio wakulima hali. Pendekezo lililotolewa na Sutton kwenye sura yake laweza kutoa utatuzi wa suala hili kwa kuwa kuna ushahidi wa wafugaji wa Sahel kuambatishwa na mundu na vifaa vingine vilivyotambuliwa kuwa vilitumika kwenye utamaduni wa maeneo yahiyo karibu na maji. Hata hivyo, mtawanyiko wa lugha ndani ya familia ya Naija-Kongo utaonekana kuwa unaambatana na utengano wa kijografia wa makundi mbalimbali hasa ya kilimo, utengano ambao ni wa nyuma zaidi kwa kuwezesha vijisehemu pekee vya familia ya Naija-Kongo kujipambanusha wazi kabisa kiisimu.

Tukigeukia upande wa lugha za Kibantu basi tunakabili na hali tofauti kabisa. Kuna lugha za Kibantu zaidi ya 2000 katika Afrika ya Mashariki, Kusini na kati ambazo zina mfanano wa msamiati na maumbo ya kiisimu. Kwa hali hii lugha hizo zinahusiana, uhusiano ambao ulitambuliwa mapema mnamo mwaka 1862 na Bleek ambaye aliunda jina "Bantu" kwa ajili ya lugha hizi kwa sababu zote zilitumia neno "Bantu" kwa kwa maana ya watu. Mtawanyiko baina ya lugha mbalimbali za Kibantu sio mkubwa kama ule wa baina ya lugha mbalimbali za Afrika ya Magharibi na makadirio mengi yanaonyesha kuwa mtawanyiko huu ulitokea takriban mwaka 2000 hadi 3000. Hata hivyo, kuna nadharia za kiisimu mbalimbali kuhusu jinsi Wabantu walivyojitenga kutoka lugha nyinginezo za Afrika ya Magharibi, na kati ya hizi, mbili zimekuwa zikiungwa mkono mara nyingi. Joseph Greenberg, katika uchunguzi wake wa lugha za Kiafrika kwa ujumla alilikabili tatizo hili kwa kiwango kipana na alitumia ushahidi wa kiisimu kwa kutumia data kutoka lugha zipatazo 800. Kwa kutumia maneno ya msingi aligundua kwamba lugha za Kibantu zimekaribiana sana na lugha nyinginezo za Afrika Magharibi kuliko kwa mifano, Kiingereza kilivyokaribiana na Mame-jerumani uhusiano ambao mara nyingi wanaisimu

wameuona kuwa ni wa karibu sana. Kulingana na mahesabu aliyofanya imeonekana kwamba asilimia 42 ya msamiati wa Kibantu unapatikana katika lugha za Afrika ya magharibi zilizo karibu kabisa, ikilinganishwa na asilimia 34 tu ya maneno ya Kiingereza katika lugha ya Mame-Jerumani. Hivyo basi aliweka chimbuko la Kibantu kwa uthabiti kabisa kuwa kwenye eneo la mpakani niwa Nigeria na Kamerun. Marehemu Profesa Guthrie alifuata mkondo wa kiwango kifinyu baada ya kujishughulisha kwa miaka mingi na uchunguzi wa Bantu-linganishi na alichambua lugha na lahaja za Kibantu kama 350 hivi. Alitenga mashina ya maneno ya jamii moja ambayo yalitakiwa kuwa na maana moja ileile katika angalau lugha tatu tofauti. Akitumia seti za kawaida alitengezea Fahirisi ya pamoja ya Kibantu ambayo ilionyesha asilimia ya maneno ya kawaida katika lugha yoyote ya Kibantu. Isoglas (au misitari inayounganisha Kibantu kinachofanana) zilizochorwa zikionyesha eneo-chanzo ambalo kiwango cha watu waliobaki kilikuwa zaidi ya asilimia 50, likiwa katika nyanda za nyasi kusini ya msitu wa Zaire kwenye milima ya chanzo cha mito Zambezi-Zaire. Ni katika eneo - chanzo hili ambako alidhani Mame-bantu waliotokea. Kwa hali hii kuna makubaliano ya pamoja kuhusu chanzo cha lugha za Kibantu kuwa katika Afrika ya Magharibi na kutokubaliana kuhusu kitovu cha mtawanyiko wao. Wataalamu walio tayari kupendekeza kronolojia wanaweka upanukaji wa Kibantu kuwa kati ya miaka 2000 na 3000 iliyopita na kukubali kwamba chuma kilikuwa kikitumiwa na wale waliotawanyika, na wote wanakubali huo mtawanyiko wa haraka; wengine wanasema ulikuwa na haraka mno.

Nafasi ya kilimo

Kilimo, kwa kiasi fulani, ni kumudu mahitaji ya chakula cha mtu na, kwa kiasi fulani, kuwa na makazi ya kudumu kinyume na misafara ya daima ya wawindaji - wakusanyaji. Ukubwa wa vikundi uliongezeka na mfumo wa kijamii ulikuwa changamano zaidi na mwishowe mfumo wa kisiasa uliweza kukua. Kilimo, hasa kilimo cha mashamba na cha bustani, kwa kawaida, kilihitaji wakazi wengi zaidi na ongezeko katika idadi ya wakazi wote kwa ujumla. Wanaakiolojia huzitambua jamii za wakulima kwa ushahidi wa moja kwa moja na ule usio wa moja kwa moja. Ushahidi wa moja kwa moja unajumlisha ugunduzi wa mbegu au nafaka zikiwa katika hali ya ukaboni kwenye machimbo ya kiakiolojia zilizoendelea zaidi. Ushahidi usio dhahiri au ule wa kuhusishwa (ushahidi wa kimazingira), unajumlisha ugunduzi wa zana na vyombo ambavyo vinafikiwa vilitunika kwa kulimia, kuvunia na kwa kutayarishia vyakula vilivyotokana na mazao. Kwa bahati, mbaya hali ya tabia ya nchi ya Afrika Kusini mwa Sahara inazuia ugunduzi mpana wa ushahidi wa moja kwa moja. Kwa kawaida, ogani huclukna siku chache kuchanganuka baada ya kuachwa. Kwa jumla, udongo katika maeneo mengi ya tropiki una mikroba na hauruhusu kutunzika kwa chavua. Mahali chavua inapopatikana, kwa mfano kwenye mbuga na maziwa yaliyo selemu za juu sana kutoka usawa wa bahari, maeneo haya yametengwa mbali mno kutoka kwenye ardhi inayofaa kulina na kwa hiyo haiwezi kutoa ushahidi wa kilimo cha zamani. Tatizo jingine ni kwamba zana na vifaa vya kilimo vilivyo vingi vinakanganya. Kisu cha kumenyea vyakula vya mboga kinaweza kutumiwa kwa kazi

nyingine, vijaa vinaweza kutumiwa kwa kupondea udongo mwekundu kwa ajili ya rangi au kwa kutwangia na kusagia vyakula ambavyo havikulimwa bali vilipatikana, kwa kawaida, katika miktadha mingi ya enzi ya chuma ya nyuma. Mengi ya mazao ya chakula ya Afrika kama vile ndizi, viazi vikuu na mizizi nuingineyo hayatoi chavua na yanalimwa kwa vijiti vya kuchimbulia ili kuzuia kuharibu tyuba. Kwa hali hii, wanakiolojia inabidi wategemee ushahidi usio wa kukisia wanapolusisha kilimo, na kuwepo kwa maeneo ya makazi makubwa, kuwepo kwa kile kinachoonekana kama nyumba za kudumu, matumizi ya vyombo vya udongo au kuwepo kwa makaburi mengi. Kama itakavyojionyesha dhahiri kwenye Sura ya 26 wawindaji - wakusanyaji chakula katika Afrika kwa nadra waliishi katika makazi makubwa, mara nyingi walitumia vyonibo vya udongo na iwapo uvuvi wao au shughuli nyingine maalumu za uwindaji au ukusanyaji wa chakula zilikuwa na mafanikio makubwa, basi waliweza kutengeneza makazi ya kudumu kidogo kama yale ya Khartoum ya mwanzo au Ishango ya enzi ya mawe ya nyuma. Hivyo basi inawezekana, kwa masikitiko, kuhitimisha kwamba mpaka sasa ushahidi wetu wa kutanzua historia ya kilimo cha mwanzoni katika Afrika Kusini mwa Sahara bado ni mfinyu na kwamba nahitimisho yetu yanaweza kuwa ni makisio tu.

Mpaka mwishoni mwa miaka ya 1950 ilidhaniwa na wengi kuwa kilimo kilichelewa katika sehemu nyingi za Afrika Kusini mwa Sahara, lakini kwa kiasi kikubwa kilitokea kwa wakati mmoja na uanzishaji wa teknolojia ya chuma katika sehemu zote za Afrika isipokuwa baadhi ya sehemu za Afrika ya Magharibi na kwamba wazo lilitawanyika kutoka kwenye bonde la nuto Nili hadi mwishowe kufikia sehemu iliyobaki ya Afrika. Lakini ushahidi mpya kutoka Sahara na sehemu nyingine unaonyesha kwamba mambo hayukuwa moja kwa moja namna ile. Maswali ya kwanza dhidi ya mtazamo huu wa chanzo cha kilimo cha Afrika yalifanywa na Murdock aliyependekeza kiini cha sehemu kubwa ya kilimo cha Afrika kuwa magharibi ya Afrika ya Magharibi karibu na vyanzo vya mito Niger na Senegal katika uwanda wa Futa Jallon. Ingawa sehemu kubwa ya nadharia tete ya Murdock haiwezi sasa kuthibitishwa kwa undani zaidi, ingawaje ni wazi kwamba viazi vikuu, namna moja ya mpunga (*Oryza glaberrina*), mtama, mawese na mazao mengine mengi ya chakula yalikuwa ya asili.


Ingawa asili, wakati na namna ya maendeleo ya kilimo cha Kiafrika, yakubalika kwa jumla, ukiacha kando uwezekano wa kuwapo kwa jumuiya za wakulima wa intama katika Bonde la Ufa huko Kenya, kwamba mwanzo wa kilimo cha mashamba katika sehemu za Afrika zinapozungumzwa lugha za Kibantu ulitokea wakati mmoja na wakati wa kuzuka kwa teknolojia ya chuma. Inakubalika na wengi vilevile kwamba mazao makuu ya kilimo kauka sehemu za Afrika wanakoishi Wabantu, kama vile ndizi, viazi vikuu, ulezi na mtama, viliingizwa ama kutoka Afrika ya Magharibi au mintarafu ndizi, kutoka Asia ya kusini-mashariki kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Ng'ombe wa mwanzoni kabisa walikuwa wa kabla ya enzi ya chuma na wanapatikana Afrika ya Mashariki tangu mapema mwanzoni mwa elfia ya kwanza kabla ya enzi zetu na kutokana na ushahidi uliorejewa na Parkington katika Sura 26 itaonekana kwamba kondoo walikuwa wameenea kusini hadi kufikia Rasi huko Afrika ya Kusini kwenye mwanzo wa elfia ya kwanza ya enzi zetu.

Yawezekana kwamba kuenea kwa ufugaji kulikuwa na uhusiano wa hali fulani na mtawanyiko wa utamaduni wa majini uhiofananuliwa na Sutton katika Sura ya 23, kama Ehret alivyoonyesha kwa kusadikisha kabisa ushahidi wa athari ya kijamii ya lugha za Sudan ya Kati kwenye lugha za Kibantu. Amefafanua kwa mfano jinsi maneno yaliyomaanisha "ng'ombe" na istilahi zilizotunika kwa shughuli za ukamuaji zilivyoazimwa na Wabantu kutoka kwa majirani zao wa Sudan ya Kati, bila shaka pamoja na shughuli zenyewe za ufugaji wa ng'ombe na ukamuaji. Kwa misingi ya utofautisho wa kiisimu baina ya waliodhaniwa kuwa wazungumzaji wa lugha ya Wazaa Wasudani wa Kati, Ehret anadhani kwamba wafugaji wa ng'ombe waliwatangulia wakulima. Aidha anaona kuwa mwingiliano huu ulitokea kwa mara ya kwanza karibu na katikati ya miaka elfia ya kwanza kabla ya enzi yetu. Ameonyesha vilevile kwamba maneno ya Mame-Wabantu kwa maana ya "jembe" na "mtama" yalitoka kwenye lugha ya Sudan ya Kati na kwa hiyo lazima tufikirie mwingiliano wa kijamii kati ya watu wa Kinilo-Sahara na mababu wa Wabantu na kuenea kuelekea kusini kwa kilimo cha jembe na ukulima wa mtama hasa katika ulimwengu wa Kibantu. Ingawa upanukaji kidogo wa watu wawezekana kuwa ulifanyika kutokana na maendeleo haya mnamo elfia ya kwanza kabla ya enzi yetu, ushahidi wa kiakiolojia ulioelezwa kwenye sura za mbele unaonyesha waziwazi kwamba upanukaji mkubwa wa wakulima ulifanyika kwenye elfia ya kwanza ya enzi yetu katika sehemu kubwa zaidi ya Afrika ya Kibantu.

Chuma

Swali muhimu katika nijadala wowote wa wakulima kwenye nusu ya kusini ya Afrika ni lile la kuenea kwa uhunzi. Ili kusafisha magugu na vichaka, mapori na misitu, chombo cha kufyeka ndicho rahisi mno kutumia. Enzi ya mawe haikuwa na zana za namna hii na Afrika Kusini mwa Sahara hakukuwepo na enzi ya shaba nyeusi. Ushahidi wa mwanzo kabisa wa utumiaji wa shaba (nyekundu) unatoka Mauretania, na ufuaji shaba ulianza kwenye kipindi cha kati ya karne ya tisa na tano kabla ya enzi za Ukristo, kipindi ambacho ni mapema kidogo zaidi ya ufuaji chuma wa mwanzo kabisa uliothibitishwa huko Afrika ya Magharibi mahali paitwapo Targa kwenye uwanda wa Jos nchini Nigeria ambao ulianza kutoka karne ya tano au ya nne kabla ya enzi za Ukristo.

Maoni ya kutosha yamejitokeza kuhusu suala la asili ya ufuaji chuma wa mwanzo wa Kiafrika. Kuna mitazamo tofauti inayokubalika lakini hakuua hata mmoja ambao umethibitishwa kuwa ni sahihi. Mtazamo mkongwe kuhusu kuenea kwa ufuaji chuma ni kutoka bonde la Naili hasa Meroe, palipoitwa na Sayce "Birmingham ya Afrika". Hata hivyo, hakuna ushahidi thabiti wa kuenea moja kwa moja kwa uhunzi kutoka bonde la Nili kuelekea ama magharibi au kusini. Chuma katika Ethiopia, kilichoanza kutumika kutoka karne ya tano, huenda kilitoka kwenye bandari za Ptolema za Bahari ya Sham kama vile Adulis, ambazo Ethiopia ilikuwa na ushirikiano nazo.



Eneo la chimbuko la Wabantu kwa mtazamo wa Grenberg



Mpaka wa kaskazini wa Wabantu

A

Sehemu ambazo pengine zilikuwa za kilimo



Maeneo ya matumizi ya chuma kabla ya mwaka 400



Msitu

YAMS

YAMS Chanzo cha asili cha mazao ya Kilimo



Jangwa na Sahel

21.1 Nadharia tete inayohusu mwanzo wa Wabantu na mwanzo wa matumizi ya Chuma. (kutoka kwa M. Posnansky)

Ugunduzi wa tarehe za mapema zaidi kwa uhunzi wa Nigeria uliwafanya wataalamu waangalie zaidi juu ya uwezekano wa chanzo chake kuwa huko Afrika ya Kaskazini. Wafoeniki walieneza teknolojia ya chuma kutoka Levant hadi sehemu za pwani ya Afrika Kaskazini katika sehemu ya mwanzo ya elfia ya kwanza kabla ya enzi zetu. Cannah ametoa hoja kwamba kwa kuwa ufuaji chuma umechelewa, takriban mwaka +500 huko daima, karibu na Ziwa Chad, ambapo paelekea kuwapo mahali ilipopitia njia iliyotoka bonde la Nili, basi chuma lazima kilitoka kaskazini. Tarehe nyingine za mapema kidogo kwa ufuaji chuma zinapatikana kutoka Ghana, Hani (+80) na Senegal. Inawezekana vilevile, bila shaka, kufikiria kwamba uhunzi ungeweza kuja kutoka Afrika ya Kaskazini kwa kupitia Mauretania ukifuata nyayo za wafuaji shaba na kuenea kwenye ukanda wa Sudan kuelekea magharibi na kusini, ingawa katika hali hiyo tarehe lazima ziwe za mapema zaidi kwa Senegal na Mauretania kuliko Nigeria. Yawezekana, bila shaka, kufikiria njia nyingi za athari zikileta ufuaji chuma katika Afrika ya tropiki, kukiwa na njia kwenda Mauretania toka Maghreb, nyingine ikikatisha Saliara hadi Nigeria na ya tatu ikikatisha bahari ya Sham hadi Ethiopia pamoja na nyinginezo zikipita pwani ya mashariki kutoka eneo la bahari ya Sham, India au Asia ya kusini-mashariki hadi Afrika Mashariki.

Hivi karibuni wazo linetokea kuwa ufuaji chuma wawezekana ulianza humu humu Afrika. Mwanzilishi madlubuti wa mtazamo huu ni C.A. Diop ambaye anaungwa mkono na Dk. Wai Andah kwenye Sura ya 24 ya juzuu hili. Juu ya hayo inafikiriwa kuwa mengi ya maeneo ya teknolojia ya mwanzo ya chuma ya Afrika ya Magharibi, kama vile yale yanayoambatana na utamaduni wa Nok au ya Baurkina Fasso, yanafungamana na zana za mawe. Kwa hiyo, basi lazima uwezekano ubaki wazi kwamba ufuaji chuma ulijitokeza hasahasa katika miktadha ya enzi ya mawe ya nyuma.

Yale yanayosadikiwa kuwa ni majoko ya hivi karibuni ambayo sasa yanafanyiwa uchunguzi huko Kongo kwa bahati mbaya hayajaongeza lolote jipya kwenye maarifa yetu na pengine hayataonyesha alama zozote za kipindi cha kwanza cha kutumiwa kwayo. Lakini yakishapatikana na kuwekwa tarehe, yanaweza kutoa madokezo ya njia iliyofuatwa na biashara ya chuma kati ya Shaba na bahari au kufanya iwezekane kugundua tarehe kadha kwa ajili ya maendeleo haya ya nyuma.


Mpaka sasa ni tarehe chache mno zilizokwishapatikana kwa ajili ya maeneo ya enzi ya chuma ya mwanzoni kwa ujumla kiasi kwamba haiwezekani hata kuwa na hakika juu ya tarehe za uanzishaji wa ufuaji chuma katika sehemu mbalimbali za Afrika ya tropiki. Katika miaka ya mwanzo ya 1960, kwa mfano, ilifikiriwa kwamba ufuaji chuma ulianza Afrika Mashariki takriban mwaka +1000, na sasa tarehe hii imesukumwa nyuma kwa karibu miaka 750. Ukweli huu umejitokeza pia huko Ghana ambako mpaka lilipovumbuliwa joko la Hani lililotengenezwa kwenye karne ya pili ya enzi zetu, tarehe iliyokuwa ikidondolewa kwa kawaida ilikuwa takriban mwaka +900. Hata hivyo maliitimisho kadha yanaweza kufanywa. Kwanza, hakuma ushahidi wa kutosha unaoonyesha kuenea kwa moja kwa moja kutoka bonde la Nili hadi Afrika ya Magharibi hivyo wazo la mtawanyiko kutoka Meroe lina ushahidi mdogo mno wa kuliunga mkono. Pili, hakuna ushahidi chanya wa vyombo vya udongo vya kuokwa kwenye joko au shimoni

katika Afrika ya Magharibi, kwenye kipindi kabla ya mwaka +0, na ushahidi wa kiethografia wa ukuaji wa humuhumu wa ufuaji chuma bado haujafanuliwa katika mapana yake ua unataja sanasana mazingira ya elfia ya pili ya enzi za Ukristo. Kwa hivyo basi, ni lazima tuwe na mawazo yasiyofungwa kuhusu asili ya ufuaji chuma. Ushahidi mchache uliopo unaonyesha tarehe za mapema zaidi kwa Afrika ya Mashariki au ya Kati, jambo ambalo zaidi linaonyesha mtawanyiko kutoka Afrika ya Magharibi kuelekea kusini na mashariki. Ufuaji chuma ulienea kwa kasi ya kutosha kwani taruhe za mwanzo kabisa kwa Afrika ya Kusini ni takribani mwaka +400, yaani karni chache baadaye kuliko nyingi ya tarehe za Afrika ya Magharibi.

Kwa hivyo basi, kuenea huku kwa kasi kwa uhunzi, wengine watakuita kuenea kwa kishindo, kunafanana na ushahidi wa kiisimu. Ushahidi wa kiakiolojia kutoka Afrika ya Magharibi uliopatikana uliohusu elfia ya kwanza ya enzi za Ukristo, unaonyesha mfanano dhahiri wa umbo na mapambo katika sehemu kubwa ya Afrika ya tropiki - jambo ambalo linaweza kufanuliwa tu kwa kupendokeza nadharia tete ya asili moja ya vitu hivi mbalimbali (Soper, 1971, kwa Afrika ya Mashariki, na Huffman, 1970, kwa Afrika Kusini). Baada ya mfanano wa mwanzoni, tofauti ya kinajimbo ilitokea. Mwelekeo huu unajionyesha vizuri zaidi huko Zambia ambako labda uchunguzi wa undani zaidi wa vyombo vya udongo vya enzi ya chuma umefanywa kuliko sehemu nyingine katika Afrika ya tropiki. Hitutisho la Ehret, ambaye kwa misingi ya ushahidi wa kiisimu anafikiria dhahiri juu ya "mikusaniko isiyoshikamana sana ya jamii huru lakini zenye maingiliano mwafaka" zikiishi pamoja na wawindaji-wakusanyaji wasiosilimishwa, pia linakubalika sana kwa misingi ya kikiolojia. Kadiri jamii hizi za Kibantu zilivyopata uzoefu wa mazingira maalumu, ndivyo maingiliano yao na jamii za mbali zaidi yalivyopungua na lugha na tamaduni zao kujitenga.

Kubadilishana baina ya kanda mbalimbali za Bara

Jambo jingine la historia ya Afrika ya tropiki ya kipindi hiki linalohitaji kusisitizwa ni athari iliyoendelea na kuongezeka ya Afrika ya Kaskazini kwenye ukanda wa Sudan. Sahara, kama ilivyoonekana kwenye sura za mwanzo, haikuwa kuziizi au ardhi isiyo na mwenyewe bali eneo lenye historia yake kamili ambayo sehemu kubwa yake hado inahitaji kufumbuliwa. Kwa hali yake ya jangwa wakazi wake walikuwa wachache na wenye kuhamahama na kwenye kipindi hiki tunachokishughulikia, wengi wa wakazi wake bila shaka walikuwa wafugaji ambao walikuwa wakihama kutoka jangwani kwenda milimani, kama vile Hoggar, Tassili, Tibesti, na kutoka ukanda wa Sahel kuelekea kaskazini na kusini kufuatana na misimu ya mwaka. Ni vigumu sana vilevile kuweka kiwango halisi cha mahusiano kilichokuwepo ama kuelezea athari zake, ingawa katika miaka ya hivi karibuni uchunguzi wa kiakiolojia kwenye ukanda wa Sudan unaonyesha waziwazi kwamba mahusiano hayo yalikuwa ya aina mbili yasiyo ya moja kwa moja, kama yale yanayoonyeshwa na athari za kuhamahama na yaliyo ya moja kwa moja, kama yale ambayo huenda yalikuswa kwa kupitia mahusiano ya kibiashara na utunijaji wa



21.2 Vyanzo vya Shaba nyekundu na njia za misafara kuvuka Sahara (M. Posnansky 1971)

madini. Taarifa yetu kwa sasa inajumuisha kumbukumbu za fasihi ya kirasimi, michoro na nakshi za mawe huko Sahara na ushahidi wa kiakiolojia.

Kabla ya kuushughulikia ushahidi wa maandishi kuhusu ushirikiano kupitia Sahara, ni lazima tutaje ushirikiano wa namna mbili wa moja kwa moja kupitia baharini yaliyoripotiwa kuwa yalifanyika kutoka Mediterani hadi Afrika ya magharibi. Kwanza ni safari ya baharini ya karibu miaka mitatu inayosemekana kuwa ilifanywa na mabaharia wa Kifoeniki wakimhudumia Necho. Ushahidi wa kimazingira unaopinga safari hii ni mwingi sana. Safari ya pili ya baharini inasemekana ilifanywa na Mkariteji, Hanno. Mauny (1960) ameonyesha kwamba sababu zilezile za kimazingira zilizotajwa dhidi ya utawala wa Necho zitafaa kabisa kupingia safari ya Hanno. Iwapo safari hizi zilifanywa, basi bila shaka hazikuwa na athari yoyote kwa Afrika ya Magharibi. Hakuna vifaa vyovyote vya Kikariteji, Kifoeniki au Kimisri vyenye uthibitisho usio na tashwishi au ulio wa dhahiri kabisa na vilivyowekewa tarehe ambavyo viinapatikana kwenye pwani ya Afrika ya Magharibi. Wakariteji bila shaka walipata dhahabu kwenye pwani ya Atlantiki ya Moroko kama maelezo ya "Biashara bubu ya mali kwa mali" ya Herodotus yanavyoonyesha, lakini kuna shaka iwapo mabaharia wa kale walifika kusini zaidi ya mto Senegali.

Ushahidi mwingi zaidi wa ushirikiano kwenye kipindi cha kabla ya Uislamu unatoka kwenye sanaa ya mawe na ushahidi wa kiakiolojia. Sanaa ya mawe inaonyesha kwamba njia nyingi za mawasiliano na ukanda wa Sudan zilikuwa wazi mapema tangu mwaka -500. Michoro hasa ni ya mikokoteni, baadhi ikikokotwa na farasi na baadhi na maksai. Lhote (1953) ameeleza kwamba hakuna mikokoteni huko Air au Tibesti isipokuwa karibu na Fezzan. Mingi kati ya michoro ya maksai iko karibu na njia ya magharibi. Pengine hatupaswi kuwa na mahitimisho mengi kutokana na mikokoteni Daniels amehitimisha kwamba mikokoteni inaonyesha zaidi matumizi makubwa yaliyoenea sehemu nyingi ya aina ya gari ya kawaida kuliko mfumo tata wa barabara za Sahara. Pale ambapo data imeweza kupatikana, kama vile yale yaliyohusishwa na vijiji vya enzi ya mwisho ya Neolithiki yanaonekana kuhusiana na kipindi cha kati ya -1100 na -400. Hatuna budi kukubali kutokana na sanaa ya mianuba kwamba njia za kuvuka Sahara ziliwezekana tu kwa kutumia farasi, maksai na pengine punda waliokuwa hodari. Njia ya mashariki ina makutano makubwa katika Tassili, na Lhote ameonyesha uwezekano wa kuwepo vituo vya mwisho katika pwani ya Tripoli katika inji kama Leptis, Oea na Sabratha.

Mapema katika sura hii tumezungumzia ushahidi wa machimbo ya shaba nyekundu nchini Mauretania. Ushahidi wa kiakiolojia utaonyesha kwamba njia ya magharibi ilikuwa na umuhimu mkubwa kuliko ya mashariki kupitia Tassili. Uchimbaji na utumiaji wa shaba nyekundu huenda ulitoa motisha ya kuchimba na kutumia chuma katika sehemu za kusini. Kutokana na mabaki yaliyopatikana katika makaburi ya huko Senegal kuna ushahidi wa kutosha wa athari za Kimaghreb, na mtu yeyote anaweza kuona kuwa ulusiano wa biashara uliongezeka taratibu kutoka mwanzoni katika elfia ya kwanza au ya pili kabla ya enzi zetu. Inawezekana pia kuwa ngamia walitumiwa katika biashara katika njia hii ya magharibi kabla ya kufika kwa Waarabu mwishoni mwa karne ya nane ya enzi za Ukristo kwani ngamia walikuwa wakijulikana Afrika ya kaskazini tangu karne ya kwanza kabla ya

enzi za Ukristo Caesar ametaja kukamatwa kwao mwaka -46); na walikuwa wametapakaa kote ilipofika karne ya nne.

22

Pwani ya Afrika Mashariki na dhima yake katika biashara ya baharini

Moja ya sifa kubwa ya Pwani ya Afrika Mashariki ni urahisi wa kufikika kwake kutoka Bara na baharini pia. Kufikika huku kwa kutokea bara kumekuwa muhimu sana kwa nyendo za watu kuelekea ukanda wa pwani na hii inasaidia kufafanua mchangamano wa makabila na utamaduni wa eneo hili. Bahari, kwa upande mwingine, imekuwa njia ya uawasiliano na ulimwengu wa nje. Kwa hiyo, moja ya sifa muhimu za historia ya pwani ya Afrika Mashariki kwa karibu miaka 2,000 iliyopita imekuwa sio utengano bali mwingiliano wa mikondo miwili ya utamaduni ili kujenga utamaduni mpya, yaani utamaduni wa Kiswahili wa pwani. Kitu kilicholeta mambo yote haya ni biashara ambayo iliwezesha uingizwaji wa pwani ya Afrika Mashariki katika mfumo wa uchumi wa kimataifa pamoja na matokeo yanayoambatana na mfumo huo.

Hata hivyo, upungufu wa kumbukumbu za kihistoria unafanya iwe vigumu kuijenga upya historia ya pwani ya Afrika Mashariki kabla ya karne ya saba ya enzi za Ukristo. Vyanzo vyote vilivyopo vya nyaraka na pia vile vinavyotokana na sarafu na nishani, ni matokeo ya biashara ya kimataifa, na tuna vitu vichache sana vinavyohusu historia ya pwani kabla ya kuanzishwa kwa mawasiliano ya kimataifa. Vyanzo vya awali kabisa vya nyaraka za Kiyunani-Kirumi vinarejelea japo kwa njia isiyo ya moja kwa moja (ingawa aghalabu ni ya thamani) mambo kuhusu pwani ya mashariki ya Afrika. Strabo (- 29 had + 19) ambaye alishuhudia zama za kuupanua ufalme wa Kirumi chini ya Augusto anaelezea sio tu matukio ya wakati ule na pengine yale aliyoyashuhudia kwa macho yake kuhusu biashara ya eneo la bahari ya Shara na Bahari ya Hindi, bali hutaja pia katika maelezo hayo habari chache chache za sehemu za kale za kijografia ambazo zimepotea. Pliny (+23 hadi 79) anaeleza ufalme wa Kirumi ukiwa katika upeo wa mamlaka yake; na maelezo yake juu ya biashara na usafiri katika Bahari ya Hindi na pia juu ya mtindo wa maisha ya anasa na ufukara wa jiji la kifalme la Urumi yanathaminiwa sana. Chanzo muhimu mmo cha habari kuhusu Bahari ya Hindi katika kipindi hiki na maelezo ya kwanza ya moja kwa moja, japo kidogo kuhusu pwani ya Afrika mashariki ni *Periplus Maris Erythraei*, kilichoandikwa na wakala mmoja wa biashara wa Kiyunani asiyejulikana aliyekuwa na makao yake huko Misri. Kimsingi *Periplus* ni maelezo ya mambo yaliyoshuhudiwa kwa macho.

Habari za kutosha kuhusu Bahari ya Hindi kwa jumla na hususa Afrika Mashariki

zinaonekana kwenye Jiografia ya Ptolemy iliyoandikwa yapata mwaka + 156. Ptolemy kwa mahsusi anamshukuru Marinus wa Tiro kwa habari alizoeleza kuhusu Afrika Mashariki. Huyo bila shaka alikuwa mtu aliyeishi wakati mmoja naye. Chanzo cha mwisho cha nyaraka kwa kipindi kinachohusika *Christian Topography* cha Cosomas Indicopleustez kilichoandikwa katika nusu ya kwanza ya karne ya sita ya enzi za Ukristo. Kitabu hiki hufaa zaidi kwa taarifa zake kuhusu Ethiopia, na pia kuhusu kuibaka kwa Waajemi katika Bahari ya Hindi. Kitabu hiki pia chaonyesha ujinga uliokuwapo kuhusu pwani ya Afrika Mashariki kusini mwa Rasi ya Guardafui.

Kwa bahati mbaya bado hatuna ushahidi thabiti wa kiakiolojia kuhusu pwani ya Afrika Mashariki katika kipindi hiki ili kuweza kuthibitisha na kujaliza vyanzo vya nyaraka vilivyopo. Tulichonacho ni mikusanyo kadhaa ya sarafu ambayo imegunduliwa pwani katika kipindi cha robo tatu ya karne.

Hata hivyo, yafaa ijulikane kuwa mikusanyo yote haikupatikana katika maeneo ya kiakiolojia yanayotambulikana au palipochimbwa, na kwamba mazingira ambamo mikusanyo hiyo ilivumbuliwa kwa bahati mbaya hayakurekodiwa vizuri. Tunachoweza kusema tu ni kwanza ushahidi unaotokana na sarafu na nishani haupingani na vyanzo vya nyaraka vilivyopo, na kwamba ni ishara muhimu ya mwendendo wa biashara ya kimataifa katika pwani ya Afrika Mashariki.

Ugunduzi wa kwanza kabisa ulikuwa wa sarafu sita zilizopatikana Kimoni, Kaskazini mwa Tanga 'katika kilima "chini" ya miti yenye umri wa karibu miaka 200', na inaonekana zilikuwa zimefukiwa kwa nuda mrefu. Sarafu hizi zilikuwa za kati ya karne ya tatu na ya kumi na mbili ya enzi za Ukristo. Kwa hiyo, haiyamkiniki kuwa sarafu hizi zilifukiwa kabla ya karne ya kumi na mbili. Lakini bado hakujawa na uhakika kama sarafu za awali zililetwa Afrika Mashariki kabla ya majilio ya Uislamu. Ugunduzi wa pili ulikuwa wa kipande kimoja cha dhahabu cha Ptolemy Soter (- 116 hadi - 108) ambacho huenda kilitokea sehemu fulani ya pwani.

Mikusanyo kadhaa ambayo asili yake haijulikani ilionyeshwa katika Jumba la Makumbusho la Zanzibar mnamo mwaka 1955. Mkusanyo wa kwanza, ulikuwa katika bahasha iliyoandikwa Otesiphon (mji mkuu wa falme za Parthi na Sassanid karibu na Baghdad) ulionyeshwa sarafu tano za Kiajemi za kati ya karne ya kwanza na ya tatu ya enzi za Ukristo. Freeman - Grenville, alipozichunguza sarafu hizi aliona zilikuwa bado zimegandwa na "aina maalum ya uchafu" ambao unapatikana zaidi huko Zanzibar na hii yaonyesha kwamba zilichimbuliwa mahali fulani kisiwani Zanzibar. Makundi mawili mengine ya sarafu pia yalikuwa yamegandwa na aina hiihi ya uchafu na bila shaka nayo yalichimbuliwa Zanzibar au Pemba. Yalikuwa ya muda mrefu, kuanzia karne ya pili kabla ya enzi za Ukristo hadi karne ya kumi na nne. Hii yaonyesha kwamba mikusanyo hiyo haikuwa sarafu iliyofichwa bali ni mikusanyo iliyoonekana kwa bahati tu.

Mikusanyo miwili iliyobaki ina matatizo hayahaya ya ufafanuzi. Haywood anadai kuwa aligundua mkusanyiko mkubwa wa sarafu na chombo chenye umbo kama amfora ya Kiyunani huko Bur Gao (Port Danford) mwaka 1913. Chombo hiki kilivunjika wakati wa dhoruba na kwa bahati mbaya alivitupa vipande vyake. Mkusanyo huu waelekea uko katika

mafungu mawili. Fungu la kwanza ambalo ndilo linaelekea kuwa kiini cha mkusanyo lina sarafu sabini na tano za Misri ya enzi za Ptolemy, ufalme wa Kirumi na Byzantium na ni za kipindi kuanzia karne ya kumi na tatu kabla ya enzi za Ukristo hadi nusu ya kwanza ya karne ya enzi za Ukristo. Fungu la pili lina sarafu kuini na tatu za Wameluk na Misri ilipokuwa chini ya Waturuki. Hizi sarafu ni za kipindi cha kuanzia karne ya kumi na tatu ya enzi zetu na kuendelea. Wheeler anaona kwamba "umuhimu wa ugunduzi huu hauwezi ukawa duni" kwa sababu ya kuongezeka kwa sarafu za Misri hapo badaye. Yawezekana sarafu hizi ziliongezwa kwenye mkusanyo baada ya muda mrefu kabla hazijaingia mikononi mwa wataalamu wa sarafu na nishani. Kwa hali hii, kiini cha mkusanyo kingekuwa kimeshawekwa muda fulani baada ya nusu ya kwanza ya karne ya nne.

Mkusanyo mwingine unadhaniwa ulichimbuliwa luko Dimbani, Zanzibar ya kusini na mkulima mzee, Idi Usi, ambaye sasa amefariki; na ulipitia mikononi mwa mkusanyaji asiye stadi. Sarafu hizi zimefanyiwa utambuzi wa juu juu tu. Kiini chake chaelekea kuwa na sarafu ishirini na tisa za Kirumi na moja ya Kiparthi za karne ya kwanza hadi ya nne ya enzi za Ukristo. Aidha, mkusanyo unajumuisha sarafu ya Kichina ya mwishoni mwa karne ya kumi na mbili na sarafu za baadaye za Kiislamu, Ulaya na hata za Afrika ya wakati wa ukoloni za kipindi hadi kufikia mwishoni mwa karne ya kumi na tisa. Inawezekana kushauri kwamba, kama ilivyo kwa mkusanyo wa Haywood, sarafu za baadaye huenda ziliongezwa kwenye kiini baada ya muda mrefu kúpita.

Kipengee cha Bara

Ushahidi wa kwanza kabisa kuhusu watu wa pwani ya Afrika Mashariki unatoka kwenye *Periplus* ambao unawaeleza wakazi wa pwani kuwa walikuwa "wakubwa sana kwa kimo". Oliver anadhani kuwa walikuwa Wakushi waliofanana na wakulima wa mwishoni mwa enzi ya mawe walioishi katika nyanda za juu za Kenya kuanzia takriban mwaka - 1000. Kulingana na ushahidi wa kiakiolojia uliopo wakati huo walikuwa watu wa "kimo kirefu". Kwa kuwa vifaa vya chuma vinaonekana kuwa katika orodha ya vitu vilivyolewa kutoka nje, hii imaonyesha kwamba watu wa pwani walikuwa bado hawajui kufua chuma. Kuna vikundi vidogovidogo vya watu wanaozungumza Kikushi wanaoishi karibu na pwani na katika sehemu zilizotajwa hapo juu. Watu hawa ni kama vile Wasanye waishio karibu na Tana na Wanubugu wa Usambani, ambao huenda ni vizalia vya wakazi hawa wa awali wa pwani.

Ushahidi wa kiakiolojia unaonyesha mpenyo wa haraka wa watumiaji wa chuma, pengine wasemaji wa lugha za Kibantu, kwenye bani ya karibu na pwani kunako karne za mwanzoni za enzi za Ukristo. Yawezekana pia walifuata ukanda wa pwani kuelekea juu kutoka kusini na kushika maeneo ya kusini mwa Pare na Kwale, nyuma ya Mombasa. Baadaye yaonekana walifuata mwanubao kuelekea juu hadi kufikia Barawa, na juu ya ukanda wa Pangani hadi Pare ya kaskazini na eneo la Kilimanjaro ilipofikia katikati ya elfia ya kwanza ya enzi zetu. Katika kupanuka kwao pengine waliwameza watu waliokuwa wakiishi ukanda wa pwani hapo kabla.

Kutokana na ushahidi uliopo ni vigumu kupata picha ya kutosha ya uchumi na jamii ya pwani kabla ya kuanzishwa kwa njia za ushirikiano wa kibiashara wa kimataifa. Yawezekana watu walikuwa wakulima kama Wakushi wa mwishoni mwa enzi za mawe walioishi bara. Kutokana na masimulizi ya *Periplus* ni wazi kwamba uvuvi ulikuwa na nafasi muhimu sana katika uchumi, na masimulizi haya yanatoa maelezo sahihi kabisa ya utegaji wa samaki kwa kutumia "madema", njia ambayo bado inatumika pwani, Lakini, kwa jumla, inaelekea kuwa watu waliishi pwani tu. Walikuwa na ngalawa na mashua ndogo za kushonwa" na sio majahazi ya kuendea mbali baharini. Kwa bahati mbaya, hatuna ushahidi kuhusu utaratibu wa kijamii na kisiasa katika kipindi hiki, kwani ingawa *Periplus* inataja machifu katika kila mji wenye soko, yawezekana kuwa biasbara ya kimataifa ndiyo ilikuwa sababu kubwa ya kujitokeza kwa machifu na pia kwa miji ya masoko. Kutokana na hali hii inaonekana kwamba wakazi wa pwani ya Afrika ya Mashariki kabla ya kuanzishwa kwa ushirikiano wa kibiashara wa kimataifa, walikuwa kwenye kiwango cha chini kidogo cha maendeleo ya kiteknolojia na pengine ya kijamii na kisiasa pia. Kwa hiyo, ushirikiano wa kibiashara wa kimataifa ulipoanzishwa, juhudi hizi zilifanywa na mabaharia kutoka kaskazini mwa Bahari ya Hindi, pamoja na mambo yote yaliyotokea kutokana na hali hii.

Kipengee cha bahari

Iwapo uwezekano wa kufikika kutoka bara umeifanya pwani ya Afrika Mashariki kuwa sehemu halisi ikamilishayo Afrika kihistoria, uwezekano wa kufikika kutoka baharini umeifanya iwe na historia ndefu ya uhusiano wa kibiashara, athari za kiutamaduni na miendo ya watu kutoka nchi za ng'ambo ya Bahari ya Hindi. Kwa hiyo, historia ya Magharibi mwa Bahari ya Hindi ya mpaka karne ya saba, kwa kiasi kikubwa, ni historia ya maingiliano baina ya sehemu mbili tofauti, kati ya Afrika Mashariki na Mashariki ya Kati, na kati ya Mashariki ya Kati na India, na pia ya dhima ya upatanishi iliyochukuliwa na Mashariki ya Kati baina ya Bahari ya Hindi na Mediterani.

Maingiliano ya aina hiyo yaliwezekana kutokana na maendeleo ya tekinolojia mnaifaka ya baharini na ujuzi wa kuzitumia pepo za mikondo ya Bahari ya Hindi. Sifa ya kijografia ya Bahari ya Hindi ihiyo muhimu zaidi ni kugeuka kwa pepo za Monsuni kufuatana na misimu. Ni dhahiri kwamba mwanzoni mwa enzi za Ukristo mabaharia wa Bahari ya Hindi tayari walikwishajua matumizi ya pepo hizi. Pia walikuwa wamekwishapata ufumbuzi wa tatizo la kiufundi la kujenga vyombo vikubwa vya kutosha katika eneo lisilo na chuma kwa "kushona" mbao pamoja na utembo.

Kwa hiyo, eneo lenye Monsuni za kuaninika na kiwango cha taratibu za kibiashara katika Afrika ya Mashariki husaidia kufafanua shughuli za kawaida za majahazi yatumiayo pepo za Monsuni. Kutokana na taratibu nyepesi za kibiashara ambazo zilihusisha mabadilishano ya moja kwa moja kati ya vyombo vya kigeni na miji yenye masoko, ilivyokuwa kawaida katika kipindi kabla ya karne ya saba, haielekei kama majahazi ya kaskazini yalikuwenda kusini zaidi ya Zanzibar.

Ukuaji wa Biashara Magharibi mwa Bahari ya Hindi

Ushindi wa awali kabisa wa kihistoria kuhusu magharibi mwa Bahari ya Hindi unaonyesha kwamba kinyume cha msisitizo wa kawaida utolewao katika vitabu vya kiada, hakukuwepo na ushirikiano wa kibiashara, wa moja kwa moja au vinginevyo, kati ya Afrika ya Mashariki na India kabla ya karne ya saba ya enzi za Ukristo. Hata biashara kati ya India na Mashariki ya Kati hadi wakati wa *Periplus* yaelekea ilihusu bidhaa chache tu za anasa. Bara Hindi kwa kiasi kikubwa ilikuwa likijitegemea, hasa katika bidhaa kuu za mazao ya "misitu" ambayo Afrika Mashariki ingeweza kutoa. Kusema kweh, India inaelekea ilikuwa mwuzaji mashuhuri wa meno ya ndovu nehi za nje wakati huu, jambo ambalo huenda lilichelewesha kuanza kutumiwa kwa meno ya ndovu ya Afrika.

Inaelekea kuwa uwindaji wa ndovu katika Afrika Mashariki ulichochea na ushindani mkubwa kati ya mataifa yaliyofuata himaya ya Kiyunani baada ya kifo cha Alexander. Udhhibiti wa njia za nchi kavu zinazokwenda India na Waseleusid uliwashurutisha Waptolemi wa Misri kutafuta meno ya ndovu kutoka schemu nyinginezo. Mahitaji ya kwanza kabisa yalikuwa kupata ndovu wenyewe. Kwa hiyo waligeukia kwenye pwani ya Afrika ya Bahari ya Shamu, wakianzisha msururu wa makambi ya kuwindia ndovu hadi kufikia mdomo wa Bahari ya Shamu. Hivyo basi matokeo ya sera ya Waptolemi yalikuwa ni upanuzi mkubwa wa biashara ya meno ya ndovu.

Kupoteza mamlaka juu ya Siria wakati wa utawala wa Ptolemy wa V (- 204 hadi 181), na kukua kwa mahitaji ya bidhaa za Kiarabu na Kihindi huko Italia wakati ambapo mrima wa pwani ya Bahari ya Shamu ulikuwa unaanza kuishiwa meno ya ndovu, kuliifazimisha Misri kuanza kutumia njia ya bahari ya kusini ili kuendeleza uhusiano wa kibiashara na India. Ilipofikia mwisho wa karne ya pili kabla ya enzi zetu, Eudoxus alichukua fursa ya kunitumia nahodha wa Kihindi alyepatikana katika meli iliyoangamia, kufanya safari ya kwanza ya moja kwa moja hadi India. Biashara ya India ilitendelea kukua vya kutosha hadi wakateuliwa maafisa "wasimamizi wa Bahari ya Shamu na ya Hindi" kati ya mwaka -110 na -51. Kwa hiyo, biashara ya Misri na Bara Hindi kwa wakati ule haikuwa ya moja kwa moja, bali ilipitia vituo vya kusini-magharibi mwa Bara Arabuni. Kwa hali hii, eneo la kusini-magharibi mwa bara Arabuni lilishika nafasi muhimu ya kuwa kati na kujitwalia sehemu yake ya faida ya biashara ambayo ilijulikana kote.

Watu wa kusini-magharibi mwa bara Arabuni pia yaonekana walidhibiti tawi jingine la biashara lililoelekea kwenye pwani ya Afrika ya mashariki. Tayari inekwishaelezwa kwamba mojawapo ya sababu muhimu za upanuzi wa biashara ya Waptolemi kusini mwa Bahari ya Sham ilikuwa ni kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa za anasa za (nchi za) Mashariki (yaani za Asta), ikiwa ni pamoja na meno ya ndovu. Ni vigunu kuonyesha sawasawa kabisa ni mapema kiasi gani na ni hadi mahali gani kusini mwa pwani shughuli hizo za biashara zilikoenea kwenye kipindi cha kabla ya Urumi. Hii yatokana na kutokuwepo kwa ushahidi wa kiakiolojia. Hadi leo ni sarafu moja tu ya dhahabu ya Kiptoleimi ya mwisho wa karne ya pili kabla ya enzi zetu iliyopatikana karibu na Dar es Salaam. Papo hapo zile sarafu ishirini na mbili za Kiptoleimi kwenye mkusanyo wa

Haywood hazionyeshi uwezekano kuwa ziliwekwa kabla ya karne ya nne ya enzi za Ukristo.

Kupanuka kwa Biashara ya chini ya Warumi

Kutokana na kuanzishwa kwa Himaya ya Kirumi chini ya Agosto, mahitaji ya bidhaa za Mashariki huko Mediterani yaliongezeka sana. Kama Pliny alivyolalamika: "Kwa makadirio ya chini kabisa Bara Hindi, Uchina na Peninsula (ya Uarabuni) huchukua kutoka katika dola yetu *sesterces* milioni 100 kila mwaka - hiyo ndio idadi ya gharama tunazolipia anasa na wanawake wetu." Kupanuka kwa soko chini ya Agosto kulilicta sera ya uchokozi zaidi katika Bahari ya Shamu. Sera hiyo ililengwa kuvunja umilikaji pekee wa Waarabu katika biashara ya Mashariki. Warumi walitaka kuanzisha njia ya baharini ya moja kwa moja hadi Bara Hindi na kudhibiti ncha ya kusini ya "njia ya ubani" katika msafara wa mwaka -24 ulioongozwa na Gallus.

Pamoja na kuingia kwa Warumi katika biashara ya Bahari ya Hindi, *Periplus* yenyewe hata hivyo inatoa picha ya biashara yenye msisiku mkubwa kabisa ikiwa bado mikononi mwa Wahindi na Waarabu. Wahindi walifanya biashara zaidi katika Ghuba ya Uajemi na Bahari ya Shamu, lakini sio kusini mwa Rasi ya Guardafui. Huku wakishirikiana katika biashara ya Bahari ya Hindi na Wahindi na pia kwa kiasi hicho kuwa kikiongezeka na Warumi, Waarabu walielekea kufaidi umilikaji wa dhali wa biashara na pwani ya Afrika Mashariki. Ukweli huu wa mambo unethubitishwa na tatizo la Warumi la kutojua pwani ya Afrika kusini kwa Rasi ya Guardafui kabla ya *Perplus*. Zaidi ya hapo, ingawa *Periplus* ilitoa maelezo ya mambo yaliyoonekana kwa macho juu ya pwani ya Afrika Mashariki, kule kuwapo kwa aya nne tu zinazozungumzia pwani hii kunaonyesha kuwa eneo hili lilikuwa nje ya ufikio wa kawaida wa shughuli za Wayunani na Warumi.

Kuingizwa kwa Pwani ya Afrika Mashariki katika Mfumo wa Kiuchumi wa Kirumi

Bila kujali kiwango cha shughuli za kibiashara za Waarabu kilivyokuwa katika pwani ya Afrika Mashariki katika kipindi kabla ya Warumi, ni dhahiri kwamba shughuli hizi zilipata msisimko mpya kutokana na muungano wa kiuchumi na utajiri ulioongezeka wa dola ya Kirumi. Mahitaji ya meno ya ndovu yaliongezeaka sana, kwani Warumi walianza kuyatumia sio tu kwa kutengeneza sanamu na vitana, bali pia viti, meza, matundu ya ndege na makwama (maalum); kulikuwa hata na banda la farasi lililotengenezwa kwa ineno ya ndovu kwa ajili ya farasi wa kifalme. Kunako karne ya kwanza ya enzi yetu meno ya ndovu yaliweza kupatikana tu kutoka mbali ndani ya eneo la Nili ya Juu, kushuka chini hadi Adulis. Kwa sababu hiyo, ugavi wa meno ya ndovu kutoka pwani ya Afrika Mashariki, ingawa yalifikiriwa kuwa ya thamani ndogo kuliko yale ya Adulis, yalianza kujipatia umuhini mkubwa. Kupatikana kwa meno haya kulisaidia kuingiza maeneo zaidi katika mfumo wa kimataifa wa biashara anubao kitovu chake kilikuwa huko Mediterani kupitia taifa la kusini-magharibi mwa Bara Arabuni la Himyar. Kwa hiyo basi, uingizaji wa pwani ya Afrika Mashariki katika mfumo wa kimataifa ulikuwa sio tu kwenye kiwango cha

biashara, bali pia ulihusu kutawaliwa kisiasa na kupenywa kwa jamii. Kupenywa huku kwa jamii yawezekana ndio ulianza kujenga tabaka la machotara waliosafiri na kufanya biashara pwani. Hao ndio walikuwa mawakala wa mfumo wa kimataifa wa biashara.

Azania, kama Warumi walivyoiita pwani ya Afrika kusini mwa Rasi ya Hafun, huenda haikuwa imeunganika kiuchumi. Ilikuwa na mfululizo wa miji yenye masoko, kila mji ukiwa na chifu wake, kila munoja ukitegemea mrima mwembamba kwa kupatia bidhaa za kunza nje. Kila mji ulitenbelewa moja kwa moja na majahazi yaliyotumia pepo za Monsuni. *Periplus* inataja mahali kadhaa kama vile Sarapion, huenda maili chache kaskazini mwa Merca, Nikon, pengine Burgeo (Port Dunford), na visiwa vya Pyrale ambavyo vipo katika kikundi cha visiwa vya Lanu. Kusini mwa jamii ya visiwa vya Lamu kuna mabadiliko katika hali ya pwani, kama ilivyoelezwa kwa usahihi kabisa katika *Periplus*. Kiasi cha mwendo wa baharini wa siku mbili nibebe kuna kisiwa cha Meneuthias, "takriban stadia 300 (kama kilometa 55 hivi) kutoka bara, kikiwa katika uwanda wa chini na wenye inisitu". Pemba ni kisiwa cha kwanza kikubwa ambacho mabaharia wa kaskazini wangekifikia, na huenda kisiwa pekee ambacho kingeweza kufikiwa kwa safari ya siku mbili kutoka Lamu. Zaidi ya hapo, kusema kweli Pemba ipo kilometa 50 kutoka hara, kinyume cha Zanzibar iliyopo kilometa 36.

Mji pekee wenye soko kwenye pwani kusini mwa Rasi ya Hafun uliotajwa kwenye *Periplus* ulikuwa Rhapta, ambao labda ulikuwa kati ya Pangani na Dar es Salaam. Kwa kadri ionekanavyo Rhapta ulitawaliwa na chifu wa hapohapo lakini chini ya utawala wa jumla wa taifa la kusini-magharibi mwa Bara Arabuni. Hata hivyo, *Periplus* inaonyesha dalili kwamba utawala huo ulikuwa hasa wa umilikaji wa biashara ya nje uliofanywa na makapteni wa Kiarabu pamoja na inawakala wa Muza. Jukumu la kiuchumi la bandari lilikuwa kusafirisha nje "idadi kubwa ya meno ya ndovu", vipusa, ngamba zenye ubora wa juu kabisa na mafuta kidogo ya nazi. Hivi vilibadilishwa mara nyingi kwa bidhaa za chuma hasa "mikuki iliyotengenezwa Muza maalumu kwa ajili ya biashara hii", mashoka, majambia (masime) na misharasi, aina mbalimbali za vioo na mvinyo na ngano kidogo, si kwa biashara, bali kuwavutia wenyeji".

Kukua kwa haraka kwa biashara kunako karne za mwanzoni za enzi za Ukristo kumeonyeshwa na Ptolemy kwenye nusu ya kwanza ya karne ya pili. Kwenye pwani ya Somalia mji mpya wenye biashara nyingi uliokuwa ukiitwa Kesina ulizuka na sasa mji wa Sarapion unaelezwa kuwa ni "bandari" na Nikon (Toniki) kuwa ni "mji wenye biashara nyingi". Lakini maendeleo ya kushangaza zaidi yalikuwa yametokea huko Rhapta ambao sasa unaelezwa kuwa "mji mkuu" (katika matumizi ya Kiptolemi ukimaanisha kuwa ni mji mkuu wa taifa) na hakuna ufalme wa Kiarabu unaotajwa tena.

Hivyo kunako katikati ya karne ya pili, sehemu kubwa ya pwani ya Afrika Mashariki na angalau sehemu ya ukanda wa Pwani zilikuwa tayari zimeshaingizwa katika mfumo wa kimataifa wa biashara. Nguvu zilizoisukuma mipaka ya biashara hadi kufikia bahari za Kiafrika zilianza kupungua kadiri dola ya Kirumi ilivyoingia katika kipindi kirefu cha kuanguka kwake kwenye karne ya tatu. Kulikuwa na mabadiliko katika biashara ya kimataifa kutoka biashara ya viungo, vito vya thamani na meno ya ndovu hadi wenye

biashara ya pamba na bidhaa zilizozalisliwa viwandani. Biashara ya moja kwa moja yawezekana ilikuwa imekwishasimama kabisa, kama pengo kubwa katika ushahidi wa kisarafu linavyoonyesha, lakini ilirejeshwa kwa muda mfupi mwishoni mwa karne ya tatu na mwanzoni mwa karne ya nne wakati kulipotokea kuimarishwa tena kwa dola kisiasa. Ushahidi wa kisarafu uliopo kwa Afrika ya Mashariki hauridhishi, ingawa unaelekea kuonyesha mabadiliko yaleyale. Mkusanyo wa Haywood ulijumuisha sarafu sita za ufalme wa Kirumi za katikati ya karne ya pili ya enzi yetu, likifuatiwa na pengo ambalo halikuwa na sarafu hadi mwishoni mwa karne ya tatu na ya nne. Kipindi hiki kimewakilishwa na sarafu sabini na moja. Katika mkusanyo wa Dimbani inaelekea kuna sarafu moja tu ya karne ya kwanza. Inaelekea kuwa baki ya sarafu za Kirumi zilizotambuliwa ni za karne ya tatu na ya nne ya enzi za Ukristo.

Mafungamano Mapya ya Uhusiano wa Afrika Mashariki na Nchi za Nje

Kuvunjika kwa mfumo wa biashara ya kimataifa labda kulikuwa na athari mbaya kwa taifa lililoutegemea sana mfumo huu. Taifa hilo ni Himyar iliyoko kusini-magharibi mwa Bara Arabuni. Kupungua kwa mahitaji ya Kirumi ya ubani uliokuwa zao kuu la Himyar, na pia mahitaji ya bidhaa nyingine za anasa za Mashariki ambazo biashara yake ilidhibitiwa na taifa hili bila shaka kuliathiri usitawi wake. Kudidimia kwa taifa hili kiuclumi kulifanya kiweze kushambuliwa kwa urahisi, kwanza na Waethiopia na baadaye na Waajemi. Huko baharini pia ilikuwa imepoteza nafasi yake ya kati kwenye shughuli za kibiashara kwa Waethiopia ambao bandari yao ya Adulis ilijitokeza kama kituo cha kukusanya na kusafirisha meno ya ndovu ya Nili ya Juu kivenda Mediterani.

Hata hivyo, yaonekana Waethiopia walishindwa kumudu kuendeleza biashara ya magharibi mwa Bahari ya Hindi walivyofanya Waarabu kabla yao. Mbali zaidi kwa upande wa mashariki, Uajemi ulikuwa ukijitokeza kama taifa mashuhuri katika ubaharia. Umilikaji wa magharibi mwa Bahari ya Hindi na Waajemi kunako karne ya sita na ya saba, hasa kutokana na kudidimia kwa Waarabu na kushindwa kwa Waethiopia kushika nafasi yao, uliwafanya wawe na athari kubwa kibiashara kwenye pwani ya Afrika Mashariki. Mpaka sasa hakuna ushahidi wowote wa kiakiolojia wa kipindi kabla ya Uislamu, uliokwishapatikana pwani ya Afrika Mashariki isipokuwa labda zile sarafu tano za Kiparthi na Kisassanid ambazo ni za karne tatu za mwanzo za enzi za Ukristo, ambazo yawezekana zilichiinbuliwa huko Zanzibar.

Waajemi pia wanaweza kuwa wamechukua nafasi kubwa ya kuwa kiungo baina ya Afrika mashariki na India. Kuanguka kwa dola ya Kirumi kuliinyima Afrika Mashariki soko lake kuu la pembe za ndovu. Aidha wakati huo India ilikuwa bado inajitosheleza kabisa katika mahitaji ya pembe za ndovu. Lakini mwanzoni mwa karne ya kumi na sita mahitaji ya pembe za ndovu katika India yalianza kuongezeka sana kutokana na utengenezaji wa mapambo ya bibi arusi. Kuongezeka huku kwa mahitaji kuliitokana na mila ya Ki-Hindu ya kuyavunjavunja mapambo hayo ya bibi arusi wakati mmojawapo kati ya mume au mke alipofariki. Hadi kufikia karne ya kumi India na China zilikuwa ndiyo masoko muhimu kabisa kwa pembe za ndovu za Afrika Mashariki.

23

Afrika Masharikki kabla ya karne ya saba


Ni rahisi kupata maelezo kuhusu hali ya watu na jamii katika Afrika Mashariki baada ya mwaka +100 kuliko katika vipindi vya mapema zaidi. Utafiti mkubwa unafanywa sasa kuhusu vipindi hivi vya nyuma na matokeo yake yanasaidia kufanya masahihisho ya kudumu ya mahitimisho yote au baadhi ya yale yaliyokuwa yakishikiliwa hadi hivi karibuni.

Uchunguzi wa miaka 2000 kutoka mwaka -1000 hadi mwaka +1000 ni mgumu. Inahitaji mbinu za hali ya juu sana na idadi kubwa ya taarifa ambazo mpaka sasa akiolojia imeshindwa kuzitoa katika ukamilifu wake. Kwa hali hii, uchunguzi unaofuata ni wa makisio, wa nadharia tete au hata wa uchockozi juu ya hoja kadha ili kuamsha na kuchochea fikra na utafiti.

Kazi kubwa inayowakabili wanazuoni wetu ni jinsi gani wanaweza kuiandika upya historia ya maisha ya wakazi wa Afrika Mashariki kabla ya mwaka 1000. Hii inahitaji jitihada zielekezwe kwenye kuujenga upya muundo wa mabadiliko katika utamaduni tukitumia ushirikiano wa uvumbuzi uliofanywa na wataalamu wa akiolojia, anthiropolojia, Wanaisimu na mabingwa wengine wa mambo ya kale. Ufafanuzi wa kiisimu na uainisho wa watu, kwa kawaida, unaelekeleka na ni wa manufaa kwa wanahistoria na wananthiropolojia. Katika sura hii tumetumia mpangilio wa Greenberg wa makundi ya lugha za Kiafrika ambazo unapatikana vilevile kwenye kitabu za *Zamani* kilichohaririwa na Profesa Ogot.

Jadi ya Uwindaji katika Savana ya Kusini

Katika savana yote na katika misitu midogo iliyoenea sehemu kubwa zaidi ya Afrika Mashariki na Kusini mwa ukanda wa misitu ya Ikweta kwa miaka elfu nyingi kabla ya Enzi ya Chuma, idadi kubwa ya wakazi walikuwa wawindaji, wakusanyaji waliotumia pinde na mishale na mawe kwa kutumia ufundi wa juu. Kwa ujumla, watu hawa walikuwa na umbo ambalo sasa linawakilishwa na wale wanaoitwa Wasani wa Wakhoi-Khoi wanaoishi katika jangwa la Kalahari na ukingoni mwake. Lugha yao yawezekana ilikuwa ya Kikhoisani. Siku hizi lugha hizi zimebakia tu kuwa ni za Wakhoi na Wasani wa Afrika ya kusini na kusini magharibi ya Afrika. Pia katika Afrika ya Mashariki wanahusishwa na makundi madogo mawili tofauti yanayoishi katika Tanzania ya Kaskazini na ya kati yaani Wasandawi na Wahadza.



23.1 Ramani ya Kistasa ya Afrika Mashariki na ramani inayoonyesha msambao wa lugha na watu (kutoka kwa J.E.C. Sutton)

Wanadza wamebakia kuwa wawindaji na wakusanyaji. Ni watu ambao wanahamama na ni mafundi katika kutafuta na kupata vyakula kutokana na misitu ya maeneo yao. Kwa upande mwingine, kwa muda sasa Wasandawi wamekuwa wakiliina mazao na kufuga mbuzi na ng'ombe.

Jambo jingine linalovutia ni kwamba tofauti na sehemu nyingine za Afrika ya Mashariki, eneo hili la Wahadza na Wasandawi na lile lililoko kati ya makabila haya, lina mifumo mingi ya sanaa ya mawe ya uwindaji iliyochorwa kwenye kuta za ndani za mapango ambayo mara kwa mara mnamo enzi za mawe ya nyuma, yalitumiwa kama kambi za muda na makao ya familia. Michoro hii ina maana ya kijamii na aghalabu ya kidini ambayo bado haijaleweka vizuri; lakini pia zinatoa vidokezo vya maana sana kuhusu mbinu za uwindaji, chakula na maisha ya kila siku.

Maisha haya ya uwindaji na ukusanyaji yalikuwa na utamaduni wa kiwango cha juu na njia zake za kiuchumi. Ikiwa ukusanyaji ndio uliokuwa sababu ya kupata kiasi kikubwa cha chakula kilicholiwa, basi kazi ugumu na iliyoheshimiwa ya kupata nyama ilikuwa ya lazima kwa ajili ya mlo kamili na kwa kukidhi hamu ya kula. Yote haya yalitegemea kiwango fulani cha kuhamama, pamoja na kambi za kimisiniu na kutokuwa na makazi ya kudumu, kadiri makundi ya watu yalivyowafuata wanyama au kadiri yalivyokuwa yakitumia chakula kitokanacho na mbogamboga, na hivyo pengine kuwa kizuizi cha kuogezeka kwa idadi ya watu na kuwapo mabadiliko.

Sehemu kubwa zaidi ya eneo pana ambalo hapo awali likikaliwa na wawindaji wakusanyaji, hapo baadaye lilikuwa ndio makao ya wakulima wa Kibantu. Katika baadhi ya maeneo haya ya Kibantu huwa kunasimuliwa habari za kukutana na bahati tu na watu wageni ambao hapo kale waliishi na kuwinda katika vichaka na misitu. Masinulizi haya si maelezo sahihi ya kihistoria, lakini yanaelekea sana kuakisi kiini cha kumbukumbu ya mbali iliyorithishwa kutoka kipindi cha miaka elfu inoja na zaidi iliyopita wakati Wabantu walipokuwa wakilifanya maskani eneo hili la Afrika ya kusini na kati na polepole wakiwawekea mipaka kuwafanya Wasandawi wachache waache nyendo zao za maisha ambazo zilikuwa tofauti na kufnata za Wabantu. Namna nyingine ambayo desturi hii kongwe ya uwindaji inaweza kuonekana katika nyakati za kilimo za baadaye ni umuhimu unaopatiwa ujasiri na ujuzi wa uwindaji katika ngano za Kibantu.

Lakini Afrika ya Mashariki haikuwa sehemu ya Wabantu peke yao. Kama itakavyofanuliwa huko mbele, Uganda ya kaskazimi, sehemu kubwa ya Kenya na sehemu za kaskazini na kati mwa Tanzania, kwa muda mrefu zimekuwa zikikaliwa na wakazi tofauti, wakiwa na lugha za Kikushi Kinilotiki na nyinginezo; na baadhi yao walianza kuishi katika maeneo haya wakati wa enzi ya chuma, na wengine kabla ya hapo. Katika eneo hili la Afrika, kama iliyo kusini zaidi, pana ushahidi wa kiethnografia na wa kiakioiojia wa kuonyesha kuwepo kwa jamii nyingi za wawindaji wakusanyaji katika nyakati za hivi karibuni na za zamani.

Yawezekana kwamba wakati wa sehemu kubwa ya enzi ya mawe, maeneo haya ya kaskazini ya Afrika Mashariki yalikuwa ni ukanda wa mpaka unaobadilikabadilika

walitoka katika eneo hilo. Kinyume chake, wanaweza wakawa walitokana na mashirikiano na usimilisho wa wakazi wa awali pamoja na mahusiano yao ya jadi na wakazi na Nili ambayo yalianzishwa zamani sana. Mfano wa wazi ni mfululizo wa makaburi ya mawe ya ajabu katika eneo hili katika kipindi cha miaka elfu mbili hivi kutoka nyakati za baadaye za desturi za sehemu za maji hadi nyakati za awali za kifugaji.

Ingawa ni vigumu kuhitimisha lolote kutokana na maumbile ya wakazi, inakisiwa kwamba wakazi walio magharibi ya eneo hili walikuwa Waafrika wa jamii ya Kinegroidi. Uchunguzi wa lugha unaonyesha athari kwanza Ethiopia kwenda nyanda za juu za Afrika Mashariki na athari hizo zilibakia muda wote mashariki kidogo mwa eneo hili. Ethiopia ni chimbako la kale kabisa la familia ya lugha ya Kikushi. Nyingi ya lugha za sasa za Kibantu na Kiniloti za Kenya na Tanzania ya kaskazini zinaonyesha ushahidi wa kukopa kutoka kwenye lugha za Kikushi. Katika sehemu chache, hasa kwenye mpaka wa kusini mwa kanda hii, lugha za aina hii za Kikushi cha kusini bado zinadumu, ingawa, bila shaka, zilikuwa na mabadiliko makubwa kutoka Kikushi cha kale. Baadhi ya mambo yanayodluhirisha muingiliano huu wa utamaduni wa Wabantu na Wakushi ni maneno yanayohusiana na ufugaji. Imedhihirika kwamba majina mengi ya mifugo yana asili ya Kikushi.

Athari nyingine za utamaduni wa Kikushi katika historia ya Afrika ya Mashariki zimejitokeza pia katika njia nyingine, na kwa kiasi fulani kwenye asasi za kijamii na kisiasa, hasa muundo wa jamii uliojengwa kwa kufuata rika. Muundo huu umecnea zaidi sehemu za nyanda za juu za Kenya na sehemu za Tanzania ya kaskazini. Lakini maoni haya ni ya kijumla sana, na sio vipengele vyote vya mfumo huu vina asili katika muundo wa jamii za Wakushi. Jambo lililo la asili kabisa ya Kikushi ni mila ya kutahiri, ambayo msambao wake umesadifu sana ule wa mkopo mkubwa wa maneno kutoka Kikushi na kawaida ya kutopenda kuvua samaki, kitu ambacho umuhimu wake katika uzoefu wa kihistoria ya Afrika Mashariki kimejadiliwa hapo juu.

Hivyo tunapata picha ya wafugaji wanaozungunza Kikushi, warefu na wenye ngozi ya maji ya kunde kidogo waliopanua maeneo yao kuelekea kusini na wakajifanya wamilikaji wa ardhi zenye nyasi nzuri, nyanda na hasa nyanda za juu za Kenya na Tanzania ya kaskazini karibu miaka elfu tatu iliyopita. Yote haya yanaweza kuonekana kuwa kama kukieleza upya kiasili cha Kihamiti ambacho sasa kimekataliwa. Ukweli ni kwamba, ingawa vipengele visivyokuwa na mantiki na vilivyotiwa chumvi vya nadharia tete mbalimbali na zisizoelezwa wazi za Kihamiti zinatokana na mafundisho ya huko Ulaya na fikra za ajabu kuhusu Afrika na watu weusi, msingi halisi wa maoni haya haukuwa wa kubuni tu. Baadhi ya mtazamo ilikuwa mikali na tafsi fulani za kihistoria zilikuwa za busara sana. Kosa la hoja zilizohusu Kihamiti lipo katika dhana zake na katika kupagawa kwake kuhusu asili ya watu na mawazo. Ukiwa umeshindwa kuthamini mandhari ya mahali husika mtazamo huu ulisisitiza tu seti mahsusi ya athari kutoka nje yaani, kipengele cha Kikushi na fahari ya ufugaji, badala ya kuona hali hii kama uzoefu mmojawapo tu wa

kihistoria na kiutamaduni wa sehemu nyingi za Afrika Mashariki – uzoefu ambamo jadi kongwe ya uwindaji katika Savana ile ya sehemu za maji iliyoanzishwa wakati wa elfia ya mvua nyingi na tukio la karibuni la Wabantu kuanza kutumia chuma na kulima, ambavyo navyo pia ni vipengele muhimu.

Wabantu na jadi ya kilimo na ya matumizi ya chuma


Wakati ambapo ufugaji na mwiko wa kula samaki ulioahusiana nao, ulikuwa ndio sifa bainifu kuu ya kiutamaduni na kikabila ya Wakushi katika kanda moja ya Afrika Mashariki kwenye elfia ya kwanza, sifa bainifu ya Wabantu wa mwanzoni kwenye elfia iliyofuata ilikuwa ufuaji na utumiaji wa chuma. Jambo lililo muhimu zaidi kuliko lili suala la asili (chanzo) ni ule ukweli kwamba Wabantu wa mwanzoni walitegemea chuma na walitambuliwa kama watu waliokuwa na siri zote za ufuaji chuma. Huenda watu wa mapema zaidi wa Afrika Mashariki hawakukifahamu chuma. Zana na silaha zao walikuwa wakizitengeneza kwa mawe yanayofaa na kuyachongachonga kwa kutumia mbinu za kikale. Kwa mfano, Bonde la Ufa la mashariki katika kanda ya Kushi limebarikiwa kuwa na mawe mazuri ya aina ya Obsidiani ambalo lilitumika katika kutengeneza visu vikali vya mawe vilivyotumika katika shughuli za kuchunia au kukatia. Jamii nyingine za wakati uleule zilizoishi kuzunguka Ziwa Viktoria, hazikuwa na bahati kama vile za kwenye Bonde la Ufa. Lakini lata hivyo, zilifaulu kutengeneza zana kadha kutokana na kwatzi (quartz), chertsi (cherts) na mawe mengineyo yenye sifa nzuri za kupasuka vipande vipande, kama walivyofanya pia wawindaji wa kisavana katika maeneo ya kusini. Kwa watu wote hawa wa namna mbalimbali, kukutana kwa mara ya kwanza na wageni waliotumia teknolojia ya chuma lilikuwa jambo la kushangaza na kusisimua akili.

Upanukaji mkuu wa Wabantu ulikuwa mpana na wa haraka, na sio mfuatano wa awamu za polepole kama ilivyodhaniwa na baadhi ya watawala. Lakini halikuwa jambo la uzururaji usio na lengo wa kinomadi wala ushindi wa kijeshi uliopangwa maalumu. Zilikuwa ni harakati mashuhuri za kujipatia makazi. Upanukaji huu wa Wabantu haukulihusu eneo lote lililojadiliwa hapa. Karibu theluthi moja ya Afrika Mashariki ilibakia nje ya mipaka ya Wabantu kutokana na uwezo wa kujirekebisha na baadhi ya wakati wa mwanzoni, hasa katika kanda ndefu ya Bonde la Ufa la mashariki pamoja na wakazi wake wa kale wa Kikushi walioongezeka wakati wa enzi ya chuma kutokana kufika kwa makundi kadha ya Nilotiki. (Angalia ramani ya kisimu na sehemu zilizotangulia na zinazofuata)

Tafsiri hii ya upanukaji wa Wabantu na kukaa kwao katika Afrika ya Mashariki (na katika nchi za pande za kusini na inagharibi) mwanzoni mwa enzi ya chuma unatokana na mchanganyiko wa ushahidi wa kiisimu na wa kiakiolojia, na pia tafakuri za kijumla za kiethografia. Jambo lililo wazi kuhusu lugha nyingi za Kibantu, hasa zile zilizoko nje ya msitu wa Kongo, ni uhusiano rukubwa ulioko kati ya lugha moja na lugha nyingine ya jirani. Tofauti kati ya lugha hizi inaonekana kuwa ni za hivi karibuni yapata miaka elfu moja au mbili iliyopita. Jambo jingine linalojitokeza

Jamii za lugha,
Jamii kubwa
na matawi yake
muhimu yanayo
wakilishwa
Afrika ya
Mashariki

Makundi ya
Lugha Afrika ya
Mashariki



23.2 Makundi ya lugha na uhusiano wake Afrika ya Mashariki (kutoka kwa J.E.G. Sutton)

mbinu za kukifua tangu zama za kale. Hii ni sababu moja ya kuhusisha maeneo ya kiakiolojia ya Enzi ya Chuma ya awali, ya kipindi tangu sehemu za awali na za kati za elfia ya kwanza ya enzi ya Ukristo, katika wilaya nyingi za mashariki na kusini-kati ya Afrika zilizotwaliwa na Wabantu. Lakini sababu yenye mvuto zaidi kutokana na uchunguzi wa kulinganisha lugha za Kibantu ni kukifahamu chuma na ya kuyatambua kwa uhakika kabisa maeneo haya kuwa ni yale ya Wabantu wa awali ni ukweli tu kwamba msambao wake unasadifiana vizuri na ule wa sasa wa Wabantu. Hakuna sababu zozote za kimsingi za kubuni nadharia kwamba wakazi tofauti kabisa walienea katika eneo hili kubwa na kuwa wametoweka kabisa katika kipindi kisichozidi miaka elfu moja iliyopita.

Vitu vingi vilivyopatikana katika maeneo haya ya Wabantu wa awali si zana na silaha za chuma kwani vitu hivi vilikuwa vya thamani kubwa mno kuweza kutupwa na kama vingetupwa, kwa kawaida vingeharibika kabisa, bali vipande vya vyungu vilivyovunjika. Kutoka mwanzoni kabisa vyombo hivi vya udongo vilifanana kabisa kutoka eneo hadi eneo katika sehemu zote na makazi ya Wabantu. Aina mpya zinazidi kutambuliwa na wanaakiolojia. Labda vile vinavyojulikana zaidi ni vyombo vyenye vishimo vidogo kwa upande wa chini (au Urewa) vinavyopatikana kando ya Ziwa Viktoria na magharibi zaidi, na kuendelea hadi kaskazini mwa Ziwa Tanganyika na kusini mwa msitu huko Zaire. Licha ya vishimo chini mwa baadhi ya vyombo hivi, vingi vina kingo zenye sura mzuri sana na mapambo mazuri katika hatimviringo na maumbo mengineyo. Kusini na mashariki mwa kanda ya vyombo vya vishimo chini yake vyombo vya Enzi ya Chuma ya awali vinegawanyika katika makundi mawili makubwa. Katika Tanzania ya kaskazini - mashariki na Kenya ya kusini-mashariki, vyombo vya Kwale, kama vinavyoitwa, vinaonekana kutoka kwenye kingo za nyanda za juu hadi kufikia uwanda wa pwani. Kusini mwa Ziwa Tanganyika, na katika nchi za kusini zaidi, vyombo vingi sana vya kinajimbo vimetambuliwa. (Hivi ni pamoja na vile vya Zambia vilivyojulikana mwanzo kama vyenye vifereji).

Waniloti: Kujirekebisha na Kutofautiana

Licha ya Kibantu, kundi jingine la lugha - ama sahihi zaidi, makundi ya lugha zenye uhusiano wa mbali - lilienea sehemu kubwa ya Afrika Mashariki wakati wa Enzi ya Chuma. Hawa walikuwa Waniloti. Wakati ambapo maumbo na sura zao zinatofautiana katika mambo kadha ya kijumla na zile za Wabantu, Wanilotiki kimsingi ni wanegro. Hata hivyo ni kweli, kwamba wale wazungumzaji wa Kiniloti walioelekea mashariki na kusini kwenye kanda ya zamani ya Kikushi ya Kenya na Tanzania ya kaskazini wamewasimulisha baadhi ya wakazi wa Kiethiopia. Hii inasaidia kuelezea sababu ya sifa za kiasili za Kinegroi baina ya vikundi vya sasa vya Waitunga, Wamasai Wakalenjini na Watatonga. Hawa ndio watu ambao hapo awali waliainishwa kuwa ni "Wanilo - Haniti". Ingawa wana mengi waliyorithi katika utamaduni wao kwa Wakushi lugha zao, kwa hakika, zimebakia kuwa za Kiniloti.

Migawanyiko ndani ya lugha za Kinailotiki - kati ya Waniloti wa Nyanda za Juu, na Mito - Maziwa na wa Tambarare - ni ya undani na ya kale (tukilinganisha na mgawanyiko katika lugha za Kibantu). Ingawa tarehe halisi ya kuvunjika kwa "Kiniloti asilia" haiwezi kukadiriwa barabara, haiwezekani kuwa ni chini ya miaka elfu mbili iliyopita. Inawezekana hali hii ilianza kujitokeza Sudani ya Kusini, hasa kuelekea kwenye mpaka wa Ethiopia. Kutoka hapa wawakilishi wa kijumla wa kila moja ya yale makundi matatu walielekea kwenye sehenu za kaskazini, hata za kati za Afrika Mashariki kwenye kipindi cha miaka elfu mbili iliyopita. Hata hivyo, kuenea kwa Waniloti, hasa kundi la Waitunga katika Uganda ya Mashariki na Kenya kaskazini - magharibi, na Wamasai katika Kenya na kaskazini mwa Tanzania na Waniloti walioishi kanda ya ziwa hasa Walwo wa Uganda na magharibi mwa Kenya yalitokea katika elfia ya pili ya enzi zetu. Katika juzuu hili tutajishughulisha zaidi na kundi la Waniloti wa Nyanda za Juu, linalowakilishwa siku hizi na Wakalenjini wa nyanda za juu za Kenya ya magharibi na watatoga waliotawanyika kwenye nyika mbalimbali kaskazini mwa Tanzania.

Waniloti wa Nyanda za Juu wa awali kabisa bado hawajulikani kiakiolojia; lakini msambao wao wa sasa na ulinganishi wa ndani wa lugha unaonyesha kwamba ni lazima walikwishaanzisha makazi yao nchini Kenya miaka elfu moja iliyopita. Inawezekana kwamba kujitokeza kwao kama kundi mahususi lenye utamaduni na lugha yao wenyewe kulianza kutokana na kuja kwa chuma kwenye bonde la Nili ya juu na kwenye mianeneo ya mpaka wa Ethiopia. Katika maeneo haya na katika kanda ya Kikushi, kuna uwezekano kwamba ujuzi wa kufua chuma ulitoka kaskazini. Kauli hii inapigana na imani iliyopo kwamba ujuzi wa kufua chuma uliingizwa katika Afrika Mashariki na Wabantu. Ukweli ni kwamba ufuaji chuma katika maeneo yaliyokaliwa na Wabantu ulienea zaidi kusini na magharibi kuliko ilivyokuwa kaskazini.

Idadi kubwa ya Waniloti ilibaki katika bonde la Nili hasa Sudani ya kusini. Hapa hawakuathiriwa moja kwa moja na desturi za Kikushi na kwa ustadi mkubwa walichanganya ufugaji, ulimaji nafaka na uvuvi. Hata hivyo, kundi la Tambarare hatimaye liligawanyika katika matawi matatu makuu, na ni muhimu kuangalia jinsi walivyoweza kurekebisha maisha yao kulingana na mazingira walimoishi. Miongoni mwa kundi Wabari na Lotuko kusini mwa Sudani na kaskazini mwa Uganda kuna mabaki ya ishara ya utamaduni a Waniloti. Katika milina na nyanda zilizo kame kidogo zinazopita kaskazini mwa Uganda kuingia Kenya zinazokaliwa na kundi la Waitunga (linalowajumuisha Wakaramojong, Waturkana, na wateso n.k.) uvuvi haukuwa miongoni mwa shughuli muhimu. Hii pengine ilisababishwa na mazingira yenyewe au pengine miiko iliyoambatana na utamaduni wao. Kundi la tatu la Waniloti wa Tambarare, yaani Wamasai, lilizagaa katika sehemu kubwa za nyika sehemu za miinuko ya Kenya na kaskazini mwa Tanzania. Katika karne za hivi karibuni Wamasai wameathiriwa na kuathiriwa kwa kiasi kikubwa na utamaduni wa Waniloti wa Nyanda za Juu waliowatangulia na kwa kiasi fulani na utamaduni wa

Wakushi wa kusini. Kwa hiyo, waliingiza katika mila zao sio tu mwiko wa kula samaki, bali pia desturi ya kutahiri. Kwa kweli katika sehemu hizi zenye malisho mazuri Wamasai walifaulu kuyabana makundi ya makabila ya wakulima hadi kuyasukumia sehemu zisizofaa kwa kilimo.

Hii ni baadhi tu ya mifano tuliyoweza kutoa kuelezea upanukaji na usilimishaji wa Kihiloti ambao unaonekana kuwa wa kinasibu usimilisho wa makundi mengine ya Kiniloti pamoja na yasiyo ya Kihiloti na kwamba mifano mingi ipo na inahitaji uchunguzi wa kiakiolojia na kiutamaduni. Huko Sudani ya kusini na katika Uganda ya kaskazini na mashariki, kwa mfano, maingiliano yaliyofanyika kwenye miaka ya hivi karibuni katika elfia ya sasa na labda mapema zaidi, baina ya matawi kadha ya Waniloti wa Nyanda na wa kando ya maziwa yamekuwa changamani kama yale kati ya Waniloti, na Wakushi na kati ya Waniloti wa kale na Waniloti wanya hasa katika nyanda za juu za Kenya na Tanzania ya kaskazini.

Tatizo la "Megalithi" la Afrika Mashariki


Katika marejeo ya kale yahusuyo Afrika Mashariki kulikuwa na mjadala juu ya ustaarabu wa hali ya juu katika zama za kale. Huu ulidhaniwa kuwepo katika eneo la baina ya maziwa na zaidi hasa katika nyanda za juu za Kenya na Tanzania ya kaskazini. Mitazamo ya kihistoria ya namna hii ilitokana na misingi ya utafiti mchanganyiko wa ethinografia, mapokeo simulizi yaliyokusanywa kienyeji na akiolojia iliojumlisha mabaki au vile vilivyodhaniwa kuwa ni inagofu ya majengo na matungazi ya mawe makavu, yaani ya "megalithi". Kwa bahati mbaya, sehemu kubwa ya ushahidi wa mwanzoni haikurekodiwa vyema na ilitafsiriwa bila kujali mantiki ya kihistoria. Wakati mwingine tafsiri hizo ziliongozwa na dhana zisizohusika kabisa ili kuyapendeza maoni potofu ya wakati huo hasa yale ambayo ndiyo yaliyoambatana na kile kilichoitwa ustaarabu wa Kihamiti. Hali hii ilishikiliwa kwa hamu mno na baadhi ya waandishi ambao waliukubali bila kuuhakiki, na pengine kuutilia chuku mno bila sababu, ushahidi uliodhaminiwa kuwa ni wa msingi.

Mara nyingi ilidhaniwa kuwa aina mbalimbali za mabaki ya kiakiolojia ilibidi zihusishwe na utamaduni wa watu fulani bila kujali mazingira ambamo utamaduni huo ulizuka. Fikra za aina hii hazina mantiki na hazina budi kupuuzwa. Kudhani kwa namna hiyo ndiko kulikuwa msingi wa nadharia ya Huntingford ya ustaarabu wa Azania katika Kenya na Tanzania kaskazini ambao yasemekana ulitokana na Wahamiti, na pia wa nadharia ya Murdock kwamba Wakushi wa megailithi hapo kale waliishi katika eneo hilihili. (Murdock alikuwa anapinga nadharia ya Kihamiti za wanaandishi wa awali).

Kwa hiyo, neno kimegalithi limelimbikiziwa maana nyingi mno na halina maana yoyote ya kiutamaduni au kihistoria katika Afrika Mashariki. Hata hivyo, kuna faida, kutoa maoni na maelezo mafupi kuhusu zile sifa ambazo zimedondolewa kama ushahidi wa tamaduni za megalithi ya kale. Kusema kweli, sio yote ni majenzi ya mawe. Katika sura hii tutataja piramidi ambazo zinawakilisha makaburi

yanayoonekana mara kwa mara katika nyika za Kenya na Tanzania ya kaskazini. Nyingi ya hizi ni za mwishoni mwa enzi ya mawe, yapata miaka elfu mbili au tatu hivi na huenda zilitengenezwa na watu waliozungumza Kikushi. Lakini baadhi zinaweza kuwa za karibuni zaidi. Inawezekana, lakini kwa shaka, kwamba baadhi ya visima vilivyojengewa mawe yaliyokatwa ambavyo vinaonekana katika mbuga za kusini mwa Umasai katika Tanzania na pia yale ya Kenya ya mashariki na ya kaskazini, vinaweza kuwa vya kipindi hiki, wakati ng'ombe walipoanza kufugwa. Vivyo hivyo vilikuwa ni vijia tu vya ng'ombe vilivyomomonyolewa kwa bahati kutokana na kupitiwa kwa inuda mrefu na makundi ya ng'ombe yakivuka matuta na mitelemko kufuata maji. Yasiyoelekea kuwa ni ya kipindi cha nyuma hivyo ni mazoea ya kilimo cha kunuwagilia kilichotekelezwa katika maeneo ya Bonde la Ufa na pitio za milima ya Tanzania ya kaskazini na Kenya. Kwa upande mwingine, inaweza kuonyeshwa kuwa mazoea haya angalau yana unri wa karne chache katika baadhi ya maeneo. Yaliyo nadra zaidi na yenye umuhimu mdogo zaidi kwa hoja za kihistoria, ni matungazi ya kilimo cha pembeni mwa milima. Matuta ya namna hii yalilimwa tu katika mazingira maalumu na ya pekee sana. Baadhi ya maelezo yanazungumzia hata kuhusu monoliti (nguzo za jiwe moja tu) na falusi (sanamu-uume) katika bara ya Afrika Mashariki. Kuna shaka kubwa iwapo ni kweli kuwa vitu hivi viliwahi kuwapo Afrika Mashariki.

Hata hivyo, kuna zaidi kidogo ya haya kuhusu suala la megalithi ya Afrika Mashariki. Tunasoma pia juu ya nyumba za mawe na maboma na makazi ya mashimoni. Ingawa hapa pia kuna maelezo na tafsiri zisizo sahihi, baadhi yake yanaweza kuthibitishwa na utafiti wa kiakiolojia kuwa ya kweli. Utafiti wa aina hii unebainisha mtindo wa kujenga na kufunika kuta kwa mawe katika maeneo mawili yaliyotofautiana hata kiutamaduni japo ni ya wakati mmoja. Eneo la kwanza linajumlisha yale yanayoitwa Mashimo ya Sirikwa, ambayo ni mengi sana kwenye sehemu yote ya nyanda za juu za magharibi za Kenya. Enco la pili hali kadhalika liko upande wa magharibi wa Bonde kuu la Ufa, lakini mbali kidogo kuelekea kusini kupita mpaka wa Tanzania.



Afrika Magharibi kabla ya Karne ya saba

Uchunguzi wa data za kiakilojia zilizopo haukubaliani na imani inayoshikiliwa na watu wengi kwamba asili ya jamii za Kineolithiki na za Enzi za Chuma pamoja na maendeleo na tabia za watu hao zimetokana na athari kutoka nchi za nje. Kwa hakika, ni makosa kudai kwamba mawazo ya watu kutoka nje, hasa kutoka sehemu za kaskazini za jangwa la Sahara, ndio waliosababisha mengi ya maendeleo makubwa yanayohusiana na ukuliina wa mwanzo au ufuaji wa chuma na shaba. Bali data hizo zinaonyesha kuwa vitu vingi katika eneo lote, au baadhi tu ya eneo hilo, vilichangia kwa njia moja au nyingine na kwamba maeneo ya Kineolithi ya Afrika Magharibi na ya Enzi za Chuma kwa kiasi fulani yameeleweka kwa kuwa ndani ya inifumo ya maeneo yaliyoshikamana kwa pamoja, na kuwepo vikwazo vya kiekolojia.

Asili ya kilimo na ufugaji wanyama

Uchunguzi wa mimea na udongo wa maeneo ya tangu kale sana (ambao mpaka sasa umepuuzwa) ni muhimu sana katika kuelewa jinsi gani na lini mabadiliko kutoka kwenye uwindaji na ukusanyaji yalivyotokea huko Afrika Magharibi - hasa kwa vile ushahidi wa moja kwa moja haupatikani.

Katika muktadha huu, ufugaji una maana ya harakati za kuwatoa wanyama kutoka kwenye mazingira na maisha yao ya asili, knongoza kuzaliana kwao; kuwafanya wamhuhumie mwanadamu na kumsaidia kuzibadilisha au kuziacha baadhi ya tabia za zamani. Ulimaji mimea hapa una inaana ya upandaji wa makusudi wa mbegu za mimea na utunzaji wa miti ya matunda n.k. kwa madhumuni ya kwamba binadamu aweze kuzitumia kwa kiasi kikubwa.

Kwanza uchunguzi wa kiakilojia unaonyesha kwamba ufugaji unawezekana katika maeneo ya tropiki yaliyo kame kidogo kwenye ukanda wa savana za kitropiki kwa sababu pH ya udongo ni ya juu (+7.0) na naitrojeni na fosforasi zinaweza kuchanganyika kwa urahisi na malisho yana protini kiasi cha kutosha. Pili, uchunguzi vile vile unaonyesha kwamba katika maeneo ya tropiki yaliyo manyevu kidogo ufugaji si muhimu kama ukuliina. Hii ni kwa sababu katika maeneo ya namna hii naitrojeni, fosforasi na kalasimu hupatikana kwa kiwango kidogo na malisho huwa na nyuzinyuzi nyingi na kiwango cha juu cha ongezeko la joto. Kwa hali hii, utoaji joto na utawanyaji wake kwa wanyama ni matatizo makubwa sana kwa mifugo katika

maeneo ya tropiki yaliyo manyevu. Ili kudumisha usawa wa joto katika maeneo kama haya mifugo huwa na miili midogo ili kujipa eneo kubwa na kuwezesha usambazaji wa joto. Katika zile sehemu ambako wanyama walikuwa wakifugwa yaonyesha kuwa tatizo la joto kali limetatuliwa kwa kuwachagua wanyama walio na maumbo madogomadogo walioweza kujirekebisha kufuatana na mazingira ya kitropiki.

Tatu, uchunguzi wa kiekolojia unaonyesha kwamba mimea ya kila mwaka iliyolimwa katika sehemu nyingi za Afrika ya Magharibi, kinyume kabisa na ile ya Mashariki ya Kati ilijirekebisha na bado inajirekebisha kumea katika majira ya joto kali na unyevu mwingi. Isipokuwa kwenye nyanda za juu zilizo baridi na kame kidogo, nafaka za Mashariki ya Kati hazisitawi hata kidogo kwa sababu ya kukosa uwezo wa kukabili patojeni ambayo husitawi kwenye maeneo yenye joto kali.

Utafiti wa aina mbalimbali umeonyesha kwamba kwa jumla, kilimo na ufugaji ndiyo njia zilizotumika kwanza kupatia chakula. Kwa kiwango mahususi, uzalishaji huu wa chakula ulitofautiana kufuatana na aina za mazao yaliyolimwa, wanyama waliofungwa na jinsi mazao hayo yalivyolimwa na wanyama kufugwa na mifumo ya makazi na ya kijamii iliyotumiwa.

Kuseina kweli, utaliti wa kiekolojia na kiathnografia umeonyesha mambo yafuatayo (i) ufugaji wa mwanzoni wa ng'ombe katika Saltara ya Kaskazini na ya Mashariki; (ii) maeneo ya mwanzoni ya uzalishaji wa mazao ya mbegu, kwenye miteremko ya nyanda za juu za Sahara ya kati; (iii) maeneo ya uzalishaji wa mazao ya mbegu katika sehemu za Sahel na maeneo ya savana ya kaskazimi, kukiwa na athari zilizolingia kwenye maeneo haya kutoka kaskazini na kusini (kwa hali hii, inaonekana kwamba delta ya mto Niger, ukingo wa milima ya Futa Jallon katika bonde la juu la mito Sengal, Niger na Gambia, na mazingira ya Kisudani kwa jumla, huenda ndiyo yaliyokuwa maeneo ya ukulima wa mwanzo katika Afrika Magharibi. Mazao yaliyokuwa yakilimwa mi nafaka kama vile mpunga, mtama, maweke na mahindi); (iv) Ulimaji na ufugaji katika maeneo ya Sahel ya Kati na ya Mashariki na sehemu za maeneo ya Savana ya Kaskazimi ambapo ukame wa Sahara huenda vilichangia sana, na (v) mizizi na miti tofauti pembezoni mwa maeneo ya msitu upande wa kusini zaidi.

Maeneo haya ya mwanzoni ya 'Kineolithiki' yalijipambanua kwa namna mbalimbali za makazi, kijamii na mbinu za utumaji ardhi. Hata hivyo, katika sehemu kadha kama vile Tiemassas, Senegal na Paratoumbian, Mauretania kulikuwa na muingiliano bayana wa shughuli mbalimbali za uchumi.

Maeneo ya ufugaji ng'ombe ya mwanzoni ya kinolithi ya Kaskazini Mabaki ya ng'ombe wa kufugwa wenye pembe fupi yaliyogunduliwa sehemu mbalimbali kaskazini mwa bara yameonyesha kuwa ng'ombe walikuwa wakifugwa tangu mwaka -5590 (± 200) huko Uan Muhuggiag, na kati ya mwaka -3830 hadi -3790 kwenye maeneo ya Libya ya kusini - magharibi na Adrar Bous Air. Kwenye eneo la Ua Muhuggiag mabaki ya kondoo vile vile yalipatikana. Hata hivyo yaelekea

kuwa ng'ombe wenye pembe fupi hawakuwepo katika bonde la mto Nili kabla ya ufalme wa kumi na moja (-2600), ingawa kuna ushahidi kwamba kulikuwepo na ng'ombe wenye pembe ndefu huko Kom Ombo nchini Misri wakati wa Pleistosini.

Hata hivyo ushahidi wa kitamaduni unaonyesha kwamba huko Libya kulikuwako na mabadiliko ya mapema zaidi kutoka uwindaji na ukusanyaji kwenda katika ufugaji, ambao ulienea kuelekea kusini mashariki hadi kufikia Adrar Bous Tenereen, (kati ya -4000 na -2500). Ufugaji ulizidi kuenea sehemu za kusini magharibi ng'ombe walikuwa wakifugwa Tichitt aamu ya Khimiya, baada ya -1500). Katika maeneo haya, wafugaji wanaelekea kuwa walikuwa wazawa wa moja kwa moja wa wakazi wa mwanzoni na huenda njia mpya ya maisha ilibadilishwa au ilijumuishwa na njia ya upandaji mboga ya Kineolitliiki. Iwapo ni hivyo, basi dhana ya ufugaji wa ng'ombe, ama ilihamishiwa kwenye maeneo haya, au kando kando niwa eneo kubwa la asili la ufugaji wa ng'ombe. Taaluma ya kukisia tarehe kwa kutumia redio-kaboni 14, inaonyesha uwezekano wa upanuzi wa ng'ombe kutoka ndani kabisa ya Sahara kwenda Sahara ya kusini na kanda za Sahel za Afrika Magharibi. Kwa kiasi fulani kuenea huku kuitokana na ukame uliokuwa ukinyemelea polepole sehemu ambayo sasa ni jangwa la Sahara.

Upandaji mbegu wa awali katika maeneo ya Kineolitliiki

Nyanda za juu za Sahara ya Kati

Ushahidi uliopatikana unaonyesha kwamba upandaji wa mbegu, lakini sio namna yoyote nyingine ya ukulima, pengine ulianza mapema zaidi katika nyanda hizi kuliko sehemu nyingine yoyote ya kusini. Ushahidi wa mwanzoni kabisa wa namna hii ya Kineolitliiki unatoka hasa kwenye maeneo yenye pango yaliyoko Amekni na Maniet katika uwanda wa juu wa Hoggar. Huko Amekni, Camps alipata punje mbili za chavua ambazo kutokana na umbo lake, zinafikiriwa kuwakilisha aina fulani ya nafaka, aina ya *Pennisetum*, inayofikiriwa kuwa iliotesha katika miaka ya -6100 na -4850. Kutoka Maniat, Pons na Quezel walizitambua punje mbili za chavua za nyakati za takribani mwaka -3600 ambazo zawezekana kuwa ni za nafaka zilizolimwa.

Ushahidi mwingine usio thabiti sana kuhusu ukulima wa mimea ya mbegu katika eneo hili unatoka kwenye pango lililoko Sefar kwenye uwanda wa juu wa Tassili, ambalo kufuatana na tarehe zilizopatikana kwa redio kaboni 14 ni takribani mwaka -3100. Michoro iliyoona katika pango hili yaelekea kuonyesha ukulima, ambapo ushahidi wa kisimu unaonyesha ukale zaidi wa kilimo cha mtama katika Sahara ya kati. Licha ya kuhisi katika pango, watu wa kale wa eneo hili vile vile waliishi katika vijiji vikubwa na vya kudumu au katika makazi kando ya milima au kingo za miteremko zilizokabiliana na maziwa au wadi na walitumia zana kama vile mashoka ya kukwatua, mawe ya kusagia na vijaa, mawe yenye vishimo na vyombo vya udongo.

Sahara ya kusini, Sahel na sehemu za maeneo ya savana ya Afrika Magharibi

Katika sehemu hizi za Afrika Magharibi mara nyingi maendeleo ya Kineolitliiki



24.1 Afrika Magharibi: Maeneo muhimu kipindi kabla ya historia

yamekuwa yakidhaniwa ni matokeo ya athari kutoka kaskazini. Huenda zikawapo sababu za kukubaliana na maoni haya kwani baadhi ya viwanda vya enzi ya mawe ya nyuma vilivyokuwako katika eneo hili vinaonyesha kushabihiana na vile vilivyokuwa katika uwanda wa Hoggar au Sahara ya mashariki na Maghrib wakati wa kipindi cha Paleolithiki. Lakini ushahidi wa kiakiolojia ya inwanzoni niwa enzi ya Kiniolithi (enzi ya mwisho ya mawe) unaohusiana na eneo hili umeonyesha tabia za kipekee, hasa katika vyombo vya udongo, zana na ukubwa wa jamii. Mengi ya makazi ya wakati huo yalijengwa juu ya mitereniko au kwenye tanbarare za inaziwa. Ushahidi huo unaweza kutengwa katika makundi matatu yanayoakisi tofauti katika miundo ya kiuchumi na kijamii.

- (i) Kwenye ukingo wa kaskazini wa eneo hili kuna viwanda kama vile vya Tenereen na Bel-air (Senegal), ambavyo vina namna mbalimbali za mikrolithi za kijometri na/au mitupo na maeneo madogo ya makazi.
- (ii) Kwenye maeneo ya kati, kama vile Borku, Ennedi, Tilemsi, Ntereso na Daima, viwanda vinapatikana ambavyo vinakosa maikrolithi za kijometri lakini vina namna nyingi za mitupo, ndoana na chusa, zana kadha za mawe ya kukwatua na kunoa. Maeneo ya makazi ni makubwa kidogo.
- (iii) Kundi la tatu la viwanda lililoko kusini, linalowakilishwa kimsingi na Nok na Kintampo, halina kabisa mikrolithi za mitupo, lakini li tajiri katika zana za mawe ya kukwatua na yakunoa. Eneo hili lina makazi yaliyo makubwa zaidi na ya kudumu zaidi.

Maeneo ya Bonde la Tilemsi

Ushahidi kutoka sehemu za Karkarichinkat unaonyesha kwamba wakati wa awamu ya hivi karibuni ya unyevu katika Sahara (-2000 hadi -1300) eneo hili lilikalikiwa na wafugaji wakiwa na namna ya kuishi isiyotofautiana sana na ile ya baadhi ya wafugaji wa kinusu-nomadi wa siku hizi kama vile Wanuer wa Sudan na Wafulani wa Afrika Magharibi. Maeneo ya Karkarichinkat Kusini yanafanana na vituo vya uvuvi na ufugaji, kama unavyoonyesha ushahidi wa makombe mengi ya chaza, mifupa ya samaki na masalia ya *Bos*, kulikuwa na vifaa vichache tu vya mawe au pengine havikuwako kabisa isipokuwa ndoana. Kinyume chake ni kwamba wingi wa vifaa vya udongo, maumbo ya udongo ya wanyama na aina mbalimbali za mitupo zilizopatikana Karkarichinkat Kaskazini vyote vinaonyesha unabadiliko kutoka kwenye maji yaliyotulia na ushiriki mkubwa katika ufugaji, uwindaji na pengine ukuliina wa mazao.

Makundi ya kiutamaduni yaliyoishi Tilemsi ya kaskazini, karibu na Asselar yalikuwa na uzalishaji uliofanana na wa Tenereen ya eneo la Sahara na angalau yenye umri mrefu kama huo. Mifupa imetambuliwa kuwa ni ya mwaka -4400. Makundi yote mawili yana vijaa, inashoka na visu vya kukwatulia. Huko Asselar na Karkarichinkat, imedhihirika kwamba licha ya kufuga ng'ombe watu pia waliwinda wanyama-pori. Uchunguzi uliofanywa na Camps huko Admer Erg kusini mwa

Tassili -n- Ajjer unaoneysha kwamba wafugaji wenye viwanda vilivyofanana na vya Tenereen alikuwepo katika sehemu za kaskazini kwenye mawanda yaliyopakana nayo tangu karibu mwaka wa elfia nne kabla ya enzi yetu.

Eneo la Dhar Tishit

Utafiti uliofanywa katika sehemu hii ya Mauretania ya kusini umeonyesha mfuatano wa awamu nane, zenye tarehe kamili ya enzi ya mwisho ya mawe zikiwa na kumbukumbu zenye uhakika zinazotoa madokezo juu ya matatizo ya unzalishaji chakula katika eneo hili na katika eneo la mito Senegal na Niger kwa jumla.

Maelezo yanayoonekana kuwa ya kweli kuhusu mwelekeo wa maendeleo yaliyopatikana Tishit, kutokana na kupatana vizuri zaidi na data za akiolojia, ingekuwa kama ifuatavyo - uoteshaji na uzalishaji maalum wa *cenchrus biflorus* katika awamu ya Khimiya (-1500), halafu uimarishaji na upanuzi wa uzalishaji huu wa mwanzo na uzalishaji wa miene mingine kadha wakati wa awamu kama ya Naghez (-1100).

Eneo Kusini mwa Ziwa Chad

Eneo hili, linalojulikana kwa jina la Firki, linajumlisha nyanda za udongo mweusi wa mfinyanzi zinazotanda kutoka kingo za kusini za Ziwa Chad, ambalo hapo kale lilikuwa kubwa zaidi. Eneo hili lina ruwaba na maji ya kutosha. Udongo unahifadhi sana unyevu mara tu ukishavama katika ardhi, na uhifadhi huu sasa uneongezwa kwa kulima matuta yanayozunguka mashamba. Mafuriko ya msimu yalilifanya eneo hili liwe zuri kwa makazi ya wakulima na wafugaji mvua nyingi au jua kali vilizopunguza sana sehemu za niakazi ya kuishi na matumizi ya kuduunu ya maeneo haya, hapo awali yalisababisha kuongezeka kwa vilima.

Uchimbuzi wa baadhi ya vilima hivi huko Nigeria ya kaskazini, Kamerun na Chad, mpaka sasa umeshaonyesha mfuatano wa kukaliwa kwa vipindi vya muda ambao mara nyingine unasemekana kukaribia au kuzidi miaka 2000. Lebcuf, ambaye alikuwa anafanya utafiti huko Chad, anaamini kwamba vilima hivi vinahusiana na Sao, kama inavyoelezwa katika mapokeo simulizi. Ingawa jina hili lina thamani kubwa ya kitamadani na kikabila, niwandishi huyu anakubaliana na wasiwasi wa Cornah wa kutumia mapokeo simulizi kwa kuainisha watu ambao baadhi yao waliishi miaka 2500 iliyopita.

Ushahidi uliopatikana Daima unaonyesha kwamba kunako mwanzoni mwa karni ya sita kabla ya enzi yetu kulikuwepo na wafugaji wa enzi ya mwisho ya mawe walioishi katika eneo hili wakifuga ng'ombe na kondoo au mbuzi, wakitumia mashoka ya mawe yaliyokwatuliwa ambayo mali ghafi yake ilichukuliwa kutoka mbali sana na kuletwa katika eneo hili lisilo na mawe kabisa; na wakaunda vifaa na zana za mifupa iliyokwatuliwa. Wakazi hawa wa mwanzoni wa eneo hili, pengine walijenga kwa nyasi na miti tu, na hawakuwa na metali ya aina yoyote.

Matokeo ya uchunguzi kutoka maeneo kama vile Rop na Dutsen Kongba yanaonyesha kabisa kwamba kiwango cha matumizi kamili ya mawe cha Kiniolithiki

pia kiliutangulia kidogo tu utamaduni mashuhuri wa enzi ya chuma wa Nok (yaani kabla ya -2500) wa sanamu zinazochongwa kwa mawe madogo ya kisavaua katika uwanda wa Jos. Yawezekana kabisa kuwa watu wa Nok waliwauzia zana za namna hii watu walioishi katika maeneo ya kaskazini, yasiyo na mawe na huenda vilevile vyombo vya udongo, ambavyo mara nyingi vikiwa vimerebwa huko Daima, viliwakilisha bidhaa nzuri zenye upande mwekundu uliokwatuliwa ukiwa na chanuo za meno au ruleti (aina ya vitufe).

Maeneo ya Kintampo - Ntereso, Ghana ya Kati

Ushahidi wa kiakiolojia unaonyesha kuwapo kwa kundi la kinegroidi lililojishughulisha na uzalishaji wa chakula mapema kabisa kwenye miaka ya -1300 hadi -1400, mpaka sasa umeshapatikana katika sehemu kuu nne za Ghana: inashariki ya miliina ya Banda, uwanda wa juu karibu na Kinampo, maeneo yenye nito yaliyotanda baina ya misitu wazi ya bonde la Volta, na nyanda za Accra zilizopo kusini.

Makundi haya ya maeneo sasa yanaweza kutofautishwa zaidi na inazingira ya mahali yalipo kuliko ushahidi wa utamaduni halisi. Udongo wa kukandikia uliochomwa ulitumiwa sana huko Kintampo, na unaonyesha makazi ya kudumu. Mtawanyiko mkubwa wa mashoka ya kukwatuliwa na "tupa" pengine huitwa *terracotta cigars*) katika maeneo ambako mawe ya kufaa hayapo, unaonyesha kuwepo kwa nainna fulani ya biashara baina ya maeneo haya. Ushahidi kutoka sehemu tatu kati ya nne za Kintampo pia unaonyesha kwamba eneo la Kintampo lilitanguliwa na cneo jingine likiwa na mapokeo ya vyombo vya udongo, zana za mawe na mabaki ya wanyama yaliyo tofauti kabisa, ambayo yanadhihirisha kiwango kikubwa cha uwindaji na ukusanyaji na/au ukulima wa mwanzoni.

Maeneo ya ukingoni mwa msitu

Eneo jingine lenye viwanda lililo tofauti kwa tabia likilinganishwa na viwanda vya enzi ya mwisho ya mawe vilivyotangulia, lilitokea baadaye kwenye maeneo ya ukingo wa msitu wa Afrika Magharibi, na katika maeneo ya mbuga za Burkina Fasso. Aina hii ya viwanda inafanana na ile ya Kineolithi iliyo kaskazini zaidi kwenye sehemu za Senegal, Mali na Mauretania.

Wazalishaji chakula wa mwanzoni wa eneo la msitu (wanaoitwa Wancolithi wa Kiguinea) waliishi mapangoni na pia katika maeneo ya wazi. Mifano ya mapango haya ni Yengema, Kamabai na Yagala nchini Sierra Leone; Kakimbon, Blande na mapango ya Nyani nchini Guinea; Bosumpra huko Ghana; na Iwo Eleru na Ukpa nchini Nigeria. Kutoka Iwo Eleru pia unapatikana ushahidi unaodokeza kwamba wahenga na kadhalika Wancolithiki walikuwa wa Kinegroidi. Maeneo ya wazi yanayojulikana sana ni pamoja na bonde na mteremko wa riin huko Burkina Fasso ya kaskazini ya kati, na maeneo yaliyoko pwani mwa Senegal yanayokusanya sehemu za Rarenno, Tiemassas na Cap Manuel.

Lililo muhimu ni kwamba ushahidi wa kiakiolojia kutoka ukanda wa Mali-Mauretania Senegal unaelekea kuunga mkono nadharia ya Porteres kwamba mipunga ya Kiafrika yenye gamba jekundu (*Oryza glaberrima* na *Oryza Stapfii*) huenda ililimwa kwanza kwa njia ya kiasili ya kilimo cha unyevu kama miaka 3500 iliyopita kwenye mabonde mapana yaliyofurika maji ya Niger kati ya Segou na Timbuktu nchini Mali, eneo ambalo mto Niger unagawanyika katika vitawi kadha na maziwa kadhaa; na kutoka hapa ukulima wa namna hii yawezekana ulienea kupitia mito ya Gambia na Casamance hadi kuwafikia wakazi wa pwani wa Senegambia. Ni muhimu kukumbuka pia kuwa ushahidi wa elimu-mimea unafutulia mbali kabisa wazo la kwanza ukulima wa mpunga ulitokana na knanzishwa kwa ujuzi wa kulima nafaka. Porteres ameonyesha kwamba wakati ambapo ngano ya kiasili (*emmer*) ilitoa mbegu zinazoweza kuliwa ili kwamba ukulima ungeweza kutokana na ukusanyaji wa mbegu, jambo hili lisingewezekana kutokea kwa mpunga wa Kiafrika, kwani aina yake ya awali haikuzaa mazao ambayo yangeweza kukusanywa.

Hivyo basi, kwa jumla, ushahidi unaonyesha kwamba maeneo ya nyanda za juu za Sahara na Sahel yalikuwa ndio kitovu cha ukulima wa kwanza kabisa uliojitegemea wa baadhi ya mazao ya nafaka hasa *Pennisetum* na mtama, ambapo maeneo ya ukingoni mwa misitu ya Nigeria yaliushuhudia ukulima wa mwanzoni kabisa wa kiasili wa mazao kadha ya jamii ya viazi na michikichi. Kwa upande mwingine eneo la ukingoni mwa msitu lilikuwa ndio eneo la ukulima wa mpunga. Akijishughulisha zaidi na mtama, Portères alionyesha kwamba Afrika Magharibi ilikuwa imepiga hatua kubwa katika kilimo cha mpunga ikilinganishwa na sehemu nyingine kama Ethiopia na Afrika Mashariki na Bara Hindi; na wala haionyeshi kuwa aina hizi zilitokana na mchanganyiko wa mbegu zilizoingizwa kutoka sehemu nyingine.

Wakati ambapo ushahidi unaotokana na redio-kaboni 14, kuuonyesha kuwa sehemu ya Sahara ya kati (c. -7000) ilikuwa ndio chimbuko la ukulima wa kimsingi wa Kineolithiki, tunadhihirishiwa vilevile kwamba mabadiliko ya kwendea kwenye uzalishaji wa chakula katika maeneo ya ukingoni mwa insitu yalitokea mapema zaidi kuliko yalivyotokea kwenye kanda za Sudan na Sahel. Kule Iwo Eleru mabadiliko haya yalitokea mara tu baada ya mwaka -4000 (-3620) na yakaendelea hadi mwaka -1500. Kwenye pango la Ukpa katibu na Afikpo (5° 54' N 7° 56' E Shaw, +1969) vyombo vya udongo vya Kineolithi na ukulima wa kutumia jembe ni wa mwaka -2935 (+140) na kuendelea hadi mwaka -95.

Neolithiki ya Guinea inatokea baadaye kidogo upande wa mashariki huko Sierra Leone na upande wa Kaskazini nchini Burkina Fasso. Kwenye pango la Yengema, tarehe za vyombo vya udongo zinazowakilisha mwanzo na mwisho wa Neolithiki na vyombo vya udongo zinaonyesha kipindi cha kuanzia mwaka -2500 hadi -1500. Huko Kamabai kipindi cha Kineolithiki kinaanzia mwaka -2500 hadi +340 (+100). Kwenye eneo la kaskazini ya Burkina Fasso (Rim), aina hii hii ya uundaji ilikuwepo kati ya mwaka -1650 na +1000.

Lakini sifa bainifu za Neolithiki ya Guinea zilizojitokeza kwenye maeneo ya ukingoni mwa msitu, na tarehe zake kwa kuhusiana na maeneo ya utamaduni wa

mwanzoni wa uzalishaji chakula kwenye kanda za savana na Sahel, hazionyeshi tu kwamba mabadiliko ya kwenda katika uzalishaji wa chakula yalitokea mapema zaidi kwenye maeneo ya msitu bali kwamba mabadiliko haya haya hayakuathiriwa na athari za kaskazini.

Hivyo, kusema kwamba maeneo ya “mwanzoni kabisa ya Kineolithi” ya Afrika Magharibi yalikuwa na sifa bainifu za kiasili, mengi yao yakidhihirisha hatua za kujitokeza kwa mabadiliko ya kiuchumi na kijamii, hakuna maana kwamba kila eneo lilikuwa limejitenga pekee. Ushahidi kidogo uliopo unadokeza kwamba wakazi wa maeneo mengi kati ya haya walikuwa wa Kinegroidi.

Katika Sahara, Mneolithiki alionekana kuwa ni mchanganyiko wa makabila ya Kimediterani ua nyakati za Kineolithiki. Wakati yakisambaa kuelekea kusini, bila shaka yalikuwa ndio chanzo cha makundi kadhaa yenye ngozi zaidi yanayoishi katika sehemu ambayo sasa inaitwa Savana.

Ukweli kwamba Wanegroidi wa Kineolithiki wa mwanzoni wa Afrika ya Magharibi hawakuishi katika makundi ya kitamaduni yaliyojitenga, umeonyeshewa pia na kufanana kwa miundo ya vyombo vya udongo. Iwapo tarehe zi sawa basi inawezekana kwamba miundo hii ya vyombo vya udongo bila shaka ilienea kutoka Sahara ya kati kwenda sehemu za Sahel na Savana. Kwa upande mwingine, kupamba kwa ruleti (vitufe) kulikuwa ni sifa maalumu ya kusini, ambapo mapambo ya mistari ya mawimbi yenye vidoa na mistari ya mawimbi yaliyoenea sana baina ya maeneo ya Kinailotiki hayakuwepo kabisa kusini, lakini yalikuwepo kidogo katika baadhi ya maeneo ya Sahara ya inashariki na ya kati.

Sasa inaonekana kwamba kulikuwa na angalau maeneo manne ya msingi ya maendeleo ya Kineolithiki, mawili kati yao yalikuwa kaskazini kabisa mwa Afrika Magharibi. Hasa katika nyanda zilizo wazi katika eneo la kaskazini, mtindo wa uhanuishaji wa mifugo kufuatana na misitu, ilianzishwa mapema sau. Kwenye maeneo ya maziwa na mabonde na miteremko ya milima, uzalishaji wa mimea ya nafaka, na pengine ukulima mchanganyiko ulikuwa maarufu. Kwa upande mwingine mabonde na maeneo ya ukingoni mwa msitu yaliyokuwepo kusini yalifaa sana kwa ukulima wa mazao ya jamii ya viazi na michikichi.

Maeneo mawili makuu yameshatambuliwa huko Afrika Magharibi, moja kaskazini katika ukanda wa Sahel na Sudan, na jingine kusini katika ukingo wa eneo la msitu. Hivyo yote mawili yalikuwa katika sehemu zenye nuisimu inayopingana, insimu inmoja ukiwa haufai kwa uzalishaji mazao (joto, ukame au baridi). Mimea katika mazingira ya namna hii hujitunzia akiba ya kutosha ya chakula ili kuiwezesha kurudia tena maisha yenye nguvu wakati hali ya hewa inayofaa irudipo. Akiba hizi zilikuwa za namna ya mizizi na mashina kwa ukanda wa kusini na za namna ya mbegu kwa ukanda wa Sudan ya kaskazini.

Katika maeneo ya insitu na savana yenye mabadiliko kidogo sana au yasiyo na mabadiliko kabisa ya hali ya hewa kwa upande mwingine, mimea ilikua polopole na kwa mwendo unaolingana. Haikuhitaji jitihada kubwa ili kuishi, wala kulimbikiza

akiba - sifa ambayo huenda ilisaidia uanzishaji wa kilimo katika maeneo yote mawili. Ukanda wa Savana ya kati, uliobanwa kati ya maeneo mawili hayo yaonekana ulikuwa ni mahali pa kukutania athari za maeneo haya.

Hata hivyo, katika maeneo yote matatu makuu ya kitamaduni, mabadiliko kutoka ukusanyaji chakula hadi ulimaji chakula yaligeuka kidogo kwa namna kadhaa, mtazamo wa binadamu wa mazingira yake ya kiasili. Baada ya kuwa mkusanyaji, sasa alikuwa mzalishaji na "mhifadhi", na kwa hiyo (kupitia biashara ya masafa marefu) alibadilisha baadhi ya vitu ambavyo majirani zake hawakuwa navyo, kwa bidhaa ambazo kundi lake lilizihitaji. Mabadiliko ya kiuchumi pia yalisaidia kuleta maendeleo ya kazi za kiufundi na teknolojia mpya kupanuka kwa biashara na pia juu ya mabadiliko muhimu ya kijamii. Lakini mabadiliko haya ya kijamii yalitofautiana katika viwango vyake kwa kufuatana na namna ya msingi wa kilimo uliokuwa umeanzishwa.

Enzi ya chuma

Maendeleo ya enzi ya chuma yanaonekana hayakutofautiana sana na yale ya Kineolithiki isipokuwa kwanba hatua za mwanzoni kabisa za mabadiliko ya kwenda kwenye enzi ya chuma katika Afrika ya Magharibi yaliyotokea katika sehemu zote mbili za kanda ya Sahel/savana na sio katika maeneo ya msitu yaliyokuwa kusini: Kwa jambo hili, kama ilivyo kwa uzalishaji chakula wa mwanzoni, ushahidi wote wa kitamaduni na wa kikronolojia unaonyesha kwamba kulikuwa na mambo mengi ya kiasili katika harakati hizi za uhunzi.

Kama ilivyoelezwa kwa undani zaidi mahali pengine, ushahidi kulusu enzi ya chuma ya mwanzoni katika Afrika Magharibi hugawanyika kufuatana na hali ya nchi kikronolojia na kufuatana na makundi yake mbalimbali yakiwemo: (i) vyombo vya udongo, zana za chuma na za mawe yaliyochukuliwa; (ii) vyombo vya udongo, chuma na/au metali, pengine kwa kuhusiana na matendo kadhaa yanayoambatana na slughuli a mazishi, na (iii) vyombo vya udongo tu.

Katika maeneo ambako dalili za ufuaji chuma zimechanganyika na ufundi na uchongaji unawe uliostawi kwa kawaida huwa ndio aina za kale kabla ya makusanyiko ya enzi ya chuma, na huenda yakawa yanadhihirisha mabadiliko kutoka enzi ya mawe kwenda enzi ya chuma. Maeneo ya viwanda vilivyomo katika hatua ya mabadiliko ya namna hiyo yamepatikana katika sehemu kadhaa za Afrika Magharibi, na pia mahali penginepo yakiwemo maeneo ya Maziwa Makuu ya Afrika Mashariki. Kwa kawaida viwanda vya namna hii vinamasalia ya chuma, visu, vipande vya mishale na mikuki, nyundo za mawe, aina mbalimbali za maumbo ya shoka au tezo na pete za mawe.

Tofauti za kimaeneo zinaonekana pia katika vyombo vya udongo tangu enzi ya chuma ya mwanzoni. Kwa mfano, Bailloud ameonyesha kuwa mitindo miwili kutoka Ennedi inahusiana na ile ya Telimorou na Chigeou iliyoenea wakati wa mabadiliko ya enzi ya mwisho ya Kineolithiki enzi ya chuma ya mwanzoni. Mitindo hiyo yaelekea kuhusiana na *céramique cannelée* za Coppens kutoka Chad, na mtindo wa Taiwanga

kutoka Borku. Mtindo wa Telimorou unahusishwa vilevile na maeneo ya kale kabisas ya vijijini na ambapo unafikiriwa kuwa ni mtindo wa elfia ya kwanza kabla ya enzi zetu. Bailloud na Courtain wote wawili wanaonyesha mfanano wa mitindo hii ya vyombo vya udongo na ile ya Kundi C huko Unubi, ingawa tarehe za kundi la Unubi zaelekea kuwa ni za mapema zaidi (zikianza kiasi cha mwaka -2000). Mifano ya zana za mawe ambazo bado zinatumiwa ni vijaa, mawe yenye vishimo na pia mashoka yaliyokwatuliwa na kuwekewa makali. Hata katika kipindi kilekile, na wakati ziangaliwapo jadi za kisanaa, baadhi ya maeneo ya Nok yalikuwa na sifa za kipekee zinazodokeza tofauti za maeneo hayo. Kwa mfano, mashoka ya kukwatua hayapatikani kabisa huko Taruga na kuna tofauti katika vyombo vya udongo vya nyumbani kati ya Samun Dukiya, Taruga na Katsina Ala.

Sio tu kwamba utamaduni wa Nok ulikuwa umeshajijenga na kuwa madhubuti zaidi ya miaka 2500 iliyopita, bali yaelekea kuwa athari zake zilifika mbali. Kwa mfano, baadhi ya sifa za mtindo za utamaduni wa Nok ziko sambamba na sanamu za udongo za Dainia, ambako ufuaji chuma ulianza kiasi cha karne ya tano au ya sita ya enzi ya Ukristo.

Connah anafikiri kwamba karibu kwenye karne ya nane wakazi wa asili wa Daima waliingiliwa na wakazi wengine ambao walitunika chuma kwa ustawi zaidi na ambao walikuwa wakulima wa nafaka. Hawa walikuwa na mahusiano mapana zaidi kuliko wahenga wao. Lakini mila ya kuzika kwa kumkunjia maiti ziliendelea, kama ilivyokuwa kwa utengenezaji wa sanamu za udongo. Hawakuzika maiti wao katika mitungi mikubwa inayojulikana kama mitungi ya So, ingawa aina hii ya vyombo vya udongo inapatikana pia katika sehemu ya juu ya makaburi kuonyesha kuwa mtindo huu wa mazishi uliendelea katika vipindi vilivyofuata.

Maeneo niengi muhimu ya vilima ya vijiji vya kale yalipatikana kwenye vilinia vilivyokuwa ukingoni mwa mito kwenye bonde la chini la mto Chari katika Jamhuri ya Chad, katika eneo nusu kipenyo cha kilomita 100 kutoka Ndjamen. Maeneo haya yalitoa baadhi ya vitu ambavyo vilipatikana pia huko Nok na Daima, vikiwa ni pamoja na sanamu nzuri za udongo mwekundu, binadamu na wanyama, mapambo ya mawe, silaha za shaba nyekundu na shaba nyeusi, na maelfu ya viga. Vilevile mitungi mikubwa ya kuzikia ilitumika hapa na vijiji vilizungukwa na ngome.

Nigeria ya Kusini

Willet anaamini kwamba sifa nyingi mno za utamaduni wa Nok, hasa wa sanaa yake, zinapatikana katika utamaduni za baadaye za sehemu nyinginezo za Afrika Magharibi, kiasi cha kwamba ni vigumu kutoamini kuwa utamaduni wa Nok, kama tunavyofahamu, unawakilisha utamaduni wa kale kabisa ambao ndio uliotoa mila nyingi za sanamu. Iwe kauli hii ni kweli au si kweli, kwa hakika kuna kufanana kukubwa sana baina ya sanaa ya Nok na ya Ife ambako hatudhani kuwa kumetokea kwa nasibu tu. Kama ilivyo huko Nok, mila ya sanamu za kiasili ni ya karibuni

mwaka +960 (+130), na sanamu nzuri za vichwa zilikuwepo Ife na Benin, na kwa kiwango kidogo katika miji mingine ya kikale ya Kiyoruba.

Machimbo ya Igbo-Ukwu yanaonyesha waziwazi kwamba ufuaji chuma katika Nigeria ya kusini - mashariki ni wa mapema kiasi cha karne ya tisa ya enzi za Ukristo; lakini hakuna chochote kinachoonyesha kuwa uhunzi huo haukuwepo mapema zaidi kabla ya hapo. Kwa kuwa ufuaji chuma ulikuwa ni kazi ya ustadi wa juu, basi ulishuglulikiwa na jamii na koo maalumu tu. Wahunzi mashuhuri kabisa wa Kiigbo ni wale wa kutoka Awka, mashariki ya Onitsha ambao kwanza walipata chuma kutoka kwa wayeyusha madini wa Kiigbo wa Udi, waliokuwepo mashariki ya Awka, na ni hapo baadaye tu ndipo walipopata chuma cha kutoka Ulaya. Wahunzi wengine baina ya Waibo walikuwa wayeyusha chuma wa Abiriba, baina ya Waigbo wa mto Crossa; wafuaji chuma na shaba nyeupe waliopo karibu na tuta la Okigwe-Aroichnku, na wahunzi wa Kinkwero kwenye sehemu ya kusini ya eneo hili.

Eneo moja lililochimbwa huko Awka lilitoa -lupa kumi na tano za chuma na upanga wa chuma. Vitu vyote hivi vinafanana na vile vinavyotengenezwa na wahunzi wa Awka hadi sasa, ildadi kubwa ya kengele za kusubu za shaba nyeusi na vitu vinginevyo vya mwaka + 1495 (+95) ambavyo hudhaniwa na baadhi ya wanataaluma wa kigeni kuwa visingeweza kuundwa na wahunzi wa Awka.

Hajjulikani uhusiano wa mjuda/utamaduni kati ya Ife na Igbo-Ukwu ulikuaje, ingawa Willet anadhani kwamba yawezekana Ife ilikuwa mapema zaidi kuliko inavyofikiriwa sasa na hata inawezekana ukiwa ulikuwa karibu zaidi na Nok kuliko ushahidi wa sasa unavyoonyesha (yaani karne ya 13 mpaka ya 14 wakati wa enzi za Ukristo). Iwapo shanga za Ife ndizo hizo hizo shanga za "akori" kutoka Pwani ya Guinea, kama unavyoeleza ushahidi wa Frobenius na ushahidi wa *kiethnografia* kutoka kusini mwa Nigeria, basi yawezekana kwamba shanga za vioo za Igbo Ukwu zilitengenezwa Ife. Iwapo ni hivyo, basi tarehe ya utamaduni wa Ife inaanzia nyuma kabisa, sawa na wakati vyombo vya Igbo Ukwu vilipogunduliwa (yaani karne ya tisa ya enzi ya Kikristo). Kutokana na haya, ni muhimu pia kwamba kutoendelea kwa mila huko Ife kuhusu utengenezaji sanamu za mawe, vioo na ufinyanzi, kunakwenda sambamba na yaliyotokea Daima; na kwamba kutoendelea kwa utamaduni huko Daima kunaanzia baina ya karne ya sita na karne ya saba wakati wa enzi za Ukristo.

Enzi ya chuma katika sehemu za magharibi kabisa

Katika sehemu ya magharibi kabisa Enzi ya Chuma haifahamiki sana kuliko enzi ya Nok na maeneo yaliyoko karibu nayo. Kwa mfano, taarifa zilizopo kuhusu Mauretania hazihusu enzi ya chuma bali zinahusu "enzi ya shaba nyekundu". Kwenye eneo la Niger ya kati, na hasa eneo la Senegambia, hadi hivi sasa kilichopatikana ni sehemu tu ya mfululizo kikronolojia.

Machimbo yaliyofanywa na N. Lambert huko Akdjudjt ayanaonyesha kwamba uyeyushaji wa shaba katika Sahara ya magharibi ni wa tangu mwaka -570 hadi -400; yawezekana pia ikawa ndio wakati wa biashara ya shaba katika Sahara. Makadirio

katika maeneo mamojawapo ya kati ya haya yanaonyesha kuwa tani 40 za shaba zilitolewa kutoka chimbo hili, na inawezekana kwamba sehemu ya shaba hii ilipelekwa kuuzwa huko Sudan kutoka Sahara ya Magharibi.

Idadi kubwa ya vifaa vya shaba kutoka kwenye makusanyo ya maeneo haya na ya majumba ya makumbusho, na pia vile vinavyotajwa vitabuni, inaonyesha kuwa matumizi ya madini haya, ingawa yalikuwa kidogo, yalienea sana Afrika Magharibi kwa muda mrefu sana - ingawa shaba haikuwa maarufu sana kama vile mbao, chunia na udongo wa mfinyanzi. Shaba pamoja na mchanganyiko wake wa madini mengine, ililetwa katika namna mbalimbali ambazo hazikubadilika sana kwa kipindi cha karne nyingi, kama vile mikuo, vikuku (*manila*) pete, nyaya, kengele na vitasa.

Wafrika walitofautisha kati ya shaba nyekundu, yaani shaba katika hali yake ya uhalisi, shaba nyeusi na shaba ya manjano au shaba nyeupe. Kwa bahati mbaya haya yanaonekana kwa dhahiri katika maandiko mengi yaliyopo. Uchunguzi wa kispektografia unahitajika kufanywa ili kuonyesha aina halisi ya madini yaliyotumika kutengeneza kitu, na mapendeleo ya watumiaji wa mwanzoni wa shaba na mchanganyiko wake na madini menginye.

Eneo la Niger ya Kati

Kuna sehemu tatu ambako uchimbuzi unefanywa kuhusiana na enzi za chuuna katika eneo hili. Sehemu hizo ni:-

- (i) ndagano ya Niger – Bani katika bonde la mto Bani;
- (ii) kaskazini na kaskazini - mashariki mwa Masina na Segu; na
- (iii) mashariki mwa sehemu ambapo mto Niger unapinda kuelekea magharibi nchini Burkina Fasso.

Chungu kikubwa chenye kuta nene, kilichonakshiwa kwa mfululizo wa ruleti unaobetabeta kila mara, kilipatikana katika maeneo yote matatu na aghalabu kilitumiwa kama chungu cha kuzikia. Katika sehemu nyinginezo, vyungu vya mazishi huonekana vikiwa viwili au vitatu, ikiwa ni pamoja na vifaa vya nyumbani vilivyoambatana na maiti. Nchini Burkina Fasso (Rim), zana muhimu zilizohusika ni za chuma, zana za mawe ya kukwatua na kuchua na vyombo vya udongo vya nyumbani. Vilevile vifaa vya shaba nyeusi na vya shaba nyekundu vilikuwepo kwenye eneo la pindo la Mto Niger. Pia kwenye maeneo ya Masina na Segu, lakini sio Bani au Rim kwenda Mashariki kabisa, kulikuwepo na udongo wa kurembea wa aina ya kipckee na wenye maumbo mengi; sahani na mabakuli mazuri yenye kuta nyembamba baadhi yao yalikuwa na visehemu vilivyojichomozachomoza yakiwa yamewekewa viweko au yenye matako bapa; vikombe vya umbo la mguu; na madumu na magudulia yenye umbo la pia.

Huko Segu na Timbuktu baadhi ya watu hawa wa “enzi ya chuma” walikuwa hasa wakulima wakilima mtama na mpunga, ambapo wengine walikuwa hasa wavuvi wakitumia nyavu pamoja na viinikizo vya udongo niwekundu badala ya chusa za

mifupa. Kulikuwa na minara mizuri ya kumbukumbu ya kabla ya Uislamu, ikiwa na mawe yaliyopambwa vizuri kisanaa, na baadhi ya vitu hivi vilivyogunduliwa vimeenea ekari kadhaa, na kutoa dalili ya kuwako kwa makazi makubwa. Lakimi ni sehemu chache tu za maeneo haya ndizo zimefanyiwa uchunguzi, ambao ni wa juujuu tu, ingawa mengi ya maeneo haya yaliporwa na Wafaransa.

Huko Kouga, kwa mfano, machimbo ya chungu yalionyesha tarehe ya -950 (± 120) katika kiwango cha nyuma kidogo ikiwa na chombo cha kijadi kilichopakwa rangi nyeupe juu ya rangi nyekundu. Sehemu za nje za vigae zilikuwa na alama za mtama, ngano na pengine mahindi. Inaelekea kwamba katika eneo hilo na pia katika maeneo kadhaa mengine ya sehemu hii ya Afrika Magharibi, kulikuwepo na kiwango cha enzi ya chuma cha mapema zaidi kikiwa na vigae vilivyorembwa au visivyo na marembo, zana za mifupa na mawe, na vikuku. Mila za kitamaduni zinazohusiana na haya nchini Burkina Fasso zilitoa tarehe za awali zaidi kwenye karne ya tano/sita ya enzi ya Ukristo.

Eneo la Senegambia

Makaburi vilevile yamegunduliwa katika sehemu kadha za eneo hili, hasa huko Rao kwenye mlango wa mto Senegal na katika Senegal ya kaskazini kandokando mwa mto huo. Ingawa sehemu kubwa ya vitu hivi bado havijafanyiwa uchunguzi wa ndani zaidi, uchunguzi wa juujuu unaonyesha kwamba maiti walizikwa katika masanduku ya mbao yaliyofunikwa na kilima cha udongo chenye urefu usipungua mita 4, na kwamba pamoja na maiti, kulikuwepo zana za chuma, vikuku vya shaba nyekundu, shanga, dhahabu, vito vya thamani, vyungu, mabakuli, vikome na madumu kadhaa, vyote vikiwa na sura nibalimbali na visivyo na rangi lakini vikiwa vimepambwa kwa mtindo mbalimbali. Machimbo ya hivi karibuni yameonyesha kuwa maziko haya ni ya mwaka +750, ambacho ni kipindi cha baadaye kabisa kabla ya kipindi tunachokishughulikia kwenye sura hii.

Uchunguzi wa majaa kadhaa ya magamba kwenye eneo lenye ukubwa wa kilomita 22 kwa kilomita 6 huko Kasamansa ya chini, umeonyesha mfuatano wa kitamaduni ukianzia mwaka - 200 hadi +1600 ukiingiliana na utamaduni halisi wa mwanzoni wa Dyola. Sapir anaamini kwamba awanu ya mwanzoni kabisa inayojulikana hadi sasa (-1200 hadi +200), iliopatikana katika maeneo ya Loudia na Quolof tu, inawakilisha awamu ya mwisho ya Kineolithi na wala si ya mwanzoni. Maingiliano na athari za kitamaduni zinaonyeshwa na vyombo vya udongo vya kipindi hiki, ambavyo vina mbinu za kureniba kama vile inistari ya mawimbi, zilizofanana na za vyombo vya udongo vya Kineolithiki vilivyoenea sana kutoka Cap Vert hadi Algeria ya Kusini na hata Afrika ya Kati.

Data za kiakiolojia ya kipindi hiki zinaakisi makazi yenye watu wachache katika vituo vidogo kwenye miinuko ya mchanga ya chini, pengine ikiwa imeota majani na miti na kuzungukwa na msitu. Yaelekea, ingawa waliishi pwani, wakazi hao hawakujishughulisha na uvuvi. Vilevile mifupa iliyokutwa katika eneo hili haikuweza

kuonyesha ni ya wanyama gani na hivyo kufanya utambuzi wa chakula chao kuwa mgumu.

Wachunguzi wa mambo ya kale wanadhani kuwa kutokuwepo kabisa kwa mabaki ya konokono au mifupa ya samaki, na badala yake kuwepo kwa vigae badala ya kombe zilizotengenezwa kuwa vyombo, ni dalili kwamba maisha ya wakazi hawa hayakutegemea sana bahari. Aubreville anadhani kwamba hapo kale msitu mnene ulienea sehemu yote inayozunguka Uwanda wa Juu wa Cussouye mpaka ulipoangamishwa kwa moto na kugeuzwa kuwa mashamba ya mpunga yaliyo wazi. Iwapo hivi ndivyo, basi hii inaweza kuwa na maana kwamba wakazi hawa wa kipindi cha kwanza walikuwa wakulima wa mpunga wa mlimani au mpunga wa sehemu za akavu.

Uvumbuzi vilevile umeonyesha kuwa uwindaji wa wanyama uliongezeka baada ya mwaka +300, kiliino cha mpunga nacho huenda kiliongezeka katika kipindi hiki japokuwa uchunguzi kamili wa mabaki ya mpunga pamoja na mimea mingine bado haujafanyika.

Tunachoweza kusema ni kwamba ushahidi tulionao hautuwezeshi kuelezea asili ya kilimo cha mpunga kwenye sehemu zenye vidimbwi na tingatinga. Hata hivyo, inaweza kufaa kueleza hapa kwamba kufuatanana na maoni ya Porteres, Senegambia ilikuwa na umaarufu wa pili kwa uzalishaji wa aina ya *Oryza Glaberrima*, kituo kikuu cha uzalishaji huo kikiwa sehemu fulani ya karibu na Niger ya kati.

Inaelekea eneo la Kasamanse karibu na pwani lilikuwa maarufu kwa ukulima wa mpunga katika sehemu zinazofurika maji. Wakati huu matumizi ya zana za chuma yaliwezesha kusafisha mbuga za mikoko na kulima matuta kwenye udongo inzito wenye topc kwa ajili ya mashamba ya mpunga. Kusema kweli tutafanya vizuri iwapo tutatafuta vituo vya kwanza vya ukulima wa *Oryza glaberima* kwenye udongo tifutifu wa mabonde ya ndani, wa ardhi kavu au wa mlimani kwa mpango wa kutawanya au kupandikiza kwenye vishimo baada ya kusafisha mashamba wakitumia nyenzo za mawe.

Inependekezwa na wataalamu kama vile Arkell kwamba mapokeo ya ufagaji chuma ya Afrika Magharibi yalitoka Misri au Unubi, ambapo wataalamu wengine, kama vile Mauny, wanasema yalitoka Karitoji. Kusema kweli, shaba nyekundu na shaba nyeusi baadaye ilifuliwa kwa namna ileile kama chuma, ambapo huko Misri na Unubi shaba nyekundu na chuma zilifuliwa kwa njia zinazotofautiana kabisa. Ushahidi uliopo, hauziungi mkono nadharia hizi mbili zinazohusu kuenea kwa maarifa ya ufuaji chuma. Inaonekana, kwa mfano, Wagaramanti wa Libya na watu wa Meroit walianza kutumia mikokoteni, na pengine zana za chuma, karibuni wakati uleule (-500) ulipoanza ufuaji chuma katika eneo la Nok la Nigeria ya kaskazimi. Kusema kweli, kutokana na tarehe za baadhi ya maeneo zinaonyesha kwamba ufuaji chuma unaweza hata ukawa ulijitokeza katika eneo la Nok mapema zaidi kwenye mwaka -1000.

Nadharia ya kuenea kwa ufuaji chuma katika Afrika Magharibi haitili maanani

sana masuala mengi yanayohusiana na hatua hii: yaani, jinsi gani, lini na mahali gani hatua zilichukuliwa kubadili vifaa vilivyofanyizwa kwa mawe na udongo na kuwa madini inapya yaliyo madhubuti na yanayodumu zaidi ambayo yangepaa zaidi kuliko mawe kwa kutengenezea silaha na pia kuweza kutumika kwa namna nyinginezo mbalinibali. Kuhusiaua na swala hili Diop na Trigger wameeleza sawasawa kabisa kwamba "tarehe za mwanzoni kwa uacneo ya Enzi ya Chuma katika Afrika Magharibi na Afrika ya Kusini lazima zitumiwe kutukumbusha kwamba yawezekana pia kuwa ufuaji chuma ulikuwa ukiendelea wenyewe katika sehemu moja au kadha kusini mwa Sahara bila ya kutegemea kuiga kutoka sehemu nyingine".


Biashara ya kabla ya historia na nchi za awali za Afrika Magharibi

Vyombo vilivyopatikana kutoka katika makaburi ya Fezzan vinaonyesha kwamba vitu vya Kirumi vililetwa hapo kati ya karne ya kwanza na ya nne ya enzi za Ukristo. Inaelekea kwamba baada ya kuchukua nafasi ya Wakariteji kwenye pwami ya Tripolitania mwishoni mwa karne ya pili kabla ya enzi zetu, Warumi kwa upande wao waliagiza meno ya ndovu na watumwa kutoka Sudani, huku Wagaramanti wakiwa ndio wateja wao wakuu. Baada ya kufifia kwa utawala wa Kirumi, biashara nayo ilififia; lakini iliinuka tena baada ya Brizantina kutekwa tena baada ya nuwaka +533 na kabla Waarabu hawajawashida Wafezzan. Hivyo uchunguzi wa hivi karibuni wa kiakiolojia unaonyesha waziwazi kwamba aina fulani ya biashara ya masafa marefu wakati wa kipindi cha kabla ya historia ilifanywa na watu wa Sahara na Afrika Kaskazini. Lakini hata hivyo, jambo hili halithibitishi ukweli wa madai kama yale yaliyofanywa na Posnansky kwamba ili kugundua asili ya biashara ya masafa marefu ya Afrika Magharibi, uchunguzi wetu sharti uanzie kwenye michanga ya Sahara. Hata kama ungekuwa una malengo mazuri, msisitizo huu si sahihi na matokeo yake pia hayawezi kuwa ya kweli. Kwani mtazamo huu unakataa ukweli kwamba kulikuwepo na mfumo wa ndani ya biashara ya masafa marefu katika Afrika Magharibi ambao ulitangulia sana, na ambao kusema kweli ndio uliwezesha kuendeleo ya biashara ya kuvuka Sahara.

Kwa maoni ya mwandishi huyu, ushahidi uliopo unaonyesha nyakati za mwanzoni mwa enzi ya chuma kwa mfumo changamano na mpana wa biashara ya masafa marefu, hasa katika mazao ya viwanda vya ufundi baina ya wakazi wa pwani na wakulima wa bara kwa upande mmoja, na pia kati ya wakulima wa bara wa kusini na jamii za kifugaji zaidi za kaskazini kwa upande mwingine. Bidhaa muhimu za mumo humo, zilizotumika kwa biashara, zilijumlisha chuma na mawe (kwa ajili ya zana za silaha), ngozi, chumvi, nafaka, saniaki wakavu, nguo, vyombo vya udongo, vitu vya mbaao, kola na maembo ya mawe na chuma.

Mfumo wa biashara ya ndani na mazao ya viwanda vya ufundi vilivyokuzwa ndani ya Afrika Magharibi ulizipa sura na kuzihifadhi njia za biashara kati ya ulimwengu wa Afrika Magharibi na ule wa Sahara. Biashara ya ndani ya namna hii vilevile ilichochea ukuaji wa vijiji vikubwa zaidi na miji katika nyakati za enzi ya mwisho ya

Neolithiki na enzi ya chuma ya nyuma. Taarifa za kiakiolojia ambazo zinakusanyika sasa, hasa kuhusu maeneo ya misitu ya Afrika Magharibi, zinaendelea kuonyesha kwamba kutokea kwa baadaye kwa mataifa ya Asante, Benin na Yoruba, pamoja na utamaduni wa Igbo-Ukwu, kulitegemea sana matumizi makubwa yaliyofaulu ya mazingira yao na watu wa mwanzoni waliotumia chuma (na wakati mwingine wale ambao hawakutumia chuma).



Afrika ya Kati

Mambo mawili yaliyo muhimu kwa historia ya Afrika, ni kuenea kwa ufuaji wa madini na mtawanyiko wa ajabu wa lugha za Kibantu.

Kwa muda mirefu kumekuwa na mwelekeo ulio wazi wa kuyaunganisha masuala haya mawili na kulielezea suala moja kwa kuhusiana na jingine. Kuenea kwa ufuaji wa madini kunaonekana kama ni matokeo ya kutawanyika kwa Wabantu, na kwa upande wa pili, kupanuka huku kunadhaniwa kwamba kuliwezesha na kumiliki kwa zana za chuma ambazo zilifanya iwezekane kuukabili msitu wa ikweta.


Wanaisimu ndio walikuwa wa kwanza kutoa nadharia kwamba lugha za Kibantu zilitokea kwanza kwenye nyanda za juu za Nigeria na Cameroon. Wanaakiolojia nao walifuatia mkondo huu huu na walijitahidi kuyafanya maono yao katika nyanja zao mbalimbali yalingane na nadharia hii tete. Lakini nyanja zinazoshughulikiwa na sayansi hizi si sawa, na ni jambo la kusikitisha kuona kwamba neno Bantu, ambalo ni istilahi ya kiisimu, lilitumiwa kwa dhana ya ethnolojia ya Wabantu na jamii zao, na tokea hapo kwa dhana ya kiakiolojia ya enzi ya chuma ya Wabantu.

Usuli wa Kijiografia

Eneo linaloshughulikiwa katika sura hii ni Afrika ya Kati, yaani jamhuri ya Zaire na nchi zilizo jirani yake za Gabon, Kongo, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Rwanda, Burundi na Zambia ya kaskazini.

Eneo hili linafanya bonde kubwa lenye mwinuko wa wastani wa mita 400. Kuzunguka uwanda huu mkubwa wa ndani, ardhini inainuka mfano wa ngazi na kuwa milima au nyanda za juu. Maeneo ya karibu na Ikweta yana mvua ya kutosha kwa kipindi chote cha mwaka. Kaskazini na kusini kuna kanda zenye misimu miwili ya mvua ambayo inaungana na kufanya msimu mmoja; kwenye eneo la kuanzia latitudo 5° au 6° kuna msimu mmoja wa mvua. Wastani wa kiwango cha joto kwa mwaka ni mkubwa kiasi cha kutosha, na kiwango kinapanuka zaidi kulingana na umbali kutoka Ikweta.

Bonde la kati linetandwa na msitu mnene wa Ikweta unaopakana na savana. Katika maeneo yaliyo na msimu wa ukame unaojulikana, nyasi huwa nyingi, lakini mara nyingi kuna kanda za misitu kandoni mwa mito.



25.1 Ramani ya Afrika ya Kati inayoonyesha mahali mlimotajwa katika matani

Enzi ya mawe ya nyuma

Jamii za enzi ya mawe ya nyuma za wawindaji na wahemeaji wakusanyaji zilitumia sana zana maalumu. Kwa kawaida, tofauti hufanywa kati ya mapokeo mawili yanayopingana; yale ya eneo la viwanda la Tshitolia na yale ya eneo la viwanda vya mikroliti ambayo mifano yake mizuri inayojulikana ni ile ya Nachikufa na Wilton.

Kiwanda cha Tshitolia kipekee kabisa kikilinganishwa na viwanda vingine vya enzi ya mawe ya nyuma vya Afrika ya Kati. Kijiografia, kiwanda hiki kipo katika eneo la kusini na hasa kusini - mashariki ya bonde la Zaire. Kiwanda cha Tshitolia kinaonekana kinaendeleza mapokeo ya eneo la Lupembia, na kimejitenga na eneo hili kutokana na mwelekeo wake wa kupunguza ukubwa wa zana na kuzifanyia maumbo mapya: vipande vyenbamba vya mishale vilivyopakwa harufu kali, maikrolithi za kijiometri (segmenti, trapeza). Baadhi ya zana za kukwatuliwa zinapatikana vilevile mwishoni mwa Tshitolia. Kikronolojia kiwanda cha Tshitolia kinaonekana kiliendelea kuanzia karibuni mwaka -12000 hadi -4000 na pengine hadi mwaka -2000 au katika mahali maalumu, hata kufikia mwanzoni mwa enzi za Ukristo.


Kimsingi, Nachikufa ni kiwanda cha maikrolithi ambacho kinaelekea kilianzishwa kaskazini mwa Zambia zaidi ya miaka 16000 iliyopita. Kilikuwa na hatua tatu zilizofuatana. Hatua ya zamani kabisa ilitengeneza zana za maikrolithi kwa nuunganisho wa idadi kubwa ya mawe yaliyotobolewa na zana za kusagia. Hatua ya pili, ambayo ilianza kiasi cha mwaka -8000, ina sifa ya kuwapo kwa zana zilizokwatuliwa. Hatua ya mwisho ya kiwanda hiki, iliyoanza karibuni mwaka -2000, inajipanbanua kwa kuwa na idadi kubwa ya segmenti ndogondogo, vyombo vya udongo na vifaa vichache vilivyotengenezwa kwa chunia - hivi vya mwisho huenda vimetokana na biashara. Mapokeo ya Nachikufa yanaonekana kuwa yaliendelea hadi kwenye karne ya kumi na tisa.

Kuna ushahidi wa kiwanda cha Wilton, ambacho ni cha maikrolithi kamili, katika Zambia ya kusini na sehemu kubwa ya Afrika ya Kusini. Zana za kukwatuliwa, vilevile zilipatikana mwishoni mwa maendeleo ya kiwanda hiki.

Inaelekea nyumba zilijumlisha vibanda vya matawi na nyasi vilivyofanana na vibanda vya Wasani wa jangwa la Kalahari. Maiti walizikwa papohapo, bila vyombo au zana zozote katika makaburi yao. Maiti hao walilizwa kwa namna mbalimbali.

Hakukuwepo na kilimo wala ufugaji. Machimbo yameonyesha kwamba chakula kilifanana na kile cha watu wa siku hizi na hasa kilijumulisha namna mbalimbali za vyakula vya mboga, kutokana na mimea pori, ambapo vilijalizwa kwa uwindaji na uvuvi. Wakazi wa Gwisho walikuwa na eneo kubwa sana, na waliwinda wanyama wanaopatikana katika nyanda na pia wa msituni.

Kuna idadi kubwa ya viwanda vya mikrolithi katika Afrika ya Kati ambavyo hasvijachambuliwa kiasi cha kutosha na haviwezi kuingizwa katika kundi la viwanda tulivyoviorodhesha hapo juu. Pengine baadhi ya viwanda hivi ni namna nyingine tu za viwanda vilevile ambavyo vimerekebishwa kwa ajili ya vifaa na shughuli maalumu.



25.2 Ramani ya Afrika ya Kati inayoonyesha maeneo ya makazi ya Neolithiki na enzi ya chuma ya mwanzoni.

Kuna ushahidi kidogo wa kuthibitisha kuwepo kwa tofauti kati ya enzi ya mawe ya nyuuna na ya Neolithiki. Hata hivyo, sifa za kiethnolojia zinazoonekana kimapokeo kuwa zilitokana na Neolithiki ni nyingi sana katika maeneo kadha, kwa mfano Uele, Ubangi, na kwa kiwango kidogo, Zaire ya Chini. Hili liliwafanya wanaakiolojia wa mwanzoni wa Afrika ya Kati kutofautisha Neolithiki ya Uele, Ubangi na Leopold. Lakini hivi vinavyoitwa viwanda, kwa jumla haitambuliwi kabisa isipokuwa kwa ajili ya zana zake za kukwatuliwa zilizokusanywa juu ya ardhi au zilizopatikana kwa kunumuliwa.

Kuhusu kiwanda cha Ubangi, sasa kuna eneo lililochimbwa huko Batalimo, kusini mwa Bangui, katika Jamhuri ya Afrika ya Kati. Eneo hii limetoa vishoka au tezo, shoka lenye makali yaliyokwatuliwa kidogo, idadi kubwa ya vifaa vya tasnia isiyokuwa ya maikrolithi, na vyombo vya udongo vyenye mapambo mengi; magudulia marefu yenye shingo pana, vyungu vyenye vitako bapa na mabakuli.

Tarehe zinazotokana na joto-angavu zinaonyesha kuwa vyombo hivi vya udongo vilikuwa vya takribani mwaka + 380 (+ 220). Kwa baadhi ya wataalamu tarehe hii inaweza kuonekana kuwa ni ya karibuni mno lakini kwa kuwa hakuna ushahidi mwingine, basi haiwezi kukataliwa.

Huko Zaire ya Chini, kuanzia Matadi hadi Kinshansa, mashoka yenye makali yaliyokwatuliwa kwa kiasi cha kutosha, yanapatikana; wakati mwingine yakiwa na vyombo vya udongo vyenye vitakovywa bapa. Wakati wa uchimbuzi wa hivi karibuni kwenye pango la eneo hili, shoka lililokwatuliwa lilipatikana likiwa pamoja na vyombo hivi vya udongo na majivu ya miti, na kielezo chake; baada ya kupimwa ka kutumia redio-kaboni kilitoa umri wa -390 hadi -160. Majaribio ya uchimbuzi kwenye pango lingine lililoko umbali wa karibu maili 6 hivi, pia ulionyesha shoka la kukwatua likiwa pamoja na vyombo hivyo hivyo vya udongo.

Nchini Gabon tabaka za maeneo mbalimbali, kama lile la Njole, lililoko maili 120 mashariki mwa Libreville, zinaonyesha kiwango cha Neolithiki likiwa na mashoka yenye makali yaliyokwatuliwa, vyombo vya udongo na vipande vya kwatzi.

Enzi ya chuma ya mwanzoni

Kulikuwa na mahusiano kati ya watu wa enzi ya mawe iliyokuwa ikiusogelea mwisho wake na wafuaji wa kwanza wa madini. Ukweli huu umethibitishwa kwa jumla. Lakini hatuelewi iwapo mabadiliko haya ya kiethnolojia yalileta mabadiliko makubwa katika jamii zinazohusika.

Enzi ya chuma ya mwanzoni, kwa kawaida inahusishwa na vyombo vya udongo vilivyo na vitako vilivyobonyea kidogo. Vyombo hivi vya udongo, vilivyofamuliwa kwa mara ya kwanza mnamo mwaka 1948, sasa vinajulikana kwa jina la Urewe. Vimepatikana katika sehemu za Kenya, na katika eneo la ziwa huko Uganda. Baadhi ya mifano iliyopatikana huko Kasai vilevile inaelekea kuwa ni mojawapo ya eneo hili pana la mtawanyiko wa Urewe. Tarehe nyingi za aina za vyombo hivi vya udongo ni za kati ya mwaka +250 na +400. Lakini angalau katika eneo moja lililoko Katuruka,

katika sehemu za Buhaya, Tanzania, tarehe zilizo za mapema zaidi zimepatikana. Kwa bahati mbaya bado ni vigumu kutathmini maana halisi ya ugunduzi huu.

Vyombo vya Urewe vinafanana sana, na mara nyingi imefikiriwa kwamba mifano hii tofauti ilikuwa na asili moja na kwamba tofauti zinazowakilishwa na vyombo hivi ni mabadiliko madogo tu ya mahali na wala si hatua tofauti za kikronolojia. Ni kweli kwamba havionekani katika matabaka yaliyo katika mfuatano wa safu.

Tangu mwanzoni kabisa, ufuaji wa chuma unaonekana kuwa uliambatana na tabia kadhaa za kitamaduni kama vile ufinyanzi wa vyombo vya udongo na ujenzi wa vijiji vya kakandika. Kwa kawaida inakubalika vilevile kwamba kilimo na ufugaji vilifanyika kwa wakati huohuo mmoja.

Tangu mwanzoni kabisa, ufuaji wa chuma zunaonekana kuwa uliambatana na tabia khaa za kitamaduni kama vile ufinyanzi wa vyombo vya udongo na ujenzi wa vijiji vya kukandika. Kwa kawaida inakubalika vilevile kwamba kilimo na ufugaji vilifanyika kwa wakati huohuo mmoja.

Kuwepo kwa vyombo vya Urewe kunaonekana vizuri zaidi katika eneo la ziwa (Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Tanzania) na pia Zaire, kwenye eneo la Kivu. Kwa muda mrefu vyombo vya udongo vya Zambia vya enzi ya chuuma ya mwanzoni (vyenye marembo ya vifereji) viliwekwa kwenye kundi la vyombo vya udongo vyenye vitako vivyo na vishimo. Lakini kusena kweli vinaonekana kwamba vinaweza kugawanywa katika aina kadha zinazotokana na inaeneo.

Mabaki kadha ya majengo kwa ajili ya kuishi au maghala, yametunzwa. Mfululizo wa mashimo manane yenye kingo sambamba zilizonyooka, zikiwa na nusukipenyu chenye kupita kidogo mita 1 na kina cha wastani wa karibu mita 2, yalikuwa na vyungu na vigae, vipande vya kalibu, vitu vilivyotengenezwa kwa chuma na mavi ya chuma. Mashimo manne kati ya haya yalizungukwa na handaki la duara, pengine likiwa ni mabaki ya tabaka la juu.

Ushahidi pekee usio wa moja kwa moja unaonyesha kwamba kulikuwepo na shughuli za kilimo lakini hakuna dalili zenye uhakika kuhusu kuwepo kwa ufugaji.

Vipande vingi vya mavi ya chuma, hasa lile pande moja kubwa kutoka sehemu ya chini ya kalibu na vipande kadhaa vya maboinba vinaonyesha kwamba kulikuwepo na unyeyushaji wa chuma, kama sio katika maeneo ya makazi, basi angalau karibu na maeneo hayo.

Baadhi ya vitu vilivyochimbuliwa kutoka mashimo hayo ni pamoja na vipande vingi vya mikuki, visu, mishale, vikuku na mafurungu, pete za vidole vya mikono na pete za vidole vya miguu. Vikuku au mafurungu na mapambo mengineyo yalitengenezwa piakwa shaba nyekundu.

Utumiaji wa mawe uliendelea, kama inavyodhihirishwa na mawe mengi ya kusagia na michi mingi ya kutwangua, vyombo vya kupondea, nyundo (pamoja na nyundo za wahunzi), fuawe, na zana nyingi ambazo zilitumiwa kwa kukunia/kuparuria, kukatia au kusugulia. Udongo wa mfiyanzi na ngeu vilitumiwa kuwa ni rangi.

Kwa kawaida, midomo ya vyombo vya udongo ilikuwa duara na yenye mkunjo ikiwa minene ukingoni. Sehemu zote za chini (vitako) zilikuwa za duara, isipokuwa kwa vyungu viwili tu ambavyo vilikuwa na kishimo kilichobonyezwa kwa vidole.

Mapambo, ambayo yalitiwa kabla ya kuoka, mara nyingi yanaonekana mabegani au juu ya mabega. Mitindo inajumusha jamii ya mifuo iliolala sambamba na kukatizwa na mifupa ya samaki waitwao mikunga na mizunguko ya kuendelea juu mithili ya hesi. Mfumo wa alama za miraba pembetatu zilizoinama kidogo na kukatishana mara kwa mara hufanya mtindo wa sura iliyoko shingoni na mabegani.

Mifano ya vyombo vya udongo vinavyofanana na vile vya Maporomoko ya Kalambo vimepatikana katika maeneo kumi na moja ya jimbo la kaskazini la Zambia, vikiwa vimetawanya kwenye eneo la zaidi ya maili za mraba 97,000.

Kukoskana kwa machimbo mengi na tarehe zenye uhakika kunazifanya data chache tulizonazo kuwa za makisio tu. Vyungu vinne, viwili katika yake vikiwa na vitako vilivyobonyea, vilivyopatikana karibu na Tshikapa, vinaelekea kuwa mi vya mtindo wa Urewe; kwa upande mwingine magundulia mengi na vigae vilivyopatikana katika pango la karibu na Mbuji-Mayi vinaendelea kukumbusha sana vyombo vya udongo vya kiwanda cha Maporomoko ya Kalambo.

Uchunguzi zaidi wa vyombo vya udongo unaonyesha kuwapo kwa makundi mengi, baadhi yake yakiwa yameenea schemu kubwa sana. Makundi yote haya hayahusiani na vyombo vya Urewe. Kwa kuwa uchimbuzi haukuwa mpana, hatuwezi kujaribu kutafuta kronolojia ya vyombo hivi vya udongo au vitu vingine vya metali.

Katika eneo la Bouar la Jamhuri ya Afrika ya Kati kuna vilima kadhaa vyenye ukubwa mbalimbali vikiwa na mawe ya mraba juu yake pengine marefu hadi kufikia mita tatu. Wakati mwingine kuna safu ya makaburi, na inaonekana kama vilima hivi vilikusudiwa kuonyesha makaburi.

Hata hivyo hakuna mifupa iliyopatikana, ingawa vitu vilivyotengenezwa kwa chuma vimevumbuliwa. Zipo tarehe sita za radio kaboni. Mbili ni za mwaka wa elfia ya sita na ya tano kabla ya enzi zetu na nne nyingine ni za kuanzia karne ya saba kabla ya enzi za Ukristo. Tarehe ya kwanza inaonekana kuwa ni ya wakati wa ujenzi wa vilima, ya pili wakati vilima vilipotumika tena kwenye enzi za chuma.

Makaburi ya Sanga na Katoto yapo katika bonde la Zaire ya Juu, kwenye makaburi ya Upemba, na ni maeneo ya enzi ya chuma ya mwanzoni yanayojulikana sana katika Jamhuri ya Zaire.

Likiwa kwenye ukingo wa Ziwa Kisale, karibu na Kiukondja, eneo la mazishi la Sanga, lililogunduliwa muda mrefu uliopita, lilichimbuliwa kwa mpangilio mnamo mwaka 1957 na 1958. Uchimbaji mpya ulifanywa mwaka 1974. Jumla ya makaburi 175 yameshafukuliwa, lakini ni wazi kwamba sehemu kubwa ya eneo hili bado inahitaji kuchunguzwa.

Baada ya uchimbaji wa mwaka 1958 makundi matatu ya vyombo vya udongo yaliainishwa na ilionekana kama kwamba yangeweza kuwekewa kronolojia. Kundi la Kisale (lililo kubwa kupita yote) lilionekana kuwa ndilo kongwe kuzidi makundi yote,

likifuatiwa na kundi la Mulongo (kutokana na jina la mahali kaskazini - mashariki ya Sanga); na mwisho kundi la vyombo vya udongo mwekundu unaoteleza.

Uchimbaji wa mwaka 1958 ulionyesha kwamba makundi haya matatu yalikuwa ya wakati mmoja. Kwa kuwa hakuna kronolojia ya ndani, tarehe mbili za redio kaboni zinatuwezesha kukadiria umri wa eneo hili. $+710 (\pm 120) + 880 (\pm 200)$.

Tarehe ya kwanza ilipatikana kutoka katika kaburi ambamo mkao wa maiti ulikuwa si wa kawaida kabisa, na chungu kimoja ingawa ni cha kundi la Kisale, hakikufanana na vyungu vinginevyo. Tarehe nyingine inatoka katika kaburi ambalo halikuwa na vifaa vilivyoo na sifa ya tamaduni hizi tatu. Kwa hiyo hatuelewi tarehe yake sawasawa.

Zaidi ya hayo, wasiwasi wa tarehe hizi unababaisha thamani yake. Tunachoweza kusema kwa uhakika ni kwamba, katika miaka mia kadhaa, baadhi ya makaburi ya Sanga yanarudi kipindi cha nyuma cha kati ya karne ya saba na ya tisa. Machimbo yanatupatia kidokezo cha eneo lenyewe la mazishi na, kwa kupitia kidokezo hicho, twapata mwangaza kidogo wa jamii ya Sanga ya kale.

Kanuni za mazishi zinaonekana zilikuwa zinatatanisha. Mengi ya makaburi yanaelekea upande wa kaskazini au kaskazini mashariki makaburi ya Mulongo- yale ya udongo mwekundu unaoteleza yanaelekea kusini. Kwa kawaida maiti alilala *decubitus dorsal* na alizikwa pamoja na vifaa ambavyo bila shaka vilikusudiwa vimrahishishie nambo katika dunia nyingine. Vyombo vya udongo havionyeshi kabisa alama za kuchakaa, na kufanana sana kwa baina ya vyombo kadhaa katika kaburi fulani kunaelekea kuonyesha kwamba vyombo hivi vilitengenezwa mahususi kwa ajili ya shughuli za maziko. Magudulia haya huenda yalijazwa chakula na vinywaji. Maiti alipambwa kwa vito vya shaba, chuma na meno ya ndovu. Inaonekana kama kwamba watoto waliozaliwa kabla ya wakati wao kufikia vilevile walizikwa. Wakati mwingine maiti alikuwa na kifurushi cha misalaba midogo midogo mkononi mwake. Kuna mwelekeo ulio wazi wa ukubwa wa magundulia kulingana na umri wa maiti.

Picha ya jumla ya Sanga anayoipata mtu ni ya ustaarabu ambao watu wanawekea umuhimu zaidi uwindaji na uvuvi kuliko ukulima. Hata hivyo majembe na mito ya mawe yamepatikana makaburini, kama yalivyopatikana mabaki ya mbuzi na kuku.

Kwa kuwa mifupa bao haijachanganuliwa, data pekee ya kiantropolojia tuliyo nayo ni uchunguzi wa kiodontolojia wa baadhi ya mabaki ya wanadamu. Uchunguzi huu hasa unaonyesha kujitokeza kwa mara kwa mara kwa meno yaliyokatwa. Hatuelewi ukubwa wote wa eneo la mazishi, ambao ungeweza kutupatia fununu ya idadi ya watu ya huo wakati.

Hivyo, ustaarabu wa Sanga, unaonekana ulikuwa jambo kubwa lakini kwa kadiri ya ufahamu wetu wa sasa, ulikuwa umejitenga. Huenda ugunduzi wote kwa jumla ni wa kipindi kirefu zaidi kuliko inavyoonyeshwa na tarehe mbili za redio kaboni.

Uchimbaji mpya ulifanywa mwaka 1974. Lengo kubwa lilikuwa kuchunguza ni kwa kipindi cha muda gani eneo la mazishi limekuwa likitumika na kupata kronolojia yake ya ndani, kuliwekea mipaka eneo hili, na kujaribu kutafuta eneo la makazi.

Makaburi mapya thelathini yalichunguzwa; huenda yatatuwezesha kukamilisha kronolojia na kupata madokezo kadhaa juu ya ukubwa wa eneo la mazishi. Lakini kwa sababu ya kupanuka kwa kijiji cha kisasa, eneo la makazi halikuweza kupatikana.

Hata hivyo, huko Katongo, maili 6 kutoka Sanga, uchimbuaji unaelekea kuwa umeonyesha kiwango cha makazi, chini ya mlima mmoja, yaliyo kwenye umbali wa chini ya nusu maili kutoka eneo moja la makaburi, uchimbuaji pia ulionyesha kuwepo kwa makundi ya vyombo vya udongo yaliyotambuliwa huko Sanga.

Vyombo vya makaburini ni vizuri kama vile vya Sanga na hapa pia vinaonyesha kwamba jamii ilisitawi ikiwa na kiwango cha juu cha maendeleo ya kiteknolojia. Kuwepo kwa majembe na mawe niengi ya kusagia kunaonyesha kwamba kilimo kilikuwa muhimu lakini uwindaji na uvuvi ulifanyika pia.

Kuwapo kwa shanga za kioo na narembu yanayotokana na makombe kutoka Bahari ya Atlantiki na ya Hindi, kunaonyesha shughuli za biashara zilizoenea masafa ya mbali kiasi cha kutosha.

Vyombo vya udongo vya Katoto ni vya kiasili, kama vile vya Sanga, na vinaonekana kutofanana sana. Baadhi ya namna ya urembeshaji inakumbusha vyombo vya Urewe, lakini kwa kuwa hakuna vyombo vya Urewe vilivyopatikana katika eneo la Shaba haiwezi kusemwa kwamba vyombo vya udongo vya Katoto ni maendelezo ya mtindo wa Urewe, badala ya tukio rahisi la ukaribiano tu. Kusema kweli baadhi kubwa ya namna hizi za maumbo nifano wa niufupa ya samaki na maumbo yenye duara za kati, zimeenea sana. Mashimo yalitokea baadaye zaidi kuliko makaburi, na wakati mwingine yaliyaleta shida makaburi. Shimo mojawapo kati ya mashimo hayo limepatiwa tarehe ya redio kaboni +1190 (± 60).

Eneo la mazishi la Katoto linakamilisha picha iliyodokezwa na uchimbuaji wa Sanga. Lakini ni ajabu kwamba makazi mawili makubwa ya namna hii, yakiwa yamekaribiana vya kutosha na ya kipindi kilekile, yalikuwa yanafanana kidogo sana.

Licha ya wingi wa vifaa vya makaburini, hatujui mengi kuhusu watu waliozikwa katika makaburi haya. Hatuelewi walikuwa watu gani, walitokea wapi au walikufa kwa sababu zipi, na tuna ushahidi mchache sana wa kutuwezesha kufikiria jinsi gani waliishi. Ukubwa wa maeneo haya mawili ya mazishi yanaonyesha kwamba kuelekea mwishoni mwa wa elfia ya kwanza ya enzi ya ukristo kingo za Lualaba ya juu zilikuwa eneo la mkusanyiko mkubwa wa watu, uliosaidia kuanzishwa kwa ustaarabu mkubwa. Uchimbuaji unaondelea sasa katika maeneo kadhaa utatufundisha mengi zaidi kuhusu ustaarabu huo.

Asili ya Wabantu

Kama tulivyosema, neno 'Bantu' kwanza kabisa lina maana ya kundi la lugha. Lakini polepole linepata maana ya nyongeza ya kiethnografia, na hata ya kianthropolojia. Kusema kweli ulikuwa uainisho wa kiisimu ambao ulitumiwa kama msingi na watafiti wa nyanja nyinginezo.

Kutokana na kutokuwepo kwa ushahidi wa maandishi, akiolojia haituwezeshi

kuonyesha mahusiano ya moja kwa moja kati ya ushahidi uliopo wa enzi ya chuma na dhana ya kiisimu ya neno 'Bantu'.

Majaribio mengi yamefanywa kuunganisha inafanikio ya makundi ya Wabantu na maarifa ya ufuaji chuma. Lakini imeonekana, kutokana na kulinganisha istilahi za maarifa ya ufuaji madimi katika lugha za Kibantu, kwamba kuna tofauti kubwa katika msamiati wa msingi wa uhunzi. Hata hivyo baadhi ya majengo yanaonyesha utumiaji wa chuma kwenye kiwango cha Bantu-asili kwa mfano maneno yenye maana ya ufuaji chuma, nyundo na mivukuto. Je, maneno haya yalikuwemo katika lugha ya mgawanyiko, au yaliingia katika lugha kutoka lugha nyingine kwenye kipindi fulani kisichojulikana wakati wa harakati za kuenea kwa lugha? Inawezekana kwamba yale maneno yaliyojiimarisha barabara yanatokana na insogeo wa maana kutoka lugha za Kibantu kabla ya kwenda kwenye lugha za kisasa. Hivyo, neno lenye maana ya 'fua' litakuwa ni matumizi maalumu tu ya ueno 'gonga' ('piga?'). Mwisho, istilahi nyinginezo za uhunzi zinaonekana kuwa na asili moja katika lugha za Kibantu na zisizo za Kibantu, jambo ambalo linaonyesha kwamba katika makundi yote mawili ya lugha kumetokea maneno yanayotokana na lugha nyingine.

Mtu afikiriapo jinsi uwezo wa kufua madini ulivyokuwa muhimu katika jamii za kimapokeo za Afrika, inakuwa vigumu kuona kwa nini hatupati dalili zozote za wazi za kiisimu iwapo 'Wabantu' walifua madini kabla ya kuenea kwao.

Mwisho, bado hakujaifanywa utafiti wa kutosha wa anthropolojia kuhusu 'Wabantu'. Makala yaliyoandikwa na J. Hiernaux (1968) ndiyo makala pekee yanayotoa taarifa chache za ukweli. Hiernaux anaonyesha ufanano wa kibioolojia baina ya watu wazungumzao Kibantu. Uchunguzi kidogo mno uneshafanywa katika uwanja huu wa palekontolojia ya binadamu kwa kiasi kwamba ni vigumu sana kutofautisha kiunzi cha mifupa kamili ya 'Wabantu' wa wakati huu na kile cha kundi jingine la Kiafrika, au hata la Ulaya. Tutasema nini basi juu ya viunzi mifupa vilivyoharibiwa au vile ambavyo ni vipandepande tu ambavyo mara nyingi ndivyo vinavyotolewa na akiolojia?

Mabaki pekee ya binadamu yaliyochunguzwa vizuri yanatoka Ishango, katika Hifadhi ya Virunga nchini Zaire. Kwa bahati mbaya umri wa mabaki haya hauwezi kukadiriwa barabara, na haikuwezekana kuyahusisha na aina yoyote halisi.

Hali za jamii wakati wa enzi ya chuma ya mwanzoni

Hakuna mengi yanayojulikana kuhusu aina ya inaisha ya mwanzoni mwa enzi ya chuma. Ushahidi uliopo unatofautiana kufuatana na kiwango cha uchunguzi uliokwishafanywa: maeneo yaliyoko Zambia na sehemu za mazishi za Sanga na Katoto, huko Shaba, yanatoa data zilizo madhubuti kabisa.

Mabaki ya makazi ni ya nadra katika Afrika ya Kati. Yanayojulikana ni yale tu ya Gombe, Maporomoko ya Kalambo na pengine Katongo.

Ushahidi pekee wa shughuli za kilimo za mwanzoni mwa enzi ya chuma,

unajumulisha majembe ya chuma yenye umbo linalofanana sana na majembe ya kisasa. Mashimo yaliyochimbwa ardhini yanafikiriwa yalitumiwa kuwa ni stoo, na majengo madogoinadogo ya kukandika yalikuwa ni ghala za nafaka. Ukweli kwamba kuna mabaki mengi ya mawe ya kusagia hakumfanyi mtu kusadiki sana, kwani jamii zilizoisishi kwa kuwinda na kukusanya chakula vilevile zilikuwa na zana za kusagia.

Uchumbuaji umeonyesha vipande vya mishale na mikuki, na mabaki ambayo lazima yalikuwa ya mbwa na kuwindia; vile vile mitego ya nyavu huenda ilitumiwa.

Umaarufu wa uvuvi umeonyeshwa na ndoana zilizopatikana kwenye makaburi ya Sanga na Katoto. *Trefoil braseros* (aina ya jamii za kunde) za Sanga zinafanana sana na zile zilizotumiwa katika mitumbwi yao na mabaharia wa sehemu za Ikweta za Zaire.

Tofauti lazima iwekwe kati ya aina mbili za biashara, biashara ya eneo moja tu hasa biashara ya metali, vyombo vya udongo, vikapu, samaki wa kukaushwa na chumvi, na biashara ya masafa marefu ambayo ilijishughulisha na makombe (kauri za konasi), shanga za kioo, na metali kama shaba. Nchini Zaire, katika sehemu za Sanga na Katoto, makombe na shanga zote zinatoka pwani ya mashariki, isipokuwa konasi tu huko Katoto zinatoka Bahari ya Atlantiki, umbali wa kama maili 900 ukienda moja kwa moja. Vijisalaba vidogovidogo vya shaba vilivyotumiwa kama sarafu, vimepatikana mbali sana kutoka kwenye maeneo yaliyokuwa yakitoa shaba.

Matanuu ya kuyeyushia chuma, pamoja na vyombo vya udongo vyenye vitako vilivyobonyea vimepatikana huko Kivu, Rwanda, Burundi na Buhaya katika Tanzania ya kaskazini magharibi. Ni muhimu kuonyesha kwamba katika maelezo pekee ya uyeuyushaji wa chuma nchini Rwanda, yaliyotolewa na Bourgeois (1957), duara la matofaili la kuchoma imetumika katika ujenzi wa tanuu ambalo linafanana kidogo na mabaki yaliyoonekana na Hiernaux na Maquet.

Mabaki ya vyombo vya udongo si ushahidi thabiti wa enzi ya chuma kwani, kama tulivyoona, vyombo vya udongo vinapatikana pia katika muktadha wa enzi ya mawe ya nyuma na Neolithiki. Kwa kawaida, haiwezekani kuvitofautisha vyombo vya udongo vya enzi ya chuma kutoka vile vya vipindi vya awali zaidi.

Magudilia yalitengenezwa kwa kuupigapiga na kuuvuta udongo wa mfinyanzi katika chane au nyugwe ambazo aghalabu zilipangwa katika niapande. Tofauti za sura na mapambo ni kubwa mno kiasi cha kwamba hapa tunaonyesha baadhi tu ya zile zilizokuwa za kawaida sana.

Kwa kadiri akiolojia inavyotuwezesha kuamua, jamii za enzi ya chuma ya mwanzoni hazikutofautiana sana na zile za sasa na zilionyesha aina inayofanana katika tofauti zilizokuwepo. Mbinu za kilimo zilizotumiwa wakati huo hazikufaa kwa uanzilishaji wa makazi makubwa, na zilisababisha hali fulani ya kuhamahama.

Maeneo ya mazishi ya Sanga na Katoto ni ya kipekee kwani ni inatokeo ya makazi ya kipindi kirefu sana au ya mkusanyiko mkubwa sana wa watu kwenye kingo ya mto Lualaba. Thamani ya vifaa vilivyomo katika baadhi ya makaburi, hasa huko Katoto, inaweza kuwa ni dalili za tofauti za kijamii.

Wingi na ustadi wa utengenezaji wa vifaa vya chuma, shaba, mawe, miti, mifupa na udongo wa mfinyanzi si kwamba unadhihirisha tu umahiri wa mafundistadi bali pia luenda ukawa unadhihirisha kiwango fulani cha ngawanyo wa ujuzi wa kazi.

Mukaburi yote yaliyovumbuliwa yanatoa ushahidi wa desturi za mazishi zinazoonekana vizuri kabisa. Maiti walivishwa mapambo mengi sana - vikuku, pete, mikufu, vipuli, nyugwe za shanga za mukombe. Kauri, konasi na shanga za kioo au mawe huenda zilituniwa, pamoja na mambo mengine, kuwa ni sarafu katika hali ileile kama ilivyokuwa kwa vijisalaba vidogovidogo. Mwisho, sanamu ya Afrika ya Kati yenye tarehe iliyo kongwe kuzidi zote inatoka Angola na ni ya mwaka +750.

Hitimisho

Mara kadhaa nimesisitiza hatari ya kutumia matokeo ya muda ya uchunguzi unatokana na sayansi moja ili yasaidie kufikia mahitimisho katika sayansi nyingine. Uhusiano wa harakaharaka mara nyingi unaleta nadharia za juujuu tu ambazo ni vigumu kuzidumisha iwapo zitaangaliwa katika muundo halisi wa taaluma zao maalumu. Hata hivyo, jaribio lolote la kueleza hali ya jamii za enzi ya chuma ya mwanzoni, au asili ya watu wazungumzao Kibantu, linahitaji ukusanyaji wa data za kiakiolojia na zisizo za kiakiolojia.


Ufafanuzi wa kiantropolojia □ kiakiolojia kiisimu uliohusisha kuenea kwa lugha za Kibantu na kuenea kwa ufuaji chuma ulililingana sana na wazo la mageuzi kutoka kwenye machimbuo yaliyoko katika eneo la *Fertile Crescent*, wakati huohuo ukikana kwamba Afrika ingeweza kuufikia ugunduzi huu yenyewe.

Maendeleo ya hivi karibuni yamezifanya nadharia hizi kufikiriwa upya. Wanaisimu wanazidadisi mbinu na matokeo ya glotokronolojia. Tarehe mpya zinatoa mwangaza mpya juu ya asili ya ufuaji chuma katika Afrika ya Kati. Mabaki ya ufuaji chuma kwenye eneo la Katuruka yamechunguzwa na kuonekana kuwa ni ya kipindi cha takribani mwaka -500 au -400.

Katika hali yetu ya kutojua mambo mengi, na tukitilia maanani ushahidi mpya, ni wazi kwamba matatizo yanayoambatana na ueneaji wa chuma na asili ya lugha za Kibantu ni changmani zaidi kuliko tulivyofikiria na hayawezi kufanywa mepesi bila kuzua mambo mengi yenye kupingana.

Kwa hiyo basi inaonekana hakuna maana kuendelea kutoa nadharia tote mpya kuhusu uhamaji na asili ya ufuaji chuma kila uchimbuaji unapotoa tarehe mpya. Hata hivyo tunaweza kujaribu kuhusisha nambo kadhaa yaliyo muhimu na yanayofaa. Kuhusu asili ya ufuaji chuma, tarehe mpya zilizopendekezwa kwa ajili ya Katuruka, zinaelekea kuonyesha uhusiano na tarehe za karibu kipindi kilekile cha tarehe zilizotolewa kwa Mezoe. Kwa hiyo inawezekana kufikiria kuwa ufuaji chuma ulionea kuelekea kusini kutoka Meroe, lakini katika hali hiyo ufuaji huo utaonekana kuwa ulionea kwa haraka sana. Hata hivyo sababu hii haitufanyi tufutilie mbali uwezekano wa kuwepo asili nyingine ambayo ingeweza kuwa ni ya mahali pale pale.

Kama msomaji atakavyokuwa ameona, thamani ya taarifa zetu kuhusu enzi ya



25.3 Vifaa vilivyopatikana Sangha: (a) Vyombo vyenye marembo ya kiantropomofia, sura kutoka juu na pembeni; (b) Vikuku vya pembe ya ndogu; (c) Mkufu wa shaba; (d) Firimbi ya chuma; (e) Kaunta ya udongo mwekundu wa mfinyanzi (f) kidani cha juwe; (g) kidani cha pembe ya ndovu; (h) nusu kipande cha mkufu wa pembe ya ndovu; (i, j, k) Aina za ufinyanzi (Maonyesho ya Tervuren: J. Hiernaux, E. De Bougrée na J. De Buyst, 1971)

chuma ya mwanzoni katika Afrika ya Kati hazilingani na wala hazikukamilika. Uchunguzi wa mwanzoni ulitoa nadharia ambazo sasa zinatetereka kutokana na mkusanyiko wa data mpya. Kazi kubwa zaidi, pana zaidi, na yenye utaratibu na mpangilio mzuri zaidi na iliyoratibiwa vyema - lazima ifanyike kabla hatujafikia ufafanuzi wa kuridhisha wa matukio ya kipindi hiki muhimu katika historia ya Afrika ya Kati.



26

*Kusini mwa Afrika:
wawindaji na wachumaji matunda*

Maoni ya Kamati ya Sayansi ya Kimataifa

Kamati ya Sayansi ya Kimataifa ingependelea kuwa sura hii, kama zilivyo sura nyingine, iwekwe katika utaratibu wa kronolojia ulivyopangwa maalumu kwa Juzuu la Pili. Hivyo Kamati iliinwomba mhariri wa Juzuu hili kumweleza jambo hili mwandishi wa sura hii. Hata hivyo mwandishi huyu hakuona uwezekano wa kufanya mabadiliko makubwa katika maandishi yake. Hivyo Kamati inaichapisha sura hii katika umbo lililokubaliwa baada ya majadiliano na mwandishi. Hata hivyo Kamati haina budi kuonyesha wasiwasi wake kulusu rubinu zilizotumiwa, hasa katika aya ya kwanza, na pia kuchanganyikana kwa habari inayotolewa wakati mmoja kuhusu zama za paleolithiki na za hivi sasa.

Utafiti wa hivi karibuni umeonyesha kwamba watu waliokuwa wanatumia chuma walikwisha kufika kusini mwa mto Limpopo katika karne ya nne au ya tano ya enzi za Ukristo. Ingawa maelezo mengi hayajachapishwa, inaonekana kamba watu walioishi enzi za chuma katika sehemu za Transvaal na Swaziland walikuwa wakulima na wafugaji, na walifinyanga vyungu ambavyo vilifanana na vile vilivyojulikanā kuwa vilitengenezwa Zimbabwe, Zambia na Malawi karibu wakati huo huo. Haijulikani kama mtawanyiko ambao ulionekana kama ulikuwa wa haraka wa watu hao wa enzi ya chuma ya mwanzo uliendelea kusini zaidi kwa kasi hiyo hiyo. Lakini tarehe za mwanzo kabisa za ufuaji chuma katika sehemu ya Natal ni za baadaye, yaani ni karibu na mwaka, wa 1050. Pia haijwezekana bado kutaja ni wakati gani ambao vikundi vilivyokuwa vikitumia chuma viliweza kuifikia sehemu ya kusini kabisa ya maeneo walioyafikia katika mtawanyiko wao, yaani sehemu ya mto Fish katika maeneo ya Mashariki ya Rasi. Ijapokuwa kuna shaka ambayo bila shaka itachunguzwa zaidi inafahamika kuwa watu waliokuwa wakitumia chuma waliwaingilia na kuwatawanya wenyeji wa sehemu zile ambao walijihusisha zaidi na uwindaji na ukusanyaji wa chakula msituni. Watu hawa kwa jumla hawakufahamu ufuaji chuma, ufugaji na ulimaji wa mimea ya chakula. Ni katika maeneo tu yasiyofaa kwa mkulima mfugaji k.v. miteremko iliyochoyongwa ya Drakensberg ndiimo

wawindaji waliweza kujinusuraisha na adhari za ueneaji wa watumiaji chuna wa hapo awali. Hata huku kurudi nyuma hakukuleta mafanikio hasa kwa wakati huu ambapo ardhi inaendelea kuchukuliwa.

Mtawanyiko wa pili, ambao kwa namna nyingi ulileta madhara, ulianza katika Rasi mnamo katikati ya karne ya kumi na sita. Wenyeji wa sehemu zile ama walihama kwenda kafanya kazi ya utumishi katika koloni ambalo lilikuwa likiongezeka ukubwa, au walikufa kwa magonjwa yaliyoletwa na hao wakoloni. Wenyeji wa sehemu hii waliitwa kwa jumla jina la "Ottentoo" au "Hottentot". Lakini polepole upambanuzi uliweza kufanywa kati ya wafugaji (Walkhoikhoi ambao majina yao mengi ya kikabila yalikuwa yanajulikana) na wawindaji (wale Watukoko au *Bosjesmen*, ambao pia walijulikana kwa jina la Sonqua Khoikhoi). Ni dhahiri kuwa vikundi hivi vilikuwa na uhusiano wa karibu kwa vile waliongea lugha zilizofanana, walitumia aina moja ya teknolojia ya maisha na utamaduni. Kadhalika, walifanana sana katika sura na maumbile yao. Kwa vile vitu hivi viliwafanya wawe tofauti na wenyeji wengine, hasa wale wakulima waliokuwa wakitumia chuma sehemu za kaskazini na mashariki, walifikiriwa kama watu wa namna ya pekee. Hivi sasa wanajulikana kama wafugaji wa *Kikhoikhoi* na wawindaji wa *Kisan*. Majina haya mara nyingi huunganishwa ili kuunda jina *Khoisan*.

Inaonekana kuwa haiwezekani kabisa katika hali hii kujiwekea mipaka wa kronolojia kama ilivyopangwa katika juzuu hili. Hata hivyo inwandishi amejaribu kueleza mambo fulani fulani ya hali thabiti ya maisha. Amewaachia waandishi wa Majuzuu mengine yanayohusika na maeneo haya kuelezea inabadiliko ambayo yametokea katika maisha ya watu hawa katika karne zilizopita, kutokana na uhusiano wao na watu wa nchi za mbali. Vile vile waandishi hawa wataangalia mchango wa hao wageni katika historia ya kusini mwa Afrika kwa jumla. Hii itapunguza haja ya kurudia rudia mambo.

Wakhoisani

Sura hii itaeleza mambo yote yanayojulikana katika maisha wa wawindaji na wafugaji ambao walijikuta wamebanwa katika ya wukulima wanaotumia chuma na Wakoloni wa kizungu katika sehemu za kusini mwa Afrika. Kwa vile wakoloni walijua kusoma na kuandika na hao wakulima waliokuwa wanatunika chuma hawukujua maandishi kuhusu maisha ya jadi ya San na Khoi Khoi na uhusiano wao na vikundi vingine yameandikwa kwa kupendelea zaidi sehemu ya magharibi ya Rasi. Kwa namna fulani, upendeleo huu umefanywa kuwa mkubwa zaidi kutokana na uvunbizi mkubwa wa akiolojia katika ukanda wa milima ya Rasi ukilinganishwa na sehemu nyingine nyingi za kusini mwa Afrika. Hata hivyo maelezo yatakatolewa, ingawa mara nyingi yatahusu pande za kusini na magharibi, yataeleza namna walivyoishi Khoi Khoi na San katika eneo lote. Ni dhahiri kwamba maelezo mengi ya hali za kila sehemu hayawezi kupatikana.

Kwa sababu mbalimbali kuna ushahidi mwingi wa kuweza kutufahamisha jinsi

vikundi vya Khoisan vilivyoishi. Kwa kuwa waliweza kubakia mpaka nyakati hizi za karibuni, kungekuwa na ushahidi mwingi wa kiakiolojia hasa katika mabaki ya vitu, wanyama na mimea. Kwa kuwa watu hawa walipata kuwa na uhusiano na jamii zilizojua kusoma na kuandika, kuna maandishi mengi ya kihistoria kuhusu maisha yao ya jadi. Aidha, baadhi ya vikundi vya kienyeji vimeacha kumbakumbu zake katika picha zilizochorwa au kuchongwa miambani ambazo zinatupa maelezo mengi kuhusu maisha yao ya kijamii, kiuchumi kiteknolojia na hata kidini. Kitu muhimu ni kwamba mazingira katika sehemu nyingi za kusini mwa Afrika hayajabadilika sana tangu yalipokaliwa awali na wawindaji na wafugaji. Baada ya miaka 250 ya shughuli za kilimo, bado inawezekana kuweka kumbukumbu na kufuatilia mambo mengi yanayohusu sababu mbalinubali katika mazingira ambayo kwa namna fulani yaliukilia hali ya makazi katika kipindi kabla ya historia.

Kwa vile wachungaji wa Kikhoikhoi na wawindaji wa Kisan wote hawakutumia vyombo vya metali vya kukata, kuparuzi au kuchanja, wanapaswa kuchunguzwa kama watu wa enzi za mawe. Na mara nyingi wametazamwa kulingana na ala za mawe walizotengeneza.

Wawindaji na Wakusanyaji wa Kisan

Uchunguzi wa hivi karibuni wa mila na desturi za wawindaji na wakusanyaji umeonyesha umuhimu wa vitu vilivyokusanywa au kuokotwa kama sehemu ya chakula cha vikundi vinavyohusika katika aina hii ya uchumi. Ni wazi kutokana na maelezo ya Kung na G/wi wa Kalahari kwamba vyakula vilivyokusanywa na wanawake vilitosheleza malitaji yao ya kila siku ingawaje wanaume na watoto pia walikusanya chakula porini kilichoitwa *veldkos*-. Umuhimu wa chukula kinachokusanywa, ambacho sehemu yake kubwa huwa mbogani kwamba kina uhakika wa kupatikana katika sehemu fulani maalumu na kinaweza kutegemewa kukidhi mahitaji ya siku hadi siku. Nyama ambayo ina protini nyingi hupatikana kutokana na wanyama wawindwao au kutegwa na wanaume. Ingawa nyama hii ni muhimu, huwa hakuna uhakiki wa kupatikana kwake. Hivyo haichukuliwi kama chakula cha kawaida cha kila siku. Hii haina maana kwamba wawindaji waanze kuitwa wakusanyaji chakula mwtu, ila ni kwamba shughuli za uwindaji au ukusanyaji wa chakula hutegemea sana aina ya mazingira na vyakula au mawindo yaliyoko. Vikundi kama hivi huweza kuishi kwa chakula kilichokusanywa, lakini pia hunufaika mara chache chache na chakula kinachotokana na mawindo.

Kwa kawaida, karibu maelezo yote ya kihistoria kuhusu wanyama waliotumiwa kama kitoweo na watu wa kale hutaja neno "mawindo". Hii ina maana kuwa aina nyingi sana za wanyama ziliwindwa. Hii imethibitishwa na idadi kubwa ya wanyama waliochimbuliwa katika sehemu kama vile Die Kelders na Nelson Bay Cave, ambapo kuna masalio ya wanyama wengi, kuanzia panya wadogo hadi kufikia tembo, na hata nyangumi. Lakini wanyama walioko katika sehemu hizi zaidi ni wale wanyama wadogo wadogo kama vile kobe, dazi, fuko, panya na wanyama wadogo wa ardhini

wanaokula majani kama vile dondoro na wengine wa namna ile. Mifupa ya wanyama wanaoishi kwa kula nyama hutokea kwa nadra. Hii inaweza kuwa na maana kwamba wanyama wa namna ile waliwindwa tu ili kupata ngozi. Wanyama wakubwa wanaoishi kwa kula majani kama vile kongoni, pofu na kifaru huonekana mara chache zaidi kuliko wale wanyama wadogo wadogo. Vile vile kuna dalili chache sana za wanyama kama vile tembo, kiboko na nyati. Ingawa idadi ya hao wanyama inaonyesha kuwa wawindaji walipendelea zaidi kuwaleta wanyama wadogo wadogo maskani kwao na kuwachinja wanyama wakubwa mahali pa mawindo, ni dhahiri kuwa wanyama wa ardhini na wale wadogo wanaoishi kwa kula majani ndio walipendelewa zaidi katika mawindo.

Kwa hivyo chakula cha vikundi vya San kimeelezewa sana katika nyaraka za historia na za kiakiolojia, ingawa mtawanyiko wa machimbo ya maumbo ya kale haufanani. Kuna sehemu ambazo bado hazijafanyiwa uchunguzi au hazina mambo yoyote ya kale yaliyohifadhiwa vizuri. Kwa kawaida, chakula cha kila siku kilikuwa kile kilichokusanywa. Hii ilikuwa ni pamoja na vyakula vya mizizi, vyakula vingine vya mimea, asali na wadudu kama vile nzige, panzi, mchwa na viwavi. Vile vile kulikuwa na wanyama wanaoishi kwa kula majani na mara chache kulikuwa na wanyama wakubwa pia. Vikundi vilivyokuwa kando ya baliari vilivua samaki, kamba wa miambani, wanyama na ndege wa baharini. Pia walikusanya kiasi kikubwa cha chaza, hasa koa na kome.

Teknolojia iliyotumiwa kupatia chakula hiki inajidhihirisha katika aina ya mawe, mifupa, miti na kamba ambazo zimeonekana katika mapango na mahali walikoishi katika maeneo yote ya kusini mwa Afrika. Vile vile habari zimeweza kupatikana katika maelezo ya wasafiri wa hapo mwanzoni katika sehemu hizi. Kuna michoro mingi kwenye miamba ambayo inaonyesha wanawake wakiwa na fimbo zilizowekewa uzito walizotumia kuchimbia (Angalia picha 26.1). Mara nyingi wanawake hawa huonekana wamebeba mifuko ya ngozi bila shaka kwa ajili ya kubebea vyakula nyumbani. Utengenezaji wa vitu vya ngozi, umeenea zaidi katika sehemu kavu za maskani ya miambani na mapangoni katika maeneo ya Rasi.

Karibu watu wote waliozungumzia kuhusu wawindaji wa Kisan wamegusia sana upinde na mishale yenye sumu kama silaha muhimu zilizotumika zamani. Ingawa ni vigumu kupata mabaki ya kila kifaa kilicho kamili katika machimbo, kuna nufano ya sehemu zote za vifaa hivi katika mapango ya magharibi na mashariki ya Rasi. Vitu vilivyopatikana hadi sasa kati ya mabaki hayo ya vikundi vya mawindaji wa San ni selemu za pinde, matete ya kutengenezea mishale, ncha zilizochongwa na mifupa, mishipa iliyowekewa mafundo, na misubili iliyopakwa rangi. Hata hivyo, wanyama wengi hawakuuliwa kwa upinde, ila walinaswa na mitego iliyotengenezwa kwa kaniba za mimea, na kutawanywa katika mbuga. Mbinu nyingine za kuwinda zimetajwa katika maelezo ya kihistoria, lakini hazijathibitishwa na ushahidi wa kiakiolojia. Kwa nufano, wasafiri wengi katika karne ya kumi na nane walieleza juu ya mashimo mengi anibayo yalikuwa yamechimbwa karibu na kingo za inito, yakiwa na nguzo

26.1 Michoro ya kwenye miamba:
Wanawake wakiwa na fimbo za
kuchumbia zilizotengenezwa kwa
mawe laini



26.2 Michoro ya kwenye miamba:
Kundi kubwa la watu, wengi wao
wakitambulika kama wanaume, wakiwa
wamechorwa wakiwa wanacheza dansi.
(J.E. Parkington)



zilizochongoka zilizosimikwa ndani yake. Inadhaniwa kuwa mashimo haya yalichimbwa ili kuwaua wanyama wakubwa kama vile tembo, vifaru, viboko na nyati.

Inadhaniwa pia k uwa mashimo haya yalikuwa yameenea sehemu kubwa kutoka kusimi mwa Mto Orange hadi mashariki kufikia Gamtoos.

Ni dhahiri kuwa mbinu nyingi za uvuvi zilitumiwa na wawindaji na wakusanyaji. Nyingi ya mbinu hizi zimo katika maandishi. Labda mbinu ambazo zinastaajabisha zaidi ni zile za kutumia madema. Mitego hii imeonekana hasa katika sehemu za chimi za Mto Orange na imelezwa katika maandishi ya Lichtenstein na Borrow kama mbinu za Wabosjesman ambao, bila shaka, walikuwa Wasan. Mitego hii iliwekwa katika mito na inasekema kubwa ilitengenezwa kwa fito, matawi ya miti na mianzi iliyochongwa au kuwekwa katika umbo la dohani ambayo, bila shaka, inafanana na ile inayotumiwa hivi sasa katika maeneo ya mito Kafue na Limpopo. Ingawa hakuna dalili za mitego hii katika vitu vya kale vilivyochimbuliwa, michoro mingi ya miambani iliyoko Lesotho na Mashariki ya Griqualand inabainisha aina ya mitego hii ambayo iliunganishwa na inatete au maboma ya miti na kuweza kushika samaki wengi wa maji matamu.

Hivyo teknolojia ya San ilijidhihirisha zaidi katika mbinu za kuwinda na kukusanya kwa kutumia vitu kama vile mawe, mifupa, miti, kamba, matete, ngozi, simbi, pembe za ndovu, kano na inajani. Aidha, mara nyingi vitu vingi vilitunika katika kuunda ala moja. Mawe yalitumika tu kuchongea ncha, kukatia au kuparua ncha za ala zenye kuhitaji ufundi mkubwa. Mara nyingi, vyombo vyenye ncha ya mawe viliwekwa mipini ya miti au ya mifupa. Mawe yaliyotumika zaidi ni yale yenye chembe laini na yaliyokaa sawasawa kama vile chalisidoni, ageti, silkriti au sleti ngunu. Vile vile mawe magumu ya kung'aa yalitumiwa pia. Mbwe zinazong'aa, majabali vilitumiwa kama mawe ya kusagia rangi na nafaka. Inastaajabisha kuona kuwa wasafiri wachache tu wa karne ya kumi na saba na kumi na nane wameeleza au kutaja utengenezaji wa ala za mawe. Labda walitaka kuonyesha jinsi baadhi ya ala za mawe zilivyobadilishwa ua badala yake kutumia mifupa, miti na chuma. Hii ina maana kuwa mali ghafi nyingi zilitumiwa katika shughuli hizi, na hivyo inawezekana kuvitofautisha hivyo vikundi kwa kulinganisha namna ya matumizi ya mawe peke yake.

Uchunguzi wa kiakiolojia unaelekea sana kuchunguza hali ya maisha ya vikundi vya San katika makao yake. Matokco ya uchunguzi huu ni kwamba sasa tunaweza kueleza mahitaji ya wawindaji na wakusanyaji yalikuwa ya aina gani kufuatana na mazingira yao ambayo wasafiri wa mwanzo hawakiyafahamu. Hata hivyo, kumbukumbu za kihistoria na taarifa kutokana na michoro ya miambani vinaweza kutudhihirishia zaidi habari zinazojitokeza kutokana na uchimbuaji unaofanyika sasa kwa wingi pamoja na uchambuzi mkubwa wa mifupa ya wanyama na masalio ya mimea.

Ukiwaliganisha na wawindaji na wakusanyaji wa Kalahari na wale wa mbali zaidi inaonekana kuwa pengine vikundi vya San vilikuwa vidogo na vyenye kuhamahama

sana. Ila tu makundi ambayo yalikuwa makubwa ni kama yale ya watu kati ya 150 na 500 yaliyotolewa mfano na Barrow na yale yaliyotajwa na Thunbarg yaliyokuwa na kambi ya vibanda hamsini.

Makundi haya yalionekana mwishoni mwa karne ya kumi na nane wakati ambao wawindaji walikuwa wakijikusanya kwa wingi sana ili waweze kujihami dhidi ya magaidi wa Kizungu, ambao michoro ya miambani inaelekea kuthibitisha kwamba vikundi vingi vya kijamii vilikuwa na watu wasiozidi ishirini kila kimoja, ingawa vikundi vikubwa zaidi kuliko hivyo pia vilionekana. Kuna ushahidi mkubwa kuhusu uhusiano kati ya wanawake na fimbo za kulimia, na kati ya wanaume na pinde katika michoro ya miambani. Hii inaonyesha kuwa kulikuwa na mgawanyo wa kazi katika vikundi ya San.

Mara nyingi imekwishaonekana kwamba vikundi vya wawindaji na wakusanyaji vilikuwa vikisafiri katika vikundi vikubwa mbali mbali ili kuongeza ufanisi wa matumizi ya mali waliyonayo. Mara nyingi vikundi hujigawa katika jamii ndogo ndogo iwapo mali ni kidogo, na kuungana tena katika vikundi vikubwa ikiwa mali iliyopo inahitaji nguvu za watu wengi wote wakusanyike sehenu moja. Maisha ya namna hii vile vile husaidia kudumisha uhusiano wa kidugu kati ya vikundi vya jirani ambavyo hutumia fursa za mikusanyiko mikubwa kuweza kupeana habari, kubadilishana vitu, teknolojia inpya na hata wanawake, kufuatana na mila. Wakati baa linapotokca, kuna masharti ambayo lazima yafuatwe kama vile kukiruhusu kikundi kingine kwa muda ili kuweza kujinasua kwenye matatizo. Kadhalika, matatizo ya biuafsi yanaweza kutatuliwa na kikundi kimoja au kingine kwa kuacha kikundi kimoja na kijiunga ama kwa muda au kwa kudumu na kikundi kimoja walimokuwemo jamaa zao. Ingawa utambuzi wa mambo haya ni zaidi taarifa muhimu tuliyonayo kwa wakati huu inatokana na kumbukumbu za kihistoria na labda kwa namna fulani, kutokana na michoro ya miambani.

Uchunguzi mmoja wa ukubwa wa vikundi kama ilivyoonyeshwa katika michoro ya miambani katika sehemu za inagharibi ya Rasi ulionyesha idadi ndogo sana ya watu hawa ambao walikuwa ni kumi na wanne tu katika kikundi kimoja. Idadi hii ilifanana sana na ile iliyomo katika kumbukumbu za magaidi mwishoni mwa karne ya kumi na nane. Hata hivyo, kuna mifano ya michoro ya miambani ambayo inaonyesha watu wanaofikia thelathini au arubaini, ambayo inamaanisha kuwa mikusanyiko kama hiyo ilikuwa ya watu wanaopata mia moja au zaidi (angalia kielelezo 25.5).

Uwekaji akiba ya nafaka wakati wa neema kwa ajili ya wakati wa njaa si jambo la kawaida kwa vikundi vya Kalahari vya sasa, kwani watu hawa waliyaona mazingira kama dhala ya asili ambayo kila mara inatoa mchanganyiko fulani wa chakula kisichohitaji kuongezwa. Inaonekana kuwa hapakuwa na ulazima wa kuhifadhi chakula baada ya kupanga vizuri mawindo ya mwaka mzima katika sehemu zinazofaa na kwa kutunia kwa uangalifu chakula kinachopatikana kwa wingi ili kifae wakati wa njaa. Chakula kilikusanywa na kuliwa siku hiyo hiyo, au kwa muda wa siku chache, hasa kama chakula kilichopatikana ni kingi kuliko kawaida kama vilc


mnyama mkubwa. Hali katika sehemu za kusini inaonekana ilifanana na hiyo kwa sababu katika kumbukumbu za akiolojia hakuna dalili kubwa ya kuonyesha ya kuwa nafaka ilihifadhiwa katika mashimo. Kadhalika, wasafiri wa mwanzo hawakueleza kuwa hifadhi ya chakula ilikuwa kama sehemu muhimu ya maisha ya Wasan. Kufuatana na maandishi ya Kolb, ambaye alikuwa na taarifa kutoka kwa watu wengi walioshuhudia maisha ya Wakhoikhoi na San mwishoni mwa karne ya kumi na saba, inaelekea kwamba “ingawa mashama yamejaa matunda na vyakula vya mizizi ambavyo wangeweza kuvihitaji wakati wa neema na kuvitumia wakati wa njaa, ni desturi ya wanawake kukusanya tu kiasi kile ambacho kingewatosheleza jamii zao kwa siku ile”. Waandishi wengine wa hapo awali wametaja hifadhi ya panzi waliokaushwa, mizizi iliyotwangwa ya mimea ya kana na aprikoti zilizokaushwa. Inaonekana kuwa vitu hivi havikuwa na umuhimu mkubwa kiuchumi kama ilivyo mizizi, mihogo na mahindi. Katika sehemu za kusini mwa Rasi, kuna ushahidi ambao bado haujachapishwa kwamba kulikuwa na mashimo makubwa ya kuhifadhi nafaka katika sehemu za mapango yaliyokaliwa na Wasan. Taarifa ambazo bado hazijathibitishwa zinataja kuwa mbegu ambazo zimegunduliwa katika mashimo hayo huenda zilikusanywa kwa ajili ya mafuta na siyo kwa ajili ya chakula.

Kutokana na ushahidi uliotolewa ni dhahiri kuwa vikundi vya Wasan vilikuwa vikundi vyenye kuhamahama ambavyo vilielewa sana mali asili ilivyobadilika kulingana na wakati na mahali. Kwa kutumia data mbali mbaali kutoka katika kumbukumbu tofauti, maandishi zaidi yanachapishwa kuhusu chakula cha msingi, aina za mawindo, uvuvi na mbinu za kukusanya chakula mwituni.

Wachungaji wa Kjikhoi Khoi

Picha ya uwindaji na ukusanyaji katika mazingira yaliyoainishwa haiwezi kuwa kamili, hususa katika kuelezea kipindi cha kabla ya ukoloni, kama vile tangu mwaka B2000. Katika kila sehemu ya makazi iliyoonyeshwa katika kielelezo 26.7 isipokuwa Bonteberg na Gordon Bay (ambako bado hayajatafutwa sana), kuna mabaki ya mifugo ambayo hali yake inaonyesha kuwa ni ya zama za baadaye za utumiaji mawe. Kwa vile hakuna kondoo, mbuzi au ng'ombe wa kienyeji, na kwa vile mikusanyiko hii ilifanyika kabla ya kufika kwa Wazungu au Wachungaji wa Kinegro, lazima tuchukulie kwainba kumbukumbu hizi zinaonyesha kuwa mifugo hii imetokea sehemu nyingine. Kufuatana na kipimo cha redio-kaboni, tarehe za mwanzoni kabisa za kuwepo kwa mifugo na vigae katika makazi ya zamani kutoka Angola hadi Mashariki ya Rasi zimeonyeshwa katika kielelezo 26.8. Pia tuna taarifa chache kuhusu vitu hivi kutoka sehemu za ndani ya bara na pia tarehe za mwanzoni za watu waliokuwa wakitumia chuma, kupenya kusini mwa Afrika wakiongea lugha za Kibantu na wakiwa wakulima na wafugaji. Ingawa mambo mengi yatabadilika baada ya uchunguzi zaidi ni vizuri kujaribu kutoa maelezo kuhusu asili na lugha ya wachungani wa Kikhoikhoi.


KUWEPO KWA VYUNGU NA MFUGO ENZI YA MAWE
YA BAADAYE KUSINI MWA AFRIKA



Hali ya sasa

- Uhusiano mzuri wa mwanzo karne ya 14 na vungu
- Uhusiano wa wasiwasi karne ya 14 na vungu au tarehe za kabla ya vungu
- Uhusiano mzuri wa mwanzo na mifugo
- Uhusiano usio na mashaka kabla ya vungu LSA

26.4 Tarehe za mapema ambazo zipo kwa ajili ya vungu na mifugo kwenye Enzi ya Mawe ya baadaye Kusini nwa Afrika



26.3 Kusini mwa Afrika, ikionyesha maeneo ya Enzi ya Mawe ya Baadaye, nyingi ya sehemu hizi ikionyesha mifugo katika karne ya kwanza ya Enzi ya Kikristo.

Jambo linalodhihirika ni kwamba, vigae vilianza kuonekana kwa mara ya kwanza katika makazi ya zamani kutoka Angola hadi kusini mwa Rasi katika kipindi cha -2000 hadi -1600. Jinsi vigae zaidi vinavyoendelea kupatikana ndivyo itakavyowezekana kujua tarehe zake kwa usahihi zaidi. Inawezekana pia kwamba matumizi ya redio-kaboni yataonyesha tarehe zinazofanana kwa vitu vitakavyopatikana katika eneo lote. Kuna tarehe nne tu kabla ya -2000 ambazo zimegunduliwa hadi sasa, na kuna sababu za kufikiri kuwa tarehe hizi zote zinapotoshwa sana au ni za wakati kabla ya kufinyanga vyungu katika eneo hilo.

Jambo la pili ambalo pia ni la muhimu kuzingatia ni kwamba, kila mara uchunguzi wa dalili za mifugo unapofanywa, inaonekana kwamba mifugo imekuwepo wakati sawia na vigae kufuatana na kumbukumbu za kiakiolojia. Inawezekana tarehe za maeneo jirani zinapekwa pamoja ili kuwa na mpangilio mmoja wa mahali pale ambapo vitu hivi hujitokeza kwa wakati mmoja. Ingawa njia hii inawezekana isionekane kuwa ni ya haki, lakini inaweza kutetewa kwa kuwa inaepuka matatizo yanayosababishwa na mbinu za kutumia sampuli. Hii ina maana kwamba vigae na mifugo vilienea haraka, kwa wakati mmoja na katika maeneo yale yale. Neno "vilienea" haliwezi kuepukika kwa vile ingawa ujuzi wa ufinyanzi ungeweza kuvumbuliwa bila vitu vingine kuhusishwa, hilo haliwezi kufanyika kwa ufugaji wa mifugo. Kadhalika ufinyanzi wa vyungu hauonyeshi alama za kuwa vimebanwa au kuwa hafifu kwa kuwa teknolojia hiyo ndiyo kwanza ilikuwa imeanzishwa.

Ingawa uchunguzi ungali unaendelea wa kuona namna chuma na mifugo vilivyoenea kusini mwa Afrika kupitia njia ya mashariki, ushahidi wa hivi sasa unaonyesha kuwa vitu hivi viliingizwa katika sehenu ya kusini ya mto Limpopo mnamo karne ya nne au tano. Hivyo tarehe za baadaye za utumiaji wa mawe za kuhusiana na ufinyanzi wa vyungu na ufugaji ni za zamani zaidi kuliko zile za utumiaji vyuma na katika sehemu za kaskazini na mashariki ni zaidi ya miaka mia mbili hadi mia tatu. Muda huu hauwezi kuelezeka kwa vipimo vya redio-kaboni.

Maelezo haya juu ya mazingira, utawanyikaji na kronolojia yanaonyesha kuwa wafugaji fulani, ambao pia walikuwa wafinyanzi, walitawanyika haraka katika sehemu za kusini mwa Rasi kwa kutumia njia ya pwani ya magharibi kando ya bahari takribani mwaka -2000. Bila shaka vikundi vya wawindaji vilichanganyika na vikundi vya wafugaji hawa, na bila shaka palikuwa na mabadiliko makubwa ya idadi ya watu na uchumi wao, ingawa mambo haya hayajaandikwa sana. Inaonekana kuwa wadukizi hawa walikuwa ni wafugaji wa KikhoikKhoi.

Bila shaka, ni jambo la kupendeza kujaribu kufikiria asili, sababu na madhumuni ya kujidukiza huku. Lakini, kwa vile tuna data kidogo, kufikiria kwenyewe lazima kuwe kudogo sana. Uchunguzi uliofanyika Zambia na Zimbabwe umcjugawa katika enzi ya chuma na enzi ya mawe. Matokeo yake ni kwamba sehemu ya juu katika mapango, makao ya ndani ya zamani au makao ya wazi yenye vyungu, yamefikiriwa kuwa ni ya enzi ya mawe iliyoingiliwa na enzi ya chuma. Ni dlahiri kwamba katika sehemu hizi, inawezekana kuwa palikuwa na vikundi vilivyokuwa na utaalumu wa

mawe, lakini uchumi wao ukiwa unajumlisha ufugaji na ufinyanzi vyungu tofauti na vile vya wakulima ambao walikuwa tayari wanatumia chuma. Katika Zimbabwe, vyungu vinavyojulikana kama Bembata vinahesabiwa kuwa tofauti na vile vya watumiaji chuma na mara nyingi viligunduliwa pamoja na "Wilton" yaani, ala za mawe za kipindi cha mwisho cha enzi ya mawe. Bado haijulikani vizuri kama hii ilimaanisha kutawanyika kwa wafugaji kabla ya enzi ya chuma au la. Hata hivyo, ushuhuda wa mawazo haya unaweza kupatikana katika ueneaji wa michoro ya kondoo wenye mikia minene kutoka Ziombabwe. Kondoo hao wanaaminika kuwa walihusiana na wakati wa utumiaji chuma, nao walikuwa kondoo waliokuwa wakichungwa na Wakhoikhoi, katika sehemu za Rasi, katika karne ya kumi na tano, kumi na sita na kumi na saba za baada ya Enzi ya Kikirsto.

Iwapo mtawanyiko wa vikundi vilivyokuwa vikitunika mawe na kuchunga kondoo katika sehemu za Zimbabwe na Zambia utakubalika, basi kuna uwezekano kuwa vikundi hivi vilitoka Afrika Mashariki, maana kuna mfanano wa utamaduni lugha na hata wakibiolojia. Kuwapo kwa wachungaji ambao pia walifinyanga vyungu vyenye vishikio kubakia kwa lugha zenye vidoko kama vile Kihatsa na Kisandawe na madai kwamba vikundi vya Wahottentot vina asili ya Kihamitiki. Vyote hivi vimetumiwa katika nyakati mbalimbali kuonyesha kuwa wachungaji hawa wa kusini mwa Afrika wasiotumia chuma wana asili ya kaskazini-mashariki. Ingawa uhusiano huu haujathibitika, na katika hali nyingine umekataliwa, mfululizo wa alama kama vifinyange, ufugaji wa kondoo, aina za kondoo na ng'ombe, tekuolojia isiyotumia chuma, ala za mawe, na hata lugha, ikiwa vitalakikishwa vitaweza kutupa sababu kubwa za kuamini kuwa asili halisi ya Wakhoikhoi ni Afrika ya Mashariki. Hii pia ingemaanisha kuwa mifarakano iliyosababisha kuhama kwa wingi kwa watu waliokuwa wakiongea lugha za Kibantu kutoka mashariki kuelekea kusini, ndiyo inawezekana ilisababisha uhamaji wa kuelekea magharibi; na yawezekana hata kuelekea upande wa Rasi. Kutokuwapo kwa vyungu vya aina ya Wakhottentot au vya mwambao na Rasi katika sehemu za Transvaal, Swaziland, Natal, Orange Free State, au Transkei kunaweza kumaanisha kwantha ukulima ndio ulikuwa kitu bora zaidi katika maeneo haya ambayo yana maji mengi wakati wa mvua na kiangazi. Aidha, wachungaji ambao hawakulima mazao yoyote na wenye kuhamahama sana wangeweza tu kutawanyika kupitia sehemu kavu za Namibia na kaskazini mwa Rasi hadi kufikia sehemu za malisho za magharibi za kusini mwa Rasi.


Inaonekana kuwa kondoo waliletwa kupitia njia ya magharibi, lakini ng'ombe waliwafikia wachungaji wa Kikhoikhoi kutoka mashariki, kwa Wabantu ainbao wakati huu walikuwa wakikaa katika sehemu za Transkei. Ushahidi wa maelezo haya unadhihirishwa na michoro mingi inayofikiriwa kuwa ya mwishoni mwa enzi ya mawe ya kondoo wenye mikia minene katika sehemu za magharibi ya Rasi. Lakini hapakuwepo na michoro kama hiyo ya ng'ombe, ingawa ng'ombe, walikuwa wakichorwa kwenye miamba katika sehemu zinazokaliwa sana na Wabantu. Aidha, kuwepo kwa mifupa ya ng'ombe wakati sawa na mifupa ya kondoo katika machimo

ya mwishoni mwa enzi ya mawe kusini mwa Rasi bado hakujarekodiwa katika maandishi.

Hivyo kuna sababu zinazotufanya tufikiri kwamba wafugaji kondoo waliokuwa wamehusiana na wawindaji waliotumia mawe, na ambao walitofautiana kimaumbile na wazungumzaji wa lugha za Kibantu, walipokwishapokea mifugo na vyungu kutoka kwa majirani wa Afrika Mashariki walihama kuelekea magharibi na baadaye kuelekea kusini wakiwa wanatafuta malisho. Hatimaye walifika Rasi baada tu ya miaka -2000. Watu hawa huenda walichanganyika na wawindaji waliokuwa sehemu hizi au kupigana nao, au kustahimili kuishi nao. Baadaye walikutana na kuhusiana na Wabantu katika eneo ambalo sasa linajulikana kama Transkei. Mtawanyiko mdogo wa vyungu, ala zilizochongwa za mawe na mifupa ya wanyama katika njia iliyoelezwa hapo juu inaweza kumaanisha kuwa walikuwa wanahamama sana. Kwa hiyo, mabaki waliyoacha yalikuwa kidogo mno kuweza kuonekana kwa wanaakiolojia kwa urahisi.

Hakuna ushahidi unaonyesha kuwa Wakhoikhoi wa Rasi walikuwa wamezoea kutumia chuma kabla ya kufika kwa walowezi wa Kizungu. Hata hivyo Wanamakua waliweza kutengeneza shanga na sahani za shaba katika karne ya kumi na saba.

Uhusiano kati ya Wasan, Wakhoikhoi na vikundi vingine kama vile wakoloni waliohamia sehemu hizo au wakulimawaliokuwa wakitumia chuma, ulitofautiana sana kama ulivyokuwa kati ya Wasan na Wakhoikhoi. Katika sehemu ya magharibi Wasan na Wakhoikhoi walifukuzwa kutoka katika ardhi yao na kuangamizwa au kumezwa katika jamii ya wakoloni. Idadi fulani ya miambani katika magharibi ya Rasi inaonyesha magari yaliyofunikwa, watu wenye farasi na silaha za wakulima wanaolama. Katika sehemu ya mashariki ugomvi kati ya wakulima wa enzi ya chuma na wawindaji haakuandikwa sana. Hata hivyo michoro ya miambani inaonyesha ng'ombe. Katika michoro hii watu wafupi wenye pinde wanaonekana wakiwaibia ng'ombe watu warefu waliokuwa wameshika mikuki na ngao. Uhusiano wa baadaye kati ya watu hawa umeandikwa baada ya wakoloni, ambao walijua kusoma na kuandika, kuhamia Natal na kwenye mitereniko ya milima ya Draakensberg. Wafugaji wa Kikhoikhoi labda kwa vile walikuwa na mambo mengi yanayofanana na Wabantu ambao walikuwa wakulima na wafugaji, waliweza kuwa na uhusiano mzuri na watu kama vile Wahosa na Watswana. Maelezo kuhusu Wagonakua yaliyoandikwa na Le Vaillant yanaonyesha kuwa ulikuwapo uwiano mkubwa wa kihistoria kati yao na jirani zao Wahosa ambao waliweza hata kuoana. Inaonekana kuwa ni kosa kubwa kufikiri kuwa kuna tofauti kubwa ya kiuchumi, kilugha, kimaumbile na kitamaduni kati ya vikundi mbalimbali vya kale kusini mwa Afrika. Kitu ambacho pengine hakiwezekani kuwa kweli zaidi ni kule kufikiria kuwa tofauti hizi zingaliweza kufanana kiasi hicho.



*Mwanzo wa
Enzi za Chuma
kusini mwa Afrika*

Tukio la kitamaduni, Kusini mwa Afrika, linalojuliana kwa wanahistoria kuwa ni mwanzo wa nyakati za utumiaji chuma, limeweza kuleta katika eneo hili namna ya maisha ambayo ni tofauti kabisa na yale ya awali. Mabadiliko hayo ndiyo yaliyoleta tabia mpya ambayo ndiyo iliyosababisha maendeleo ya kihistoria yaliyofuata katika eneo lote. Katika elfia ya kwanza baada ya enzi zetu, kikundi kikubwa cha watu kilihama kuelekea kusini mwa Afrika. Kikundi hiki cha Kinego kilikuwa cha wakulima waliokuwa na uchumi wao, namna yao ya kuishi na labda hata sura na lugha zao zilikuwa tofauti sana na za wenyeji wa sehemu zile. Kikundi hiki ndicho kilichoanzisha maarifa kuhusu utumiaji wa chuma na ufinyanzi vyungu. Hapo awali, maarifa haya yalikuwa hayajulikani katika sehemu hizi. Sura hii itahusika zaidi na namna, asili na maendeleo ya jamii hizi za awali za utumiaji chuma.

Wanaakiolojia wanatambua kuwa kwa jumla, utamaduni wa jamii zilizoanzisha utamaduni wa kutumia chuma Kusini mwa Afrika unafanana. Mabaki ya jamii hizi yanaonyesha kuwa kulikuwa na ufundi wa hali ya juu wa kutengeneza vitu vya chuma Kusini mwa Afrika hapo mwanzoni na ufundi huu ulikuwa tofauti na utumiaji chuma wa baadaye. Tofauti hii ilijitokeza hasa ukiangalia wakati na pia kuhusiana kwa ufundi huu wa mwanzoni na ufinyanzi vyungu wa kutoka kwenye asili moja. Mtawanyiko wa ufundi huu wa kwanza wa utumiaji chuma unavuka inipaka ya eneo la kusini mwa Afrika ambalo linaongelewa hapa. Ufundi huu unaweza kugawanywa katika sehemu nyingi za maeneo. Kwanza, mgawanyo unaweza kufanywa kufuatana na mitindo ya utengenezaji vyungu. Vilevile, katika sehemu nyingi makundi haya yanaweza kuthibitishwa kwa kuwepo vitu visivyohusiana kitamaduni.

Vyombo vilivyofinyangwa vya wakati wa mwanzoni wa utumiaji chuma vinaonekana kuwa vililetwa katika eneo hili lote katika karne chache za mwanzo za enzi za Ukristo. Utamaduni huu ulibakia katika sehemu nyingi hadi kuondolewa kwake na utamaduni tofauti wa utumiaji chuma wa hapo baadaye, hasa mwanzoni mwa elfia hii ya sasa. Tarehe za mwisho zinatofautiana kila sehemu. Utumiaji chuma wa mwanzo ulifutika katika karne ya nane katika sehemu fulani na katika sehemu nyingine unaonekana kuwa na kiwango fulani cha mwendelezo kati ya utumiaji chuma wa mwanzo na ufinyanzi vyungu wa kijadi uliopo sasa. Kwa manufaa ya wasomaji, katika maandishi haya yanayogusia sehemu nyingi, nimeonelea



27.1 Kusini mwa Afrika: Mahali panapohusika na enzi ya chuma ya mwanzoni na maeneo yaliyotajwa: kwenye matini

ni zungumzie tamaduni za enzi ya chuma ya mwanzo hadi kufikia kuondolewa kwake au hadi karne ya kumi na moja ya enzi za Ukristo. Hii inafuatana na tarehe za mwanzo katika sehemu hiyo. Hivyo nimeacha kuzungumzia mabaki ya baadaye ya tamaduni za utumiaji chuma wa kwanza. Habari hii itazungumziwa mahali pengine pamoja na enzi ya chuma ya baaaye.

Ni dhahiri kuwa enzi ya chuma ya manzoni ni sehemu moja tu ya shughuli za binadamu wa kusini mwa Afrika katika elfia ya kwanza ya enzi zetu. Katika sehemu nyingi jamii za enzi ya mawe ya mwishoni zilicendelea kuishi maisha yake ya kijadi wakati wote huu. Wenzao waliokuwa kusini, sehemu ambayo haikufikiwa na utamaduni wa kutumia chuma wa mwanzoni, wanaoneka kuwa walikuwa wanatumia vitu fulani vya utamaduni ambao ulikuwa umeigwa kutoka enzi ya chuma ya mwanzoni waliokuja kukaa sehemu zile. Kuigwa huku kulitokea baada ya kuhusiana kwao kwa moja kwa moja au kwa kupitia vikundi vingine. Vikundi hivi vya mwisho vya utumiaji mawe na vikundi vingine vilivyohusika vimeelezwa na J.E. Parkington, katika sura ya 26 juzuu hili.

Ukusanyaji wa habari kuhusu enzi ya chuma ya mwanzo kusini mwa Afrika kwanza kabisa, lazima ufuatane na ushahidi wa kiakiolojia. Tofauti na matukio ya nyakati za baadaye za utumiaji chuma, matukio ya wakati huu kwa vile yalitokea katika miaka elfia ya kwanza ya enzi za Ukristo yako nje ya mipaka ya fasihi B simulizi. Kama ilivyoonyeshwa katika sura moja ya hapo awali, kumekuwa na majaribio ya kuunda historia ya wakati wa utumiaji chuma mwanzoni ambao haukuwa na maandishi kwa kutumia vipengele vya lugha peke yake. Katika ujuzi wetu wa sasa, inaonekana kamba ni bora zaidi kuyachukulia matokeo ya lugha kuwa ni ushahidi wa nyongeza ukilinganishwa na ushahidi unaotokana na akiolojia.

Utafiti wa Kikanda wa Usahidi wa Kiakiolojia

Kusini mwa Zambia, Angola na Malawi

Mwandishi wa sura hii hivi karibuni alifanya uchunguzi wa enzi ya chuma ya mwanzoni katika eneo la Zambia. Matokeo yake ni kwamba vikundi tofauti vimeweza kutambuliwa hasa kutokana na aina ya vyungu vilivyohusiana na huo utamaduni wa chuma. Hapa tutazungumzia tu matokeo ya uchunguzi huu katika sehemu ya kusini mwa nchi hiyo. Vikundi viwili vinavyohusiana vinaweza vikatenganishwa katika eneo la Copperbelt na nyanda za juu za Lusaka. Kikundi cha Chondwe katika eneo la Copperbelt kinajitambulisha kwa kuwa na vyombo vinavyotokana na ufanyanji vyenye ncha nene au zisizotofautishwa na sehemu nyingine. Sehemu muhimu ya upambaji huwa ni misitari yenye kuonyesha pembe tuzilizotofautishwa kwa naruna ambayo inaonekana kama umbo la utepe uliojitokeza na sehemu zenye umbo kama vitana zilizotiwa mifuo. Masalio ya vijiji ishirini ambavyo hadi sasa vimeweza kuonyesha vyungu vya namna hii, yametawanyika kando kando ya mito na vijito. Kwa kawaida,

vitu hivi hukutwa karibu na “midambo” iliyojipanga katika mistari ikipakana na sehemu za juu za vijito vya mto Kafue. Tarehe zilizopatikana kwa kutumia kipimo cha redio-kaboni ya maeneo ya vikundi vya Chondwe katika sehemu za Kangonga na Chondwe, zinaonyesha ni ya karne ya sita hadi ya kumi na moja ya enzi zetu. Lakini uchunguzi wa aina ya vyungu unaonyesha kuwa maeneo mengine ya vijiji yanaweza kuwa ya zamani zaidi. Utengenezaji wa ala za chuma na shaba umeonekana katika nyakati zote za kuwepo kwa vijiji hivyo. Hata hivyo, uchimbaji wa shaba katika eneo hilo unaonekana kuwa haukufanyika sana katika sehemu za mwanzo za utumiaji chuma, ingawa ulivutia uhusiano mkubwa wa kibiashara.

Katika sehemu ya kusini, hasa kwenye nyanda za juu za Lusaka, kuna makazi ya zamani ya utumiaji chuma wa mwanzoni unaohusiana na kikundi cha Kapwirimbwe. Vyungu vya kikundi hiki ni tofauti na vile vya kikundi cha Chondwe kwa ukubwa na vingi vina unene wa ncha. Aidha vyungu hivi ni nadra kuonekana na mapambo yenye umbo kama vitana. Badala yake kuna alama nyingi zilizokatwakatwa. Katika kijiji cha Kapwirimbwe, ambacho kiko kilomita 13 mashariki ya Lusaka, makazi ya muda yameweza kupewa tarehe za karne ya tano ya enzi za Ukristo. Kulikuwa na mabaki mengi ya majengo ya “*daya*” ambayo sasa yamebomoka. Mengi ya majengo haya yanaonyesha kwamba yalikuwa ni mitanuu ya kuyeyushia chuma.

Katika magharibi ya Zambia, ni maeneo machache ya enzi ya chuma ya mwanzoni ambayo yamekwishakugunduliwa. Kuna makazi ya zamani karibu na Misheni ya Sioma katika Zambezi ya Juu ambayo yanafikiriwa kuwapo kutoka karne za kati za elfia ya kwanza. Makazi mengine ambayo yako karibu na mto Lubusi, magharibi ya Kamoja, yanafikiriwa ni ya robo ya mwisho ya elfia hiyo. Maeneo haya yametoa vyungu vilivyo tofauti na vile vya vikundi vya mashariki, ingawa hapana shaka ni vya enzi ya chuma ya mwanzoni.

Hapa, ni vizuri izingatiwe kuwa maeneo ya enzi ya chuma ya tangu elfia ya kwanza ya enzi zetu hivi sasa yanajulikana kutoka sehemu za kusini zaidi za Angola, kama vile huko Feti-la-Chonya, ambapo makazi ya awali ya enzi ya chuma yanafikiriwa kuwa ya karne ya saba au ya nane. Uhusiano kati ya makazi haya na utumiaji chuma wa mwanzoni wa hali ya juu hauwezi kuonyeshwa kwa vile hakuna maelezo mengi kuhusu ala zinazohusika, mbali na ukweli kwamba vyote vilikuwepo B chuma na chungu. Katika sehemu za kaskazini zaidi na Namibia, kuna masalio ya makazi ya Kapako ambayo yameonyesha kuwako kwa vyungu. Hivi vimeelezwa kuwa ni vyungu vinavyohusiana na vile vya Kapwerimbwe. Kufuatana na vipimo vya redio-kaboni vyungu hivyo ni vya tangu mwishoni mwa elfia ya kwanza.

Maeneo kadhaa yameonekana kusini mwa Kafue, katika sehemu zenye rutuba ya nyanda za juu za Jimbo la kusini la Zambia. Maeneo haya yanaonyesha vijiji vilivyokuwa vikitumia chuma hapo awali. Baadhi ya makazi yalikuwa yamekaliwa kwa muda mrefu zaidi kuliko mahali pengine. Makazi ya zamani zaidi ya namna hii yalikuwepo wakati wa karne ya nne.

Makazi haya ya enzi ya chuma ya mwanzoni yanaonekana kuwa na watu wengi

zaidi kuliko sehemu nyingine ambako wenzao waliweza kunusurika wakati ukulima na ufuaji chuma vilipoanzishwa.

Eneo la bonde la mto Zambezi karibu na Livingstone linaonekana kuwa ndilo lililofanyiwa uchunguzi zaidi wa kiakiolojia katika sehemu yote ya kusini mwa Afrika hasa katika suala la ufuaji chuma. Kikundi cha Damba cha enzi ya chuma ya mwanzoni katika eneo hili kina mambo fulani yanayofanana na kikundi cha Kalundu na pia kufanana na makazi ya Gokomera katika Zimbabwe. Imefikiriwa kwamba misingi ya kustawi kwa kikundi cha Dambwa ni kule kuwapo kwa kituo cha pili cha mtawanyiko wa utamaduni wa enzi ya chuma, kusini mwa Zambezi. Mwanzo haya yametokana na kuwako kwa hatua ya mwanzo, ambayo haijulikani sana, lakini inayoweza kuelezwa na mkusanyiko mdogo wa vigae kutoka eneo la Stumpa karibu na Machili. Shaba haonekani katika sehemu hii na hivyo lazima ililetwa sehemu hiyo kwa biashara. Vituo viwili vya karibu zaidi vilivyokuwa na shaba ni eneo la Kafue Hook katika Zambia na karibu na Wankie nchini Zimbabwe. Ala za shaba zilizokutwa kwenye maeneo ya vikundi vya Dambwa ni pamoja na bangili na vito vya thamani.

Katika Jimbo la Mashariki la Zambia, kikundi cha kwanza kilichokuwa kikitumia chuana kinaonekana kilifikia sehemu hiyo katika karne ya tatu ya enzi za Ukristo. Lakini kikundi hiki kilibakia kidogo mno baada ya kutawanyika. Inaonekana kuwa sehemu kubwa walibaki na namna yao ya maisha ya "utumiaji mawe" hadi kufikia elfia ya sasa na hadi kipindi cha baadaye toka enzi ya chuana ya nyuma. Vyungu vya maeneo haya ya kikundi cha Kamnama, mashariki mwa Zambia, vina uhusiano mkubwa na vile vya wakati ule ule katika makazi ya sehemu za karibu na Malawi, ambapo kuna taarifa kamili kuhusu mabadiliko mbalimbali ya enzi ya chuma kwa mujibu wa ushahidi wa kiakiolojia. Taarifa hii sasa inekamilika kwa sehemu kubwa ya nchi hiyo, ambayo iko magharibi ya Ziwa.

Katika sehemu za kaskazini ya Malawi, eneo lililo kusini mwa mto Rnkuru kando ya mlima Phope, limetoa ushahidi wa kuendelea kwa muda mrefu kwa shughuli za enzi ya chuma ya mwanzo kwa muda mrefu wa kati ya karne ya pili na ya tano ya enzi zote. Vitu vilivyopatikana ni pamoja na vigae, mifupa ya wanyama wa mwinu, ushahidi wa unyeyushaji chuma na shanga za sinbi. Shanga za kioo hazikuonekana. Vyungu hivyo vinahusiana na vile vya Kamnama; na kuna uhusiano wa jumla kati ya vitu hivi na vyombo vya enzi ya chuma ya mwanzoni katika Afrika Mashariki hasa ufanyanzi uliotoka Kwalu, ndani kidogo ya Mombasa. Vitu vinafyofanana kutoka milima ya Lumbule karibu na Livingstone vimepewa tarehe za katikati ya elfia ya kwanza. Eneo la Mavarambo katika sehemu za kaskazini mwa Malawi linaonekana kuiwakilisha vizuri hali ya enzi ya chuma ya mwanzoni katika eneo hilo. Kinaonyesha uhusiano fulani na kikundi cha Malambo, kaskazini ya Zambia. Eneo la Mwavarambo ni la kipindi kutoka karne ya kumi na moja hadi karne ya kumi na tatu. Ugunduzi wa maeneo mengi kusini mwa Malawi, yakihusiana na kikundi cha Nkope, unaonyesha kuwaopo kwa makazi yanayofanana na hayo ya kipindi cha kuanzia karne ya nne hadi ya kumi na moja. Vyombo vya ufanyanzi vya enzi ya chuma mwanzoni



27.2 Maeneo ya kusini mwa Afrika: Sehemu za Enzi ya Chuma ya Awali na mengine yanayohusiana ambayo yametajwa kwenye matini

katika sehemu za Malawi na maeneo ya karibu katika Zambia, vinaunda kiungo cha wazi cha aina ya vyungu kati ya vile vya Afrika Mashariki na vile vya Zimbabwe. Lakimi viko tofauti sana na vile vya Chondwe, Kapwirimbwe na Kalundu katika sehemu za magharibi zinazovuka maeneo ya Lungwa. Kwa bahati mbaya, hakuna data zinazoonyesha maeneo ya enzi ya chuma ya mwanzoni nchini mashariki ya Ziwa Malawi. Ukweli ni kwamba hakuna data zozote zilizopatikana sehemu hii.

Afrika Kusini ya Zambezi

Katika Zimbabwe, picha ile ile ya jumla ya tofauti za kimkoa za viwanda vya enzi ya chuma ya awali vya aina moja inajitokeza. Hapo awali tulizungumzia viwanda vya mikoa miwili ya kaskazini ya nchi hiyo ambavyo vinahusiana sana na vikundi vya Zambia. Katika sehemu kubwa za Zimbabwe iliyobaki, tamaduni za enzi ya chuma ya mwanzoni zinaonyesha kufanana sana kimsingi. Wataalamu wamekubaliana, kwa jumla, kwamba kama namna tatu ya vyungu vinavyohusiana. Ufinyanzi wa Ziwa unaonekana kuwa ulikuwa na misingi yake mashariki ya sehemu ya milima karibu na Inyanga ukiendelea hadi karibu na Harare upande wa Magharibi na kwenye mipaka ya Msumbiji kuelekea mbuga za chini upande wa kusini. Ufinyanzi wa Zhisso (ambao zamani ulijulikana kama Kopje I ya Chui) uko kusini-magharibi karibu na Bulawayo. Ufinyanzi wa Gokomera umetawanyika sana katika maeneo ya kusini na kati. Aina hizi tatu zinaonyesha kuhusiana sana. Ni kweli kwamba uchunguzi wa hivi karibuni umeonyesha kuwa, katika maeneo fulani fulani, kuna kuingiliana kwa hali ya juu kati ya vikundi hivi. Hii ina maana kwamba tofauti hizi haziwezi kutenganishwa kwa wazi wazi kama vilivyo vikundi fulani vya utumiaji chuma wa nyakati za mwanzoni huko Zambia.

Picha iliyo wazi ya makazi ya enzi ya chuma ya mwanzoni huko Zimbabwe inaweza kupatikana Mabveni katika Wilaya ya Chibi. Katika sehemu hizi, mabaki ya namna tatu za ujenzi wa milingoti na "*daga*" yamekwisha kufanyiwa uchunguzi. Baadhi ya mabaki haya yamefikiriwa kuwa yalikuwa ghala ambayo hapo mwanzoni ilijengwa kwenye mawe juu ya ardhi. Kuwapo kwa kuta za mawe matupu hakukuweza kuhusishwa kwa kauli moja na makazi ya enzi ya chuma ya mwanzoni. Hata hivyo majengo haya ni tofauti kiufundi yakilinganishwa na yale ya wakati huu. Ufinyanzi vyungu ulikuwa tofauti kwa vile vyombo vyote vilifinyangwa kwa midogo mirefu pamoja na mapambo yenye umbo la vitana yakiwa upande upande. Vilevile ncha zilikuwa nene. Vikundi hivi pia vilifinyanga mabakuli yenye midogo mipana. Sanamu za udongo zinazoonyesha kondoo na binadamu pia zimegunduliwa, pamoja na shanga zilizotengenezwa kwa chuma, shaba na simbi. Uhusiano wa kibiashara na watu wa mwambao unadhihirishwa na kuwapo kwa simbi baharini na shanga za kioo. Kondoo ndio mifugo pekee iliyogunduliwa. Eneo hili laonekana ni la kuanzia kipindi fulani katika theluthi mbili za kwanza za elfia ya kwanza. Uthibitisho wa taarifa hizi unatoka kwenye makazi ya mwamba yaliyoko huko katika Misheni ya Gokomere kaskazini mwa Ngome ya Victoria, ambako mifupa ya wanyama iliyogunduliwa ni

pamoja na pembe za mbuzi wanaofugwa. Makazi ya enzi ya chuma huko Gomera ni ya kuanzia karne ya tano na ya saba. Shughuli ya awali kabisa ya enzi ya chuma ya "Acropolis" katika Zimbabwe Kuu ni mfano mwingine wa viwanda vya enzi ya chuma ya mwanzoni huko Gokomera na mwisho wake wafikiriwa kuwa katika kipindi kati ya karne ya tatu na ya tano.

Maendeleo makubwa ya uchumi yanaonekana kwenye eneo hili katika karne za mwishoni za enzi ya chuma ya mwanzoni. Katika maumbo yake ya baadaye vyombo vya Ziwa vyaonekana kufanana na shanga za kioo zilizoagizwa kutoka nje. Aina ya ufinyanzi inayoweza kulinganishwa na hiyo inaweza pia kupatikana katika maeneo yenye matugazi na kuta za mawe, na pia machimbo ya dhahabu na shaba yaonyeshayo kwamba watengenezaji wake walivyohusisha mno matumizi mazuri ya mali ya asili ya nchi yao kuliko wale waliowatangulia na kwamba walikuwa na uhusiano na mfumo wa biashara wa Bahari ya Hindi.

Ni katika muda huu pia ndipo ng'ombe wa kufugwa wanapoonekana kwa mara ya kwanza katika kumbukumbu za kiakiolojia za Zimbabwe. Mabaki ya wanyama hawa hayaonekani katika maeneo ya awali kabisa ya makazi ya enzi ya chuma kusini mwa Zambezi, ambapo wanyama wa kufugwa wanaowakilishwa ni kondoo na mbuzi tu. Kumbukumbu za mwanzo kabisa kuhusu ng'ombe zipo katika kipindi cha maeneo ya karne ya nane, nazo hazitokei kwa wingi kabla ya kuanza kwa enzi ya chuma ya nyuina.

Maeneo yatoayo vyungu aina ya Zhidso, yaliyoko huko Bulawayo, yanafanana na viwanda vya enzi ya chuma ya mwanzoni katika sehemu za mashariki. Hivi sasa inaonekana kuwa aina hii ya ufinyanzi vyungu haiwakilishi shughuli za mwanzo za enzi ya chuma katika sehemu hiyo. Shughuli hizi huenda ndizo zaonekana katika maeneo kama Mandau na Mandilinyangwa katika milima ya Matopo, ambako vigae vilivyogunduliwa vinahusiana sana na vyombo vya awali vya Gokomera na vyungu vya enzi ya chuma ya mwanzoni vya kikundi cha Dambwa katika eneo la Maporomoko ya Victoria. Inaonekana kuwa katika sehemu kubwa ya kusini-magharibi ya Zimbabwe, watu wa enzi ya chuma ya mwanzoni walibakia wachache sana, hadi wakati wa kuendeleza viwanda vya Zhiso mwishoni mwa elfia ya kwanza. Uchunguzi wa michoro kwenye miamba unaonyesha namna watu wa mwisho waliotumia mawe walivyonusurika kwa wingi wakati huu wote, hasa katika milima ya Matopo.

Machimbo yaliyofanyika katika milima ya Zhiso katika maeneo ya Matopo yameonyesha kuwapo kwa mabaki ya majengo ya milingoti na *daga* na mkusanyiko wa mawe ambao umefikiriwa kwamba ulikuwa ukitumiwa kuwa ni ghalala za kuwekea nafaka. Pia palikuwa na vyungu vilivyopambwa kwa michoro yenye maumbo ya vitana. Vitu hivi vimeonekana ni vya kati ya karne ya tisa na ya kumi na mbili.

Ueneaji wa viwanda vya enzi ya chuma ya mwanzoni kusini mwa Limpopo katika elfia ya kwanza umekwisha kuonyeshwa. Hata hivyo hakuna ushahidi mkubwa, na huu ulioko haukukamilika. Vyungu ambavyo vinafanana na vile vya Malapati

vimegunduliwa Matakoma katika maeneo ya Soutspansheberg, kaskazini mwa Transvaal. Hadi sasa, hakuna tarehe halisi zilizopatikana kuhusu eneo hili, lakini kufanana kwa eneo hilo na eneo la Malapati hufanya yafikiriwe kuwa ya nusu ya pili ya elfia ya kwanza. Karibu na Tzaneen katika sehemu za kaskazini-mashariki ya Transvaal, vyungu vya aina ya enzi ya chuma ya mwanzoni vimefikiriwa kuwa vya karne ya tatu au ya nne. Hii inaonyesha kuwa ueneaji wa vitu hivyo kusini mwa mto Limpopo haukukawia sana kabla ya kuingia kwake Zimbabwe.

Ugunduzi kadhaa wa ala zilizotengenezwa katika enzi ya chuma umeweza kufanyika hata kusini ya mbali zaidi. Ala hizi zinafikiriwa kuwa za kuanzia elfia ya kwanza. Hata hivyo, haijulikani kama inatokana na viwanda vya enzi ya chuma. Katika Castle Peak, huko Ngwenya katika magharibi ya Swaziland, kuwepo kwa enzi ya chuma kinafikiriwa kuwa karne ya nne au ya tano. Taarifa ya awali ya waliokichimbua chungu hiki kinachohusiana ua vifaa na vitu vya sana vya enzi ya chuma ya nyuma, huonyesha kwamba ni vya enzi ya chuma ya awali.

Usanisi wa Kiakiolojia

Ingawa kuna mtawanyiko na thamani zisizolingana za uchunguzi wa kiakiolojia juu ya enzi ya chuma ya mwanzoni, ilivyoonekana katika muhtasari wa maelezo yaliyotangulia, kuna mielekeo kadhaa ya jumla inayojitokeza. Katika maeneo yanayozungunziwa, uchunguzi wa aina za vyungu unaturuhusu kuitambua migawanyiko miwili mikubwa ya enzi ya chuma ya mwanzoni. Mgawanyiko wa kwanza unajulikana sana katika Zambia ya kati na ya kusini inakowakilishwa na katika vikundi vya Chondwe, Kapwirimbwe na Kalundu. Mgawanyiko huu umetapakaa mbali ingawa umbali wake kwa upande wa magharibi haujulikani. Mgawanyiko mwingine hutapakaa Malawi, mashariki ya Zambia na eneo linalojulikana kuwa makazi ya enzi ya chuma ya mwanzoni kusini mwa Zambezi. Kikundi cha Dhambwa katika eneo la Maporomoko vya Viktoria yaliyoko katika bonde la Zambezi, kina vitu vingi vinavyofanana na vile vilivyopo kwenye migawanyiko hii miwili. Uainishaji huu unathibitishwa, kwa namna fulani, na uchunguzi wa maswala ya uchumi wa nyakati za utumiaji chuma wa mwanzoni, kama ilivyoelezwa hapa chini.

Uchumi wa Uzalishaji Chakula

Ushahidi madhubuti kuhusu uchumi wa uzalishaji chakula wa jamii za enzi ya chuma ya mwanzoni, umeonekana mara chache sana. Kuwapo kwa vijiji vikubwa na vya kudumu kwa kadiri fulani kunaonyesha kuwa uchumi ulihusiana sana na uzalishaji chakula. Isitoshe, ugunduzi wa majembe ya chuma na idadi kubwa ya mawe ya kusagia unaonyesha kuwa kulikuwa na namna fulani ya kilimo. Ushahidi zaidi wa kufanana kwa namna ya kulima na kufuga uneweza kupatikana kutokana na maeneo machache sana. Mifupa ya ng'ombe imeonekana kuwa ya zamani katika sehemu chache tu kama vile katika makazi ya kusini mwa Zambia kama vile Kapwirimbwe,

Kalundu na Kumadzulo. Ng'ombe hawaonekani kuwa katika maeneo ya kusini mwa Zambezi kabla ya karne ya nane, kama vile katika Coronation Park, Makuru na Malapati. Uchunguzi wa michoro ya miambani katika Zimbabwe unadhihirisha kuwa kondoo waliingizwa katika nchi hiyo kabla ya ng'ombe. Hii ni kwa sababu kondoo wenye mikia minene wanaonekana mara nyingi kwenye michoro hii, lakini sio ng'ombe. Ushahidi kutoka Broederstroom unaonyesha kwamba ng'ombe walikuwepo mapema huku Transvaal, ambapo yawezekana labda walitokea magharibi.

Uchimbaji Madini na Ufuaji Chuma

Ni metali ya aina tatu tu ambazo yalitumiwa sana katika enzi ya chuma ya kusini mwa Afrika. Madimi haya, kwa kufuata umuhimu wake, yalikuwa ni chuma, shaba na dhahabu.

Chuma kimetapakaa sana katika sehemu hii katika maumbo mbalimbali. Mahali ambapo chuma kizuri hakikuwepo, chuna rojorojo kiliyeyushwa, ingawa hakikutoa chuma nyingi. Ufuaji chuma unaonekana kuwa uliingizwa katika maeneo yote ikiwa pamoja na vitu mbalimbali vinavyounda tamaduni za enzi ya chuma kama livyoelezwa. Hakuna ushahidi kwamba chuma kilichimbwa kwa wingi, zaidi ya kuchimbua mashimo ya kina kifupi. Mara nyingi mawe ya madini yalikusanywa tu kutoka juu ya ardhi. Mpaka sasa hakujapatikana maelezo zaidi ya matanuu ya kuyeyushia chuma ya enzi ya chuma ya mwanzoni kusini mwa Afrika. Hata hivyo, ni vizuri kuzingatia kwamba uyeuyushaji chuma kama inavyoonekana, ulifanyika mara nyingi katika vijiji. Hii inaonyesha kwamba miiko, ambayo hapo baadaye ilifanya kuwa uyeuyushaji chuma ufanyike kando kabisa na mahali walipo wanawake, haikuwepo katika wakati huo. Kwa jumla, vyombo vilivyotengenezwa kwa chuma vilikuwa ni vya matumizi ya nyumbani. Vitu hivi ni pamoja na visu, mishale, ncha za mikuki na vitu vya namna hiyo. Inaonekana kuwa hapakuwa na biashara za mbali zinazohusu chuma au vyombo vilivyotengenezwa kwa chuma.

Mashapo ya shaba yametawanyika mahali padogo zaidi kuliko chuma. Ala za shaba, hata hivyo, zimeonekana sana katika maeneo ya enzi ya chuma ya mwanzoni, ingawa hazionekani mara nyingi kama zinavyoonekana katika maeneo ya vipindi vya baadaye. Ni vigumu kuonyesha kama teknolojia ya kutumia shaba ilitumika katika sehemu zote katika tarehe za awali za enzi ya chuma ya mwanzo ilivyokuwa kuhusiana na teknolojia ya chuma. Katika eneo la Lusaka, kwa mfano, shaba ilikuwa ikifahamika hadi mwishoni mwa enzi ya chuma ya mwanzoni.

Ni dhahiri kuwa shaba ilifikiriwa kuwa ni kitu cha anasa, na matumizi yake yalionekana zaidi katika kutengeneza vitu vidogo vya mapambo ya binafsi kama vile shanga na bangili vyembamba zilizosukwa kwa kuzungushwa. Metali hii ilifanyiwa biashara katika umbo la fito. Mfano wake mmoja ni ule uliogunduliwa Kumadzulo. Hakuna uchunguzi uliofanyika kuhusu uyeuyushaji shaba wa nyakati za mwanzo za utumiaji chuma.

Uchimbaji wa dhahabu wa enzi ya chuma kusini mwa Afrika unaonekana kuwa

ulitokea zaidi nchini Zimbabwe na kwenye maeneo ya jirani. Kiasi kidogo cha uchimbaji wake katika kipindi kabla ya historia nchini Zambia, Afrika Kusini na mahali kwingine, yamekwishatolewa taarifa. Hata hivyo, hakuna uchunguzi wa ndani ambao umekwisha kufanywa. Kwa upande mwingine, zaidi ya machimbo ya dhahabu elfu moja ya kipindi kabla ya historia yamekwisha kuelezwa katika Zimbabwe na maeneo yanayopakana ya Bostswana na Transvaal. Machimbo mengi ya kale yameharibiwa na machimbo ya hapo baadaye katika sehemu hizo yaliyofanyika katika miaka themanini iliyopita. Hivyo, ni machimbo machache sana yenye maelezo ya ndani. Ni vigumu sana kujua wakati gani wa zama za kale machimbo haya ya dhahabu za Zimbabwe yalifanyika. Kipimo cha redio-kaboni kinaonyesha kuwa machimbo ya zamani kabisa katika sehemu hiyo ni yale ya Aboyne na Geelong. Haya yanafikiriwa kuwa ya karne ya kumi na mbili.

Ingawa vitu vingi vya dhahabu vinaweza kugunduliwa katika maeneo ya enzi ya chuma ya Zimbabwe sehemu kubwa ya vitu hivi ilichukuliwa na watu ambao walikuwa wakitafuta hazina katika miaka ya mwanzoni ya kuja kwa Wazungu. Hivyo, data iliyopo haitoshelezi kuonyesha vitu vilivyogunduliwa vilitokea wapi na vina uhusiano gani na nambo ya kale kwa jumla. Idadi ndogo ya dhahabu iliyogunduliwa katika machimbo ya kiakiolojia yaliyozuliwa yanetokana na miktadha ya baadaye ya enzi ya chuma.

Usanifu Majenzi

Ni maeneo machache sana ambayo yana habari inayoweza kutupa niwangaza kuhusu mitindo mbalimbali ya kusanifu majenzi na maelezo kamili ya miundo ya enzi ya chuma ya mwanzoni katika sehemu hii. Vilevile bado kuna mashaka kuhusu jinsi maeneo haya yanavyowakilisha niaumbile ya usanifu majenzi wa kusini mwa Afrika katika wakati huo. Kumandzulo imetoa ushahidi wa mipango ya nyumba kumi na moja za majenzi ya milingoti na "daga". Majengo haya yalikuwa ya nusu mstatili ya kiwa na viguzo vingi vya pembenne. Urefu wa kuta ulikuwa inita 2.3 tu. Hakuna ushahidi wa majengo yanayofanana uliokwishapatikana kutoka maeneo ya enzi ya chuma yaliyopo kusini mwa Afrika. Hata hivyo, alama za hapa na pale kutoka makazi mengine kama vile Dambwa na Chitope, yanaonyesha kwamba mbinu za ujenzi zinaonekana Kumandzulo zilitumiwa zaidi, ingawa maumbo ya nusu mstatili yanayoonekana katika nyumba za Kumandzulo hayaonekani mahali pengine.

Ujenzi wa kutumia mawe ulienea sana katika enzi ya chuma katika majimbo ya kusini mwa Zambezi. Hata hivyo mtindo huu hauonekani kuwa ulitawanyika nchini Zambia katika karne za mwisho za enzi iliyofuata ya chuma.

Hitimisho

Kwa ufupi, huu ndio ujuzi tuliona kuhusu nyakati za awali za utunijaji chuma kusini mwa Afrika. Sura hii inayatazama mambo yaliyotokana na matukio haya ya

kitamaduni kama kitu kinachohusu utaalumu wa mambo ya kale. Ni dhahiri kuwa uchunguzi wa isimu ya mambo ya kihistoria unaweza pia kuleta mchango mkubwa katika kujua mambo ya enzi ya chuma ya mwanzo. Haya yameelezwa katika sura iliyotangulia.

Katika eneo la kusini mwa Afrika ambalo limezungumziwa, kuna migawanyiko mikubwa miwili ya enzi ya chuma ya mwanzoni kwa mujibu wa taarifa za uchunguzi wa mambo ya kale. Migawanyiko hii inaweza kufikiriwa kuwa ni migawanyo ya kawaida ya viwanda vya enzi ya chuma ya mwanzoni. Lakini migawanyo hii inaweza kupambanuliwa kwa maumbile ya vyungu vinavyohusiana. Mgawanyiko inmoja ulienea kuelekea kusini kati ya bonde la Luangwa na Ziwa Malawi hadi Zimbabwe na kaskazini ya Transvaal. Watu wake walikuwa ni wafugaji wa kondoo na mbuzi, na wanaonekana kutokua na ng'ombe hapo mwanzoni. Mgawanyiko wa pili huenea kuanzia sehemu ya kati na kusini za Zambia, lakini yaelekelea imcenea pia kwenye eneo kubwa kuelekea magharibi. Katika eneo hili ng'ombe walikuwa wakijulikana katika enzi ya chuma ya mwanzoni na bila shaka ng'ombe waliwufikia wachungaji wa Khoisan wa maeneo ya kusini kuliko yote katika bara hili kutokca kwa maeneo ya wenyeji hawa. Eneo hilo la Wakhoisan halikufikiwa na shughuli za viwanda vya enzi ya chuma ya mwanzoni.

Tatizo la mtawanyiko usiolingana na uchunguzi wa akiolojia limezuia uwezekano wa kupata maoni mengi kuhusu migawanyo zaidi enzi ya chuma ya mwanzoni. Ukiangalia kwenye ramani inayoonyesha mtawanyiko wa uchunguzi wa mambo ya kale, sehemu yote ya Msumbiji haina chochote. Hivyo, matukio yote ya kihistoria katika eneo lote kati ya Bahari Kuu ya Hindi na Ziwa Nyasa hayajulikani hadi sasa. Sehemu kubwa za Angola na Afrika Kusini hazijafanyiwa uchunguzi wa kutosha. Wakati upungufu huu utakaporekebishwa, itabidi kufanywe inabadiliko makubwa katika usanisi uliofanywa hapa.

Imeonyeshwa kuwa utamaduni ulioingizwa kusini mwa Afrika na watu wa enzi ya chuma ya mwanzoni, ndio uliokuwa msingi wa maelekeo mengi ya tamaduni za kihistoria katika sehemu hiyo na kufikia hadi nyakati za karibuni. Kitu kinachoweza kuwavutia wanahistoria katika muktadha huu ni jinsi tofauti za maumbile ya kimkoa za wakati wa baadaye zinavyoweza kufnatiliwa hadi enzi ya chuma ya mwanzoni. Jadi ya kujenga nyumba kwa mawe nchini Zimbabwe na Transvaal, uchimbaji wa dhahabu nchini Zimbabwe na utengenezaji wa vyombo vya shaba katika maeneo ya Copperbelt ni mifano ya mambo yaliyoanza katika enzi ya chuma ya mwanzoni katika maeneo yake, ingawa hayakustawi hadi hapo baadaye. Uendelezaji kati ya enzi ya chuma ya mwanzoni na ile ya nyuma katika maeneo mengi, ni kitu ambacho bila shaka kilijitokeza nara nyingi hata kuliko iliyofikiriwa na watu. Lakini ni baada tu ya kufanya uchunguzi wa ndani zaidi hasa katika maeneo ambayo hayajavumbuliwa kiakiolojia, ndipo mchango kamiliwa uchunguzi huu wa enzi ya chuma ya mwanzo kwa historia ya kusini mwa Afrika utakapoweza kntathminiwa.


Uchunguzi wa Kiutamaduni

Historia ya watu wa Bukini (Madagascar) imeshughulikiwa katika taaluma nyingi. Hata hivyo, ingawa nadharia tete mbalimbali muhimu zimewahi kutolewa asili hasa ya watu hawa bado imetandwa na fumbo. Waandishi wengi wamekubaliana kwamba ingawa bara la Afrika, ambalo liko karibu sana na Bukini, limekiathiri kisiwa hicho na desturi zake za Kiafrika, mambo yenye asili ya Malaya na Polynesia ambayo yanaonekana dhahiri kabisa katika utamaduni wa watu wa Bukini, hasa kwenye sehemu za miinuko ya kati ya kisiwa hiki kikubwa, yanastahili kutiliwa mkazo. Kuwako kwa pande mbili za asili ya watu wa Bukini kunafafanua hali tofauti za maumbile kati ya wananchi wa kisiwa hicho ambao wote hutumia lugha ya Kiindonesia. Ijapokuwa lugha hii imegawanyika katika lahaja tatu, hakuna wasiwasi wowote kwamba lahaja hizo tatu zinatokana na lugha moja.

Isimu

de Houtman, mwanazuoni wa Kiholanzi, ndiye aliyekuwa wa kwanza kutoa rai kwamba nchi ya Bukini iko katika kundi la lugha la Malaya-Polynesia.

Van der Tuuk baadaye alidhihirisha kwa njia ya kisayansi, uhusiano baina ya Kimalagasi na lugha za Kiindonesia. Baada ya hapo, Dahl alionyesha kuwa Kimalagasi kilikuwa kimeathiriwa na Kibantu, siyo tu katika msamiati, bali pia katika mpangilio wa sauti zake za usemi. Jambo hili la athari ya Kibantu ni la muhimu sana kwa ajili ya hoja ya muingiliano wa Waafrika na Waindonesia ambao utafafanuliwa baadaye. Herbert ameonyesha katika kazi zake kadhaa kwamba mara nyingi maneno ya Kiindonesia nchini Madagascar yamegawanyika katika sehemu mbili. Mgawanyiko huo umedhihirisha kwa namna kadhaa kwamba asili ya wenyeji wa Bukini ilichimbuka kutoka kusini mashariki ya Asia. De amechanganua msamiati wenye asili ya Kiindonesia unaotuwzesha kufahamu ni aina ipi ya ustaarabu iliyoletwa Bukini na wahamiaji. Mwisho historia ya elimu ya taratibu ya matamshi na usemaji wa maneno (glotokronolojia), imedhihirisha msamiati wa msingi wenye asili ya Kiindonesia (kwa asilimia 94), na kutoa fununu kuhusu muda unaotenganisha



28.1 Ramani ya Bukini inayoonyesha sehemu zinazotajwa kwenye makala.

Kimalagasi cha kisasa na lugha ya jadi. Hata hivyo, ingawa vipengele muhimu vya maneno ya Kimalagasi vimo katika kikundi kidogo cha Kiindonesia, tuisahau kuwa asili nyingine kama mila za Kihindi, Kiarabu, na lugha za Kiafrika pia zilijiingiza katika lugha hiyo. Mwingiliano huo tunaodokezewa katika athari hizi unatusaidia kuyaelewa maingiliano na mchanganyiko kutokana na uhamaji wa Kiindonesia kuelekea upande wa magharibi.

Anthropolojia Maumbo

Utafiti katika somo hili umethibitisha kwamba wenyeji wa Bukini wana asili za namna mbili: asili ya Kimongoli na asili ya Kinegro.

Rakoto-Ratsimamanga amefikia hoja muhimu kuhusu mgawanyiko na maumbile ya kiini cha rangi ya watu (pigmenti) inayopatikana mara kwa mara baina ya wakazi wa sehemu za nyanda za juu zilizoko katikati. Rakoto-Ratsimamanga anatofautisha aina nne za umbo na muundo wa maneno ambayo kutokana nayo, jamii ya watu imegawanyika kwa uwiano ufuatao:

Aina ya Waindonesia na Wamongoli	alisimia 37
Aina ya Wanegro-Wakibaharini	“ 52
Aina ya Wanegro-Waafrika	“ 2
Aina ya Wazungu	“ 9

Mtu huenda akauliza hapa ikiwa sehemu kubwa kama hiyo ya watu wenye damu ya Kinegro ina asili ya Kibaharini. Utafiti na uchunguzi wa damu uliofanywa na Pigache wadhihirisha waziwazi kabisa kuwa Wanegro wa Bukini wana asili ya Kiaafirka, na siyo Kimelanesia.

Ethnolojia na Elimu ya Muziki

H. Deschamps ndiye alikuwa wa kwanza kubainisha mchango wa utamaduni wa Waafrika na Waindonesia katika ustaarabu wa Bukini. Fani za kiutamaduni za Kiafrika zapatikana kwenye ustaarabu wa Bukini, kama vile mila za kufuga ng'ombe, kuwako kwa Ibada za nyoka zinazoelekezwa kwa wafalme waliokufa sehemu za magharibi na huko Betsile na baadhi ya mambo yanayohusiana na taratibu za vikundi vya kisiasa vinavyoonekana katika sehemu za majimbo ya pwani.

Ustaarabu wa Bukini una msingi wa upande wa Mashariki, kama vile mijengo mingi ya nyumba, utamaduni wa kulima mpunga kwenye matungazi yanayonyunyiziwa maji, na mambo kadha wa kadha ya kuabudu mizimu, kazi mbalimbali za ufundi kama kutumika mivukuto yenye vilango viwili, ngalawa, sehemu za chini ya ardhi yenye jiwe la volkano linalopata maji na vyombo vinginevyo ambavyo havifahamiki sana kama vile keeke ya upinde inayozunguka, na aina ya chuma cha kuvunjia nazi kilichotundikwa juu. Vitu hivyo vyote ambavyo

vimechunguzwa katika sehemu ya pwani ya magharibi ya Bukini, na ambavyo vinapatikana kufikia umbali wa Mashariki ya Polynesia, vina usawa wa umbo.

Inawezekana kuhitimisha kwamba wahenga wa Bukini ni Waindonesia na Waafrika, na kwamba maumbile ya Kiindonesia yaliyoshamiri katika lugha ya Kimalagasi hayapunguzi dhima ya za Afrika katika kukaliwa kisiwa hicho. Bara hili kubwa ni jirani na Bukini, lilichangia idadi kubwa ya watu na kuipa nchi sifa nyingi za ya kiutamaduni pamoja na taratibu zake za kijamii za kisiasa. Mchanganyiko kama huu haupatikani katika Visiwa vya Ngazija au katika pwani ya Afrika ambako nako Waindonesia pia wanadhaniwa kuwa walifika.

Nadharia mbalimbali kuhusu asili ya Wamalagasi zimegawanyika katika pande mbili tofauti, yaani Afrika na Indonesia. Ingawa hivyo, ni kweli kwamba baadhi ya waandishi kama vile Razafintsalama (ambaye kutokana na minyambuo ya kietimolojia elfu kadha, ameshikilia kuwa kisiwa hiki kikubwa kilipata kutawaliwa na Masufi wa Kibudha) wana maoni tofauti kabisa. A. Grandidier alitoa umuhimu mkubwa mno kwa bara la Asia akiamini kwamba mbali na Wamakua waliowasili hivi karibuni, wahenga wote wa Malagasi walitoka sehemu ya Kusini na Mashariki ya Asia, likiwa ni pamoja na Wanegro ambao kwa lengo hili anawaita Wamelanesia. G. Ferrand analikubali wazo hili ambalo, linahitilafiana na ushahidi wa kijiografia bila sababu tosha na kusisitiza vipengele zaidi vya Kiafrika vya asili ya Wamalagasi. Alibainisha awamu za kihistoria zifuatazo:

Pengine kipindi cha kabla ya usemaji wa lugha za Kibantu;
kipindi cha usemaji wa lugha za Kibantu cha kabla ya enzi za Ukristo;
kipindi kabla ya kipindi cha Waindonesia wa Merina kutoka karne ya pili hadi karne ya nne, kilichohusisha uhamaji kutoka Sumatra wakati ambapo wageni hao waliimarisha utawala wao kwa waliokuwa wakizunguniza lugha za Kibantu; kuwasili kwa Waarabu kuanzia karne ya saba hadi karne ya kumi na moja; kuja mpya ya Wasumatra katika karne ya kumi, ambao miongoni mwao tunamkuta

Ramini, mhenga wa Wazifindraminia na Rakuba, mhenga wa Wahova; mwisho Waajemi; na kufikia mwaka wa 1500, Wazafikasinambo.

Makazi ya mwanzo Bukini

Kabla ya kuingia kwa undani zaidi katika asili za Kiindonesia na Kiafrika ya watu wa Bukini, yatupasa tutathmini nadharia zinazojaribu kuhusisha Bukini na uhamaji wa kale kutoka eneo la Mediterani.

Wafoeniki, Wayahudi, au watu wanaosimuliwa katika *Periplus?*

Katika kushughulika na nchi zilizokuwa mbali na mipaka ya na nchi za ulimwengu wa kale, Wafoeniki, Wamisri, Wasabe, Wayunani, na Wayahudi mara nyingi

wanapewa sifa zilizopita kiasi cha mchango katika historia ya nchi hizo. Kwa mfano, Bent (1893) aliwahasisha Wafoeniki na kuanzishwa kwa Zimbabwe, naye C. Poirier alibainisha eneo la Sofala kama na nchi za Punt na Ophir.

Kwa mujibu wa baadhi ya waandishi wasafiri wa kale walifika pia nchini Madagascar. F. de Mahy alidhani kwamba aligundua mabaki ya Wafoeniki huko Majunga lakini katika utafiti wetu, mimi na Ferrand, hatukuweza kuthibitisha nadharia tete hiyo. Katika maelezo yake A. Grandidier anataja kuwa Wayunani na hivyo hivyo Waarabu nao walitembelea Bukini. Kwa mujibu wa maelezo yake tangu kale kisiwa hiki kilijulikana kwa Wayumani na Waarabu kwa majina Menuthias, Djafouna, Chezbezar waliyoyatoa wao kwa kisiwa hiki, na vile vile maelezo sahihi lakini mafupi ambayo wametuchia hayakujulikana kwa wanajiografia wa Kizungu, ambao walizipata habari za kuweko kwa kisiwa hicho kutoka kwa Wareno, katika mwaka 1500.

Kwa hakika jina la pekee la Kiyunani "Menuthias", ambalo linapatikana kwenye *Ptolemy na Periplus*, lilitumiwa kumaamisha kisiwa cha Pemba, au labda Zanzibar, au Mafia. Kuna mwandishi mmoja anayejulikana kwa jina la F. Du Mesgnil aliamua kuandika kazi aliyoiita *Bukini, Homer, na Ustaarabu wa Kimesena* ambayo ilitoa picha ya wazi ya udadisi katika kazi hiyo.

Ngano kuhusu kuhama kwa Wayahudi haziwezi kupuuzwa kwa urahisi. Padri Joseph Briant katika juzuu lake dogo *Wayahudi nchini Bukini*, anashawishika kwamba kundi misafara miwili ya Wayahudi wahamaji waliowasili Bukini, wala si msafara mmoja. Inathibitisha hoja yake kwa kulinganisha maneno mia kadhaa ya Kimalagasi na ya Kiyahudi.

Tafiti kama hizo katika asili ya Kiyahudi ya baadhi ya inaeneo ya Kimalagasi inaanzia kwa Flacourt ambaye aliamini kwamba wageni wa kwanza kuwasili pwani ya Mashariki mwa Bukini walikuwa ni "Zaffe-Hibrahim", yaani watu wa ukoo a Ibrahim, waliokuwa wakaaji wa kisiwa cha Bikira Maria Mbarikiwa na nchi nyinginezo jirani. Kwenye dibaji yake katika kitabu cha *Historia ya Kisiwa kikuu cha Bukini*, Flacourt anafafanua ushahidi wa makisio yake kwa kuthibitisha kuwako kwa majina yanayopatikana katika Biblia, desturi ya kutahiri na mwiko a kutofanya kazi siku ya Jumamosi.

G. Ferrand anakanusha uwezekano wa uhamaji huu wa Wayahudi. Anasema kwamba kuwako kwa maneno machache ya Kisemitiki kisiwani Madagascar kunasababishwa na Wamalagasi wachache waliosilimishwa na kuhusu kutofanya kazi siku ya Jumamosi, anasema hakukutokana na desturi asilia za Kiyahudi, bali lilikuwa tukio la kawaida katika desturi za Wamalagasi. Jumamosi ni siku tu ya mwisho, ambayo ni kitu cha kawaida katika mila ya Kimalagasi; huko pwani ya mashariki miiko hutokea siku za Jumanne Alhamisi au Jumamosi kulingana na eneo. Aidha yaelekea mnamo karne ya 17, kuwepo kwa tohara miongoni mwa wageni kadhaa kulisababisha waandishi Wakristo wa Kifaransa kujaribu kuzitafutia asili ya Kiyahudi.

Nadharia tofauti kuhusu asili ya Wamalagasi kabla ya enzi ya Uislamu. Poirier anapambanua pande mbili za mchango wa Uislamu imeelezwa kwa karibuni na Poirier ambaye anaona uwili wa michango ya Waislamu chini Bukini. Wakati ambapo watangulizi wake wanadai kwamba zile desturi za Kiislamu zilizokuwa zikiendelea Bukini zilidhihirisha asili ya Kiyahudi, Poirier anafikiria kwamba desturi hizo zilikuwa ni za dini ya kizamani zilizoletwa Bukini kutoka Bara Arabuni. Hata hivyo, data ya kiakiolojia kutoka Afrika Mashariki na Bukini haitoi ushahidi wowote wa kuthibitisha nadharia ya Poirier. Kuwasili kwa wingi kwa Waarabu, kulikoathiri utamaduni wa Waswahili kulianza mnamo karne ya nane.

Majilio ya Kwanza ya Waindonesia

Ingawa itakuwa mi pupa kujaribu kutoa tarehe ya uhamaji wa Waindonesia, wa mwanzo lakini kwa sababu tutakazozitoa baadaye, tunaweza tukafikiria kwamba uhamaji wao ulianza mnamo karne ya tano ya enzi za Ukristo. Inawezekana kuwa waliendelea kuhama hadi kufikia karne ya 12, kama anavyofikiri Deschamps. Jina "Waindonesia-Wakongwe" limetolewa kwa wahamaji wa mwanzo waliofanya masiliano na Waafrika na ambao pengine walishirikiana nao. Wahamaji waliowasili baadaye, waliojulikana kama Waindonesia-Mamboleo, walikuwa Wahenga wa Wamerina. Luja hii ya niwishi ya uhamaji imehifadhi vizuri zaidi maumbile ya asili ya kibiolojia, kwa sababu ilipita njia ya nuoja kwa moja, lakini yawezekana kwamba kwa sababu ya idadi yake ndogo, ilichukua lugha ya Waindonesia-Wakongwe waliowasili awali huko Bukini.

Kama zana za mawe zilizotumika zamani zingalionekana, zingalituwezesha kuifahamu awamu ya awali ya historia ya Bukini lakini hadi wakati huu hakuna zana zozote za mawe zilizogunduliwa na ninafikiri kwamba Wamalagasi wa kwanza walikuwa wameshapata ujuzi wa kutumia metali. Tunajira kwamba katika pwani ya Afrika Enzi ya Mawe ilitanguliwa na Enzi ya Chuma, baina ya karne ya kwanza na ya nne ya enzi ya Ukristo. Enzi ya shaba nyeusi nchini Indonesia ilikuwa mapema zaidi na kilicho muhimu zaidi staarabu tofauti zilizokuwepo hapo pamoja; vilevile kulikuweco na vikundi vichache huku Indonesia vilivyoendelea kutumia zana za mawe hata baada ya karne ya 10. Kama zana za mawe ziko nchini Bukini au la ni jambo ambalo bado lina mvutano.

Ama kuhusu vyombo vya kusafiria, mara nyingi kumekuwa kukiulizwa kama Waindonesia wa elfia ya kwanza ya enzi zetu walikuwa na meli madhubuti zilizoweza kusafiri baharini kwa mwendo nurefu. Huko Mashariki mwa Bahari ya Hindi Deschamps ameonyesha kuwa kulikuwa na meli ambazo zingeweza kutumika picha za awali kabisa ya meli hizo zikionekana katika sanamu ya hekalu la Boroubudu, (Java karne ya 8) inayonyesha meli yenye mrengu, milingoti miwili na tanga.

Baada ya kuutambua mchango wa Waindonesia kwa ukaliaji wa Bukini, inabakia kazi ya kugundua njia mbalimbali walizozitumia. Waandishi wengi wameeleza

kuwepo kwanza kwa njia kuu ya Ikweta ya kusini²; ambayo kinadharia ilitoka Java hadi Bukini; mkondo huo wa Ikweta ya Kusini ukiwa na nguvu kati ya pwani za Java kusini na eneo jirani za Rasi Amber kuanzia mwezi wa Agosti hai Septemba. Sibree ameeleza maoni yake kwamba matumbawe yaliyotokana katika mlipuko wa Krakatoa yalisafiri kwa njia kama hii ambayo hatimaye iliyafikisha pwani ya Bukini.

Ingawa si kitu ambacho kilikuwa hakiwezekani kabisa, wazo la njia ya moja kwa moja kutoka vifungu visiwa vya Uhindimi hadi Bukini, halielekei kama lilitumiwa kwa sababu ambazo Donque anazieleza vizuri; ingawaje njia nyingine ya moja kwa moja ya Java na Bukini haina vipingamizi wakati wa majira ya baridi kusini, wakati ambapo vimbunga vya tropiki havipo, lakini yafaa tubaini kuwepo kwa vipengele vinavyoweza kutangua nadharia tete hii, kwani safari ya moja ka moja ni ya umbali wa karibu maili 4000 kwenye bahari ambapo hakuna hata mahali pa kutia nanga. Kwa hivyo, yatupasa tufikirie njia iliyopita kusini mwa India ya Sri Lanka Deschamps anadokeza taarifa kuhusu nuashambulizi ya maharania kwenye eneo hili, mnamo nusu ya kwanza ya elfia ya kwanza ya enzi za Ukristo.


Safari kutoka kusini niwa India hadi Bukini haina matatizo. Vile vile njia iliyopitia pwani za kusini mwa Afrika Magharibi ilifahamika tangu zama za *Periplus*; na wingi wa sarafu za Kichina zilizopatikana Siraf zinathibitisha umuhimu biashara baina ya Mashariki ya Kati na Mashariki ya Mbali. Kutoka Mashariki ya Kati, wasafiri walipitia pwani za Afrika, kama walivyokuwa wakifanya siku za ustawi wa Rhapta na yawezekana kwaniba uvumbuzi wa Visiwa vya Ngazija ulitokea baada ya ule Bukini.

Kama alivyoamini Deschamps, (na kama Kent pia alivyoamini kwa namna tofauti japokuwa ya udadisi), Wainonesia waliosalia sehemu za pwani ya Afrika ndio waliokuwa chimbuko la makao ya awali nchini Madagascar. Athari ya Wainonesia katika sehemu za pwani ya Afrika imepewa wasifu wa ziada. Mchanganyiko wa mimea ya Kimalasia iliyokuja Afrika kutoka Kusini-Mashariki mwa Asia hauthibitishi kwamba kuna uhusiano wa mimea hivyo na nchi ya Indonesia. Kulingana na *Periplus*, miwa na pengine minazi ilifika kila moja peke yake.

Kornell alidhani kwamba kwa ngalawa katika sehemu zote za Bahari ya Hindi unathibitisha ueneaji wa athari ya Wainonesia. Deschamps, kwa upande wake, aslisema kuiwa ngalawa hizi zinaonyesha njia iliyofuatwa na wahamaji waliowasili Bukini. Makisio ya Deschamps yana uzito, ingawa bado yanajadiliwa kwani uhusiano baina ya utamaduni wa Waswahili na utamaduni wa Wamalagasi unaweza kuwa ndio uliosababisha kuingia kwa maneno ya asili za lugha za kigeni.

Mwisho wa Uhamaji wa Wainonesia kuelekea Magharibi
Kuna uwezekano wa kukomeshwa kwa misafara ya Wainonesia wakati wa kuenea kwa athari ya dini ya Kiislamu, mnamo mwanzo wa elfia ya pili.

Safari za Wainonesia kupitia pwani za Afrika zilikoma mapema, lakini haina maana kwamba uhusiano ulivunjika baina ya nchi za Mashariki ya Mbali na zile za



28.2 *Ufinyanzi wa Kichina, Ustaarabu wa Voleman*

28.3 *Kaburi la Antalaotse la Antsohemebary*



Magharibi ya Bahari ya Hindi. Kinyume chake kuna ishara nyingi zinazodhihirisha ukuaji wa biashara hii ya Bahari ya Hindi, ambayokwa kiasi kikubwa ilikuwa mkononi mwa Waislamu waliokuwa wamekwishakuzifahamu vizuri njia zote za biashara. Ramani ya Ibn Majid inatoa latitudo za miji iliyokuwa katika pwani za Afrika na ile ya ajimbo ya Indonesia pamoja na vituo vingine kufikia mapana ya Bahari ya Hindi ambavyo viliweza kuvukwa kutoka upande mmoja hadi mwingine kwa siku thelathimi au arobaini.

Haiyumkiniki kwamba ingawa Waindonesia walikoma kutenibelea pwani ya Afrika, bado waliendelea kusafiri moja kwa moja kutoka Bara Hindi kusini na hadi Bukini, pengine kutokea maeneo ya kusini mwa India. Waindonesia-Mamboleo pengine nao walifuata njia hii.

Uhamaji wa Waafrika na Waswahili

Mjadala huu kuhusu nadharia mbalimbali za asili ya Kiindonesia za Wamalagasi zisitufanye tukasahau mchango muhimu na pengine mkubwa, wa Afrika, katika kuyastawisha makazi ya watu wa Bukini. Deschamps ametoa nadharia tete mbili katika jitihada zake za kufafanua uhusiano ulioko baina ya Waafrika na Waasia. Kwanza anasema kulikuwa na mchanganyiko wa kiutamaduni na kikabila katika eneo la pwani ya Afrika Mashariki. Pili, yawezekana Waindonesia walivamia nchi jirani za pwani ya Afrika kutoka Bukini. Kent, anauona uhusiano huu kama uliosababishwa na athari ya Waindonesia nchini Afrika, na hatimaye kutawaliwa kwa Bukini. Hata hivyo, wakati huu hatuna ushahidi wa kiakiolojia kutoka sehemu za pwani ya kusini (Tanzania -Msumbiji), na binafsi sikubaliani na nadharia hizi isipokuwa zikitazamwa tu kama nadharia tete. Kuna uwezekano kwamba uhusiano baina ya Waafrika wa Waindonesia ulianza katika Visiwa vya Ngazija au Bukini ya Kaskazini.

Baadhi ya mawazo yanayorudiwa mara kwa mara kwamba mbilikimo ndio waliokuwa wenyeji wa asili Kisiwani Bukini, hayalingani na ushahidi wa kiakiolojia wala wa kibaharia. Kisiwa cha Bukini kilijitenga tangu enzi za na ni jambo lifahamikalo kuwa nabilikimo si mabaharia, wala hawakushiriki katika harakati za ukuzaji na unedelezaji wa ustaarabu wa Kibaharia wa Waswahili. Mbali na hayo, nakabila yao, kama lile la Waniikea waliodhaniwa kuwa kundi la mwisho la Mbilikimo kuishi Bukini, si wadogo hivyo.

Ni maoni yangu kwamba Wamalagasi wenye asili ya Kiafrika ni Wabantu ambao pengine walianza kuwasili hunio kisiwani mnanio karne ya tisa kama Waindonesia, lakini haelekei kuwa uhamaji wa Waafrika uliendelea hadi wa nyakati za karibuni za historia (karne ya kumi na sita). Yaelekea kwamba Waafrika wengi waliwasili wakati mmoja na katika hali sawa na zile za majilio ya Waswahili Waislamu, au wasiokuwa Waislamu.

Ijapokuwa msamiati mwingi wa Kimalagasi ni ule wa Kiindonesia, tusiusahau mchango wa Kibantu. Hali kadhalika, lugha ya Kreoli inayotumiwa Antilles, Picha



28.4 *Sanamu ya Antsary: Sanaa ya Antranasy karibu na Ngome ya Dauphin*

ambayo ina asilimia 95 ya maneno ya Kifaransa, na maneno machache tu ya Kiafrika inapaswa kutiliwa maanani. Mchango wa Kibantu katika Kimalagasi uko katika pande mbili. Upane mmoja unahusu msamiati, na wa pili ni juu ya mtindo na muundo wa maneno. Maneno ya Kibantu yamejikita kote katika lahaja za Bukini. Ni dhahiri kuwa makazi ya Waafrika kisiwani Bukini hayakuanzishwa hivi karibuni, athari yao inaonekana katika misingi asilia ya ustaarabu wa Kimalagasi. Lugha ya Kimalagasi ina fani halisi zinazothibitisha athari asilia za Kibantu. Athari hii ni kubwa mno na ni ya namna ambayo haielezeki mpaka kwanza kuelezwe tabaka la Waafrika wa Kibantu miongoni mwa Wamalagasi. Ingawa kwa wakati huu haiwezekani kuelezea mchango wa kiutamaduni, lakini waandishi wengi wamekuwa wakizitilia maanani hali za maingiliano baina ya Madagascar ya kaskazini na ya magharibi. Katika kitabu chake Mellis anasisitiza tofauti zilizoko kati ya watu wanaoishi kwenye upwa wa bahari (*antandrano*) na wale waishio bara (*olo boka antety*). Tofauti hizi zinaonekana katika raratibu zao za mazishi.

Uhamaji wa Wabantu wa pwani kuanzia karne ya tisa unatufahamisha mchango wa Waafrika katika makazi ya Bukini; lakini inatupasa tueleze sababu zilizofanya lugha ya Kiindonesia kutumika kama lugha ya mawasiliano. Baadhi ya Wabantu lazima waliingiliana na Waindonesia na yawezekana kwamba baina ya Waafrika tofauti waliokuwa wakiongea lugha au lahaja tofauti, pengine Kiindonesia kilikuwa kinafaa zaidi. Hata hivyo, Bukini lazima paliendelea kuwa mahali pa maingiliano ya lugha mbalimbali; hasa upande wa pwani karibu na Baly, na Maintirano (Bambala ya Mariano); upande wa Tsiribihina (kulingana Drury); na miongoni mwa baadhi ya makabila ya Wazimba sehemu za bara ya kisiwani (kulingana na Birkeli na Herbert). Maisha ya Wavazimba wa kale yalitegemea uchumi wa kizamani. Wazimba wa Pwani walikuwa wavuvi; wale waliokuwa wakiishi bara walitegemea vyakula vya mwitu kwenye mazingira yao kuchuma matunda mwitu aina ya fursadi. Kuwinda na kutafuta asali kulitoshleza mahitaji yao. Mwandishi Drury alisema kwamba Wavazimba wa Tsiribihina walikuwa wavuvi wa samaki wa mtomi. Uchunguzi wa machimbo umeonyesha malundo ya kombe zilizoliwa na hao wachuma matunda ya mwitu karibu na sehemu ya Ankazoaka na Ankatso.

Uhusiano kati ya Waafrika na Waindonesia ulianza awali ya makazi humo Bukini. Mnamo karne ya kumi, Wabantu wachache wa pwani walikuwa wamekwisha kusilimishwa. Jambo livutialo kuhusu uhusiano huo ni kuwa Waislamu na Bukini wanashirikiana na makabila ya Magharibi pamoja na pwani za Kaskazimi-Magharibi katika umoja wa ngano inayosimulia chanzo cha asili yao yaani Ngano ya Mojomby, au "Kisiwa kilichopotea". Ngano hii nimeifanua katika maandishi yangu mengine kulingana na vile nilivyosimuliwa na Waantalaotse wa Ghula ya Boina. Kulingana na wasimuliaji wangu, Selimany Sebany na Tonga, wahenga wa wenyeji wa Kajembi na Antalaotse, waliishi pamoja katika kisiwa kilichokuwa baina ya pwani ya Afrika na Visiwa vya Ngazija. Walikuwa ni wafanya biashara na walikuwa ni Waislamu.

29

Jamii za kusini mwa sahara Katika enzi ya awali ya chuma

Katika sura zilizotangulia tulijishughulisha na akiolojia ya sehemu mbalimbali za Afrika Kusini mwa Sahara. Utafiti uliofanywa ulianza majira ya elfia ya mwisho kabla ya enzi za Ukristo na kuendelezwa kwenye elfia ya kwanza ya enzi za Ukristo. Madhumuni ya sura hii ni kuchunguza baadhi ya mifumo niaalumu inayoonekana kuendelea katika historia ya Afrika nyakati hizi. Majira haya yalishuhudia mabadiliko ya kanuni yaliyojitokeza kote. Uchumi ulibadilika kutoka ule wa kutegemea zaidi maeneo ya ardhi na kufikia aina ya uchumi anibao uliweza kuzidhibiti njia za kupata chakula kutokana na mimea na wanyama pia. Teknolojia pia ilibadilika kutoka kwenye utumiaji wa mawe na miti na kwenda kwenye tekiolojia tata zaidi ya kutumia metali mbalimbali pamoja na mawe. Wakati huu kulikuwa kumeshawekwa misingi ya jamii za Kiafrika kama tuzijuavyo hivi leo; mipaka iliyokuwepo baina ya watu wenye lugha mbalimbali ikabadilika kidogo, idadi ya watu ikaongezeka kwa kiasi kikubwa na kwa haraka, na makundi ya kijamii na ya kisiasa yalianza kupata mfumo wa hali ya juu hasa wakati ambapo mataifa ya Kiafrika yalipoanza kujitokeza. Lakini, kwa namna fulani, manibo kadha ya msingi kuhusu idadi ya watu kusini mwa Sahara yalikuwa yameshawekwa misingi tangu katika robo ya mwisho ya elfia ya kwanza ya enzi ya Ukristo.

Shida mojawapo inayotatiza maelezo fasaha ya mifumo iliyochimbuka wakati huo ni kwamba utafiti wa akiolojia haukuwa sawa katika sehemu zote. Ziko sehemu kubwa ambazo hazijachimbuliwa kabisa hasa katika baadhi ya nchi kubwa kama vile Angola, Msunbiji, Zaire, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Cameroon, Dahomey, Ivory Coast, Mali, Upper Volta, Sierra Leone na Bukini. Na hata katika zile nchi ambazo zimefanyiwa utafiti mkubwa, kama vile Senegal au Chad, utafiti wenyewe unejishughulisha na yale yanayohusiana na nchi hizo tu. Ni muhimu kufahamu kuwa ingawa mashirika yaliyojishughulisha na zana za kale yalianza karne ya kuni na tisa katika sehemu ya Afrika ya Kaskazini (k.m. Misri, 1058), baadhi kubwa ya nchi zilizoko kusini mwa Sahara zimeanzisha utafiti tokea wakati nchi hizo zilipopata uhuru na kuanzishwa kwa majumba ya niakumbusho ya taifa na vyuo vikuu. Kwa muda wa miaka kumi iliyopita maendeleo ya "kronolojia ya redio-kaboni" yamebadilisha ujuzi wetu wa kipindi cha awali cha enzi ya chuma na kwa hivyo

hutuwezesha kutoa kauli za jumla kuhusu kipimo cha wakati uliotumika katika maendeleo mbalimali ya kiuchumi.

Uvumbuzi wa Madini

Shaba ya Nyekundu

Shaba ilichimbuliwa kwa mara ya kwanza huko Mauritania kwenye robo ya kwanza ya elfia ya mwanzo kabla ya enzi za Ukristo. Umbo la vyombo vya shaba nyekundu vinavyopatikana nchini humo vinatufahamisha kwamba sababu za uchimbaji wa madini hayo zilitokana na maingiliano baina ya Mauritania na Moroko. Kuna maelezo machache tu kuhusu umbo la machimbo ya asili, ingawa inaaminiwa kwamba hayakuwa na kina kirefu. Machimbo ya Mauritania ndiyo ya pekee yanayohitibisha uhakika wa kuchimbuliwa kwake kabla ya +1000. Madini mengine ya shaba nyekundu yanapatikana nchini Mali na Niger katika sehemu za Nioro na Tekedda. Madini haya yalikuwa yakichimbuliwa katika elfia ya pili ya enzi za Ukristo. Lakini tarehe ya uvumbuzi au mwanzo wa machimbo hayo haujulikani.

Kwa mujibu wa ushahidi unaotokana na waandishi wa Kiarabu na maandishi mengine ya zamani, ni kwamba shaba nyekundu ilikuwa ni bidhaa katika biashara ya eneo la Sahara tangu katika elfia ya kwanza ya enzi yetu, ilikuwa inasafirishwa hadi kusini na huenda kwa kubadilishwa na dhahabu iliyokuwa ikipelekwa kaskazini. Uvumbuzi wa vidongo vya madini ya Macden Idjafen haku magharibi ya Sahara ni uthibitisho wa jinsi biashara hiyo ilivyokuwa muhimu katika kipindi kilichofuata (mnamo karne ya kumi na moja au kumi na mbili ya enzi zetu). Kitu muhimu zaidi katika kukielewa kiasi cha biashara hiyo ni baadhi ya zana zilizotoka Igbo - Ukwu, nchini Nigeria Mashariki. Ikiwa vyombo hivi ni vya karne ya tisa, kama alivyodai mchimbaji Thurstan Shaw pamoja na Wai-Andah katika sura ya ishirini na nne, basi hiyo ni dalili kuwa biashara hiyo ilikuwa imeenea mnamo karne ya nane au ya tisa ya enzi zetu; kuenea ambako kunatufanulia sababu za kuwako kwa vyombo vingi vya shaba nyekundu na uwezekano wa kuwako kwa zana nyingine ambazo hazijavumbuliwa katika sehemu mbalimbali.

Chimbuko muhimu la shaba nyekundu lililochimbwa wakati huu lilipatikana kwenye eneo la Shaba, Zaire, ambako machimbo ya Sanga na Katoto nchini Zaire yamedhihirisha idadi kubwa ya vitu vya shaba nyekundu. Hata hivyo ni muhimu kufahamu kuwa katika mgawanyiko wa kitamaduni wa pande tatu uliopendekezwa na mchimbaji Nenquin katika kipindi cha awali kabisa cha Kisali unahusiana na makaburi ishirini na saba, ambayo mawili tu kati ya hayo ndiyo yaliyokuwa na vipande vya shaba nyekundu. Yaani ni kwamba ingawa shaba nyekundu ilikuwa ikifuliwa na kutengenezwa mapambo wakati wa kipindi cha Kisali, kuanzia karne ya saba hadi ya tisa enzi zetu, lakini haikuwapo kwa wingi.

Ukanda wa shaba nyekundu wa Zambia kaskazini ulikuwa akichimbwa wakati huu. Tarehe ya machimbo hayo ni $+400 \pm 90$ kama ielezwavyo kutoka Kansanshi.

Hata hivyo, katika wakati huu, shaba nyekundu zilipatikana kwa wingi upande wa Zambia kusini kuliko Zambia kaskazini vitu vya shaba nyekundu vya mwanzo kutoka Zambia kusini labda vilipatikana kutoka eneo la Sinoaia la Zimbabwe na vyanzo vingine vya Zambia Mashariki. Hadi wakati huu, hatujui chochote kuhusu uchimbaji wa madini katika sehemu hizi. Sehemu zingine katika Afrika shaba nyekundu ilikuwa adimu sana haikupatikana katika Afrika ya Mashariki, mpaka baadaye kabisa.

Chumvi

Chumvi ilihitajika kwa wingi wakati maisha ya kilimo yalipoanza. Wawindaji na wachum vyakula mwitu walijipatia chumvi mwilini kutokana na wanyama waliowawinda na chakula kibichi walichokichuma. Chumvi inakuwa bidhaa muhimu katika nchi zenye ukame ambako vyakula vibichi havipatikani na ambako watu hutokwa na jasho kwa wingi. Hali kadhalika chumvi huhitajiwa zaidi na jamii zinazotegemea aina chache za vyakula, kama ilivyo kwa wakulima wenye ardhi ya rutuba. Haijulikau ni lini chumvi ya Taghaza na Awlil katika eneo la Sahara ilipoana kutchimbwa. Maandishi ya Waarabu katika nyakati za robo ya mwisho ya elfia ya kwanza ya enzi zetu yanadhihirisha kwamba chumvi ilikuwa bidhaa mojawapo katika biashara ya Sahara. Inawezekana kuwa utoaji wa chumvi ulikuwako tangu zama za uchimbaji wa shaba nyekundu pamoja na ustawi wa makao ya Tishit nchini Mauritania. Katika sehemu zote mbili, maisha ya maskani na kijamii yalilazimisha matumizi ya chumvi. Kuna habari nyingi kuhusu shughuli za uchimbaji madini katika kipindi cha zamani, ambazo zitajadiliwa katika juzuu zifuatazo za historia hii. Lakini hakuna habari zozote wakati huu. Inawezekana kwamba katika wakati huo, uchimbaji ulikuwa ukifanywa kwa kutumia mbinu rahisi. Kwenye sehemu nyingi za Sahara chumvi ilipatikana juu ya ardhi kama mashapo yaliyokaushwa na hali ya ukame baada ya mwaka -2500. Labda wanadamu walichunguza yale mabonde ya maziwa, vidimbwi na mabwawa yaliyowavutia wanyama wa mwituni. Chumvi inayozagaa juu ya ardhi inaonekana wazi kwa sababu ya rangi yake.

Chuma

Madini ya chuma yalikuwako nchini Swaziland zamani za kipindi cha kati cha enzi ya mawe. Madini hayo yalitumiwa kama kiimi cha rangi ya mwili. Inaonekana kuwa wakati huu viini hivi vya rangi za mwili, na ngeu za aksaidi ya chuma iliyotumiwa pia kama rangi ya mwili na baadaye kutumiwa kwa kuchorea mapambo maweni, zilitafutwa kwa dhati katika enzi ya mawe. Kipande cha madini haya kilifikishwa kwenye Bonde la Olduvai na watumia zana wa mwanzo kwenye Enzi ya Mawe. Ilipofikia wakati wa mwisho wa Enzi ya mawe manganizi, Speklati na hematiti zilikuwa zinachimbwa kama kawaida huko Zambia, Swaziland na kaskazini ya Rasi. Katika baadhi ya uchimbaji uliofanywa na Doornfontein inadhihirika kwamba uchimbaji ulikuwa ukiendelea mara kwa mara. Kuna kiasi cha tani 4,5000 za speklati zilizopatikana kwenye chemba na vijia vilivyokuwepo ndani ya migodi.

ldadi hiyo inawezekana ilichimbuliwa na makabila ya Wakhoisan kutoka karne ya tisa ya enzi yetu na kuendelea. Kuwako kwa madini hayo na ujuzi wa madini ya metali kulichochea ukuaji wa haraka wa teknolojia ya chuma mnamo nusu ya kwanza ya elfia ya kwanza ya enzi zetu.

Kwingineko kusini mwa Sahara hastuna dalili dhahiri za uchimbaji wa madini ya chuma. Inaelekea kwamba chimbuko kubwa la madini ya chuma lilisambaa tu katika ardhi ya nchi za eneo la joto. Hata hivyo, chuma nyororo kilitumiwa katika sehemu ya nchi ya bonde la Casamance nchini Senegal na huko Machili, Zambia..

Dhahabu

Kuna hakika kwamba madini ya dhahabu yalikuwa yakichimbwa Afrika ya Magharibi katika kipindi kinachojadiliwa na nyingine ikikusanywa na tope la mito. Ingawa maandishi ya Kiarabu hudokeza habari kuhusu machimbo haya, hadi sasa hakuna madini wala machimbo yaliyovumbuliwa nchini Afrika ya Magharibi wala tarehe ya machimbo hayo kutolewa. Hakuna ushahidi ulio wazi kuhusu utaratibu wa usafishaji wa madini yalivyopatikana. Taratibu hizo huenda zilifanana na zile zilizofafamuliwa katika maandishi ya vipindi vilivyofuata. Eneo lenye ushahidi wa uchimbuaji dhahabu ni lile lililoko karibu na maeneo ya maji ya mito ya Niger na Senegal nchini Guinea na Mali, na ambayo yanajulikana kwa majina ya Bambouk na Boure. Uko ushahidi bora zaidi (umejadiliwa na Phillipson katika sura ya 27), kuhusu kuwako kwa milango ya kuingilia ndani ya migodi ya mashariki-kaskazini mwa Zimbabwe; lakini hakuna ushahidi wa kuthibitisha kama shughuli za madini hayo ni za zamani kabla ya karne ya nane au karne ya tisa ya enzi zetu. Yaelekea kuwa madini hayo yalipondwapondwa kwa mawe ya kusagia.

Jiwe

Uchimbaji wa mawe ulitekelezwa kwa madhumuni mbalimbali. Jambo muhimu ni kwamba uchimbaji huo ulitoa nyanzo kwa zana za mawe ya kusaga, mawe ya kukwatuliwa; na kwa kuchongea mawe ya kusagia. Jamii nyingi zilitumia majabali yaliyoubika kama mawe ya kupazia katika kazi zao za kila siku. Watu walipeleka nafaka zao kwenye majabali hayo ambapo waliweza kukausha vyakula na kusaga nafaka zao na mboga. Majabali ya aina hiyo hayakupatikana kila mahali. Kwa ajili hii mawe ya kusagia yalitafutwa na kusafirishwa masafa marefu. Eneo lote la Sahara-Kusini lina mashimo kadiri ya upana wa sentimita 10 mpaka 12 na urefu wa sentimita 50. Hayo ni mashimo yathibitishayo mahali ambamo mawe yalitumiwa kuundia mashoka, patasi na tezo. Kuna uwezekano kwamba utaratibu wa kusaga mawe japo kwa kiasi kidogo, kusaga na kuuza jiwe lililokwisha tengenezwa au lile ambalo bado halijakamilika, uliendelea katika kipindi chote hali ukipungua nguvu kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya chuma badala ya mawe. Kuadimika kwa zana na bidhaa za mawe kuliendelea polepole katika sehemu nyinginezo ambazo hata kufikia elfia ya pili ya enzi zetu, bado zana hizo zilikuwa zikitumika. Ni zana chache za mawe ya

kusagwa zinazopatikana Afrika ya Mashariki, ingawa huko Afrika ya Magharibi ziko kwa wingi.

Utafiti wa mawe ya thamani ya kutengenezea shanga ulikuwa ukiendelea, ijapokuwa shughuli hizo bado hazijachunguzwa kwa ukamilifu. Mawe yaliyopatikana kwa wingi ni ya vito vya akiki, ageti, mawe ya "jasapa", na mawe ya kifuwele. Shanga zilizotengenezwa kutokana na vito hivi zilipatikana ndani ya makaburi kama yale yaliyoko kwenye eneo la pango la Mto Njoro nchini Kenya ambazo tarehe yake inasemekana kuwa mi karne ya kumi kabla ya enzi zetu. Shanga nyingine zilipatikana katika sehemu zilizokuwa makao ya watu.

Huko Lantana nchini Niger, machinibo ya mawe mekundu aina ya "Jaspa" yanaamimiwa kuwa ni ya kale sana, lakini haiwezekani kakadiria tarehe yake hasa. Mawe hayo ya jaspa yangali yakiendelea kuuzwa nchini Nigeria kwa matumizi ya kutengenezea shanga. Kwa jumla, shanga zilikuwa haba, lakini utafiti wa mawe ya shanga unadhahirisha harakati maalumu za kutafuta aina ya mawe fulani yaliyofahamika. Shanga zilianza kutengenezwa tangu enzi ya mawe; ufundi huo uliendelea hadi kufikia enzi ya chuma hadi baadaye, ambapo nafasi yake ilichukuliwa na shanga za bei rahisi, katika biashara ya shanga zilizotengenezwa kwa kowa.

Biashara

Aina fulani ya mabadilishano imekuwa ikifanyika kati ya miakabila, pengine tangu zama za awali za enzi ya mawe. Mabadilishano ya mawe ya kung'aa au ya vito na asali badala ya nyama, na pengine hata wanawake, labda yalionyesha dalili ya kujumuika ili kutafuta chakula. Uwezekano huo unatokana na mifano ya wawindaji na wakisanyaji chakula wa siku hizi. Mabadilishano kama hayo, ambayo yalikuwa na umuhimu wa kidini na kiuchumi, yangekuwa ya kawaida kadiri jamii zilivyostawisha maisha ya kilimo, ingawa hata katika nyakati za niwishi za enzi ya mawe wavuvi na wakisanyaji wa vyakula baharini au wawindaji lazima walikuwa wakiishi maisha matulivu. Hali hii ya maisha ilihitaji zana za mawe na zana nyinginezo, ambazo zilikuwa hazipatikani katika eneo hilo. Zana nyingine zinazohitaji ujuzi na ustadi, kama vile miundu, zilikuwa kati ya bidhaa za biashara. Lakini ni vyema kuhitimisha kuwa kilimo, kikimaamisha kilimo cha vipindi au msimu, kingeweza kuwa kinachangia kuongeza biashara. Sehemu kubwa ya biashara hii labda ilikuwa kwenye kiwango kidogo na niawanda ya sehemu jirani, lakini ingejumuisha bidhaa kama vile

chumvi, aina fulani ya mawe, na baadaye shanga, zana za chuma; kola; miniea iliyotumika kuwa ni dawa au kwa mambo ya kimila, nyama kwa jamii zenye ardhi ya rutuba, zana maalumu au sumu ya kuwindia wanyama na kuvulia samaki, samaki wa kukaushwa, pamoja na bidhaa nyinginezo za tunu kama mibegu, kucha za wanyama, mieno, vito vya mawe ya thamani, mifupa na kadhalika. Vitu hivi vya tunu bado vinahusishwa na nambo ya uchawi, na hadi leo vingali vikiuzwa katika vibanda vichache vya masoko ya Afrika ya Magharibi. Isipokuwa kwa bidhaa chache, kama zana za mawe, mawe ya kusagia, na chumvi, ambavyo tayari viniekwisha

zungumziwa katika sehemu iliyotangulia, hakuna habari zaidi kuhusu biashara hii.

Mkondo wa biashara uligeuka wakati wa chimbuko la matumizi ya metali. Shaba nyekundu na dhahabu zilitumika kwa wenyeji kuliko mawe na zilihitajika mno na jamii zilizoishi kaskazini mwa Sahara, na wale wa Mashariki ukingoni mwa Bahari ya Hindi. Katika wakati huu, biashara ilikuwa bado haijasambaa sana kufikia eneo lote la Sahara, ingawa kulikuwa kumeshawekwa mfumo wa biashara hiyo. Vile vile tuna ushahidi kidogo kuhusu masoko na vituo vya ugawaji wa bidhaa kwenye eneo la Sahara-Kusini, ingawa maandishi ya Waarabu yanatupa fikra ya kwamba nchini Ghana, katika mji wake mkubwa wa kale, masoko hayo yalikuwako kabla ya biashara kuongezeka kutokana na harukati za Waarabu kuzitaka nchi za Afrika ya Kaskazini.

Bidhaa za shanga za kowa (glasi) zilipatikana katika tarafa mbali mbali nchini Zambia. Shaba ilipatikana Zaire na Zimbabwe, kwenye nyukati za kipindi cha mwisho cha elfia ya kwanza. Aina zote mbili za bidhaa zililetwa kutoka nchi za nje.

Masuala yanayojitokeza Katika Historia ya Afrika

Katika robo ya Mwisho ya Elfia ya Kwanza ya Enzi za Ukristo

Ni muhimu kuchunguza ikiwa, kutokana na data nyingi iliyotolewa kwenye sura nane zilizopita hitimisho lolote linaweza kufikiwa kuhusu hali ya jamii ya Kiafrika mnamo mwisho wa kipindi cha mwanzo cha enzi ya chuma. Kipindi hiki kilishuhudia mabadiliko ya kiuchumi ya nchi za Afrika kusini mwa Sahara kutoka ule wa uwindaji na uchumaji wa vyakula vya mwanu hadi ule wa kutegemea uchumi wa kilimo. Idadi ya watu iliongezeka; hivyo kuendeleza maisha matulivu ya vijijini na kuundwa kwa makundi ya kijamii. Ni vigumu kusema kwa yakini mfumo wa kijamii ulikuwa wa namna gani. Lakini inaelekea kwamba watu waligawanyika katika vijiji vidogo kulingana na ukoo mmoja ama koo mbili za watu. Idadi ya watu huenda ilikuwa ndogo kwenye sehemu nyingi za nchi kufikia kiasi cha watu wachache kwa kila mraba wa kilomita moja. Baada ya harakati zilizosababishwa na matumizi ya chuma, ambayo yaliruhusu usafishaji wa maeneo ya miti Afrika maskani ya jamii yaliendelezwa. Kuna ushahidi wa jamii inayoongea lugha moja kutengana na kuishi katika sehemu mbalimbali za nchi pamoja na ushahidi wa mitindo ya ufinyanzi wa vyungu iliyongezeka na mapambo ambayo yaliendelezwa katika sehemu nyingi mnamo +600 hadi +1000. Makisio ya kidemografia ambayo yamekitwa kwenye ushahidi wa kihistoria uliopo Afrika Kaskazini na data za kiethnografia na zile za sensa ya kikoloni, yanaonyesha idadi ya watu chini ya milioni kumi kwa eneo lote la kusini mwa Sahara kabla ya +1000. Kama ishara za mapokeo simulizi kuhusu mabadiliko katoka kwenye jamii zenye nasaba kwa mama kwenda kwenye nasaba za mama miaka mia tano iliyopita yanaweza kuwa kielelezo, hasa Afrika Mashariki, basi tunashughulika zaidi na jamii za nasaba kwa mama kwenye sehemu kubwa ya maeneo ya Afrika ya tropiki.

Katika wakati huo mi vigumu kugundua imani za kidini kuliko katika wakati wa

kale za uwindaji na uvunaji vyakula vya niwitu, mwishoni mwa enzi ya niawe; na hii ni kwa sababu jamii za enzi ya uwindaji na unichunaji vyakula niwituni ziliacha vidokezo kwenye sanaa zao za uchoraji juu ya niawe. Yawezekana kuwa wakulima wa awali walichora kwa kupaka rangi maweni. Uchoraji huu unawezakuchakuliwa kuwa ni chimbuko la mitindo ya sanaa ya Afrika ya Kati na Mashariki, hasa katika eneo la ziwa Victoria na Zambia. Hakuna fununu yoyote inayoonyesha tarehe ya chanzo cha sanaa hii, bali kumalizika kwake kunafahamika. Mila na desturi za nuzishi ni vipengee vinavyodhihirisha imani fulani za kidini. Inaelekea vyakula vinavyozikwa na mtu kaburini vinaambatana na imani ya jamii kwanba vitahitajika ahera. Lakini haya siyo naelezo pekee yanayoweza kupatikana. Ukubwa au udogo wa kaburi, uzuri wa bidhaa za naiti kaburini na sherehe za mazishi ya fahari husaidia kupambanua kama tabaka la jamii ya yule maiti ni kiwango cha kisiasa, kiuchumi, kijamii au ikiwa ni jamii inayofuata taratibu za kimila na desturi. Hadhi ya mazishi pia ni kielelezo cha kukitambua kizazi cha ukoo wa waliofiwa. Katika karne hii ya ishirini ziko desturi za mazishi zilizofanana na hizo desturi tunazozitungumzia. Yako makabila ambayo, ingawa watu wake hawana hisia wala imani ya kidini, bado wanatekeleza desturi hizi za kuwazika watu wao kwenye makaburi yaliyojengwa kwa nakshi. Kuwako kwa makaburi ya vichunguu na yale yaliyojengwa minara hakuthibitishi kuwako kwa imani ya kidini, ana katika Mungu mmoja au kundi la miungu. Lakini desturi hii inathibitisha wazi imani ya jamii kuhusu maisha ya baadaye huko ahera, pamoja na kuonyesha niwendelezo wa utawala wa kisiasa, au wa kundi teule.

Wakati huu tawala za jamii mbalimbali zilianza kuzuka. Tawala hizo zilijikita katika vituo viwili muhimu. Kituo cha kwanza ni ukanda wa Sudan na cha pili ni eneo la Afrika ya Kati kuzunguka chemchemi za mto Lualaba. Ukanda wa Sudani ulikuwa na maeneo matatu muhimu; -eneo la Ghana kusini mwa Mauritania na Senegal; eneo la bara la Delta ya mto Niger upande wa juu wa Segu; na eneo la Ziwa Chad. Vituo hivi vilijengeka katika mahali ambako biashara ilikuwa imeanza kustawi na kilimo kuendelezwa mapema zaidi kuliko katika nchi za kusini. Masimulizi ya kimapokeo na desturi za kundi tawala zilitoa dini tawala ambazo zingeweza kusaidia kuhakikisha na kuthibitisha nguvu za ajabu za mamlaka yake. Kiongozi wa lile kundi la wateulc, hata kama siye kiongozi mteule asilia huchukuliwa hivyo na kuaminiwa hivyo ikionekana kuwa ni mzaliwa wa ukoo wa kiongozi asilia au akionekana kuwa ni kivuli cha yule kiongozi asilia; kwa hivyo hupewa wasifu wa mbashiri. Wasifu huo wa uungu wa kiongozi si za asili bali zinajengeka katika fikra za watu polepole kwa kukusudiwa au wakati mwingine uungu huo wa kiongozi hujijenga mawazoni bila ya kakusudiwa. Jambo hili husababishwa na hisia za raia kutaka kuhifadhi unyofu na uadilifu wa chifu.

Tunapoacha nadharia tete na kuingilia mambo ya hakika, tutaona kwamba kuna eneo moja tu ambalo tunaweza kusema kwa hakika kwamba lilikuwa na utawala wa kifalme, hasa katika miaka hii tunayoizungumzia. Eneo hili lilikuwa upande wa ukingo wa Magharibi ya Sudan ambako ufalme wa Ghana ulikuwa umeshajikita

mnamo +700. Yamkinika ufalme huo ulianza kuchipuka zamani za miaka elfu kabla ya hapo. Ukuaji wa ufalme huo ulisababishwa na mambo yafuatayo:- Ghana ilikuwa na fursa ya kudhibiti madini ya thamani (shaba nyekundu, chuma na dhahabu katika utaratibu wa uchimbaji wake). Nchi hii ilidhibiti biashara ya chumvi. Vile vile Ghana ilikuwa katika eneo la msingi wa maendeleo ya maisha ya kilimo kama yanavyowakilishwa na mfululizo wa Tichitt. Taarifa kamilifu za maelezo juu ya ufalme wa Ghaua zitapatikana katika juzuu ifuatayo. Mbali na hayo, si jambo la ajabu kwamba ukuaji wa ufalme wa Ghana ya kale na ujengaji wa megalithi ya Senegambia na vichunguu vya makaburi ya kitajiri nchini Senegal yalikuwa maendeleo ya wakati mmoja. Pengine hizi zilikuwa sehemu zilizohusiana na namua moja ya kukua kwa uchumi.

Sura zilizotangulia zinadhihirisha kuwa mwisho wa kipindi kinachozungumziwa hapa haulingani na vile unavyoonekana katika nchi za kaskazini mwa Afrika. Majilio ya Waarabu kaskazini mwa Afrika, hatimaye yaliathiri kwa dhahiri au kwa hali isiyokuwa dhahiri mahali kwingi upande wa Afrika ya Magharibi na Mashariki. Tumeona kwamba kufikia mwaka +800 sehemu nyingi za Afrika zilikuwa zimo katika enzi ya chuma. Misitu ilikuwa inaanza kukatwa kwa ajili ya kuendeleza kilimo katika nchi za Afrika ya Magharibi na kusini mwa Afrika ya Kati. Idadi ya watu ilikuwa ikiongezeka. Hatua ya kwanza ya mapinduzi ya kilimo ilihusika na upanuzi wa makundi madogo ya wakulima waliokuwa kwenye ardhi zenye rutuba na ambao walijipatia protini yao kutokana na matamizi ya mbinu zao za jadi ya enzi ya mawe, kama watu wao wa kale walivyokuwa wawindaji na wakusanyaji mazao-mwituni. Zana zao nyingi za kuwindia zilikuwa sawa na zile za watu wa kale kama vile nyavu, mifupa na ndoana za pembe za samaki, mirembe za mishale ambayo mara nyingine huwa imepandwa na maikrolithi ama vipande vya pembe za kulungu zilizochongwa ncha, ama vigumba vingine vyenye maumbile hayo. Wakati mwingine zana hizi zilibadilishwa kwa matumizi ya zana ghali ua madhubuti zaidi na mishale yenye vigumba vya chuma na ndoana za samaki zilizotengenezwa kwa njia rahisi. Taratibu na imani yao ya kidini pia inaonekana ilitokana na watu waliowatangulia. Hata hivyo, kadiri maisha yao yalivyogeuka na kuwa ya kutulia, kinyume cha maisha ya kuhamahama ndivyo walivyostawisha imani mpya zinazohusu imani za kilimo pamoja na metali. Baadhi ya imani hizi zinaweza kuwa zilisambazwa na watu walioleta imani hizo za kilimo na metali. Wakulima wa enzi ya chuma walikuwa na kipaji cha kufinyanga vyungu, kuwamba ngoma, kusuka vikapu, kuyeyusha vyumba na kufua zana. Dini zao zilianza kujishughulisha na imani za miungu waumbaji. Taratibu za imani zao zilijikita kwenye ahakikisho wa wokovu kutokana ua mazingira ya maumbile ambayo yanaweza kumdhuru mkulima zaidi. Inaonekana kuwa mila na muziki wao ulikuwa wenye ufafanuzi. Utamaduni wao wakuonekana ulikuwa na namna mbalimbali na ufahamu wao wa jadi na mwelekeo wa kijamii ulikuwa umestawishwa kwa uthabiti. Mabadiliko ya kanuni yalitokea miongoni mwa jamii na hatimaye yaliathiri vipindi vyote vilivyofuata vya historia ya Afrika.



Hitimisho

Katika juzuu hili jitihada zilifanyika kadri ilivyowezezana ili kuonyesha mikondo mikuu katika historia ya awali ya Afrika, mabadiliko makuu yaliyotokea, mahusiano ya kimsingi kati ya maeneo mbalimbali ya bara la Afrika, na hali ya jamii na vikundi vya Waafrika katika kipindi kinachozungumziwa.

Juzuu hili linadokezea juu ya muundo wa kufanyia utafiti, na njia kuu zinazoweza kutumiwa ili kufanyia utafiti huo. Hata hivyo, tayari inawezekana kufikia mahitimisho fulani na kutambua baadhi ya nadharia, ingawa yafaa kususitizwa kuwa bado kuna mengi yanayohitaji kufanyika na kuwa kunahitajika kufanywa uchunguzi mkubwa na wenye kina kirefu.

Sura zinazozugumzia Misri zimedhihirisha kuwa kabla ya elfia ya tatu kabla ya enzi zetu, Misri ilikuwa imefikia kiwango cha juu cha utambuzi wa mambo hali za kijamii na cha utajiri, ukilinganisha na sehemu nyingi nyinginezo za dunia. Utamaduni wa kale wa Misri, mbali ya kuwa ni wa zamani, na unaotokana na hali ya nchi yenyewe, - ambao kila uchao ulikuwa unanzisha mambo mapya - ulidumu kwa kiasi cha miaka elfu tatu. Utamaduni huo haukutokana tu na kuwa na mazingira muafaka, bali pia ulitokana na juhudi za kuyadhibiti mazingira hayo na kuyatumia kwa manufaa. Bila shaka vipengee vya maumbile vilikuwa na nafasi muhimu na iliyojitokeza katika uendelezaji wa ustaarabu wa kikale wa Misri. Lakini, kwa upande mwingine, nafasi hii ilisaidiwa na ikawa na athari kutokana na juhudi za Wamisri kudhibiti mazingira yao na kuyashinda matatizo yaliyojitokeza.

Ingawa Misri iliathiriwa na utamaduni hususa kutoka Mashariki, makala yaliyomo katika juzuu hili yanaonyesha jinsi ustaarabu wa Misri ulivyotokana na msingi wa Kiafrika kwa kiasi kikubwa na pia kuwa Misri, ambayo ni sehemu ya Afrika, ilikuwa kituo kimojawapo cha ustarabu wa kilimwengu katika zama za kale, na kuwa kiasi kikubwa cha ujuzi wa sayansi, sanaa na fasihi kilitoka kwenye eneo hilo na athari zake zilifika hata Uyunani. Katika nyanja za hisabati (jiometri, hesabu n.k.), majimu na upimaji muda tiba, usanifu majengo, muziki na fasihi (nathari, mashairi, tanzia n.k.), Uyunani ilizipokea elimu hizi, za Kimisri, ikazikuzana na kuzisambaza sehemu nyingi katika nchi za Magharibi - kutoka kwenye Ufarao na Misri ya Kiptolemi. Kupitia Uyunani na Foeniki, ustaarabu wa kale wa Misti ulienea si tu hadi Ulaya, bali pia Afrika Kaskazini na hata katika baadhi ya nchi za Bara Hindi. Kuna maoni

yanayotofautiana sana kuhusu watu wa Misri ambalo bado ni suala linalohitaji kuchunguzwa barabara. Kinachotumaimiwa ni kwamba maendeleo makubwa yaliyoko katika mbinu za anthropolojia ya kimaumbile yatasaidia kufikia mahitisho maalumu kuhusu jambo hili katika siku za karibuni.

Kwa mujibu wa ushahidi uliotolewa katika juzuu hili, Unubi, imekuwa na uhusiano wa karibu na Misri tangu zama za awali, kutokana na sababu mbalimbali: sababu za kimaumbo, hususa maumbo ya kijiografia yaliyofanana hasa baina ya Unubi na sehemu za kusini kabisa mwa Misri ya Juu; sababu za kihistoria na za kisiasa; na sababu za kijamii ambazo zinadhihirika katika utamaduni na dimi. Hivyo, tangu mwanzoni mwa ufalme wa kwanza wa Misri, na kwa njia ya Ufalme Mkongwe, Wamisri walilishughulikia sana eneo la kaskazini la Nubia ambalo walilichukulia kuwa mi sehemu ya nchi ya Misri. Wamisri walifanya biashara na Wanubi, wakatumia maliasili za Unubi, na Wanubi walipoanza kuonyesha upinzani wao, Wamisri walipeleka majeshi kuukomesha upinzani huo.

Hata hivyo, tangu zama za kale Unubi ilikuwa ni sehemu ya kipekee kijiografia na kijamii. Tangu mwanzo wa historia, Unubi ilikuwa inakaliwa na watu ambao utamaduni wao ulifanana na ule wa bonde la kaskazini la Mto Nili. Lakini, tangu mwaka -3200, Wamisri walianza kuwapita majirani zao wa kusini katika mambo ya utamaduni na wakapiga hatua kubwa katika ustaarabu, ilihali Unubi ikaselelea kwenye kiwango cha kabla ya historia kwa muda mrefu. Katika nusu ya kwanza ya elfia ya pili kabla ya enzi ya Ukristo, utamaduni uliokuwa ukiitwa utamaduni wa Kerma, ambao ulikuwa ustaarabu mkubwa na wenye ufanisi, ulisitawi huko Unubi. Ingawa ustaarabu huo uliathiriwa sana na utamaduni wa Kimisri, lakini vile vile ulikuwa na sifa zake za kipekee. Baada ya mwanzo wa elfia ya kwanza kabla ya enzi zetu, ambapo nguvu za Misri zilianza kufifia, ufalme wa kienyeji ulianzishwa, na Napata ukafanywa kuwa mji mkuu. Hivyo baadaye ufalme huo ulitawala hata Misri. Utawala wa miaka hamsini wa Kinubi nchini Misri katika kipindi cha saba (sehemu ya kwanza ya Ufalme na Ishirini na Tano) ulikamilisha muungano wa Misri na Unubi. Fahari na utukufu wa nchi hii kubwa ya Kiafrika ilikuwa ni kubwa, kama inavyoelezwa na wandishi maarufu.

Baada ya mji mkuu wa Unubi kuhamishiwa Meroe, Unubi ilipitia katika kipindi cha maendeleo na ufanisi, na inaendeleza uhusiano na jirani zake, hadi karibu na karne ya tisa. Uenezaji wa ufalme wa Kimeroe katika magharibi na kusini na nafasi yake katika kutawanya fikra na mbinu zake na uenezaji wake wa athari za kimagharibi na kimashariki bado yangali yanatafitiwa na kujadiliwa. Vilevile, hata baada ya kuchapishwa kwa juzuu hili, kuna haja ya kuchochea juhudi zaidi za kuzifumbua hati za Kimeroe. Miswada 900 iliyoko hivi saa itaweza kutoa maelezo ya aina nyingi. Kadhalika, miswada hii itadhihirisha lugha mpya fasaha ambayo ni ya asili ya Kiafrika halisi pamoja na lugha ya wakati wa enzi za Mafarao.

Tangu karne ya nne ya enzi zetu, Ukristo, ulianza kuenea katika Unubi ambako mahakalu yaligeuzwa kuwa makanisa. Harakati za Kikristo katika Unubi zilikuwa

kubwa, mafanikio yake yalikuwa mengi, na athari zake kwa majirani zilidhihirika.

Kutokana na mahali iliyopo, Unubi ilikuwa na dhima maalumu na mara nyingine kuwa na jukumu la kulazimishwa kusuluhisha kati ya Afrika ya kati na Mediterani. Ufalme na Napata, Dola ya Meroe na ufalme wa Kikristo ulionyesha kuwa Unubi ilikuwa kiungo kati ya kaskazini na kusini. Kwa kupitia Unubi utamaduni, mbinu na vitu vikafika kwenye maeneo yaliyoizingira. Ni kwa kufanya utafiti tu ndipo tutaweza kugundua kuwa ustaarabu wa Kimisri na wa Unubi katika Afrika ulikuwa na athari inayolingana na ile ya ustaarabu wa Kiyunani na wa Kirumi katika Ulaya.

Ingawa hapo mwanzoni Ethiopia iliathiriwa kwa sababu mbalimbali, lakini ilianzisha utamaduni ambao unatambulika kuwa ulitoka kusini mwa Bara Arabuni. Vitu vilivyopatikana, vya tangu kipindi cha pili cha kabla ya Aksum vinaonyesha kuwa kulikuwapo na utamaduni mahali hapo ambao ulikuwa umeingiza athari za kigeni.

Ufalme wa Aksum, ambao uliendelea tangu karne ya kwanza ya enzi za Ukristo, au kwa muda wa miaka elfu moja, ulikuwa na umbo mahsusi lililotofautiana na lile la utamaduni wa kipindi cha kabla ya Aksum. Ustaarabu wa Aksum, kama ule wa Misri ya kale, ulitokana na maendeleo yaliyoanza mapema sana. Ustaarabu huo ulikuwa wa Kiafrika, nao ulianzishwa na wenyeji wake, ingawa athari fulani ya Kimeroe inaweza kuonekana katika ufinyanzi kwenye kipindi cha pili cha kabla ya Aksum.

Katika karne ya pili na ya tatu, athari za Kimeroe zilikuwa zimetapakaa katika Ethiopia. Nguzo ya Aksum ambayo ndiyo kwanza ilikuwa imegunduliwa, pamoja na alama ya Kimsri ya miaka (Ankh), na vifaa vilivyohusiana na Wathor, Ptah na Horus, na aina ya mende, vinabaimisha jinsi imami za Kiaksuni zilivyoathiriwa na Meroe na Misri.

Ufalme wa Aksum ulikuwa ni nguzo muhimu ya kibiashara kwenye njia za kutokea eneo la dola ya Warumi hadi Bara Hindi na kutoka Bara Arabuni hadi Afrika kaskazimi, pamoja na kuwa ufalme huo ulikuwa kituo kikubwa cha kutawanya utamaduni. Mpaka hivi sasa, ni vipengee vichache tu vya utamaduni wa Aksum na uasili wake wa Kiafrika, ndivyo ambavyo vimeshachunguzwa; na bado kuna mengi ya kutekelezwa.

Majilio ya Ukristo nchini Ethiopia, kama vile katika Misri na Meroe, yalisababisha mabadiliko mengi katika utamaduni na maisha ya watu. Kuendelea kwa Ukristo katika Ethiopia na athari zake ndani na nje ya nchi hiyo, ni mambo ya kusisimua ambayo yanahitaji kufanyiwa utafiti barabara katika siku zijazo.

Kutokana na uhaba wa maelezo ya kihistoria, ujuzi zaidi kuhusu ukuaji wa utamaduni wa kienyeji wa Libya na mrejesho wake kwa uanzishaji wa ustaarabu wa Kifoeniki, itabidi usubiri hadi wanaakiolojia na wanahistoria watakapokuwa wamekwishafanya utafiti zaidi.

Kiwango chetu cha sasa cha ujuzi wetu kinatufanya tuchukulie kuwa uingiaji wa Maghreb katika historia iliyowekewa kumbukumbu unaanza na majilio ya Wafoeniki

katika mwambao wa Afrika kaskazini, ingawa mahusiano ya Kikarteji na ya watu wa Sahara, hata na watu walioishi kusini zaidi hayaeleweki vizuri.

Papo hapo inafaa ieleweke kuwa utamaduni wa Afrika Kaskazini ambao ulikuwa ni wa Kiafrika hautokani na athari za Kifoeniki peke yake.

Kipindi cha Ufoeniki katika Maghreb kiliingizwa katika historia kuu ya ulimwengu wa Mediterani, kwa sababu utamaduni wa Kifoeniki ulichanganyika na sehemu za utamaduni wa Kimisri na wa Kimashariki na ulitegemea mahusiano ya kibiashara na nchi nyingine za Mediterani. Hata hivyo, vipindi vya baadaye vya falme za Numidia na Mauritania vilishuhudia ukuaji wa utamaduni wenye sifa za mchanganyiko wa Kilibya na Kifoeniki.

Ingawa ujuzi wetu wa Sahara na utamaduni wake wa kikale ni duni na usiokamilika, maelezo kadhaa yanaweza yakatolewa. Ni hakika kuwa mabadiliko ya hali ya hewa hayakuliu jangwa na kwamba shughuli za binadamu ziliendelea; na kwamba lugha na maandishi yaliimarika kwa kuomba kwa. Kuongezeka matumizi ya ngamia ilimaamisha kuwa njia za usafiri ziliendelezwa na kulifanya jangwa la Sahara kushiriki kwa kiasi kikubwa katika ubadilishanaji wa kitamaduni kati ya Maghreb na Afrika ya tropiki.

Kwa hiyo tunaweza kutoa kauli kwamba Sahara haikuwa kikwazo wala eneo lililokuwa halifai, bali lilikuwa eneo lenye utamaduni wake na historia yake ambayo bado inahitaji kutafitiwa ili kugundua mtiririko wa athari ya Maghreb kwenye ukanda wa Sudani. Siku zote kulikuwepo na uhusiano mkubwa kwenye jangwa la Sahara na Afrika kusini mwa Sahara ambao uliathiri sana historia ya Afrika.

Mpaka hivi sasa, imekuwa ni desturi kusema kuwa historia ya Afrika kusini mwa Sahara ilianza kama karne ya kumi na tano ya enzi za Ukrist[†] ni kwa sababu mbili kuu: kwanza kutokana na upungufu wa hati za maandishi na utenganisho wanaoufanga wanahistoria akilini mwao kati ya sehemu ile ya bara kwa upande mmoja na Misri ya kale Afrika kaskazini kwa upande wa pili.

Ijapokuwa kuna mengi ambayo yanatokana na upungufu wa utafiti uliokwihafanywa, juzuu hili limeweza kusaidia kuonyesha uwezekano wa umoja wa kitamaduni wa bara zima katika nyanja mbalimbali.

Nadharia ya uhusiano wa kijenetiki kati ya lugha za Misri ya kale na za Kiafrika imeshajadiliwa. Iwapo utafiti utaithibitisha nadharia hii, basi utakuwa umethibitisha umoja imara wa lugha katika bara zima. Mfano wa miundo ya kifalme, uhusiano wa imani za kidini, zikiwemo upashaji tohara, utambikaji, na imani kuhusu masiha kwa jumla, na zana zilizotumiwa katika kilimo na shughuli nyingine, ni mambo ambayo yanahitaji kuchunguzwa kwa undani katika siku zijazo.

Urithi wa kitamaduni tulioupata sisi na uliotokana na jamii zilizoishi Misri,

Angalia sura 29, "Jamii za Afrika Kusini mwa Sahara kwenye Mwanzo wa Enzi ya Mawe". Inajadili matokeo yaliyopatikana kwenye sura kumi za mwisho za juzuu hii kuhusu kusini mwa Afrika Kusini mwa Sahara.

[†] Waaandishi kadhaa wa Afrika ya Kusini mwa Sahara kabla ya kame ya kumi na tano.

Unubi, Ethiopia na Maghreb, ni wa muhinu sana. Iniani ya Mungu nimoja iliyoletwa na Wakristo, na kabla yao, Mayahudi, ilileta mapinduzi nuakubwa katika iniani za Waafrika; na bila shaka ndiyo iliyorahisisha Uislamu kuingia Afrika. Ukweli huu unadhirisha uwezo na sifa kubwa ya Waafrika ya kwenda na wakati ingawa kuna manibo mengi yanayohitaji kufanyiwa uchunguzi zaidi.

Vivyo hivyo, utimizaji wa sharti la tatu la kuandika Juzuu I na II, yaani, ufufuaji wa mfumo wa kale wa njia za biashara za Afrika tangu zama za mwanzoni mwa historia, ua uthibitisho wa kadiri ya maeneo yaliyolimwa katika kipindi hichohicho kutokana na uchanganuzi wa picha zilizopigwa kwa setelaiti, utasaidia kupanua na kuongeza kina cha ujuzi wetu kuhusu mahusiano ya kitamaduni na ya kibiashara ya wakati huo na kiasi anibacho bara la Afrika lilivyokuwa limekaliwa.

Utafiti zaidi katika majina ya kabila na majina ya mahali utawezesha kuthibitisha mikondo ya uhamaji na mahusiano ya kikabila yasiyotambulikana kuanzia ncha moja hadi ya pili ya bara la Afrika.

Nina matumaini kuwa juzuu hili litashawishi nchi za Kiafrika kushughulika zaidi na kusaidia akiolojia ya Afrika ya kale.

Bibliografia

- Abel, A. (1972) 'L'Éthiopie et ses rapports avec l'Arabie préislamique jusqu' à de ca. 615',
- Abraham, D. P. (1962) 'The early political history of the Kingdom of Mwene Mutapa, 850-1589', *Historians in Tropical Africa* (Salisbury: Chuo Kikuu cha Rhodesia na Nyasaland)
- Abraham, D. P. (1964) 'The ethnohistory of the empire of Mutapa, problems and methods' kwenye J. Vansina, R. Mauny na L.V. Thomas (wah.), *The Historian in Tropical Africa* (London/Accra/Ibadan: Oxford University Press) kur. 104-26)
- Adams, W. Y. (1962a) 'Pottery kiln excavations', *Kush*, 10 kur. 62.-75.
- Adams, W. Y. (1962b) 'An introductory classification of Christian Nubian pottery', *Kush*, 10. kur. 245-88
- Adams, W. Y. (1964a) 'Post-pharaonic Nubia in the light of archaeology', *JEA*, 50 kur. 102-20
- Adams, W. Y. (1965b) 'Architectural evolution of the Nubian church 500-1400 AD', *JARCE*, 4 kur. 87-139
- Adams, W. Y. (1965c) 'Post-pharaonic Nubia in the light of archaeology II', *JEA*, 51. kur. 160-78
- Adams, W. Y. (1966a) 'The Nubian campaign: retrospect', *Mélanges offerts à K. Michalowski* (Warsaw), kur. 13-20
- Adams, W. Y. (1966b) 'Post-pharaonic Nubia in the light of archaeology III', *JEA*, 52, kur. 147-62
- Adams, W. Y. (1967) 'Continuity and change in Nubian cultural history', *SNR*, XLIII, kur. 11-19
- Adams, W. Y. na Nordstrom, H. A. (1963) 'The archaeological survey on the west bank of the Nile, third season 1961-2', *Kush*, 11, kur. 1-46
- Adams, W. Y. na Verwers, C. J. (1961) 'Archaeological survey of Sudanese Nubia', *Kush*, 9, kur. 7-43
- Addison, F. S. A. (1949) *Jebel Moyo (The Wellcome Excavation in the Sunday)*; Juz. 2 (London: Oxford University Press
- Aldred, C. (1980) *Egyptian Art in the Days of the Pharaohs* (London: Thames and Hudson)
- Alexander, J. (1980) 'The spread and development of iron using in Europe and Africa', kwenye R. E. F. Leakey na B.A. Ogot (wah.), *Proceedings of the 8th Panafrican Congress of Prehistory and Quaternary Studies*, kur. 327-30)
- Alexander, J. na Coursey D,G. (1969) 'The origins of yam cultivation', kwenye P.H.Ucko na G. W. Dimbleby (wah.) *The Domestication and Exploitation of Plants and Animals* (London: Duckworth), kur. 123-9
- Ali Hakem, A. M.(1972) 'Meroitic settlement of the Butana central Sudan', kwenye P. H. Ucko, R. Tringham na G. W. Dimbleby (wah.) *Man, Settlement and Urbanism* (London: Duckworth), kur. 639-46
- Allen, J. W. T. (1949) 'Rhapta', *TNR*, 27 kur. 52-9
- Amblard, S. (1984) Tichitt Walata – Civilisation et Industrie Lithique, Editions Recherche sur les civilisation, Memoire na. 35, (Paris: ADPPF)
- Andah, B. W. (1973) 'Archaeological reconnaissance of Upper-Volta', tasnifu (Berkeley, Chuo Kikuu cha California.
- Andah, B. W. (1979) 'Iron Age beginnings in West Africa: reflections and suggestions', *WAJA*, 9 kur. 125-41
- Anfray, F. (1963) 'Une campagne de fouilles à Yeha', *AE*, 5 (Februari – Machi 1960, kur. 171-92
- Anfray, F. (1967) 'Matara', *AE*, 7 kur 33-97
- Anfray, F. (1972) 'L'archéologie d'Axoum en 1972', *Paideuma*, XVIII, uk.71
- Afray, F. na Annequin, G. (19650 'Matara. Deuxième, troisième et quatrième campagnes de fouilles', *AE* 6, kur. 49-86
- Anfray, F. Caquot, A na Nautin, P. (1970) 'Une nouvelle inscription grecque d'Ezana, roi d'Axoum', *JS*, kur.

260-73

- Anquandah, J. (1982) *Rediscovering Ghana's Past* (London: Longman)
- Applegate, J. R. (1970) 'The Berber language', *CTL*, VI kur. 586-661
- Arkell, A. J. (1949) *Early Khartoum. An Account of the Excavations of an Early Occupation Site carried out by the Sudan Government Antiquities Service 1944-1945* Oxford: Oxford University Press
- Arkell, A. J. (1961) *A History of the Sudan from the Earliest Times to 1821* (London: Chuo Kikuu cha London, Athlone Press)
- Arkell, (1966) 'The iron age in the Sudan' *CA*, 7, 4, kur. 5451-78
- Armstrong, R. G. (1964), *The Study of West African Language* (Ibadan: Ibadan University Press)
- Atherton, J. H. (1972) 'Excavations at Kambamai and Yagala rock shelters, Sierra Leone', *WAJA*, 2 uk. 39 na kuendelea
- Aubreville, A. (1948) ('Etude sur les forêts de l'Afrique équatoriale française et du Cameroun'), *BS*, 2 uk. 131
- Aumassip, G. (1986) *Le Bas-Sahara dans la Préhistoire* (Paris: Editions du Centre National de la Recherche Scientifique)
- Aurigemma, S. (1940) 'L'éléfante di Leptis Magna', *AI*, kur. 67-86
- Badawy, A. (1968) *A History of Egyptian Architecture (The New Kingdom): From the Eighteenth Dynasty to the End of the Twentieth Dynasty 1580-1085 BC* (Berkeley, Calif. Los Angeles: University of California Press)
- Baillooud, G. (1969) 'L'évolution des styles céramiques en Ennedi (République du Tchad)', *Actes 1er Coll. Intern. Archéol. Afr., Fort Lamy*, 1966, kur. 31-45
- Balout, L. (1967) 'L'Homme préhistorique et la Méditerranée occidentale', *ROMM*, Aix-en-Provence, 3
- Baradez, J. (1949) *Vue aérienne de l'organisation romaine dans le Sud-Algérien. Fossatum Africae* (Paris: AMG)
- Barraux, M. (1959) 'L'auge de Sima', *BAM*, n.s., XXXVII, kur. 93-9
- Barrow, J. (1801-4) *An Account of Travels into the Interior of Southern Africa in the Years 1797 and 1798* Juzuu 2 (London: T. Cadell and W. Davies)
- Basset, H. (1921) 'Les influences puniques chez les berbères', *RA*, 62, kur. 340
- Bates, O. (1914) *The Eastern Libyans* (London: Macmillan)
- Bates, O. na Dunham, D. (1927) 'Excavations at Gammai', *HAS*, 8 kur. 1-122
- Bayle des Hermans, R. de (1972a) 'Aspects de la recherche préhistorique en République Centrafricaine', *Africa Tervuren XVIII*, ¾ kur. 90-103
- Bayle des Hermans, R. de (1972b) 'La civilisation mégalithique de Bouar. Prospection et fouille 1962-6 par P. Vidal, Recension', *Africa Tervuren, XLII*, 1 kur. 78-9
- Beauchêne, M. C. de (1970) 'The Lantana mine near the Rapoa/Niger confluence of Niger', *WAAN*, 12, uk. 63
- Beck, P. na Huard, P. (1969) *Tibesti, carrefour de la préhistoire saharienne* (Paris: Arthaud)
- Bedaux, R. na Bolland, R. (1980) 'Tellem, reconnaissance archéologique d'une culture de l'Ouest africain au Moyen Age: Les textiles', *Journal des Africanistes*, 50, 1 kur. 9-24
- Beek, G. W. Van (1967) 'Monuments of Axum in the light of south Arabian archaeology', *JAOS*, 87, kur. 113-22
- Bénbou, M. (1976) *La résistance africaine à la romanisation* (Paris: Maspero)
- Bernus, S. (1983) 'Découvertes, hypothèses, reconstitution et preuves: Le cuivre médiéval d'Azelik-Takedda (Niger)', kwenye M. Echard (mh.) *Métallurgies africaines: nouvelles contributions, Mem. Soc. Afr.* Kur. 153-71
- Bermus, S. na Ecbard, M. (1985) 'Metal-working in the Agadez region (Niger): An ethno-archaeological approach', kwenye P. T. Craddock na M.J. Hughes (wah.) *Furnaces and Smelting Technology in Antiquity* (London: British Museum, Occasional Paper, 48) kur. 71-80
- Bisson, M. S. (1975) 'Copper currency in central Africa: the archaeological evidence', *WA*, 6 kur. 276-92
- Blankoff, B. (1965) 'La préhistoire au Gabon', *BSPPG*, kur. 4-5
- Bloch, M. na Verin, P. (1966) 'Discovery of an apparently neolithic artefact in Madagascar', *Man*, 1 kur. 240-1
- Boshier, A. na Beaumont, P. (1972) 'Mining in southern Africa and the emergence of modern man', *Optima*, 22 kur. 2-12
- Boubbe, J. (1959-60) 'Découvertes récentes à Sala Colonia (Chellah)' *BSAC*, kur. 141-5
- Bourgeois, R. (1957) 'Banyarwanda et Barundi, Tombe I - ethnographie', *ARSC*, XV, kur. 536-49
- Bovill, E. W. (1968) *The Golden Trade of the Moors* 2nd edn (London: Oxford University Press)
- Brabant, H. (1965) 'Contribution odontologique à l'étude des ossements trouvés dans la nécro-pole protohistorique de Sanga, République du Congo', *AMRAC*, 54
- Breasted, J. H. (1951) *A History of Egypt from the Earliest Times to the Persian Conquest* 2nd edn (London:

- Hodder and Stoughton)
- Briggs, L. C. (1957) 'Living tribes of the Sahara and the problem of their prehistoric origin', *Third Pan-African Congress on Prehistory*, Livingstone, 1955 (London: Chatto), kur 195-9
- Budge, E. A. T. Wallis (1928) *A History of Ethiopia, Nubia and Abyssinia, according to the Hieroglyphic Inscription of Egypt and Nubia and the Ethiopian Chronicle*, Juz. 2 (London: Methuen)
- Budge, E. A. T. Wallis (1966) *A History of Ethiopia*, Juz.1 (Netherlands: Cosferhout NB, Anthropological Publications)
- Bynon, J. (1970) 'The contribution of linguistics to history in the field of Berber studies', kwenye D. Dalby (mh.), *Language and history in Africa* (London: Cass), kur. 64-77
- Cabannes, R. (1964) *Les Types hémoglobiniques des populations de la partie occidentale du continent africain (Maghrib, Sahara, Afrique noire occidentale)* (Paris: CNRS)
- Callet, F. (1974) *Histoire des rois de Tanaran'ny Andriana*, Juz. 1-3, translated by G. S. Chaput and E. Ratsimba (Tananarive: Librairie de Madagascar)
- Caminos, R. A. (1975) *New Kingdom Temples of Buhen*, Juz. 2 (London: Egypt Exploration Society)
- Camps, G. (1954) 'L'inscription de Béja et le problème des Dii Mauri' *RA*, 98, kur. 233-60
- Camps, G. (1960a) 'Les traces d'un âge du bronze en Afrique du Nord', *RA*, 104 kur. 31-55
- Camps, G. (1960b) 'Aux origines de la Berbérie: Massinissa ou les debuts de l'histoire', *Libyca*, 8, 1
- Camps, G. (1961) *Monuments et rites funéraires protohistoriques: aux origines de la Berbérie* (Paris: AMG)
- Camps, G. (1974) 'Le Gour, mausolée berbère du VIIIe siècle', *American Anthropologist*, VIII, kur.191-208
- Camps, G. (1982) 'Beginning of pastoralism and cultivation in Northwest Africa and the Sahara', *The Cambridge History of Africa* (Cambridge: Cambridge University Press), kur. 584-623
- Camps, G. Dellbrias, G. na Thommeret, J. (1968) 'Chronologie absolue et succession des civilisations préhistoriques dans le Nord de l'Afrique', *Libyca*, XVI, uk. 16
- Camps-Fabrer, H. (1953) *L'Olivier et l'huile dans l'Afrique romaine* (Algiers: Imprimerie officielle)
- Caquot, A. na Leclant, J. (1959) 'Ethiopie et Cyrenaïque? A propos d'un texte de Synesius', *AE*, III, kur.173-7
- Carter, P. L. (1970) 'Late stone age exploitation patterns in southern Natal', *SAAB*, 25, 98, kur. 55-8
- Carter, P. L. na Flight, C. (1972) 'A report on the fauna from two neolithic sites in northern Ghana with evidence for the practice of animal husbandry during the 2nd millennium BC' *Man*, 7, 2, kur. 277-82
- Carter, P. L na Vogel, J. C. (1971) 'The dating of industrial assemblages from stratified sites in eastern Lesotho', *Man*, 9 kur. 557-70
- Castiglione, L. (1970) 'Diocletianus und die Blemmyes', *ZAS*, 96, 2, kur. 90-103
- Caton-Thompson, G. (1929) 'The Southern Rhodesian ruins: recent archaeological investigations', *Nature*, 124, ku.619-21
- Caton-Thompson, G. (1929-30) 'Recent excavations at Zimbabwe and other ruins in Rhodesia', *JRAS*. 29, kur.132-8
- Chaker, S. (1973) 'Libyque: épigraphie et linguistique', *Encyclopédi berbère*.9
- Chamla, M.C. (1970) 'Les hommes épipaléolithique de Columnata (Algerie occidentale)', *Mém. CRAPE*, XV, kur. 113-14
- Chamoux, F. (1953) *Cyrène sous la monarchie des Battiades* (Paris: de Boccard)
- Chaplin, J. H. (1974) 'The prehistoric rock art of the Lake Victoria region', *Azania*, IX, kur. 1-50
- Charles-Picard, G. (1954) *Les Religions de l'Afrique antique* (Paris: Plon)
- Charles-Picard, G. na C. (1958) *La Vie 'quotidienne à Carthage au temps d'Hannibal, IIIe siècle avabt Jesus-Christ* (Paris: Hachette)
- Charles-Picard G. (1959) *La Civilisation de l'Afrique romaine* (Paris: Plon)
- Charles-Picard, G. (1968) *Les Cahiers de Tunisie. Melanges Saumagne*, kur. 27-31
- Chastagnol, A. na Duval, N. (1974) 'Les survivances du culte impérial dans l'Afrique du Nord à l'époque vandale. Mélanges d'histoire ancienne offerts à W. Seston', Publications de la Sorbonne, Etude IX, kur. 87-118
- Clittick, N. (1966) 'Six early coins from new Tanga', *Azania*, 1, kur. 156-7
- Cblittick, N. (1969) 'An archaeological reconnaissance of the southern Somali coast', *Azania*. IV, kur.115-30
- Clark, J. D. (1970) *The Prehistory of Africa* (London: Thames and Hudson)
- Clark, J. D. (1974) 'Iron age occupation at the Kalambo Falls', kwenye J. D. Clark (mh.), *Kalambo Falls Prehistoric Site*, Juz. II (Cambridge: Cambridge University Press), kur. 57-70
- Clark, J. D. na Fagan, B. M. (1965) 'Charcoal, sands and channel-decorated pottery from northern Rhodesia', *American Anthropologist*, LXVII, kur. 354-71

- Clark, J. D. na Walton, J. (1962) 'A late stone age site in the Erongo mountains, south west Africa'. *Proc. PS*, 28 kur. 1-16
- Cohen, D. na Maret, P. de (1974) 'Recherches archéologiques récentes en République du Zaïre.', *Forum-Université Libre de Bruxelles*, 39, kur. 33-7
- Connah, G. (1967) 'Excavations at Daima, N.E. Nigeria', *Actes VI Congr. PPEQ*, kur. 146-7
- Connah, G. (1981) *Three thousand Years in Africa* (Cambridge: Cambridge University Press)
- Connah, G. (1987) *African Civilization: Precolonial Cities and States in Tropical Africa: An Archaeological Perspective* (Cambridge: Cambridge University Press)
- Contenson, H. de (1963a) 'Les premiers rois d'Axoum d'après les découvertes récentes', *JA*, 248, kur. 78-96
- Contenson, H. de (1961) 'Les principales étapes de l'Éthiopie antique', *CEA*, 2 5 kur. 12-23
- Contenson, H. de (1963a) 'Les subdivisions de l'archéologie éthiopienne. Etat de la question', *R. Arch.*, kur. 189-91
- Contenson, H. de (1963b) 'Les fouilles de Haoulti en 1959. Rapport préliminaire', *AE*, 5 kur. 41-86)
- Contenson H. de (1963c) 'Les fouilles à Axoum en 1958. Rapport préliminaire', *AE*, 5, kur. 3-39
- Cooke, C. K. (1971) 'The rock art of Rhodesia', *SAJS*, special issue 2, kur. 7-10
- Coon, C. S (1968) *Yengema Cave Report* (Philadelphia, Pa: Chuo Kikuu cha Pennsylvania)
- Coppens, Y. (1969) 'Les cultures protohistoriques et historiques du Djourab', *Actes 1er Coll. Intern. Archeol. Afr.*, kur. 129-46)
- Cornevin, R. (1967) *Histoire de l'Afrique. Vol. I: Des origines au XVIe siècle*, 2nd edn (Paris: Payot)
- Cosmas Indicopleustes (1909) *The Christian Topography of Cosmas Indicopleustes*, translated by E.O. Winstedt (Cambridge: Cambridge University Press). *Topographic chrétienne*, translated by W. Walsca (Paris: Cerf)
- Coulbeaux, J. B. (1928) Histoire politique et religieuse d'Abyssinie depuis les temps les plus reculés jusqu'à l'avènement de Menelik II, Juz. I (Paris: Geuthner)
- Crowfoot, J. W. (1911) *The island of Meroe*, *Archaeological Survey of Egypt, Memoire 19* (London) uk.37
- Crowfoot, J.W. (1927) 'Christian Nubia', *JEA*, XII, kur. 141-50
- Culwick, A. L. na G. M. (1936) 'Indonesian echoes in central Tanganyika', *TNR*, 2, kur. 60-6
- Dahl, O. Ch. (1951) 'Malgache et Maanjan, une comparaison linguistique', *AUEI*, 3
- Dahle, L. (1989) 'The Swahili element in the new Malagasy English dictionary', *Antananarivo*, III, kur. 99-115
- Dalby, D. (1970) 'Reflections on the classification of African languages', *ALS*, II, kur. 147-71
- Dalby, D. (1967) 'The prehistorical implication of Guthrie's comparative Bantu. II. Interpretation of cultural vocabulary', *JAH*, XVII, kur. 1-27
- Daniels, C. M. (1968a) *Garamantian Excavations: Zinchechra 1965-1967* (Tripoli: Department of Antiquities)
